

UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!

Kumbukumbu la Torati

NA BOB UTLEY,
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFAIRI
(UFAIRI WA BIBLIA)

MWONGOZO WA USOMAJI WA FASIRI MFUATANO
AGANO LA KALE, VOL.03

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL,
MARSHAL, TEXAS
(Limetolewa 2011)

ORODHA YA YALIYOMO

Maelezo ya sahihi ya Vyanzo vya Kiufundi vilivyotumika katika Fasiri hii “Unaweza Kuelewa Biblia”	i
Maelezo sahihi ya Muundo wa Maneno ya Kiebrania Yanayogonganisha Fasili ya Maandiko	iii
Vifupisho Vilivyotumika katika Fasiri Hii	ix
Neno Toka kwa Mwandishi:Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia	x
Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika.....	xii
Utangulizi wa kitabu cha Kumbukumbu la Torati.....	1
Kumbukumbu la Torati 1	6
Kumbukumbu la Torati 2	37
Kumbukumbu la Torati 3	49
Kumbukumbu la Torati 4	58
Kumbukumbu la Torati 5	82
Kumbukumbu la Torati 6	104
Kumbukumbu la Torati 7	113
Kumbukumbu la Torati 8	123
Kumbukumbu la Torati 9	131
Kumbukumbu la Torati 10	139
Kumbukumbu la Torati 11	146
Kumbukumbu la Torati 12	154
Kumbukumbu la Torati 13	164
Kumbukumbu la Torati 14	174
Kumbukumbu la Torati 15	184
Kumbukumbu la Torati 16	192
Kumbukumbu la Torati 17	200
Kumbukumbu la Torati 18	210
Kumbukumbu la Torati 19	219
Kumbukumbu la Torati 20	225
Kumbukumbu la Torati 21	230
Kumbukumbu la Torati 22	240
Kumbukumbu La Torati 23.....	247
Kumbukumbu la Torati 24	257
Kumbukumbu la Torati 25.....	266
Kumbukumbu la Torati 26	272

Kumbukumbu la Torati 27	278
Kumbukumbu la Torati 28	286
Kumbukumbu la Torati 29	301
Kumbukumbu la Torati 30	308
Kumbukumbu la Torati 31	315
Kumbukumbu la Torati 31:30-32:52.....	325
Kumbukumbu la Torati 33	348
Kumbukumbu la Torati 34	360
Kiambatisho cha Kwanza: Utangulizi wa Unabii wa Agano la Kale.....	365
Kiambatisho cha Pili: Pitio Sahihi la Kihistoria la Mamlaka za Mesopotamia.....	369
Kiambatisho cha tatu: Jedwali la Agano la Kale.....	369
Kiambatisho cha nne: Kanuni ya Imani.....	379

ORODHA YA YALIYOMO YA MADA MAALUM

Israeli (Jina lake), 1:1.....	7
Mahali ulipo Ml. Sinai, 1:2	9
Kalenda za Mashariki ya Karibu ya Kale, 1:3.....	10
Majina ya Uungu 1:3.....	11
Tarehe ya Kutoka kwa Waisraeli Misri1:3.....	14
Waisraeli wa Mwanzo walioishi Palestina, 1:4	26
Elfu, (<i>Eleph</i>)1:54.....	21
Haki, 1:16	22
Maneno yatumikayo kwa Mashujaa/Makundi ya Watu, 1:28	28
Kuamini, Tumaini, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale(אמן) 1:32, 1:6	29
Umri wa Uwajibikaji, 1:39.....	33
Bahari ya Shamu, 1:40	34
Safari ya Jangwani, 2:1.....	38
Lugha ya Wanadamu Kuuelezea Uungu, 2:15	42
Bwana akaufanya mgumu Moyo wake, 2:30.....	46
Moyo, 2:30.....	46
Mkono, 3:11.....	53
Istirahi kwa ajili ya Ufunuo wa Mungu kwa kutumia Kumbukumbu la Torati na Zaburi, 4:1.....	59
Upendeleo wa Kiinjilisti wa Bob, 4:6	61
Moto, 4:11	64
Agano 4:13.....	65
Tabia za Mugu wa Israeli, 4:31	70
Utabiri wa baadaye wa Agano la Kale dhidi ya utabiri wa Agano Jipya,.....	70
Kujua4:35.....	76
Milele (Olam) Katika Agano la Kale, 4:40.....	78
Ardhi, Nchi, Dunia (ארץ) 5:8.....	85
Wema, (<i>Hesed</i>), 5:10	86
Sabato, 5:12	88
Mtakatifu, (שׁוֹדֵק) 5:12	89
Utambuzi wa Kutoka 20:12-17 (Usiue), 5:17	92
Amani na Vita, 5:17.....	97
Utukufu 5:24	101
Imani katika Mungu Mmoja,6:4.....	106
Fidia /Komboa, 7:8.....	116
Kuimiliki Nchi, 8:1	124
Mungu anawajaribu watu wake, 8:2	125
Ubaba wa Mungu, 8:5.....	126

Matendo ya neema ya YHWH kwa Israeli, 9:4-6	133
Agano lililoahidiwa kwa mababa wa Imani, 9:12.....	133
Nyongeza ya baadaye kwenye Kumbukumbu la Torati, 10:12.....	141
Mahitaji ya Agano la YHWH, 10:12.....	143
Madhara ya Kuabudu Sanamu, 11:16-17	150
Kushawishika kwa Israeli kwenye Ibada ya Ustawi, 5:3	156
Jina la YHWH 12:5	157
<i>Molech</i> , 12:31	162
Unabii wa Agano la Kale 13:1	165
Ibada kwa walio katika huzuni, 14:1.....	175
Sheria za Vyakula katika Agano la Kale, 14:3.....	176
Chukizo, 14:3.....	177
Mtazamo wa Kibiblia kuhusiana na Ulevi na kileo, 14:26.....	180
Pasaka, 16:1	193
Uandishi wa Vitabu Vitano vya Musa, 17:14.....	204
Pasipo hatia,18:13.....	215
Hukumu ya Kifo katika Israeli, 21:21.....	235
Kujitundika, 21:221	237
Laana, 21:23.....	237
Uwakilishi wa namba katika Maandiko, 23,2,3	250
Kuwasaidia Wahitaji, 24:13.....	262
Uzani na Vipimo vya Mashariki ya Karibu ya Kale, 25:13.....	269
Zaka, 26:12.....	275
Amina, 27:15.....	282
Toba katika Agano la Kale, 30:2.....	309
Sikukuu za Israeli, 31:10.....	318
Ushairi wa Kiebrania, Mtazamo wa ndani wa Sura ya 32.....	326
Kivuli kama Stiari ya Ulinzi	334
Malaika na Pepo katika Agano la Kale, 32:17	335
Uovu Binafsi, 32:1.....	337
Wafu wako wapi?, 32:22	339
Baraka, 33:1	349
Kuweka Mikono, 34:9	363

MAELEZO SAHIHI YA VYANZO VYA KIUFUNDI VILIVYOTUMIKA KWENYE MFULULIZO WA FASIRI HII YA AGANO LA KALE

A. Kimisamiati

Kuna maneno mengi mazuri mbali mbali yanayopatikana katika lugha ya Kiebrania cha kale.

1. *Hebrew and English Lexicon of the Old Testament* kilichoandikwa na Francis Brown, S. R. Driver, na Charles A. Briggs. Yanaegemea juu ya misamiati ya Kijerumani ya William Gesenius. Yanajulikana kwa vifupisho vya BDB.
2. *The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na Ludwig Koehler na Walter Baumgartner, yaliyotafasiliwa na, M. E. J. Richardson. Yanajulikana kwa vifupisho vya KB.
3. *A Concise Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na William L. Holladay na inaegemea juu ya maneno ya Kijerumani (#A).
4. Idadi tano mpya za usomaji wa neno la kithiolojia lililoandikwa *The New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, kilichohaririwa na Willem A. Van Gemeren. Yanajulikana kwa vifuapisho vya NIDOTTE.

Ambapo kuna aina ya maneno muhimu, nimeonyesha tafasiri mbali mbali za Kiingereza (NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB) toka kwenye tafasiri za “nenokwa-neno” na “mlinganyo wa nguvu” (kama vile Gordon Fee & Douglas Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 28-44).

B. Kisarufi

Utambulisho wa kisarufi mara nyingi huzingatia juu ya John Joseph Owens' *Analytical Key to the Old Testament* katika juzuu ya nne. Hili limehakikiwa na Benjamin Davidson's *Analytical Hebrew and Chaldee Lexicon of the Old Testament*. Vitu vingine vya kusaidia kwa ajili ya visarufi na sintaksi ambazo zinatumiwa sana katika vipengere vya juzuu za agano la kale za mtiririko wa “kuelewa Biblia” ni “ule msaada wa mfuatano wa watafasiri” toka kwa United Bible Societies. Kimeandikwa “kitabu kidogo cha mkononi _____.”

C. Kimaandiko

Mimi nimejikita kwenye uvuvio wa konsonanti za maneno ya Kiebrania (sio katika hoja za voweli za Kimosoreti na maoni. kama ilivyo katika maandiko yote yaliyonukuliwa kwa mkono, kwenye maandiko ya kale, kuna baadhi ya sura zenye maswali. Hili huwa hivyo mara nyingi kwa sababu ifuatayo:

1. *hapax legomenon* (maneno yaliyotumika mara moja tu katika Agano la Kale la Kiebrania)
2. Maneno ya kinahau (maneno na vifungu ambavyo maana yake iliyo wazi imekwisha potea)
3. Kutojulikana kihistoria (kukosekana kwa habari kuhusu ulimwengu wa kale)
4. Wingi wa elimu-maana ya Kisemitiki wa misamiati finyu ya Kiebrania
5. Matatizo yanayohusianishwa na uandishi wa maaandishi ya Kiebrania ya kale ya waandishi wa mwanzo kwa kutumia mkono.
6. Waandishi wa Kiebrania waliosomea huko Misri waliojisikia kuwa huru kuyahariri maandiko waliyoyanakili kwa ajili ya kuyafanya kuwa kamili na ya kueleweka wakati wa siku zao (NIDOTTE kur. 52-54).

Kuna vyanzo mbalimbali vya maneno na maandiko ya Kiebrania nje ya tamaduni ya kimaandiko ya Kimasoreti.

1. Torati ya Kisamaria
2. Magombo ya Bahari ya Chumvi
3. Mafunjo ya Nash (Amri Kumi za Mungu)
4. Magombo ya Severus (Vitabu Vitano vya Musa)
5. Baadhi ya sarafu, herufi na vigae vya vyungu vilivyopatikana baadaye (vipande vya vigae vya vyungu vilivyotumika kuandikiapo maandiko),

Lakini kwa maeneo mengine, hakuna uhusiano wa kimachapisho katika Agano la Kale kama yale yaliyoko katika machapisho ya Agano Jipya la Kiyunani. kwa ajili ya ufasaha wa makala mazuri juu ya uendelevu wa kimaandiko ya andiko la Kimasoreti (miaka ya 900 B.K) angalia “Uendelevu wa andiko la Agano la Kale” na Bruce K. Waltke katika toleo la NIDOTTE, juzuu. 1, kur. 51-67.

Andiko la Kiebrania lililotumika ni *Biblia Hebraica Stuttgartensia* toka German Bible Society, 1997, ambayo inaegemea juu ya Mswaada wa Leningrad (1009 B.K). Mara chache, matoleo ya kale (maandiko ya kale ya Kiyunani, Kiarama Targums, Syriac Peshitta, na Latin Vulgate) yanazungumzika kama Kiebrania ni kigumu au kinatatiza kwa wazi.

MAELEZO SAHIHI YA MUUNDO WA MANENO YA KIEBRANIA YANAYOLETA MGONGANO NA FASILI YA MAANDIKO

I. Maendeleo mafupi ya kihistoria ya Kiebrania

Waebrania ni sehemu ya kifamilia ya lugha ya Shemu kusini mwa Asia. Jina (lililotolewa na wasomi wa sasa) limetokana na Mwana wa Nuhu, Shemu (kama vile Mwa. 5:32; 6:10). Kizazi cha Shemu kimeorodheshwa katika Mwa. 10:21-31 kama Waarabu, Washamu, Waarameni, na Waashuru.

Kiukweli, baaadhi ya lugha za Kisemiti zinatumiwa na mataifa yaliyorodheshwa katika ukoo wa Hamu (kama vile Mwa. 10:6-14), Wakaanani, Wafoeniki, na Waethiopia.

Waebrania ni sehemu ya kikundi cha kaskazini Magharibi mwa lugha hizi za Kisemiti. Wasomi wa leo wana mifano ya kikundi cha lugha ya kale toka :

- A. Waamori (*Mari Tablets* tokea karne ya 18 K.K. huko Akadi)
- B. Wakaanani (*Ras Shamra Tablets* tokea karne ya 15 Ugariti)
- C. Wakaanani (*Amarna Letters* tokea karne ya 14 wakaanani wa huko Akadi)
- D. Wafoeniki (Waebrania walitumia alfabeti za Wafoeniki)
- E. Wamoabu (Mawe ya mfalme Meshu, 840 K.K)
- F. Waaramaiki (lugha rasmi ya Himaya ya Uajemi iliyotumika katika Mwa. 31:47; Yer. 10:11; Dan. 2:4b-6; 7:28; Ezr. 4:8-6:18; 7:12-26 na iliongewa na Wayahudi katika karne ya kwanza huko Palestina)

Lugha ya Kiebrania iliitwa “lugha ya Kaanani.” Mara ya kwanza iliitwa “Kiebrania” katika utangulizi Mhubiri (Hekima ya Yohana Bin Sira) kuhusu 180 K.K. na baadhi ya maeneo mengine ya awali, kama vile *Anchor Bible Dictionary*, juzuu 4, kur. 205na kuendelea) sana sana yanakaribiana kufanana na Wamoabu na kabila lililotumika huko Ugariti. Mifano ya ya Waebrania wa kale wanaopatikana nje ya Biblia ni

1. Kalenda ya Gaza, 925 K.K. (andiko la kijana wa shule)
2. Andiko /ujumbe wa Siloam, 705 K.K (maandiko yaliyopatikana katika njia za chini)
3. Vigae vya waebrania, 770 K.K (kodi inakiriwa kwenye vigae vya chungu)
4. Herufi zilizoandikwa kwenye vigae, 587 K.K (mawasiliano kwenye vita)
5. Mihuri na sarafu za watu wa Makabi
6. Baadhi ya maandiko yaliyopatikana katika magombo ya Bahari ya Chumvi
7. Maandiko mbali mbali (kama vile “lugha[Kiebrania], “ ABD 4:203 nakuendelea)

Kama ilivyo lugha zingine za Kisemiti, inaainishwa na maneno yaliyoundwa na konsonanti tatu (mizizi mitatu ya kikonsonanti). Ni lugha thabiti isiyopindikwa. Mizizi mitatu ya konsonanti inabeba msingi wa maana ya neno, wakati kiambishi awali, kiambishi tamati, au maneno ya nyongeza yanaonyesha utendaji wa kisarafu (voweli zinaongezeka baadae, kama vile Sue Green, *Linguistic Analysis of Biblical Hebrew*, uk 46-49).

Misamiati ya Kiebrania inaonyesha tofauti kati ya lugha ya mjazo na ushairi. Maana ya neno imehusianishwa na asili ya ngano/hadithi (sio usanifu wa lugha). Mchezo wa neno na mchezo wa sauti ni vitu vya kawaida (*paronomasia*)

II. Dhana ya utabiri

A. VITENZI

Neno la kawaida linalotarajiwa ni KITENZI, KIWAKILISHI, KIIMA (likiwa na vivumishi vyake), KISHAMIRISHO (kikiwa na vivumishi chake). KITENZI cha msingi kisicho pungua ni *Qal*, chenye muundo wa UMOJA, JINSI YA KIKE, na TIMILIFU. Ni namna misamiati ya Kiebrania na Kiaramaiki inavyopangwa. VITENZI vinanyumbulishwa majina kuonyesha

1. Namba-umoja, wingi, umiliki wa vitu viwili
2. Jinsi-jinsi ya kiume na jinsi ya kike (isio na jinsi)
3. Dhamira-elekezi, tegemezi, shurutishi (kwa kulinganisha lugha za Magharibi ya leo, uhusiano wa kitendo kuelekea ukweli halisi)
4. Njeo-(dhana)

- a. WAKATI TIMILIFU, inayomaanisha kutimiliza, kwa maana ya kuanza, kuendelea, na kuhitimisha kitendo. Mara zote muundo huu ulitumika kwa ajili ya kitendo kilichopita, tukio linatokea. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema “muundo mzima ulioelezwa kwa wakati timilifu pia umezingatiwa kuwa wenye uhakika. Wakati usiotimilifu unaweza kuonyesha hali ya kuwezekana au shauku au yenye kutarajiwa, lakini wakati timilifu unaliona hili kama lenye uhakiki, halisi na kweli” (uk. 36). S. R. Driver, *A Treatise on the Use of the Tenses in Hebrew*, inaelezea kama: wakati timilifu unaofanya kazi kuonyesha vitendo vyenye kutimilizwa ambavyo hakika vinasimama wakati ujao, lakini vinachukulia kama vyenye kujitegemea juu ya kusudi lisilobadilika la nia thabiti ambalo laweza kuongewa kama kitu halisi kilichochukua nafasi: kwa hiyo suluhisho, ahadi, au tamko, hasa lile la ki-Ungu mara nyingi linatamkwa katika njeo ya wakati timilifu” (uk. 17 mf., utimilifu wa kinabii). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anaelezea muundo wa kimaneno kwa namna hii: “...inaiangalia hali kutokea nje, kwa ukamili wake. Kwa namna hiyo kinaelezea ukweli mrahisi, ingawa kinawezakuwa ni kitendo au hali (ukijumuisha hali ya kuwa au fikra). Kinapotumika katika vitendo, mara nyingi inakitazama kitendo kama kilicho kamili toka kwenye hoja ya mzungumzaji mwenye ustadi au msimuliaji (ikiwa ni kamili au sio kamili kwa maana ya uhalisia au ukweli na sio hoja). Utimilifu unaweza kuhusika katika kitendo /hali ya wakati uliopita, uliopo au ujao. Kama ilivyoelezwa hapo juu, muda, ambao unashawishi namna gani mtu anaweza kutafasiri utimilifu kwenda kwenye njeo ya lugha iliyobobea kama Kiingereza, lazima ipimwe toka kwenye muktadha” (uk. 86)
- b. WAKATI USIOTIMILIFU, unaoelezea kitendo kilichoko katika mchakato (kisichotimilifu, chenye kujirudia, chenye kuendelea, au chenye udharura), mara nyingi huenenda kuelekea lengo. Mara nyingi muundo huu ulitumika kwa kitendo cha wakati uliopo na ujao. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema “NYAKATI ZOTE ZISIZOTIMILIFU zinawakilisha hali yakutokukamilika. Zinaweza kuwa ni zenye kujirudia au kuendelea au za dharura. Kwa maneno mengine, au kwa sehemu Fulani inaanza au kiasi Fulani inahakikiwa. Kwa namna zozote katika baadhi ya maana haijamalizika, yaani, haijakamilika” (uk. 55). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anasema “ni vigumu kupunguza kiini cha kutokutimia kwenda dhana moja, kwa vile inajumuisha vyote dhima na dhamira. Muda mwingine wakati usiotimilifu hutumika kwa namna ya kuarifu na kutengeneza maelezo pingamizi. Wakati mwingine inakitazama kitendo zaidi kitegemezi, kama kinadharua, dharura, chenye kuwezekana na nakadharika” (uk. 89)
- c. Neno lililoongezewa *waw*, linalounganisha KITENZI kwenye kitendo cha KITENZI kilichopita
- d. Dhana SHURUTISHI, inayosimamia juu ya uhiari wa mnenaji na kitendo muhimu cha wasikilizaji
- e. Katika Uyahudi ya kale muktadha mpana uliweza kuamua mwelekeo wa muda wa uandishi uliokusudiwa.
- B. Miundo mikuu saba iliyobadilishwa na maana zake. Kiuhalisia miundo hii inatenda pamoja na nyenzake katika muktadha na haipaswi kutengwa
1. *Qal (Kal)*, ni muundo wa kawaida na wa msingi katika miundo yote. Unadokeza kitendo rahisi au hali ya nafsi. Hakuna kisababishi au ulazima uliotumika.
 2. *Niphal*, ni muundo wa pili ulio wa kawaida sana. Mara nyingi huwa katika hali ya KUTENDWA, lakini muundo huu pia hutenda kama wenye kubadilishana na kujirejea. Pia hauna kisababishi au ulazima uliotumika.
 3. *Piel*, muundo huu ni muundo tendaji na huelezea kuhusu kukifanya kitendo kuwa katika hali ya nafsi. Maana ya msingi ya shina la neno *Qal* inajitokeza au kuendelea kwenye hali ya nafsi.
 4. *Pual*, ni neno mfanano TENDWA wa neno *Piel*. Mara nyingi huelezewa kwa KIAMBATA

5. *Hithpael*, ambalo ni shina la kujirejea au kubadilishana. Linaelezea usisitaji wa kitendo au hali ya kudumu ya kitendo kulinganisha na shina la neno *Piel*. Muundo adimu TENDWA unaitwa *Hothpael*.
6. *Hiphil*, ni muundo tendaji wa usababishaji shina tofauti na neno *Piel*. Unawezakuwa na dhana ya ruksa, lakini mara nyingi unarejelea kwenye sababu ya tukio. Ernst Jenni, Mjerumani mwenye asili ya kiebrania mwana sarufi, anaamini kuwa neno *Piel* linadokeza kitu fulani kuja kwa hali ya nafsi, wakati *Hiphil* inaonyesha jinsi inavyotokea.
7. *Hophal*, ni neno mlingano TENDWA kulinganisha na neno *Hiphil*. Haya mashina ya mwisho mawili ndiyo madogo yaliyotumika kati ya yale mashina saba.

Wingi wa habari hii unapatikana toka *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, cha Bruce K. Waltke na M. O'Connor, kur. 343-452

Chati ya kundi na kisababishi chake. Namna moja katika uelewa wa muundo wa KITENZI cha Kiebrania ni kukiangalia chenyewe katika kipengere cha mahusiano ya IRABU. Baadhi ya mashina ya maneno yanatofautiana na mashina ya maneno mengine (yaani *Qal* - *Niphal*; *Piel* - *Hiphil*), chati iliyoonyeshwa hapa chini inajaribu kuangazia kwenye utendaji wa msingi wa mashina ya KITENZI na visababishi vyake.

IRABU au KIIMA LINALOFUATA	HAKUNA KUNDI LINALOFUATA	KUNDI TENDAJI LINALOFUATA	KUNDI TENDEWA
TENDAJI	<i>Qal</i>	<i>Hiphil</i>	<i>Piel</i>
YA KATI TENDWA	<i>Niphal</i>	<i>Hophal</i>	<i>Pual</i>
KUJIREJEA/KUTENDEANA	<i>Niphal</i>	<i>Hiphil</i>	<i>Hithpael</i>

Chati hii imechukuliwa toka katika majadiliano mazuri ya muundo wa kivitenzi katika uelewa wa utafiti wa lugha ya Akkadia (kama vile Bruce K. Waltke, M. O'Conner, *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, ukurasa wa 354-359)

R. H. Kennett, *A Short Account of the Hebrew Tenses*, ametoa onyo lenye kufikirika kuwa muhimu. "mara nyingi nimeweza kuanzisha katika mafundisho, kuwa kiongozi cha wanafunzi kilicho kigumu katika vitenzi vya Kiebrania ni kupata maana iliyoelezewa katika fikra za Waebrania wenyewe; kuwa ndiyo kusema, kuna tabia ya kutoa kwa mwelekeo wa kufanana kwa kila njeo za Kiebrania kama namba fulani ya muundo wa Kilatini au Kiingereza ambapo njeo hiyo mahsusi kwa kawaida yaweza kutafasiriwa. Matokeo ni kushindwa kutofautisha wingi wa hivi vivuri venye maana, ambavyo vinatoa uhai aina hiyo na nguvu kwenye lugha ya Agano la Kale. Ugumu katika matumizi ya vitenzi vya Kiebrania uko tu katika hoja ya mtizamo, kwa hiyo moja kwa moja yanatofautiana na ya kwetu, kutokana na kile Waebrania wanaangalia kitendo; muda wa mambo, ambao pamoja nasi ni upendeleo wa kwanza, kama neno lenyewe, "njeo" linavyoonyesha, kwao kuwa ni chaguo la pili. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa mwanafunzi kwa uwazi aweze kuchukua, sio kwa wingi miundo ya Kilatini au Kiingereza ambayo inaweza kutumika kutafasiri kila njeo za Kiebrania, bali kiasi Fulani dhana ya kila kitendo, kama kilivyowasilishwa katika fikra za Waebrania. Jina la 'njeo' kama lilivyotumika katika vitenzi vya Kiebrania vinapotosha. Kile kinachoitwa 'njeo' za Kiebrania hakielezei muda lakini kwa kidogo hali ya kitendo. Hakika hakikuwekwa kwa ajili ya kuleta mkanganyiko ambao ungaliweza kutokea kupitia matumizi ya neno 'kauli' kwa namna zote mbili ya nomino na vitenzi, 'kauli' zingalikuwa nzuri zaidi kwenye usanifu kuliko 'njeo.' Mara nyingi ni lazima kitu kiwekwe akilini kuwa haiwezekani kutafasiri kitenzi cha Kiebrania kwenda kwenye Kiingereza bila kutumia udhibiti ambao haupo kabisa katika Kiebrania. Waebrania wa mwanzo kamwe hawakufikiria kitendo chaweza kuwa katika wakati uliopita, uliopo na ujao, lakini walifikilia tu kwenye *utimilifu* yaani., kitendo kilichokwisha tendeka, au *kisicho timilifu*, yaani., kama katika njia ya kusonga mbele. Tunaposema kuwa njeo Fulani ya Kiebrania wakati

timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao katika Kiingereza, hatumaanishi kuwa mawazo ya Kiebrania ya hicho kama wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao, lakini tu kuwa lazima itafasiliwe katika Kiingereza.

Wakati wa kitendo Waebrania hawakujaribu kuelezea kwa namna yeyote ya muundo wa kuongea kwa maneno (utangulizi na uk.1). kwa angalizo la pili, Sue Groom, *Linguistic Analysis of Biblical Hebrew*, anatumkumbusha sisi, “hakuna namna ya kuweza kujua ikiwa muundo wa wasomi wa sasa wa elimu maana na uhusiano wa maana katika lugha zilizokufa au kupotea ni taswira ya fikra zao, au lugha zao mama, au maeneo hayo yalikuwepo katika Waebrania wenye hadhi” (uk. 28).

- C. Dhamira (ambazo ni mifanano ilichukuliwa toka kwenye lugha za kimagharibi ya sasa)
1. Imetokea, inaendelea kutokea (NI KAULI ELEKEZI), mara nyingi inatumia njeo WAKATI TIMILIFU au WAKATI UNAOENDELEA (KAULI ZOTE ENDELEVU ziko katika KAULI ELEKEZI).
 2. Itatokea, ingalia tokea (KAULI TEGEMEZI)
 - a. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU ya wazi
 - 1) Zenye KUFUNGAMANA (likiongezewa herufi h), nafsi ya kwanza KAULI ISIOTIMILIFU ambayo mara nyingi huelezea kutakia heri, hitaji, au kutia moyo (yaani., matendo ya hiari ya mzungumzaji)
 - 2) ASILI NA UFAFANUZI ZAIDI WA NENO (badiliko la ndani), mtu wa tatu KAULI ISIOTIMILIFU (inawezakuwa mtu wa pili katika sentensi kanushi) ambayo mara nyingi inaelezea ombi, ruhusa, maonyo, au ushauri
 - b. Hutumia njeo ya WAKATI TIMILIFU ikiwa na *lu* au *lule*. Miundo hii inafanana na sentensi YENYE MASHARTI DARAJA LA PILI katika lugha ya Koine ya huko Uyunani. Maelezo yasiyo sahihi (Kishazi chenye kuelezea tamko ndani ya sentensi yenye masharti) yenye kuleta hitimisho lisilo sahihi (Kishazi kikuu ndani ya sentensi yenye masharti).
 - c. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU na muktadha wa *lu*, vile vile maelekezo wa wakati ujao, kuangalia matumizi ya KAULI TEGEMEZI. Baadhi ya mifano inapatikana kwa J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament* ni Mwa.13:16; Kumb. 1:12; I Fal. 13:8; Zab. 24:3; Isa. 1:18 (kama vile kur. 76-77).
- D. *Waw* – Kinyume chake/yenye matokeo yaliyofuatana/rejeshi. Huu muonekano wa kipekee wa isimu zenye kushughulikia kupanga maneno ya kisarufi ya Kiebrania imeleta mkanganyiko mkubwa kwa miaka mingi. Imetumika kwa namna nyingi mara nyingi ikizingatia juu ya uwasilishaji. Sababu ya mkanganyiko ni wale wasomi wa mwanzo walikuwa watu wa Ulaya na wakajaribu kutafasiri katika ulelewa wa lugha zao za asili. Na hili lililopoonekana kuwa gumu wakaanza kulaumu lugha ya Kiebrania kuwa ni ya zamani, lugha ya kikale. Lugha za Ulaya ni NJEO (za muda) zinazogemea kwenye VITENZI. Baadhi ya namna na madokezo ya visarufi yaliainishwa na herufi WAW ambayo iliongezwa kwenye shina la KITENZI TIMILIFU au KITENZI ISIOTIMILIFU. Hii inabadilisha namna ya kitendo kilivyo tazamwa.
1. Katika simulizi za kihistoria VITENZI vinaunganishwa pamoja katika mfuatano vikiwa na mwongozo wa kawaida
 2. Kiambishi awali cha *waw* kinaonyesha uhusiano maalum kikiwa na KITENZI kilichopita.
 3. Muktadha mpana mara nyingi ni kiini cha uelewa wa mfuatano wa KITENZI. VITENZI vya Kisemiti haviwezi kutathimini utengano. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anaeleza utofauti wa Waebrania katika matumizi ya neno *waw* kabla ya KAULI TIMILIFU na KAULI ISIOTIMILIFU (kur. 52-53). Kama wazo la msingi la KAULI TIMILIFU ni muda uliopita, kuongezeka kwa neno *waw* mara zote linatenda kwa dhana ya wakati ujao. Hili pia ni kweli kwa KAULI ISIOTIMILIFU ambayo wazo lake la msingi ni la wakati uliopo au wakati ujao; kuongezeka kwa neno *waw* lililowekwa katika wakati uliopita. Hili ni badiliko la muda lisilo la kawaida ambalo linaelezea kungezeka kwa neno *waw*, sio kwenye badiliko la maana yake ya msingi ya njeo yenyewe. KAULI TIMILIFU ya neno *waw* inatenda kazi vizuri kwenye unabii, wakati KAULI ISIOTIMILIFU ya neno *waw* inatenda vizuri kwenye simulizi (kur. 54,68). Watts anaendeleza

ufafanuzi wake, “ kwa ajili ya kuonyesha tofauti iliyopo ya msingi kati ya neno *waw* kiunganishi na neno *waw* linalojirudia, utafasiri ufuatao unatolewa:

- 1) Neno *waw* ambalo ni kiunganishi hutokea mara nyingi kuonyesha ufanano.
- 2) Neno *waw* kwa mfululizo linatokea mara zote kuonyesha mwendelezo. Ni muundo pekee wa neno *waw* unaotumika ukiwa na mfululizo wa kauli isiotimilifu. Uhusiano kati ya kauli zisizotimilifu zilizounganishwa nayo yaweza kuwa ni mfuatano wa muda, matokeo ya kimantiki, sababu za kimantiki, au tofauti za kimantiki. Kwa namna yeyote ile kunamfuatano”(uk.103)

E. KITENZIJINA-Kuna aina mbili ya vitenzijina

1. KITENZIJINA CHA MOJA KWA MOJA, chenye “nguvu, kinachojitegemea, kinachoshambulia maelezo yaliyotumika kwa ajili ya matokeo ya kuvutia.....kama kiima, mara nyingi hakina kitenzi kilichoandikwa, kitenzi ‘kuwa” kikiwa kinaeleweka, hakika, neno linabaki kusimama lenyewe wazi,”(J. Wash Watts, *ASurvey of Syntax in the Hebrew Old Testament*,” uk. 92).
2. KITENZIJINA KINACHOJENGA, ambacho “kinahusiana kisarufi kwenye sentensi na vihusishi, viwakilishi milikishi, na uhusiano uliojengeka” (uk.91). J. Weingreen, *A Practical Grammar for Classical Hebrew*, anaelezea hali ya muundo:
“ikiwa maneno mawili (au zaidi) yanaunganikana kwa karibu ambapo kwa pamoja yanatengeneza wazo moja ambatani, neno lenye kujitegemea (au maneno) yanasemekana kuwa katika hali ya muundo.” (uk. 44).

F. VIWAKILISHI VYA KUULIZA

1. Mara zote huonekana kwanza kwenye sentensi.
2. Umuhimu wa kufasiri
 - a. *ha-* haitarajia mwikio
 - b. *halo’-* mwandishi anategemea jibu la “ndiyo”

KAULI HASI

1. Mara nyingi hujitokeza kabla ya maneno yenyewe yanayo kanushwa.
2. Neno mojawapo kanushi ni *lo’*.
3. Neno *al* lina kidokezo cha dharura na hutumika kwa namna ya HALI YA KUSIHI na KAULI AMRISHI.
4. Neno *lebhilti*, linamaanisha “ili kwamba.....sio” linatumika likiwa na VITENZIJINA.
5. Neno *en* linatumika likiwa KAULI ENDELEVU.

G. SENTENSI ZENYE MASHARTI

1. Kuna aina nne ya sentensi zenye masharti ambazo kimsingi zinafanana katika lugha ya Koine ya huko Ugiriki.
 - a. Kitu Fulani kinaonekana kuwa kikitokea au mawazo kama yalivyotimilizwa (DARAJA LA KWANZA katika Kiyunani)
 - b. Kitu Fulani kinyume na ukweli ambacho utimilisho wake hauwezekani (DARAJA LA PILI)
 - c. Kitu fulani ambacho kinawezekana au hata kuonekana kutokea(DARAJA LA TATU)
 - d. Kitu fulani ambacho ni yumkini kutokea, kwa hiyo utimilisho ni agharabu(DARAJA LA NNE)
2. ALAMA ZA VISARUFI
 - a. Vinafikiliwa kuwa kweli au hali iliyopo inatumia KAULI TIMILIFU ELEKEZI au KAULI ENDELEVU na mara zote kishazi kidogo kinatambulishwa kwa
 - 1) *’im*
 - 2) *Ki*
 - 3) *hin* au *hinneh*
 - b. muundu ulio kinyume na ukweli mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU kikiwa na utangulizi wa KIAMBATA *lu* au *lule*
 - c. zaidi muundo wenye uyumkini mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU katika kishazi kidogo, mara zote *’im* au *ki* vinatumika kama kauli ya mwanzo ENDELEVU

- d. Yumkini muundo mdogo hutumia KAULI TEGEMEZI ISIOTIMILIFU katika kishazi kidogo na mara zote *'im ni* utambulisho wa KAULI ENDELEVU.

VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIHI HII

AB	Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman
ABD	Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman
AKOT	Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens
ANET	Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard
BDB A	Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs
IDB	The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick
ISBE	International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr
JB	Jerusalem Bible
JPSOA	The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America)
KB	The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner
LAM	The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa
LXX	Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1970
MOF	A New Translation of the Bible by James Moffatt
MT	Masoretic Hebrew Text
NAB	New American Bible Text
NASB	New American Standard Bible
NEB	New English Bible
NET	NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition
NRSV	New Revised Standard Bible
NIDOTTE	New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren
NIV	New International Version
NJB	New Jerusalem Bible
OTPG	Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith
REB	Revised English Bible
RSV	Revised Standard Version
SEPT	The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1970
TEV	Today's English Version from United Bible Societies
YLT	Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young
ZPBE	Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney

NENO TOKA KWA MWANDISHI: NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni wetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

Kanuni ya Kwanza

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

Kanuni ya Pili

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafasiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtizamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara, kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua, kueleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafasiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafasiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumiya nadharia mbalimbali za tafasiri.

- A. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.

- B. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
- C. Toleo Today's English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS⁴ na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
- D. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
- E. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

Kanuni ya Tatu

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Kanuni ya Nne

Kanuni ya nne ni kutazama juu ya uwasilishajiwa fasihi. Waandishi wa mwanzo waliovuviwa hchagua kuandika kuandika jumbe katika miundo tofauti (mf.usimuliaji wa kihistoria, tamthiliya za kihistoria, ushairi, unabii, injili (fumbo, walaka, matukio ya kmafunuo). Miundo hii tofauti ina aina maalum a utafsiri (tazama Gordon Fee and Doug Stuart, *How to Read the Bible for All Its Worth*, D. Brent Sandy and Ronald L. Giese, Jr., *Cracking Old Testament Codes*, or Robert Stein, *Playing by the Rules*)

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumaliza, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving'ang'anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
East Texas Baptist University
Juni 27, 1996

MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA: UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOHIBITIKA

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa. Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihita digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliunganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko. Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtazamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru, lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:

I. Dhahanio


- A. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.

- B. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya nje mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
- C. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
- D. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
1. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
 2. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
 3. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
 4. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
 5. Umbo la kisarafu husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
 6. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe
 7. Vifungu vinavyofanana


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

II. Mbinu zisizofaa

- A. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
- B. Kutoujali muundo wa ki-historia wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
- C. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
- D. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
- E. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:



Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya “mwitikio wa msomaji” (unamaanishwa nini kwangu). Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: “Biblia inaangazia zaidi katika fasihi”. Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao.

Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. uandishi wa awali
 - a. muundo wa kihistoria
 - b. mazingira ya fasihi
2. uchaguzi wa mwandishi wa awali
 - a. muundo wa kisarufi (vipashio)
 - b. matumizi ya maneno ya kisasa
 - c. aina ya uwasilishaji
3. uelewa wetu ulio sahihi
 - a. vifungu nuhimu vyenye kufanana

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasihi wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasihi ufuatao:

A. Mzunguko wa kwanza wa usomaji

1. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti, kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
 - a. Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
 - b. Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
 - c. Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
2. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
3. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
4. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
 - a. Agano la kale
 - 1) Simulizi za waebrania
 - 2) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
 - 3) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
 - 4) Alama za siri za ki-sheria

- b. Agano jipya
 - 1) Simulizi (Injili, matendo)
 - 2) Hadithi za mafumbo (Injili)
 - 3) Barua/nyaraka
 - 4) Fasihi za mafunuo

B. Mzunguko pili wa usomaji

1. Soma kitabu kizima tena, ukitaftuta kufahamu mada muhimu au masomo.
2. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
3. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

C. Mzunguko wa tatu wa usomaji.

1. Soma tena kitabu kizima, ukitaftuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
2. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
 - a. Mwandishi
 - b. Tarehe
 - c. Wapokeaji
 - d. Kusudu mahsusi la uandishi
 - e. Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
 - f. Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
3. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha Biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
4. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

D. Mzunguko wa nne wa usomaji

1. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
 - a. Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
 - b. Mwenendo linganifu (TEV, JB)
 - c. Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
2. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
 - a. Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
 - b. Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
 - c. Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
3. Taja vipengele vifuatavyo:-
 - a. Istilahi muhimu
 - b. Istahili zisizo za kawaida
 - c. Muundo muhimu wa kisarufi
 - d. Maneno magumu, ibara, na sentesi
4. Angalia njia muhimu zilizosambamba
 - a. Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
 - 1) Vitabu vya thiolojia
 - 2) Biblia za marejeo
 - 3) Itifaki
 - b. Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.

- c. Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.
5. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
- a. Soma biblia
 - b. Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
 - c. Tangulizi za biblia
 - d. Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

iv. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama “uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi”. Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!

Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema “asema Bwana” lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni “zetu” na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Biblia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

v. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

- A. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
- B. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
- C. Omba kwa ajili ya shauku kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1 na kuendelea)
- D. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
- E. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

- A. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*, kr. 17-18
“Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa

kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni.”

- B. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti)* Uk.75:

Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.

- C. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:

Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ie hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

VI. Njia hizi za Fasihi

Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

- A. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya “mduara wa usomaji #3” angalia taarifa hizi.
- B. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
- C. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
1. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
 2. The New King James Version (NKJV)
 3. The New Revised Standard Version (NRSV)
 4. Today's English Version (TEV)
 5. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa “mada ya sentensi” au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

- D. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
1. Mazingira ya fasihi
 2. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
 3. Habari za kisarufi
 4. Usomaji wa neno
 5. Njia muhimu zilizo sambamba

- E. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
1. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswada wa “Upokeaji wa Maandiko halisi”.
 2. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
 3. The Today’s English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
 4. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
- F. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
1. Tofauti za mswada
 2. Maana ya maneno mbadala
 3. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
 4. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho.
- G. Karibia na kila sura maswali muhimu ya kujadiliana yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya kutafsiri katika sura hiyo.

UTANGULIZI WA KITABU CHA KUMBUKUMBU LA TORATI

I. UMUHIMU WAKE

- A. Ni mojawapo kati ya vitabu vinne vya Agano la Kale chenye kurejelewa mara kwa mara katika Agano Jipya (yaani, Mwanzo, Kumbu kumbu la Torati, Zaburi, na Isaya). Kitabu cha Kumbu Kumbu cha Torati kimerejelewa mara 83
- B. Rejeo toka kwenye mtiririko wa fasiri za Agano la Kale la mwanazuoni Tyndale, “Kumbukumbu la Torati” na J.A.Thompson:
“Kumbukumbu la Torati ni moja kati ya vitabu vikubwa vya Agano la Kale. Ushawishi wake juu ya dini za asili na mtu binafsi kwa kipindi chote hakijawahi kupitwa na kitabu kingine chochote katika Biblia” (uk. 11)
- C. Hiki chawezakuwa ni mojawapo ya kitabu pendwa cha Yesu kwenye vitabu vya Agano la Kale:
1. Alikirejelea mara kadhaa pindi alipojalibiwa na shetani akiwa nyikani
 - a. Mt. 4:4; Lk 4:4 – Kumb. 8:3
 - b. Mt. 4:7; Lk 4:12 –Kumb. 6:26
 - c. Mt. 4:10;Lk 4:8 –Kumb. 6:13
 2. Yumkini ni maelezo baada ya ile hotuba ya kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7)
 3. Yesu alirejelea kwenye Kumbukumbu la Torati sura ya 6:5 kama amri iliyo kuu (kama vile Mt. 22:34-40; Marko 12:28-34; Lk. 10:25-28).
 4. Yesu aliirejelea hii sehemu ya Agano la Kale (Mwanzo-Kumbukumbu la Torati) mara kadhaa kwa sababu wale Wayahudi wa enzi zake waliamini ni moja ya kipengere chenye mamlaka kwenye sheria za kanisa.
- D. Huu ni mojawapo ya mfano mkubwa katika maandiko wa kuutafasiri upya ufunuo wa Mungu uliopita kwenye hali mpya. Moja ya mfano huu ungalikuwa ni tofauti ndogo iliyopo kati ya amri kumi katika kitabu cha Kutoka 20:11 dhidi ya Kumbukumbu la Torati 5:15. Kutoka 20 ilitolewa kwenye Mlima Sinai na kuongelea kile kipindi cha kutangatanga nyikani na Kumbukumbu la Torati 5 lilitolewa kwenye nyanda za Moabu likiwaandaa watu kwenye maisha ya kimakazi kule Kanani.
- E. Kumbukumbu la Torati ni mtiririko wa jumbe zilizotolewa na Musa kwenye nyanda za Moabu (Mashariki mwa Yordani). Hotuba zote tatu zilianza na kupaita jina mahali halisi kwenye hotuba zake. Hotuba zote zawezakuwa zinarejelea sehemu ile ile.
1. “ng’ambo ya Mto Yordani katika nyika, huko Araba inayotazamana Sufu, kati ya Parani na Tofeli na Labani na Hazarothi na Dizahabu,” 1:1
 2. “Ng’ambo ya Yordani katika nchi ya Moabu,” 1:5
 3. “ng’ambo ya Yordani, katika bonde linalotazamana na Beth-peor, katika nchi ya Mfalme Sihoni,” 4:46
 4. “katika nchi ya Moabu,” 29:1
- F. Kumbukumbu la Torati pia ni kiini cha mjadala uliopo siku za leo kati ya wanazuoni wa Agano la Kale kuhusiana na kuanza kwake kiuhalisia. Utafiti wa leo umegawanyika juu ya nadharia kuhusiana na utungo wa vitabu vyote vya Kumbukumbu la Torati na vile vitabu vitano vya Musa.

II. JINA LA KITABU

- A. Katika Kiebrania majina ya vitabu vya *Tonakh* (vitabu vitano vya Musa) ni mojawapo ya yale maneno kumi ya mwanzo, mara nyingi ndilo neno lao la mwanzo:
1. Mwanzo, “hapo mwanzo”
 2. Kutoka, “na haya ndiyo majina yake”
 3. Mambo ya Walawi, “na akaitwa”
 4. Hesabu, “katika jangwa”
 5. Kumbukumbu la Torati, “na haya ndiyo maneno”
- B. Katika buku la sheria za Kiyahudi kitabu cha Kumbukumbu la Torati huitwa “urudiaji wa sheria” (*Mishnah Hattorah* toka Kumb. 17:18)

- C. Katika tafasiri ya Kiyunani ya Agano la Kale, iitwayo LXX, iliyoandikwa mnamo mwaka wa 250 K.K, Kumbukumbu la Torati huitwa “amri ya pili” kwa sababu ya kutafasiriwa visivyo kwa 17:18 (yaani., “fatisha nakala ya sheria hii”).
- D. Tunalipata jina letu la Kiingereza toka kwenye toleo la Kilatini la Jerome ambalo huita “amri ya pili” (Deutronomium).
- E. Ni kitabu cha maelekezo namna ya kulitunza agano la Mungu
 - 1. “kitabu hiki cha sheria,” 28:61
 - 2. “sheria hii,” 1:5; 4:8; 17:18,19; 27:3,8,26
 - 3. Vifungu vingine vya maelezo, 4:1,45; 6:17,20; 12:1

III. **URASIMISHAJI-** Hiki ni kitabu cha kuhitimisha kwenye vitabu vitano vya Musa ambacho kinaunda moja ya migawanyo mitatu ya sheria za Kiebrania

- A. Torati au sheria –Mwanzo –Kumbukumbu la Torati
- B. Manabii :
 - 1. Manabii wa mwanzo-Yoshua-Wafalme (isipokuwa Ruthu)
 - 2. Manabii waliofuatia- Isaya-Malaki (Danieli na Maombolezo)
- C. Maandiko:
 - 1. Megilloth (vitabu 5 vya Agano la Kale)
 - a. Wimbo ulio bora
 - b. Mhubiri
 - c. Ruthu
 - d. Maombolezo
 - e. Esta
 - 2. Danieli
 - 3. Vitabu vya hekima
 - a. Ayubu
 - b. Zaburi
 - c. Mithari
 - 4. Mambo ya Nyakati

IV. **NAMNA YA UWASILISHAJI**

- A. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati ni mchanganyiko wa uwasilishaji mbalimbali
 - 1. Simulizi za kihistoria
 - a. Sura ya 1-4
 - b. Sura ya 34
 - 2. Uhimizaji –sura ya 6-11
 - 3. Miongozo, sura ya 12-28
 - 4. Zaburi/tenzi za rohoni/nyimbo-sura 32
 - 5. Mibaraka –sura 33
- B. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati kinajielezea chenyewe kama kitabu cha mwongozo toka kwa YHWH kwa ajili ya uzima (Torati) katika 29:21; 30:10; 31:26. Ni kitabu chenye kufundisha kuhusu imani na maisha tutakayoishi kwenye vizazi vijavyo.
- C. Mafunuo ya Mungu yaliyoandikwa huwa mbadala wa kiongozi maalum wa Ki-Mungu . viongozi binafsi wao watabaki, lakini ufunuo ulioandikwa unasisitizwa kama wenye mamlaka.

V. **UANDISHI**

- A. Tamaduni za Kiyahudi
 - 1. Tamaduni za kale zinakubaliana kuwa mwandishi alikuwa ni Musa.
 - 2. Hili limeelezewa katika:
 - a. Talmud-*Baba Bathra* 14b

- b. *Mishnah*
 - c. Hekima ya Yoshua Bin Sira 24:23 (kilichoandikwa mnamo mwaka 185 K.K)
 - d. Filo wa Iskanderia
 - e. Flavia Yosefati
3. Maandiko yenyewe:
- a. Waamuzi 3:4 na Yoshua 8:31
 - b. Musa akanena
 - 1) Kumb. 1:1,3
 - 2) Kumb. 5:1
 - 3) Kumb. 27:1
 - 4) Kumb. 29:2
 - 5) Kumb. 31:1,30
 - 6) Kumb. 32:44
 - 7) Kumb. 33:1
 - c. "YHWH akanena na Musa"
 - 1) Kumb. 5:4-5,22
 - 2) Kumb. 6:1
 - 3) Kumb. 10:1
 - d. "Musa akaandika":
 - 1) Kumb. 31:9,22,24
 - 2) Kut. 17:14
 - 3) Kut. 24:4,12
 - 4) Kut. 34:27-28
 - 5) Hes. 33:2
 - e. Yesu anarejelea au kudokeza toka Kumbukumbu la Torati na kunena "Musa akasema"/ Musa akaandika":
 - 1) Mt. 19:7-9; Mk. 10:4-5-Kumb. 24:1-4
 - 2) Mk. 7:10-Kumb. 5:16
 - 3) Lk. 16:31; 24:27,44; Yh 5:46-47; 7:19,23
 - f. Paul anadai kuwa Musa ndiye mwandishi:
 - 1) Rum. 10:19-Kumb. 32:21
 - 2) 1 Kor. 9:9-Kumb. 25:4
 - 3) Gal. 3:10-Kumb. 27:26
 - 4) Mdo. 26:22; 28:23
 - g. Petro anadai kuwa Musa ndiye mwandishi katika hotuba zake za Kipentekoste-Mdo. 3:22
 - h. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anadai kuwa Musa ndiye mwandishi-Ebr. 10:28; Kumb. 17:2-6
- B. Utafiti wa sasa
1. Wengi wa wanathiolojia wa karne ya 18 na 19, wakiifuata nadharia ya Graf-Wellhausen ya uandishi mbalimbali (JEDP), wanadai kuwa kitabu cha Kumbukumbu la Torati kiliandikwa na kuhani/nabii kipindi cha utawala wa Yoshua huko Yuda kuunga mkono mabadiliko ya kiroho aliyoyafanya. Hili lingalimaanisha kuwa kitabu kiliandikwa katika jina la Musa mnamo mwaka wa 621 K.K.
 2. Hili lilisimamia juu ya:
 - a. 2 Fal. 22:8; 2 Nya.34:14-15, "nimekipata kitabu cha sheria katika nyumba ya Bwana"
 - b. Sura ya 12 inajadali eneo moja kwa ajili Hema na baadaye Hekalu
 - c. Sura ya 17 inajadili mfalme ajaye
 - d. Ukweli kwamba kukiandika kitabu kwa kutumia jina la mtu maarufu tokea huko nyuma lilikuwa jambo la kawaida katika Masharika ya Karibu ya Kale na katika mazingira ya Kiyahudi
 - e. Ufanano wa mtindo, misamiati na sarufi kati ya Kumbukumbu la Torati na Yoshua, Wafalme na Yeremia

- f. Kumbukumbu la Torati linaandika juu ya kifo cha Musa (sura ya 34)
 - g. Udhahili wa matoleo mengine ya kihariri katika vitabu vitano vya Musa:
 - 1) Kumb. 3:14
 - 2) Kumb. 34:6
 - h. Wakati mwingine namna mbalimbali isioelezeka katika utumiaji wa majina ya Uungu: El, El Shaddai, Elohim, YHWH, dhahili katika muktadha wa pamoja na vipindi vya kihistoria.
- C. Pana baadhi ya matoleo ya kihariri yaliyo dhahili. Waandishi wa Kiyahudi waliojifunzia huko Misri ambapo mara kwa mara waliyaboresha maandiko ya kale. Waandishi wa huko Mesopotamia hawakupenda kuongeza kitu chochote.
- Baadhi ya mifano katika Kumbukumbu la Torati ni:
- 1. 27:3,8
 - 2. 28:58
 - 3. 29:21,29
 - 4. 30:10,19
 - 5. 31:24

VI. TAREHE

- A. Kama kiliandikwa na Musa kuna uwezekano mwingine unaohusiana na muda na kipindi cha kutoka kule Misri.
- 1. Kama 1 Fal. 6:1 inamaanisha kuchukuliwa kifasihi hivyo ni mnamo mwaka wa 1445 K.K (karne ya 18 ya utawala wa Thutmose III na Amenhotep II):
 - a. Tafasiri ya agano la Kale la Kiebrania ina miaka 440 badala ya miaka 480
 - b. Hesabu hii yaweza kuaksi kizazi na wala sio miaka (kiuwakilishi)
 - 2. Ushuhuda wa elimu kale mnamo mwaka wa 1290 K.K kwa ajili ya wana wa Israel kutoka utumwani (utawala wa Kimisri karne ya 19):
 - a. Sethi I (1390-1290) aliuondoa mji mkuu wa Misri toka Thebe kwenda eneo la Delta-Zoan/Tanis.
 - b. Ramese II (1290-1224):
 - 1) Jina lake lilitokea katika mji uliojengwa na watumwa wa Kiebrania (kama vile Mwa. 47:11; Kut. 1:11)
 - 2) Alikuwa na mabinti 47
 - 3) Mwanae wa kwanza hakufanikiwa kufanya vizuri kama ilivyotarajiwa
 - c. Miji yote mikubwa ya Palestina iliyozungushiwa kuta iliagamizwa na kwa haraka ikajengwa tena mnamo mwaka wa 1250 K.K
- B. Nadharia za utafiti wa leo za uandishi mbalimbali:
- 1. J (YHWH) 950 K.K
 - 2. E (Elohim) 850 K.K
 - 3. JE (muunganikano wa hizo za mwanzo) 750 K.K
 - 4. D (Kumbukumbu la Torati) 621 K.K
 - 5. P (Makuhani) 400 K.K

VII. VYANZO VINGINE VYA KUTHIBITISHA MUUNDO WA KIHISTORIA

- A. Mikataba ya Wahiti ya Millenia ya 2 K.K inatupatia mfanano uliopo kihistoria kwenye muundo wa Kumbukumbu la Torati (vile vile pia kitabu cha Kutoka-Mambo ya Walawi na Yoshua 24). Mpangilio wa mkataba huu ulibadilika kwenye Millenia ya 1 K.K. Hili linatupatia ushahidi kwa ajili ya historia ya kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Kwa usomaji zaidi katika eneo hili, tazama G.E. Mendenhall's *Law and Covenants in Israel and the Ancient Near East* and M. G. Kline, *Treaty of the Great King*.
- B. Mpangilio wa Wahiti na Kumbukumbu la Torati unafanana:
- 1. Utangulizi wake (Kumb. 1:1-5, utangulizi wa mnenaji, YHWH) statement
 - 2. Tathimini ya matendo ya nyuma ya mfalme (Kumb. 1:6-4:49, matendo ya Mungu yaliyokwisha pita juu ya Israel)

3. Maneno yaliyotumika katika mkataba (Kumbukumbu la Torati 5-26)
 - a. Kwa ujumla (Kumbukumbu la Torati 5-11)
 - b. Kwa uainisho (Kumbukumbu la Torati 12-26)
4. Matokeo ya mkataba (Kumbukumbu la Torati 27-29):
 - a. Faida zake (Kumbukumbu la Torati 28)
 - b. Hasara zake (Kumbukumbu la Torati 27)
5. Ushuhuda wa miungu (Kumb. 30:19; 31:19, pia 32, wimbo wa Musa ulitumika kama ushahidi):
 - a. Nakala ya mkataba iliwekwa ndani ya Hekalu mlimo na miungu
 - b. Nakala nyingine iliwekwa ndani ya hekalu la mtumishi ili kusomwa kila mwaka
 - c. Utofauti wa mikataba ya Wahiti toka kwa ile ya Waashuru na ile ya Syria ilikuwa:
 - 1) Mtazamo wa kihistoria wa matendo yaliyopita ya mfalme
 - 2) Fungu la laana lilikuwa halisomwi sana
- C. Mpangilio wa mkataba wa Wahiti kwa kiasi kidogo ulibadilishwa (kipengere kimojawapo kiliondolewa) katika Millenia ya kwanza K.K. Muundo wa Kumbukumbu la Torati unaendana na kipindi cha Musa na Yoshua kwa ufasaha!
- D. Kwa ajili ya mjadala mzuri wa mikataba hii ya Wahiti tazama K. A. Kitchen, *Ancient Orient and Old Testament*, kur. 99-102.

VIII. **VIPENGELE VYA KIFASIHI** (muktadha)

- A. Utangulizi wa kitabu, 1:1-5
- B. Hotuba ya mara ya kwanza, 1:6-4:43 (matendo ya YHWH yaliyopita kwa ajili ya siku za leo)
- C. Hotuba ya mara ya pili 4:44-26:19 (sheria ya YHWH kwa ajili ya leo na siku zote)
 1. Kwa ujumla- amri kumi za Mungu (5-11)
 2. Mifano ainishi na matumizi yake (12-26)
- D. Hotuba ya mara ya tatu, 27-30 (sheria ya YHWH kwa ajili ya siku za mbeleni 27-29)
 1. Laana (27)
 2. Mibaraka (28)
 3. Kufanywa upya kwa agano (29-30)
- E. Maneno ya mwisho ya Musa, 31-33
 1. Hotuba ya “kuwaaga”, 31:1-29
 2. Wimbo wa Musa, 31:30-32:52
 3. Mibaraka ya Musa 33:1-29

IX. **KWELI KUU**

- A. Maandalizi ya mwisho kabla ya kuingia katika nchi ya ahadi. Agano la Mungu na Abraham (Mwanzo 15) limekwisha kutimilizwa!
- B. Mwanzo 12:1-3 inaahidi nchi pamoja na uzao. Agano la Kale linaangazia juu ya nchi; agano jipya litaangazia juu ya “uzao” (kama vile Wagalatia 3).
- C. Musa aliwaanda watu kwa ajili ya maisha ya ukulima dhidi maisha ya ufugaji. Alibadili agano la Mlima Sinai kwa ajili ya nchi ya ahadi. Kwa maana hiyo Kumbukumbu la Torati ni katiba ya Israel.
- D. Kitabu kinasisitiza juu ya uaminifu wa Mungu wakati uliopita, wa sasa, na ujao. Ingawa, agano ni lenye kuamuru, Israel ni sharti iitikie na iendelee katika imani, toba na utii. Ikiwa hatatenda laana ya sura ya 27-29 itakuja kuwa kweli. Musa ni mfano halisi wa upendo wa Mungu na haki! Hata kiongozi wa kipekee wa Mungu anawajibika kwa ajili ya kutii. Ukaidi mara zote huwa na madhara!

KUMBUKUMBU LA TORATI 1

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA*			
NKJV	NRSV	REV	NJB
Amri ya mwanzo ya kuingia Kanaani (1:1-4:43)	Uhakiki wa kihistaoria	Utangulizi	Hotuba ya kwanza ya Musa
1:1-8	1:1-5	1:1-5	Muda na mahali 1:1-3 1:4-5 Maelekezo ya mwisho
pale Mlima Horebu	1:6-8	1:6-8	1:6-8
Viongozi wa kikabila Wachaguliwa		Musa anawateua waamuzi	
1:9-18	1:9-18	1:9-15 1:16-18	1:9-18
Kukataa kwa Israeli kuingia Katika nchi	1:19-21	Wapelelezi wanaondolewa toka Kadesh Barnea	Kadesh: Waisraeli wanapoteza imani
1:19-25	1:19-21	1:19-21	1:19-28
	1:22-25	1:22 1:23-25	
1:26-33	1:26-33	1:26-28 1:29-33	1:29-33
Adhabu kwa ajili ya uasi Wa Israeli		Bwana anaiadhibu Isareli	Maelekezo ya Yahweh huko Kadesh
1:34-40	1:34-40	1:34-38 1:39-40	1:34-40
1:41-46	1:41-45	1:41 1:42-45	1:41-46

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Taz. uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu nimwongozokwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari. Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1:1-5

¹ Haya ndiyo maneno Musa aliyowaambia Israeli wote ng'ambo ya Yordani barani, katika Araba lililoelekea Sufu, kati ya Parani, na Tofeli, na Labani, na Hazerothi, na Dizahabu. ² Ni mwendo wa siku kumi na moja kutoka Horebu kwa njia ya mlima wa Seiri mpaka Kadesh-barnea. ³ Ikawa mwaka wa arobaini, mwezi wa kumi na moja, siku ya kwanza ya mwezi, Musa akawaambia wana wa Israeli kama yote aliyopewa na Bwana ya kuwaamuru; ⁴ alipokwisha kumpiga Sihoni mfalme wa Waamori, aliyekuwa akikaa Heshboni, na Ogu mfalme wa Bashani, aliyekuwa akikaa Ashtarothi iliyo katika Edrei; ⁵ ni ng'ambo ya Yordani katika nchi ya Moabu, alipoanza Musa kufunua torati hii, akisema,

1:1 “Haya ndiyo maneno” Jina hili la kitabu ni la Kiebrania. KITENZI cha Kiebrania cha neno “akawaambia” (BDB 180, KB 210, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) NI KISHAMIRISHO kwenye NOMINO ya neno “maneno” (BDB 182). Kwa sababu kitabu chenyewe kinasema kuwa haya ni maneno ya Musa, ninaamini kuwa hili halijumuishi uwezekano wa kwamba kazi yote hii ni ya ya mhariri, au mtungaji. Kiukweli tuna maneno ya Musa, ambayo kiuhalisia ni maneno ya YHWH (mf., 7:4; 11:13-14; 17:3; 29:6). Hili sio kusema kwamba hakuna baadhi ya matoleo ya kihariri au kwamba Musa anashuhudia kifo chake. Lakini wingi wa nyezo na thiolojia unamhusu Musa.

Vifungu vinavyofanana vinaonekana kukigawa kitabu cha Kumbukumbu la Torati katika vipengere kadhaa:

1. “Haya ndiyo maneno,” 1:1 (1:1-5, utangulizi kwenye hotuba ya mara ya kwanza)
2. “Hii ndiyo sheria,” 4:44 (4:44-49, utangulizi kwenye hotuba ya mara ya pili)
3. “Hii ndiyo amri,” 6:1
4. “Haya ndiyo maneno ya agano,” 29:1 (mwanzo wa hotuba ya mara ya tatu)
5. “Hii ndiyo mibaraka,” 33:1

Wakati nikitoa maoni juu ya suala lenye mkanganyiko la uandishi/tarehe, ngoja nieleze kwa wazi kuwa ninaamini kuwa maaandiko yote yamevuvuwa (k.v. II Tim. 3:15-17). Suala la uandishi na tarehe ni suala la kanuni za kiufasiri, na sio suala la uvuvio! Roho Mtakatifu ni mwandishi wa Kiungu wa maandiko yote ya sheria za kanisa. Je hili ni dhanio la kabla? La hasha! Lakini ni dhahania muhimu, ambalo linatakiwa kupitiwa upya na kusomwa kabla ya ufafanuzi wowote wa maandiko kuthibitisha. Maandiko yenye uvuvio na urasimishaji ni nguzo pacha ambapo mamlaka ya Kibiblia inakaa!

☑ **“Musa aliyowaambia”** Palikuwepo na kundi kubwa la watu waliobaki huko Misri wakiwa na Musa na ingalikuwa haiwezekani kimwili kwake yeye kuweza kusema nao kwa wakati mmoja. Yumkini alizungumza na viongozi na wakayarudia waliyoambiwa kwenye makundi madogo au hii kifasihi ni njia ya kumaanisha walaka ulioandikwa.

☑ **“Israel wote”** Tazama Mada Maalum hapa chini

MADA MAALUM: ISREALI (JINA LAKE)

- I. Maana ya jina lenyewe haijulikani (BDB 975)
 - A. *El*/Stahimili

- B. Na *El* Tustahimili (KITENZI AMRISHI)
 - C. *El* kuitunza
 - D. Na *El* Tushindane
 - E. *El* Shindana
 - F. Yeye ashindanaye na Mungu (neni la mzaha Mwa. 32:28)
 - G. mwenye kutegemewa (IDB, juzuu 2, uk. 765)
 - H. Iliyofanikiwa
 - I. Yenye furaha
- II. Matumizi yake katika Agano la Kale
- A. Ni jina la Yakobo (mchukua nafasi ya mwingine, mshika kisigino, BDB 784, k.v. Mwa. 25:26) linabadilishwa baada ya kushindana na mtu mweleka katika mto Yaboki (k.v. Mwa. 32:22-32; Kut. 32:13). Mara nyingi maana ya majina ya Kiebrania ni majina ya utani, na wala si asili ya neno (k.v. Mwa.32:28). Israel likajakuwa jina lake (mf., Mwa. 35:10; 32:13).
 - B. Likajakuwa likitumika kama jina la pamoja kwa wanawe wote kumi na wawili (mf., Mwa. 32:32; 49:16; Kut. 1:7; 4:22; 28:11; Kumb. 3:18; 10:6).
 - C. Likajateuliwa kuwa taifa lililoundwa na makabila kumi na mawili kabla ya kukimbilia uhamishoni (k.v. Mwa. 47:27; Kut. 4:22; 5:2) na baadaye (k.v. Kumb. 1:1; 18:6; 33:10).
 - D. Baaada ya kuunganisha utawala wa Sauli, Daudi, na Suleimani makabila yaligawanyika chini ya Rehoboamu (k.v. I Fal. 12).
 1. tofauti ilianza hata kabla ya kugawanyika rasmi (mf., II Sam. 3:10; 5:5; 20:1; 24:9; I Fal. 1:35; 4:20)
 2. waliyachagua makabila ya Kaskazini mpaka pale anguko la Samaria kwa Ashuru lilipotokea katika mwaka wa 722 K.K. (k.v. II Fal. 17)
 - E. Lilitumiwa na Wayuda kwenye baadhi ya maeneo (mf., Isaya 1; Mika 1:15-16).
 - F. Baada ya kuchukuliwa mateka huko Ashuru na Babeli likajakuwa tena ni jina la pamoja kwa ajili ya kizazi chote cha Yakobo (mf., Isa. 17:7,9; Yer. 2:4; 50:17,19).
 - G. Lilitumiwa na watu wa kawaida kuleta mkanganyiko toka kwa makuhani (k.v. I Nya. 9:2; Ezra 10:25; Neh. 11:3).

☐“**Ng’ambo ya Yordani**” Yumkini hili linamaanisha “katika eneo la” (BDB 719). Sentensi mbili zinazofuata ni zenye kuainisha mahali pa kijiografia palipokuwa kambi ya Israel wakati Musa alipowapa huu ufunuo. Limekujakuwa nahau kwa ajili ya (1) eneo mashariki ya Yordani (k.v. Hes. 35:14; Kumb. 1:1,5; 4:41,46,47,49) na (2) eneo la Magharibi (k.v. Kumb. 3:20,25; 11:30; 9:1). Linahitaji vifungu vingine kuelezea kando ya Mto inamaanisha nini (k.v. R. K Harrison, *Introduction to the Old Testament*, kur. 636-638).

☐“**barani**” Hii sio sehemu ya jangwa bali ni eneo la nchi lililokuwa la makazi (BDB 184), ambalo ni kame kipindi chote cha mwaka isipokuwa kipindi cha baridi na mwanzoni mwa majira ya kipupwe.

☐“**Araba**” Kiuhalisia huu ni “uwanda mkavu” (BDB 787). Hili linarejelea ukingo wa mto Yordani (yaani., Bonde la Ufa) ambalo linaelekea mpaka Bahari ya Galilaya kwenye ghuba ya Agaba (hasa tokea Uturuki mpka Msumbiji). Hivyo, linarejelea eneo lote la Kusini (matumizi ya leo) na upande wa Kaskazini mwa Bahari ya Chumvi na hatuna uhakika kamili ni upande upi unamaanishwa. Laweza kurejelea Mashariki mwa ukingo wa mto Yordani (k.v. 3:17; 4:49) au ukingo wa Magharibi (k.v. 11:30). Mstari wa 1ni muhtasari wa safari ndefu ya Waisraeli toka Misri kwenda Sinai.

☐“**Sufu**” Hili (ni neno la Kimisri lililokopwa) kiuhalisia ni neno “mafunjo” (BDB 693). Hili laweza kurejelea au kwenye mimea ya maji chumvi (k.v. Yona. 2:5) au zaidi mimea ya maji baridi (k.v. Kut. 2:5). Hapa laweza kutafasiriwa kama “eneo la mafunjo” au mji wa Sufu na waweza kuhusiana na mst. 40 (yaani., Bahari ya Shamu kiuhalisia ni, “bahari yenye mafunjo”).

☐“**Parani**” Neno “parani” (BDB 803) laweza kurejelea eneo la nyika ambalo lilikuwa upande wa Kaskazini mwa nyika ya Sinai, lakini Kusini mwa nyika ya Yudea (k.v. Hes. 13:3,26). Chemichemi ya Kadesh-Barnea ilipatikana katika eneo hili la nyika. Tazama Mada Maalum katika 2:1. Hata hivyo, katika mstari huu neno Parani linaonekana kutojulikana mahali lilipo (yumkini ni mji) upande wa mashariki wa kingo za mto Yordani.

☐“**Tofeli**” Neno lenyewe linamaanisha “chokaa” (BDB 1074). Hii ni sehemu isiojulikana, lakini inavyoonekana ni pande za mashariki mwa Yordani kwenye eneo la Moab.

☐“**Labani**” Neno linamaanisha “kitu cheupe” (BDB 526 III). Hii ni sehemu isiojulikana. Baadhi ya wanazuoni wanaitaja hii sehemu kuwa kwenye njia itokayo Sinai kuelekea Moabu (Libna ya Heb. 33:20-21), wakati wengine wasema ni mji ulioko mashariki mwa kingo za mto Yordani huko Moabu.

☐“**Hazerothi**” Ni jina la mahali hapa (BDB 348) ambalo limesababisha wazuoni wengi kudai kuwa mahali palitajwa baada ya “Araba” ni mahali penye kambi ya Israel kati ya Mlima Sinai na nyanda za Moab (k.v. 1:2). Kama ndivyo, Labani ingalikuwa Libna (k.v. Hes. 33:20-21) na Hazerothi ingalirejelea kwenye Hes. 33:17-18. Hapa palikuwa ni mahali ambapo Aroni na Miriam waliuwawa baada ya kwenda kinyume na uongozi wa Musa au ndoa mpya aliyofunga na mwanamke wa Kikushi (k.v. Hesabu 12).

☐“**Dizahabu**” Jina hili (ni muunganikano na Kiarama lenye maana ya “mahali pa” na Kiebrania “dhahabu”) likimaanisha “mahali penye dhahabu” (BDB 191). Walimu wa sheria walilihusianisha hili kwa Misri walipowapa Wayahudi dhahabu pindi walipokuwa wakiondoka Misri (k.v. Kut. 3:22; 11:2; 12:35), lakini kimuktadha, hili lilikuwa ni jina la mahali. Mahali penyewe hapajulikani. Huenda ni (1) Mashariki mwa kingo za Yordani huko Moab na hivyo karibia na sehemu zingine zilizotajwa au (2) kwenye uelekeo wa Mlima Sinai kwenda Moab.

1:2 “ni mwendo wa siku kumi na moja kutoka Horebu. . .Kadesh-barnea” Mstari huu wawezakuwa ni ufupisho wa harakati zote za Waisrael toka Mlima Horebu/Sinai kuelekea chemichemi za Kadesh, lakini kama ndivyo, hauendani vizuri na mistari ya 1 na 3. Hili lingaliweza jumuishwa kuonyesha kuwa safari ingalichukua mwendo wa siku kumi na moja, lakini kutokana na kutokuamini kwao iliwachukua muda wa kizazi chao chote (miaka 38 na zaidi). Huu mwendo wa siku kumi na moja unaonekana kuthibitisha mahali ulipo Mlima Horebu/Sinai kama ilivyo Kusini mwa rasi ya Sinai. Tambua kuwa mahali Musa alipopewa amri kumi panaitwa “Horebu.” Horebu ni neno la Kiebrania likimaanisha “takataka” au “majonzi” (BDB 352, KB 349). Sinai (BDB 696) sio neno la Kiebrania, na inaonekana kurejelea sehemu zote mahali ambapo Musa aliwapeleka Waisrael kukutana na YHWH (mf., Horebu, Kut. 3:1; Kumb. 1:6,19; 4:10,15; 5:12 na Sinai Kut. 19; Law. 7:38; 25:1; 26:46; 27:34; Hes. 1:1,9; 3:1,4,14; 9:1,5).

Ni kwa nini jina “Horebu” mara nyingi linatumika katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati na “Sinai” mara nyingi kutumika katika kitabu cha Kutoka haijulukani.

Kuna aina mbalimbali ya fasihi katika maandiko ya Musa. Hili lingalirejelea kwenye:

1. simulizi za mdomo zilizoandikwa na maandishi tofauti
2. Musa akitumia maandishi mbalimbali
3. mabadiliko yaliyofanywa na maandishi waliokuja baadaye kwa sababu zisizo julikana
4. mchanganyiko wa fasihi

MADA MAALUM: MAHALI ULIPO MLIMA SINAI

- A. Kama Musa alikuwa akiongea kiuhalisia na sio kimethali juu ya “safari ya siku tatu” alipokwenda kumwomba Farao (Kut. 3:18; 5:3; 8:27), huo haukuwa muda wa kutosha kwao kupata mahali pa kimila katika rasi ya kusini mwa Sinai. Kwa hiyo, wasomi wengine wanaelekeza huo Mlima kuwa karibu na chemichemi za Kadesh-Barnea (angalia video kwenye idhaa ya Historia, “The Exodus Decoded”).
- B. Mahali pa kimila palipoitwa, “Jebel Musa,” katika nyika ya uovu, pana vitu vingi ndani yake.

1. Uwanda mkubwa kabla ya Mlima
 2. Kumbukumbu la Torati 1:2 inasema ilikuwa yapata safari ya siku kumi na moja toka Mlima Sinai mpaka Kadesh-Barnea.
 3. Neno “Sinai” (BDB 696, KB 751) ni neno lisilo la Kiebrania. Laweza kuhusianishwa na nyika ya uovu, ambalo linarejelea kwenye vichaka vidogo vidogo vya mbugani. Neno la Kiebrania la la Mlima ni Horeb (yaani., nyika, BDB 352, kama vile Kut. 3:1; 17:6; 33:6).
 4. Mlima Sinai pamekuwa ni mahali pa kimila tangu karne ya Nne B.K. Upo katika “nchi ya Wamidiani,” ambayo inajumuisha sehemu kubwa ya rasi ya Sinai na Arabia
 5. Inaonekana kuwa elimukale imethibitisha mahali penyewe pa baadhi ya miji iliyotajwa katika maelezo ya Kitabu cha Kutoka (Elim, Dophkah, Rephidim) yanavyosema kuwa upande wa Magharibi mwa Rasi ya Sinai.
- C. Wayahudi kamwe hawakupenda eneo la kijografia la Mlima Sinai. Waliamini kuwa Mungu aliwapa sheria na utimilifu wa ahadi yake toka Mwa. 15:12-21. “ambapo” halikuwa tatizo na hawakukusudia kurejea kwenye eneo hili (yaani., hapakuwepo na hija ya mwaka)
- D. Eneo la kimila la Mlima Sinai halikuweza anzishwa mpaka kwenye hija ya Silvia, iliyoandikwa yapata mwaka 385-8 B.K (k.v F. F. Bruce, Commentary on the Book of the Acts, uk. 151).

Jina jingine lililotumika katika Agano la Kale mahali ambapo YHWH aliwapa “Amri Kumi” palikuwa “Horebu” (BDB 352, KB 350, kama vile Kut. 3:1; 17:6; 33:6; Kumb. 1:2,6,19; 4:10,15; 5:2; 9:8; 18:16; 29:1; 1 Falm. 8:9; 19:8; 2 Nya. 5:10; Zab. 106:19; Mal. 4:4). Asili hii yaweza kuhusiana na konsonanti tatu za Kiebrania inayomaanisha “mabaki,” “ukiwa,” au “hame” (BDB 352, KB 349). Inaonekana kuwa “Horebu” inarejelea mkusanyiko wa Milima na “Sinai” ni moja ya kilele chake.

☐ **“Mlima Seiri”** BDB 973 inasema neno “Seiri” laweza kumaanisha (1) mbuzi; (2) nywele; (3) vichaka vyenye kuwa na miti mingi; wakati KB 1989 inadai kuwa linamaanisha “nywele.” Katika Agano la Kale hili neno linahusiana na Edomu (k.v. Mwa. 14:6; 36:20-21,30; Kumb. 1:2,44; 2:1,4-5; 33:2). Mara nyingi linaanishwa kama mlima (k.v. Gen. 14:6; 36:8-9; Kumb. 2:1). Kwa hiyo, mwanzoni lilikuwani eneo la safu ya milima ya Horebu jirani na Edomu.

☐ **“Kadesh-barnea”** Hii chemichemi kubwa kwenye mpaka wa Edomu (k.v. Hes. 20:16), yapata maili 50 kusini mwa Beersheba, ikiwa na majira manne ya kuchipua ya asili. Jina lake lina vitu viwili muhimu. Cha kwanza ni kutoka kwenye Kiebrania kwa ajili ya neno “takatifu” (BDB 873). Cha pili hakijulikani. Pakajakuwa ni ni kitovu cha shughuli kipindi cha kutangatanga jangwani (k.v. Hesabu 13-14).

1:3 “mwaka wa arobaini” Hii ndiyo tarehe pekee katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati. “Arobaini” (BDB 917) imetumika mara nyingi katika Biblia kiasi kwamba inaonekana kurejelea kipindi kirefu, kisichoelezeka cha muda. Utaratibu halisi wa kupanga matukio unaonekana kuwa ni miaka 38 (kutoka Sinai mpaka nyanda za Moabu).

☐ **“mwezi wa kumi na moja, siku ya kwanza ya mwezi”** Mwandishi anafanya kila jitihada kuonyesha mahali na muda juu ya maneno haya kwa Waisrael. Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: KALENDA YA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE

Wakaanani (I Kgs. 6:1,37-38; 8:2)	Washumeri-Wababeli Kalenda ya Nippur	Waebrania (kalenda ya Geezer)	kalenda Inayoendana kwa leo
Abib	Nisanu	Nisan	Mwezi wa tatu-mwezi wa Nne
Zin (majira ya kuchipua)	Ayaru	Iyyar	Mwezi wa Nne-Mwezi wa Tano
	Simanu	Sivan	Mwezi wa Tano-mwezi wa Sita

	Du-uzu	Tammuz	Mwezi wa Sita-mwezi wa Saba
	Abu Alulu	Ab Elul	Mwezi wa Saba-mwezi wa Nane Mwezi wa Nane-mwezi wa Tisa
Ethanim (vyanzo vya maji vya kudumu)	Teshritu	Tishri	Mwezi wa Tisa-mwezi wa Kumi
Bul (mvua kuanza kunya)	Arah-samna	Marcheshvan	Mwezi wa kumi-mwezi wa kumi na moja
	Kislimu	Chislev	Mwezi wa kumi na moja-mwezi wa kumi na mbili
	Tebitu	Tebeth	Mwezi wa kumi na mbili-Mwezi wa kwanza
	Shabatu	Shebat	Mwezi wa kwanza-mwezi wa pili
	Adaru	Adar	Mwezi wa pili-mwezi wa tatu

☐“Musa akawaambia wana wa Israeli kama yote aliyopewa na Bwana ya kuwaamuru” Mungu mwenyewe ndiye mwandishi; Musa ni Mwongozaji, lakini maelekezo yote haya yalitoka kwa Yahweh mwenye kutengeneza agano. Kuna mchanganyo mwingi katika majina ya miungu kwenye maandiko ya Musa. Ifuatayo ni mifano toka kwenye Kumbukumbu la Torati 1-4.

BWANA (YHWH), 1:3,8,27,34,37,41,42,43,45; 2:12,14,15,17,21,31; 3:2,20,21,26(mara mbili); 4:12,14,15,21,27

1. BWANA (YHWH) Mungu wetu (*Elohim*), 1:1,19,20,25,41; 2:29,36,37; 3:3; 4:7
2. BWANA (YHWH) Mungu wetu (*Elohim*), 1:10,21,26,30,31,32; 2:7 (mara mbili),30; 3:18,20,21,22; 4:2,3,4,10,19,21,23(mara mbili),24,25,29,30,31,34,40
3. BWANA (YHWH), Mungu (*Elohim*) wa baba zenu, 1:11,21; 4:1
4. Mungu (*Elohim*), 1:17; 2:33; 4:24 (mwenye wivu), 31(Mungu wa rehema), 32,33
5. BWANA (*Adon*) Mungu (YHWH), 3:24
6. BWANA (YHWH), Mungu wangu (*Elohim*), 4:5
7. BWANA (YHWH), Yeye ndiye Mungu (*Elohim*), 4:35,39

Pamekuwepo na mitazamo mengi kuhusiana na huu mkanganyiko:

1. Watunzi mbalimbali
2. Waandishi mbalimbali
3. Wanathiolojia wa kipekee
4. Fasihi mbalimbali

Wanazuoni wa Agano la Kale lazima wakubali kuwa utunzi, mtungo, uboreshaji, na kazi za kiuandishi zinazohusiana na vitabu vya sheria za kikanisa za Agano la Kale ni ni fumbo. Lazima tuwe waangarifu kutoruhusu nadharia zetu za leo za fasihi za kimagharibi au madhanio yetu ya awali ya kithiolojia yahitaji mtu mmoja tu mwenye kuitafasiri. Fumbo linamaanisha siri.

MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

A. *El*(BDB 42, KB 48)

1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, “kuwa shupavu” au “kuwa mwenye nguvu” (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb. 7:21; Zab. 50:1).

2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra), akaitwa “baba wa miungu” na “bwana wa mbinguni”
 3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika kwa namna ya kuainisha tabia za Mungu.
 - a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sana BDB 42 & 751 II), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
 - b. *El-Roi* (“Mungu aonaye” au “Mungu ajifunuaeye Mwenyewe” BDB 42 & 909), Mwanzo 16:13
 - c. *El-Shaddai* (“Mungu Mkuu” au “Mungu mwenye huruma zote” au “Mungu wa mlima”), BDB 42 & 994) Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
 - d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16
 - e. *El-Berit* (Mungu wa Agano”), BDB 42 & 136), Waamuzi 9:46
 4. *El* inalinganishwa na
 - a. YHWH katika Zaburi. 16:1-2; 85:8; Isa. 42:5, Hes. 23:8
 - b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu 5:8, “Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
 - c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
 - d. “wivu” katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
 - e. “reheema” katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31
 - f. “mkuu na mzuri” katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
 - g. “maarifa” katika I Sam. 2:3
 - h. “kimbilio langu” katika II Sam. 22:33
 - i. “mlipa kisasi wangu” katika II Sam. 22:48
 - j. “mtakatifu” katika Isa. 5:16
 - k. “muweza” katika Isa. 10:21
 - l. “wokovu wangu” katika Isa. 12:2
 - m. “mkuu na mwenye nguvu” katika Yer. 32:18
 - n. “anayepatiliza: katika Yer. 51:56
 5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Yoshua 22:22 (*El*, *Elohim*, *YHWH*, kurudiwa)
- B. *Elyon* (BDB 751, KB 832)
1. Maana yake ya msingi ni “juu,” “aliyetukuzwa,” au “kuinuliwa” (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme. 18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
 2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
 - a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
 - b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
 - c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
 - d. *El* - Hes. 24:16
 - e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya “Mungu aliye Juu”) katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
 3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
 - a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
 - b. Balaamu, Hes. 24:15
 - c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
 - d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)
- C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi (BDB 43, KB 52)
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
 2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahimu walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Yosh. 24:2).
 3. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)

4. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7.
5. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104). Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*Elohim* KUR. 1,2,5; YHWH, kur. 2,6; hata *Adoni*, uk. 4) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.
6. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.
7. Inashangaza kwamba jina lililozoeleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
 - a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa “wingi wa ukuu,” mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
 - b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7).
 - c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipya Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).

D. YHWH (BDB 217, KB 394)

1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo
 - a. Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili, Zaburi 104)
 - b. Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu (Zaburi 103).
Mwanzo 2:4-3:24 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.
2. Katika Mwanzo 4:26 inasema “wanadamu wakaanza kuliitia jina la BWANA” (YHWH). Hata hivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezwa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hata hivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, juzuu 2, kur. 409-11).
 - a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, “kuonesha upendo wa dhati”
 - b. kutoka katika mzizi wa kiarabu “kupuliza” (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
 - c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) “kuzungumza”
 - d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVU ikimaanisha “Yeye anayetoshela,” au “yeye anaye anzisha”
 - e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* “Yeye ambaye yupo,” au “Yeye aliyepo sasa” (katika namna ya wakati ujao, “Yeye atakayekuwako”)
 - f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* “yeye asababishaye kuwa”
 - g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania “kuishi” (mfano Mwanzo. 3:20), maana “Mungu mmoja tu aishiye milele”
 - h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, “nitaendelea kuwa

vile nilivyokuwa” au “nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa” (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezwa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili

(1) *Yah* (mfano Hallelu – yah, BDB 219, kama vile Kut. 15:2; 17:16; Zab. 89:8; 104:35)

(2) *Yahu* (majina mfano Isaya)

(3) *Yo* (majina mfano Yoeli)

3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lililofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania “mmiliki,” “Mkuu,” “mume,” “bwana”—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka “bwana.” Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.
4. Kama ilivyo kwa *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
 - a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa), Mwanzo 22:14
 - b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), BDB 217 na 950, *Qal* HALI YA KUENDELEA),Kutoka. 15:26
 - c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), BDB 217 na 651,Kutoka. 17:15
 - d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye, BDB 217 na 872, *Piel* HALI YA KUENDELEA),Kut. 31:13
 - e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani BDB 217 na 1022), Waamuzi. 6:24
 - f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi ,BDB 217 na 878), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
 - g. *YHWH - Ro’i* (YHWH ni mchungaji wangu,BDB 217 na 944, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Zab. 23:1
 - h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu, BDB 217 na 841), Yer. 23:6
 - i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa,BDB 217 na 1027), Eze. 48:35

1:4

NASB, NRSV “baada ya kushindwa”

NKJV “baada ya kuuwawa”

TEV “Bwana alipokwisha kumpiga”

NJB “alipokwisha kumpiga”

KITENZI (BDB 645, KB 697, *Hiphil* KITENZIJIINA) kinamaanisha “kukata” na maana ya kithiolojia ni kuwa alikuwa ni YHWH mwenyewe. Yeye ndiye chanzo na msababishaji!

☐“**Sihon**” Sihoni (BDB 695) alikuwa ni Muamori mfalme wa eneo hilo baada ya Ogu, mfalme wa Bashani, mashariki mwa Mto Yordani. Musa aliamriwa na Mungu (k.v. 2:4-9) wasiwashambulie jamaa za Kiyahudi wa Moabu na Edomu (uzao wa Lutu wanawe wa pekee, k.v. Mwa. 19:30-38). Njia nyingine tofauti kwenda Yordani ilikuwa kupitia eneo la Sihoni. Mji mkuu wa Heshboni ndio ulikuwa mji wa kwanza mkubwa jeshi la Isaraeli kuutwaa (k.v. 2:26-37; Hes. 21:21-32).

☐“**Ogu**” Ogu (BDB 728) alikuwa ni mfalme wa eneo lililoitwa Bashan, lililokuwa na miji miwili mikubwa (k.v. Yosh. 12:4) na vijiji vingi (k.v. 3:1-10). Inavyoonekana alikuwa ni mmoja wa Warefai (majitu, k.v. 3:11) walioishi Kaanani (k.v. 2:20; Yosh 12:4). Ulikuwa ni uzao wa haya majitu (k.v. 2:11) huko Hebroni ulisababisha Israel kuikataa taarifa ya wapelelezi wawili waaminifu (k.v. Hes. 13:22).

MADA MAALUM: TAREHE YA KUTOKA KWA WAISRAELI MISRI

Pamekuwepo na maoni mbali mbali ya kisomi juu ya tarehe ya kutoka kwa Waisrael Misri.

A. Kutoka 1 Falm 6:1, "miaka 480 toka kuondoka kwa Waisraeli Misri hadi ujenzi wa hekalu la Sulemani"

1. Suleimani alianza kutawala katika mwaka 970 K.K. Hii inahesabiwa kwa kutumia vita vya Qarqar vya mwaka 853 K.K kama tarehe ya mwanzo iliyojulikana
 2. Hekalu lilijengwa katika Mwaka wake wa nne (965 K.K), na kuondoka kwa Waisrael kulitokea yapata Mwaka 1445/6 K.K
 3. Hili linaonekana kutokea katika karne ya 18 wa utawala wa ki-Misri.
 - a. Yule Farao mkandamizaji angalikuwa ni Thutmose III (1490-1436 K.K)
 - b. Yule Farao aliye sababisha Waisraeli kuondoka Misri angalikuwa Amenhotep II (1436-1407 K.K)
 - 1) Wengine wanaamini ushahidi toka Yeriko uliosimamia kuwa hapakuwepo na mawasiliano ya kidiplomasia kati ya Yeriko na Misri wakati wa utawala wa Amenhotep III (1413-1377 K.K).
 - 2) Maandishi ya Amarna yanaweka kumbukumbu ya mawasiliano ya kidiplomasia yaliyoandika kwenye makombe kuhusu (Habiru) wachungaji waliokuwa wakihama hama na kuenea kote nchi ya Kanani katika utawala wa Amenhotep III. Kwa hiyo, kuondoka kwa Waisrael Misri kulitokea katika utawala wa Amenhotep II.
 - 3) Kipindi cha waamuzi hakikuwa kirefu kama karne ya 13 ndio tarehe ya Waisraeli kuondoka Misri.
 4. Uwepo wa tatizo juu ya tarehe hizi
 - a. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) yana miaka 440, na sio 480.
 - b. Yawezekana kuwa miaka 480 ni uwakilisho wa vizazi 12 vyenye miaka 40 kila kimoja, kwa hiyo, ni hesabu ya ujumla.
 - c. Kuna vizazi kumi na viwili vya makuhani kati ya Aaron na Suleiman (kama vile 1 Nyakati 6), tena kumi na viwili toka Suleimani hadi hekalu la pili. Wayahudi, kama walivyo Wayunani, walihesabu vizazi kama Miaka arobaini. Kwa hiyo, kuna kipindi cha miaka 480 nyuma na mbele (uwakilishaji wa kutumia hesabu, kama vile uhesabuji tena wa tarehe za Waisrael kuondoka Misri na kushinda wa Bimson).
 5. Pia kuna maandiko matatu yaliyotaja tarehe hizi.
 - a. Mwanzo 15:13,16 (kama vile Mdo. 7:6), miaka 400 ya ukandamizwaji
 - b. Kutoka 12:40-41 (kama vile Gal. 3:17)
 - 1) MT (maandishi ya Kimasoretic)-Miaka 430 ya kuishi kwa muda huko Misri
 - 2) LXX (Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani)-Miaka 215 ya kuishi kwa muda huko Misri
 - c. Waamuzi 11:26-Miaka 300 kati ya siku ya Yeftha na kushinda kwake (inaunga mkono tarehe 1445)
 - d. Mdo. 13:19-Kuondoka Misri, kutangatanga jangwani, na kushinda-Miaka 450
 6. Mwandishi wa kitabu cha Wafalme alitumia nukuu maalum za kihistoria na hakuweka hesabu ya ujumla (Edwin Thiele, A Chronology of the Hebrew Kings, kur. 83-85
- B. Ushahidi wa mfano toka elimukale inaonekana kuelekeza hadi tarehe za 1290 K.K. au karne ya 18 ya utawala wa ki-Misri
1. Yusufu aliweza kuwatembelea baba yake na Farao siku moja. Farao wa kwanza mzawa aliyeanza kuondoa Mji mkuu toka Thebesi na kuurudisha Nile Delta, mahali palipoitwa Avaris/Zoan/Tanis, ambao ulikuwa Mji wa kale ulioitwa Hyksos, ulikuwa Seti (1309-1290 K.K). Angelikuwa ni Farao wa ukandamizaji.
 - a. Inapendeza kuoanisha vipande vya habari kuhusu kutawala kwa Hyksos huko Misri.
 - 1) Mawe yaliyowekwa kwa ajili ya mipaka yamepatikana kipindi cha Ramese wa II kuadhimisha kupatikana Mji Mkuu wa Misri, Avaris mwanzoni mwa miaka 400 kipindi cha utawala wa Hyksos mwaka 1700 K.K
 - 2) Unabii wa Mwanzo 15:13 unaongelea juu ya miaka 400 ya ukandamizaji
 - b. Hii inadokeza kuwa kuja kwa Yeftha kwenye utawala kulikuwa chini ya Hyksos. Utawala mpya wa ki-Misri unarejelewa katika Kut. 1:8
 2. Hyksos, ni neno la ki-Misri linalomaanisha “watawala wan chi ngeni,” lilikuwa ni kundi la watawala wa kisemiti huko Misri, walioidhibiti Misri kipindi cha utawala karne ya 15 na 16 (1720-1570K.K).

Baadhi wanaoanisha na kuingia kwa Yeftha kwenye utawala. Tukitoa mika 430 ya Kut. 12:40 toka kwenye miaka 1700K.K, tunapata miaka takribani 1290 K.K.

3. Mtoto wa Seti I alikuwa Ramese II (1290-1224 k.k). jina hili limetajwa kama moja ya mji ulijengwa na watumwa wa Kiebrania, Kut. 1:11. Pia Wilaya hii katika Misri karibu na Goshen Inaitwa Ramese, Mwa.47:11. Avaris/Zoan/Tanis ulijulikana kama "nyumba ya Ramese" toka mwaka 1300-1100K.K
 4. Thusmoses III alijulikana kama mjenzi mkuu, kama alivyokuwa Ramese II.
 5. Ramese II alikuwa na mabinti 47 walioishi sehemu mbali mbali.
 6. Elimukale inaonyesha kuwa mingi ya miji ya Kaanani iliyozungushiwa ukuta (Hazor, Debir, Lachish) iliharibiwa na kujengwa tena yapata miaka ya 1250 K.K. Katika kuiruhusu miaka 38 ya kutangatanga jangwani, inaendana na tarehe za 1290K.K. Wana akiolojia wamepata ushahidi wa Israel kuwa kusini mwa Kaanani juu ya mawe ya kumbukumbu yaliyowekwa kwa ajili ya mipaka wakati wa utawala wa mrithi wa Ramese, aitwaye Merneptah (1224-1214 K.K, kama vile mawe ya mipaka ya Merneptah, yaliyoandikwa 1220 K.K).
 7. Edomu na Moabu inaonekana kupata utambulisho wa nguvu wa kitaifa katika mwaka 1300 K.K. nchi hizi mbili hazikuwa zimeungana katika karne ya kumi na tano.
 8. Kitabu, Redating the Exodus and Conquest by John J. Bimson, kilichochapishwa na chuo kikuu cha Sheffield, 1978, wanabishana juu ya ushahidi wa elimukale kwa ajili ya tarehe.
- C. Pamekuwepo na nadharia ambayo inaweza onekana katika historia, iitwayo "Exodus Decoded," inayodai kuwepo na njia ya moja kwa moja upande wa Kaskazini (yaani., "njia ya Wafilisti"), hata mapema yapata miaka ya 1445 K.K., katika kipindi cha Hyksos (yaani., "wachungaji wa kifalme," 1630-1523 K.K.)

MADA MAALUM: WAISRAELI WA MWANZO WALIOISHI PALESTINA

A. Kuna orodha nyingi za watu.

1. Mwanzo 15:19-21 (10)

- | | | | |
|--------------|-------------|---------------|-------------|
| a. Wakeni | d. Wahiti | g. Waamori | j. Wayebusi |
| b. Wakenizi | e. Waperizi | h. Wakanaani | |
| c. Wakadmoni | f. Warefai | i. Wagirgashi | |

2. Kutoka 3:17 (6)

- | | |
|--------------|-------------|
| a. Wakanaani | d. Waperizi |
| b. Wahiti | e. Wahivi |
| c. Waamori | f. Wayebusi |

3. Kutoka 23:28 (3)

- a. Wahivi
- b. Wahiti
- c. Wahiti

4. Kumbukumbu la Torati 7:1 (7)

- | | | |
|---------------|--------------|-------------|
| a. Wahiti | d. Wakanaani | g. Wayebusi |
| b. Wagirgashi | e. Waperizi | |
| c. Waamori | f. Wahivi | |

5. Yoshua 24:11 (7)

- | | | |
|-------------|---------------|-------------|
| a. Waamori | d. Wahiti | g. Wayebusi |
| b. Waperizi | e. Wagirgashi | |

c. Wakanaani

f. Wahivi

B. Asili ya majina haya haijulikani kwa sababu ya kukosa vielelezo vya kihistoria. Mwanzo 10:15-19 inajumuisha mengi kati yao kama inavyohusiana na Mwana wa Hamu.

C. Maelezo mafupi ya watu hawa waliotajwa

1. Wakeni — BDB 884, KB 1098
 - wasio Waisrael
 - jina linahusiana na "mfua chuma" au "mhunzi," ambalo lingalirejelea kazi ya kufua bati au muziki (kama vile Mwa. 4:19-22)
 - lilihusianishwa na eneo la Mlima Sinai Kaskazini mwa Hebron
 - jina lilihusiana na Yethro, Mkwewe Musa (kama vile Amu. 1:16; 4:11)
2. Wakenizi — BDB 889, KB 1114
 - nduguze Wayahudi
 - ukoo wa Edomu (kama vile Mwa. 15:19)
 - waliishi huko Negebu
 - yumkini wakaishilia Uyahudi (kama vile Hes. 32:12; Yos. 14:6,14)
3. Wakadmoni — BDB 870 II, KB 1071 II
 - hawakuwa Waisrael, yumkini kizazi cha Ishmael (kama vile Mwa. 25:15)
 - jina linahusiana na "mtu wa Mashariki"
 - waliishi huko Negebu
 - yumkini wanahusiana na "watu wa Mashariki" (kama vile Ayu. 1:3)
4. Wahiti — BDB 366, KB 363
 - hawakuwa Waisrael
 - kizazi cha Sethi
 - walitokea ufalme wa Anatolia (Asia Ndogo, Uturuki)
 - walikuwepo mwanzoni kabisa huko Kaanani (kama vile Mwanzo 23; Yos. 11:3)
5. Waperizi — BDB 827, KB 965
 - hawakuwa Waisrael, yumkini Hurrians
 - waliishi kwenye maeneo ya misitu ya Uyahudi (kama vile Mwa. 34:30; Amu. 1:4; 16:10)
6. Refaimu — BDB 952, KB 1274
 - hawakuwa Waisraeli, yumkini majitu (kama vile Mwa. 14:5; Hes. 33:33; Kumb. 2:10-11,20)
 - waliishi kwenye kingo za Mto Yordani (kama vile Mwa. 15:20; Yos. 12:4; 13:12; Kumb. 2:8-11,20; 3:13) au Kingo za Magharibi (kama vile Yos. 15:8; 17:15; 2 Sam. 5:18,22; 23:13; 1 Nya. 20:4)
 - kizazi cha wapiganaji
7. Waamori — BDB 57, KB 67
 - kundi la watu wa Kisemiti toka Hamu (kama vile Mwa. 10:16)
 - wakawa wenye cheo kikuu kwa kizazi cha Wakaanani (kama vile Mwa. 15:16; Kumb. 1:7; Yos. 10:5; 24:15; 2 Sam. 21:2)
 - jina laweza kumaanisha "watu wa Magharibi"
 - ISBE, juzuu. 1, uk. 119, inasema neno linamaanisha
 - a. kizazi cha Wapalestina kiumla
 - b. idadi ya watu wa nchi ya milima waliopingwa na watu wa uwanda wa Pwani
 - c. kikundi cha watu maalum wakiwa na Mfalme wao
8. Wakanaani — BDB 489, KB 485

- toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:15)
 - wakawa wenye cheo kikubwa kwa kabila zote za Wakanaani Magharibi mwa Yordani
 - maana ya Kanaani haijulikani, yumkini "mfanya biashara" au "rangi ya hudhurungi"
 - kama kikundi cha watu walioishi kando ya uwanda wa Pwani (kama vile Hes. 13:29)
9. Wagirgashi — BDB 173, KB 202
- toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:16) au kiwastani "toka mwana wa [yaani., nchi ya] Wakaanani," ISBE, juzuu. 2, uk. 1232)
10. Wayebusi — BDB 101, KB 382
- toka Hamu (kama vile Mwa. 10:16)
 - toka Mji wa Wayebusi/Salemu/Yerusalem (kama vile Yos. 15:63; Yos. 19:10)
 - Ezek. 16:3,45 inadaid kilikuwa kizazi mchanganyiko toka kwa Waamori na Wahiti
11. Wahivi — BDB 295, KB 297
- toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:17)
 - ikatafasiriwa na maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) kama Waamori (kama vile Mwa. 34:2; 36:20-30; Yos. 9:7)
 - yumkini toka kwenye neno la Kiebrania "pango," kwa hiyo, waishio mapangoni
 - waliishi katika uwanda wa juu wa Lebanoni (kama vile Yos. 11:3; Amu. 3:3). katika 2 Sam. 24:6-7 imewaorodhesha mbele ya Tiro na Sidoni

☐ **"Astarothi"** Mji huu (BDB 800) ulipewa jina baada ya mke wa mungu wa ustawi wa Kanaani *BaalAsherah/Astarte*. Kwa sababu ya kuendelea kuwataja Warefai, yawezekana kuwa huu mji ndio unarejewa katika Mwa. 14:5.

☐ **"Edrei"** Huu ulikuwa ni mojawapo ya kati ya miji mikuu ya Ogu (k.v. Yosh. 12:4; 13:12).

1:5 "katika nchi ya Moabu" Hapa ndipo Waisrael waliweka kambi kabla ya kuingia kwenye nchi ya ahadi. Ni sehemu iliyopo magharibi mwa Bahari ya chumvi upande wa mashariki mwa kingo za Mto Yordani, mahali ambapo kitabu cha Kumbukumbu la Torati kiliandikwa.

☐ **"alipoanza Musa"** KITENZI hiki (BDB 383, KB 381, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinadokeza "kujitoka kwa hiari" (k.v. Mwa. 18:27; Kut. 2:21; Amu. 19:6).

☐ **"kufunua torati hii"** KITENZI hiki (BDB 91, KB 106, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha kuweka wazi au namna ya kueleweka. Neno hili linaonekana hapa tu na tena mara mbili ambapo limetafasiriwa "andika" (k.v. 27:8; Hab. 2:2). Maelekezo ambayo hayako wazi au kueleweka hayana maana na, hatari katika muktadha huu wa kimaagano. Neno "sheria" (yaani., Torati BDB 260) ni neno la Kiebrania kwa ajili ya neno "mafundisho" au "maelekezo" (k.v. 4:8,44; 27:3,8,26; 28:58,61; 29:20,28; 30:10; 31:9,11,12; 32:46). Katika muktadha huu linarejelea kwenye hotuba za Musa kuufika ujumbe kwa Israeli upande wa Mashariki mwa Mto Yordani ng'ambo ya Yeriko, juu ya nyanda za Moabu, mara tu kabla ya Waisraeli walipopita Mto Yordani pasipo yeye.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 1:6-8

⁶ Bwana, Mungu wetu, alituambia huko Horebu, akasema, Mliyokaa katika mlima huu vyatosha; ⁷geukeni mshike safari yenu mwende nchi ya milima ya Waamori, na mahali pote palipo karibu ya hapo, katika hiyo Araba, na nchi ya vilima-vilima, na huko Shefela, na Negebu, na pwani-pwani, nchi ya Wakanaani, na Lebanoni, mpaka mto huo mkubwa, mto wa Frati. ⁸ Angalieni, nimewawekea nchi mbele yenu, ingieni mkaimiliki nchi Bwana aliyowaapia baba zenu, Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, kwamba atawapa na uzao wao baada yao.

1:6 “Bwana” Hili ni jina la kipekee kwa ajili ya Mungu wa Israeli (yaani., YHWH, BDB 217). Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.

☐ **“Mungu wetu”** KIWAKILISHI CHA NAFSI WINGI kinamaanisha uhusiano wa maagano, ulioanzishwa na kukubaliwa huko Mlima Sinai. Hili ni jina la uungu, *“Elohim”* (BDB 43). Linatumika kwa Mungu kama muumbaji, mtoaaji, na mwezeshaji wa uumbaji wote (mf., Mwa. 1:1-2:3). Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.

☐ **“Horebu”** Tazama angalizo katika 1:2.

☐ **“mlivyokaa katika mlima huu vyatosha”** Sasa Mungu anawaambia watu wake ni wakati wao kufanya ambacho mwanzo aliwaamuru, waishi Kaanani (k.v. Mwa. 15:13-21; Hesabu 13-14)! Walikaa katika Mlima Horebu kwa muda wa mwaka mmoja (linganisha Kut. 19:1 na Hes. 10:11).

1:7

NASB “geukeni na muianze safari yenu”

NKJV “geukeni na muishike safari yenu”

NRSV “ianzeni safari yenu”

TEV “mvunjeni kambi na muende”

NJB “mwendeni, mwendelee na safari yenu”

KITENZI cha kwanza (BDB 815, KB 937, *Qal KAULI SHURUTISHI*) kinamaanisha “geukeni,” lakini kinatumika katika maana mbalimbali:

1. Geuka na kutazama huko na huko, Kut. 2:12; 16:10; Hes. 12:10
2. Geuka ubadili mwelekeo, Mwa. 18:22; 24:49; Kut. 14:25; 21:33; Kumb. 1:7,24; 2:3; 9:15; 10:5
3. Geukieni miungu mingine, Law. 19:4; Kumb. 29:18; 30:17; 31:18,20
4. msiwatafute, Law. 19:31; 20:6
5. mkaribiaeni
 - a. jioni, Kumb. 23:11
 - b. asubuhi, Kut. 14:27

KITENZI cha pili (BDB 652, KB 704, *Qal KAULI SHURUTISHI*) kinamaanisha “ondoa,” “vuta,” au “kusudia,” ambacho hutumika mara nyingi katika kitabu cha Hesabu kwa Waisraeli kuiondoa kambi yao. Matumizi haya yanaendelea katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (mf. 1:7,19,40; 2:1,24). Mwanzoni lilirejelea kung’oa vigingi vya hema.

☐ **“mwende”** Huu ni mfanano wa tatu wa neno *Qal KAULI SHURUTISHI* (BDB 97, KB 112).

☐ Kuna migawanyo mitano ya sura ya nchi huko Palestina tokea kaskazini hadi kusini iliyotajwa:

1. “kwenye nchi ya milima ya Waamori” – Hili linarejelea upande wa kingo za mashariki mwa mto Yordani na himaya za Sihoni na Ogu.
2. “huko Araba” – Hili linarejelea kwenye bonde la mto Yordani kusini mwa Bahari ya Chumvi (BDB 787, k.v. 1:1,7; 2:8; 3:17; 4:49; 11:30; Yosh. 8:14; 11:2,16; 12:3; 18:18)
3. “kwenye vilima vya nchi na mabondeni” – Hili linarejelea kwenye eneo la magharibi na kusini mwa Bahari ya Chumvi, baadaye ikajakuwa ni mahali pa kabila la Efrahimu na Yuda.
4. “Negevu” – Hii ni nchi ya jangwa kame kusini mwa Bahari ya Chumvi na upande wa magharibi (BDB 616)
5. “Pwani” – Huu ni uwanda wa Pwani tokea Misri hadi Lebanoni (yaani., Shefela, BDB 410). Haya yote yametumika pamoja kurejelea kwenye nchi aliyoahidiwa Ibrahim katika Mwanzo 15.

1:8 Mstari wa 8 ni mtiririko wa amri:

1. “Tazama” - BDB 906, KB 1157, *Qal KAULI SHURUTISHI*
2. “Ingia” - BDB 97, KB 112, *Qal KAULI SHURUTISHI*
3. “Miliki” - BDB 439, KB 441, *Qal KAULI SHURUTISHI* (tazama Mada Maalum katika 8:1)

☐“**Nimewawekea nchi mbele yenu**” Neno la Kiebrania kwa ajili ya neno “nimewawekea” linafanana na neno “nimewapa” (BDB 678, KB 733, *Qal*/ PKAULI YA WAKATI TIMILIFU). Kwa hiyo Mungu alikuwa anawapatia nchi kama alivyomwahidi Ibrahimu (Mwa. 12:1, mstari 5; 15:12-21; Kut. 6:8), lakini walitakiwa kuimiliki. Tambua dhana ya kimasharti hata ya agano hili la kimsingi (mf., 4:1; 5:33; 6:18; 8:1; 16:20; 30:16,19).

☐“**nchi Bwana aliyowaapia baba zenu, Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo**” Tazama Mada Maalum: Ahadi ya Agano kwa mababa wa imani kwenye 9:5. Tazama 4:37; 6:10; 9:5; 10:11,15; 30:20; Mwa. 12:5-7; 13:14-17; 15:18; 26:3; Kut. 32:13; 33:1. Nchi hii ingalijumuisha eneo toka Kadesh-Barnea kusini mwa Byblos na Zefani, Zedadi and Lebohamath eneo la kaskazini (yumkini kuelekea mashariki mwa chanzo cha maji cha mto Euphrates, k.v. Mwa. 15:18). Tazama MacMillan Bible Atlas, uk. 47. Pana sehemu mbalimbali ambapo mipaka ya pamoja ya nchi ya ahadi imetolewa (Kut. 34:1-12; Kumb. 1:6-8; 3:12-20; 11:24; Yosh. 1:3-4). Ilikuwa ni kipindi cha utawala wa Daudi kwamba eneo hili lote lilikuwa chini ya umiliki wa Israeli.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1:9-15

⁹ Nami wakati ule niliwaambia, nikasema, Siwezi mimi mwenyewe kuwachukua peke yangu. ¹⁰ Bwana, Mungu wenu, amewafanya kuwa wengi, nanyi, angalieni, mmekuwa leo mfano wa nyota za mbinguni kwa wingi. ¹¹ Bwana, Mungu wa baba zenu, na awafanye kuwa wengi mara elfu kuliko mlivyo, na kuwabarikia, kama alivyowaahidi. ¹² Nitachukua peke yangu mimi mwenyewe udhia wenu, na mzigo wenu, na mateto yenu? ¹³ Jitwalieni watu wenye akili na fahamu, watu wanaojulikana, kwa kadiri ya kabila zenu, nami nitawafanya wawe vichwa juu yenu. ¹⁴ Nanyi mkanijibu, mkaniambia, Jambo ulilonena ni jema la kufanya. ¹⁵ Basi nikatwaa vichwa vya kabila zenu wenye akili, waliojulikana, nikawafanya wawe vichwa juu yenu, maakida ya elfu elfu, na maakida ya mia mia, na maakida ya hamsini hamsini, na maakida ya kumi kumi, na wenye amri, kwa kadiri ya kabila zenu.

1:9 “Nami wakati ule” Hiki ni kifungu chenye kujirudia katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Sura nne za mwanzo ni mapitio ya matendo ya huruma ya YHWH kwa niaba ya Israel. Lahaja hii ni namna ya kuonyesha tendo lililopita (k.v. 1:9,16,18; 2:34; 3:4,8,12,18;4:14).

☐“**Siwezi mimi mwenyewe kuwachukua peke yangu**” Tazama Kut. 18:13-26 kwa ajili ya ushauri wa Yethro kwa Musa kuhusu tatizo hili (yaani., Musa kuwa ndiye mwamuzi pekee).

1:10 “ Bwana, Mungu wenu, amewafanya kuwa wengi” Hii ilikuwa ni sehemu ya ahadi ya Mungu kwa mababa wa imani (mf., Mwa. 13:16; 17:2,20; 22:17; 48:4; Law. 26:9; Kumb. 7:13).

☐“**mfano wa nyota za mbinguni**” Kifungu hiki pia kinapatikana katika Mwa. 15:5; 26:4; Kumb. 10:22; 28:62. Vifungu vingine mfanano vilivyotumika kuonyesha hesabu isiyohesabika (k.v. Mwa. 16:10) ya Waisraeli ni: “vumbi la nchi” (k.v. Mwa. 13:16; 28:14; Hes. 23:10); na “mchanga wa bahari” (k.v. Mwa. 22:17; 32:12). Yote haya yalitoka kwa mtu ambaye hakuwa na mtoto yapata 100 (yaani., Abraham)!

Katika Kumb. 1:28 Waisraeli, ambao walikuwa wengi kama nyota za anga, walikuwa na hofu kuhusu makazi yao huko Kanaani kwa sababu ya:

1. Wengi wao/idadi yao
2. Maumbo yao
3. Miji iliyozungushiwa boma

Ni kejeli ya namna gani hii!

1:11 “Mungu wa Baba zenu” Mara nyingi haya majina yenye kujirudia yanadai kuwa Mungu Yule Yule alisema na Ibrahim, Isaka, na Yakobo bado yu hai katika maisha na hatma za vizazi vyao.

☐“**atawafanya kuwa wengi mara elfu**” Dhahili hiki ni kifungu cha kilahaja. Hesabu ya 1,000 ilikuwa ni mara kumi zaidi (mara tatu) na, kwa hiyo, ni alama ya ukubwa au wingi k.v. Zab. 90:4; II Pet. 3:8). Hapa kuna orodha ya matumizi yenye kukosoa mno toka kwenye toleo la NIDOTTE, juzuu. 1, uk. 417:

1. Kazi ya Mungu katika kubariki, Kumb. 1:11; Ayubu 42:12; Zab. 144:13
2. Baraka za nguvu, Yosh. 23:10
3. Apizo la nguvu kwa wasio amini, Kumb. 32:30; Isa. 7:23; 30:17; Amosi 5:3
4. Kustahimili ukuu wa Mungu, Zab. 90:4
5. Ahadi za agano la Mungu, Kumb. 7:9; Zab. 105:8
6. Ghadhabu ya Mungu dhidi ya upendo wa Mungu, Kut. 34:7; Kumb. 5:9-10
7. Baraka za kuwepo hekaluni mwa Mungu, Zab. 84:10

1:12 “mateto” Hili linamaanisha “madai” (BDB 936).

1:13 “Jitwalieni” KITENZI hiki(BDB 396, KB 393) ni *Qal* KAULI SHURUTISHI. Tambua kwamba Musa alikuwa akiwaamuru watu (yaani., viongozi wao) kuchukua majukumu (waliojitwalia) kwa ajili ya jamii pamoja na yeye mwenyewe (Musa aliowachagua). Waamuzi hawa wapya (yaani., viongozi wa kikabila) walipaswa kuwa:

1. “wenye hekima” - (BDB 314) ikimaanisha kuwa na uwezo wa kufikiri na chaguo la Kimungu (mf., Yusufu, Mwa. 41:33,39; David, II Sam. 14:20; Suleimani, I Fal. 2:9; 3:12; 5:21)
2. “kupambanua” - (BDB 106, KB 122, *Niphal* KAULI ENDELEVU) ikimaanisha mtu fulani mwenye maamuzi mazuri, kupambanua, na mwenye akili (mf., Joseph, Mwa. 41:33; kinyume na Yer. 4:22)
3. “uzoefu” - (BDB 393, KB 390, *Qal* KAULI TENDWA YA WAKATI ENDELEVU).

Hili ni la kawaida lenye kuwa na maana pana.

- a. NASB, TEV, NJB, JPSOA – mwenye uzoefu
- b. NKJB – mwenye maarifa
- c. NRSV, REB – mwenye sifa nzuri
- d. JB – mwenye uzoefu
- e. NIV – mwenye kuheshimiwa
- f. NET - anayejulikana

☐**“Nitawafanya wawe vichwa juu yenu”** KITENZI(BDB 962, KB 1321) ni *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kikitumika kwa maana ya HALI YA KUSIHI. Musa aliwachagua hawa watu waliochaguliwa kwenye nafasi za uongozi na kutoa hukumu/maamuzi (mf. Kut. 1:11; 18:21; Kumb. 17:14,15; Amu. 11:11). Hata hivyo, kiukweli, alikuwa YHWH “aliywafanya” (BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, mst. 15), ikionyesha uchaguzi wa Mungu (mf. 4:20,34; I Fal. 11:37). Mchakato wa kibinadamu hufuata mpango wa Kimungu!

1:15 “, maakida ya elfu elfu, na maakida ya mia mia, na maakida ya hamsini hamsini, na maakida ya kumi kumi” Mgawanyo huu baadaye ukajakuwa ni sehemu ya jeshi (k.v. Kut. 18:21). Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: ELFU (*eleph*)

Neno la Kiebrania *eleph* linamaanisha "elfu" (BDB 48, KB 59 II). Linatumika kwa maana mbali mbali katika agano la Kale.

1. sehemu ya familia, Yos. 22:14; Amu. 6:15; 1 Sam. 23:23; Zak. 9:7; 12:6
2. sehemu ya jeshi, Kut. 18:21,25; Kumb. 1:15
3. uhalisia wa tarakimu elfu, Mwa. 20:16; Kut. 32:28
4. ishara ya namba, Mwa. 24:60; Kut. 20:6; 34:7; Kumb. 7:9; Yer. 32:18
5. lenye kufanana na neno la lugha ya Ugaritiki *alluph* linaloamaanisha "mtemi," Mwa. 36:15

Haya madokezo tofauti yanasababisha watafasiri wa leo kuuliza uhalisia wa hesabu

1. za wana wa Israeli waliotoka Misri
2. jamii ya kikabila ya jeshi la Israeli

☐
NASB, NKJV “maakida”

NRSV, TEV “afisa wa serikali”

NJB “waandishi”

Hili neno (BDB 1009) mwanzoni kabisa lilirejelea kwa mwandishi, lakini linaonekana kutoendana na matumizi katika Kumb. 1:15; 20:5,8,9; au Yosh. 1:10,32. Katika muktadha huu inavyoonekana linarejelea mwamuzi wa ngazi ya chini au msaidizi wa viongozi wa kikabila. *The Handbook on Deuteronomy* by UBS kinasema, “nikusanyieni wazee (Hes. 11:16) na waamuzi (Kumb. 16:18; Yosh. 8:33), na katika muktadha wa kijeshi pia (Kumb. 20:5,8,9; Yosh. 1:10; 3:2)” uk. 26.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA):

¹⁶ Nikawaagiza wakati ule waamuzi wenu, nikawaambia, Sikizeni ninyi maneno kati ya ndugu zenu, mkaamue kwa haki kati ya mtu na nduguye, na mgeni aliye pamoja naye. ¹⁷ Msitazame nafsi za watu katika hukumu; mwasikize wadogo na wakubwa sawasawa; msiche uso wa mtu awaye yote; kwa kuwa hukumu ni ya Mungu; na lile neno liwashindalo mnilettee mimi, nami nitalisikiza. ¹⁸ Nikawaamuru wakati huo mambo yote yaliyowapasa ninyi kuyafanya.

1:16-17 Musa akawaagiza hawa waamuzi wapa wa kikabila waamue kwa haki (k.v. 16:19; 24:17). Kutokupendelea ni tabia ya Mungu (k.v. 10:17). Israeli ilimaanisha kuwa ni watu na jamii inayoonyesha tabia za YHWH ili kwamba dunia ipate kuweka imani yao katika Yeye. Tangia anguko (yaani., Mwanzo 3) hili limekuwa ndiyo mpango wa Mungu. Israeli ikashindwa, lakini Mwisraeli kamili (yaani., Yesu, k.v. Isaya 53) akashinda (mf. Yh 14:5-7, 8-11).

☐ **“Mgeni”** Wasio Wayahudi walitakiwa kutendewa sawasawa katika eneo la kisheria (k.v. Law. 19:33-34,35). Israel ilitakiwa kuwatendea kwa upendo (k.v. Law. 23:22; Kumb. 10:19; 24:17; 27:19). Israeli wamekuwa wageni katika Misri (k.v. Kut. 22:21; 23:9) na kujua namna walivyo yapitia!

☐ **“kwa haki”** Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: HAKI

"Haki" ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya ni upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana yenyewe.

Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (kitenzi, BDB 842, KB 1003; nomino jinsi ya kiume, BDB 841, KB 1004; nomino jinsi ya kike, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalumu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii inatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wanadoa wa mwanzo walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21).

Mungu aliahidi kufanya marekebisha na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae. Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko, hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya agano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

1. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya mahakama)
2. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kuzuliwa)

3. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
4. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwikitiko wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

1. Toba
2. Imani
3. Utii kwenye stadi ya maisha
4. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, uliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo. Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa mwalimu wa sheria aliyefundishwa, anatumia neno *dikaio sunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiebrania, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana). Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaeleza katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii) na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msisitizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungu [utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka]).

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu pale Edeni. Biblia inaanza kati ya Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochgulwiwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

1. Mungu ni wa haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
 - a. Warumi 3:26
 - b. 2 Wathesalonike 1:5-6
 - c. 2 Timotheo 4:8
 - d. Ufunuo 16:5
2. Yesu ni haki
 - a. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
 - b. Mathayo 27:19
 - c. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
3. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki.
 - a. Mambo ya Walawi 19:2

- b. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
- 4. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
 - a. Warumi 3:21-31
 - b. Warumi 4
 - c. Warumi 5:6-11
 - d. Wagalatia 3:6-14
- 5. Iliyotolewa na Mungu
 - a. Warumi 3:24; 6:23
 - b. 1 Wakorintho 1:30
 - c. Waefeso 2:8-9
- 6. Iliyopokelewa kwa imani
 - a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
 - b. 2 Wakorintho 5:7,21
- 7. kupitia matendo ya Mwana
 - a. Warumi 5:21
 - b. 2 Wakorintho 5:21
 - c. Wafilipi 2:6-11
- 8. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
 - a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
 - b. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
 - c. Waefeso 1:4; 2:10
 - d. 1 Timotheo 6:11
 - e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
 - f. 1 Yohana 3:7
 - g. 1 Petro 2:24
- 9. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
 - a. Matendo 17:31
 - b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni atabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

1. agizo la Mungu
2. zawadi ya Mungu
3. tendo la Kristo
4. maisha yatupasayo kuishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na barua zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa dhana ya kuwa huru. Calvin anasistiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

1. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
2. injili ni ukweli (msistizo wa Augustine na Luther)
3. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuunganishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

☐“**Mwasikilize wadogo na wakubwa sawasawa**” Neno “upendeleo” kiuhalisia ni “mwonekana” (BDB 815). KITENZI(BDB 647, KB 699, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinamaanisha “kutendea.” Suala hapa ni kuwa jinsi mtu anavyomwendea mwamuzi, mwamuzi asijaribu kutazama au kujua ni nani alikuwa akimwendea, bali ni kusikiliza mashitaka kwa haki pasipo upendeleo. Mwamuzi alitakiwa kuyatendea mashitaka yote kwa haki (k.v. Law. 19:15).

☐“**msiche uso wa mtu awaye yote**” KITENZI hiki(BDB 158 III, KB 185, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinamaanisha “hofu” au “uoga.” Katika muktadha huu “hofu” inahitajika. Katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati hili neno linatumika kwa namna mbili. Viongozi/waamuzi wa Mungu hawapaswi kuhofu majibizo ya watu kwenye maamuzi yao (1:17) na watu wa Mungu hawapaswi kuhofu jumbe za manabii wa uongo (18:22). Hili neno mara nyingi linatumika katika kitabu cha Zaburi kuelezea thamani ya agano la mwamini na hofu ya YHWH (mf. 33:8; 22:23).

☐“**na lile neno liwashindalo mniletee mimi**” Musa alikuwa ni mwakilishi wa Mungu kwa watu. Alionekana kama nabii (k.v. mst. 18; 18:15-22).

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 1:19-21

¹⁹Tukasafiri kutoka Horebu, tukapita katikati ya jangwa lile kubwa la kutisha mliloliona, njia ile ya kuiendea nchi ya vilima vya Waamori, kama Bwana, Mungu wetu, alivyotumuru, tukafika Kadesh-barnea. ²⁰ Nami nikawaambia, Mmefika nchi ya vilima ya Waamori, anayotupa sisi Bwana, Mungu wetu. ²¹ Tazama, Bwana, Mungu wako, ameiweka nchi mbele yako; haya panda, itamalaki, kama Bwana, Mungu wa baba zako, alivyokuambia; usiogope wala usifadhaike.

1:19-25 “Tukasafiri” KITENZI(BDB 652, KB 704, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kila mara linatumika kwenye safari ya kutoka Misri (k.v. Kut. 12:37; 13:20; 14:15; 16:1; na mara nyingi katika Hesabu 33). Mistari hii inahusiana na safari ya kutoka Mlima Sinai kwenda Kadesh-barnea.

1:19 “Horebu” Majina yote mawili ya milima mitakatifu, Horebu na Sinai, yanatumika kwa maana inayofanana. Horebu ni neno la Wasemiti. Sinai si neno la Kisemiti lakini yawezekana linahusiana na mtu wa jangwani. *Sin* ni neno kwa ajili yam mea mdogo umeao jangwani. Wengine wanaamini kuwa Horebu ni safu ya milima na Sinai ndiyo kilele, lakini hatuyajui haya kwa uhakika.

☐“**jangwa lile kubwa la kutisha mliloliona**” Mara nyingi neno “jangwa” (BDB 184) linamaanisha nchi isiokaliwa na watu, lakini safari hii iliwalazimu kupitia jangwa la rasi ya Sinai. Palikuwepo na vyanzo viwili vya maji. Mungu aliwapa maji na chakula kimiujiza kipindi cha miaka arobaini. Leo hii, hili jangwa linaitwa *Et Tih*, likimaanisha “kutangatanga.” Safari hii iliwachukua maili 100 na kukatiza nchi ya milima na mabonde.

☐“**nchi ya vilima vya Waamori**” Hili lingalirejelea upande wa mashariki mwa nchi ya Kaanani (yaani., Negevu, Araba).

☐“**kama Bwana, Mungu wetu, alivyotumuru**” Kwa ajili ya majina ya Uungu tazama mada maalum katika 1:3. Mungu aliwaongoza kwa:

1. Maneno ya Musa
2. Wingu la utukufu(*Shekinah*), lililosimama juu ya hema. Wingu lilipotembea Israel walilifuata.

☐“**tukafika Kadesh-barnea**” Kwa Kiebrania la neno takatifu ni *kadosh* (BDB 871), ambapo tunapata neno “Kadesh.” Kadesh-barnea linamaanisha “takatifu-(lisilolulikana),” yumkini neno “mji mtakatifu” au “mahali patakatifu.” Yalikuwa ni mazingira muhimu ya kambi kwa Waisrael kama ilivyokuwa kwa Ibrahim kwa sababu palikuwa na chemichemi kubwa katika eneo hilo.

1:20-21 mistari hii imesababisha matatizo kwa watoa maoni kwa sababu ya mabadiliko ya utumiaji wake kati ya VIWAKILISHI “wangu/wetu” na “wako/wenu,” ambayo ni ya kawaida kwenye kitabu chote cha Kumbukumbu la Torati. Hii ndiyo sababu mojawapo ya baadhi kuamini kuwa kitabu cha Kumbukumbu la Torati kiliandikwa na watu mbalimbali. Nafikiri kuwa Musa alikiandika sehemu kubwa ya mafunuo, lakini ni dhahili kuwa maandiko yake yamehaririwa na waandishi waliokuja baadaye na yaweza kujumuisha maoni ya mwandishi wa mwanzo.

1:21 “Tazama, Bwana, Mungu wako, ameiweka . . . itamalaki” Hili lawezakuwa ni rejeo kwenye mst. 8, ambapo Mungu, kupitia Musa, aliwaambia watu kuitamalaki nchi aliyowaahidi wazee (k.v. 12:5-7; 13:14-17; 15:18; 26:3). Mstari huu, kama ilivyo mistari ya 7 na 8, inajumuisha amri mbalimbali:

1. “tazama” - BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. “panda” - BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. “itamalaki” - BDB 439, KB 441, *Qal* KAULI SHURUTISHI
4. “usiogope” - BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini likitumika kwa maana ya KUAMURU
5. “usihofu” - BDB 369, KB 365, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini likitumika kwa maana ya KUAMURU

☐
NASB, NRSV “usiogope wala usifadhaike”
NKJV “usiogope wala kukata tamaa”
TEV “usiwe na wasi wala usiogope”
NJB “usiogope wala kukata tamaa”

Katazo hili toka kwa YHWH lilisimamia juu ya imani yao kwenye ahadi ya agano na uwepo wake! Kifungu hiki kinajitokeza mara kumi na mbili katika Agano la Kale (mf., 31:8; Yosh. 1:9; 8:10; 10:25; I Nya. 22:13; 28:20; II Nya. 20:15; 32:7; Yer. 30:10; 46:27).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 1:22-25

²² Nanyi mkanikaribia kila mmoja wenu, mkasema, Na tupeleke watu mbele yetu, ili watupeleleeze nchi na kutuletea habari za njia itupasayo kuipandia, na za miji tutakayoifikia. ²³ Neno hili likanipendeza sana; nikatwaa watu kumi na wawili, mtu mmoja wa kila kabila. ²⁴ Nao wakageuka, wakapanda mlimani wakafika bonde la Eshkoli, wakalipeleleza. ²⁵ Wakatwaa baadhi ya matunda ya nchi ile mikononi mwao, wakatuletea huku chini, wakatuletea habari tena, wakasema, Nchi hii anayotupa Bwana, Mungu wetu, ni nchi njema.

1:22 Hesabu 13:1-3 ni mazingira kwa ajili ya huu mstari. Inakumbusha amri za Musa kwenye makabila:

1. “tupeleke” - BDB 1018, KB 1511, *Qal* HALI YA KUSIHI
2. “watupeleleeze” - BDB 343, KB 340, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, ikitumika kwa maana ya KUAMURU
3. “watuletee” - BDB 996, KB 1427, *Hiphil* KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika kwa maana ya KUAMURU

1:23 “nikatwaa watu kumi na wawili, mtu mmoja wa kila kabila” Musa alikuwa malidadi wa kujaribu na kujumuisha kila kabila ili kila mmoja ajisikie wa muhimu.

1:24 “bonde la Eshkoli” Neno hili (BDB 79) linamaanisha “kishada” au “shina.” Hesabu 13:23-24 inasema kuwa walikata kishada kimoja cha matunda ya mizabibu achacho kilikuwa kikubwa cha kuweza kuchukuliwa na wanaume wawili kwenye upondo. Hivi ndivyo bonde lilipata jina la Kiebrania, lakini mahali lilipo kusini mwa Palestina hapajulikani, yumkini mahali fulani karibu na huko Hebroni (k.v. Hes. 13:22,23).

☐**“wkalipeleleza”** Neno “wkalipeleleza” (BDB 920, KB 1183, *Piel* KAULI ISIOTIMILIFU) ni tofauti kwa ajili ya neno “mguu” (BDB 919), ambalo linadokeza kuwa wakalitembelea eneo lote la nchi. Hawakuwa na wanyama wa kuwapanda na hakika ilikuwa ni safari ya imani kwao kuitembea nchi yote hii na kuonekana kwa wakazi wake.

1:25 “Nchi hii anayotupa Bwana, Mungu wetu, ni nchi njema” ni uthibitisho wa nguvu kiasi gani wa kimaagano! Ingawa , hawakuendelea juu ya tamko la kithiolojia, lakini ni juu ya hofu zao (mf., mst. 21).

ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA):1:26-33

²⁶ Lakini hamkukubali kukwea huko, mlihalifu neno la Bwana, Mungu wenu; ²⁷ mkanung'unika hemani mwenu, mkasema, Ni kwa sababu Bwana ametuchukia, ndipo akatutoa katika nchi ya Misri, apate kututia katika mikono ya Waamori, ili kutuangamiza. ²⁸ Twakwea kwenda wapi? Ndugu zetu wameiyeyusha mioyo yetu, wakituambia, Wale watu ni wengi, ni warefu kuliko sisi; miji nayo ni mikubwa, imejengewa kuta hata mbinguni; na zaidi ya hayo huko tumewaona Waanaki. ²⁹ Ndipo nikawaambieni, Msifanye hofu, wala msiwache. ³⁰ Bwana, Mungu wenu, anayetangulia mbele yenu, ndiye atakayewapigania, kwa mfano wa yote aliyowafanyia huko Misri mbele ya macho yenu; ³¹ na huko jangwani, ulipoona alivyokuchukua Bwana, Mungu wako, kama mtu amchukuavyo mwanawe, njia yote mliyoiendea, hata mkafikilia mahali hapa. ³² Lakini katika jambo hili hamkumwamini Bwana, Mungu wenu, ³³ aliyewatangulia njiani, usiku kwa moto, kuwaonyesha njia mtakayoiendea, na mchana kwa hilo wingu, ili apate kuwatafutia mahali pa kusimamisha hema zenu.

1:26 “mliharifu” KITENZI(BDB 598, KB 632, *Hiphil* KAULI ISIOTIMILIFU) ikajakuwa ni neno la kawaida katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (mf., 1:26,43; 9:7,23,24; 21:18,20; 31:27; na pia katika Zaburi). KISHAMIRISHO chake katika Kiarama kinamaanisha “kubishana” na katika lugha ya Syria, ni “kushindana.” Linaonyesha ukaidi, kutokutii!

☐ **“Neno la Bwana Mungu wenu”** Neno katika mistari ya 8 na 21 ilikuwa ni kwa ajili yao kukwea na kuimiliki nchi.

1:27 “mkanung'unika hemani mwenu” Watu walikuwa mahemani mwao wakinung'unika (BDB 920, KB 1188, *Niphal* KAULI ISIOTIMILIFU); hawakulifanya tendo hili wazi, lakini Bwana akaona mioyo yao (k.v. Zab. 106:25) na kutambua kuwa walikuwa wakiharifu dhidi yake (yaani., “maneno ya uchongezi,” Mith. 16:28; 18:8; 26:20,22). Mungu anajua sio kile tu tunachoongea (k.v. mst. 25c), bali hata kile kilichoko mioyoni mwetu—mienendo yetu (k.v. Hes. 14:1-6).

☐ **“Bwana ametuchukia”** Katika mistari huu watu wanatilia shaka mwenendo na asili ya Mungu (mf., 9:28). Wamekwisha kusahau ahadi zote za ajabu za Mungu wakati wakisafiri toka Mlima Sinai kwenda Kadesh na kuanza kutazama kwenye hali yao ya wakati huo, ambayo waliangalia kama yenye kuangamiza.

1:28 “Ndugu zetu wameiyeyusha mioyo yetu” Watu walijaribu kuwalaumu wapelelezi kwa ajili ya kutokuamini kwao. Neno “kuiyeyusha” (BDB 587, KB 606) ni stia kwa ajili ya mtu mwenye hofu na kupoteza mapenzi ya kuhimili (k.v. 20:8; Yosh. 2:11; 5:1; 7:5; na yumkini 14:8).

☐
NASB, REB “wakubwa na warefu”
NKJV, Peshitta “wengi na warefu”
NRSV, TEV,
NJB, NIV “wenye nguvu na warefu”
NET “wengi zaidi na warefu”

Ni dhahili toka kwenye tafasiri mbalimbali kuwa swali ni kuhusu neno la kwanza. Je ni kisawe au linaongeza habari mpya? KIVUMISHI(BDB 152) kimsingi kinamaanisha “kubwa.” Kinatumika kwenye:

1. Ukubwa katika wingi
2. Ukubwa katika idadi
3. Ukubwa katika nguvu
4. Ukubwa katika thamani yake

Neno lenyewe ni la kawaida na lina maana pana kiasi kwamba muktadha ndiyo unaweza kuielezea maana yake.

Tafasiri ya agano la kale la Kiebrania linaonekana kulielewa hili neno kama “lenye umaarufu zaidi na uweza.” Sehemu ya tatizo la utafasiri ni nafasi ya “majitu” katika agano la Kale!

☐“miji nayo ni mikubwa, imejengewa kuta hata mbinguni ”Kutoka katika elimukale tunapata ushahidi kuhusu baadhi ya hii miji. Lachishi ulikuwa ni mji wa Waamori ulioko kusini ambao ulikuwa na ukuta wenye unene wa futi 29. Kuta za mji huu zilikuwa na mnara adimu ulioinuliwa juu. Mmoja anaweza kutambua ni kwa jinsi gani Waisraeli walijawa na furaha walipoiona miji hii (“imejengewa” BDB 130, KB 148, *Qal* KAULI TENDWA ENDELEU YA WAKATI ULIOPO ikimaanisha “kutopitika kiurahisi”). Kutiwa chumvi kwenye neno hili yaani“imejengewa kuta hata mbinguni” linatumika kwa maana ile ile ya ki-istiari kama jina la *Ziggurats* huko Babeli (k.v. Mwa. 11:4).

☐“Anakimu” Neno (BDB 778 I) kiuhalisia linamaanisha “wenye shingo ndefu.” Hili linarejelea majitu (k.v. Mwa. 6).

MADA MAALUMU: MANENO YATUMIKAYO KWA MASHUJAA/MAKUNDI YA WATU WAREFU/WENYENGUVU

Watu hawawakubwa/warefu/wenye nguvu wanaitwa kwa majina mbali mbali

1. *Nephilim* (majitu,BDB 658, KB 709) - Mwa. 6:4; (angalia Mada Maalum: Wana wa Mungu katika Mwanzo 6; Hes. 13:33)
2. *Rephaim* (huenda BDB 952 II, KB 1274) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:11,20; 3:11,13; Yosh. 12:4; 13:12; II Sam. 21:16,18,20,22; I Nya. 20:4,6,8
3. *Zamzummin* (BDB 273), *zuzim*(BDB 265) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:20
4. *Emim* (BDB 34) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:10-11
5. *Anakim* (wana wa *Anaki*, BDB 778 I) - Hes. 13:33; Kumb. 1:28; 2:10-11,21; 9:2; Yosh. 11:21-22; 14:12,15; 15:14; Amu. 1:20

Angalia namna Mwanzo 14:5 ilivyotaja wanaume watatu wakubwa wa haya makundi (kama vile LXX, Vulgate). Neno *Warefai* pia linatumika kwa viumbe walioko kule kwenye shimo *sheol* (kama vile Ayubu 26:5; Zab. 88:10-11; Isa. 26:14,19).

1:29

NASB “msifanye hofu wala msiwache”

NKJV “msitiwe hofu wala kuwaogopa”

NRSV “msihofu wala kuwaogopa”

TEV “msiwaogope hawa watu”

NJB “usihofu wala kuwaogopa”

KITENZI cha kwanza(BDB 791, KB 888, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) kinamaanisha “sabaisha hofu.” Kwa lugha ya Kiarama kinamaanisha “kutetemeka” na kwa lugha ya Kishamu “kuingiwa kwa nguvu” (k.v. 7:21; 20:3; 31:6). KITENZI cha pili(BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI ISITIMILIFU) kinamaanisha “uoga” au “hofu.” Hili ni neno la kawaida kwa ajili ya uoga:

1. Wa maadui - Kumb. 1:21,29; 2:4; 3:2,22; 7:18,19; 20:1,3; 31:6; Yosh. 11:6
2. Watu wa dunia huwaogopa watu wa Mungu - Kumb. 28:10 (k.v. Yosh. 4:24); Yosh. 9:24
3. Israeli yapaswa kumwogopa/kumhofu/kumheshimu YHWH - Kumb. 4:10; 5:5; 6:2,13,24; 10:12,20; 13:11; 14:23; 17:13,19; 19:20; 21:21; 25:18; 28:58; 31:12; Yosh. 4:24

1:30 “ Bwana, Mungu wenu, anayetangulia mbele yenu ” Hiki ni kifungu cha nguvu chenye kutia moyo kinachoelezea zawadi nzuri ya Mungu—uwepo wake binafsi na mtoaji.Tambua katika mst. 30 aliwatangulia kwenye vita (k.v. 9:3); katika mst. 33 aliwatangulia mbele kuwaongoza kulipita jangwa.

☐“ndiye atakaye wapigania” Huu ndiyo mfano wa “vita takatifu” au *herem* (kujitoka kwenye maangamizo)(BDB 355, mf., Kumb. 2:24; 3:6; 7:2; 20:16-18; Josh. 6:17,21;8:26;10:1,28,37;11:12, 20-21). Hii ni hukumu ya Mungu juu ya Waamori/Wakanaani kwa ajili ya dhambi zao, sio kwa ajili ya Mungu kuwapendelea watu wake (k.v. Mwa. 15:16). Mungu alikwisha wapa watu wa Kanaani nafasi nyingi za kufanya toba, lakini hawakuweza, kwa hiyo

hukumu yake ilikuwa juu yao. Pia Mungu atawahukumu watu wake pindi watakapoenenda kwa namna ya mienendo ya Wakanaani (yaani., Waashuru na Wababeli walioko uhamishoni)! Hapa, Mungu anawaambia watu wake wasihofu bali waamini katika Yeye kwa sababu alikuwa katika upande wao (mf., Kumb. 3:22; 20:4; Yosh. 10:14,42; 11:5-6)!

1:31 “alivyokuchukua Bwana, Mungu wako, kama mtu amchukuavyo mwanawe” Neno “kuchukua” (BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI TIMILIFU) laweza kurejelea kuchukuliana na mtu katika hali ya kimwili au kitu fulani au “kuchukuliana na mtu.” Mungu kama Baba (yaani., mzazi) ni stiari ya ajabu ya kibiblia, familia binafsi (k.v. 8:5; 32:6; Kut. 4:22; Zab. 27:10; 68:5; 103:13; Mith. 3:12; Isa. 1:2; 63:16; Yer. 3:19; Hos. 11:1-4; Mal. 1:6; Mdo. 13:18). Katika Agano la Kale neno “mwana” ni stiari jumuishi kwa ajili ya ubaba wa YHWH kwa ajili ya Israeli, lakini likajakuwa ni la mtu binafsi kwenye ufalme wa Daudi na uzao wake wa kifalme (yaani., Masihi, Zab. 2:2,7; Mdo. 13:33).

1:32 “lakini katika jambo hili” Hili linajumuisha uwepo binafsi, maalum wa Mungu na uangalizi toka kwenye mwito wa Ibrahim (Mwanzo 13) wakati wa kutoka Misri (Kutoka -Hesabu).

☐ **“hamkumwamini Bwana, Mungu wenu”** KITENZI (BDB 52, KB 63, *Hiphil* KAULI ENDELEVU) ni neno kuu la kithiolojia. Ndiyo msingi wa kiini binafsi cha mahusiano ya agano.

MADA MAALUM: KUAMINI, TUMAINI, IMANI NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE.

- I. Maelezo ya awali
Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyoenezwa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.
Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale
 - A. Watu binafsi na jamii
 - B. Ukabiliano binafsi na utii wa aganoImani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani usomaji wa neno). Dhana hii binafsi imeelezwa vizuri katika
 - A. Ibrahim na uzao wake
 - B. Daudi na IsraeliWatu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadilika jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majaribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.
- II. Asili kuu iliyotumika
 - A. אמן (BDB 52, KB 63)
 1. KITENZI
 - a. Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (yaani 2 Fal. 10:1,5; Esta 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)
 - b. Shina la neno *niphal*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu
 - 1) Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14
 - 2) Kwa vitu, Isa. 22:23
 - 3) Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5
 - c. Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini
 - 1) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6
 - 2) Waisrael katika Misri waliamini, Kut. 4:31; 14:31 (ilikanushwa katika Kumb. 1:32)
 - 3) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24
 - 4) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9

- 5) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16
 - 6) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12
 2. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)
 3. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile. Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno “amina” katika agano la kale na agano jipya.
 - B. אמת (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli
 1. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1
 2. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8
 3. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16
 - C. אמונה (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu
 1. Katika mikono, Kut. 17:12
 2. Katika muda, Isa. 33:6
 3. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2
 4. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138
- III. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale
- A. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).
 - B. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katika aya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (אמן).
 1. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rumi 4 na Wagalatia 3.
 2. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pembeni kwa uthabiti) kamwe hautakuwa
 - a) Rum. 9:33 “aibisha” au “katisha tamaa”
 - b) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu
 3. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (kama vile Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)
- IV. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale
- A. Petro anaunganisha
 1. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
 2. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pembeni)
 3. Zab. 118:22 – 1 Pet. 2:7 (jiwe lililokataliwa)
 - B. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo iliielezea Israel kama “jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe” toka
 1. Kumb. 10:15; Isa. 43:21
 2. Isa. 61:6; 66:21
 3. Kut. 19:6; Kumb. 7:6
 na sasa anatomia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (kama vile 1Petro. 2:5,9)
1. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii
- A. Utumiaji wake

Neno “akaamini” linatokana na neno la Kiyunani *pisteuō* ambalo pia laweza kutafasiliwa “ kuamini,” “sadiki,” au “imani.” Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoa kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili “kuamini” unapatikana katika Yohana 8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

B. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi

1. *eis* inamaanisha “ndani ya” muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu
 - a. ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
 - b. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
 - c. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
 - d. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
 - e. ndani ya Yesu (Yohana 12:11; Mdo. 19:4; Gal. 2:16)
 - f. ndani ya nuru (Yohana 12:36)
 - g. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
2. *ev* inamaanisha “katika” kama ilivyo katika Yohana 3:15; Mk 1:15; Mdo 5:14
3. *epi* ikimaanisha “katika” au “juu ya” kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
5. *hoti*, likimaanisha “kuamini kwamba,” inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
 - a. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
 - b. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
 - c. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
 - d. Yesu ni Masiha (Yohana 11:27; 20:31)
 - e. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
 - f. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
 - g. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
 - h. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
 - i. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
 - j. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
 - k. Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

V. Hitimisho

- A. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)
 1. Toba (angalia Mada Maalumu: Toba)
 2. Sadiki/amini (angalia Mada maalumu)
 3. Utii
 4. Usitahimilivu (angalia Mada maalumu: Usitahimilivu)
- B. Imani ya Kibiblia ni
 1. Uhusiano binafsi (imani ya awali)
 2. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (imani katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
 3. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)

Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwa katika sura na mfanano (kama vile Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba “urafiki wa karibu.” Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za “kifamilia” (yaani., utakatifu, kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Petro. 1:15-16). Anguko (kama vile Mwanzo) liliathiri uwezo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (kama vile Ezek. 36:27-38), akitupatia “moyo mpya” na “roho mpya” inayotuwezesha kupitia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye! Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua

Mungu (wote kwa maana ya Wayunani na Waebrania)

- C. Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipya), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusiano na Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipya katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, iliyoonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (kama vile Efe. 2:8-9 na 10)Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

1:33 “aliyewatangulia njiani, usiku kwa moto, kuwaonyesha njia mtakayoiondea, na mchana kwa hilo wingu, ili apate kuwatafutia mahali pa kusimamisha hema zenu” Mungu allitangulia mbele ya watu usiku kwa moto na mchana kwa wingu, ambalo linajulikana kama “*Shekinah* wingu la utukufu” (mf., Kut. 13:21-22; 14:19,24; 19:16-18; 20:21; 24:15,18; 33:9-10; Law. 16:2; Hes. 9:15-23; 14:14; Zab. 78:14) Hili wingu linaonyesha uwepo wa uungu na linapatikana kwenye kitabu kizima cha biblia (mf., I Fal. 8:10,12; Ezek. 1:4; Dan. 7:13; Mt. 24:30; 26:64; Mdo. 1:9-11; I Thess. 4:17; Uf. 1:7). Atakuja mawinguni!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1:34-40

³⁴ Bwana akaisikia sauti ya maneno yenu, akaghadhibika, akaapa, akasema, ³⁵ Hakika yangu hapana mmoja miongoni mwa watu hawa wa kizazi hiki kibaya atakayeiona nchi hiyo nzuri, niliyowaapia baba zenu kuwapa, ³⁶ isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune, huyo ataiona; nami nitampa yeye na watoto wake nchi hiyo aliyoikanyaga; kwa kuwa amemfuata Bwana kwa kila neno. ³⁷ Na Bwana alinikasirikia mimi kwa ajili yenu, akasema, Wala wewe hutaingia humo; ³⁸Yoshua mwana wa Nuni asimamaye mbele yako ndiye atakayeingia; mtie moyo; kwa kuwa yeye atawarithisha Israeli. ³⁹Tena, wadogo wenu, mliosema watakuwa mateka, na wana wenu, wasiokuwa leo na maarifa ya mabaya wala mema, ndio watakoingia, nao ndio nitakaowapa, nao wataimiliki. ⁴⁰ Na ninyi basi geukeni, mshike safari yenu, mwende jangwani kwa njia ya Bahari ya Shamu.

1:34 “akaghadhibika, akaapa” Kifungu kilekile, “akaapa” (BDB 989 KB 1396, *Niphal* KAULI ISITIMILIFU), lilitumika wakati Mungu akijitoa mwenyewe kwenye uhusiano wa maagano pamoja na Israeli. Hapa anajitua Mwenyewe kwenye matokeo ya agano kwa ajili ya kutokutii–laana. Tambua kuwa ahadi ya Mungu kwa Ibrahim ilikuwa ni vizazi vilivyofanikiwa, lakini laana ilikuwa tu kwa kizazi kimoja, ambao ulikuwa ndiyo uovu wa awali (yaani., kutokuamini katika ahadi za YHWH za kuwapa Kanaani) kizazi kilichotoka Misri.

1:35 Wanaume wote wa umri wa kwenda jeshi (yaani., miaka 20 na kuendelea), waliokataa kufuata maagizo ya YHWH na kuimiliki nchi, wataadhibiwa na watu watatangatanga jangwani mpaka umauti utakapowajilia (yaani., miaka 38). Kitabu cha Waebrania kwenye agano Jipya, sura ya 3-4, kinarijadili suala hili la kutokuwa na imani. Ni wapelelezi wawili tu kati yao ndiyo walirudia taarifa nzuri, Kalebu (k.v. mst. 36) na Yoshua (k.v. 1:38),hawakujumuishwa. Kutolitii agano matokeo yake yalikuwa ni laana ya agano kwa ajili ya Israel (k.v. Kumbukumbu la Torati 27-29) na Musa (k.v. Kumb. 3:26-27).

☐“nchi hiyo nzuri” Hiki ni kifungu chenye kujirudia (k.v. Kut. 3:8; Kumb. 1:35; 3:25; 4:21,22; 8:7,20; Yosh. 23:13). Neno nzuri lilimaanisha (1) uwepo wa Mungu (yaani., Mungu ni “mwema,” Zab. 86:5; 100:5; 106:1; 107:1; 118:1,29; 145:9; na pia tambua ufanano wa Amosi 5:4,6,14,15) na (2) “nchi inayotiririsha maziwa na asali” (mf. Kut. 3:8,17; 13:5; 33:3; Hes. 13:27; 14:8; 16:13,14; Kumb. 6:3; 11:9; 26:9,15; 27:3; 31:20; Yosh. 5:6).

1:36 “nchi hiyo aliyoikanyaga ” Nchi ambayo Kalebu ataitwaa na hatimaye kuimiliki ipo maeneo ya Hebroni. Tunafikiria ipo karibu na bonde la Eshcoli (k.v. Yosh. 15:13), mahali ambapo majitu yaliishi!

☐“kila neno” Hii inamaanisha “kwa moyo wote” (BDB 569, KB 583, *Piel* KAULI ILIYO TIMILIFU). Inarejelea kwa mtu asiye na michanganyo ya mienendo; Kalebu alimpenda YHWH kwa moyo wake wote na kumufuata Yeye. Ni stiari ya kujitua kwa ukweli (mf. Hes. 14:24; 32:11-12; Yosh. 14:8,9,14; I Fal. 11:6). Linafanana na kifungu, “kwa moyo

wako wote na roho yako yote” (k.v. Kumb. 6:5; 10:12; 13:3; 30:2; I Fal. 9:4; 11:4).

1:37 “Na Bwana alinikasirikia mimi kwa ajili yenu” Musa alikuwa akijaribu kuwalaumu watu kwa ajili ya ukaidi wao (k.v. Kumb. 3:26, kama vile Adam alivyojaribu kufanya, k.v. Mwa. 3:12), lakini tambua Hes. 20:7-13,24; 27:14; Kumb. 4:21. KITENZI“alinikasirikia” (BDB 60, KB 72, *Hithpael* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) inatokana na NOMINO ya neno “tundu la pua” au “pua.” inavyoonekana linarejelea kwenye (1) kutanuka kwa matundu ya pua kama alama ya hasira au (2) kutoa sauti ya kukoroma. Hili neno linatumika kwa mwendelezo kwa ajili ya hasira (lugha za kibinadamu) ya kiungu (k.v. Kut. 32:12; Kumb. 1:37; 4:21; 9:8,20; II Kgs. 24:20). Matumizi mengine ya neno hili lenye kuendana na kifungu, “si mwepesi wa hasira,” ambalo linasisitiza juu ya subira ya Mungu na ustahimilivu (mf. Kut. 34:6; Hes. 14:18; Neh. 9:17; Mhubiri. 14:29).

1:38 “³⁸Yoshua mwana wa Nuni asimamaye mbele yako” Kifungu, “asimamaye mbele yenu,” ni nahau ya Kiebrania yenye kumrejelea kiongozi. Yoshua alikuwa ni msaidizi wa Musa na hili lawezakuwa ni unabii wa kazi za uongozi siku za baadaye.

☐“**mtie moyo**” KITENZI(BDB 304, KB 302, *Piel* KAULI SHURUTISHI) kinamaanisha “kumtia nguvu” (mf., 3:28). YHWH Mwenyewe amelifanya hili katika Yosh. 1:6,7,9,18!

☐“**kwa kuwa yeye atawarithisha Israeli**” Ahadi hii inarejea nyuma kwenye nabii zilizotolewa kwa wazee (mf. Mwanzo 12, 15, 18, 26) kuhusiana na kizazi chao kuimiliki Kanaani (mf. 3:28; 31:7; Yosh. 11:23).

1:39 “Tena, wadogo wenu, mliosema watakuwa mateka” Hili linarejelea kwenye Hesabu 14:3,31. Kwa sababu ya wakubwa kutokuamini kwao Mungu anawaambia kuwa watoto wenu hakika watairithi nchi kama alivyokwisha kuahidi.

☐“**wasiokuwa leo na maarifa ya mabaya wala mema**” Kihistoria hili linarejelea watoto waliotoka huko Misri. Mungu hakuwapa majukumu mpaka pale walipopata uwezo wa kulielewa agano na kuapa kilisimamia. Katika andiko hili pande mbili zaweza kuonekana katika:

1. “nitawapeni” (ukuu wa Mungu, k.v. mst. 8)
2. “wataimiliki” (uchaguzi wa mwanadamu na kuwajibika, k.v. mst. 8)

Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: UMRI WA UWAJIBIKAJI

Kanisa, likimfuatisha Paulo, limejielekeza juu ya Mwanzo 3 kama chanzo cha dhambi ya mwanadamu. Hili limekuwa ndani ya msisitizo wa Augustino/Calvin juu ya umiliki wa moja kwa moja (yaani., mwanadamu kutoweza kujongea kwa Mungu pasipo msaada). Hili likajakuwa ni nguzo tano za Calvin zenye kusisitiza ukuu wa Mungu na kanuni za msingi za mkristo. Hata hivyo, walimu wa sheria kamwe hawakutilia maanani juu ya Mwanzo 3 kama chanzo cha uovu (baadhi walitilia mkazo juu ya Mwanzo 6), bali juu ya uwajibikaji binafsi unaosimamia juu ya maarifa na kujitolea kikamilifu. Wangalidai makusudio mawili (*yetzers*), moja jema na lingine ovu. Mfano wa hali ya juu ungalikuwa ni msemu, “katika kila moyo wa mwanadamu kuna mbwa wawili, mmoja mzuri mwingine mbaya. Yule anepeshwaye sana ndiye anayekuja kuwa mkubwa.” Kwa hiyo, wanadamu peke yao wanawajibika baada ya kipindi cha ukomavu na maarifa ya agano/kujitolea kikamilifu (yaani., *Bar Mitzvah* kwa ajili ya vijana wenye umri wa miaka 13 na *Bat Mitzvah* kwa ajili ya mabinti wa umri wa miaka 12). Mifano mingine ya Kibiblia ya mtazamo wa kithiolojia ni Yona 4:11 na Isaya 7:15-16.

Kuyaweka haya katika maneno yanayokinzana:

1. Paulo/Augustino/Calvin waliangalia juu ya ukuu wa Mungu na kutokuweza kwa mwanadamu.
2. Walimu wa sheria/Yesu/Paulo waliangalia juu ya uwajibikaji wa kimaagano.

Sio suala la huenda ni hili/au, bali ni yote! Uwe mwangalifu na muundo wa kithiolojia! Tambua kuwa ukweli wa kibiblia umewasilishwa katika hali ya jozi zenye kujawa na mvutano. Waamini wanapaswa kuishi maisha ya kiungu ndani ya mvutano huo, na sio kwenye shauku ya haraka, maswali lahisi au ucheze mchezo wa

1:40 “njia ielekeayo Bahari ya Shamu” Hii inaonekana kuwa rejeo kwenye barabara iitwayo “Njii Kuu ya Mfalme” inayoelekea kandokando ya ghuba ya Aqaba tokea Elath hadi Kadesh-barnea (k.v. Hes. 14:25; 20:17; 21:22). Hii hairejelei kwenye ziwa lililoko huko Misri walilolipita mwanzoni wakati Waisraeli wakitoka Misri, hadi hapo itakapomaanisha hivyo“ .

MADA MAALUM: BAHARI YA SHAMU (BDB 410 MUUNDO WA MANENO BDB 693 I)

I. Jina

A. Kiuhalisisia jina lake ni *Yam Suph*.

1. "ziwa la magugu" au "ziwa la mafunjo" (mzizi wa lugha ya Kimisri)
2. "Bahari iliyoko pembezoni (mwa nchi)" (mzizi wa lugha ya kisemiti)

B. Hili linaweza kurejelea

1. maji chumvi, 1 Fal. 9:26 (Ghuba ya Aqaba); Yona 2:5 (Bahari ya Mediterranean)
2. maji baridi, Kut. 2:3; Isa. 19:6

C. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania ni tafasiri ya kwanza kuliita "Bahari ya Shamu." Yumkini hawa watafasiri walikuwa wakihusianisha na Bahari ya Edomu. Huu uteuzi uliwezesha na toleo la Latin Vulgate na baadaye na King James English translation.

II. Mahali lilipo

A. Kuna maziwa mengi yanayorejelewa kwa jina hili.

1. Ziwa jembamba kati ya Misri na rasi ya Sinai yapata urefu wa maili 190 (Ghuba ya Suez)
2. Ziwa kati ya rasi ya Sinai na Arabia yapata urefu wa maili 112 (Ghuba ya Aqaba)

B. laweza kuhusishwa na eneo la bwawa fupi lenye tope sehemu ya kaskazini mashariki mwa Nile delta karibu na Tanis, Zoan, Avaris, Rameses, iliyoko pwani ya kusini mwa Ziwa Menzaleh (eneo lenye tope jingi).

C. laweza kutumika kistiari kumaanisha maji ya ajabu upande wa kusini, mara nyingi likitumika kumaanisha ziwa lililoko pembezoni (mwa nchi). Hii inamaanisha laweza kurejelea:

1. Bahari ya Shamu ya leo (Ghuba ya Suez au Ghuba ya Aqaba, k.v. 1 Fal. 9:26)
2. Bahari ya Hindi (k.v. Herodotus 1.180)
3. Ghuba ya Persia (k.v. Josephus)

III. Suph katika Hesabu 33

A. Katika Hes. 33:8 maji yaliyogawanyika kimiujiza huitwa *suph* (BDB 693 I, "mafunjo" au "magugu").

B. Katika Hes. 33:10,11 Waisrael walisemekana kuweka kambi *yam suph* (ziwa la mafunjo/magugu).

C. kuna aina mbili tofauti za maji.

1. ya kwanza yasiyo ya Bahari ya Shamu (Ghuba ya Suez)
2. ya pili yumkini ni Bahari ya Shamu (Ghuba ya Suez)

D. Neno *suph* linatumika katika Agano la Kale kwa namna tatu.

1. Umbo la maji lililogawanywa na YHWH kuwaruhusu Waisraeli kupita, lakini wanajeshi wa Kimisri wakazama ndani
2. kuenea kaskazini magharibi mwa Bahari ya Shamu (Ghuba ya Suez)
3. kuenea kaskazini mashariki mwa Bahari ya Shamu (Ghuba ya Aqaba)

E. yumkini *Yam suph* haimaanishi "bahari ya mafunjo" kwa sababu

1. hapakuwepo na mafunjo kwenye Bahari ya Shamu (maji chumvi)
2. asili ya neno dhaniwa la Kimisri linarejelea kwenye nchi, na sio ziwa

F. Neno *Suph* laweza kutokana na mzizi wa Kisemiti wa neno "mwisho" (BDB 692) na kurejelea kwenye maji yasiojulikana na maaajabu upande wa kusini (tazama Bernard F. Batts, "Red Sea or Reed Sea? What Yam Suph Really Means" in *Approaches to the Bible*, juzuu 1, kr. 291-304).

ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA): 1:41-46

⁴¹ Ndipo mkanijibu, mkaniambia, Sisi tumefanya dhambi juu ya Bwana, tutakwea kupigana kwa mfano wa yote tuliyoamriwa na Bwana. Mkajifunga kila mtu silaha zake za vita, mkafanya wepesi kukwea mlimani. ⁴² Bwana akaniambia, Uwaambie, Msiende, wala msipigane; kwani mimi si kati yenu; msije mkapigwa mbele ya adui zenu. ⁴³ Basi niliwaambia, msinisikize, bali mliasi amri ya Bwana, mkajikinai, na kukwea mlimani. ⁴⁴ Na Waamori waliokuwa wakikaa katika mlima huo, waliwatokea juu yenu, wakawafukuza, kama wafukuzwao na nyuki, wakawapomoshea Seiri mpaka Horma. ⁴⁵ Mkarudi mkalia mbele za Bwana; Bwana asiisikize sauti yenu, wala hakuelekeza masikio yake kwenu. ⁴⁶ Ndipo mkakaa Kadeshi siku nyingi, kwa kadiri ya hizo siku mlizokaa.

1:41 “tumefanya dhambi juu ya Bwana, tutakwea kupigana” Haya ni madhara ya wazi yanayohusiana na toba. Kithiolojia hili linaonyesha kuwa mara nyingi fursa walioipoteza, kwa sababu ya kutokuamini kwao, haiwezi kurejeshwa. Huu muktadha kwa wazi unaonyesha kuwa walikuwa hawamtii YHWH (k.v mst. 43). Huu ukweli wa kithiolojia ni kitovu lengwa cha simulizi nyingi za kihistoria ya Agano la Kale.

1:42 “Mimi si kati yenu” Namna ya ushindi haikuwa juu ya nguvu yao ya kijeshi, bali ni uwepo wa YHWH (k.v mst. 43).

1:43 Tambua maelezo yenye kufanana juu ya Israel:

1. “msinisikize” - BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU
2. “mliasi amri ya Bwana” - BDB 598, KB 632, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU
3. “mkajikianai” - BDB 267, KB 268, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU

Kama Israel ingamsikiliza YHWH mapema na kukifanya hiki kitu wanalifanikiwa, lakini kwa kukifanya hivi sasa inaonyesha dhahili mwendelezo wao binafsi wa kuutetea ukaidi! Muktadha huu kwa wazi unaonyesha kuwa utii ni wa muhimu kuhusiana na ahadi yao ya agano, uwepo na nguvu!

1:44 “Na Waamori waliokuwa wakikaa katika mlima huo” Tazama Mada Maalum: Waisraeli wa Mwanzo walioishi Palestina katika 1:4.



NASB “akawafukuza”

NKJV “kuwafukuza kurudi nyuma”

NRSV “wakawapomoshea chini”

TEV “kuwafukuza”

NJB “wakawakimbiza”

KITENZI(BDB 510, KB 507, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU) kinamaanisha “kuwapiga na kuwaangusha.” Hili limeandikwa katika kitabu cha Hes. 14:45. KIVUMISHI kilitumika kukamua mafuta toka kwenye mizeituni (k.v. Kut. 29:40; Hes. 28:5). Linatumika kwa ajili ya kumteketeza (1)ndama wa dhahabu (k.v. Kumb. 9:21) na (2) kuziteketeza sanamu (k.v. Mika 1:7).

☐“toka Seiri” Seiri inarejerea Edomu.



NASB, NKJV,

NJB “Horma”

NRSV, TEV “kama vile Horma”

Horma linamaanisha “eneo lililozuiwa.” Neno (BDB 356) linamaanisha “moyo wa uharibifu,” linaloaksi kwenye Hes. 21:3. Mwanzoni kabisa iliitwa Zephathi (k.v. Amu. 1:17). Baada ya Waisraeli kuuangamiza, waliuita kwa ajili ya YHWH(kama ilivyo Yeriko, Yohua 6-7). Mji huu ulikuwa umekalia eneo la kabila la Simioni, kaskazini mashariki mwa Beersheba. KIHUSISHI(BDB 723 III) kinadokeza kuwa Wakanaani/Waamori waliwafukuza Waisrael huko Edomu (Seiri) kwenda eneo hili kaskazini mashariki mwa Beersheba, ambapo waliwashinda moja kwa moja!

YHWH hakuwa pamoja na uasi wao na watu wenye majivuno!

1:45 “Mkarudi mkalia mbele za Bwana” Kwan je watu walionekana wakilia, lakini Mungu alijua mioyo yao. Yalikuwa ni masikitiko yaliyojikita kwenye matokeo ya jambo, na wala sio toba.

☐ **“Bwana asiisikize sauti yenu, wala hakuelekeza masikio yake kwenu ”** Sio kwamba Mungu hakuwasikia, bali hakujisikizisha kwao. Aliwasikia, lakini akasema “hapana.” Dhambi mara zote huleta madhara, hata dhambi iliyokwisha samehewa!

MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozowa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni nini kusudi la msingi la kitabu cha Kumbukumbu la Torati?
2. Kwa nini Sihoni na Ogu imetajwa hapa kiufupi wakati wameelezwa kiundani katika sura ya 2 na 3?
3. Orodhesha vitu muhimu vinavyohusiana na muundo wa kimahakama wa Musa?
4. Ni wapi wale majitu walikotoka?
5. Kwa nini Mungu aliikasirikia Israeli?
6. Je! toba ya Israeli iliweza kuathiri maamuzi ya Mungu?

KUMBUKUMBU LA TORATI 2

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Miaka ya jangwani	Pitio la Kihistoria (1:1-3:29)	Miaka katika jangwa 1:46-2:1	Tokea Kadesh mpaka Arnoni
2:1-7		2:2-6	2:1-7
		2:2-7	
2:8-15	2:8b-13a	2:8-9	2:8-13a
		2:10-12	
	2:13b-15	2:13-15	2:13b-15
2:16-23	2:16-25	2:16-19	2:16-25
		2:20-23	
2:24-25		2:24-25	
Mfalme Sihoni		Israeli inamshinda	Mapambano ya ufalme wa
Anashindwa		Mfalme Sihoni	Sihoni
2:26-37	2:26-30	2:26-27	2:26-29
		2:28-30	2:30-37
	2:31-37	2:31-37	

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

Ainicho Fupi la Sura ya 2

- A. Mahusiano ya Israeli na Edomu, mstari wa 4-7
- B. Mahusiano ya Israeli na Moabu, mstari wa 8-15
- C. Mahusiano ya Israeli na Amoni, mstari wa 16-19
- D. Mistari ya 20-23 ni maelezo ya ziada yanayohusiana na Warefai (Angalia Mada Maalum katika 1:28)
- E. Mahusiano ya Israeli na Waamori katika ukingo wa Mashariki wa Yordani, mstari wa 24-37

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 2:1-7

¹Ndipo tukageuka, tukashika safari yetu kwenda jangwani kwa njia ya Bahari ya Shamu, kama alivyoniambia Bwana; tukawa kuizunguka milima ya Seiri siku nyingi. ²Bwana akanena, akaniambia, ³Mliviyouzunguka mlima huu vyatosha; geukeni upande wa kaskazini. ⁴Nawe waagize watu, uwaambie, Mtapita kati ya mpaka wa ndugu zenu wana wa watu, uwaambie, Mtapita kati ya mpaka wa ndugu zenu wana wa Esau waketi Seiri; nao watawaogopa; basi jiangalieni nafsi zenu sana; ⁵msitete nao; kwa maana sitawapa katika nchi yao kamwe, hata kiasi cha kukanyaga wayo wa mguu; kwa kuwa nimempa Esau milima ya Seiri kuwa milki yake. ⁶Nunueni vyakula kwao kwa fedha, mpate kula; na maji nayo nunueni kwao kwa fedha, mpate kunywa. ⁷Kwa kuwa Bwana, Mungu wako, amekubarikia katika kazi yote ya mkono wako; amejua ulivyotembea katika jangwa kubwa hili; miaka arobaini hii alikuwa nawe Bwana, Mungu wako; hukukosa kitu.

2:1 “Jangwani” Kuna “nyika” kadhaa zinazohusiana na safari ya Wana wa Israeli Kutoka Misri.

MADA MAALUM: SAFARI YA JANGWANI

1. Jangwa la Shuri - katika kaskazini mashariki mwa Misri (mfano Kut. 15:22)
2. Jangwa la Parani – ghuba ya kati ya Sinai (mfano Mwa. 21:21; Hes. 10:12; 12:16; 13:3,26)
3. Jangwa la Sin – ghuba ya kusini mwa Sinai (mfano Kut. 16:1; 17:1; Hes. 33:11,12, pia likiitwa “jangwa la Sinai,” mfano Kut. 19:1,2; Hes. 1:1,19; 3:4; 9:1,5)
4. Jangwa la Zin – kusini mwa Kanaani (mfano Hes. 13:21; 20:1; 27:14; 33:36; 34:3; Kumb. 32:51)

☐ “kwa njia ya Bahari ya Shamu” Hii inamaanisha njia ya Araba (kama vile TEV “njia ya Ghuba ya Akaba”), katika Bonde la ufa la Yordani ambalo liko kaskazini na kusini pande zote za Bahari ya chumvi (kama vile mstari wa 8). Ni bonde kubwa pana ambalo linaanzia karibu na miji ya Elathi au Ezioni-geberi katika ghuba ya Akaba na kwenda kupita katikati ya Edomu na Moabuna Moabu na ufalme wa Waamori mpaka Dameski, Siria. Katika Agano la Kale linaitwa “Njia Kuu ya Mfalme” (mfano Hesabu 20:17 na 21:22).

Neno “Bahari ya Shamu” (BDB 410 MUUNDO WA MANENO pamoja na 693) dhahiri ni “bahari ya mafunjo/magugu.” Neno hili linatumika kwa “Maji yasiyojulikana na yenye maajabu yaelekeayo kusini.” Linaweza kumaanisha maji ambayo wana wa Israeli walivuka katika safari ya kutoka Misri na, kama hapa 1:40, maji yanaitwa Ghuba ya Agaba upande wa mashariki zaidi mwa ukingo wa Sinai. Katika kifungu cha Agano la Kale, neno linamaanisha Bahari ya Hindi. Angalia Mada Maalum katika 1:40.

☐ “kama BWANA alivyoniambia” Kumbukumbu la Torati linajitambulisha lenyewe kama ufunuo kutoka kwa YHWH kwenda kwa Musa (kama vile Mistari ya 1,2,9,17,31). YHWH aliwaongoza watu wake kwa:

1. ufunuo wa moja kwa moja kwa Musa (kama vile mstari wa 2)
2. mtembeo wa wingu la utukufu liitwalo *Shekinah*
3. matumizi ya *Urim* na *Thummim* (yaani Kuhani Mkuu)

☐ “Mlima Seiri” Hii inarejerea nchi ya Edomu (kama vile mistari ya 5; 1:2; Kutoka. 3:1; 17:6).

2:3

NASB	“mlivyozunguka”
NKJV, NRSV	“zunguka”
TEV	“tanga tanga”
NJB	“kwenda mbali sana”

Hiki KITENZI (BDB 685, KB 738, *Qal* KITENZIJINA HALISI katika mstari wa 3 na *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU katika mstari wa 1) inamaanisha “kugeuka,” “kuzunguka,” “kuzunguka.” Wana wa Israeli hawakuwa na mwelekeo sawia kwasababu ya kuwa kizazi kiovu kisichoamini. Walizunguka zunguka huko Kadeshi-barnea kwa miaka thelathini na minane, lakini YHWH yuko tayari kutoa mwelekeo sawasawa kwa Musa. “Geuka kwa kuzunguka” au “zunguka” inashabihiana na andiko hili vizuri zaidi.

☐ **“Sasa geuka kaskazini”** Hii inaweza kurejerea kwa Hesabu 20, ambapo Wana wa Israeli waliuliza ikiwa wangeweza kupitia nchi ya Edomu lakini watu wa Edomu hawakuwaruhusu. Waliomba kupita katika nchi ya Wamoabu lakini nao walisema hapana. Hii inaweka kumbukumbu kwa tukio la mapema (kama vile ICC uk. 34). Hapa wanaomba ikiwa wapitie katika njia Kuu ya Mfalme ambayo inapitia katikati ya nchi hizi. Walikuwa tayari kununua chakula na maji lakini watu wa Edomu na Wamoabu (ndugu wa wana wa Israeli kupitia Lutu na Esau) walisema, “Hapana.” Kuliko kupita Edomu, walipita katika mipaka yao.

Kama ilivyo maneno mengi ya Kiebrania, hili (BDB 815, KB 937) lina maana ya kibayana inayoeleweka (mfano, hapa) na maanailiyokuzwa kimaana kisitari. “Geuka” ni neno la Kiebrania ambalo mara kwa mara linatafsiriwa kama “tubu” (mfano, 2 Wafalme 17:13; 2 Nyakati 30:6; Isa. 44:22; Yer. 3:11-4:2; Hosea 14:1).

2:4 “amri” Hili neno (BDB 845, KB 1010, *Piel* KAULI SHURUTISHI), kama “geuka” (BDB 815, KB 937, *Qal* KAULI SHURUTISHI) katika mstari wa 3, inaonesha kwamba Musa anaweka kumbu kumbu amri za YHWH (kama inavyofanya *Hithpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inavyotumika kama KAULI AMRISHI katika mstari wa 5, “msiwachokoze”). Yeye mwenyewe aliwaongoza katika safari yao.

☐

NASB “ndugu zenu”

NKJV “ndugu zenu”

NRSV “ndugu zenu”

TEV “ndugu zenu wa mbali”

NJB “ndugu zenu”

Tafsiri ya Kingereza inaonesha maana zaidi za neno la Kiebrania “ndugu” (BDB 26). Linatumika mara kadhaa juu ya Edomu (wazao wa Esau, kama vile Hes. 20:14; Kumb. 2:4,8; Obadia mstari wa 10)

☐ **“nao watawaogopa”** Hii ni kauli ya kinabii ambayo inarejerea wimbo wa Ukombozi ambao Miriam anamtukuza Mungu kwa ajili ya kuvuka Bahari ya Shamu. Mungu alitabiri kwamba “Edomu na Wamoabu wangewaogopa Waisraeli” (kama vile Kutoka 15:15).

2:4, 9, 19 Katika sura hii nzima kuna kauli za maana zinazounganisha mamlaka ya kiungu ya Mungu:

“Nitawapa” (mstari 5, 9, 19)

“Nimewapa” (mstari 5, 9)

“Bwana alitoa” (mstari wa 12)

“BWANA Mungu wetu anatupatia” (mstari wa 29)

“Mungu alimweka katika mikono yetu” (mstari wa 33)

Sura hii inaonesha ukuu wa YHWH katika mipaka ya kimataifa (kama vile 32:8; Neh. 9:22), kwasababu kila ya tungo hizi inaweka mkazo kwamba YHWH ni yeye aliyewapa ardhi watu fulani ili warithi. Sura hii inaonesha kwamba YHWH hakuwapa tu peke yao wana wa Israeli bali aliwapa na baadhi ya mataifa mengine. Baadhi walipoteza ardhi zao kwa sababu ya dhambi (kama vile Mwa. 15:16) na Israeli nayo iliwahi poteza ardhi yake kwa muda fulani (yaani uahamisho wa Ashuru na Babeli) kwasababu ya dhambi zake. Hii inaeleza kwamba YHWH ni Mungu wa Ulimwengu wote. Katika nyakati za ibada za miungu wengi, habari hii ni nzuri juu ya ibada ya Mungu mmoja. Kuna Mungu mmoja na Mmoja tu, Kumb. 6:4-6. Ni yeye awapaye ardhi hata Waedomu, Wamoabu, Waamori, n.k. (hasa, Kumb. 32:8 katika Tafsiri ya Agano la Kale ye Kiyunani [LXX]).

☐

NASB, NRSV

REB “hivyo mkawe waangalifu”
 NKJV “hivyo jiangalieni wenyewe mkawe waangalifu”
 TEV (“inaunganisha kifungu hiki na kinachofuata katika mstari wa 5, “lakini msianzishe vita”)
 NJB “nanyi mtalindwa vyema”

Kifungu bayana ni “hivyo jiangalieni” (KIUNGANISHI, KITENZI [BDB 1036, KB 1581, Niphal KAULI YA WAKATI TIMILIFU], na KIELEZI [BDB 547]). Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale ni sawasawa na TEV.

Tungo hii katika namna tofauti tofauti inatumika mara kadhaa katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 2:4; 4:9,15,23; 6:12; 8:11;11:16; 12:13,19,30; 15:9; 24:8). Inamaanisha, “wekeni fahamu zenu katika kufikiri hili,” “kuweni makini na kile mnachokifanya,” “Fikiri sawasawa juu ya maana za matendo yenu.”

2:5

NASB “hata kiasi cha kukanyaga wayo wa mguu”
 NKJV “hata kiasi cha kukanyaga wayo wa mguu”
 NRSV, NJB “hata kiasi cha urefu wa mguu”
 TEV “hata kiasi cha mraba wa mguu”

Hili ni neno nadra la Kiebrania (BDB 204). Linarejerea mahali pa kukanyaga. Asili hiyo hiyo ya neno inatumika katika 11:24 na Yosh. 1:3. Katika maana kwamba hili lilikuwa ni neno la kutia moyo kutoka kwa YHWH. Alikuwa ametoa ardhi kwa wote Edomu na Moabu. Ilikuwa ni yao kila sehemu yake! Alikuwa yuko katika mchakato wa kuwapa ardhi wana wa Israeli. Zawadi yake yenye msaada wa ardhi ilikuwa ya usalama.

Sasa lazima iongezwe kwamba hatimaye kwasababu ya dhambi, mataifa haya (yaani Edomu na Moabu) walipoteza ardhi yao na waliangamizwa kama watu. Zawadi zote za ardhi zilikuwa za masharti. Na hii iko hivyo hivyo kwa Israeli (yaani uhamisho wa kishuru na Babeli). Maagano yote ya Mungu (isipokuwa Mwanzo 6 na 15) ni yenye masharti.

Ahadi zake na ukombozi wake ni hakika (bila masharti), lakini kila mtu/taifa lazima liitikie na kuendelea kwa mwenendo ule ule! Mahusiano yanayoendelea na yenye utifu wa kiimani ni muhimu. YHWH anataka Imani, toba, utii na ustahimilivu katika Agano la Kale na Agano Jipya.

2:6 Israeli walitakiwa kununua chakula na maji kama ishara ya kutambua ukuu wa Edomu juu ya ardhi yao ambayo walipewa na YHWH.

1. “Nunueni chakula” (BDB 991, KB 1404, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
2. “Nunueni maji” (BDB 500, KB 497, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)

2:7 “Miaka hii arobaini BWANA Mungu wenu amekuwa pamoja nanyi:hamkukosa chochote” Kifungu hiki kinaelezea upendo wa Mungu hata katikati ya uasi wa Israeli kinyume naye (yaani kukosekana kwa imani katika ahadi zake za kuwapa ardhi ya Kanaani).

Kipindi cha kutangatanga Jangwani kilikuwa hukumu kwa kizazi cha Wana wa Israeli wenye imani haba, lakini kiligeuka kuwa muda wa uwepo binafsi wa YHWH na utoaji. Walimuwa Kiyahudi wanakiita kipindi cha fungate kati ya YHWH na Israeli. YHWH alitoa:

1. ulinzi
2. mwongozo binafsi
3. chakula
4. maji
5. nguo ambazo hazikuchakaa
6. ushindi katika vita

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2:8-15

⁸Basi tukapita kando yao ndugu zetu wana wa Esau, waketio Seiri kutoka njia ya Araba, kutoka Elathi na kutoka Esion-geberi. Tukageuka tukapita njia ya bara ya Moabu. ⁹Bwana akaniambia, usiwasumbue Wamoabi, wala usishindane nao katika mapigano; kwa kuwa sitakupa katika nchi yake kuimiliki; kwa sababu

Ari nimewapa wana wa Lutu kuimiliki. ¹⁰(Walioketi humo hapo kale ni Waemi, nao ni watu wakubwa, wengi, warefu, mfano wa Waanaki; ¹¹na hawa nao wadhaniwa kuwa majitu kama Waanaki;lakini Wamoabi huwaita Waemi. ¹²Na Wahori nao walikuwa wakikaa Seiri hapo kale, lakini wana wa Esau waliwafuata; wakawaangamiza mbele yao, wakakaa badala yao; kama alivyofanya Israeli nchi ya milki yake aliyopewa na Bwana.) ¹³Sasa basi ondokeni, mkakivuke kijito cha Zeredi. Nasi tukakivuka kile kijito cha Zeredi. ¹⁴Na siku tulizokuwa tukienda kutoka Kadesh-barnea hata tulipovuka kijito cha Zeredi, zilikuwa ni miaka thelathini na minane; maana, hata walipokwisha kuangamizwa watu wa vita kutoka kati ya marago, kizazi chao chote, kama walivyoapiwa na Bwana. ¹⁵Tena mkono wa Bwana ulikuwa juu yao ili kuwaangamiza, kuwatoa kati ya marago, hata walipokoma.

2:8 “Basi tukapita kando yao ndugu zetu wana wa Esau, waketio Seiri”Matumizi ya neno “ndugu” kwa namna fulani ni kinyume. Walikuwa ndugu. Walitokea katika ukoo mmoja, Isaka na Rebeka lakini hawakuwa wakionekana kama ndugu.

Neno “Seiri” linarejerea mlima mrefu katika nchi ya Edomu. Hivyo neno “Seiri” na “Edomu” vinafanana.

2:8, 27 “Njia Araba”Hii inarejerea “Njia Kuu ya Mfalme,” kutokea Ghuba ya Agaba mpaka Dameski (kama vile mstari wa1 na Hes. 20:17,19; 21:22).

2:8 “Elathi”Dhahiri hii ni “miti ya minazi” (BDB 19). Hili linawezekana likawa karibu na Ezioni-geberi (kama vile I Wafalme 9:26), ambalo lipo mwishoni, kaskazini mwa Ghuba ya Agaba.

☐**“Njia ya Jangwa la Akaba”**Biblia ya Macmillan Bible Atlas, ramani ya 10, inaonesha hii njia ya jangwa ni kama ile “Njia Kuu ya Mfalme,” lakini kuelekea mashariki. Mwishoni mwa Kusini inapitia Edomu na inajulikana kama “njia ya jangwa la Edomu” (kama vile 2 Wafalme 3:8). Njia Kuu ya Mfalme na njia ndogo ya jangwa inakutana na Rabbath-bene-ammon, ambayo inaenda mpaka mashariki mwa Yeriko.

2:9 “Msiwasumbue Moabu wala kuwachokoza wao katika vita”Hii ni sawasawa na 2:5 juu ya Edomu. Maneno ni tofauti lakini wazo ni lile lile.

Vyote VITENZI ni AMRISHI:

1. “kusumbua” (BDB 849 III, KB 1015, *Qal* HALI YA KUSIHI, kama vile Kutoka 23:22; Esta 8:11)
2. “kuchokoza” (BDB 173, KB 202, *Hithpael* HALI YA KUSIHI, mstari 19,24; Mith. 28:4; Dan. 11:10)

☐**“Ari”**Hii ni kama rejea ya Moabu kwa ujumla au mji wake mkuu (kama vile Hes. 21:15,28; Kumb. 2:9,18,29;Isa. 15:1). Hili lilikuwa upande wa kushoto ukingonimwa Mto Arnoni.

☐**“wana wa Lutu kama milki”**Tazama Mwa. 19:37-38.

2:10-12Mistari hii ni maoni ya kiuhariri, kama ilivyo mistari ya 20-23; 3:9,11,13-14. Maneno yote yafuatayo yanamaanisha majitu: (1) *Emim*(mistari ya 10,11); (2) *Anakim*(mistari ya 10,11,21); na (3) *Rephaim*(mistari ya 11,20). Maneno haya yanaweza kumaanisha aidha (a) ukubwa au urefu wa kimo; (b) watokao katika ukoo fulani; au (c) baadaye katika Isaya na Yeremia, yanatumika kumaanisha ulimwengu wa wafu.Yumkinihapa panarejerea kimo. Tazama Mada Maalum katika 1:28.

2:12 “Wahori”Kuna mijadala kadhaa juu ya mahusiano kati ya Wahori (BDB 360) na Wahuri (ABD, juzuu 3, kr. 335-338). Sifikirii kuwa hawa ni wale wale (ABD, juzuu 3, kur. 288). Naamini walikuwa watu wa aina mbili tofauti ingawa hakuna namna ya kulifanya hili kuwa fundisho (NET Bible, ku. 348 #5). Wahori walikuwa kundi la kikabila lililoishi katika ukanda wa Edomu/Seiri kabla ya Edomu kuwa taifa (kama vile Mwa. 14:6;36:20-30).

2:13 “Sasa inuka na uvuke”VITENZI hivi viwili (BDB 877, KB 1086 na BDB 716, KB 778) vyote ni *Qal* KAULI SHURUTISHI. YHWH bado anamwambia Musa ni nini hasa cha kufanya.

☐“**kijito cha Zeredi**”Hili ni jina la ghuba ya Moabu na Edomu (kama vile Hes. 21:12). Ni bonde lenye kujaa mchanga ambalo hutiririsha maji wakati wa masika, ni kijito cha muda, sio mto. Michanga ile mara kwa mara hutengeneza “njia.” Iitengeneza mpaka kati ya Edomu na Moabu. Maana ya neno “Zeredi” (BDB 279) haijulikani.

2:14 “Na muda uliotuchukua. . .ilikuwa miaka thelathini na minane”Huu ni mstari wa unao dokeza muhtasari wa Kipindi cha Kutanga tanga jangwani (kama vile mstari wa 7).

2:14, 16 “vizazi vyote vya watu wa vita”Hawa “watu wa vita” ilihusisha kila mwanaume kati ya miaka 20 na miaka50 (kama vile Kutoka. 30:14; 38:26; Hes. 1:3; 14:29). Kizazi hiki chote cha wasioamini (yaani kukosekana kwa imani katika ahadi za YHWH) kilitakiwa kufa (kama vile mstari wa 15) kabla ya kizazi cha Wana wa Israeli kilichozaliwa jangwani kumiliki Nchi.

☐“**kama BWANA livyokuwa ameapa**”Tazama Hes. 14:28-29; Kumb. 1:34-35.

2:15 “mkono wa Bwana”Tazama Mada maalum hapa chini.

MADA MAALUMU: LUGHA YA WANADAMU KUELEZEA UUNGU

- I. Aina hii ya lugha (yaani., Uungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
 - A. Viungo vya mwili
 1. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
 2. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
 3. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15
 4. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
 5. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
 6. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
 7. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
 8. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
 9. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
 10. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22
 - B. Matendo ya mwili (angalia mifano)
 1. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
 2. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
 3. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
 4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
 5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
 6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6
 - C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
 1. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
 2. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
 3. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
 4. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19
 - D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
 1. Baba
 - a. Wa Israeli- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
 - b. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
 - c. Sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17

2. Mzazi – Hosea 11:1-4
3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

- A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!
- B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)
- C. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwingine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)
- D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).

III. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika *The International Standard Bible Encyclopaedia*, kurasa za. 152-154

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 2:16-25

¹⁶Basi ikawa, walipokwisha angamizwa kwa kufa watu wote wa vita kati ya watu, ¹⁷Bwana aliniambia, akasema, ¹⁸Hivi leo ivuke Ari, mpaka wa Moabu; ¹⁹na utakaposongea kuwaelekea wana wa Amoni, usiwasumbue wana wa Amoni, wala usishindane nao; kwa kuwa sitakupa katika nchi ya hao wana wa Amoni kuwa milki yako; kwa sababu nimewapa wana wa Lutu iwe milki yao. ²⁰(Nchi hiyo nayo yadhaniwa kuwa ni nchi ya Warefai, hapo kale Warefai walikaa humo; lakini Waamoni huwaita Wazamzumi; ²¹nao ni watu wengi, wakubwa, warefu, kama Waanaki; lakini Bwana aliwaangamiza mbele yao; wakawafuata wakakaa badala yao; ²²kama vile alivyowafanyia wana wa Esau, waliokaa Seiri, alipowaangamiza Wahori mbele yao; wakawafuata, wakakaa badala yao hata hivi leo; ²³na Waavi waliokuwa wakikaa katika vijiji mpaka Gaza waliangamizwa na Wakaftori waliotoka Kaftori, na hawa wakakaa badala yao.) ²⁴Ondokeni, mshike safari yenu, mvuke bonde la Arnoni; tazama, nimemtia Sihoni Mwamori mfalme wa Heshboni mkononi mwako, na nchi yake; anzeni kuimiliki, mshindane naye katika mapigano. ²⁵Hivi leo nitaanza mimi kutia utisho wako na kuhofiwa kwako juu ya watu walio chini ya mbingu kila mahali, watakosikia uvumi wako, na kutetemeka, na kuingiwa na uchungu kwa sababu yako.

2:16 “watu wote wa vita wakiisha kuangamizwa”Hii inaonesha uwiano kati ya upendo wa Mungu na haki ya Mungu. Kusudi la Mungu sio tu kuadhibu bali kusaidia watu wake kujifunza kutokana na makosayao. Hivyo aliwafanya watu hawa chini ya hukumu yake ya mauti watangetange kwa muda wa miaka 38. Hakikuwa kifo cha ghafla bali kifo kabla ya kutimia kwake. Kila mtu aliyekuja Kadash-barnea, miaka 20 na kuendelea walifariki isipokuwa Yohana na Kalebu.

2:19Hii inafanana na 2:5 na 2:9. Hivi ni VITENZI vile vile sawasawa na mstari wa 9. Hapa cha kwanza (BDB 849, KB 1015)ni cha HALI YA KUSIHI kwa maana, lakini si kimuundo. Cha pili (BDB 173, KB 202) ni *Hithpael* HALI YA KUSIHI. Pia Waamoni walikuwandugu wa Waisraeli kupitia Lutu.

2:20 “(pia inachukuliwa kama nchi ya Warefai)”Hiki kilikuwa ni kikundi cha kikabila kilichoishi katika eneo hili. Pia hawa walikuwa wakiitwa Wazamzumi. Mstari wa 21 unatonesha wao walikuwa ni sehemu ya majitu(kama vile mstari wa 9.) Tazama Mada Maalum katika 1:28.

☐“Zamzumi”Tazama Mwanzo 14:5.

2:21 YHWH alikuwa amekwisha kuwa mwaminifu kwa uzao wa Esau(mistari ya 5,22) na Lutu (mistari ya 9-10, 21-22). Vile vile msamiati wa“vita vitakatifu” uliotumika kuelezeaushindi wa Israeli katika vita ndio uliotumika kuelezea ushindiwao wa makabila ya nchi za Edomu na Waamoni.

2:23

NASB, NRSV,

TEV, REB “Waavi”

NKJV “Waavi”

NJB “Waavi”

Neno hili (BDB 732) lina maana mbili:

1. Kundi la watu waliokaa hukokusini mwa Palestina. Hawa walitawaliwa na watu wa Aegea (yaani Wafilisti). Hata Albright anawahusianisha wao na makazi ya Hyksos (kama vile ABD, juzuu.1, ukr. 531). Sura hii imeorodhesha wakazi wa asili wa maeneo walioshindwa na kutawanyika kwa kukosa ardhi.
2. Baadaye katika Yoshua neno hili linakuwa jina la mji katika maeneo waliopewa kabila la Benjamini (kama vile Yosh.18:23). Baadhi ya wanazuoni wamefikirikuwa walikuwa ni watu kutoka Ai.

☐“**na Wakaftori waliotoka Kaftori**”Neno hili (BDB 499) linaweza kuwa kisiwa cha Krete, Kipro, Kapadokia, au kaskazini mwa Misri (kama vile Mwa. 10:13-14). Hatuna uhakika juu ya hili. Kaftori (wingi wa Waftori) walikuwa yawezekana majirani au ndugu wa Wafilisti (kama vile Mwa. 10:14; Yer. 47:4; Amosi9:7).

2:24Mstari huu una amri kadhaa:

1. “Inuka” - BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile Mwa. 13:17
2. “anzisha” - BDB 652, KB 704, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile Kumb. 1:19; 2:1
3. “pita” - BDB 716, KB 778, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile Isa. 23:12
4. “Tazama” - BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI SHURUTISHI
5. “Anza” - BDB 320 III, KB 319, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, kama vile Kumb. 2:31
6. “miliki” - BDB 439, KB 441, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile Kumb. 1:8,21; 2:31; 9:23
7. “shindana” - BDB 173, KB 202, *Hithpael* KAULI SHURUTISHI, kama vile Kumb. 2:5,9,19; Dan. 11:10

YHWH anaamuru, anatia moyo na kuwapa changamoto watu Wake kumwamini na kulitii neno lake kwasababu wazazi wao hawakufanya hivyo. Ardhi ilikuwa mali yao ikiwa wangepanyia kazi imani yao!

☐“**Waamori**”Tazama dokezo katika 1:4.Mji mkuu wa ufalme huu ulikuwa Heshboni. Huu ulifanyika kuwa mpaka wa kikabila wa Reubeni.

2:25 “Nitaanza kuweka”Maneno haya mawili ni KAULI SHURUTISHI katika mstari wa 24. Mungu alikuwa tayari kuwashindia kwa niaba yao ikiwa wangemwamini na kuingia katika vita na wakazi wa maeneo yale husika!

☐“**utisho na kuhofiwa**”Neno la kwanza (BDB 808) linamaanisha “kushangaa” au “kuogopa”:

1. maadui wa Israeli watawaogopa - Kumb. 2:25; 11:25; Zab. 105:38
2. Waisraeliwatamuogopa YHWH ikiwa watatenda dhambi - Kumb. 28:66,67
3. YHWH anatakiwa kuogopwa - Zab. 119:120

Neno la pili (BDB 432) linamaanisha “kumcha”:

1. kumcha Mungu - Kut. 20:20
2. heshima kwa Mungu - Zab. 2:11; 5:; 90:11; 119:38
3. hofu ya kifo - Zab. 55:4-5
4. Hofu ya Israeli - Kumb. 2:25

☐“**kila mahali chini ya mbingu**” Dhahirihuu ni utiaji chumvi wa maneno (yaani, nchi nzima, 4:19; Dan. 9:12). Hii inarejerea wakazi wa Kanaani.

☐“wataogopa na kutetemeka”Hii ni sawa na neno “kuogopa na kuwa na hofu.” KITENZI cha kwanza (BDB 919, KB 1182, *Qa*WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “kutikisika” au “kutetemeka” (kama vile Mith. 29:9; Isa. 14:9). KITENZI cha pili(BDB 296, KB 297, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) humaanisha “kucheza,” “kuzungushwa” (kama vile Maombolezo. 4:6) au “kuminywa” (kama vile Isa. 23:4; 26:18 [kuzaa]).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2:26-31

²⁶Nikatuma wajumbe kutoka bara ya Kedemothi kwenda kwa Sihoni mfalme wa Heshboni na maneno ya amani, kusema. ²⁷Nipishe katikati ya nchi yako; nitakwenda kwa njia ya barabara, sitageuka kwenda mkono wa kuume wala wa kushoto. ²⁸Nawe uniuzie chakula kwa fedha nile; unipe na maji kwa fedha, ninywe; ilarunipishe katikati kwa miguu yangu, hayo tu; ²⁹kama walivyonifanyia hao wana wa Esau waketiio Seiri, na hao Wamoabi waketiio Ari; hata nivuke Yordani niingie nchi tupewayo na Bwana, Mungu wetu. ³⁰Lakini Sihoni mfalme wa Heshboni hakutuacha kupitia kwake; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, alimfanya mgumu roho yake, akamtia ukaidi moyoni mwake, apate mtia mkononi mwako kama alivyo hivi leo. ³¹Kisha Bwana akaniambia, Tazama, nimeanza kumtoa Sihoni na nchi yake mbele yako; anza kuimiliki, upate kuirithi nchi yake.

2:26 “Kedemothi”Hii inamaanisha eneo (au makazi) kaskazini mwa Mto Arnoni, lakini mahali lilipo eneo hili halijulikani. Hili baadaye lilifanyika kuwa mji wa walawi (kama vile Yosh. 21:37).

2:27 “Nipishe katikati ya nchi yako; nitakwenda kwa njia ya barabara”KITENZI cha kwanza (BDB 716, KB778, *Qa*HALI YA KUSIHI) mara nyingi kinatumika katika muhtasari wa kihistoria (kama vile 2:4,8,13,14,18,24,27,28,29,30;3:18,21,25,27,28; 4:14,21,22,26). Dhana nyingine ya kimaandiko ni kuwa neno la kiebrania ‘njia’ au “barabara,” likiwa na KIHISISHI liko mara mbili. Hii ni njia ya kusisitiza kwamba wasingepita kando ya njia kuu. Hii inarejerea kwa Njia kuu ya Mfalme ambayo inapitia Edomu, Moabu na ufalme wa Sihoni. Musa anaelezea kwamba walikuwa wamepita katika falme hizi bila kusababisha vurugu hata hivyo mfalme wao asingewaruhusu kupita humo. Hii ilikuwa ni kama ahadi ile ile (kama vile mstari wa 29) waliyofanyiwa na Musa wakiwa Edomu (kama vile mstari wa 6).

☐“sitageuka kwenda mkono wa kuume wala wa kushoto”Tazama Musa anazungumza kwa kuwajumuisha wote. Migongano mingi ya biblia inaweza kuchagizwa na kukosekana kwa asili ya ujumuishi wa ufunuo wa kibiblia dhidi ya mitazamo ya jamii za kisasa za magharibi. Haki na upendeleo wa mtu mmoja mmoja umekingwa na ujumuishi wa kijamii wa Agano la Kale.

Kifungu hikikimejikita katika nahau ya Agano la Kale la imani ya kibiblia kama pitio au njia (mf, Zab. 119:105). Mapenzi ya Mungu yanawekwa wazi kidhahiri. Dhana hii ni ya wazi hapa (yaani barabara). Hivyo kifungu cha maneno, “kugeuka kushoto au kulia” ni cha wazi. Mara nyingi hutumika kistiari kwa maisha ya kiroho (mf Hes. 20:17; 22:26; Kumb. 5:32;17:11,20; 28:14; Yosh. 1:7; 23:6; IWafalme. 22:2).

2:30 “Bwana, Mungu wako, alimfanya mgumu roho yake, akamtia ukaidi moyoni mwake”KITENZI cha kwanza(BDB 904,KB 1151, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha ya “kufanywa mgumu” katika namna ya kuwa msumbufu au mkaidi/mwenye shingo ngumu:

1. *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inatumika katika 1:17; 15:18
2. *Hiphil* inatumika katika Kut. 7:3; 13:15 kwa kuhusianisha na Mungu kuufanya moyo wa Farao kuwa mgumu kabla ya kuanza kutoka utumwani
3. *Hiphil* inatumika katika Kumb. 10:16 kumhusu YHWH kuwaonya wana wa Israeli kutokufanya mioyo yao kuwa migumu au kutokuwa wakaidi

Kipengele cha 2 kinafanana na kuufanya mgumu moyo wa Sihoni (yaani utashi).

KITENZI cha pili (BDB 54, KB 69, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “kuwa imara.” Mara nyingi hutumika kwa namna chanya (kama vile Kumb. 3:28; 31:6,7,23), balihapa kimetumika kumaanisha “shingo ngumu” (Kumb. 15:7; II Nyakati. 36:13).

Tukio hili ni sawa na lile lililotokea kwa Farao: (1) Mungu aliufanya moyo wake kuwa mgumu (kama vile Kut. 7:3; 9:12;10:1,20,27; 11:10; 14:4,8,17) au (2) Farao aliufanya kuwa mgumu moyo wake mwenyewe (kama vile Kut.

8:15,32; 9:34). Mistari hii inaonyesha uweza wa Mungu na utashi wa mwanadamu aliopewa na Mungu. Muktaadha unaonyesha kwamba Farao (katika Kutoka) na Sihoni (katika Kumbukumbu la Torati) walikuwa na utashi au kwanini Musa achukue muda kutoa wazo la amani kwao? Maana yake ni kwamba Mungu anaendesha mambo yote. Mungu aliweka mazingira lakini walikataa (tazama *Hard Sayings of the Bible*, kur. 142-143). Warumi 9 na 10 zinaonyesha mkanganyiko huu.

Sura ya 9 inajikita katika uweza wa Mungu wakati sura ya 10 ina vitu kadhaa vya kiujumla (kama vile mstari wa 4, “kila mtu”; mistari ya. 11,13, “yeyote”; mst. 12, “wote”[mara mbili]). Tazama Mada maalum hapa chini.

MADA MAALUM: BWANA AKAUFANYA MGUMU MOYO WAKE

Ukinzani huu unaoonekana umekuwa mgogoro wa kithiolojia kati ya mifumo ishindanayo ya kithiolojia:

1. Uweza wa Mungu dhidi ya utashi huru wa kibinadamu
2. Augustine dhidi ya Pelagius
3. Calvin dhidi ya Arminius

Kwangu mimi zote ni kweli za Kibiblia. Zote lazima zichukuliwe katika ukinzani wa kithiolojia. Dhana ya “agano” inashikilia zote mbili. Mungu siku zote huja kwanza, huanzisha ajenda na hutoa wito kwa mwanadamu aliyeanguka, (mfano Yohana 6:44,65), lakini tunawajibika kwa chaguzi zetu (mfano Yohana 1:12; 3:16). Jukumu la kibinadamu na matokeo yake hutoa uhuru wa kibinadamu (yaani ufanisi wa nafsi)! Matendo ya kimaadili yanajikita katika uchaguzi halisi. Maandiko huelezea kweli zote mbili (yaani pande za kithiolojia)!

Tazama uweza wa Mungu, “nimeanza kukomboa” na utashi huru wa kibinadamu, “anza kukaa, ili uweze kumiliki ardhi”!

Ni hakika inawezekana kwamba ugumu wa kithiolojia kwetu sisi unatangiwa na kuelewa kwetu vibaya nahau za kale za kiebrania za kithiolojia. Imani kwa Mungu mmoja ya Israeli ambayo ni ya kipekee lilindwa kwa namna zote. Kusudi la YHWH la kusababisha vitu vyote kutokea ilikuwa ni njia ya kiebrania kukiri imani kwa Mungu mmoja. Hakuna kinachotokea chenyewe tu. Kulikuwa na kisababishi kimoja na kimoja tu—YHWH. Maandiko ambayo yanaelezea hili yamesababisha watu wa sasa:

1. kusema mabaya yanayotokea pia ni Mungu
2. kuelezea muundo usio badilika wa uweza wa Mungu

MADA MAALUMU: MOYO (AGANO JIPYA)

Neno la Kiyunani *kardia* limetumika katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania na Agano Jipya kuashiria neno la Kiebrania *lēb* (BDB 523, KB 513). Limetumika kwa njia tofauti kadhaa (kama vile Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon*, toleo la 2 kr. 403-404).

1. Kitovu/Kituo cha maisha ya kimwili, neno mbadala kwa mtu (kama vile Matendo 14:17; 2 Kor. 3:2-3; Yakobo 5:5)
2. Kitovu cha maisha ya kiroho (yaani, adilifu)
 - a. Mungu anatumia mioyo (kama vile Luka 16:15; Rum. 8:27; 1 Kor. 14:25; 1 The. 2:4; Ufu. 2:23)
 - b. Imetumika kwa maisha ya kiroho ya mwanadamu (kama vile. Mt. 15:18-19; 18:35; Rum. 6:17; 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 2:22; 1 Pet. 1:22)
3. Kitovu cha maisha ya kifikra (yaani, uwezo wa kufikiri, kama vile Mt. 13:15; 24:48; Matendo 7:23; 16:14; 28:27; Rum. 1:21; 10:6; 16:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18; 4:18; Yakobo 1:26; 2 Pet. 1:19; Ufu. 18:7; moyo ni sawa na mawazo katika 2 Kor. 3:14-15 na Flp. 4:7)
4. kitovu cha maamuzi binafsi (yaani, matakwa, kama vile. Matendo 5:4; 11:23; 1 Kor. 4:5; 7:37; 2 Kor. 9:7)
5. Kitovu cha hisia za ndani (kama vile. Mt. 5:28; Matendo 2:26,37; 7:54; 21:13; Rum. 1:24; 2 Kor. 2:4; 7:3; Efe. 6:22; Flp. 1:7)
6. Mahali pa pekee kwa shughuli za kiroho (kama vile. Rum. 5:5; 2 Kor. 1:22; Gal. 4:6 [yaani, Kristo katika mioyo yetu, Efe. 3:17])
7. Moyo ni njia mbadala ya ki-sitiari ya kumrejerea mtu (kama vile. Mt. 22:37, kwa kunukuu Kumb. 6:5). Mawazo, sababu, na matendo vikichangia kikamilifu kwenye moyo kubainisha kikamilifu mtu alivyo. Agano la Kale lina baadhi ya matumizi ya maneno ya kushangaza.

- a. Mwa. 6:6; 8:21, "Mungu alihuzunishwa katika moyo," pia tazama Hosea 11:8-9
- b. Kumb. 4:29; 6:5; 10:12, "kwa moyo wako wote na nafsi yako yote"
- c. Kumb. 10:16; Yer. 9:26, "Roho zisizo na tohara" na Rum. 2:29
- d. Ezek. 18:31-32, "moyo mpya"
- e. Ezek. 36:26, "moyo mpya" dhidi ya "moyo wa jiwe" (kama vile Ezek. 11:19; Zak. 7:12)

2:31KAULISHURUTISHI tatu katika mstari wa 24 zinarudiwa:

1. "Angalia" - BDB 906, KB 115, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. "Anza" - BDB 320, KB 319, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
3. "kalia" - BDB 439, KB 441, *Qal* KAULI SHURUTISHI

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 2:32-37

³²Ndipo Sihoni alipotutoka juu yetu yeye na watu wake wote, kupigana huko Yahasa. ³³Bwana, Mungu wetu, akamtoa mbele yetu, tukampiga yeye na wanawe, na watu wake wote. ³⁴Tukatwaa miji yake yote wakati huo, tukaharibu kabisa kila mji uliokuwa na watu, pamoja na wanawake na wadogo; tusimsaze hata mmoja; ³⁵ila ng'ombe zao tuliwatwaa kuwa mawindo yetu, pamoja na nyara za miji tuliyoitwaa. ³⁶Kutoka Aroeri iliyo katika ukingo wa bonde la Arnoni, na huo mji ulio ndani ya bonde, mpaka kufika Gileadi, hapakuwa na mji uliokuwa mrefu kutushinda; Bwana, Mungu wetu, aliiweka wazi yote mbele yetu; ila nchi ya wana wa Amoni hukuisongelea; ³⁷upande wote wa mto wa Yaboki, na miji ya nchi ile ya milimani, na kila mahali alipotukataza Bwana, Mungu wetu.

2:32 "alipotutoka juu yetu" Sihoni alipoteza kwasababu aliondokakwenye miji yake yenye ngome na alishindwa katika uwanda usio kuwa na milima. Huu ni mfano mzuri wa wapi Mungu alitumia kiburi cha mwanadamu kufanikisha kusudi Lake.

☐ "Yahasa" Mahali penyewe hapajulikani lakini ni upande wa mashariki mwa Yordani katika ufalme wa Sihoni na yawezekana kusini mwa mji mkuu, Heshboni, kwasababu Wana wa Israeli walikuwa wakija kutokea kusini.

2:33 "Mungu wetu, akamtoa mbele yetu" Kama ulivyo mstari wa 31, Uweza wa Mungu (mstari wa 32a, Mungu alimtoa" BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) na uhuru wa mwanadamu (mstari wa 32b, "tulishinda" BDB 645, KB 697, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) vyote vinaelezwa kwa udhahiri.

2:34 "tusimsaze hata mmoja" Hii ilikuwa ni kanuni ya vita vitakatifu (*herem*, BDB 355 I, kama vile 3:6). Wote waliuwawa kwasababu watu wale walikuwa ni wenye dhambi kwa muda mrefu sana (kama vile Kumb. 7:16; 20:14). Mwanzo 15:16 inasema "dhambi ya Waamori imetoshwa" na hivyo Mungu alikuwa amesubiri kwa muda mrefu ili wamrejeele kwake.

Mwishowe hawakutubu hatimaye hukumu ikawajia juu yao. Ikiwa hawakuwa wameharibiwa, wangeharibu ibada na thiolojia iliyotolewa katika Mlima Sinai. "Vita Vitakatifu" ilikuwa ni hukumu na mpaka wa kuwazuia!

2:35 "ila ng'ombe zao tuliwatwaa kuwa mawindo yetu, pamoja na nyara za miji tuliyoitwaa" Hii ni mfano wa hazina yenye ukomo (mfano, 3:6-7; Yosh. 8:2,27; 11:14). Hawa walikuwa wanaweza kuchukua baadhi ya nyara baada ya kuwa wamewaangamiza watu. Hii ilikuwa ni sehemu ya dhana ya vita vitakatifu ya Agano la Kale. Vita vilikuwa ni vya YHWH hivyo pia na nyara (mfano Yeriko, YOSHUA 7).

2:36

NASB "huo mji ulio ndani ya bonde"

NKJV "huo mji ulio ndani ya bonde"

NRSV "huo mji ulio ghuba yenyewe"

TEV "huo mji ulio katikati ya bonde"

NJB "mji ulio ndani ya bonde"

Aina mbalimbali za tafsiri za Kingereza zinaonesha uwezekano. Kwangu mimi, mji usingeweza kujengwa katika korongo kwasababu ya hatari ya mafuriko ya ghafla, hivyo bonde linaonekana kuwa bora zaidi.

☞“**hapakuwa na mji uliokuwa mrefu kutushinda**”Watu wa Mungu hapo kabla walikuwa wamekata tamaa na kurudi nyuma kwasababu miji ilikuwa imewekewa ngome vizuri sana na wakazi wake walikuwa warefu sana. Sasa Wayahudi walikuwa wakisema “Wale watu ni wakubwa sana lakini tutashindana nao kwa msaada wa Mungu”(kama vile Kumb. 1:28).

2:37Eneo la mapigano lilikuwa linajulikana vizuri sana (kwa amri ya Mungu, kama vile mistari ya 5,9,19).

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ifuatilie njia ya mapigano katika ramani.
2. Majitu yalikuwa ni watu gani?
3. Mtu anaelewaje na kuhusika na mstari wa 34?

KUMBUKUMBU LA TORATI 3

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Mfalme Ogu Anaangamizwa	Pitio la Kihistoria (1:1-3:29)	Israeli Inamteka Mfalme Ogu	Mateka ya Mfalme Ogu
3:1-11	3:1-7	3:1-2 3: 3-7	3:1-7
	3:8-17	3:8-10 3:11	3:8-11
Nchi ya Mashariki mwa Yordani Inagawanywa		Makabila yaliyoishi Mashariki mwa Yordani	Kugawanywa kwa ng'ambo ya Yordani
3:12-17		3:12-13a 3:13b-14 3:15-17	3:12-17 Maagizo Mengine
toka kwa Musa			
3:18-22	3:18-22	3:18-20 3:21-22	3:18-22
Musa Anazuiwa Kuingia Katika Nchi ya Ahadi		Musa Haruhusiwi Kuingia Kanaani	
3:23-29	3:23-29	3:23-25 3:26-28 3:29	3:23-28 3:29

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi") *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (mzunguko #3, uk viii) Linganisha mgawanyo wa somo lako na tafsiri nne hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 3:1-7

¹Ndipo tukageuka, tukakwea njia ya Bashani; na Ogu, mfalme wa Bashani, akatutokea juu yetu, yeye na watu wake wote, kuja kupigana huko Edrei. ²Bwana akaniambia, Usimwogope; kwa kuwa nimentia mkononi mwako, yeye na watu wake wote na nchi yake; nawe utamtenda mfano wa ulivyomtenda Sihoni, mfalme wa Waamori, aliyekuwa akikaa Heshboni. ³Basi Bwana, Mungu wetu, akamtia mikononi mwetu na Ogu mfalme wa Bashani, na watu wake wote; tukampiga, asisaziwe cho chote. ⁴Tukatwaa miji yake yote wakati huo; hapakuwa na mji tusiotwaa kwao miji sitini, nchi yote ya Argobu, ndio ufalme wa Ogu ulio katika Bashani. ⁵Miji hiyo yote ilikuwa yenye maboma marefu, na malango, na makomeo, pamoja na miji isiyokuwa na maboma, mingi sana. ⁶Ukaiharibu kabisa, kama tulivyomfanya huyo Sihoni, mfalme wa Heshboni, kwa kuharibu kabisa kila mji uliokuwa na watu, pamoja na wanawake na watoto. ⁷Lakini wanyama wote wa mji, na nyara za miji, tulitwaa kuwa mawindo yetu.

3:1 “tukageuka. . . tukakwea” Kifungu hikikinairejelea Njia Kuu ya Mfalme. Hii ilikuwa barabara yang’ambo ya Mto Yordani iliyokuwa ikinyooka moja kwa moja kupitia katikati ya mji wa Edomu, Moabu, na Ammoni. Hii ilikuwa njia kuu ya misafara kutoka Ghuba ya Agaba kuelekea Dameski.

☐ **“Bashani”** Majina haya yanamaanisha “laini” (BDB 143), katika maana ya nchi ya kilimo kikubwa (yaani, isiyo na miamba). Hii ilikuwa ardhi yenye rutuba na yenye vichaka kusini mwa ng’ambo ya Mto Yordani eneo la kaskazini mwa Mto Yarmuki au pengine ni Mto Yaboki kusini mwa vilima vya MI. Hermoni, ambapo inamaanisha kuwa eneo hili lilimega sehemu ya eneo liljulikanalo kama Gileadi. Hili lilijulikana sana kwa sababu ya vichaka vyake na makundi mengi ya mifugo.

☐ **“Ogu, mfalme wa Bashani”** Tazama Hes. 21:33-35; Kumb. 1:4.

☐ **“huko Edrei”** Mji huuuko njiapandaya Mto Yarmuki na ulikuwa moja ya makazi ya kifalme. Makao makuu yake yalikuwa Ashtarothi upande wa kaskazini. Ogu alikutana na Waisraeli katika eneo hili, pengine alitumia mto kama sehemu ya ulinzi.

3:2 “Bwana akaniambia” Tazama maelezo katika 2:2.

☐ **“Usimwogope”** Hiki KITENZI (BDB 431, KB 432, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana AMRISHI) mara nyingi kinatumika katika Kumbukumbu la Torati (mf. 1:19,21,29; 2:4; 3:2,22; 4:10). Mungu alikuwa akipigana badala yao (yaani, vita takatifu, mf. Hes. 21:34; Yosh. 10:8; 11:6).

☐
NASB, NKJV “nimentia mkononi mwako”
NRSV “nimentia nguvuni mwako”
TEV “nakwenda kumleta”
NJB “nimentia matesoni mwako”

Hiki KITENZI (BDB 678, KB 733, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “toa,” “weka” au “panga.” Hiki ni KITENZI cha kawaidajumuishi. Yatambue matumizi yake katika kipengele cha kifasihi cha Kumbukumbu la Torati (kama vile 1:8, 15, 20, 21,25,27,35,36,39; 2:5,7,9,12,24,25,28,29,30,31,33,36; 3:2,3 12,13,15 16,18 19 20; 4:1,8,21,38,240). YHWH ndiye mtoaji. Kuna Mungu mmoja pekee!

☐“**na watu wake wote; tukampiga, asisaziwe cho chote**” Hii ndiyo lugha na uhalisia wa kifungu “vita takatifu.” Hii inaakisi dhana ya Kiebrania ya neno *herem*, au “chini ya katazo” (kama vile mst.6). Ifuatayo ni sampuli wakilishi ya marejeleo ya AK kuhusiana na neno hili lenye kuonyesha namna linavyotumika katika njia tofauti tofauti. Hii dhana ya neno *herem* au “vita takatifu,” “katazo,” au “zuio”:

1. maangamizi ya jumla—hakuna chenye uhai kilichosalia hai, hakuna kitu cho chote kilichosalimishwa (kama vile Kumb. 20:16-18; I Sam. 15:3; Yosh. 7)
2. waue watu wote, ila wabakize ng’ombe (kama vile Kumb. 2:34, 35; 3:6, 7)
3. waue watu pekee (kama vile Kumb. 20:10-15)

3:4 “nchi yote ya Argobu” Hili neno “nchi” (BDB 286) ambalo kifasihi linamaanisha, “mshipi,” linatumika kumaanisha:

1. kamba aina ya mshipi
2. futi kamba
3. sehemu ya nchi (yaani, eneo, kama vile Yosh. 17:5, au urithi, kama vile Kumb. 32:9; Yosh. 17:14)
4. kundi la watu (yaani, kundi la manabii, kama vile I Sam. 10:5,10)

☐“**Argobu**” Neno hili (BDB 918) ni jina la eneo au sehemu fulani ya nchi. Hili liko katika nchi ya Bashani (kama vile 3:4,13,14; I Fal. 4:13). Asili ya neno hili inaweza kuhusianishwa na neno “mshamba” (BDB 918) au “bumbuazi” (BDB 918), lakini haijulikani.

3:5 “Miji hiyo yote ilikuwa yenye maboma marefu, na malango, na makomeo,” Miji hii ilikuwa imejengwa kutokana na mawe makubwa yaliyotokana na volkano na haya yalikuwa na ukubwa wa kutokutikisika. Haya yalimaanisha mwonekano wa kutisha. Ukubwa wake ungeweza kuaksi idadi kubwa ya watu wa jamii moja walioishi eneo hili. Hata hivyo, imani ya Waisraeli ilikuwa na nguvu kuliko hofu yao juu ya haya majitu (kama vile 2:20-24).

Kitabu cha *Handbook on Deuteronomy* toka Umoja wa Vyama vya Biblia kinataja kwamba “malango na makomeo” huenda yanarejelea malango yaliyokuwa yamewekwa mara mbili kwa makomeo ya chuma ukingoni mwa kila lango, kr. 68-69. Hiki kinaweza kueleza juu ya wingi wa neno “malango”: (1) huenda kulikuwa na lango zaidi ya moja, au (2) hii inaweza kuwa sifa bainifu ya malango ya ndani na ya nje (yaani, vyuma vya siri).

3:6

NASB, NKJV,

NRSV “imeharibiwa kabisa”

TEV “imeharibiwa”

NJB “laana ya uharibifu”

REB “chini ya katazo zito”

JPSOA “imeangamizwa”

KITENZI hiki (BDB 355, KB 353) kinatumika mara mbili katika mstari huu (*Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI na *Hiphil* ya KITENZI JINA HALISI). Maana yake ya msingi ni kukitenga kitu fulani kwa ajili ya Mungu ambapo hiki kinakuwa kitakatifu sana kwa matumizi ya mwanadamu na chapaswa kuharibiwa. Kwa kawaida hiki kinatumika katika dhana za neno “vita takatifu” (kama vile 2:34; 7:2; Kut. 22:20; Yosh. 6:17,21) kudai kwamba ushindi na, uharibifu ulikuwa wa YHWH. Katika dhana hizi za kuviteka vitu vilivyotolewa kwa ajili ya Mungu ni za Wakanaani na mali zao. Hawa wanahukumikiwa kwa sababu ya dhambi zao za kuchukiza na kutokuwa tayari kutubu (kama vile Mwa. 15:16; Law. 18:24-26; Kumb. 9:5). Kwa mjadala ulio mzuri juu ya “vita takatifu” tazama *Ancient Israel*, na Roland deVaux, juzuu 1, kr. 258-267.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 3:8-11

⁸ Tukaitwaa na nchi wakati huo, katika mikono ya hao wafalme wawili wa Waamori waliokuwa ng'ambo ya Yordani, tokea bonde la Arnoni mpaka kilima cha Hermoni; ⁹(na hiyo Hermoni Wasidoni huiita Sirioni, na

Waamori huiita Seniri); ¹⁰miji yote ya nchi tambarare, na Gileadi yote, na Bashani yote, mpaka Saleka na Edrei, nayo ni miji ya ufalme wa Ogu katika Bashani. ¹¹(Kwani aliyesalia katika mabaki ya Warefai ni Ogu pekee, mfalme wa Bashani; tazama, kitanda chake kilikuwa kitanda cha chuma; kitanda hicho je! Hakiko Raba kwa wana wa Amoni? Urefu wake ulikuwa ni mikono kenda, na upana wake mikono minne, kwa mfano wa mkono wa mtu)

3:8 “Tukaitwaa na nchi . . . katika mikono ya hao wafalme wawili” Mstari wa24 unasema “mkono wa Mungu wenye nguvu” ambao, ni wa lugha za kibinadamu (tazama Mada Maalum katika 2:15) unaonyesha uweza na ukuu wa Mungu. Kwa mara nyingine ni mwingiliano kati ya ukuu wa Mungu na juhudi za mwanadamu.

☐ **“kilima cha Hermoni”** Ml. Hermoni ulikuwa kusini mwa mpaka wa nchi ambayo Mungu aliwapa Waisraeli. Huu ni mlima mkubwa sana ndani ya eneo zima lililo humo Lebanoni, kaskazini mwa Bahari ya Chinnereth (yaani, Galilaya). Jina lake (BDB 356) linahusiana na neno *herem* (kitu kilichotengwa) na eneo lenye mahekalu mengi (kama vile *Ancient Israel*, Roland deVaux, juzuu 1, kur. 279-282). Hili liko mpakani mwa nchi iliyotekwa (kama vile Amu. 1:1).

3:9 “Wasidoni” Huu ni mji mkuu katika Fonike (kama vile I Fal. 16:31). Huu ulikuwa kaskazini mwa pwani ya kaskazini mwa Tiro, ambapo baadaye ulikuja kuwa mji mkuu. Kutajwa kwake badala ya Tiro kunaonyesha ukale wa andiko hili.

☐ **“Sirioni”** Hili neno (BDB 970, Zab. 29:6) lililotumika kuzungumzia Ml. Hermoni limebainiwa katika maandiko ya Ki-Ugariti pia hili linaonysha ukale wa andiko hili.

☐ **“Seniri”** Hili neno (BDB 972, kama vile I Nya. 5:23; Wimbo Ulio Bora 4:8; Eze. 27:5) limebainiwa katika maelezo ya Shalmaneser III, mfalme wa ki-Ashuru aliyeishambulia Dameski.

3:10

NASB, TEV “tambarare”

NKJV “uwanda”

NRSV, NJB “eneola nchi lililoinuka kwa usawa”

Hili neno (BDB 449) linamaanisha “sehemu yenye usawa.” Hili lingeweza kurejelea uwanda au eneo la nchi iliyoinuka kwa usawa. Hapa linarejelea eneo lililoinuka kwa usawa kati ya Mto Arnoni na mji wa Heshbon kama vile 4:43; Yosh. 13:9,16,17,21; Yer. 48:8,21).

Eneo hili lililoinuka ilikuwa sehemu ya Moabu na baadaye lilikuja kuwa urithi wa kikabila wa Reubeni (kama vile Yosh. 20:8).

☐ **“Gileadi”** Hili neno (BDB 166) ni la maana inayojulikana. Fasili maarufu (kejeli) imetolewa katika Mwa. 31:48. Hili linaweza kurejelea:

1. kabila (mf. Hes. 26:29; Amu. 5:17)
2. nchi (mf. Mwa. 37:25)

Mara nyingi hili linalirejelea eneo lililo upande wa kusini mwa Mto Yordani kutoka Mto Arnon kaskazini mwa nchi ya Bashani.

☐ **“Saleka”** Mji huu unaonekana kuunda mpaka wa kusini mashariki mwa Bashani na unatumika mara nyingi, kandokando ya Ml. Hermoni, kudhihirisha ukubwa wa mji wa Bashani (kama vile Yosh. 12:5; 13:11; I Nya.5:11).

3:11 Hili linaonekana kuwa oni la kihariri, kama 2:10-12,20; 3:9.

☐ **“Warefai”** Neno hili linaweza kumaanisha (1) watu wa desturi moja; (2) wenye nguvu; au (3) ufalme wa wafu. Hapa muktadha unaonekana kuyazungumzia majitu. Tazama Mada Maalum katika 1:28.



NASB, NKJV “kitanda chake kilikuwa kitanda cha chuma”

NRSV, NJB “kitanda chake, ni kitanda cha chuma”

TEV “jeneza lake, limetengenezwa kwa jiwe”

REB “jeneza lake ni la jiwe”

Hili neno (BDB 793) kimsingi linamaanisha “kilichotengenezwa kwa mbao.” Hiki kinaweza kutumika kama kiunzi cha fito, kiti cha kukalia, kitanda, tandiko, kiti/cha utawala. Hapa kinaweza kurejelea mahali pa kulala:

1. kitanda - II Sam. 17:28; Ayubu 7:13; Zab. 6:6; 41:3; Amosi 6:4
2. kiti cha kukalia - Mit. 7:16
3. jeneza (la mwamba, yaani, mahali pa mwisho pa mtu kupumzika/kulala)

Inawezekana kwamba “chuma” kinarejelea jeneza la jiwe lenye rangi ang’avu (kama vile NET Bible, uk. 350). NIDOTTE, juzuu 1, uk. 741, inasema, “hakuna msaada wa kifasihi juu ya mapendekezo kwamba hili lilikuwa jeneza la jiwe au jabali.”

☑ **“Raba”** Haya yalikuwa makao makuu ya ufalme waAmoni (kama vile Yosh. 13:25). Hivi leo ni makao makuu ya Yordani, Amani.

☑ **“mkono wa mtu”** Kifasihi hii ni, “kwa mfano wa mkono wa mtu,” ambayo ilikuwa nahau ya “mkono wa usawa.” Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: MKONO

Kuna mikono miwili (BDB 52, KB 61) ndani ya Biblia. Mkono wa kawaida ni ule umbali uliopo kati ya kidole kirefu sana cha mwanadamu na kiwiko chake, kwa kawaida ni nchi zipatazo 18 (yaani, Mwa. 6:15; Kut. 25:10,17,23;26:2,8,13,16; 27:1,9,12,13,14,16,18; Hes. 35:4,5; Kumb. 3:11). Pia kuna mkono mrefu zaidi (mkono wa kifalme) unaotumika katika ujenzi (yaani, hekalu la Suleimani), ambalo lilijulikana sana humo Misri (yaani, vidole 21), Palestina (yaani, vidole 24), na wakati mwingine Babeli (yaani, vidole 30). Huu ulikuwa urefu upatao nchi 21 (kama vile 2 Nya. 3:3; 40:5; 43:13).

Watu wa kale walikuwa wakitumia sehemu za mwili wa mwanadamu kama vipimo. Watu wa Mashariki ya Karibu ya Kale walitumia:

1. mikono iliyonyooshwa
2. urefu kutoka katika kiwiko hadi kidole cha kati (mkono)
3. upana kutoka kidole kilichokunjwa hadi kidole kidogo(umbali, kama vile Kut. 28:16; 39:9; I Sam. 17:4)
4. urefu kati ya vidole vyote vinne vya mkono uliokujwa (upana wa mkono, kama vile Kut. 25:25; 37:12; I Fal. 7:26; II Nya. 4:5)
5. urefu wa maungio ya kidole (upana wa kidole, Yer. 52:21)

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 3:12-17

¹²Na nchi hiyo tuliitwaa ikawa milki yetu, wakati huo; tokea Aroeri iliyo kwenye bonde la Arnoni, na nusu ya nchi ya milima ya Gileadi, na miji iliyokuwamo, niliwapa Wareubeni na Wagadi; ¹³na nchi ya Gileadi iliyobaki, na Bashani yote, maana huo ufalme wa Ogu niliwapa nusu ya kabila ya Manase; nchi yote ya Argobu, nayo ndiyo Bashani yote. (Na nchi hii yaitwa nchi ya Warefai. ¹⁴Yairi, mwana wa Manase, alitwaa nchi yote ya Argobu, hata mpaka wa Wageshuri na Wamaaka; akaziita nchi hizo Hawoth-yairi, kwa jina lake mwenyewe, hata hivi leo, maana, hizo nchi za Bashani.) ¹⁵Na Makiri nilimpa Gileadi. ¹⁶Na Wareubeni na Wagadi niliwapa tokea Gileadi mpaka bonde la Arnoni, katikati ya bonde, na mpaka wake; mpaka mto wa Yaboki, nao ni mpaka wa wana wa Amoni; ¹⁷na nchi ya Araba nayo, na mto wa Yordani, na mpaka wake, tokea Kinerethi mpaka bahari ya hiyo Araba, nayo ni Bahari ya Chumvi, chini ya matelemko ya Pisga, upande wa mashariki.

3:12 “Wareubeni na Wagadi” Haya makabila mawili ndiyo yaliyouwaa ufalme wa Sihoni (kama vile Yosh. 13:15-23,24-28).

3:13 “nusu ya kabila” Wana wa Yusufu waliunda nusu kabila za Manase na Efraimu (kama vile Mwa. 41:50,52; 48:1-7). Urithi wa Manase uligawanywa, nusu yake upande wa mashariki mwa Mto Yordani na nusu yake upande wa magharibi.

3:14 “Yairi” Nenokuliko “mwana wa” linamaanisha “uzao wa” (kama vile Hes. 32:41). Vizazi vilivyo vingi vinaachwa kwa kutowekwa ndani ya ukoo huu. Mistari 12-13 asili yake ni ya moja kwa moja na mist. 14-17 inatoa maelezo zaidi (kama vile NIC, *Deuteronomy*, Craigie, uk. 121).

☐ **“mwana wa Manase”** Neno “Mwana” hapa lina maana ya uzao mdogo kuliko mwana wa kuzaa (kama vile I Nya. 2:22).

☐ **“Wageshuri na Wamaaka”** Haya ni makundi ya watu wa rangi moja na jamaa moja (BDB 178 na 591). Hawa waliishi kaskazini mwa mpaka wa nchi ya Bashani (kama vile Yosh. 13:13). Israeli haikupigana na watu hawa.

☐ **“Hawoth-yairi”** Hii inamaanisha “miji,” “dini,” au “ufalme” (BDB 795 II) wa Yairi.

☐ **“hata hivi leo”** Kifungu hiki kinakirejelea kipindi kiichofuatiakuliko tukio (kama vile 2:22; 3:14; 4:38; 10:8,15; 29:28; Yosh. 7:26; 8:28,29; 9:27; 13:13; 14:14; 16:10; 22:3,17; 23:8; Amu. 1:21,26; 10:4; 18:12,30; 19:30). Mstari 5 unaonekana kuwa na msukumo ule ule. Suala ni “kwa kiasi gani” baada ya hapo. Kifungu hiki kinaweza kurejelea “muda mfupi baadaye” (mf. Yosh. 6:25; 23:9) au kinaweza kumaanisha vizazi vilivyofuatia. Ni nani aliyeyaandika maneno ya Musa? Ni nani aliyevipanga Vitabu Vitano vya Musa? Ni nani aliyekuwa mhariri wa mwisho? Utafiti wa leo hauwezi kuyajibu maswali haya!

3:15 “Na Makiri” Hesabu 32:39-40 inatuarifu zaidi juu ya mtu huyu.

3:17 “Araba” Hili lilikuwaneno lingine la Bonde la Mto Yordani, ambalao linapitia eneo la juu la Bahari ya Galilaya zamani Bahari ya Magombo ya Chumvi chini ya Ghuba ya Agaba katika Rasi ya Sinai (tazama maelezo katika 1:1). Huu ni ufa wa kijiografia ambapo Mto Yordani unapitia, kutoka vilima vya juu vya Ml. Hermoni kuelekea Bahari ya Chumvi.

☐ **“Kinerethi”** Hili ni (BDB 490) jina la mji ulio ndani ya Galilaya ambao ulikuwa karibu na ziwa kubwa lenye kujulikana na kwa majina mengi ndani ya Biblia”

1. Kinerethi (mfa. Hes. 34:11; Yosh. 12:3; 13:27)
2. Galilaya (mf. Mt. 4:18; Marko 1:16; Yohana 6:1)
3. Genesareti (mf. Luka 5:1)
4. Tiberia (mf. Yohana 6:1; 21:1)

☐ **“bahari ya hiyo Araba”** Hii (kama vile 4:49; Yosh. 3:16; 12:3, pia inaitwa “Bahari ya Tambarare” katika II Fal. 14:25) ni jina lingine la Bahari ya Chumvi (kama vile Mwa. 14:3; Hes. 34:3,12; Yosh. 3:16; 15:2,5; 18:19) au, kama iitwavyo hivi leo, inaitwa Bahari ya Iliyokufa. Pia hii inaitwa “bahari ya mashariki” (kama vile Eze. 47:18; Yoeli 2:20; Zek. 14:8) au kama “bahari” (kama vile Isa. 16:8; Yer. 48:32).

☐ **“Pisga”** Mlima huu (BDB 820) unatambuliwa kwa au uko karibu na Ml. Nebo (BDB 612 I, kama vile 32:49; 34:1). Huenda hivi ni vilele pacha vya muundo mmoja au jina moja la safu na kilele chake kirefu zaidi. Milima hii ni matokeo ya mmomonyoko wa uwanda wa Moabu juu ya Araba. Jina hili ni la kawaida katika kitabu cha Agano la Kale kuliko jina Nebo (kama vile Hes. 21:20; 23:14; Kumb. 3:17,27; 4:49; 34:1).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 3:18-22

¹Nikawaamuru wakati huo, nikawaambia, Bwana, Mungu wenu, amewapa ninyi nchi hii mwimiliki, basi vukeni ng'ambo wenye silaha mbele ya ndugu zenu, wana wa Israeli, nyote mlio mashujaa. ¹⁹ Lakini wake wenu na watoto wenu, na wanyama wenu wa mji, (nawajua kwamba mna wanyama wengi), na wakae katika miji yenu niliyowapa; ²⁰ hata Bwana awapumzishe ndugu zenu kama ninyi, nao pia waimiliki nchi wapewayo na Bwana, Mungu wenu, ng'ambo ya Yordani; ndipo mtakaporudi kila mmoja aende katika milki yake niliyowapa. ²¹Nikamwamuru Yoshua wakati huo, nikamwambia, Macho yako yameona yote aliyowatenda Bwana, Mungu wenu, wale wafalme wawili, navyo ndivyo atakavyoutenda Bwana kila ufalme huko uvukiako.

²² Msiwache, kwa kuwa Bwana, Mungu wenu, ndiye awapiganiaye

3:18 “Bwana, Mungu wenu, amewapa ninyi nchi hii” Kifungu hikikinaurejelea ukingo wa mashariki (ng'ambo ya mto Yordani) mwa Araba.

☐ **“vukeni ng'ambo wenye silaha mbele ya ndugu zenu”** Kwa kuwa Reubeni, Gadi, na nusu ya Manase waliishi upande wa mashariki mwa Mto Yordani eneo ambalo lilikuwa tayari limekwisha kutekwa, sasa iliwapasa kwenda katika mapigano kwanza na kupigana kwa ajili ya nchi ya ndugu zao (kama vile mist. 19-20) kabla ya kuishi katika nchi yao wenyewe.

3:19 “wanyama wengi” “wanyama wengi” waliokuwa nao ni wale waliowateka kwenye vita kutoka sehemu zote (1) Misri na (2) ng'ambo ya mataifa ya Mto Yordani.

☐ **“niliyowapa”** Chimbuko la baraka zote ni Mungu (KITENZI kinachotumika mara kwa mara “niliyowapa” BDB 678, KB 733, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU). Hawa hawakupata mateka wa vita kama wao wenyewe.

3:20 “awapumzishe ndugu zenu kama ninyi, nao pia waimiliki nchi wapewayo” Kitabu cha Waebrania ni fasiri bora ya Agano Jipya kuhusiana na Vitabu Vitano vya Musa. Katika Waebrania 4, neno “pumzika” limetumika katika namna tatu:

1. siku ya saba ya mapumziko kama Mungu alivyopumzika baada ya uumbaji, Sabato
2. Waisraeli walipumzika baada ya kuiteka Nchi ya Ahadi (kama vile 12:10; 25:19; Yosh. 23:1)
3. mbingu, pumziko la milele la siku ya saba. Hapa neno “pumzika” linanarejelea ulinzi, #2.

3:21 Kwa sababu ya utoaji wa YHWH ndani ya jangwanaushinding'ambo ya Mto Yordani, Iliwapasa Waisraeli kumwamini na kuendelea mbele!

3:22 “Bwana, Mungu wenu, ndiye awapiganiaye” Hizi si juhudi, ujuzi, au chimbuko la kibinadamu, bali ni nguvu za Mungu (kama vile 1:30; 20:4; Kut. 14:14; 15:3).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 3:23-29

²³Nikamnyenyekea Bwana wakati huo, nikamwambia, ²⁴Ee Bwana Mungu, umeanza kumwonyesha mtumishi wako ukubwa wako, na mkono wako wa nguvu; kwani kuna mungu gani mbinguni au duniani awezaye kufanya mfano wa kazi zako, na mfano wa matendo yako yenye nguvu? ²⁵Nami nakuomba nivuke, nikaione hiyo nchi nzuri iliyoko ng'ambo ya Jordani, mlima ule mzuri, na Lebanoni. ²⁶Lakini Bwana alikuwa amenikasirikia kwa ajili yenu, asinikize; Bwana akaniambia, Na ikutoshe, usinene nami zaidi jambo hili. ²⁷Kwea katika kilele cha Pisga ukainue macho yako upande wa magharibi, na kaskazini, na kusini, na mashariki, ukatazame kwa macho yako, kwa maana huuvuki mto huu wa Yordani. ²⁸Lakini mwagize Yoshua umtie moyo mkuu, umtie na nguvu; kwani ndiye atakayevuka mbele ya watu hawa, na nchi utakayoiona atawarithisha yeye. ²⁹Basi tukakaa katika bonde lililoelekea Beth-peori.

3:23-29 Haya ni maelezo ya kipekee sana kutoka kwa Musa. Hii ndiyo sehemu pekee ndani ya Biblia ambayo imelinukuu ombi la Musa kwa ajili ya hao wenyewe. Katika maeneo mengine aliwaomba watu au nchi. Hili ni tazamio ndani ya moyo wa mtu, aitwaye Musa.

3:23

NASB, NKJV,

NJB “nikamsihi”

NRSV “nikajitetea”

TEV “nikamuomba kwa bidii”

Nikamuomba Bwana (BDB 335, KB 334, *Hithpael* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama viile I Fal. 8:33 ,47,59; II Nya. 6:37; Ayubu 8:5; 9:15; Zab. 30:8; 142:1; Hosea 12:4) kwa bidii. Musa alikuwa katika maumivu makubwa juu ya kutokubaliwa kuingia katika Nchi ya Ahadi.

3:24 “Ee Bwana Mungu” Hili neno “Bwana” hapa ni neno *adonai* (BDB 10), ambalo ni neno la Kiebrania lenye maana ya “mmiliki,” “mtawala,” “mwanamme,” au “Mwenye mamlaka.” Hili neno “Mungu” ni neno la Kiebrania YHWH (BDB 217). Anasema “Bwana, YHWH.” Jina hili limetumika kwa uchache sana katika maandiko ya Musa. Hii ni lugha ya Musa ya kimaombi. Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.

☐ **“umeanza kumwonyesha mtumishi wako ukubwa wako”** Musa alijitetea kulingana na maarifa ya ukaribu wake na YHWH, Tabia yake (tazama maelezo kamili katika 4:31 na 10:17), Matendo yake lazima yangemshawishi YHWH kumwacha kuvuka ng’ambo ya Mto Yordani, lakini YHWH haangalii sifa ya watu!

☐ **“kwani kuna mungu gani mbinguni au duniani awezaye kufanya mfano wa kazi zako, na mfano wa matendo yako yenye nguvu”** Je! hii ndiyo dhana kwamba Mungu ndiye Mungu mkuu miongoni mwa wengi, iitwayo ufuasi wa mungu mmoja mkuu miongoni mwa wengi (yaani, Kut. 15:11 na Kumb. 4:7; 5:7, tazama *The Jewish Study Bible*, kr. 379-380)? Je! hii inamaanisha kwamba Musa anakiri kuwepo kwa miungu mingine, lakini YHWH ndiye mwenye nguvu zaidi? Au ni dhana ya kuwepo Mungu mmoja (mf. 4:35,39; 6:4; Kut. 20:2-3; Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5,6-7,14,18,21,22), Mungu mmoja na wa kipekee? Hakika hatujui. Kwa kiasi fulani ningependa kuamini kwamba Musa hairejelei miungu mingine, bali nguvu nyingine za kiroho, mf. wakati mwingine anaitwa *elohim* (kama vile Zab. 8:5; 82:1,6; 1 Sam. 28:13).

25 “Nami nakuomba nivuke, nikaione” Kifungu hiki kina VITENZI viwili:

1. “nivuke” - BDB 716, KB 778, *Qal* ya HALI YA KUSIHI
2. “nikaone” - BDB 906, KB 1157, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini katika maana ya KUSIHI

3:26 “Bwana alikuwa amenikasirikia” Huu ni mfano wa lugha ya kibinadamu (“amenikasirikia” BDB 720, KB 780, tazama Mada Maalum katika 2:15). Ni kwa namna gani tunaweza kueleza juu ya kughadhabika kwa Mungu pasipo kutumia maneno ya kibinadamu? Hatuwezi, bali yatupasa kukumbuka kwamba Mungu si mwanadamu na hafikirii na kutenda kama wanadamu. Tunayatumia maneno ya kibinadamu kutoa wasifu wa asili ya Mungu kwa kujua kwamba wanadamu walio anguka hawawezi kutoa wasifu wa Mungu. Dhambi ya Musa katikati ya umati (kama vile 32:51; Hes. 20:10-12; 27:12-14) ilileta athari katikati ya umati!

☐ **“kwa ajili yenu”** Tazama maelezo katika 1:34,37.

☐ **“Na ikutoshe, usinene nami zaidi jambo hili”** Musa alikuwa akielekea ukingoni (kama vile Hes. 20:2-

13; 27:13; Kumb. 1:37; 3:23-27), “Tafadhari, niruhusu niingie katika Nchi ya Ahadi.” Mwishowe Mungu akasema, “usinene nami zaidi” (BDB 414, KB 418, *Hiphil* ya KITENZI AMRISHI).

3:27 Mstari huu na mst. 28 ina mfululizo wa amri katika kuyajibu maombi ya Musa:

1. “Kwea” - BDB 748, KB 828, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. “ukainue” - BDB 669, KB 724, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. “ukatazame” BDB 906, KB 1157, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
4. “mwagize” - BDB 845, KB 1010, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
5. “umtie moyo” - BDB 304, KB 302, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
6. “umtie na nguvu” - BDB 54, KB 65, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

Mungu alitoa mahitaji kwa Musa na kwa Israeli (kumtia nguvu Yoshua, kama vile mst. 28b,c).

☐ **“kilele cha Pisga”** Tazama maelezo katika mst. 17.

☐ **“ukainue macho yako upande wa magharibi, na kaskazini, na kusini, na mashariki, ukatazame kwa macho yako”** Huuni mfano kamili wa pendo la Mungu na ghadhabu yake. “Nasema hutaingia, bali ukaitazame.”

☐ **“kwa maana huuvuki mto huu wa Yordani”** Mungu haangalii heshima ya mtu. Musa alikuwa mtu muhimu wa Mungu, lakini alimkaidi Mungu hadharani na hivyo kupata maumivu ya matokeo ya ukaidi huo (kama vile Ayubu 34:11; Zab. 28:4; 62:12; Mit. 24:12; Muh. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 14:12; I Nya. 3:8; II Nya. 5:10; Gal. 6:7-10; II Tim. 4:14; I Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12).

3:29 “Beth-peori” Kiuhaliasia hii ni “nyumba/hekalu la Peori” (BDB 112). Peori ulikuwa mlima au mji uliokuwa kaskazini magharibi mwa Moabu. Hapa palikuwa mahali pa Israeli kufanyia ibada ya sanamu (*Ba'al* ibada ya ustawi, kama vile Hsabu 22-23). Baadaye pakawa urithi wa Reubeni (kama vile Yosh. 13:20).

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! ni maarifa gani ya kitheolojia yamhusuyo Mungu tunayojifunza kutokana na maelezo haya?
2. Ni kwa namna gani unamhusianisha Mungu wa mist. 3 na 6 pamoja na Mungu wa Agano Jipya?
3. Je! mst. 24 unafundisha juu ya kuwepo kwa miungu mingine?
4. Ni kwa namna gani Mungu alionyesha huruma na bado kwa Musa katika mst. 27?

KUMBUKUMBU LA TORATI 4

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Musa anaamuru hukumu 4:1-8	Hitimisho la maelezo ya Awali 4:1-4 4:5-8	Musa anawasihi Israeli kuwa watiifu 4:1-4 4:5-6 4:7-10	Uasi wa Baal-Poeri kinyume cha hekima ya kweli 4:1-8 Ufunuo katika Horebu: Matakwa yake 4:9-14
4:9-14	4:9-14		
Jihadhari na ibada ya sanamu 4:15-24		4:11-14 4:15-24	4:15-20 Hukumu ijayo na ya ubadilishaji 4:21-24
4:25-31	4:25-31	4:25-31	4:25-28 4:29-31 Utukufu wa kuchaguliwa Na Mungu
4:32-40	4:32-40	4:32-40	4:32-34 4:35-38 4:39-40
Miji ya makimbilio Mashariki mwa mto Yordani 4:41-43	Kiambatanisho 4:41-43	Miji ya makimbilio mashariki mwa mto Yordani 4:41-43	Miji ya makimbilio 4:41-43
Maelekezo wakati wa Kuzipokea sheria za Mungu 4:44-49	Hotuba ya pili ya Musa (4:44-26:19:28) 4:44-49	Maelekezo wakati wa kuzipokea sheria za Mungu 4:44-49	Hotuba ya pili ya Musa (4-44-11:32) 4:44-49

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi) *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozokwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kila aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4:1-4

¹Na sasa, Ee Israeli, zisikilizeni amri na hukumu niwafundishazo, ili mzitende; mpate kuishi na kuingia na kuimiliki nchi awapayo Bwana, Mungu wa baba zenu. ²Msiliongeze neno niwaamurulo wala msilipunguze, mpate kuzishika amri za Bwana, Mungu wenu, niwaamuruzo. ³Macho yenu yameona aliyoyatenda Bwana kwa sababu ya Baal-peori; maana wote waliomfuata Baal-peori, Bwana, Mungu wako, amewaangamiza kutoka kati yako. ⁴Bali ninyi mlioambatana na Bwana, Mungu wenu, mnaishi kila mmoja wenu, hata leo.

4:1 “zisikilizeni” Kitenzi hiki (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI) kimetumika mara nyingi katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (mf, 1:16; 4:1; 5:1; 6:3,4; 9:1; 20:3; 27:10; 33:7). Maana yake ya msingi ni “kusikia ili kutenda.” Inalenga katika tendo, sio kusikiliza (kama vile Yakobo 1:22-25). Sura hii ina maonyo kadhaa, mistari. I, 2, 6, 9, 13, 14, 15, 19, 23, na 26 (kama vile Mika 1:2; 3:1; 6:1).

☐“**amri na hukumu**” Hizi zilihusisha mafunuo ya Mungu yaliyokusanywa. Ni maagano yote yaliyohitajika na mafunuo ya Mungu juu yake. Ni mfanano katika maana ya neno Torati (Fasihi.“mafundisho,” yaani, Sheria za Musa).

MADA MAALUM: ISTILAHU KWA AJILI YA UFUNUO WA MUNGU (Kwa kutumia Kumbukumbu la Torati na Zaburi)

- I. “Amri ya Serikali,” BDB 349, “fanya kuwa sheria, tamko, au agizo”
 - A. JINSI YA KIKE, קק (KB, 346) – Kumb. 4:1,5,6,8,14,40,45; 5:1; 6:1,24; 7:11; 11:32; 16:12; 17:19; 26:17; 27:10; Zaburi 2:7; 50:16; 81:4; 99:7; 105:10,45; 148:6
 - B. JINSI YA KIUME, קקק (KB, 347) – Kumb. 6:2; 8:11; 10:13; 11:1; 28:15,45; 30:10,16; Zab. 89:31; 119:5,8,12,16,23,26,33,48, 54,64,68,71,80, 83,112,124,135, 145,155,171
- II. “Sheria,” BDB 435, KB 1710, “maelekezo” Kumb.1:5;4:44;17:11,18,19;27:3,8,26;28:58,61;29:21,29;30:10;31:9; Zaburi 1:2;19:7;78:10;94:12;105:45;119:1,18,29,34,44,51,53,55,61,70,72,77,85,92,97,109,113,126,136,142,150, 153,163,165,174
- III. “Shuhuda” BDB 730, KB 790, “Sheria za ki-Ungu”
 - A. WINGI קקקק – Kumb. 4:45; 6:17,20; Zaburi 25:10; 78:56; 93:5; 99:7; 119:22,24,46,59,79,95,119,125,138,146,152,167,16
 - B. עקקק au עקקק – Zaburi 19:7; 78:5; 81:5; 119:2,14,31,36,88,99,111,129,144,157
- IV. “Maagizo” BDB 824, KB 959, “Shitaka” Zaburi 19:8;103:18;111:7;119:4,15,27,40,45,56,63,69,78,87,93,94,100,104,110,128,134,141,159,168,173
- V. “Amri” BDB 846, KB 622 – Kumb. 4:2,40; 5:29; 6:1,2,17,25; 8:1,2,11; 10:13; 11:13; 15:5; 26:13,17; 30:11,16; Zab. 19:8; 119:6,10,19,21,32,35,47,48, 60,66,73,86,96,98,115,127,131,143,151, 166,176
- VI. “Hukumu/Maagizo,” BDB 1048, KB 651, “maamuzi” au “haki” – Kumb. 1:17; 4:1,5,8,14,45; 7:12; 16:18; 30:16; 33:10,21; Zab. 10:5; 18:22; 19:9; 48:11; 89:30; 97:8;105:5,7; 119:7,13,20,30,39,43,52,62, 75,84,102,106,120,137, 149,156,160,164; 147:19; 149:9
- VII. “Njia zake” BDB 202, KB 231, Mwongozo wa YHWH kwa maisha ya watu wake – Kumb. 8:6; 10:12; 11:22,28; 19:9; 26:17; 28:9; 30:16; 32:4; Zab. 119:3, 5,37,59
- VIII. “Maneno yake”
 - A. BDB 182, KB 211 – Kumb. 4:10,12,36; 9:10; 10:4; 17:19; 18:19; Zab. 119:9,16,17,25,28,42,43,49, 57,65,74, 81,89,101,105,107,114,130,139,147, 160,161,169
 - B. BDB 57, KB 67

1. "Neno" – Kumb. 33:9; Zaburi 119:11,67,103,162,170,172
2. "Ahadi" – Zaburi 119:38,41,50,58,76,82,116,133,140,148,154
3. "Amri" – Zaburi 119:158

Haya yote yanarejerea ufunuo maalum wake Mungu kwa Israeli. Kimsingi yanafanana. Angalia Mada Maaalum: Uvuvio.

☐“**niwafundishazo**” Musa alitumika kama wakili wa YHWH kwa ajili ya ukombozi na ufunuo (yaani, nabii, kama vile 3:14; 4:1-17; 18:15-18; 34:10-12).

☐“**ili mazitende**” KITENZIJINA (BDB 793, KB 889, *Qal* ya KITENZIJINA HALISI CHA MUUNDO WA MANENO) kinawahimiza watu kuisikia sheria ya Mungu na kisha kuitii (kama vile. 16:12; 30:8).

☐“**mpate kuishi na kuingia na kuimiliki nchi**” Tambua sharti la asili la agano la Mungu (mf. 5:33; 8:1; 16:20; 30:16,19). VITENZI hivi ni *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU. KITENZI cha mwisho katika mst. 1 (toa) ni *Qal* ya KAULI ENDELEVU. Zawadi ya Mungu inategemea na matendo ya wana wa Israeli!

☐“**Mungu wa baba zenu**” Hii inarejelea kwa mababa wa imani (Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, kama vile 1:11,21; 4:1,31,37; 6:3; 12:1; 26:7; 27:3). Maagano yote na mababa wa imani yalikusishia masharti (isipokuwa katika kitabu cha Mwanzo 6-9 na 15:12-21).

4:2 “Msilongeze neno wala msilipunguze” Hili haliwarejelei waandishi waliokuwa wakiyaandika maandiko ya sheria, bali ni heri kwamba wewe huwezi kuongeza asili ya sheria (kama vile 12:32; Mit. 30:5-6; Mhu. 3:14; Yer. 26:2). Haya makatazo juu ya kuongeza au kuondoa ni tabia ya fasihi ya kale ya mashariki ya karibu. Kuna tofauti ndogo kati ya amri kumi kama zilivyoandikwa katika kitabu cha Kutoka 20 na kitabu cha Kumbukumbu la Torati 5.

4:3 “Baal-peori” Hii inarejelea sehemu ambayo wana wa Israeli waliacha kumfuata YHWH na kuifuata miungu ya ustawi ya Moabu (kama vile Hes. 25:1-9).

4:4 “Bali ninyi mlioambatana na Bwana” Neno la Kiebrania “ambatana,” “shikamana” (BDB 180) limetafsiriwa kama KITENZI katika toleo la NASB. Ni kinyume cha “kujiungamanisha” katika mst. 3 (yaani., *Ba’al*). Muundo wa KITENZI hiki cha neno umetumia:

1. kuambatana na mke wa mtu katika kitabu cha Mwanzo 2:24
2. Ruthu kuambatana na Naomi katika kitabu cha Ruthu 1:14.

Hili linadokeza tabia ya utiifu au kuwajibika. Imetumika sambamba na neno “upendo” katika kitabu cha Mwanzo 34:3; I Fal. 11:2; Mit. 18:24 (tazama NIDOTTE, juzuu. 1, uk. 911).

Hata katika uchaguzi wa Mungu, mwanadamu anapaswa kuupokea istahilivyo. Hata kama Mungu aliichagua Israeli kuwa taifa lake la kikuhani (kama vile Kutoka 19:5-6), kila mmoja anapaswa kumchagua Mungu. Huu ni uwiano kati ya ufalme wa Mungu na mwanadamu huru. Pia ni uwiano wa itikio la ushirikiano (“wewe” HALI YA WINGI) dhidi ya mwitikio wa mmoja mmoja (“kila mmoja wako”).

Hakuna KITENZI katika mst. 4; dhana ya MANENO inawasilisha VIVUMISHI viwili (BDB 180, 311).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4: 5-8

⁵Angalieni nimewafundisha amri na hukumu, vile vile kama Bwana, Mungu wangu, alivyoni amuru, ili mazitende katika nchi mwingiayo ili kuimiliki. ⁶Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili. ⁷Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, kama Bwana, Mungu wetu, alivyo, kila tumwitapo? ⁸Tena liko taifa gani kubwa, lililo na amri na hukumu zenye haki kama torati hii yote, ninayoiweka mbele yenu leo.

4:5

NASB, NRSV "angalieni"
NKJV "kwa hakika"
TEV -----
NJB "tazama"

Hii ni *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 906, KB 1157). Ilikuwa ni njia ya fasihi inayodai kwamba Musa alitimizwa wajibu wake na sasa watu walipaswa kuupokea kwa shukrani.

4:6

NASB "Zishikeni basi , mkazitende"
NKJV "kuweni makini mkazishike"
NRSV "ni lazima uzishike kwa bidii"
TEV "zitiini kwa uaminifu"
NJB "zitunze, zitie katika matendo"

Kuna VITENZI viwili katika hii tungo:

1. "zishikeni" (BDB 1036, KB 1581, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU), ambayo humaanisha "tunza," "angalia," au "linda." KITENZI hiki kimetumika mara nyingi katika vitabu vitano vya Musa (Kumbukumbu la Torati, kama vile 2:4; 4:2,6,9,15,23,40; na sehemu zingine kadhaa)
2. "mkazitende" (BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) humaanisha "tenda" au "mkafanye." KITENZI pia kimetumika mara nyingi katika Agano la Kale (mf. Kumb. 4:1,3,6,13,14,16,23,25).

4:6 "hekima" Neno hili (BDB 315) limetumika katika Mit. 1:2,7 na KIVUMISHI katika 1:6. Hekima ni maarifa ya Mungu na mapenzi yake. Ni kile anachotafuta mwanadamu kwa sababu wameumbwa katika sura na kufanana na Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27), na kwa ajili ya ushirika nae (kama vile mist. 7-8).

☐ **"akili"** Neno hili (BDB 108) ni mfanano na lile la hekima. Lengo lake ni dhahili, uchaji-Mungu, maisha ya furaha (mf, Kumb. 32:28; Mit. 2:1-22; 3:13-18).

☐ **"Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili"** Je, Mungu aliichagua Israeli kwa sababu aliwapenda sana kuliko wengine? Mungu anawapenda watu wote sawa (Yohana 3:16; I Tim. 2:4; II Pet. 3:9). Mungu alihitaji tu sehemu ya kuanzia. Alimchagua Ibrahimu na uzao wake kuwa ufalme wa makuhani duniani (kama vile Mwa.12:3; Kut. 19:4-6; Mdo. 3:25; Gal. 3:8). Wao walikua uchaguzi kwa ajili ya kusudi zaidi kuliko uchaguzi kwa sababu ya upendo maalumu. Tazama Mada Maalumu hapa chini.

MADA MAALUM: UPENDELEO WA KIINJILISTI WA BOB

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiinjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Yer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31), wale wote walioumbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israel, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.

Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anaoanisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.

2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israeli. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihirisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Ibrahimu, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, "kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu"). Israeli ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakilisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihirisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
 - a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
 - b. Yereimia – 3:17; 4:2; 16:19
 - c. Mika 4:1-3
 - d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa "agano jipya" (kama vile Yer.31:31-34; Eze. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna "moyo mpya," "mawazo mapya," na "roho mpya." Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimarisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni "fumbo la Mungu," lililofichika lakini sasa limedhihirishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya limejikita shabaha yake juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israeli ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumaini utaendelea kuchukua muda kusoma Mada Maalum: Kwanini Ahadi za kiagano za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti sana na Ahadi za kiagano za Agano Jipya. Unaweza ukaipata mtandaoni katika tovuti www.freebiblecommentary.org.

4:7 "Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao" Hii inarejelea uwepo binafsi wa Mungu (yaani, kuwepo kila mahali daima) na Israeli katika muundo wa wingu la utukufu (*Shekinah*) (kipindi cha kutanga tanga jangwani) na baadae sanduku la Agano (ng'ambo ya mto Yordani na katika kipindi cha utawala wa kifalme).

☛**"kila tumwitapo"** Hii inaonyesha kwamba Wayahudi wana uhakika kwamba Mungu aliyeumba dunia ndiye Mungu atakayewakubalia watakapo muomba. Mwenye nguvu na umiliki (mf, Zab. 34:18; 145:18)! Mungu aliye wa matendo, kinyume kabisa na sanamu za Wakanaani!

4:8 "amri na hukumu. . .torati" tazama mada maalumu katika 4:1.

☑“haki” Hii ni stiari kutoka katika mafunjo ya mto. Haki ya Mungu ni kiongozi au mtawala ambaye kwake tunapimwa. Torati inasisitizwa katika tabia ya Mungu. Tazama Mada Maalumu katika 1:16.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4:9-14

⁹ Lakini, jihadhari nafsi yako, ukailinde roho yako kwa bidii, usije ukayasahau mambo yale uliyoyaona kwa macho yako, yakaondoka moyoni mwako siku zote za maisha yako; bali uwajulishe watoto wako na watoto wa watoto wako; ¹⁰ siku ile uliyosimama mbele za Bwana wako huko Horebu, Bwana aliponiambia, Nikusanyieni watu hawa, nami nitawasikizisha maneno yangu, ili wajifunze kunicha mimi siku zote watazoishi duniani, wakapate na kuwafundisha watoto wao. ¹¹ Mkakaribia, mkasimama chini ya ule mlima; mlima ukawaka moto mpaka kati ya mbinguni, kwa giza na mawingu, na giza kuu. ¹² Bwana akasema nanyi kutoka kati ya moto; mkasikia sauti ya maneno, lakini hamkuona umbo lo lote; sauti tu. ¹³ Akawahubiri agano lake, alilowaamuru kulitenda, yaani, zile amri kumi; akaziandika juu ya mbaao mbili za mawe. ¹⁴ Bwana akaniamuru wakati ule niwafundishe maagizo na hukumu, mpate kuzitenda katika nchi ile mtakayoivukia ili kuimiliki.

4:9

NASB “Lakini, jihadhari nafsi yako, ukailinde roho yako kwa bidii”
NKJV “lakini, chukua tahadhali ya nafsi yako, na ukajilinde kwa bidii”
NRSV “lakini kuwa mwangalifu na ukajihadhali sana”
TEV “ukajilinde! Uwe na uhakika. . .”
NJB “lakini uwe mwangalifu, kama umuhimu wa maisha yako”

Tungo hii ina KAULI SHURUTISHI mbili kutoka katika asili ile ile:

1. “jihadhari” - BDB 1036, KB 1581, *Niphal* KAULI SHURUTISHI, kama vile 4:15; Yoh. 23:11; Yer. 17:21).
2. “ukailinde” - BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI SHURUTISHI katika maana ya “kuzitenda” (kama vile 7:12).

Utiifu ni uzima –na-tukio la kufa (kama vile 30:15-20)!

☑“usije ukayasahau. . .yakaondoka” Tazama Kumb. 8:11-20.

☑“moyoni” Katika saikolojia ya Kiebrania hisia hukaa ndani kabisa. Moyo ni kiini cha ufahamu (hasa kumbukumbu) na haiba. Mungu anasema, “usiisahau torati!” Tazama Mada Maalumu: Moyo katika 2:30.

☑“siku zote za maisha yako” Utendaji wa mtindo wa maisha unahitajika (kama vile mst. 10; 6:2; 12:1; 16:3).

☑“bali uwajulishe watoto wako na watoto wa watoto wako” Hii ni dhana iliyojirudia katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (kama vile mst. 10; 6:7, 20-25; 11:19; 31:13; 32:46; na muhtasari wa Kut. 10:2; 12:26; 13:8,14). Ikiwa waaminio hawatawafundisha watoto wao juu ya Mungu, watashindwa kama wazazi (inaongelea kibiblia)! Imani husonga mbele kupitia familia (kama vile 5:10; 7:9)!

4:10 “siku ile uliyosimama mbele za Bwana wako huko Horebu” wasikilizaji walikuwa ni wana wa kizazi cha wale waliotoka Misri. Maelezo haya yanarejelea katika kitabu cha Kutoka 19-20. Kukumbuka matendo makuu ya wokovu wa Mungu (yaani, Kutoka) ni dhamira iliyojirudia rudia (kama vile 5:15; 7:18; 8:2,18; 9:7,27; 11:2; 15:15; 16:3,12;24:9,18,22; 25:17; 32:7).

☑“ili wajifunze kunicha mimi” Matendo ya Mungu kama alivyotenda katika Mlima Horebu, hivyo basi waambatane nae kwa hofu ya Kimungu (kama vile Kut. 20:20; Mit. 1:7; 9:10; Mhu. 12:15; Isa. 11:2-3; Zab. 34:11).

4:11 “mlima ukawaka moto” Moto ni kielelezo cha uwepo wa Mungu (kama vile Kut. 19:18; Kumb. 5:23; 9:15; Ebr. 12:18). Yumkini ikawakilisha utakaso. Tazama Mada Maalumu hapa chini.

MADA MAALUM: MOTO (BDB 77, KB 92)

Moto unavyovidokezochanyanahasikatikamaandiko.

- A. Chanya
 1. Husisimua (kama vile Isaya 44:15; Yohana 18:18)
 2. Huwashanuru (kama vile Isaya 50:11; Mt. 25:1-13)
 3. Hupikia (kama vile Kutoka 12:8; Isaya 44:15:16; Yohana 21:9)
 4. Husafisha (kama vile Hes. 31:22-23; Mithali 17:3; Isaya 1:25; 6:6-8; Yer. 6:29; Malaki 3:2-3)
 5. Utakatifuwa Mungu (kama vile Mwa. 15:17; Kutoka 3:2; 19:18; Ezek. 1:27; Waebrania 12:29)
 6. Uongoziwa Mungu (kama vile Kutoka 13:21; Hes 14:14; Wafalme 1. 18:24)
 7. Uwezeshajiwa Mungu (kama vile Mdo. 2:3)
 8. Ulinziwa Mungu (kama vile Zekaria 2:5)
- B. Hasi
 1. Huunguza (kama vile Yos 6:24; 8:8; 11:11; Mt. 22:7)
 2. Huangamiza (kama vile Mw. 19:24; Walawi 10:1-2)
 3. Hasira (kama vile Hes 21:28; Isaya 10:16; Zek. 123:6)
 4. Adhabu (kama vile Mwa. 38:24; Walawi 20:14; 21:9; Yoshua 7:17)
 5. Isharayambayayasikuyamwisho (kama vile Ufunuo 13:13)
- C. Hasiraya Mungudhidiyadhambimaranyingihudhihirishwakwatanuruyamoto.
 1. Hasirayakehuunguza (Kama vile Hos 8:5; Sefania 3:8)
 2. Humiminamoto (kama vile Nah 1:6)
 3. Moto wamilele (kama vile Yer. 15:14; 17:4; Mt. 25:41; Yudaayaya 7)
 4. Hukumuyasikuyamwisho (kama vile Mt. 3:10; 5:22; 13:40; Yohana 15:5; The. 2. 1:7; Petro 2. 3:7-10; Ufu 8:7; 16:8; 20:14-15)
- D. Moto maranyingihuonekanakatikanuru
 1. Mwa. 15:17
 2. Kutoka 3:2
 3. Kutoka 19:18
 4. Zaburi 18:7-15; 29:7
 5. Eze. 1:4, 27; 10:2
 6. Ebr. 1:7; 12:29
- E. Kama zilivyo stiari nyingikatika Biblia (yaani, chachu, simba) motounawezakuwa baraka au kufuatanamazingira au muktadha.

☐“**kwa giza na mawingu, na giza kuu**” Uwepowa YHWH kimwili unaweza kufahamika katika njia mbili:

1. Hali ya volkano - Kut. 19:18; Zab. 68:7-8; 77:18; 97:2-5; Amu. 5:4-5; II Sam. 22:8; Isa. 29:6; Yer. 10:10
2. tetemeko - Kut. 19:16,19; Zab. 68:8; 77:18; Amu. 5:4; Isa. 29:6; Nahumu 1:3

Hivyo basi, giza kuu (kama vile 5:22; II Sam. 22:10; I Fal. 8:12; II Nya. 6:1) linaweza kuwa:

1. mawingu ya majivu
2. mawingu ya mvua

Kufunikwa huku kulikuwa ni kwa ajili ya ulinzi wa Israeli (kama vile Kut. 19:18). Walifikiri kwamba ikiwa wanadamu watamuona Mungu basi watakufa (kama vile Mwa. 16:13; 32:30; Kut. 3:6; 20:19; 33:20; Amu. 6:22-23; 13:22).

4:12 “lakini hamkuona umbo lo lote” Mungu hana umbo la kimwili (kama vile Yohana 4:24). Alimruhusu Musa kumwona “nyuma yake” katika Kut. 33:23. YHWH hatamani uwakilishi wa kimwili kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka dhambini mwenye mwelekeo wa ibada ya sanamu (kama vile mistari. 15-19).

4:13 “Akawahubiri agano lake” KITENZI hiki (BDB 616, KB 665, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU), kinapotumiwa na Mungu kama lengo, kinaonyesha ufunuo mpya (mf, II Sam. 7:11; Isa. 42:9; 45:19; Amosi 4:13).

Njeo ya WAKATI USIO TIMILIFU inadokeza kwamba “amri kumi” sio ufunuo wote wa YHWH. Zaidi vitabu vya Kutoka na Kumbukumbu la Torati ni ufafanuzi wa kuhusisha amri kumi za Mungu. Tazama Mada Maalumu hapa chini.

MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), "Agano," sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihirisha kutoleta ushawishi. Yumkini ubashiri mzuri ni “kukata” ikimaanisha sadaka ya mnyama inayojumuishwa kwenye agano (kama vile Mwa. 156:10,17). Hata hivyo, kiini dhahiri cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji.

Agano ni namna ambayo Mungu wa kweli (angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu Mmoja) anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu kwa wazi unaonekana katika dhana ya Agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. Uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. Utunzaji na ahadi ya Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)
3. Wito wa Abrahamu (kama vile Mwanzo 12)
4. Agano pamoja na Abrahamu (kama vile Mwanzo 15)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. Kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wakati kati ya Edeni
2. Kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na majina kuwakusanya wanyama wote
3. Kwaimani Abraham anapaswakuia chafamili yake, nakumfuata Mungu, nakuaminika kikizazikijacho
4. Kwa imani Musa anawatoa wana wa Israel toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana (kama vile Walawi 26, Kumbukumbu la Torati 27-28)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika “agano jipya” (kama vile Yer. 31:31-34; Ebr. 7:22; 8:6,8,13; 9:15; 12:24). Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18:31 na Ezek. 36:27-38 (tendo la YHWH). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Lengo la yote ni sawa:

1. Urejesho wa ushirika na YHWH uliopotea katika Mwanzo 3
2. Uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubarifu. Sheria za Mungu zikajakuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano la Mungu, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwanzo 3; Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea, angalia Mada Maalum: Kuamini katika Agano Jipya). Yesu anaita ushirika wake mpya na waamini “agano jipya” (kama vile Mt. 26:28; Marko 14:24; Lk. 22:20; 1 Kor. 11:25). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana Kristo (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15), maelezo elekezi ya ukubalifu (Warumi 4) wito wa ushurutishi wa kuwa mtakatifu (kama vile Mt. 5:48)! Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, bali ni katika utii (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani, Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekana kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika Agano Jipya (angalia Mada Maalum: Uasi)

☐“amri kumi” Ni dhahili hii inamaanisha “amri kumi” (BDB 797 MUUNDO WA MANENO 182) na inafahamika katika Kiyunani kama amri kumi za Mungu. Ni kwa muhtasari, maelezo mafupi ya ufunuo wa Mungu (kama vile Kumb 20; Kumb 5).

☐“akaziandika” Mungu mwenyewe aliandika (lugha ya kibinadamu kumhusu Mungu, tazama Mada Maalumu katika 2:15) “amri kumi” (kama vile Kut. 31:8; 32:15-16). Kufichua uhalisia wa maelezo haya hakuathiri asili ya Uungu wa sheria!

☐“mbao mbili za mawe” Kutokana na uvumbuzi wa sasa wa mambo ya kale na kile tunachokiita mikataba ya Wahiti wa Suzerain (wa millenia ya 2 K.K.), tunafahamu kwamba kitabu cha Kumbukumbu la Torati kimefuata muundo na muhtasari wake. Nafikiri kwamba “mbao mbili” zinarejelea kwenye nakala mbili, hasa amri kumi zilizohitajika kwenye makubaliano haya (pia yalifanyika makubaliano ya nyaraka za matendo makuu yaliyopita, yaani, Kumbukumbu la Torati 1-4). Hii kihistoria iliimarisha kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Tazama utangulizi wa kitabu, VII.

4:14 “mpate kuzitenda” Haitoshi kufahamu mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yako, lakini hutenda hivyo (kama vile mist. 1,2,5,6; Luka 6:46; Yakobo 2:14-20).

ANDIKO NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4: 15-20

¹⁵Jihadharini nafsi zenu basi; maana hamkuona umbo la namna yo yote siku ile Bwana aliyosema nanyi kutoka kati ya moto; ¹⁶msije mkajiharibu nafsi zenu, mkajifanyia sanamu ya kuchonga, mfano wa sura yo yote, mfano wa mwanamume au mwanamke, ¹⁷mfano wa mnyama ye yote aliye duniani, au mfano wa ndege ye yote arukaye mbinguni, ¹⁸au mfano wa kitu cho chote kitambaacho juu ya ardhi, au mfano wa samaki ye yote aliye majini chini ya nchi; ¹⁹tena usije ukainua macho yako hata mbinguni, na ulionapo jua, na mwezi, na nyota, jeshi la mbinguni lote pia, ukashawishwa na kuviabudu, na kuvitumikia, ambavyo Bwana, Mungu wako amewagawanyia watu wote chini ya mbingu zote. ²⁰Bali Bwana amewatwaa ninyi, na kuwatoa katika tanuu ya chuma, katika Misri, mpate kuwa watu wa urithi kwake, kama mlivyo leo hivi.

4:15

NASB “Jihadharini nafsi zenu basi”

NKJV “kuweni waangalifu kwa nafsi zenu”

NRSV “kuwa mwangalifu na kujihadhari sana”

TEV “kwa mema yako, jihadhari”

NJB “jihadhari kwa kile utendacho”

KITENZI hiki (BDB 1036, KB 1581, *Niphal* yaKAULI YA WAKATI TIMILIFU) kimetumika katika 4:2,6,9 (mara mbili),15,23,40. Matendo ya wana wa Israeli yalikuwa ni masharti ya kuwaunganisha na agano la YHWH. Walihitajika kuwa na bidii sana ili kuepuka ibada ya sanamu (kama vile 5:8-10).

4:16 “msije mkajiharibu nafsi zenu, mkajifanyia sanamu ya kuchonga” Hii ni rejea katika ndama ya dhahabu (kama vile Kut. 32) inayoungamanishwa na YHWH. Wana wa Israeli hawakuruhisiwa kumwakilisha YHWH kimwili kwa kitu chochote (kama vile mist. 16-18,23,25; 5:8; Kut. 20:4).

☐“mfano wa mwanamume au mwanamke” Mwelekeo wa mwanadamu ni kumtengeneza Mungu afanane na mwanamume au mwanamke. Ikiwa tutamweka Mungu katika muundo wa mwanadamu, tutamweka katika muundo ambao tunaweza kuutawala.

4:17 “mfano wa mnyama ye yote” Hii yumkini ikarejelea kwa (1) baadhi ya mataifa hutumia wanyama kuwakilisha miungu yao na miungu ya kike au (2) sifa za wanyama katika kumwelezea Mungu.

4:18 “kitambaacho juu ya ardhi” Hii inawezekana kurejelea kwa mdudu kombamwiko ambaye aliabudiwa na Wamisri.

4:19 “jua, na mwezi, na nyota, jeshi la mbinguni lote” Watu wa kale, kama vile (darubini) za kisasa, walihisi kwamba nyota ziliwakilisha majeshi au nguvu zilizotawala maisha ya wanadamu. Kuabudu mfumo wa nyota kunaonekana kulianzia huko Babeli (Mwanzo 1 yumkini ikawakilisha matokeo ya aina hii ya ibada ya sanamu, kama ilivyo Kutoka 20 inavyowakilisha matokeo ya waabudu sanamu wa Kimisri). Israeli ilikataa kwa nguvu zote aina hii ya ibada ya sanamu!

☐**“ambavyo Bwana, Mungu wako amewagawanyia watu wote”** KITENZI hiki (BDB 323, KB 322, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “kugawa,” lakini katika maana ya mgao au gawanya. Hii inaweza kudokeza kwamba Mungu alitumainisha kuabudu nyota, lakini nafikiri badala yake ni namna nyingine ya kuonyesha ukuu wa YHWH juu ya ulimwengu mzima (kama vile 29:26; 32:8). Ibada ya sanamu kamwe haukuwa mpango wa Mungu au mapenzi yake kwa mwanadamu.

4:20 “tanuu ya chuma” tanuu huchukua mawe yenye madini, na kuyachoma na kukifanya chuma kutumika. Huu ni mfanano wa Mungu kutenda kwa wana wa Israeli huko Misri (kama vile I Fal. 8:51; Yer. 11:4 na sitiari ile ile katika Isa. 48:10).

☐**“mpate kuwa watu wa urithi kwake”** Hiki kilikuwa ni cheo maalumu kwa ajili ya watu wa agano wa YHWH (mf, Kut. 19:5; Kumb. 7:6; 14:2; 26:18; Tito 2:14; na I Pet. 2:9). Walikuwa na urithi wa kiroho (YHWH na nchi) kwa sababu YHWH aliwachagua wao hata kabla ya uumbaji (kama vile 32:8-9; Zab. 33:6-12; Yer. 10:16; 51:19) ili kumwakilisha yeye katika ulimwengu.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4:21-24

²¹Tena Bwana alinikasirikia kwa ajili yenu, akaapa ya kwamba sitavuka Yordani, na ya kwamba sitaingia nchi ile njema, awapayo Bwana, Mungu wenu, iwe urithi. ²²Lakini mimi nitakufa katika nchi hii, sina ruhusa kuvuka Yordani; bali ninyi mtavuka, na kuimiliki nchi ile njema. ²³Jihadharini nafsi zenu, msije mkalisahau agano la Bwana, Mungu wenu, alilolifanya nanyi, mkajifanyia sanamu ya kuchonga, mfano wa umbo la kitu cho chote ulichokatazwa na Bwana, Mungu wenu, ²⁴kwa kuwa Bwana, Mungu wenu, ni moto ulao, Mungu mwenye wivu.

4:21 “Tena Bwana alinikasirikia kwa ajili yenu” Musa alikuwa anawakumbusha watu hukumu ya Mungu juu yake kwa sababu ya kutokutii kwake (kama vile 1:37; 3:26; Hes. 20:7-13). Ikiwa hawatatii, wataadhibiwa pia!

4:23 “Jihadharini nafsi zenu” KITENZI hiki (BDB 1036, KB 1581, *Niphal* KAULI SHURUTISHI) kimerudiwa mara nyingi katika sura hii. Kuna manufaa ya agano, lakini pia matokeo ya agano (kama vile 4:25; sura 27-29).

☐**“msije mkalisahau agano”** KITENZI hiki (BDB 1013, KB 1489, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) pia kimepatikana mara kadhaa katika sura hii (kama vile mist. 9,23,31) na pia katika 6:12; 8:11,14,19[mara mbili]; 9:7; 24:19[mara mbili]; 25:19; na 30:13; 31:21; 32:18. Hii ni dhamira kuu inayojirudia rudia!

4:24 “wivu” YHWH anaelezewa katika kifungu hiki kwa njia mbili:

1. “moto ulao” (BDB 77 na BDB 37, KB 46, *Qal* KAULITENDAJI ENDELEVU, kama vile Kut. 24:17; Kumb. 4:24; 9:3; Ebr. 12:29) ambayo humaanisha
 - a. YHWH ndiye Mungu mtengeneza agano la Sinai
 - b. Ni Mungu wa hukumu ikiwa agano litaachwa
2. “Mungu mwenye wivu” (BDB 888 na 42, kama vile Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 5:9; 6:15; Yosh. 24:19) ambapo humaanisha yeye binafsi, mpenda ahadi kwa Israeli, ambalo linafanana na agano la ndoa (kama vile Hosea

1-3). Kuvunjika kwa agano matokeo yake ni kukataliwa (mf, Yosh. 24:19; Nahumu 1:2). Neno lina uwanja mpana:

- a. ghadhabu - Mit. 6:34; Wimb. 8:6
- b. hasira - Mit. 14:30; 27:4
- c. wivu - Mwa. 26:14; Hes. 5:11-22; Eze. 31:9
- d. mashindano - Mhu. 4:4
- e. Moyo wa ibada - Hes. 11:29
(orodha kutoka NIDOTTE, juzuu 3, uk. 938)

Tazama Mada Maalumu: Mungu anaelezewa kama mwanadamu (lugha ya kibinadamu) katika 2:15.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4:25-31

²⁵ Utakapozaa wana, na wana wa wana, mkisha kuwa katika nchi siku nyingi, mkajiharibu na kufanya sanamu ya kuchonga kwa umbo la kitu cho chote, mkafanya ambayo ni maovu machoni pa Bwana, Mungu wako, na kumtia hasira; ²⁶ nawashuhudizia mbingu na nchi hivi leo, kwamba karibu mtaangamia kabisa juu ya nchi mwivukiayo Yordani kuimiliki, hamtafanya siku zenu ziwe nyingi juu yake, ila mtaangamizwa kabisa. ²⁷ Na Bwana atawatawanya kati ya mataifa, nanyi mtasalia watu kidogo hesabu yenu kati ya makabila, mtakakopelekwa mbali na Bwana. ²⁸ Na huko mtatumikia miungu, kazi za mikono ya watu, miti na mawe, ambao hawaoni, wala hawasikii, hawali, wala hawanusi. ²⁹ Lakini huko, kama mkimtafuta Bwana, Mungu wako, utampata, ukimtafuta kwa moyo wako wote, na roho yako yote. ³⁰ Na wakati uwapo katika mashaka, ukiisha kupatwa na mambo haya yote, siku za mwisho, utamrudia Bwana, Mungu wako, na kuisikiza sauti yake; ³¹ kwa kuwa Bwana, Mungu wako, ni Mungu wa rehema; hata kukosa wala kukuangamiza, wala hatalisahau agano la baba zako alilowaapia.

4:25 “mkisha kuwa katika nchi siku nyingi ” Hii daima haikuwa ahadi ya mmoja mmoja, lakini ni ahadi ya kundi kwa jamii ambapo wazazi waliwafundisha watoto juu ya Mungu na watoto kuwaheshimu wazazi. Familia imara hutoka katika jamii thabiti (mf, mist. 9, 10, 40 na 5:16,33).

☐ **“mkajiharibu”** KITENZI (BDB 1007, KB 1469, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “kuharibu” au “kuangamiza” na, kwa nyongeza ya stiari, inakuja kurejelea uvunjwaji wa agano (yaani., ibada ya sanamu, kama vile. 4:16,25; 9;12; 31:29).

☐ **“na kumtia hasira”** Tungo hii ni *Hiphil* ya KITENZI JINA HALISI (BDB 494, mf, 32:21; I Fal. 15:30; 16:13). Tena, lugha ya kibinadamu inaelezea majibu ya YHWH kwa dhambi ya mwanadamu! Tazama Mada Maalumu katika 2:15.

4:26 “nawashuhudizia mbingu na nchi hivi leo” Hii ilikuwa ni sehemu ya mikataba ya Wahiti wa Suzerain (kunahitaji ushahidi wa nguvu za kiroho, kama vile Utangulizi wa kitabu, VII). Hivi ni vitu viwili vikuu vya kudumu katika uumbaji wa kimwili. Mara nyingi waliitwa na Mungu kutenda kama mashahidi. Pia inafunua hitaji la muundo wa kisheria wa Israeli wa kuwa na mshahidi wawili katika baraza (kama vile Kut. 35:30; Kumb. 17:6; 19:15). Tungo imetumika mara nyingi katika kuunganisha uthibitisho wa agano na YHWH (kama vile 4:26; 30:19; 31:28).

☐ **“kwamba karibu mtaangamia kabisa juu ya nchi”** Tazama Kumb. 27-29, lakini tambua uwiano wa kitheolojia wa mstr. 31. Bila msaada, mwanadamu aliyeanguka hana tumaini la utiifu wa agano! (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-36).

4:27 “atawatawanya kati ya mataifa” Hii inaonekana kutabiri kufukuziwa mbali kwa watu wa agano na Ashuru (722 K.K.) na Babeli (605, 597, 586, 582 K.K.), ambao ulitabiriwa katika 28:64 na 29:28.

☐ **“mtasalia watu kidogo hesabu yenu”** Hii ni sehemu ya matokeo yanayohusishwa na uvunjaji wa agano. Ni kinyume cha baraka za agano alizoahidiwa Ibrahimu katika Mwa. 15:5.

4:28 “mtatumikia miungu, kazi za mikono ya watu” KITENZI “tumikia” (BDB 712, KB 773, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kimetumika katika maana ya kuabudu au utendaji wa kazi za kiimani:

1. Uhakika wa YHWH - Kut. 3:12; 4:23; Kumb. 6:13; I Sam. 7:3
2. Kuikataa miungu mingine - Kut. 23:33; Kumb. 4:19,28; Yosh. 23:7; Amu. 2:10,19; 10:6,10; I Sam. 22:10; I Fal. 16:31; II Fal. 17:12

Asili hii ya Kiebrania inakuja kama cheo cha heshima cha mtumishi wa YHWH:

1. Mababa wa imani - Kut. 32:13; Kumb. 9:27
2. Kaleb - Hes. 14:24
3. Musa - Kut. 14:31; Hes. 12:7; Kumb. 34:5; I Fal. 8:53
4. Yoshua - Yosh. 24:29
5. Daudi - I Sam. 23:10; 25:39
6. Isaya - Isa. 20:3
7. Masihi - Isaya 53; Zek. 3:8
8. Nebukadreza - Yer. 25:9; 27:6; 43:10
9. Koreshi - Isa. 44:28; 45:1
10. Taifa la Israeli - Isa. 41:8; 44:1-2; 45:4

Rejea katika mist. 26,27,28 unaonyesha tabia ya asili ya ahadi za Mungu (yaani, mstr. 26, YHWH anawatoa nje ya nchi; mst. 27, YHWH anawatawanya katika nchi zingine; mstr. 28, wanaona kuabudu sanamu iliyochongwa kwa mkono) na upumbavu wa kuabudu sanamu!

4:29 “mkimtafuta Bwana” KITENZI (BDB 134, KB 152, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “kumtafuta” kama katika kurejesha uhusiano wa agano na YHWH, uliovunjwa kwa kutokutii. Toba inahitaji msimamo mkuu (yaani, “kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote,” kama vile 26:16; 30:2,10).

Msamaha wa Mungu daima unapatikana kwa toba ya kweli (kama vile mst. 29-31; 30:1-3,10). Toba ya kweli sio huduma ya kutamka, lakini ni imani kamilifu. Toba ni mabadiliko ya mtindo wa maisha, sio mhemuko. Tunaona mifano ya chini, toba ya maisha mafupi katika Hosea 6:1-3 na Yeremia 3:21-25.

Ikiwa watamtafuta, watampata (kama vile Yer. 24:7; 29:13). YHWH sio mgumu kupatikana. Anatarajia watu wake waaksi tabia yake! Tazama Mada Maalumu katika 30:2.

4:30 Musa alitabiri uasi wa Israeli, kama alivyotabiri Yoshua (kama vile Yosh. 24:19-28). Anguko lina uharibifu wa mwanadamu kiroho juu ya uwezo wa kumtii Mungu (kama vile Warumi 1-3; Wagalatia 3).

Tambua kwamba mst. 26 unaonekana kudokeza hukumu ya haraka, mst. 27 unadokeza Ashuru (722 K.K.) na Babeli (605, 597, 586, 582 K.K.) uhamishoni na mst. 30 unaongelea mpangilio wa nyakati za mwisho (“katika siku za mwisho”). Israeli ni lazima iunganike na YHWH kimaagano. Anaweza kutenda haya kwa utiifu wa agano (ambao kitabu cha Warumi 1-3 na Wagalatia 3 vinasema haiwezekani) au anaweza kutenda kwa agano jipya la imani/toba katika Yesu. Waaminio wote wanaomba kwa ajili ya uamusho wa nyakati za mwisho kati ya watu wa Kiyahudi (inawezekana Zek. 12:10 au Warumi 11).

4:31 “Mungu wako, ni Mungu wa rehema” kwa ajili ya majina ya uungu (*El, YHWH, Elohim*) tazama Mada Maalumu katika 1:3.

KIVUMISHI hiki “rehema” (BDB 933) kinamaanisha “huruma” au “rehema.” Ni mojawapo ya sifa kadhaa zilizotumika kumwelezea Mungu wa Israeli. Tazama Mada Maalumu inayofuata.

MADA MAALUM: TABIA ZA MUNGU WA ISRAELI

1. Mwenye huruma (BDB 933, KB 1216) – Kut. 34:6; Kumb. 4:31; 2 Nya. 30:9; Zab. 86:15; 103:8; 111:4; Neh. 9:17,31; Yoel 2:13; Yona. 4:2
2. Mwingi wa fadhili (BDB 337, KB 333) – Kut. 34:6; 2 Nya. 30:9; Zab. 86:15; 103:8; 111:4; Neh. 9:17,31; Yoel 2:13; Yona. 4:2
3. Si mwepesi wa hasira (BDB74 MUUNDO WA MANENO BDB 60) – Kut. 34:6; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17;

Yoel 2:13; Yona. 4:2

4. Amejaa huruma (BDB 912 I MUUNDO WA MANENO BDB 338) – Kut. 34:6-7; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoel 2:13; Yona. 4:2
5. Mwaminifu (au "kweli," BDB 54, angalia Mada Maalum: Kusadiki, Amini, Imani, na Uaminifu katika Agano la Kale) – Kut. 34:6; Kumb. 7:9; Zab. 86:15; Isa. 49:7; Yer. 42:5
6. Mwenye kujaa msamaha (BDB 699, KB 757) – Neh. 9:17
7. Hatawasahau ninyi (BDB 736 I, KB 806) – Neh. 9:17,31
8. Hughairi mabaya (BDB 636, KB 688, *Niphal* ya KAULI ENDELEU + BDB 948) – Yoel 2:13; Yona. 4:2
9. Mungu Mkuu (BDB 42, 152) – Neh. 1:5; 9:32
10. Mungu Mkuu na mwenye kuogofya (BDB 152, 431) – Neh. 1:5; 4:14; 9:32
11. Atunzaye maagano (BDB 1036, 136) – Neh. 1:5; 9:32
12. Mwenye rehema kwa wampendao (BDB 338) – Neh. 1:5; 9:32 (angalia Mada Maalum: Wema (*hesed*))

Haya yote yanaelezea hisia za Mungu dhidi ya watu wake, Israeli. Tabia yake haibadiliki (kama vile Mal. 3:6), kwa hiyo, haya pia yanatumika pia kwa wale wafuasi wake waaminifu (yaani., 2 Kor. 1:3).

☐“hatakukosa wala kukuangamiza, wala hatalisahau agano la baba zako alilowaapia” KunaVITENZI vitatu vinavyokanusha:

1. hatakukosa - BDB 951, KB 1276, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (neni kwa neno “hatakupungukia”), ambacho kinamaanisha kuacha au kutelekeza (kama vile 31:6,8; Yosh. 1:5; 10:6; I Nya. 28:20; Ebr. 13:5)
2. kukuangamiza - BDB 1007, KB 1469, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, ambacho kinamaanisha “kuangamiza,” “kuharibu,” na “maangamizo” (kama vile 9:26; 10:10; Yer. 30:11)
3. hatasahau - BDB 1013, KB 1489, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (kama vile Law. 20:45, tazama Mada Maalumu: Ahadi za maagano kwa mababa wa imani katika 9:5)

Jambo gumu kitheolojia ni kwa namna gani unazichukulia ahadi za Mungu kwa umakini katika kifungu hiki katika uhusiano wa mahitaji ya agano lililopita. Kutoweza kwa Israeli kuyatunza maagano kumenakiliwa katika historia yao na katika maandiko ya Paulo (kama vile Warumi 2-3; Wagalatia 3). Kuhitajika kwa ajili ya “agano jipya,” hakusisitizwi katika matendo ya mwanadamu lakini katika mapenzi ya kiroho na matendo ndio jawabu la Mungu (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38). Mungu kamwe habadiliki, lakini ni kama alivyotenda Israeli! Hitaji la Mungu kwa ajili ya watu wenye haki haliwezi kufaa katika bidii ya mwanadamu au mapenzi! Tunahitaji moyo mpya na roho mpya!

Ni lazima ufanye maamuzi! Agano la kale kutazamishwa kupitia Agano jipya au Agano jipya kutazamishwa kupitia Agano la kale?

Je lengo ni katika Israeli au ulimwenguni? Je ni jambo la imani au mashindano? Ikiwa kuna “waliotengwa” katika mpango wa ukombozi wa milele wa Mungu, je sio kanisa (yaani, mgawanyo), lakini Israeli!

MADA MAALUMU: UTABIRI WA BAADAE WA AGANO LA KALE DHIDI YA UTABIRI WA AGANO JIPYA ("UTANGULIZI WA MUHIMU" WA UFUNUO)

Katika miaka ya masomo yangu ya elimu juu ya siku za mwisho wa nchi nimegundua kwamba Wakristo wengi hawana au hawapendi mtiririko, ulioboreshwa, ulioendelea unaoonesha nyakati za mwisho. Kuna Wakristo wenye mlengo mkubwa wa eneo hili la Ukristo kwa ajili ya theolojia, saikolojia, au sababu ya kimadhehebu. Wakristo hawa wanaonekana kusumbuliwa sana na namna gani jambo hili litaisha, na kwa namna fulani kukosa ule umaana wa Injili! Waamini hawawezi kuathiri ajenda ya Mungu juu ya mwisho wa nchi, lakini wanaweza kushiriki katika mamlaka ya Injili (rejea Mathayo. 28:19-20; Luka 24:46-47; Matendo ya Mitume 1:8). Waamini wengi wanakiri kuja kwa mara ya Pili kwa Kristo na kule kutimilizwa kwa mwisho kwa ahadi za Mungu. Tatizo la kiutafsiri linainuka kutoka katika namna ya kuelewa kutimilizwa huku kutoka katika utata kadhaa wa kibiblia Mvutano kati ya mifano ya kinabii ya Agano la Kale na mifano Mipya ya Kitume ya Agano jipya.

1. Mvutano kati ya Uungu mmoja wa Biblia (Mungu mmoja kwa ajili ya wote) na kuchaguliwa kwa Israeli (watu maalumu)

2. Mvutano baina ya kipengele cha sharti cha agano na ahadi za kibiblia (“ikiwa...basi”) na uaminifu usio na masharti wa Mungu kwa ukombozi wa binadamu aliyeanguka
3. Mvutano kati ya aina ya uandishi wa Mashariki ya Karibu na mifano ya uandishi wa kimagharibi
4. Mvutano kati ya Ufalme wa Mungu wa sasa na ujao.
5. Mvutano kati ya imani katika kurudi kwa Kristo na imani kwamba matukio kadhaa lazima yatokee kwanza.

Naomba tujadili mivutano hii moja baada ya nyingine.

MVUTANO WA KWANZA (Agano la Kale, kabila, utaifa na kipengele cha jiografia dhidi ya waamini wote dunia nzima). Manabii wa Agano la Kale walitabiri juu ya urejesho wa Ufalme wa Kiyahudi katika Palestina iliyo katikati ya Yerusalemu ambapo mataifa yote ya dunia yatakusanyika kumsifu na kuutumikia utawala wa Daudi, lakini si Yesu wala Mtume yoyote wa Agano jipya aliwahi kuweka msisitizo katika ajenda hii. Si uvuvio wa Agano la Kale (rejea Mathayo 5:17-19)? Je waandishi wa agano jipya wameondoa sehemu matukio muhimu yanyakati za mwisho?

Kuna vyanzo kadhaa vya taarifa kuhusu mwisho wa ulimwengu.

1. Manabii wa Agano la Kale (Isaya, Mika, Malaki)
2. Waandishi wa mambo ya mwisho wa nchi wa Agano la Kale (rejea Ezekieli 37-39; Daniel 7-12; Zakaria)
3. Waandishi wa kati ya maagano, waandishi wayahudi wa siku za mwisho wasio wakanoni (kama I Enoch kinachosemekana kilitakiwa kifuata baada ya Yuda)
4. Yesu mwenyewe (rejea Mathayo 24; Marko 13; luka 21)
5. Nyaraka za Paulo (rejea 1 Wakorintho 15; 2 Wakorintho 5; 1 Wathesalonike 4-5; 2 Wathesalonike 2)
6. Nyaraka za Yohana (1 Yohana na Ufunuo)

Je haya yote yanatufundisha kwa hakika ajenda ya mwisho wa nchi (matukio, mfululizo, watu)? Kama sio kwanini? Je si yote kuwa yamevuviwa (isipokuwa maandishi ya kati ya maagano ya Kiyahudi). Roho alifunua ukweli kwa waandishi wa Agano la Kale kwa namna na sehemu ambayo wangeelewa. Hata hivyo, kupitia ufunuo endelevu roho alipanua dhana hii ya Agano la Kale juu ya siku za mwisho wanachi katika namna pana (“maajabu ya Kristo,” rejea Waefeso 2: 11-3:13). Ifuatayo ni baadhi ya mifano inayoendana:

1. Jiji la Yerusalemu katika Agano la Kale imetumika kama ulinganifu kwa watu wa Mungu (Sayuni), lakini inatajwa katika Agano Jipya kama neno linaloelezea kupokelewa na Mungu kwa watubuo wote, wanadamu waaminio (“Yerusalemu Mpya” ya Ufunuo 21-22). Maana kubwa zaidi ya kithiolojia iliyokuzwa ya jiji linavyoonekana kuwa watu wapya wa Mungu (Wayahudi waaminio na Mataifa) inatajwa kwa mbele katika ahadi za Mungu kukomboa binadamu aliyeanguka katika Mwanzo 3:15, kabla hata hapajawa na Muiyahudi yoyote au Mji mkuu wa Kiyahudi. Hata wito wa Ibrahimu (rejea 12:1-3) ulihusisha mataifa (rejea Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5) angalia Mada Maalumu: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH.
2. Katika Agano la Kale, maadui wa watu wa Mungu ni mataifa yaliyozunguka Mashariki ya karibu, lakini katika Agano Jipya wamekuza kwa wasioamini wote, wampingao Mungu, watu wenye uvuvio wa kishetani. Vita imehamishwa kutoka kijiografia, migogoro ya kikanda kwenda ulimwenguni kote, mgogoro wa kiulimwengu (rejea Wakolosai).
3. Ahadi ya ardhi ambayo ni sehemu ya Agano la Kale (ahadi ya Mwanzo, rejea 12:7 13:15; 15:7,15, 16; 7:8) sasa imekuwa dunia nzima. Yerusalemu mpya inashuka chini kwa nchi iliyumbwa tena, sio Mashariki ya Karibu tu au kinginecho (rejea Ufunuo 21-22).
4. Baadhi ya mifano mingine ya dhana za kinabii ya Agano la Kale inayokuzwa
 - a. Mbegu ya Ibrahimu sasa imetahiriwa kiroho (Warumi 2:28-29)
 - b. (rejea Hosea 1:10; 2:23, ikinukuliwa kutoka Warumi 9:24-26; pia Walawi. 26:12; Kutoka 29:45, imenukuliwa kutoka 2 Wakorintho 6:16-18 and Kutoka 19:5; Kumbukumbu la torati 14:2, imenukuliwa katika Tito 2:14)
 - c. Hekalu sasa ni Yesu (rejea Mathayo 26:61; 27:40; Yohana 2:19-21) na kupitia yeye kanisa la nyumbani

(rejea 1 Wakorintho 3:16) au kwa mwamini mmoja mmoja (rejea 1 Wakorintho 6:19)

- d. Hata Israel na tabia za zinazofunua maneno ya Agano la Kale sasa zinamaanisha watu wote wa Mungu (kama vile "Israeli," rejea Warumi 9:6;Wagalatia 6:16, kama "Ufalme wa Makuhani," rejea 1 Petro 2:5, 9-10; Ufunuo 1:6)

Mifano ya kinabii imekuwa ikitimizwa, ikikuzwa, na sasa ikujumuisha. Yesu na waandishi wa Kitume hawawasilishi nyakati za mwisho kama ile ya manabii wa Agano la Kale (rejea Martin Wyngaarden, *The Future of The Kingdom in Prophecy and Fulfillment*) watafsiri wa kisasa wanaojaribu kutengeneza mifano ya Agano la Kale au kugeuza kimaarifa ya kitabu cha Ufunuo kwenda katika kitabu cha Kiyahudi na kulazimisha maana isiyoelweka, yenye utata kauli za Yesu na Paulo! Waandishi wa Agano Jipya hawawakatai manabii wa Agano la Kale, lakini huonesha kilele cha walichomaanisha kwa ujumla. Hakuna mfumo uliopangwa katika mwisho wan chi kunakozungumzwa na Yesu au Paulo. Kusudi lao kimsingi kabisa ni kiukombozi au kichungaji.

Hata hivyo ndani ya Agano Jipya kuna mvutano. Hakuna mfumo rasmi wa wazi wa matukio ya siku za mwisho. Katika namna nyingi kwa mshangao mkubwa Ufunuo unatumia dhana za Agano la Kale katika kuelezea mwisho badala ya mafundisho ya Yesu (rejea Mathayo 24; Marko 13)! Inafuata namna ya uandishi ulioanzishwa na Ezekieli, Danieli, na Zakaria, lakini ilikua wakati wa kati ya Agano la Kwanza na Jipya (fasihi ya Kiyahudi ya nyakati za mwisho wa nchi). Hii ilikuwa najia ya Yohana ya kuunganisha Agano la Kale na Jipya. Inatazama taratibu za nyakati za kale ya uasi wa mwanadamu na kujithatiti kwa Mungu katika ukombozi! Lakini hata hivyo lazima izingatiwe kwamba ingawa Ufunuo unatumia lugha ya Agano la Kale, watu na matukio, inayatafsiri katika ufahamu wa karne ya kwanza ya Rumi(rejea Ufunuo 17).

MVUTANO WA PILI (Hali ya uwepo wa Mungu mmoja dhidi ya watu wateule)

Msisitizo wa Kibiblia upo kwa my mmoja, roho, muunmbaji-mkombozi, Mungu(rejea Kutoka 8:10; Isaya 44:24; 45:5-7,14,18,21-22; 46:9; Yereimia 10:6-7). Upekee wa Agano la Kale katika siku zake lenyewe ilikuwa ni hali ya Mungu mmoja. Mataifa yote yazungukayoyalikuwa yakiabudu miungu mingi. Umoja wa Mungu ndio moyo wa Ufunuo wa Agano la Kale (rejea Kumbukumbu la Torati 6:4) uumbaji ni eneo kwa ajili ya kusudi la ushirika kati ya Mungu na mwanadamu, aliyembwa kwa sura na mfano wake(rejea Mwanzo 1:26-27). Hata hivyo, mwanadamu aliasi, atatenda dhambi dhidi ya upendo wa Mungu, uongozi, na kusudi (rejea Mwanzo 3). Upendo wa Mungu na kusudi lilikuwa kubwa sana na hakika kuwa alihaidi kukomboza uanadamu ulioanguka (rejea Mwanzo 3:15)!

Mvutano unaanza pale Mungu anapochagua kumtumia mtu mmoja, familia moja, taifa moja kufikia wanadamu wengineo. Uchaguzi wa Mungu wa Ibrahimu (Mwanzo 12; 15; 17; 18) na Wayahudi kama ufalme wa Makuhani (rejea Kutoka 19:4-6) ulisababisha kiburi badala ya huduma, kubaguana badala ya kujumuika kwa pamoja. Wito wa Mungu kwa Ibrahimu ulijumuisha kusudio la kubariki wanadamu wote (Mwanzo 12:3). Lazima ikukmbukwe na isisitizwe kwamba kuchaguliwa kwa Agano la Kale ilikuwa ni huduma, sio wokovu. Waisraeli wote hawakuwa sawa machoni pa Mungu, kamwe si kuokolewa kwa msingi wa haki ya uzaliwa (rejea Yohana 8:31-59; Mathayo 3:9), lakini kwa imani binafsi na utii (Mwanzo. 15:6, imenukuliwa kutoka Warumi. 4:3,9,22; Wagalatia 3:6). Israeli ilipoteza kusudi lake (kanisa kwa sasa ndio ufalme wa makuhani, rejea Ufunuo 1:6; 1Petro 2:5,9) na kugeuza mamlaka katika neema, huduma katika msimamo maalumu! Mungu alichagua mmoja kuchagua wote!

MVUTANO WA TATU (maagano yenye masharti dhidi ya maagano yasiyo na masharti)

Kuna mvutano wa kithiolojia au kugawanyika kati ya maagano yasiyo na masharti na yenye masharti. Ni kweli hakika kabisa kuwa kusudi/mpango wa ukombozi wa Mungu si wa masharti (rejea Mwanzo 15:12-21). Hata hivyo, mwitikio wa kimamlaka wa mwanadamu siku zote huwa ni wa masharti! Ule utaratibu wa "iwapo...ndipo" inaonekana katika vitabu vyote Agano la Kale na Agano Jipya. Mungu ni mwaminifu; mwanadamu si mwaminifu. Mvutano huu umesababisha hali ya kutoelewana isiyo ya kawaida. Watafsiri wamejifanya kuegemea upande mmoja tu "pembe ya kutoelewa vizuri," uaminifu wa Mungu au juhudi za mwanadamu, Ukuu wa Mungu au utashi huru wa mwanadamu. Zote ni za Kibiblia na muhimu.

Hii inahusiana na siku za mwisho wa nchi, kwenda kwenye ahadi za Mungu za Agano la Kale kwa Waisraeli. Iwapo Mungu alihaidi, basi hiyo inatoshia! Mungu anafanya kazi kwa ahadi zake; heshima yake huusika (rejea Ezekieli 36:22-38). Maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti hukutana na Kristo (rejea Isaya 53), sio Israeli! Kilele cha uaminifu wa Mungu kiko katika wa ukombozi wa wote watakao tubu na kuamini, si kwa kigezo cha nani alikuwa baba yako au mama yako! Kristo, sio Israeli ndio msingi wa Maagano yote ya Mungu na ahadi. Kama kuna sehemu ya mabano katika thiolojia katika Biblia, sio Kanisa, bali Israeli (Matendo ya Mitume 7 na Wagalatia 3).

Kusudi la ulimwengu la kutangaza Injili limekabidhiwa kwa Kanisa (rejea. Mathayo 28:19-20; Luka 24:47; Matendo ya Mitume 1:8). Hili ni sharti na kiagano! Hii haimaanishi Mungu amewakataa kabisa Wayahudi (rejea Warumi 9-11). Kunawezekana kukawa na sehemu na kusudi kwa ajili ya siku za Mwisho, kuamini kwa Israeli (rejea Zakaria 12:10)

MVUTANO WA NNE (mifano ya kiuandishi ya Mashariki ya karibu dhidi ya ile ya Kimagharibi)

Aina ya uandishi ni kipengele muhimu sana katika kuitafsiri Biblia kwa usahihi (angalia Fee and Stuart, *How To Read the Bible For All Its Worth*). Kanisa lilikua katika mazingira ya kiutamaduni wa kimagharibi (Kigiriki). Fasihi ya Mashariki ina mafumbo mengi sana zaidi, inatumia ulinganifu wa vitu visivyofanana, na yenye ishara kuliko ya kisasa, mifano ya utamaduni wa Kimagharibi. Inaweka mkazo kwa watu, makabiliano, na matukio zaidi ya ukweli kamili unaopendekezwa. Wakristo wamekuwa katika hukumu ya kutumia historia yao wenyewe na mifano ya kiunadishi kutafsiri unabii wa Kibiblia (yote Agano la Kale na Agano Jipya). Kila kizazi na ujumla ya kijiografia umetumia desturi, historian a ukawaida kutafsiri Ufunuo. Kila mmoja wao alikosea! Ni majivuno kufikiria kuwa desturi ya kimagharibi ndio mahali pa kuanzia pa unabii wa kibiblia.

Aina ya uandishi ambayo kwa asili, imevuviwa mwandishi kuchagua kuitumia kuandika ni mkataba na msomaji (Bruce Corley). Kitabu cha Ufunuo sio hadithi ya Kihistoria. Ni mkusanyiko wa barua (Sura ya 1-3), unabii, na zaidi sana maandishi yanayozungumza juu ya mwisho wa nchi. Ni makosa kuifanya Biblia iseme zaidi ya kilichokusudiwa na mwandishi wa asili ambayo ni sawa na kuifanya iseme chini ya yale yaliyokuwa yamekusudiwa! Majivuno wa Watafsiri na misingi yao ya kiimani si ya kuweka kabisa katika kitabu kama cha Ufunuo.

Kanisa halijawahi kukubaliana kuhusu tafsiri sahihi ya Ufunuo. Ninachotamani ni kusikia na kujishughulisha na biblia nzima, si vijishehemu tu. Ufahamu wa Biblia wa Kimashariki unawasilisha ukweli katika namna za safu za mivutano. Hali yetu ya Kimagharibi kuelekea ukweli unaopendekezwa sio kwamba haufai, bali hauna ulali wa usawa! Nafikiri inawezekana saa nyingine kuondoa angalau baadhi ya vifuniko katika kutafsiri Ufunuo kwa kuzingatia kusudi la kubadilika kwake kwenda kwa vizazi vinavyofuata vya waaminio. Ni wazi kwamba watafsiri wengi kuwa Ufunuo lazima utafsiriwe katika ufahamu wa siku zake na aina ya uandishi wake. Namna ya kihistoria ya kuelezea Ufunuo lazima izingatie nini wasomaji wa kwanza wangekuwa nacho, na wangeelewa. Kwa namna nyingi watafsiri wa kisasa wamepoteza maana ya ishara nyingi za kitabu. Lengo la kwanza la Ufunuo ilikuwa ni kuwatia moyo waamini wanaopitia dhiki. Inaonesha namna Mungu anavyoshughulikia Historia (kama alivyofanya kwa manabii wa Agano la Kale); ilikubali kuwa historia inaelekea kwenye muda ulioteuliwa, hukumu au Baraka (kama ilivyokuwa kwa Manabii wa Agano la Kale). Ilikubalika katika namna ya karne ya kwanza ya kiyahudi ya siku za mwisho za upendo wa Mungu, uwepo, nguvu na ukuu.

Inafanya kazi kwa namna hiyohiyo kithiolojia kwa kila kizazi cha waaminio. Inaelezea mapambano ya kiulimwengu ya wema na uovu. Maelezo ya karne ya kwanza yanaweza yakawa yalitupoteza, lakini si kweli zenye nguvu na zifarijizo. Pale watafsiri wa kisasa wa kimagharibi wanapojaribu kulazimisha maelezo ya Ufunuo kwenda kwenye historia yao ya sasa, utaratibu wa tafsiri za uongo huendelea!

Inawezekana kwamba maelezo ya kitabu yanaweza yakarudi kwa kasi kuwa kawaida (kama ilivyokuwa Agano la Kale ikilinganisha kuzaliwa, maisha na kifo cha Kristo) kwa kizazi cha mwisho cha waaminio wanapokabiliana na kutishiwa kifo na kiongozi mpinga Mungu (rejea 2 Wathesalonike 2) na desturi. Hakuna anayefahamu kutimilizwa kwa kawaida kwa Ufunuo mpaka maneno ya Yesu (rejea. Mathayo 24; Marko 13; and Luka 21) na Paulo (rejea. 1 Wakorintho 15; 1 Wathesalonike 4-5; na 2 Wathesalonike 2) pia yatapokuwa halisi kihistoria. Kubashiri, kubuni buni na kukaa katika imani za kidhebehu si sawa. Fasihi ya mwisho wa nchi inaruhusu huku kubadilika. Mshukuru Mungu kwa ajili ya taswira na ishara zinazopita hadithi za kihistoria! Mungu yupo kazini; Yeye anatalawa; Anakuja!

Watoa maoni wengi wa kisasa wanakosa sehemu muhimu ya aina hii ya uandishi! Watafsiri wa kimagharibi wa Kisasa mara nyingi hutafuta mtiririko mzuri wa kueleweka wa kithiolojia badala ya kuwa sawa na utata, ishara na aina ya uandishi ya kitamthiliya ya Kiyahudi ya fasihi ya siku za mwisho. Kweli hii inaelezwa vizuri na Ralph P. Martin katika makala yake, "Approaches to New Testament Exegesis," katika kitabu *New Testament Interpretation*, kilichohaririwa na I. Howard Marshall:

Mpaka tutakapotambua ubora wa kitamthiliya wa maandiko haya na kurejea katika namna ambayo lugha inavyotumika kama njia ya kuelezea ukweli wa kidini, tutakosea sana katika kufahamu mambo ya siku za mwisho, na kimakosa tunajaribu kutafsiri maono yake kama vile sasa noo kitabu cha mabo ya kawaida tu na chenye lengo la kufunua matukio yanayojulikana na historia yenye taarifa. Kujaribu kufanya jambo hili la mwisho ni kuingia katika kila namna ya matatizo ya kiutafsiri. Na zaidi sana inapelekea upotevu wa maana muhimu ya siku za mwisho na hivyo kupotea thamani kubwa ya ukuu wa Mungu katika sehemu ya Agano jipya kama tamko la Kitamthiliya katika lugha ya kishairi ya uungu ya Uungu wa Mungu na Kristo na mgongano wa utawala wake unaochanganya ukuu na upendo (Ufunuo 5:5,6; the Lion is the Lamb)" (ukurasa wa 235).

. Randolph Tate katika kitabu chake cha *Biblical Interpretations* (Tafsiri za Kibiblia):

Hakuna aina ya uandishi mwingine wa Biblia iliyosomwa kwa dhati sana kwa matokeo yanatokatisha tama kama vitabu vinavyoongelea mwisho wan chi kama vitabu vya Danieli na Ufunuo. Aina hii ya uandishi ilidhoofika kutokana na historia mbovu ya tafsiri zisizo sahihi kutokana na kukosa uelewa wa msingi wa aina yake ya kifasihi, muundo na kusudi. Kwasababu ya tamko hilo kufunua kile kinachotakiwa kutokea kwa muda mfupi, siku za mwisho zimekuwa zikichukuliwa kama ramani ya njia na mpango wa siku zijazo. Kosa baya ya kuchukuliwa huku ni ile dhana kwamba namna ya rejea ya vitabu iko katika nyakati anazoishi msomaji wa wakati huo badala ya wakati anaishi mwandishi. Kwenda kwa namna hii kwa bila muongozo kwa siku za mwisho (haswa Ufunuo) inazifanya kazi kana kwamba ni lugha ya siri au fumbo ambalo matukio ya sasa yanaweza kutumiak kutafsiri ishara za maandiko. Kwanza, mtafsiri lazima atambue kwamba vitabu vya siku za mwisho vinawasilisha ujumbe wake kupitia viwakilishi vya kiishara. Kutafsiri viwakilishi kikawaida wakati inalinganisha vitu ni kukosea katika kutafsiri. Jambo kubwa sio kama matukio katika siku za mwisho ni ya kihistoria. Matukio yanaweza yakawa ya kihistoria; yanaweza yakawa kuwa yalitokea, au yatatokea lakini mwandishi anawasilisha matukio na anazungumza maana kupitia taswira na namna hizo" (ukurasa wa 137).

Kutoka katika *Dictionary of Biblical Imagery*, edited by Ryken, Wilhost and Longman III:

"waasomaji wa leo mara nyingi wamefumbwa na wanachanganyikiwa na aina hii ya uandishi. Taswira isiyotarajiwa na mambo yaliyo nje ya ulimwengu huu yanaleta giza na kutoka nje katika maandiko mengi. Ukichukulia maandiko haya kwa thamani ya usoni inawaacha wasomaji wengi wakihangaika kutafuta kujua 'itatokea nini iwapo,' kwahiyo kupoteza lengo la ujumbe wa siku za mwisho" (ukurasa wa 35)

MVUTANO WA TANO (ufalme wa Mungu kwa sasa na baadaye)

Ufalme wa Mungu ni sasa, na baadaye. Hali hii ya mtafaruku wa kithiolojia inalengwa katika siku za mwisho wa nchi. Kama hakuna anayetegemea kutimilizwa kwa nabii zote za Agano la Kale kwa Waisraeli hivyo Ufalme unakuwa haswa kurejeshwa kwa Israeli katika eneo lao la Kijiografia na kuheshimiwa kabla kwa thiolojia! Hii ingesababisha kuwa kanisa lingekuwa limetwaliwa katika Sura ya 5 na Sura zinazobaki zihusiane na Israeli (ila zingatia Ufunuo 22:16).

Hata hivyo kama lengo ilikuwa katika ufalme kuanzishwa na Mesiya aliyahaidiwa na Agano la Kale, halafu ipo na kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza, na alafu lengo linakuwa kuwa hai tena, maisha, mafundisho, mauti, na ufufuo wa Kristo. Mkazo wa kithiolojia upo katika wokovu wa sasa. Ufalme umekuja, Agano la Kale linatimilizwa kwa Kristo kujitoka kwa jili ya wokovu kwa wote, siyo Yeye kutawala milele juu ya wengine!

Ni kweli ya uhakika kuwa Biblia inazungumzia kuja kote kuwili kwa Kristo, lakini msisitizo unawekwa wapi zaidi? Inaonekana kwangu kwamba unabii mwingi wa Agano la Kale linalenga kwenya kuja kwa mara ya kwanza,

kuanzishwa kwa ufalme wa kimasiya (rejea Daniel 2). Katika Agano la Kale mkazo upo kwenye kutawala milele kwa Mungu, na namna ya kushihirishwa huko kwa utawala ni huduma ya Masiya (rejea 1 Wakorintho 15:25-27). Sio swali la kipi ni kweli; yote ni kweli, lakini mkazo upo wapi? Lazima isemwe kwamba baadhi ya Watafsiri wanajikita sana kwenye kutawala milele kwa Masiya (rejea ufahamu wa kumuktadha kwenye Ufunuo 20) kwamba wamepoteza shabaha ya kibiblia kwenye kutawala milele kwa Baba. Kutawala kwa Kristo ni tukio la utangulizi. Kuja kwa Kristo kote hakukuwa wazi katika Agano la Kale, wala kutawala kwa muda kwa Masiya! Msingi wa kuhubiri kwa Yesu na kufundisha ni ufalme wa Mungu. Ni vyote (wokovu na huduma), na baadae (katika kuendelea na nguvu). Ufunuo kama shabaha yake ni utawala wa kimelenia wa Masiya (rejea Ufunuo 20), ni utangulizi, sio kilele (Ufunuo 21-22). Haiku wazi katika Agano la Kale kwamba utawala wa Muda ni muhimu; kwa kusema kweli, kutawala kwa Masiya kwa Danieli 7 ni milele, si kwa kwa millennia.

MVUTANO WA SITA (kurudi kwa Kristo kunakotarajiwa dhidi ya kuchelewa kurudi mara ya pili)

Waaminio wengi wamefundishwa kwamba Yesu anakuja hivi karibuni, punde na bila kutegemea (rejea.

Mathayo 10:23; 24:27,34,44; Marko 9:1; 13:30; Ufunuo 1:1,3; 2:16; 3:11; 22:7,10,12,20; Lakini kila kizazi kilichotegemea kilikuwa kimekosea! Uharaka (mapema) wa kuja kwa Yesu ahadi yenye nguvu ya tumaini la kila kizazi, lakini uhalisia ni kwa mmoja (na huyo ni Yule apitiaye dhiki). Waaminio laziima waishi kama vile Anakuja kesho, lakini waweke mipango na kufanyia kazi Agizo Kuu (rejea Mathayo 28:19-20) kama akikawia. Baadhi ya vifungu katika Injili na Wathesalonike wa 1 na 2 yamejikita kwenye kukawia kwa Kuja kwa Mara ya Pili (Parousia). Kuna matukio ya kihistoria ambayo lazima yatimie kwanza;

1. Kuhubiriwa kwa ulimwengu wote(rejea Mathayo 24:14; Marko 13:10)
2. Kufunuliwa kwa “mwanadamu mwenye dhambi” (rejea Mathayo 24:15; 2 Wathesalonike 2; Ufunuo 13)
3. Dhiki kuu (Mathayo 24:21,24; Ufunuo 13)

Kuna utata wa kimakusudi (rejea Mathayo 24:42-51; Marko 13:32-36)! Ishi kila siku kama vile ndiyo siku yako ya mwisho ila panga na pata mafunzo kwa ajili ya huduma ya baadaye!

MWENDELEZO NA UWIANO

Lazima isemwe kwamba shule tofauti tofauti za fasiri kuhusu siku za mwisho zote zina ukweli usio kamili. Wanaelezea na kufasiri vizuri baadhi ya maandiko. Tatizo liko kwenye mwendelezo na uwiano. Mara kwa mara kuna mpangilio wa kauli za kupendekeza ambazo zinatimia maandiko ya kibiblia kujaza mapungufu ya kithiolojia ya kabla. Biblia haifunui mantiki, mtitiriko wa matukio na mfumo wa siku za mwisho. Iko kama albamu ya familia. Picha ni za kweli lakini siku zote hazipo katika mpangilio, katika muktadha na katika mfuatano wa kimantiki. Baadhi ya picha zimeondolewa kutoka kwenye albamu na vizazi vya baadaye vya ndugu wa familia havijui kwa hakika namna ya kuzirudisha. Msingi wa fasiri sahihi wa Ufunuo ni kusudio la mwandishi wa asili kama alivyofunuliwa katika uchaguzi wake wa aina ya fasihi anayoitumia. Wafasiri wengi wanajaribu kubeba zana za kiufafanuzi na taratibu kutoka kwenye aina zingine za uwasilishaji wa Agano Jipya kwenda kwenye ufasiri wao wa Ufunuo. Wanaweka shabaha kwenye Agano la Kale badala ya kuruhusu mafundisho ya Yesu na Paulo kupangilia muundo wa kithiolojia na kuruhusu Ufunuo kufanya kazi kama kielelezo.

Lazima nikiri kwamba naikabili fasiri hii juu ya Ufunuo nikiwa na baadhi ya uoga na wasiwasi si kwasababu ya laana ya Ufunuo 22:18-19, bali ni kwasababu ya kiwango cha mkanganyiko wa ufasiri wa kitabu hiki uliosababishwa na kuendelea kusababishwa kati ya watu wa Mungu. Napenda Ufunuo wa Mungu. Ni wa kweli wakati wanadamu wote wanakuwa waongo (kama vile Rum. 3:4)! Tafadhali tumia fasiri hii kama jaribio la kuamsha mawazo na sio kutoa maana ya mwisho kama kielekezi na sio mwongozo, kama “vipi ikiwa,” na sio “hivyo Bwana asema.” Nimekabilia uso kwa uso na mapungufu yangu mwenyewe, kiupendeleo ya ajenda za kithiolojia. Lakini pia nimeyaona yale ya wafasiri wengine. Kiwastani kuonekana kwamba watu wanatafta Ufunuo wa kile wanachotegemea kukipata. Aina ya uwasilishaji unajipeleka wenyewe katika matumizi mabaya!

Hata hivyo lipo katika Biblia kwa makusudi fulani. Imewekwaji wake kama “neni” la hitimisho sio wa bahati mbaya. Lina ujumbe kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watoto wake wa kila kizazi. Mungu anataka tuelewe! Tuungane pamoja, wala tusitengeneze magenge; Ebu tuthibitisha kile kilicho wazi na kilicho cha msingi, sio yale yote yanayoweza, yataweza au yangeweza kuwa kweli. Mungu atusaidie sisi sote!

ANDIKO NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4:32-40

³² Maana uliza sasa siku zilizopita, zilizokuwa kabla yako, tangu siku ile Mungu aliyoumba mwanadamu juu ya nchi, na toka pembe hii ya mbingu hata pembe hii, kwamba kumetukia neno lo lote kama neno hili kubwa, au kwamba kumesikiwa habari ya neno kama hili? ³³ Je! Watu wakati wo wote wameisikia sauti ya Mungu ikinena toka kati ya moto, kama wewe ulivyosikia, wasife? ³⁴ Au Mungu amekwenda wakati gani akajitwalia taifa toka kati ya taifa lingine, kwa majaribu, na kwa ishara, na kwa maajabu, na kwa vita, na kwa mkono hodari, na kwa mkono ulionyoshwa, na kwa maogofya makuu, kama vile Bwana, Mungu wenu, alivyowatendea ninyi katika Misri, mbele ya macho yenu? ³⁵ Wewe umeonyeshwa haya, ili upate kujua ya kuwa Bwana ndiye Mungu, hapana mwingine ila yeye. ³⁶ Kutoka mbinguni amekusikizisha sauti yake, ili akufundishe; na juu ya nchi alikuonyesha moto wake mkuu; ukasikia maneno yake toka kati ya moto. ³⁷ Na kwa sababu aliwapenda baba zenu, kwa sababu hiyo aliwachagua wazao wao baada yao, akakutoa katika Misri kwa kuwako pamoja nawe, kwa uweza wake mwingi, ³⁸ ili kufukuza mbele yako mataifa, walio wakubwa, wenye nguvu kukupita wewe, ili kukuingiza, na kukupa nchi yao iwe urithi, kama ilivyo leo. ³⁹ Kwa hiyo ujue, leo hivi, ukaweke moyoni mwako, ya kuwa Bwana ndiye Mungu katika mbingu juu, na katika nchi chini; hapana mwingine. ⁴⁰ Basi, zishike sheria zake, na amri zake, ninazokuamuru leo, upate kufanikiwa, wewe na watoto wako baada yako, na siku zako ziwe nyingi katika nchi ile akupayo Bwana, Mungu wako, milele.

4:32 “uliza” KITENZI hiki (BDB 981, KB 1371, *Qal* KAULI SHURUTISHI) kinamaanisha Mungu kuuliza juu ya upekee wa uhusiano wa Israeli kwa uungu (kama vile mist. 32-40).

☐ **“tangu siku ile Mungu aliyoumba mwanadamu juu ya nchi”** Hii inarejelea katika Mwanzo 1-2; pia tazama Zaburi 104.

4:34 “kwa mkono hodari, na kwa mkono ulionyoshwa ” Hizi ni Nahau za kibinadamu (tazama Mada Maalumu katika 2:15) zimetumika kuelezea nguvu za ukombozi za YHWH kwa niaba ya Israeli (kama vile 5:15; 6:21; 7:19; 9:29; 11:2; 26:8). Katika baadhi ya maandiko tungo zimefupishwa kwa “mkono wenye nguvu” (kama vile 3:24; 6:21; 7:8; 9:26; Yosh. 4:24) au “mkono ulionyooka” (kama vile 9:29; Kut. 6:6). Maneno haya ya kinahau yana mfanano maalumu katika maandiko ya Kimisri yanayomsimulia “mfalme” (NIDOTTE, juzuu 3, uk. 92).

4:35 “ili upate kujua ” Miujiza ya mstr. 34 ilikuwa kwa makusudi ya kuimalisha imani ya Israeli (kama vile. Kut. 7:5,17; 10:2; 31:13). Kwa ajili ya neno “kujua” (BDB 393, KB 390, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO) tazama Mada Maalumu inayofuata.

MADA MAALUMU: KUJUA (hasa ikitumia zaidi Kumbukumbu la Torati kama kielelezo)

1. Kutambua mazuri na mabaya- Mwa. 3:22; Kumb. 1:39; Isa. 7:14-15; Yona 4:11
2. Kutambua kwa kuelewa - Kumbu. 9:2,3,6; 18:21
3. Kutambua kwa uzoefu - Kumb. 3:19; 4:35; 8:2,3,5; 11:2; 20:20; 31:13; Jos. 23:14
4. Kufikiria - Kumbu. 4:39; 11:2; 29:16
5. Kutambua wewe mwenyewe
 - a. Mtu - Mwa. 29:5; Kuto. 1:8; Kumb. 22:2; 33:9; Yer. 1:5
 - b. miungu- Kumb. 11:28; 13:2,6,13; 28:64; 29:26; 32:17
 - c. YHWH- Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
 - d. Kijinsia - Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
6. Ujuzi au maarifa ya kufundishwa - Isa. 29:11,12; Amosi 5:16
7. Kuwa mwelevu- Kumb. 29:4; Mith. 1:2; 4:1; Isa. 29:24
8. Maarifa ya Mungu
 - a. Juu ya Musa-Kumb.34:10
 - b. Juu ya Israel-Kumb.31:21

Kithiolojia #5 ni wa muhimu. Imani ya Biblia ni ushirika wa ndani, unaokuwa, wa ndani pamoja na Mungu (angalia Mada Maalumu: koinōnia). Sio kanuni za imani au maisha pekee ya kiadilifu. Ni uhusiano binafsi wa imani. Hii ndio sababu ya Paulo kuitumia nyumba ya mkristo katika Efe. 5:22-6:9 kuelezea upendo wa Kristo kwa ajili ya kanisa

☐ **“Bwana ndiye Mungu”** Tazama Mada Maalumu: Majina ya Uungu katika 1:3.

☐ **“hapana mwingine ila yeye”** Hakuna roho nyingine au mungu mfano wa YHWH (mf, mst. 39; 6:4; 32:39). Tazama muhtasari kamili katika 6:4.

4:36 “Kutoka mbinguni amekusikizisha sauti yake” Kifungu hiki kinarejelea YHWH kujifunua kimwili katika uwepo wake kwenye Mlima Herobu/Sinai, imeandikwa katika Kutoka 19.

4:37 “Na kwa sababu aliwapenda baba zenu” Hii inarejelea uchaguzi wa Mungu kwa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo (mababa wa imani katika Mwanzo 12-50, kama vile 7:7-8; 10:15).

☐ **“aliwachagua”** Uchaguzi (yaani, “chagua” BDB 103, KB 119, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) katika Agano la Kale ni kwa ajili ya huduma (mf, Koreshi, Isa. 44:24-45:7), sio wokovu kama katika Agano Jipya.

☐ **“akakutoa katika Misri kwa kuwako pamoja nawe”** Neno “pamoja” (BDB 815) kiuhalisia ni “uso,” ambalo linadokeza uwepo wa Mungu (kama vile. 5:4; Mwa. 32:30; Kut. 33:14-15; Isa. 63:9, “uwepo wa malaika wake”). Hii pia ni sababu baada ya neno “uso kwa uso” (kama vile Kut. 33:11; Kumb. 34:10 na fikra ile ile katika “mdomo kwa mdomo” ya Hes. 12:8).

Ukweli YHWH ni Mungu aliye pamoja nasi (yaani, *Immanueli* wa Isa. 7:14; 8:8,10). Dhambi ilivunja ukaribu wa ndani na YHWH akageuzia uso wake mbali (kama vile 31:17; Law. 17:10; 20:3,6; Isa. 59:2; Yer. 18:17; Eze. 7:22; 39:23,24,29).

4:38

NASB, NKJV,

NRSV “mataifa, walio wakubwa, wenye nguvu”

TEV, REB “mataifa walio wakubwa na wenye nguvu zaidi”

NJB “mataifa walio wakubwa na wenye watu wengi”

Mataifa haya yanaweza kuonekana (4:38; 7:1; 11:23; Yosh. 23:9) kama”

1. yenye idadi kubwa ya watu (kama vile 7:7)
2. wakazi wenye miili mikubwa (majitu) katika kimo (kama vile Hes. 13:22,28,33; Kumb. 1:28)

☐ **“kama ilivyo leo ”** Hii inaonyesha kuwa alama ya maelezo ya mwisho ya mhariri, lakini inaweza kurejelea kwa ufalme wa Sihoni na Ogu upande wa mashariki wa mto Yordani. Tazama muhtasari katika 3:14.

4:39 Haya ni maelezo mengine thabiti ya kuwa na imani katika Mungu mmoja. Tazama muhtasari katika 6:4.

4:40 “sheria. . .amri” Tazama Mada Maalumu katika 4:1. element

☐ **“siku zako ziwe nyingi katika nchi ”** KITENZI hiki ni neno kwa neno “kuongezeka” (BDB 73, KB 88, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Kut. 20:12; Kumb. 4:26,40; 5:16,33; 6:2; 11:9; 17:20; 22:7; 25:15; 30:18; 32:47). Tazama sehemu ya kimasharti!

☐ **“akupayo Bwana, Mungu wako, milele ”** KITENZI hiki (BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU) lazima kitafsiriwe katika nuru ya kumaanisha “kwa milele yote.” Tazama Mada Maalumu hapa chini.

MADA MAALUMU: MILELE ('OLAM)

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, עולם (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzuu 3, uk. 345). Yametumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na maudhui). Ifuatayo ni mifano iliyochaguliwa tu.

1. vitu vya kale
 - a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
 - b. mahari, Isa. 58:12; 61:4
 - c. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
 - d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
 - e. mda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. mda/ wakati ujao future time
 - a. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
 - b. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
 - c. uwepo endelevu
 - 1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
 - 2) mbinguni, Zab. 148:5
 - d. uwepo wa Mungu
 - 1) Mwa. 21:33
 - 2) Kut. 15:18
 - 3) Kumb. 32:40
 - 4) Zab. 93:2
 - 5) Isa. 40:28
 - 6) Yer. 10:10
 - 7) Dan. 12:7
 - e. Agano
 - 1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
 - 2) Kut. 31:16
 - 3) Ufu. 24:8
 - 4) Hes. 18:19
 - 5) 2 Sam. 23:5
 - 6) Zab. 105:10
 - 7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
 - 8) Yer. 32:40; 50:5
 - f. Agano maalumu na Daudi
 - 1) 2 Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
 - 2) 1 Fal. 2:33,45; 9:5
 - 3) 2 Nya. 13:5
 - 4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
 - 5) Isa. 9:7; 55:3
 - g. Masihi wa Mungu
 - 1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
 - 2) Isa. 9:6
 - h. Sheria za Mungu
 - 1) Kut. 29:28; 30:21
 - 2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
 - 3) Hes. 18:8,11,19
 - 4) Zab. 119:89,160
 - i. Ahadi za Mungu
 - 1) 2 Sam. 7:13,16,25; 22:51

- 2) 1 Fal. 9:5
- 3) Zab. 18:50
- 4) Isa. 40:8
- j. Uzao wa Abrahamu na nchi ya ahadi
 - 1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
 - 2) Kut. 32:13
 - 3) 1 Nya. 16:17
- k. Sikukuu za ahadi
 - 1) Kut. 12:14,17,24
 - 2) Ufu. 23:14,21,41
 - 3) Hes. 10:8
- l. umilele, kudumu milele
 - 1) 1 Fal. 8:13
 - 2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
 - 3) Isa. 26:4; 45:17
 - 4) Dan. 9:24
- m. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
 - 1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
 - 2) kudumu katika uwepo Wake, Ps. 41:12; 61:4,7
 - 3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
 - 4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
 - 5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1
 - 6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
 - 7) tukuza jina lake, Zab. 86:12; 145:2
 - 8) baliki jina lake, Zab. 145:1
- n. linatumiwa na Isaya kueleza enzi mpya
 - 1) agano la milele, Isa. 24:5; 55:3; 61:8
 - 2) YHWH kama mwamba wa milele, Isa. 26:4
 - 3) furaha ya milele, Isa. 35:10; 51:11; 61:7
 - 4) Mungu wa Milele, Isa. 40:28
 - 5) Wokovu wa milele, Isa. 45:17
 - 6) Wema wa milele, Isa. 54:8
 - 7) Ishara ya milele, Isa. 55:13
 - 8) Jina la milele, Isa. 56:5; 63:12,16
 - 9) Nuru ya milele, Isa. 60:19,20

Matumizi yenye hali ya ukanushi kuhusiana na adhabu ya milele kwa waharifu inapatikana katika Isa. 33:14, "moto wa milele." Isaya kila wakati anatumia "moto" kuelezea hasira ya Mungu (kama vile. Isa. 9:18,19; 10:16; 47:14), lakini katika Isa. 33:14 "ndipo anasema wa milele"
- 3. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
 - a. Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
 - b. Zab. 90:2 (Mungu pekee)
 - c. Zab. 103:17 (huruma zake)

Kumbuka, mktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani, Yeremia 7, tazama Mada Maalumu: Agano). Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipya la theolojia iliyopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale. Kumbuka pia, Agano Jipya linajumuisha ahadi zote za Agano la Kale (tazama Mada Maalumu: utabiri wa mambo yajayo ya Agano la Kale dhidi ya utabiri wa mambo yajayo ya Agano Jipya.).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4 :41-43

⁴¹ Ndipo Musa akabagua miji mitatu ng'ambo ya Yordani upande wa matokeo ya jua; ⁴² ili kwamba

amwuaye mtu apate kukimbilia huko, amwuaye jirani yake pasipo kujua, wala hakumchukia tangu hapo; ili apate kuishi akimbiliapo mmojawapo miji hiyo; ⁴³ nayo ni hii, Beseri ya barani iliyo katika nchi tambarare, kwa Wareubeni; na Ramothi iliyo Gileadi, kwa Wagadi; na Golani iliyo Bashani, kwa Wamanase.

4:41 “miji mitatu ng'ambo ya Yordani upande wa matokeo ya jua ” Miji hii iliitwa “miji ya makimbilio” (kama vile Hesabu 35; Kumbukumbu la Torati 19; Yoshua 20). Ilikuwa miji sita, mitatu kwa ajili ya kila upande wa Yordani. Miji hii yote ilikuwa ya Walawi (kama vile. Yoshua 21), ambapo mlawi, ambaye hakuwa na urithi wa nchi, aliishi. Ilikuwa ni sehemu ya “jicho kwa jicho” kama utaratibu wa haki wa Israeli. Ikiwa mtu aliuwa mwenzake wa agano bila kukusudia hivyo basi familia ilikua na haki ya kumuua (yaani, damu ya kisasi ya Hes. 35:12; Kumb. 19:6,12; Yosh. 20:3,5,9). Ikiwa mmojawapo amemuua mwingine bila kukusudia alikimbilia moja ya miji hii maalumu, iliamuliwa na wazee; ikiwa hakupatikana na mauaji ya kupangwa, basi aliweza kuishi salama katika mji (mpaka kifo cha kuhani mkuu). Hivyo anaweza kurudi nyumbani kwake salama (katika maana ya uhalali).

Tambua “ng'ambo ya Yordani” hapa inawezekana sasa kama kurejelea ukingo wa mashariki.

4:42 “pasipo kujua ” Neno la kukanusha (BDB 395) linarejelea kifo cha kutokusudia cha jamaa Mwisraeli, bila kudhamiria au chuki bila sababu. Tunaweza kuyaita ni mauaji ya mtu bila makusudi.

Shauku ya mwovu ni uhitaji wa nguvu za asili. Inakua ni moyo wa kitheolojia wa utaratibu wa sadaka. Ungamo lolote la dhambi isiyo kusudiwa linahitaji sadaka (kama vile. Kut. 21:12-14; Law. 4:2,22,27; 5:15-18; 22:14; Hes. 15:27,30; Kumb. 17:12-13; Yosh. 20:1-6). Hata sadaka kwa ajili ya taifa na kuhani mkuu katika siku ya upatanisho (Mambo ya Walawi 16) haikuweza kuifunika dhambi ya kukusudia (kama vile Zab: 51:14-17)! Je! haufurahii kuwa tuko chini ya sadaka ya Yesu katika Agano jipya?!

Katika lengo hili napenda kuongeza rejea kutoka NIDOTTE, juzuu ya 2, kujadili dhana ya:

“pasipo kujua’ au ‘pasipo kukusudia’ (Law. 4:2) yote yamepangwa na ni mashaka (kama vile 4:13,22,27; 5:15,18; 22:14; Hes. 15:22,24-29). Kwa sabababu yake baadhi ya wanazuoni wanahitimisha kwamba sadaka za kuteketezwa za dhambi ndizo pekee hushughulikia dhambi ya kutokusudia, kwamba ni dhambi, dhambi zilizoungamwa kwa makosa au dhambi zilizotendwa bila kujua tendo mahususi ilikuwa ni dhambi (tazama Melgrom, 1991, 228-29). Hata hivyo, neno ‘pasipo kujua’ kimsingi humaanisha ‘kwa makosa’ (vb. Humaanisha kuungama makosa, kutoka nje ya mstari). Ingawa inaweza pia kumaanisha kwamba makosa yalikuwa pasipo kujua au kupitiwa (tazama mf. Hes. 35:11,15,22-23; Yosh. 20:39), hili sio jambo la muhimu (tazama I Sam. 26:21; Mhu. 5:6)” (uk. 94).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 4: 44-49

⁴⁴ Na torati Musa aliyowawekea wana wa Israeli ni hii; ⁴⁵ haya ndiyo mashuhudizo, na amri, na hukumu, Musa alizowaambia wana wa Israeli walipotoka Misri; ⁴⁶ ng'ambo ya Yordani, katika bonde lililoleleka Beth-peori, katika nchi ya Sihoni mfalme wa Waamori, aliyekuwa akikaa Heshboni ndiye aliyepigwa na Musa na wana wa Israeli, walipotoka Misri; ⁴⁷ wakaishika nchi yake, ikawa milki yao, na nchi ya Ogu mfalme wa Bashani, ndio wafalme wawili wa Waamori, waliokuwa ng'ambo ya Yordani upande wa matokeo ya jua; ⁴⁸ toka Aroeri, iliyo juu ya ukingoni pa bonde la Arnoni, hata mpaka mlima wa Sioni (nao ndio Hermoni), ⁴⁹ na Araba yote iliyo ng'ambo ya Yordani upande wa mashariki, hata mpaka bahari ya Araba, chini ya matelemko ya Pisga.

4:44-45 “sheria. . . mashuhudizo. . . amri. . . hukumu” tazama Mada Maalumu katika 4:1.

4:45 “haya ndiyo mashuhudizo” Haya ni maneno ambayo mtunga Zaburi aliyatumia kuelezea Torati, au sheria ya Mungu. Neno “Torati” humaanisha “mafundisho” ya Mungu. Sheria haikutolewa kama mzigo wa kumharibu mwanadamu. Mapokeo ya fasihi simulizi ambayo yaliyokuwa pamoja na sheria yalifanya kuwa mzigo mzito. Agano la kale halina kitu zaidi ya upendo, ufunuo binafsi wa Mungu katikati ya mwanadamu mjinga. Sheria za Agano la kale zililenga dhambi kwa uzito zaidi, udhaifu wa mwanadamu, na kuhitajika mkombozi, lakini ilitolewa kwa upendo (kama vile. Zab. 19:7-9).

☞“Musa alizowaambia wana wa Israeli walipotoka Misri” Musa anazirudia amri kumi kwa mara ya pili hapa. Lakini watu waliokuwa wakisikiliza wakati huu walikuwa ni watoto mara tu zilipotolewa katika Kutoka 20 hapo Mlima Sinai. Alikuwa anawaambia tena. Musa alitenda hivyo kwa ajili ya wana wa Israeli akitarajia kwamba akina baba watafanya hivyo katika nyumba zao wenyewe. Kila kizazi kilipaswa kukiambia kizazi kipya juu ya mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yao.

4:46-49 Vifungu hivi ni muhtasari wa kihistoria wa ushindi mara mbili. Sababu ya kwamba aliruhusu ushindi mara mbili katika upande wa mashariki mwa Mto Yordani ni kushabihiana kwa dhana ya matunda ya awali. Matunda ya awali katika Uyahudi ni mavuno kidogo kuthibitisha kwamba Mungu ni mwaminifu na kwamba mavuno yote yanakuja. Baada ya Kuwashinda wafalme wawili wa Amori upande wa mashariki wa mto Yordani aliwaambia Israeli, “nakupenda. Nilikuahidi kukupa nchi. Unajua namaanisha nini, Niamini na kunitii mimi na mimi nitakupa pumziko.”

Haya ni maelezo mengine mafupi ya uzoefu wa Israeli katika kipindi cha mwisho cha kutangatanga jangwani katika Moabu.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! imani ya Agano la kale kimsingi ilikuwa ni kuitunza sheria au ni uhusiano na Mungu?
2. Je! ni kwa nini Biblia inawapa mkazo wazazi kuwafundisha watoto wao juu ya Mungu?
3. Je! ni kwa nini Mungu amemkataza mwanadamu kutengeneza uwakilishi wake wa kimwili?
4. Ni kwa namna gani Israeli ni tunu maalumu ya Mungu? Na kwa nini?
5. Orodhesha masharti mawili ya kudumu kwa ajili ya jamii imara.
6. Taja matokeo matatu ya kuvunja agano.
7. Je! kifungu hiki kinafundisha imani kwamba kuna Mungu mmoja au kutukuza mungu kati ya wengi?
8. Kwa nini Mungu aliichagua Israeli?
9. Nini lilikuwa kusudi la kisasi cha “jicho kwa jicho”?
10. Je! utaratibu wa sadaka ulihusika na dhambi za mwanadamu? Kwa nini au kwa nini sivyo?
11. Ni kwa namna gani sadaka ya Kristo ni kuu?

KUMBUKUMBU LA TORATI 5

MIGAWANYO YA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	REV	NJB
Amri kumi zinapitiwa Upya 5:1-5	Utoaji wa sheria katika mlima Sinai 5:1-5	Amri kumi za Mungu 5:1-5	Amri kumi za Mungu 5:1 5:2-5
5:6-7 5:7	5:6-7 5:7	5:6	5:6
5:8-10 5:11 5:12 5:13 5:14 5:15 5:16 5:17	5:8-10 5:11 5:12 5:13 5:14 5:15 5:16 5:17	5:8-10 5:11 5:12 5:13 5:14 5:15 5:16 5:17	5:8-10 5:11 5:12 5:13 5:14 5:15 5:16 5:17
5:18-21	5:18-21a 5:21b	5:18-21	5:18-21
5:22 Watu waliogopa uwepo Wa Mungu	5:22-27	5:22 Hofu ya watu	5:22 Musa mpanishi
5:23-33	5:28-33	5:23-27 5:28-31	5:23-27 5:28-31
5:32-33	Kumpenda Yahwe ndiyo		Asili ya sheria (5:32-6:13) 5:32-6:3

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Taz. uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu nimwongozokwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (ukisoma mzunguko wa #3, uk. viii).linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

USOMAJI WA HISTORIA YA NYUMA

- A. Roland de Vaux, *Ancient Israel*, juzuu. 1, kur. 143-144, imeorodhesha mfumo ya sheria ya Agano la Kale:
 1. Amri kuu za Mungu - Kut. 20:2-17; Kumb. 5:6-21

2. Mfumo wa agano - Kut. 20:22-23:33
 3. Kumbukumbu la Torati – Kumbukumbu la Torati 12-26
 4. Sheria ya Utakatifu – Mambo ya Walawi 17-26
 5. Mfumo maalum wa kikuhani – Mambo ya Walawi 1-7, 11-16
- Haya yote yanafikiriwa kuwa *Torati*. Ni maelekezo maalum ya Kiungu juu ya matendo na mienendo.
- B. Aina ya sheria za Kiyahudi
1. Hali ya ulaghai – sheria zinazotofautishwa na muundo wa neno “kama. . . hivyo” . kuna madhara kwenye matendo. Mara nyingi hii ni miongozo kwenye jamii.
 2. Hali ya mabishano – sheria zilizoelezewa kama za kimakatazo (mara nyingi maelezo ya NAFSI YA PILI WINGI - “hautapaswa. . .”). mara nyingi hii ni miongozo kwa ajili ya maisha ya kiroho
- C. Athari za kitamaduni
1. Kwenye yaliyomo – mifumo ya sheria za awali
 - a. Lipit-Ishtar
 - b. Mfumo wa Hammurabi
 2. Kwenye muundo – mikataba ya Wahiti (Suzerain), ambayo ilitokea sehemu mbalimbali, lakini Kumbukumbu la Torati na Yoshua 24 inafuata mpangilio wa kipindi cha mwaka 2000 K.K, unaoonyesha uhalisi wa matukio (k.v. John H. Walton, *Ancient Israelite Literature in Its Cultural Context*, pp. 95-107; K.A. Kitchen, *The Bible in Its World*, kur. 80-95; tazama utangulizi kwenye kitabu, VII.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 5:1-5

¹Musa akawaita Israeli wote, akawaambia, Enyi Israeli, zisikieni amri na hukumu ninenazo masikioni mwenu leo, mpate kujifunza na kuangalia kuzitenda. ²Bwana, Mungu wetu, alifanya agano nasi katika Horebu. ³Bwana hakufanya agano hili na baba zetu, bali na sisi, yaani, sisi sote tuliopo hapa, tu hai. ⁴Bwana alisema nanyi uso kwa uso mlimani, toka kati ya moto; ⁵(nami wakati ule nalisimama kati ya Bwana na ninyi, ili kuwaonyesha neno la Bwana; maana, mliogopa kwa sababu ya ule moto, wala hamkupanda mlimani); naye akasema,

5:1 “Israel wote” Sheria ilikuwa kwa ajili ya kila mmoja (sio kwa kundi la wasomi tu), lakini huenda Musa alizungumza kwa wazee ambao baadaye waliwambia (yaani., makabila, koo). Kwa ajili ya “Israel” tazama Mada Maalum katika 1:1.

☐ “Sikieni” Tazama kumbukumbu katika 4:1.

☐ “amri na hukumu” Tazama kumbukumbu katika 4:1.

☐ “mpate kujifunza na kuangalia kuzitenda” Kifungu hiki kina MANENO matatu:

1. “mpate kujifunza” (BDB 540, KB 531, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, k.v. 4:10; 5:1; 14:23; 17:19; 18:9; 31:12,13)
2. “kuangalia kuzitenda” (BDB 1036, KB 1581, *Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, k.v. 4:2,6,9,40; 5:10,12,29,32; 6:2,3, 17[mara mbili],25; 7:8,9[mara mbili],11,12[mara mbili], n.k.
3. “kwa uangalifu” – kiuhalisia ni “tenda” (BDB 793, KB 889, *Qal YA KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO*) Haya maneno matatu yanafupisha maana ya neno *shema* (BDB 1033, KB 1570, mf., 4:1; 5:1,23,24,25,26, 27[mara mbili], 28[mara mbili]; 6:3,4; 9:1; 20:3; 27:9), likimaanisha “sikieni mpate kuyatenda”!

5:2 “Bwana, Mungu wetu” Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu 1:3.

☐ **“alifanya”** Kiuhalisia hili ni neno “kufanya” (BDB 503, KB 500, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU [mara mbili]). Hii ilikuwa namna ya kurithibitisha agano la kale (yaani., “kufanya agano,” k.v. Mwa. 15:18; 21:27,32; 31:44; Kut. 34:27; Kumb. 5:3; 29:12; 31:16). Ibrahim akamtwaa mbuzi wa miaka mitatu, ndama wa miaka mitatu, na wanyama wengine, akawapasua vipande viwili, na akaweka kila kipande kuelekea mwenzake, na kutembea katikati ya vipande kama alama ya agano. Yumkini inadokeza laana juu ya wale wanaovunja agano (k.v. Mwa. 15:9-18; Yer. 34:18) au chakula kuweka muhuli wa agano.

☐ **“kufanya agano nasi”** Tazama maelezo katika 4:13.

☐ **“katika Horebu”** Horebu ni neno la Kiebrania lenye kumaanisha ya Mlima Sinai. Tazama Mada Maalum katika Kumb.1:2.

5:3 “baba zetu” Baadhi ya wanazuoni wanakitazama kifungu hiki kama chenye kuwarejelea wazee wa imani, Ibrahim, Isaka, na Yakobo, lakini wengine wanakitazama kama chenye kuwarejelea wazazi, kizazi cha uovu kilichofia huko jangwani (k.v. Hes. 26:63-65). Kifungu kinachofuata kinaonekana kuthibitisha chaguo la pili.

☐ **“sisi sote tuliopo hapa”** Hili linawarejelea watoto (yaani., walioko chini ya umri wa miaka ishirini) wa kizazi cha uovu. Hili kwa wazi linaonyesha kuwa maneno ya YHWH yalikuwa ufunuo kwenye kizazi hiki na kwa kila kizazi, ukijumuisha na cha leo.

5:4 “uso kwa uso” Hili linawarejelea makabiliano binafsi (sio kiuhalisia) juu ya Mlima Horebu/Sinai katika kitabu cha Kutoka 19. Hii ni nahau inayojirudia (k.v. Mwa. 32:30; Kut. 33:11; Kumb. 5:4; 34:10; Amu. 6:22; Ezek. 20:35).

☐ **“toka kati ya moto”** Hili ni rejeo la kujirudia kwenye kitabu cha Kutoka 19 (k.v. 4:12,15,33,36; 5:4,22,24,26; 9:10; 10:4).

5:5 “nami wakati ule nalisimama kati ya Bwana na ninyi, mliogopa” Watu walimwogopa YHWH kwa hiyo Musa alikuwa mpatanishi kati ya YHWH na Waisraeli (k.v. Kut. 19:16).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 5:6

⁶Mimi ni Bwana, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.

5:6 “Mimi ni Bwana” Haya yanaweza kuwa ni maelezo yaliyofasiriwa: “Mimi Ndiye.” Mimi ndiye Mungu aishiye. Mimi ndimi niliyewahi kuwepo. Neno YHWH ni muundo wa KITENZI cha Kiebrania “kuwepo” (k.v. Kut. 3:14). Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katikat 1:3.

☐ **“niliyekutoa katika nchi ya Misri”** Tambua kuwa neema ya YHWH na uchaguzi wake wa hiari uliletwa mbele ya sheria ukawasilishwa. Mungu aliichagua Israeli, bali Israeli haikumchagua Yeye. Chaguo hili lilifanywa wazi kwa Ibrahimu katika ahadi/agano lisilo na masharti Mwa. 15:12-21.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 5:7

⁷Usiwe na miungu mingine ila mimi.

5:7 “usiwe na miungu mingine ila Mimi” Neno “ila” (BDB 818 #7) kiuhalisia ni “mbele ya macho yangu,” ambayo ni nahau yenye kumaanisha “hapana mwingine wa aina yangu” (k.v. Kut. 20:3,23). YHWH ni wa pekee, wa kipekee, hajawi kuwepo! Haya ni madai ya kuwepo Mungu mmoja pekee (k.v. Kut. 8:10; 9:14; Kut. 4:35,39; 33:26; I Sam. 2:2; II Sam. 7:22; 22:32; Isa. 46:9). Haya madai ya kwanza na amri ni upekee wa imani ya Isreali katika imani ya miungu wengi huko Mashariki ya Karibu ya Kale! Tazama maelezo katika 6:4.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : 5:8-10

⁸Usijifanyie sanamu ya kuchonga, mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, au kilicho chini duniani, au kilicho majini chini ya nchi. ⁹ Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu, nawapatiliza wana uovu wa baba zao; hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, ¹⁰ nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

5:8 “sanamu” Kiuhalisia hii ni “sanamu ya kuchonga” (BDB 820). Hii inaweza kurejelea (1) ujiwasilishaji kamili wa YHWH (k.v. 4:12,15-19,23,25). Ndama wakuchonga katika kitabu cha Kutoka 32 ulikuwa ni uwasilisho wa YHWH; au (2) miungu ya kigeni (k.v. Law. 19:4; 26:1).

☐“Duniani” Tazama Mada Maalu: Ardhi, Nchi, Dunia hapa chini (אָרֶץ).

MADA MAALUM: ARDHI, NCHI, DUNIA (אָרֶץ)

Kama ilivyo mizizi ya Kiebrania, muktadha ni muhimu katika kutambua maana ya mizizi iliyokusudiwa na mwandishi wa asili. Idadi ya mipaka ya mizizi ya Kiebrania (yaani, lugha ya Kisemiti ya kale) inasababisha kila mzizi kufanya kazi katika maana tofauti na maana nyingine. Huu mzizi (BDB 75, KB 90) unaweza kumaanisha

1. Dunia yote (ingawa wachambuzi wa kale hawakubainisha kiwango na umbiile lake. Mara nyingi hutumika kumaanisha "ulimwengu usiojulikana")
 - a. Mwanzo 1-2; 6-9; 10:32; 11:1,4,8,9; 14:19; 18:18,25; 22:18, n.k.
 - b. Kutoka 9:29; 19:5
 - c. Zaburi 8:1,9; 24:1; 47:2,7; Yer. 25:26,29,30
 - d. Mithali 8:31
 - e. Isaya 2:19,21; 6:3; 11:4,9,12; 12:5
2. Dunia katika kutofautisha na mbingu
 - a. Mwanzo 1:2
 - b. Kutoka 20:4
 - c. Kumbukumbu la Torati 5:8; 30:19
 - d. Isaya 37:16
3. Stiri kwa wakazi wanadamu wakaao juu ya dunia
 - a. Mwanzo 6:11; 11:1
 - b. 1 Wafalme 2:2; 10:24
 - c. Ayubu 37:12
 - d. Zaburi 33:8; 66:4
4. Nchi au himaya
 - a. Mwanzo 10:10,11; 11:28,31
 - b. hasa. Israeli (zawadi kutoka kwa YHWH, Yeye anaimiliki)
5. udongo, kama vile Yoshua 7:21
6. chini ya ulimwengu (KB 91)
 - a. Kutoka 15:12
 - b. Zaburi 22:29; 71:20; Yer. 17:13; Yona 2:6
7. Ulimwengu mpya
 - a. Isaya 9:1-7; 65:17; 66:22
 - b. Angalia Agano Jipya, Rum. 8:19-22; Gal. 6:15; 2 Pet. 3:13; Ufu. 21:1,5

Kumbuka, muktadha, muktadha, muktadha ni muhimu. Mara nyingi mzizi tambuzi unaweza kusaidia, lakini si mara kwa mara. Kitabu amabacho kilinisaidia kuanza kufikiri kuhusu neno hili linavyotumika katika mistari tofauti ni Bernard Namm, *Christian View of Science and Scripture*. Yeye alinishawishi juu ya gharika lililowahi kutokea (yaani, Mwanzo 6-9). Iweni makini na matumizi ya thiolojia yako mwenyewe katika ufafanuzi wa Maneno ya lugha ya Kiingereza

5:9 “Msivisujudie wala kuvitumikia” Hii ni miundo miwili ya KITENZI kanushi:

1. “msiviabudu” - BDB 1005, KB 295 *Hishtaphel* KAULI ISIOTIMILIFU au *Hithpael* KAULI ISIOTIMILIFU, yenye kumaanisha “kusujudu,” “kuinamia” (k.v. 4:19; 8:19; 11:16; Kut. 20:5; 23:24)
2. “msivitumikie” - BDB 712, KB 773, *Hophal* KAULI ISIOTIMILIFU, ikimaanisha “fanya” “tumika kama mtumwa,” au “tenda vitendo vya kuabudu (k.v. 13:2; Kut. 20:5; 23:24)

YHWH alikwisha tambua tabia ya “udini” na “ushirikina” wa moyo wa mwanadamu aliyeanguka na kujaribu kuulinda ufunuo wake mwenyewe na kusudi lake toka kwenye athari za uharibifu wa ibada ya sanamu za Mashariki ya Karibu.

☐“wivu” Tazama kumbukumbu katika 4:24.

☐ KITENZI “kuwatembelea” (BDB 823, KB 955, *Qal* KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU) ina maana mbalimbali:

1. Tembelea kwa ajili ya kubariki - Mwa. 21:1; 50:24,25; Kut. 13:19; Ruth 1:6; Zab. 65:9; 106:4; Yer. 27:22; 29:10; 32:5
2. Tembelea kwa ajili ya kuadhibu - Kut. 20:5; 34:7; Yer. 11:22; 13:21; 21:14; 24:25; Amos 3:2,14; Hosea 1:4; 2:15; 4:14; 12:2

☐“uovu wa baba zao” Neno “uovu” (BDB 730) laweza kuhusiana na asili ile ile ya neno “kulaghai” (mf., II Sam. 19:20; 24:17; I Fal. 8:47; Zab. 106:6). Israeli inaadhibiwa kwa sababu ya kutokutii kwao (mf., Kut. 20:5; 34:7; Law. 18:25; Hes. 14:18; Kumb. 19:15; Yer. 25:12; 36:31; Amos 3:2).

☐“nawapatiliza wana uovu wa baba zao; hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao” Tambua adhabu ya Mungu sio ya kihole holela, bali huelekezwa juu ya wale “awachukiao” YHWH (BDB 971, KB 1338, *Qal* KAULI TENDAJI YA WAKATI UNAO ENDELEA). Hii inadokeza kuwa huambaa ambaa kwenye familia. Ushawishi wa wazazi ni wa muhimu kwenye suala la kukua kiimani (tazama kumbukumbu katika 4:10). Huko Mashariki ya Karibu ya Kale vizazi mbalimbali vya familia viliishi pamoja. Ukaidi au kutokuamini kwa kizazi kimoja kuliweza kuathiri familia nzima. Hii ni sehemu ya dhana ya Kiebrania ya ushirika (yaani., mmoja angeweza kuathiri wote—Adam, Achani, Daudi, Yesu). Hii maana ya ushirika lazima iongezwe kwenye dhana ya imani ya mtu binafsi (k.v. 24:16; II Fal. 14:6; Yer. 31:29-30; Ezekieli 18)!

5:10 “huonyesha” KITENZI (BDB 793, KB 889) ni *Qal* KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU, ambacho huendana na kitendo endelevu cha KITENZI katika mst.9.

☐“huwarehemu” Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUMU: WEMA (HESED)

Neno hili (BDB 338 I, KB 336 II) lina maeneo mapana ya maana.

- A. Lilitumika katika kuwaunganisha wanadamu
 1. Wema kwa wenzetu (mf. 1 Sam. 20:14; 2 Sam. 16:17; 2 Nya. 24:22; Ayubu 6:14; Zab. 141:5; Mit. 19:22; 20:6)
 2. wema kwa maskini na wahitaji (mf. Mika 6:8)
 3. upendo wa Israeli kumuelekea YHWH (kama vile Yer. 2:2; Hos. 6:4,6)
 4. uzuri wa muda wa maua ya kondeni (kama vile Isa. 40:6)
- B. Lilitumika kuhusiana na Mungu
 1. uaminifu wa agano na upendo
 - a. " ukombozi kutoka katika maadui na taabu" (mf. Mwa. 19:19; 39:21; Kut. 15:13; Zab. 31:16; 32:10; 33:18,22; 36:7,10; 42:8; 44:26; 66:20; 85:7; 90:14; 94:18; 107:8,15,21,31; 109:21-22; 143:8,12; Yer. 31:3; Ezr. 7:28; 9:9)
 - b. "katika ulinzi wa maisha kutoka katika kifo" (mf. Ayubu 10:12; Zab. 6:4-5; 86:13)
 - c. "katika wepesi wa maisha ya kiroho" (mf. Zab. 119:41,76,88,124,149,159)
 - d. "katika ukombozi wa kutoka dhambini" (kama vile Zab. 25:7; 51:1; 130:7-8)

- e. "katika kutunza maagano" (mf. Kum. 7:9,12; 2 Nya. 6:14; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4; Mik. 7:20)
2. kuzielezea sifa za Mungu (mf. Kut. 34:6; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoeli 2:13; Yona 4:2; Mika 7:20)
3. wema wa Mungu
 - a. "utele" (mf. Hes.14:18; Neh. 9:17; Zab. 86:5; 103:8; 145:8; Yoeli 2:13; Yer. 4:2)
 - b. "ukuu katika kiwango chake" (mf. Kut. 20:6; Kum. 5:10; 7:9)
 - c. "umilele" (mf. 1 Nya. 16:34,41; 2 Nya. 5:13; 7:3,6; 20:21; Ezra 3:11; Zab. 100:5; 106:1; 107:1; 118:1,2,3,4,29; 136:1-26; 138:8; Yer. 33:11)
 - d. Kama ngome (mf. Zab. 59:17)
 - e. ilihusiana na nguvu za Mungu (mf. Zab. 62:11c-12a)
4. matendo ya wema (mf. 2 Nya. 6:42; Zab. 89:2; Isa. 55:3; 63:7; Omb. 3:22)

Neno hili linatafsiriwa kwa njia nyingi mbalimbali katika tafsiri za Kiingereza. Nafikiri muhtasari bora wa maana yaliyo katika ufupisho yangelikuwa "hakuna kamba iliyunganisha uaminifu wa agano la Ki-Mungu" neno hili ni sambamba na neno la Agano Jipya "upendo" (*agapaō*). Munguni mwaminifu na mwenye upendo kwa sababu ya Yeye alivyo!

☐ **“maelfu”** Hii mistari miwili imenisaidia kutazama asili ya YHWH. Asili yake ya msingi ni upendo wenye kustahimili, lakini huwaadhibu wale wote wamukataao (hasa wale wenye kuwa na maarifa ya ufunuo wake, yaani., watu wa agano). Hesabu kwenye mistari hii miwili inanipa alama.

1. Akiubatiliza uovu kizazi cha tatu na cha nne
2. Akiuonyesha upendo wa agano hata vizazi elfu (k.v. 7:9)

☐ **“wale wanipendao na kuzishika amri zangus”** Ni tabia ya Kumbukumbu la Torati kuhusianisha utii kwenye agano la YHWH kwa ajili ya kumpenda YHWH (k.v. 6:5; 7:9; 10:12; 11:1,13,22; 13:3; 19:9; 30:6,16,20). Upendo wa YHWH sio wenye kubadilika, bali ni wa wazi. Huonyesha kutokupendelea. Upendo wake wa agano aliouanzisha unaendelezwa na utii wa agano.

Neno “Kuzishika” (BDB 1036, KB 1581) ni dhana muhimu kwenye sura hii (k.v. 5:1,10,12,29,32 na mara nyingi katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati). Agano la Kale lilijikita juu ya neema ya YHWH na utii wa mwanadamu/utendaji kazi. YHWH alitaka kuonyesha namna mwanadamu alivyoshindwa kujongea kwake ipasavyo (k.v. Wagalatia 3). Agano Jipya (k.v. Yer:31: 31- 34; Ezek. 36:22-38) limejikita juu ya uanzishaji wa neema ya Mungu na ukombozi katika Kristo. Waamini bado wanatakiwa kuwa watakatifu (k.v. Efe. 1:14; 2:10), lakini wamekwisha kukubaliwa na kusamehewa kwa neema kupitia imani (k.v. Efe. 2:8-9). Sasa wanatii/kutenda nje ya maana ya shukrani na upendo wa familia (yaani., “wale wote wanipendao”). Lengo ni moja, watu wa haki (kama Kristo) lakini utaratibu wa kufanya umebadilika toka utendaji wa mwanadamu hadi utendaji wa Kristo (k.v. Marko 10:45; II Kor. 5:21).

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 5:11

¹¹ **Usilitaje bure Jina la Bwana, Mungu wako; maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia, mtu alitajaye jina lake bure.**

5:11 “usilitaje” KITENZI(BDB 669, KB 724, *Qa*/ WAKATI USIOTIMILIFU) kinamaanisha “kutamka, ” au “kultitaja.” Inaonekana kudokeza kitendo cha kutamka. Waisraeli waliendelea kultitaja “jina”katika ibada (k.v. 6:13; 10:20), lakini sio majina ya miungu wengine!

Msisitizo unaanzia katika kitabu cha Mwa. 4:25-26, ambapo kizazi cha Sethi “walipoanza kuliitia jina la Bwana”; Ibrahim pia alifanya hivyo (Mwa. 12:8; 21:33); Isaka akatenda hivyo hivyo (Mwa. 26:25). Dhana ile ile inawekwa kwenye muundo wa matukio ya siku za mwisho na Yoeli 2:28-32. Hili linaendelezwa na Mtume Petro wakati wa Pentekoste na kudai kutimilizwa (k.v. Mdo. 2:14-21); Mtume Paulo anakitumia kifungu kiki kuutoa wokovu kwa ajili ya wote katika Rum. 10:9-13.

Jina linawakilisha nafsi na tabia ya YHWH. Waisraeli walipaswa kuwa ufalme wa kikuhani ulimwenguni (k.v. Kut. 19:5-6), lakini masikitiko ni kuwa kutokulitii agano, kulisababisha YHWH kuwaadhibu (k.v. Kumbukumbu la Torati 27-29), lilimaanisha kuwa ujumbe kwa ulimwengu uliondolewa na:

1. Hukumu ya Mungu kwa Israeli badala ya kuwabariki
2. Watu wa Mungu kuigeukia ibada ya sanamu
3. Watu wa Mungu kukua katika majivuno, na kujihesabia haki!

☐“bure” KITENZI (BDB 996) kinamaanisha “tupu,” “hakijawahi kuwepo,” “bure” (k.v. Kut. 20:7; Ps. 139:20). Hili ni neno lile lile lililotumika katika 5:20 kwa ajili ya mashahidi wa “uongo” .Yawezekana kuwa amri hairejei kwenye kuapa kwa jina la YHWH (k.v. 6:13; 10:20), bali ni kwa kulitumia jina lake katika ushuhuda wa uongo. Israeli ikajakuwa yenye ushuhuda wa “uongo” kwenye tabia na makusudi ya YHWH kwa sababu ya ukaidi wao wa kujirudia rudia, ambapo iliwapelekea kwenye hukumu ya YHWH (K.V. Kumbukumbu la Torati 27-29). Tazama Mada Maalum katika 4:6.

☐“maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia” KITENZI (BDB 667, KB 720, *Piel* KAULI ISITIMILIFU kikimaanisha “kutokuwa na hatia”) ni stiari ya kitu ambacho kipo safi, hivyo basi hakina hatia au kutokuwa na kosa (k.v. Kut. 20:7; 34:7; Hes. 14:18; Yer. 30:11; 46:28; Yoeli 3:21; Nah. 1:3). Kuna madhara kwenye dhambi ya mwanadamu. Kumdanganya YHWH ni dhambi kubwa, hasa kwa wale wanao mjua Yeye (k.v. Lk. 12:48; Ebr. 10:26-31)!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:12-15

¹²Ishike siku ya Sabato uitakase, kama Bwana, Mungu wako, alivyokuamuru. ¹³Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; ¹⁴lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako; siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwanao, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala ng'ombe wako, wala punda wako, wala mnyama wako ye yote, wala mgeni aliye ndani ya malango yako, ili mtumwa wako na mjakazi wako wapumzike vile vile kama wewe. ¹⁵ Nawe utakumbuka ya kuwa wewe ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri, na ya kuwa Bwana, Mungu wako, alikutoa huko kwa mkono wenye nguvu, na mkono ulionyoshwa; kwa sababu hiyo Bwana, Mungu wako, alikuamuru uishike sabato.

5:12 “Ishike” KITENZI (BDB 1036, KB 1581, *Qal* KITENZI JINA HALISI) kikimaanisha “kutunza” na kinatumika mara kwa mara katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati.

☐“sabato” Tazama Mada Maalum hapa chini

MADA MAALUM: SABATO

Hili linatokana na maana ya kiebrania "pumziko" au "kuacha kwa muda" (BDB 992). Linahusiana na siku ya saba ya uumbaji ambapo Mungu aliacha kazi zake baada ya kumaliza uumbaji wake wa mwanzo (kama vile Mwa. 2:1-3). Mungu hakupumzika kwa sababu alikuwa amechoka, lakini ni kwa sababu (1) uumbaji ulikuwa umekamilika na kuonekana unapendeza machoni pake (kama vile Mwa. 1:31) na (2) kumpa mwanadamu mwongozo kwa ajili ya ibada na pumziko. Utaratibu kama ilivyo siku ya kuabudu ulianza Mwa. 2:2-3, ambapo YHWH alitumia pumziko lake kama utaratibu kwa ajili ya wanyama (kama vile Kut. 23:12) na mwanadamu (binadamu huhitaji utaratibu wa kila mara wa kazi, pumziko, na ibada). Sabato ilianza kama ilivyo siku zote za mwanzo 1, jioni; kwa hiyo, Ijumaa jioni mpaka Jumamosi jioni ulikuwa ni muda rasmi kwa ajili ya sabato. Maelezo yote juu ya kuishika sabato yametolewa katika kitabu cha Kutoka (hasa katika sura 16; 20; 31; na 35) na Mambo ya Walawi (hasa sura ya 23-26). Hasa utumiaji wa kwanza wa siku hii kwa Waisraeli ilikuwa ni katika Kut. 16:25-26 kwenye kusanyiko la manna. Baadaye ikajakuwa sehemu ya "amri kumi" (kama vile Kut. 20:8-11; Kumb. 5:12-15). Huu ni mfano mojawapo ambapo Amri Kumi katika Kutoka 20 kwa kiasi kidogo zimetofautiana na zile zilizoko katika Kumbukumbu la Torati 5. Zile za Kumbukumbu la Torati lilimwandaa Mwisraeli kwa ajili ya makazi, maisha ya kilimo huko Kanaani.

Mafarisayo walizichukua hizi taratibu na, kwa majadiliano yao ya kusimuliana, wakazitafasiri kwa namna ya kuzitumia kwenye sheria nyingi. Yesu mara nyingi alitenda miujiza, akijua wazi anakwenda kinyume na sheria zao ili kwamba waweze kuingia kwenye mjadala. Ilikuwa sio sabato aliyoikataa Yesu, bali kujihesabia kwao haki na kukosekana kwa upendo.

☛“uitakase” Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: MTAKATIFU (קדוש)

Agano la Kale (likielezwa kwa zaidi kutoka Isaya)

A. Asili ya neno *kadosh* (BDB 872, KB 1072) halina uhakika, pengine ni Ki-kanaani (yaani, lugha ya Magharibi mwa Shamu). Inawezekana kwamba sehemu ya mzizi wa neno (yaani, *kd*) unamaanisha "kugawanya."

Hiki ni chanzo cha ufafanuzi unaofahamika wa neno "tengwa (kutoka kwenye utamaduni wa Ki-kanaani, kama vile Kumb. 7:6; 14:2,21; 26:19) kwa matumizi ya Mungu."

B. Linahusiana na uwepo wa Mungu ndani ya vitu, mahali, wakati, na watu. Halitumiki katika kitabu cha Mwanzo, bali linakuwa la kawaida katika vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi, na Hesabu.

C. Katika fasihi ya Kinabii (hasa Isaya na Hosea) hali ya kibinadamu ilikuwepo hapo awali, lakini haikuhimizwa kwa ajili ya kutenda kazi (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu). Inakuwa njia ya kueleza asili ya Mungu. (kama vile Isa. 6:3). Mungu ni Mtakatifu. Jina Lake linalowakilisha sifa yake ni takatifu. Watu wake ndio wanaopaswa kuifunua sifa Yake kwa ulimwengu unaohitaji utakatifu (ikiwa watalitii agano katika imani).

1. KIVUMISHI, BDB 872 קדוש, "takatifu," "tukufu" linatumika juu ya

- Mungu, Isa. 5:16; 6:3 (mata tatu); tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu
- Jina Lake, Isa. 40:25; 49:7; 57:15
- kukaa Kwake ndani, Isa. 57:15
- Sabato, Isa. 58:13

2. KITENZI, BDB 872 קדש, "kutengwa mbali," "wekwa wakfu"

- sifa ya Mungu, Isa. 5:16; 29:23
- Mungu, Isa. 8:13; 65:5
- malaika wa Mungu, Isa. 13:3
- jina la Mungu, Isa. 29:23
- sherehe za kidini, Isa. 30:29
- wanadamu walioweka wakfu, Isa. 66:17

3. NOMINO, BDB 871 קדש, "utengwaji," "uwekwaji wakfu"

- uzao mtakatifu, Isa. 6:13
- mlima mtakatifu, Isa. 11:9; 27:13; 56:7; 57:13; 65:11,25; 66:20
- kutengwa, Isa. 23:18
- njia ya utakatifu, Isa. 35:8
- mahali patakatifu, Isa. 43:28; 62:9; 64:11
- mji mtakatifu, Isa. 48:2; 52:1
- aliye Mtakatifu, Isa. 49:7 (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu)
- mkono mtakatifu, Isa. 52:10
- siku takatifu, Isa. 58:13
- watu watakatifu, Isa. 62:12
- Roha Mtakatifu, 63:10,11
- Kiti cha enzi cha Mungu, Isa. 63:15
- sehemu takatifu, Isa. 63:18
- miji mitakatifu, Isa. 64:10

D. Huruma ya Mungu na upendo havitenganishwi kutoka katika dhana ya thiolojia ya maagano, haki, na sifa ya muhimu. Humu ndani pana mvutano wa Mungu dhidi ya utu ulioanguka, usio mtakatifu, wenye

kuasi. Kuna mada inayotia shauku sana kuhusiana na mahuhusiano kati ya Mungu kama "mwenye huruma" na Mungu kama "mtakatifu" katika kitabu cha Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kr. 112-113.

Agano Jipya

- A. Waandishi wa Agano Jipya (isipokuwa Luka) walikuwa Waebrania wenye fikra pana, lakini waliandika katika lugha ya kawaida ya Koine. Kanisa la Agano Jipya lilitumia fasiri ya Kiyunani kufasiri kitabu cha Agano la Kale. Ilikuwa ni tafasili ya Kiyunani ya Agano la Kale, sio fasihi ya Kiyunani cha daraja la juu, fikra, au dini, iliyodhibiti misamiati yao.
- B. Yesu ni mtakatifu kwa kuwa Yeye ni wa Mungu na ni sawa na Mungu (kama vile Luka 1:35; 4:34; Matendo 3:14; 4:27,30; Ufu. 3:7). Yeye ni Mtakatifu na Mwenye Haki (kama vile Matendo 3:14; 22:14). Yesu ni mtakatifu kwa sababu hana dhambi (kama vile Yohana 8:46; 2 Cor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Pet. 1:19; 2:22; 1 Yohana 3:5).
- C. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu (kama vile Yohana 17:11; 1 Pet. 1:156-16; Ufu. 4:8; 6:10), watoto Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Law. 11:44-45; 19:2; 20:7,26; Mat. 5:48; 1 Pet. 1:16). Kwa kuwa Yesu ni mtakatifu, wafuasi Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Cor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15). Wakristo wameokolewa ili kutumika katika ufanano wa Kristo (wenye utakatifu).

5:13 "fanya kazi" Sheria zilizoko kwenye mistari ya 13-14 zimesababisha ukuaji wa mapokeo kwa njia ya simulizi (k.v. Mt. 5:21-48) kuandikwa kwa sababu swali kama, "kazi ni nini?" likawa la muhimu. Walimu wa sheria wakatunga ufafanuzi ili Wayahudi waaminifu wasije wakavunja sheria. Utata wa sheria iliyoandikwa ulisababisha uhalalishaji wa sheria sioandikwa kuanza.

5:14 "siku ya saba ni sabato" Sabato ilikuwa ni siku ya mapaumziko (BDB 992). Kuna sababu mbili zilizotolewa kwa ajili ya sabato: (1) Kutoka 20:11 inaelekeza kwenye Mwanzo 1-2, wakati Kumbukumbu la Torati linaelekeza kwenye ukandamizwaji wa Wamisri (k.v. 5:15). Ikajakuwa ni alama ya agano (kama ilivyo tohara) la watu wa YHWH (k.v. Kut. 31:13,17; Ezek. 20:12,20). Utii ulikuwa ni wa lazima (k.v. Isa. 56:2; 58:13; Yer. 17:21-22). Kama lilivyo jua na mwezi (k.v. Mwa. 1:14) sabato ilileta mgawanyo wa muda kwa ajili ya shughuli za kibinadamu (k.v. Mhubiri 3). Siku ya saba ya juma ikajakuwa ni namna ya kuzingatia siku na miaka maalum (k.v. Kutoka 23 na Mambo ya Walawi 23). Hasa, sabato ilianza Ijumaaa jioni na kwenda hadi Jumamosi jioni, kwa sababu Waisrael waliizingatia siku aina ya siku katika Mwanzo 1 ("jioni na asubuhi," k.v. Mwa. 1:5,8,13,19,23,31).

5:15 "Uikumbuke" Tazama maelezo katika 7:18.

☐ **"kuwa wewe ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri"** Musa alitumia uelewa huu wa utumwa ili kuwasababisha Waisraeli kuwaonea huruma watu wa hali ya chini katika jamii:

1. Kuwapa watumwa (na wanyama) siku ya mapumziko - 5:12-15; 16:12
2. Kuwaweka huru na kuwawezesha watumwa wa Kibrania - 15:12-15
3. Kuwa sawa na haki na wale wa hali ya chini na kutowanyima haki ya uraia - 24:17-18
4. Kuacha sehemu ya shamba na mavuno ya mazao ya mara ya pili kwa maskini - 24:19-22

Kifungu hiki pia kinatumika mara nyingi kuwaonya Israeli kutenda ipasavyo katika nuru ya rehema ya YHWH Yeye aliyewapa nchi (mf., 6:10-15) na kulitii agano (mf., 8:1-10) ili madhara yasipate kuwajilia (mf., 8:11-20)

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA):5:16

¹⁶Waheshimu baba yako na mama yako; kama Bwana, Mungu wako, alivyokuamuru, siku zako zipate kuzidi, nawe upate kufanikiwa katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.

5:16 "Waheshimu" KITENZI (BDB 457, KB 455, *Piel* KAULI SHURUTISHI) mwanzoni kabisa lilimaanisha "mtu mwenye uzito mkubwa" na kuanzisha maana ya ki-istiari ya neno "kuleta usawa" au "heshima." Heshima hii haijikiti juu ya makubaliano, bali ni kwa mamlaka na heshima. Katika maana hiyo inaleta uhusiano kati ya Mungu

na mwanadamu. Tabia ya kunyenyekea chini ya mamlaka ni ya muhimu katika maisha ya kidini! Yesu alizitaja hizi amri mara kadhaa vile vile pia katika baadhi ya sehemu za Kumbukumbu la Torati:

1. 5:16 - Mt. 15:4; Marko 7:10
2. 5:16-20 - Mt. 19:18-19a; Marko 10:19; Luka 18:20
3. 5:17 - Mt. 5:21
4. 6:4-5 - Mt. 22:37; Marko 12:29-30; Luka 10:27
5. 6:13 - Mt. 4:10; Luka 4:8
6. 6:16 - Mt. 4:7; Luka 4:12
7. 19:15 - Mt. 18:16
8. 19:15 - Mt. 5:38

Pia Paulo alidondoa kitabu cha Kumbukumbu la Torati mara kadhaa:

1. 5:16 - Efe. 6:2-3
2. 5:21 - Rum. 7:7
3. 19:15 - II Kor. 13:1
4. 21:23 - Gal. 3:13
5. 25:4 - II Kor. 9:9; I Tim. 5:18
6. 27:26 - Gal. 3:10
7. 30:12-14 - Rum. 10:6-8
8. 32:21 - Rum. 11:8
9. 32:35 - Rum. 12:19-20
10. 32:43 - Rum. 15:10 (k.v. Richard N. Longenecker, *Biblical Exegesis in the Apostolic Period*, kr. 42-43, 92-95). Inavyoonekana waandishi wa agano Jipya walitumia Agano la Kale kwa upana, lakini sio kwa kushikilia sheria!

☛ **“na mama”** Hii inaonyesha upendeleo mkubwa upande wa mama hata katika jamii ya kimashariki wanawake kisheria walikuwa sawa katika mgao wa mali. Mama wa Kiebrania aliheshimika nyumbani kwake. Amri ya wazazi iliheshimika sana (k.v. Kut. 21:17; Kumb. 27:16). Wote walitakiwa kuheshimiwa (k.v. Mith. 1:8; 6:20; 15:20; 19:26; 20:20; 23:22-25; 30:11,17).

☛ **“ili siku zako zipate kuongezeka”** Mstari wa 33; 4:40; 11:9 unaonyesha kuwa hii ilikuwa ni ahadi kwa jamii, kimsingi sio kwa mtu mmoja. Kama jamii itaainishwa kwa heshima nyumbani na kuyaheshimu maisha ya familia, hiyo familia itakuwa imara na ya kudumu kwa muda wote. Tazama maelezo katika 4:40.

5:17-21 Hizi ndiyo sheria zilizoenea kwenye jamii ya kimashariki. Kwenye ugunduzi wa maeneo ya elimukale tunatambua mfumo wa sheria za Kibabeli ya Lipit-Ishtar na Hammurabi ambazo zilikuwepo mapema zaidi ya sheria ya Musa kwa miaka mingi. Mfumo wa sheria za Hammurabi unafanana na ule wa amri kumi. Ufanano huu unaonyesha kuwa (1) kiasili kuna baadhi ya vitu ambavyo haviko sawa katika hali zote na kwa jamii na (2) kuwa Musa alikuwa bado mdogo kipindi chake na mstaraabu vile vile pia nabii wa Mungu.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:17

¹⁷Usiue.

5:17 “usiue” KITENZI cha Kiebrania cha neno “usiue” (BDB 953, KB 1283, *Qal KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU*) mwanzoni kabisa kilimaanisha “kugandamiza kwa nguvu.” Uzima ni mali ya Mungu. Hii haimaanishi kuua chochote kwa sababu Israeli ilikuwa na adhabu ya kifo (mf., Hes. 35:30) na vita takatifu (mf., 20:13,16-17). Amri inasema “usiue kwa sababu yeyote wala kurudisha kisasi” au “usiue kwa kukusudia.” Kwa maoni yangu fungu hili la maneno haliwezi kutumika kama maonyo ya kibiblia dhidi ya huduma za kijeshi au adhabu ya kifo.

MADA MAALUM: UTAMBUZI WA KUTOKA 20:12-17 (AMRI KUMI ZA MUNGU)KUTOKA 20:13, USIUE (BDB 953, KB 1283)

I. MUKTADHA

- A. lazima ikumbukwe kuwa hata sheria zilizoonekana kuwa za asili kiukweli ni za kidini. Ukuu wa Mungu juu ya uumbaji na ukombozi unafunikwa katika amri hizi. Amri hii usiue, ipo katika mtizamo sahihi, neno kuhusu mfano wa Mungu ndani ya kila mwanadamu na uangalizi wa Mungu na uhusika kwa ajili ya maisha ya mwanadamu.
- B. inahitaji kukumbukwa kuwa kila amri inaaksi jamii ya wenye imani. Katazo juu ya kuuondoa uhai kwa namna isiokubalika ni ya kimsingi na mwanzoni ilitazamwa na jamii iliyoamini. Uhusika wake ni mpana kama wa mwanadamu!

II. USOMAJI WA NENO WA ISTILAHU KUU

A. "Usiue"

- 1. Hili ni neno adimu (rasah, BDB 953, KB 1283) kwa ajili ya kuuondoa uhai, lililotumika mara 46 tu katika Agano la Kale. Kuna maneno mengine mbalimbali ya Kiebrania yaliyotumika mara mia.
- 2. Neno (*rasah*) linaonekana kuwa na maana ya asili isiyo kamili na maana pana.
 - a. Mwanzoni ilihusiana na kuuondoa uhai wa mwenza wa agano kwa njia ya kisheria, iliyokusudiwa, mara nyingi likihusiana na "mwokozi wa karibu" au "*go'el*." Utumikaji huu unahusisha udhamiraji lakini kwa maana kulipa kisasi kisheria (k.v. Hes. 35:30-34; Law. 24:13-23). Kiukweli neno *Lex Talionis*, "jicho kwa jicho," (k.v. Mwa. 9:5-6) ilikuwa ni namna ya kuzuia ulipaji kisasi. Baadaye, miji ya makimbilio (Kumb. 4:41; Yosh. 20:3) ilianzishwa ili kwamba jamaa wa agano ambaye kwa bahati mbaya akamuua mwingine kwenye hiyo jamii aweze kukimbilia huko ili kuikwepa ghadhabu ya familia iliyoumizwa.
 - b. Baadaye neno likaja kurejelea kwenye kusudi au tabia kinyume na kuuchukua uhai wa mtu. Dhana ya "kimakusudi" ikajakuwa ya kiwango cha juu! (k.v. Kut. 21:12-14; Hes. 35:11,22; Kumb. 28:24).
 - c. Utofauti huu ukajakuwa ni wa muhimu katika amri hii. Linaonekana kwenye muktadha kuwarejelea wengine ndani ya jamii ya agano. Linahusiana na kisasi cha damu au mwokozi wa karibu. Hata hivyo, neno linatumika kwenye vifungu vingine vyenye kuaksi amri kumi za Mungu, Hosea 4:2 na Yeria 7:9, zinarejelea kwenye mauaji. Hili neno linahusiana sio tu kwenye sheria bali kwenye kusudio. Linatanuka toka jirani hadi jamaa wako wa karibu.
- 3. Hakika neno halihusiani na masuala ya mfumo wa maadili wa leo wa adhabu ya kifo. Wayahudi hawakuwa na tatizo na utekelezaji kwenye jamii au vita takatifu (au, kwa suala hilo, vita isiotakatifu!).
- 4. tafasiri nzuri kwa ajili ya jamii zetu za leo ingalikuwa ni "mauaji ya kukusudia."

III. TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Amri ya sita, ya saba, nay a nane imeundwa na maneno mawili ya Kiebrania. Ni mafupi na yenye kulenga pointi.
- B. Maisha, kama yalivyo maisha mengine, yanahusiana na Mungu. Namna tuwatendeavyo wengine kunalenga fikra zetu kumhusu Mungu

IV. MIFANANO YA AGANO JIPYA

A. Yesu

- 1. upanuzi wake wa sheria hii (k.v. Mt. 5:21-26) unatupatia mwelekeo sahihi kwa ajili ya mijadala kuhusu naman ya kutumia andiko hili kwenye siku zetu za leo.
- 2. Hakika Yesu aliziondoa amri kumi toka kwenye utawala wa matendo kwenda utawala wa kusudio. Tuko hivi kwa namna tuwazavyo! "kile afikiravyo mtu moyoni mwake, ndicho kimjaacho." Maisha ya kufikilia ni ya maana na muhimu zaidi kuliko kile tukitoacho kwa sifa.

B. Yohana

1. 1 Yohana. 3:15, dhana ile ile ya chuki ifikiliwayo kama mauaji imeelezewa.
2. Maneno ya Kiyunani yaliyotumika katika Mathayo 5:21na kuendelea na 1 Yohana 3:15 ni tofauti lakini maana yake ni ile ile.
3. Tazama kwa namna chanya katika 1 Yohana 4:19-21.

V. KWELI KUHUSU UTUMIAJI WAKE

- A. Hata kama mauaji yasio ya kukusudia yanaweza kumkwepa mlipa kisasi wa damu kwa kukimbilia katika mji wa makimbilio (k.v. Hesabu 35; Yoshua 20), analazimika kupewa adhabu ya kukaa kizuizini kwenye mji huo mpaka pale Kuhani mkuu atakapokufa. Madhara ya kitendo chake alichotenda yataendelea kubaki!
- B. Ingawa mstari huu huu hauhusiani moja kwa moja na mauaji, kama ilivyo watu wa kale yumkini hawakufikiria hili tukio, andiko bado linatupatia kanuni ya kiroho kuhusiana na utakaso wa maisha ya mwanadamu na ukuu wa Mungu na kukusudia kwa ajili maisha ya mwanadamu katika sura Yake. Hili andiko linazungumza neno zito kwa ajili ya siku zetu za leo katika eneo hili!
- C. Andiko, hata hivyo halizungumzii neno la maana kwenye maswali ya leo ya: (1) adhabu ya kifo (2) vita. Kwa ajili ya Israeli, hivi havikuwa vitu viovu kwao. Waisraeli walijihusisha kwenye matendo haya yote mawili. Bado, kanuni ya maana ya maisha iliyotengenezwa ndani kwa sura ya Mungu na chini ya udhibiti wake ni kweli muhimu katika eneo hili.
- D. Andiko linalisema neno linalohitajikalo kuhusu utu na utakaso wa maisha ya mwanadamu! Sisi tuliopo katika jamii inayoamini ni watumishi, sio tu kwa matendo yetu, bali kwa ajili ya jamii yetu. Zawadi ya uzima ni ya wote na binafsi. Tunawajibika kwa ajili ya fedheha ya kimwili, kijamii, na kiakili kama tunavyowafedhehesha wengine kwenye jamii yetu. Hasa hili ni kweli kwenye jamii kama ya kwetu ambapo tunaruhusu kuwasemea na hivyo, tunabadili muundo. Sisi ni waangalizi wa ndugu zetu!

KUTOKA 20:14, USIZINI (BDB 610, KB 658)

I. MUKTADHA

- A. Ni dhahili kwamba sheria zinahusiana na heshima ya mtu kwa ajili ya Mungu ambacho ni kitu kipaswacho kuyaheshimu maisha ya jirani yako, mke, na mali (k.v. Yer. 5:8). Hili linathibitishwa kwa utaratibu tofauti wa hizi amri kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania.
- B. ufanano wa zile za kwenye Kumbukumbu la Torati zinaonyesha ushabihiano wa kuziendeleza kweli hizi za kale kwenye tamaduni zetu.
- C. kuwaheshimu wazazi kulionekana kama suluhisho la jamii iliyoimarika, vivyo hivyo kwetu, hiyo amri.
- D. Amri pia inadokeza umiliki wa Mungu na udhibiti wa maisha yetu ya kindoa na kifamilia.

II. USOMAJI WA NENO

- A. Neno kuu katika andiko hili "usizini." Ni muhimu kuwa mtu aelewe hili neno katika mwanga wa tamaduni za kale za Kiebrania.
 1. Hili neno ni tofauti katika muktadha wa Agano la Kale kwenye neno "uasherati." Kuzini kunahusiana kwa kiasi Fulani na sehemu moja kwenye mahusiano ya kingono na mtu mwenye kuo au kuolewa. Neno "uasherati" linadokeza sehemu zote mbili za wale ambao hawajaoa (k.v. Mith. 29:3; 31:3). Utofauti unapotea kwenye maneno ya Kiyunani ya Agano Jipya.
 2. Uwezekano huu unaelezea sababu kwa ajili ya msisitizo juu ya mambo ya ndoa kwa sababu ya kuhusishwa kwenye umuhimu wa kuwa na haki ambao ulijumuishwa kwenye ahadi za Mungu za kuimiliki "nchi." Kila baada ya miaka 50 (Jubilei) ardhi yote ilirejeshwa kwa wamiliki wa mwanzo (k.v. Law. 25:8-17).
 3. Suala la kuzini kitamaduni lililaaniwa hata kabla ya sheria za Musa (k.v. Mwa. 12:10 na kuendelea; 26:7 na kuendelea; 39:9).
 4. Uzinzi ulionekana kama dhambi dhidi ya:
 - a. Jirani yako – Kutoka 20:14; Kumbu. 5:18
 - b. Ndoa – Law. 18:20

- c. Mungu – Mwa. 20:1-13; 26:7-11
- 5. Adhabu yake ilikuwa ni kifo kwa pande zote mbili:
 - a. Mambo ya Walawi 20:10
 - b. Kumbukumbu la Torati 22:22-24
 - c. Ezeieli 16:40 (stiari)
 - d. Maonyo makali yanapatikana katika Mithali 1-9

III. UHUSIANO WAKE NA AGANO JIPYA

- A. Yesu alitumia Mambo ya Walawi 19:18 kama muhtasari wa ufunuo wa kale (k.v. Luka 10:27). Hili linathibitisha Amri Kumi za Mungu zinahusiana na namna tupaswavyo kuwatendea wengine.
- B. Yesu anazielezea kwa uapana hizi amri katika Mathayo 5:28. Anaweka msisitizo juu ya makusudio kuliko kitendo. Wayahudi waliona mawazo kama kitalu cha nafsi . kile mtu alichofikiri ndicho kilichomjaa moyoni mwake (Mith. 23:7). Hili linazifanya amri kumi kiwastani kuwa ngumu kuzifuata—hilo ndilo kusudi! (k.v. Gal. 2:15-3:29).

IV. MATUMIZI YA LEO

- A. Yumkini ndoa ni mfanano mzuri wa leo wa ukiri wa maisha marefu ya imani katika jina la Mungu. Ni nafsi yetu nzuri kuelewa ukweli wa dhana ya Agano la Kale (Mal. 2:14). Heshima yetu kwa ajili ya wenza wetu kwa namna zote, ukijumuisha na mambo ya ujinsia wa mwanadamu, unatusaidia kuukabili msukumo wa huu mstari.
- B. Uimara wa ndoa na uaminifu, kama ilivyo kuwaheshimu wazazi, ni nguzo muhimu ya nguvu ya kijamii na muda mrefu
- C. Inahitajika kuisitizwa kuwa tendo la ndoa ni zawadi kutoka kwa Mungu (k.v. Mwa. 1:27,28; 9:1,7). Lilikuwa ni wazo Lake na mapenzi Yake kwa mwanadamu. Miongozo haimanishi kuzuia uhuru wa mwanadamu au furaha bali ni kutoa miongozo ya Kimungu kwa mwanadamu aliyeanguka. Mipaka inadhihirika kwa ajili ya fuaraha na faida zetu za muda mrefu. Ingawa mwanadamu ameridharirisha tendo la ndoa, kwa vile wanazo zawadi zote za Mungu, bado ni kiongozi chenye nguvu ndani ya mwanadamu ambapo inatakiwa kuwa chini ya mwongozo na udhibiti wa Mungu.
- D. Tendo la ndoa lazima lilindwe ili kwamba utakatifu wa mtu (mwanamke au mwanaume) upate kuheshimika kwa sababu wamefanywa kwa sura ya Mungu (Mwa. 1:27). Mitazamo iliyoanguka juu "yangu" yote ni dhahiri katika eneo hili.

KUTOKA 20:15, USIIBE (BDB 170, KB 198)

I. MAELEZO KAMILI

- A. kama zilivyo sheria zingine kwenye amri kumi za Mungu, imani yetu, upendo, na heshima kwa ajili ya Mungu lazima vionekane katika dhana ya utakatifu na maisha yetu ya kila siku duniani. Ni chukizo kwa Mungu kudai kumfahamu Yeye na tena kumnyonya ndugu wako wa agano (k.v. 1 Yohana 2:7-11; 4:20-21).
- B. Amri hii inamaanisha kusaidia kuendeleza ushirika wa jamii ya agano. Thamani ya ushirika huu wa kiroho utawavuta wale waliochanganyikiwa na kuhangaika na ulimwengu kwenda kwake Mungu ambalo ndilo kusudi la maandiko.
- C. Kama zilizo amri zingine zilizoangazia juu ya umiliki wa Mungu wa maisha yote, vile vile nasi, hili pia! Sisi tu watumishi, na sio wamiliki. Misukumo yetu iliyoanguka dhidi ya umiliki, pasipo gharama, upo began a hili katazo (k.v. Zab. 50:10-12).

II. USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

- A. Hii ni amri ya tatu kwenye sehemu ya pili ya amri kumi za Mungu ambayo imeundwa kwa maneno mawili ya Kiebrania.
- B. Kusudi la katazo hili halipo. Hili linaungwa mkono na:
 - 1. Muktadha wa amri mbili za nyuma zenye kuhusiana na makosa makubwa.

2. Uwepo wa vifungu fananishi vyenye kutumika kwa haraka (Kut. 21:16) na kwa baadaye (Kumb. 24:7). Tazama pia Mwanzos 37.
- C. Hata hivyo, maelezo mafupi pia ni yenye kuthibitika
 1. imeandikwa kwa ajili yetu kwa uvuvio
 2. inapanua uwezekano wa katazo
 3. pia pana kifungu fananishi katika muktadha wa papo hapo chenye kufanana na cha wizi—Kutoka 22:1 na kuendelea.
 4. inavyoonekana Yesu alikinukuu kifungu hiki kufanya rejeo la neno usiibe (k.v. Mt. 19:18).
- D. pia wizi ulishughulikiwa kwenye miswaada mingine ya sheria za kale, lakini mara nyingi adhabu yake ilikuwa ni kifo, kukata kiungo cha mwili, au kufanya malipizi mara 30.
- E. kuna baadhi ya vifungu fananishi muhimu ambavyo vinaelezea huu ukweli:
 1. Mambo ya Walawi 19:1-18—"Iweni watakatifu, kwa vile Mimi Bwana Mungu wenu ni Mtakatifu"
 - a. Muundo wetu wa maisha unaaksi tabia za familia ya Baba yetu na Mungu wetu (k.v. Law. 19:18).
 - b. Imani yetu lazima iathiri maisha yetu ya kila siku, katika hali zote kwa matendo chanya na makatazo yaliyo kinyume, yote yakitaarifiwa katika kusudi lililojema (k.v. Law. 19:17).
 - c. Huruma kwa watuchukiao na wahitaji, Law. 19:9-10, 13, ni ya muhimu kama lilivyo katazo la kuwaibia majirani zetu, mst. 11.
 2. Amosi 8:4-7 – Mungu anachukua unyonyaji!
 3. Mika 6:6-8 – Mungu anahitaji makusudio yaliyo mema kwenye matendo yetu yote. Kwa nini hatuibi ni suala jingine!
 4. Kutoka 22:1 na kuendelea – Mara nyingi ukweli usioonekana kwenye mazungumzo yetu ya leo kuhusu wizi wa kutumia nguvu ni kufanya kitubio! Dhambi siku zote hugharimu!

III. MATUMIZI YA LEO

- A. Joy Davidman, C. S. mke wa Lewis, ameandika kitabu chenye kuvutia juu ya amri kumi za Mungu. Aliitafasiri hii amri "usijaribu kujipatia kitu chochote bure ." Hakika hili limetengeneza uwanda mpana zaidi ya kumiliki. Pia akasema kuwa "wingi wa mali sio dhambi wala haki kamili, bali ni mkopo, imani toka kwa Mungu."
- B. Wizi, kama zilivyo dhambi zingine za moyo ulioanguka, unashughulika na moyo mpya (k.v. Yer. 31:31-34; Ezek. 36:26; Efe. 4:28). Inashangaza namna asili ya kale ya neno "chukua" lilivyobadilika kwenda kwenye asili mpya ya neno "mgawo"!
- C. Heshima yetu kwa Mungu kwa uwazi inaonekana namna tunavyowaheshimu ndugu zetu wa agano! Ukweli huu unafunika amri za Mungu.
- D. Watu walioanguka wanaiba kwa namna nyingi!

MASWALI YA MJADALA

1. Ni kwa namna gani watu wa leo wanatenda wizi?
2. Ni kwa namna gani neno malipizi linahusiana na neno toba?
3. Ni kwa namna gani huu mstari unahusiana na mtizamo wa kibepari wa kumiliki mali nyingi?

UTOKA 20:17, USITAMANI (BDB 326, KB 328)

I. UTANGULIZI

- A. Inawezekana kuona uhusiano kati ya amri tano za mwisho kama ifuatavyo:
 1. Hesabu 6, 7, na 8 inazuia majeraha ya ndugu wa agano katika kitendo chenyewe.
 2. Hesabu 9 inazuia majeraha ya ndugu wa agano katika hotuba.
 3. Hesabu 10 inazuia maumivu ya ndugu wa karibu katika fikra.
- B. Ni kweli kwamba tendo la kutamani humvuruga yule mtu atamaniye, na sio mlengwa mwenyewe,

ambaye ni jirani. Hata hivyo, inawezekana kuwa hii amri inatarajia mawazo yatazidi matendo.

- C. Wengi wanaitazama hii amri kama dhana pekee inayopatikana pekee katika mfumo wa sheria za kale za Israeli na haipo kwenye mifumo ya sheria za Mashariki ya Karibu ya Kale. Dhana hii mpya ingalikuwa ni katazo la mawazo. Ni kweli kwamba Israeli inatabiri maisha ya kuwaza kuwa ndicho chanzo cha matendo maovu (k.v. Mith. 23:7; Yakobo 1:14-15). Hata hivyo, huu mstari unaonekana kuhusiana kwenye mawazo ambayo hutokea katika matendo.

Vifungu mbalimbali vinavyotumia neno "tamani" vikihusianishwa na matokeo ya tendo (k.v. Kumb. 7:25; Yos. 7:21; Mika 2:2).

- D. Ni kweli kwamba msisitizo umewekwa kwenye kile kilichoorodheshwa kwanza na cha mwisho, kweli muhimu ya hii amri inaonekana. Ibada maalum ya kumwabudu Mungu ndio kipaumbele, lakini mienendo na makusudio dhidi ya vitu vya ulimwengu huu vinaathiri kule kujitoa kwetu kwa Mungu. Hii misisitizo pacha pia inaonekana katika hotuba za Yesu pale mlimani, Mt. 6:33 —"Bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake; na vitu (k.v. mistari. 19-32) mtazidishiwa."

II. USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

- A. Kutoka 20:17 na Kumbukumbu la Torati 5:21, ingawa kimsingi inafanana, lakini zina tofauti mbalimbali za msingi:
1. Mke anajumuishwa kwenye dhana kubwa ya "nyumba" au mali ya mtu katika kitabu cha Kutoka 20, akiwa amewekwa pembeni huku, amewekwa kama kipaumbele, katika Kumbukumbu la Torati 5.
 2. Kifungu kwenye kitabu cha Kutoka 20 kina neno la Kiebrania "kutamani" ambalo humaanisha "shauku ya kupata," lakini Kumbukumbu la Torati 5 lina neno la pili, "tamaa" (BDB 16, KB 20), vile vile pia "kutamani." Neno "kutamani" linazungumza kuhusu tamaa inayohusiana na kitendo cha kupata kitu kilichotamaniwa lakini neno "tamaa" linaonekana kulenga juu ya tabia pekee.
 3. Pia, Kutoka 20, iliandikwa kwa wana wa Israeli wakati wa kipindi cha kutangatanga jangwani, haitaji "eneo" kwenye orodha ya umiliki, wakati Kumbukumbu la Torati 5 inarudia amri ile ile kwa ajili ya jamii iliyokaa katika nchi ya ahadi.
- B. Neno "kutamani" ni neno lisilo na upande wowote. Laweza kurejelea kwenye tamaa ya vitu (k.v. Zab. 19:10; 1 Kor. 12:31).
- C. Tamaa isiyosawa ndiyo chanzo cha anguko la shetani, Adam na Hawa, na sisi sote. Paulo anahofu mapambano yake binafsi na neno kutamani katika Warumi 7:7-8. Kutamani ni hali ya kutotosheka na ukosefu wa imani katika utoaji na uangalizi wa Mungu.
- D. Vifungu mbalimbali vya Agano Jipya vinavyohusiana na neno kutamani:
1. Jilindeni na choyo, maana uzima wa mtu hauko katika wingi wa mali (k.v. Luka 12:15; 1 Tim. 6:8-10).
 2. Kutamani kumejumuishwa kwenye orodha ya dhambi zinazomnajisi mtu (k.v. Marko 7:17-23; 1 Kor. 5:10; Efe. 5:5; Kol. 3:5).

III. MATUMIZI YA LEO

- A. Suluhu ya uchoyo na kutoridhika ni:
1. Upendo – Rum. 13:8-10
 2. Kuwa radhi na vitu ulivyonavyo – Ebr. 13:5; Fil. 4:11-13 (mkishirikiana, Fil. 4:14)
- B. Amri inasema "usifanye" lakini Kristo pekee ndiye atupaye namna ya kujizuia kutofanya hayo! Ndani Yake tunaweza kuyazuiya fikra mbaya za kimaisha kwa kiwango fulani.
- C. Mungu anajua mioyo na mawazo yetu
1. 1 Nyakati 28:9
 2. Mithali 20:27
 3. Zaburi 139:1,23
 4. Yeremia 17:10

5. Warumi 8:27

6. Ufunuo 2:23

- D. Kuwa na mali sio dhambi, lakini pale tunapoipa kipaumbele inakuwa dhambi. Mali sio hatma ya maisha yetu; watu walioumbwa kwa sura ya Mungu ni wa milele! Kutamani kunaathiri jamii ya agano kwa namna ya uharibifu!

IV. MAELEZO YA NYONGEZA TOKA KUMBUKUMBU LA TORATI 5:21:

Kumbukumbu la Torati 5:21, "usitamani. . wala usitamani," hutumia VITENZI viwili ambavyo ni visawe:

- A. "kutamani" – BDB 326, KB 325, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, ikimaanisha "kuwa na shauku iliyo kubwa" kwa ajili ya kuwa na mali, ambayo yaweza kuwa nzuri au mbaya. Katika muktadha huu ni ile isiyodhuria, shauku binafsi kwa ajili ya kitu Fulani ambacho ni mali ya ndugu wako wa agano.
- B. "tamaa" – BDB 16, KB 20, *Hipthrael* KAULI ISIO TIMILIFU, ikimaanisha "shauku kubwa" (k.v. Kumb. 14:26) au "ashiki" (mara nyingi lina muktadha wa tendo la ndoa kama ilivyo katika 5:21) zaidi na zaidi kwa ajili yangu kwa gharama yeyote (mf., Hes. 11:4; Zab. 106:14; Mith. 13:4; 21:26; 23:3,6; 24:1).

Hili linahusiana na mwenendo na makusudio ya dhambi ya mtu. Ni mhimili wa amri zote. Hii ndiyo amri pekee inayoshughulika na swali la kwa nini, na wala sio ni kwa namna gani. Hili linasema sio tu "usitende" bali "hata usiliwazie hili." Yesu akafundisha kuwa sio tu tusiue, bali tusiweke chuki, au kuonyesha hali yoyote inayoweza kusababisha kuuu. Yesu aliichukua hii amri ya mwisho na kuziinua amri zingine zilizobaki kwenye kiwango cha makusudio ya ndani na mienendo kama ilivyo juu dhidi ya tendo la nje (k.v. Mt. 5:17-48). Kote duniani kuna tofauti kati ya mtu ambaye haibi kwa sababu ya kumpendeza Mungu na yule ambaye haibi kwa sababu anaogopa kukamtwa. Mmoja anatenda hili kwenye kanuni za Ukristo na mwingine anatenda kwa sababu ya matakwa yake mwenyewe.

MASWALI YA MJADALA

1. Nini maana ya kutamani?
2. Ni kwa namna gani mtu anatamani?
3. Je mawazo yako yanatenda dhambi?
4. Kwa nini mawazo ni ya muhimu katika maisha ya Mkristo?
5. Kwa nini amri iliyopo kwenye Kutoka 20:17 kwa namna Fulani ni tofauti na ile iliyoko kwenye Kumbukumbu la Torati 5:21?

MADA MAALUM:AMANI NA VITA

- I. Utangulizi
 - A. Biblia, chanzo chetu pekee kwa ajili ya imani na utendaji, haina kifungu kamili chenye kuelezea juu ya amani (tazama Mada Maalum: Amani [Agano la Kale] na Mada Maalum: Amani [Agano Jipya]). Hakika, neno hili ni la kimafumbo katika uwasilishaji wake. Agano la Kale laweza kudokezwa kama mkabala wa amani pasipo na vita. Agano Jipya, hata hivyo, huleta mgongano kwenye maneno ya ndani ya kiroho kuhusiana na nuru na giza (yaani., Efeso. 2:2; 6:10-17).
 - B. Imani ya kibiblia, vile vile dini za ulimwengu zilizopita na zilizopo, zihitajikazo na zinazotarajiwa, ni kipindi adhimu cha mafanikio ambacho hakipo katika migongano.
 1. Isaya 2:2-4; 11:6-9; 32:15-18; 51:3; Hosea 2:18; Mika 4:3
 2. nabii za imani za Biblia ni wakala binafsi wa Masihi, Isa. 9:6-7

C. Hata hivyo, namna gani tunaishi kwenye ulimwengu tuliomo wa machafuko? Pamekuwepo na majibu mbalimbali ya Kikristo ambayo yamejitokeza ya kupanga matukio kati ya kifo cha Mitume na zama za kati.

1. Hali ya upatanishi– ingawa ni adimu kwenye mambo ya kale, ilikuwa ni wajibu wa kanisa la mwanzo kwenye jamii ya kijeshi la Rumi.
2. vita ya haki– baada ya kuongoka kwa Constantine (313 B.K) kanisa lilianza kupunguza uungaji mkono wa kijeshi kwa “serikali za Kikristo” katika kujibu mavamizi ya kikatili/kishenzi. Hili kimsingi lilihusiana na tamaduni na elimu ya Wayunani. Eneo hili mwanzoni lilitamkwa na Ambrose na kuenezwa hatimaye kuendelezwa na Augustino.
3. vita vitakatifu – hili linafanana na dhana ya vita takatifu ya Agano la Kale. Iianza kwenye kipindi cha kati kuwajibu Waislamu walioikabili "Nchi Takatifu" na himaya za kale za Kikristo huko Afrika Magharibi, Asia Ndogo, na ngome za Mashariki za Rumi. Haikuwa kwa niaba ya serikali, bali kwa niaba ya kanisa na wale waliounga mkono.
4. Hii mitazamo yote mitatu ilikuwa katika muktadha wa Kikristo ikiwa na mitazamo tofauti namna Wakristo wanavyopaswa kuhusiana na muundo wa ulimwengu ulioanguka. Kila moja ilisisitiza maandiko ya Biblia Fulani kutofautiana na nyingine. Hali ya upatanishi ilijaribu kujitenga yenyewe. Uwajibikaji wa "Vita ya Haki" umetetea mamlaka ya kiserikali kuudhibiti ulimwengu wa maovu (Martin Luther). Nafasi ya Vita Vitakatifu vimeweza tetea kwamba mavamizi ya kanisa ni anguko la muundo wa kanisa kuweza kutawaliwa.
5. Roland H. Bainton, katika kitabu, *Christian Attitudes Toward War and Peace*, kilichochapishwa na Abingdon, ukurasa wa 15, anasema, "Mageuzi yaliharakisha vita ya kidini, ambapo nafasi tatu za kihistoria zikajitokeza tena: vita ya haki kati ya Warutheri na Wangirikana, vita vitakatifu ndani ya makanisa yaliongoka, na hali ya upatanishi kati ya vuguvugu la Kikristo wenye kuitafuta kweli na baadaye kikundi cha Kikristo cha vuguvugu za kidini. Karne ya kumi na nane nadharia na utendaji ilichochea mawazo ya amani ya kibinadamu ya kuzaliwa upya. Karne ya kumi na nane kilikuwa ni kipindi cha amani shirikishi na maandamano makubwa ya kuviondoa vita. Karne ya ishiringi ilifanikiwa kuwa na vita kubwa mbili. Katika kipindi hiki, nafasi tatu za kihistoria zinajitokeza tena. Makanisa huko Amerika hasa yakachukua mtazamo wa vita vitakatifu dhidi ya vita vya kwanza vya ulimwengu; hali ya upatanishi ilikuwa ya kawaida kati ya vita mbili hizi; mazingira ya vita ya pili ya dunia ilikadiriwa kuwa vita ya haki."

D. maelezo kamili ya neno "amani" hayajulikani.

1. kwa Wayunani linaonekana kurejelea kwenye jamii ya utaratibu na kushikamana.
2. Kwa Warumi lilikuwa ni kutokuwepo kwa migongano iliyoletwa na mamlaka ya kiserikali.
3. Kwa Waebrania neno amani lilikuwa ni zawadi ya YHWH iliyojikita juu ya uwajibikaji mzuri wa mwanadamu kwake Yeye. Mara nyingi lilitumika kwenye maneno ya kilimo (k.v. Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 27-28). Sio tu mafanikio, bali ni katika ulinzi na uslama wa Kiungu kwa pamoja.

II. Nyenzo za Kibiblia

A. Agano la Kale

1. Vita Takatifu ni dhana ya kimsingi ya Agano la Kale. kifungu "usiue" ya Kut. 20:13 na Kumb. 5:17 katika Waebrania kinarejelea kwenye mauaji ya kukusudia (BDB 953; tazama Mada maalum: Mauaji), na sio kifo cha ajali au hisia kali au vita. YHWH anaonekana shujaa kwa niaba ya watu wake (k.v. Yoshua, Waamuzi na Isa. 59:17, vinadokezwa kwenye Efe. 6:14).
2. Mungu hutumia vita kuwaadhibu watu wake wakaidi – Ashuru inaifukuza Israel (722 B.K); Babel Mpya inamfukuza Yuda (586 K.K.).
3. Inasikitisha, katika namna ya mazingira ya kijeshi, kumsoma "mtumishi atesekae" wa Isaya 53, ambaye aweza kuainishwa kama mpango wa upatanishi.

B. Agano Jipya

1. Katika injili wanajeshi wanatajwa pasipo kutiwa hatiani. "watu wa umri mkubwa" huko Rumi wanatajwa mara nyingi na karibu mara zote katika maana njema.

2. Hata wanajeshi walioamini hawaamrishwi kukata tamaa kwenye kazi zao (kanisa la mwanzo).
3. Agano Jipya halitetei jibu kamili kwenye uovu wa kijamii kwa niaba ya nadharia za kisiasa au matendo, bali katika ukombozi wa kiroho. Mtazamo sio juu ya vita ya kimwili, bali kwenye vita ya kiroho kati ya nuru na giza, mema na mabaya, upendo na chuki, Mungu na shetani (Efe. 6:10-17).
4. Amani ni hali ya moyo katikati ya matatizo ya ulimwengu. Linahusiana hasa na uhusiano wetu na Kristo (Rum. 5:1; Yoh 14:27), na sio serikali. Wapatanishi wa Mt. 5:9 sio watu wa siasa, bali watangaza injili! Ushirika, na sio magomvi, lazima uainishe maisha ya kanisa, kwake na kwa ulimwengu uliopotea.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:18

¹⁸Wala usizini.

5:18 “usizini” Katika agano la kale neno kuzini (BDB 610, KB 658, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU) linarejea vitendo vya kujamiiana nje ya ndoa. Hili lilikuwa ni kosa kubwa kwa sababu ya mitizamo ya Agano la Kale la maisha baada ya kufa. Waliamini kuwa kwa namna fulani mtu aliishi wakati wa kizazi chake. Pia, umuhimu wa kurithi makabila na kupita kwenye nchi waliopewa na YHWH kufanya uzinzi lilikuwa ni jambo nyeti.

Tambua, amri ya kwanza ni kuwaheshimu wazazi, sheria ya pili ya uaminifu ni kutokuuondoa uhai wa ndugu yako; wazo la tatu ni kuwa mwaminifu maeneo unayoishi. Hata mwanamke aliyechumbiwa alitendewa kama mwanamke aliyeolewa. (k.v. Kumb. 22:23 na kuendelea. Mariam alilaumiwa kwa kutokuwa mwaminifu kwa sababu ya kuchumbiwa na Yusufu.

Wazo la uzinzi mara kadhaa lilitumika kuainisha ibada ya sanamu. Ezekieli na Hosea kimshabihiano wanamwasilisha Mungu kama mme wa Israeli, hivyo basi, mara tu Israel ilipoiendea miungu wengine, ilijulikana kama “kufanya ukahaba” na lilifikiriwa kama uzinzi wa kiroho.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:19

¹⁹Wala usiibe.

5:19 “usiibe” Yumkini hili neno ni marejeo kwenye utekaji na ghiliba (BDB 170, KB 198, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU, k.v. 24:7; Kut. 21:16), kwa sababu ya muktadha wa sheria zilizingira eneo husika. Hili linaelezea uaminifu kwa ndugu wa agano ambaye uzima wake unamhusu Mungu. Sheria zote za maeneo husika zilipelekea adhabu ya kifo. Adhabu hii ilionekana kuwa kali kwa ajili ya wizi wa kudokoa.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:20

²⁰Wala usimshuhudie jirani yako uongo.

5:20 “kushuhudia uongo” Katika jamii za kale, uliposhitakiwa kwa sababu ya kitu fulani, ilikuwa ni wajibu wa mshitakiwa kudhihirishia mshitaki kuwa hana kosa kuliko taratibu za mahakama zetu za leo huku Amerika za kumdhania mtu kutokuwa na kosa mpaka pale atakapotwa hatiani. Ilipothibitika kuwa mshitaki kakusingizia kutenda kosa hivyo mshitaki alipaswa kubeba adhabu ya kosa alilokushitakia. (k.v. 19:16-21). Kwa sababu kuzikaidi amri kumi zilisababisha kifo, kuushuhudia uongo lilikuwa ni kosa kubwa! Kutoa ushuhuda wa uongo ulidhihirisha kutokuwa mwaminifu kwenye jamii ya waaminio. Uongo huangamiza tabia njema na kuyachukua maisha ya asiyo na hatia ya dada au ndugu wa agano. Na Mungu hushughulika na uongo kwa nguvu zote (k.v. Ayubu 17:5; Zab. 101:5; Mit. 11:9; Yer. 9:8-9).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:21

²¹Wala usimtamani mke wa jirani yako; wala usitamani nyumba ya jirani yako, wala shamba lake, wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala kitu cho chote alichu nacho

5:21 “usimtamani. . .wala usitamani” Hivi VITENZI viwili ni visawe:

1. “kutamani” - BDB 326, KB 325, *Qal* KAULI ISITIMILIFU, kunamaanisha “shauku kubwa” kwa ajili ya mambo ya kindoa, ambapo inaweza kuwa kweli au si kweli. Katika muktadha huu ni shauku binafsi, isiozuilika kwa ajili ya kitu Fulani toka kwa ndugu wako wa agano.
2. “kutaka” - BDB 16, KB 20, *Hipthrael* KAULI ISITIMILIFU, kunamaanisha “kutaka” (k.v. 14:26) au “tamaa” (mara nyingi lina muktadha wa mambo ya kujamiiana kama ilivyo katika 5:21) zaidi na zaidi hasa kwa ajili yangu kwa gharama yeyote (mf., Hes. 11:4; Zab. 106:14; Mith. 13:4; 21:26; 23:3,6; 24:1).

Hili linahusiana na mienendo na misukumo ya ndani ya mtu. Ni muhimili wa amri zingine zote. Hii ni amri pekee inayoshughulika na swali kwa nini, na wala sio ni kwa namna gani. Mtu anaweza kuseama sio tu “usitende” bali “usirifikilie hili.” Yesu alifundisha kuwa hatupaswi kuua, hatupaswi kuwachukia wenzetu, au mwenendo wenye kupelekea mauaji. Yesu alichukua amri hii ya mwisho na kuziongeza amri zingine zilizobaki kwenye ngazi ya kusudi na mwenendo wa ndani kuwa juu dhidi ya tendo la nje (k.v. Mt. 5:17-48). Kuna tofauti ulimwenguni ndani ya mtu ambaye hapendi kuiba kwa sababu haimpendezi Mungu na mtu Yule asiyependa kuiba kwa sababu ana hofu ya kukamatwa. Mtu hutenda kwenye kanuni za Kikristo na mwingine hutenda kwa matakwa yake mwenyewe.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 5:22-27

²²Haya ndiyo maneno ambayo Bwana aliwaambia mkutano wenu wote mlimani kwa sauti kuu toka kati ya moto, na wingu, na giza kuu; wala hakuongeza neno. Akayaandika juu ya mbao mbili za mawe, akanipa. ²³Ikawa, mlipoisikia sauti ile toka kati ya giza, na wakati uo huo mlima ule ulikuwa ukiwaka moto, basi, mlinikaribia, naam, wakuu wote wa kabila zenu, na wazee wenu, ²⁴mkasema, Tazama, Bwana, Mungu wetu, ametuonyesha utukufu wake, na ukuu wake, nasi tunasikia sauti yake toka kati ya moto; mmeona leo ya kuwa Mungu husema na mwanadamu, naye akaishi. ²⁵Sasa basi, mbona tufe? Maana moto huu mkubwa utatuteketeza; tukiisikia tena sauti ya Bwana, Mungu wetu, tutakufa. ²⁶Maana katika wote wenye mwili ni nani aliyeisikia sauti ya Mungu aliye hai, akisema toka kati ya moto, kama vile sisi, asife? ²⁷Enenda karibu wewe, ukasikie yote atakayoyasema Bwana, Mungu wetu; ukatumbie yote atakayokuambia Bwana, Mungu wetu; nasi tutayasikia na kuyatenda.

5:22 “wala hakuongeza neno” Amri kumi (amri kumi za Mungu) na maelezo yake yote yanatoka kwa YHWH, na sio kwa Musa (linganisha Kut. 31:18 na 34:27-28). Huu ufunuo (toka kwa Mungu), sio ugunduzi wa mwanadamu au suala la uwiano. kifungu “wala hakuongeza neno” kiuhalisia ni namna ya kutetea ufunuo kamili (k.v. 4:2; 12:32). Mistari ya 22-27 inarejelea kwenye tukio la Israeli katika Mlima Horebu/Sinai na kuandikwa katika kitabu cha Kutoka 19-20. Ufunuo huu lazima uheshimiwe na kutoingiliwa kwa namna yeyote (k.v. 4:2; 12:32; Mith. 30:6; Mhu. 3:14).

5:23 “wakuu wote wa makabila zenu, na wazee” Wazee walimwendea Musa kwa sababu walipatwa na hofu (k.v. mistari ya. 25-26; Kut. 19:16,18; 20:18-20) kwa kujidhihirisha kimwili kulikoendana na uwepo wake binafsi wa YHWH katika Mlima Horebu/Sinai.

5:24 “utukufu wake na, ukuu wake” Mzizi wa neno la Kiebrania “utukufu” (BDB 458) unafanana na mzizi wa neno “heshima” (BDB 457) wa mst. 16. Yote ni maneno ya kibiashara yenye kumaanisha “kitu kizito” au “chenye kuwa na uzito,” ambalo lilikuwa likimaanisha heshima. Linatumika mara kadhaa kulihusu jina la Mungu (mf., Zab. 29:2; 66:2; 79:9; 96:8), mtu (mf., Kut. 24:16-17; 33:18,22; 40:34-35; Hes. 14:22), na matendo (mf., Kut. 16:7,12). Neno la pili “ukuu” (BDB 152) mara kadhaa limetumika kumhusu Mungu katika Kumbukumbu la Torati (k.v. 3:24; 5:24; 9:26; 11:2; 32:3; Zab. 150:2). Tazama maelezo katika 4:31 na 10:17.

MADA MAALUMU: UTUKUFU (AGANO LA KALE)

I. Maana yake ya kimsingi

Kuna maneno yapatayo ishirini yaliyo litafasiri neno “utukufu” (*doxa*) Tafasiri ya maandiko ya kale la Kiyunani, lakini neno la Kiebrania lililo muhimu sana ni *kabod* (BDB 458-459, 455-458). Maana yake ya msingi ni ile ambayo ni nzito. Lilikuwa ni neno la kibiashara lililotumika kwenye ununuzi wa miamala (yaani vipimo). likaja kuwa na elimu-maana kubwa ambapo dhana ya uzito ikajitokeza katika kilo, watu wenye nazo, mahali na vitu.

II. Ilitumiwa na YHWH

- A. ikajakuwa ndo njia ya kuelezea uwepo binafsi wa kumfunua YHWH. Ilijumuisha nguvu zake, uweza wa kifalme (yaani, uliopita mipaka) akiwa na u-mtu wake na uwepo katika umbo la kihalisia.
- B. Ildokeza YHWH katika uumbaji, kama vile Zab. 19:1; 29:3,9; 104:31
- C. Lilitumika katika udhihisho wa wazi wa Mungu kwa mwanadamu likijiungamanisha na utengenezaji wa agano la watu wake. Yeye ni “utukufu wa Israeli”, kama vile 1Sam. 15:29
 - 1) Safari yao ya kutoka Misri kama vile Hes. 14:22 (ilitabiliwa katika Mwa. 15:12-21)
 - 2) Katika wingu la utukufu lililowafunika na kuwaongoza kama vile Kut. 16:7,10
 - 3) Utoaji wa sheria zake katika mlima Sinai
 - 4) Matendo yake ya utoaji na hukumu wakati wa kutangatanga nyikani
 - a. Uwasi wa awali uliohusiana na taarifa ya wapelelezi kumi na mbili, cf. Hes. 14:9-10
 - b. Uingiliaji kati wa Musa kwa niaba yao kama vile Hes. 14:20-21
 - c. Uasi wa Kola kama vile Hes. 16:19
 - d. Mgogoro wa maji, kama vile Hes. 26:6
- D. Ombi la Musa kutaka kumwona Mungu, kama vile Kut. 33:18-23
- E. Lilitumika na YHWH mwenyewe (yaani umuhimu wake)
 - 1) 1Nya. 29:11
 - 2) Zab 106:20; Yer. 2:11; Hos. 4:7; Rum. 1:23
 - 3) Isa. 42:8; 45:7; 48:11; 58:8; 60:1-2,19 (Ufunuo 21:23; 22:5)
 - 4) Zek. 2:5,10
- F. Lilitumika katika muunganikano wa uwepo wa YHWH na/ katika
 - 1) Hema takatifu, kama vile Kut. 16:7,10; 29:43; 40:34-35; Law. 9:6,23
 - 2) Hekalu, kama vile 1 Fal. 8:11; 2 Nyakati 5:14; 7:1-3; Isa. 6:3; Hag. 2:3,9
 - 3) Sanduku la agano, kama vile 1 Sam. 4:22; Zab. 63:2; 78:61
- G. Lilitumika katika ufalme wa YHWH, kama vile 1 Nyakati 29:12-13; Zab. 24:7-10; 45:3
- H. Lilitumika na YHWH katika hali ya kuadilisha (yaani, haki), kama vile Zab. 29:3; 97:6; Isa. 42:8; 48:11; 58:8; Hab. 2:14

III. Lilitumika kwa wanadamu na mataifa

- A. Binadamu
 - 1. Likiendana na “nafsi” (yaani, *nepshesh*) kama vile Mwa. 49:6; Zab. 16:9; 108:1
 - 2. Mali, kama vile Mwa. 31:1; Zab. 49:16,17; Isa. 10:3; 61:6; 66:11-12
 - 3. Heshima, kama vile Mwa. 45:13; Zab. 8:6; Hag. 2:7
 - 4. Sifa njema, kama vile Ayubu 19:9; 29:20; Zab. 4:2; 49:17
 - 5. Uzuri, kama vile 1 Nyakati 29:12,28; 2 Nyakati 17:5; 18:13; 32:27
- B. Mataifa
 - 1) Misri,
 - 2) Efraimu, kama vile Hos. 9:11
 - 3) Samaria, kama vile Hos. 10:5
- C. Wafalme
 - 1) Ahausuero, kama vile Esta 1:4
 - 2) Israeli, kama vile Zab 21:6
 - 3) Antiochus IV, kama vile Dan. 11:39

- D. Majeshi ya mataifa
 - 1) shamu, kama vile Isa. 8:7
 - 2) Israeli, kama vile Isa. 17:4
 - 3) Kedari, kama vile Isa. 21:16
- IV. Lilitumika kwenye maelezo ya siku za mwisho
 - A. YEHOVA atarudi kwenye hekalu lake jipya, kama vile Ezek. 43:2,4,5; 44:4
 - B. YHWH atavuta ulimwengu wote kwake, kama vile Isa. 40:5; 59:19; 60:1-3; 66:18-19
 - C. YHWH ataishusha Yerusalemu “mpya” kama vile Isa. 66:10; Zek. 12:7
- V. Kusudi la uumbaji ni kumtukiza YHWH
 - A. Aliumba kwa ajili ya utukufu wake, kama vile Isa. 43:7
 - B. Utukufu ni juu yake, kama vile 1 Nya. 16:29
 - C. Imba/sifu utukufu wake, kama vile Zab. 66:2; 96:8; 115:1
 - D. Yote tuyatendayo twayatenda katika yeye, kwa ajili ya utukufu wake, kama vile 1 Kor. 10:31; 2 Kor. 4:15; Efe. 5:22; 6:5; 1 Petro 2:12
 - E. Maelezo ya kwanza ya Katekismu

☉“kuwa Mungu husema na mwanadamu” Mungu hujidhihirisha Mwenyewe na mwanadamu anaweza kuelewa na kuhusika kwake! Huu ni msingi wa uelewa wetu wa ufunuo wa Mungu na mahitaji ya agano la Mungu.

5:27 “²⁷Enenda karibu wewe, ukasikie yote atakayoyasema Bwana, Mungu wetu” Hili lina *Qal* VITENZI SHURUTISHI viwili:

1. “enenda karibu” - BDB 897, KB 1132, lenye kumaanisha “sogea karibu” au “karibia karibu.” Kumkaribia YHWH mara kadhaa kuna madhara yake (k.v. Kut. 16:7; Law. 16:1; Hes. 16:16).
2. “sikia” - BDB 1033, KB 1570, hiki ni KITENZI chenye kujirudia mara kadhaa cha neno *shema* (yaani, “tutalisikia na kulitenda”)

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 5: 28-33

²⁸Naye Bwana akasikia sauti ya maneno yenu mliyoniambia; Bwana akaniambia, Nimesikia sauti ya maneno ya watu hawa waliyokuambia; wamesema vema yote waliyosema. ²⁹Laiti wangekuwa na moyo kama huu ndani yao sikuzote, wa kunicha, na kushika amri zangu zote sikuzote, wapate kufanikiwa wao na watoto wao milele! ³⁰Enda uwaambie, Rudini hemani mwenu. ³¹Lakini wewe, simama hapa karibu nami, nami nitanena nawe sheria zote, na amri na hukumu, utakazowafunza, wapate kuzifanya katika nchi niwapayo kuimiliki. ³²Tunzeni basi, mtende kama mlivyoamriwa na Bwana, Mungu wenu; msikengeuke kwa mkono wa kuume wala wa kushoto. ³³Endeni njia yote aliyowaagiza Bwana, Mungu wenu, mpate kuwa hai, na kufanikiwa, mkafanye siku zenu kuwa nyingi katika nchi mtakayoimiliki.

5:28-33 Tambua kuwa Mungu anasema “wamesema vyema yote waliosema.” Amri hizi hazikutolewa kuwa kandamizi kwa watu. Mungu aliwapatia ili kuwapa uhuru. Mungu alizitoa sheria zake ili kutupatia maisha yote na afya, na amani. .

5:29 “Laiti wangekuwa na moyo kama huu.....na kushika amri zangu zote sikuzote” Huu mshangao wa kiutangulizi (“Laiti wangekuwa,” BDB 566 pamoja na BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI ISITIMILIFU) ni kifungu cha maneno ya kawaida katika Agano la Kale kikitumika mara ishirini na tano, hasa katika kitabu cha Ayubu (NIDOTTE, juzuu 3, uk. 209). Hapa kinaelezea hali ya kutaka (k.v. II Sam. 18:33; Zab. 55:6).

Mungu anamtamania sana mwanadamu kuwa na furaha na amani, lakini hili linahusisha uwajibikaji. Kama watalitii, litakuwa jema kwa ajili yao, kwa watoto wao, na watoto wa watoto wao na kuendelea (k.v. Kumb. 27-29).

5:30,31 Mistari hii miwili ina mfuatano wa amri:

1. “enda” - BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI, mst. 30

2. “waambie” - BDB 55, KB 65, *Qal* IMPERATIVEKAULI SHURUTISHI, mst. 30
3. “rudini” - BDB 996, KB 1427, *Qal* KAULI SHURUTISHI, mst. 30
4. “simama” - BDB 763, KB 840, *Qal* KAULI SHURUTISHI, mst. 31
5. “nitanena” - BDB 180, KB 210, *Qal* KAULI SHURUTISHI, mst. 31
6. “utakazowafunza” - BDB 540, KB 531, *Piel* KAULI SHURUTISHI (yumkini katika muktadha huu HALI YA KUSIHI katika maana), mst. 31

5:31 “sheria zote, na amri na hukumu,” Tazama Mada Maalum katika 4:1.

☐“**niwapayo kuimiliki**” Kuna MATENDO aina mbili katika kifungu hiki:

1. “niwapayo” - BDB, 678, KB 733, *Qal* KAULI TENDWA YA HALI YA KUENDELEA
2. “kumiliki” - BDB, 429, KB 441, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO

Maelezo haya yamejikita juu ya:

1. Ahadi ya Mungu kwa Ibrahim, Mwa. 12:1-3; 15:18-21
2. Ahadi ya Mungu kwa Isaka, Mwa. 26:3-5
3. Ahadi ya Mungu kwa Yakobo, Mwa. 28:13-15; 35:9-12
4. Ahadi ya Mungu kwa Israel, Mwa. 15:16; Kut. 6:4,8; Kumb. 4:38,40; 19:10; 20:16; 21:23; Yosh. 1:2,3,6,11,13,15; 2:9,24; 18:3; 21:43; 24:13

Mungu aliwapa/aliwaahidi nchi maalum kwa ajili ya Israeli, lakini Israeli ilipaswa (1) kuimiliki, (2) kuiishi, na (3) kuendeleza agano la uaminifu ndani yake (k.v. 4:40; 7:12-13; 8:1-20).

5:32 “msikengeuke kwa mkono wa kuume wala wa kushoto” Hii ni nahau inayohusiana na neno la Mungu kama njia iliyoelezwa wazi (k.v. Zab. 119:105; Mith. 6:23). Kukengeuka toka kwenye njia safi ya Mungu ilikuwa ni dhambi (k.v. 9:12,16; 17:11,20; 28:14; Yosh. 1:7; 23:6; 31:29; II Fal. 22:2; II Nya. 34:2; Mith. 4:27). Angalia maelezo katika 2:27.

5:33 “Enendeni” Katika muktadha huu neno “enendeni” linamaanisha “muundo wa maisha” (BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI ISITIMILIFU). Katika imani ya Kibiblia, sio tu sheria zinatakiwa kutunzwa, bali ni stadi ya maisha ya kila siku: ni mahusiano na Mungu ya masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki kuwa na imani. Hii imani lazima ihusike katika maisha ya Kimungu.

☐“**mpate kuwa hai**” KITENZI(BDB 373, KB 370, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kiuhalisia ni “kumpendeza” au “hali njema.” KIVUMISHI mara zote kinatumika kuelezea nchi ya ahadi (k.v. 1:25,25; 3:25; 4:21,22, n.k.). KITENZI kinaelezea maisha mema ambayo Mungu amewaahidi kwa ajili ya kulitii agano (k.v. 15:16; 19:13)

MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozowa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni uhusiano upi uliopo kati ya sheria na neema? Je Wakristo wanastahili kuzishika sheria kumi za Mungu?
2. Ni nini makusudi ya sheria?
3. Ni kwa nini amri kumi za Mungu zinatofautiana unapojaribu kulinganisha kati ya Kutoka 20 na Kumbukumbu la Torati 5?
4. Ni nini kusudi la sabato? Kwa nini tusiabudu siku ya Jumamosi?
5. Ni nini dhamira ya kuweka pamoja tunayoiona katika mistari ya 16-21?

KUMBUKUMBU LA TORATI 6

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Amri kuu	Maana ya Amri ya Kwanza	Amri Kuu	Kumpenda Yahweh ni Msingi wa sheria (5:32-6:13) 5:32-6:3
6:1-3	6:1-3	6:1-3	
6:4-5	6:4-9	6:4-9	6:4-9
6:6-9			
Onyo juu ya Uasi		Onyo dhidi ya Uasi	
6:10-15	6:10-15	6:10-15	6:10-13 Kusihi juu ya Uaminifu 6:14-15
6:16-19	6:16-19	6:16-19	6:16-19
6:20-25	6:20-25	6:20-25	6:20-25

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Tazama uk. viii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kila aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

HISTORIA YA NYUMA

Kumekuwepo na mjadala kati ya wafasiri juu ya ikiwa sura ya 6 inatengeneza hitimisho la Amri Kumi au Utangulizi kwa sehemu katika upanuzi wa dhana zinazowasilishwa katika Amri Kumi. Kwasababu ya 5:28-33 inaonekana dhahiri kwangu kwamba tunaanza sehemu mpya ambayo inasisitiza utiifu.

- A. Wengi wamedhania kwamba sura ya 6 ni upanuzi wa Amri ya kwanza ambayo inaelezea kipaumbele cha YHWH katika maisha yetu.
- B. Kuna mwendelezo wa msisitizo katika sura hii kwa ahadi za asili za YHWH kwa Ibrahimu katika Mwanzo 12:1-3 na utimilifu wake (kama vile 6:1, 3, 10, 18, na 23).

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 6:1-3

¹Na hii ndiyo sheria, na amri, na hukumu, alizoziamuru Bwana, Mungu wenu, mfundishwe, mpate kuzitenda katika nchi ile mnayoivukia kuimiliki; ²upate kumcha Bwana, Mungu wako, kushika amri zake zote, na sheria zake, ninazokuamuru, wewe na mwanao, na mwana wa mwanao, siku zote za maisha yako; tena siku zako ziongezwe. ³Sikiza basi, Ee Israeli, ukaangalie kuzitenda; upate kufanikiwa, mpate kuongezeka sana, kama Bwana, Mungu wa baba zako, alivyokuahidi, katika nchi ijaayo maziwa na asali.

6:1 “sheria, na amri, na hukumu”Tazama Mada Maalum katika 4:1.

☐“Bwana, Mungu wenu”Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.

☐“mfundishwe.....kuzitenda”Sura ya 6, pamojana hitimisho la sura ya 5, ina tabia ya msisitizo mkali juu ya hitaji la utii (kama vile 5:29,31,32,33; 6:1,2,3,4,17,24, and 25). Msisitizo huu huu wa hitaji la utii unarudiwa katika Agano Jipya (kama vile Luka 6:46; Yohana 14:21; Yakobo 2:14-26; I Yohana 5:2). Njia mojawapo ambayo inatumika kuonyesha tunampenda kiukweli ni kwamba kile anachotwambia tunakifanya. Shabaha ya utii huu inalengwa kwanza kwa Mungu na baadaye kwa ndugu zetu wa kike na wa kiume. Mungu siku zote huchukua hatua ya kuanzisha neema (faida za agano), na bado hututegemea kutii matakwa yake ya Kiagano!

☐“katika nchi ile mnayoivukia kuimiliki”Ukweli ni kwamba hii inarejerea kwa Mwa. 12:1-3. Katika Agano la Kale kipengele cha neno “ardhi” cha ahadi ya Ibrahimu kinasisitizwa wakati kwenye Agano Jipya kipengele cha neno “uzao” cha ahadi ya Ibrahim kinasisitizwa (kabila la Yuda, familia ya Yesse, uzao wa Daudi).

6:2 “ili kwamba ninyi na watoto wenu na watoto wa wanenu wamwogope Bwana Mungu wenu”Dhana hii ya kuendeleza familia na ibada inasisitizwa katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 4:9-10;5:29; 6:13; 11:19; 32:46). Ni kinyume cha kithiolojia cha Kumb. 5:9!

☐“kumcha. . .kutunza”Heshima (BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) inaonyeshwa kwa “kutunza” (BDB1036, KB 1581, *Qal* KITENZIJINA HALISI) matakwa yake yote ya kiagano!

☐“kutunza”Angalia dokezo katika 5:1.

☐“siku zote za maisha yenu”Tazama kwamba huu ni msisitizo wa mtindo wa maisha—utii wa kila siku, sio tu aina Fulani ya vipindi vya ibada au karamu za mwisho wa mwaka. Imani ya Kibiblia ni imani ya kuanzia na toba ikifuatiwa na mtindo wa maisha ya imani na toba (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21).

☐“tena siku zako ziongezwe”Kifungu hiki mara kwa mara kimefasiriwa kwa muunganiko wa Kumb.5:16 kama ahadi ya kuwa na maisha marefu kwa wale watakaowaheshimu wazazi. Hata hivyo kwasababu ya matumizi yanayoendelea ya tungo hii katika Kumb. 4:40; 5:16,33; 6:2; 11:9, ni dhahiri kuwa ni nahau kwa ahadi ya jamii thabiti, na sio urefu wa maisha wa mtu mmoja mmoja. Agano la Mungu limekusudiwa kuendeleza jamii iliyo imara, yenye uchaji wa Mungu, yenye afya na yenye matunda (kama vile mstari wa 3; na dokezo kamili katika 4:40).

6:3Tazama namna VITENZI na dhana zinavyorudiwa rudiwa tena.

☐“ili mkafanikiwe”Tungo hii inafanana na kifungu, “ili siku zenu ziwe nyingi,” cha mstari wa 2. Tazama tungo inapatikana katika 5:33; 15:16; 19:13

☐“ili mkazidi sana. . .katika nchi itiririkayo maziwa na asali”Itajwe kwamba mbinu ya YHWH ya msingi wa kuyavuta mataifa kuwa karibu nae ilikuwa ni kuibariki Israeli kwa namna ya upekee. Hata hivyo kutotii kwa Israeli hakukuwaruhusu mpango huu wa Mungu kuwafikia. Sehemu ya laana na Baraka katika Kumb. 27-29 ni ya msingi katika kuelewa historia ya wana wa Ibrahimu. Waliambiwa dhahili juu ya utele ambao ungewapata ikiwa

wangemfuata Mungu na laana ambayo ingewafuata ikiwa wangeacha kutii. Historia ya Israeli ni moja ya matukio ya kutotii.

Kifungu cha maneno, “nchi itiririkayo maziwa na asali,” ni kifungu chenye utata wa kiufundi katika nyaraka zote za Ugariti na Misri kuashiria Palestina. Inatumika mara kwa mara (kama vile Kutoka 3:8,17; 13:5; 33:3; Mambo ya Walawi 20:24; Hes. 13:27; 14:8;16:13; Kumb. 6:3; 11:9;26:9; 27:3; 31:20).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 6:4-9

⁴Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. ⁵Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. ⁶Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; ⁷nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. ⁸Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. ⁹Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako.

6:4 “sikiza”Hiki ni KITENZI cha Kiebraniashema (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI). Angalia dokezo kamili katika 4:1. Inamaanisha “kusikiliza ili kufanya.” Hii ndiyo shabaha ya agano la Kibiblia. Matumizi ya KITENZI hiki katika Kumbukumbu la Torati inamaanisha kwamba lilitumika kiruturujia katika nyakati fulani zilizowekwa (mfano, 4:1; 5:1; 9:1; 20:3; 27:9-10).

Maombi haya katika Kumb. 6:4-6, tokea wakati wa hekalu la pili (516 K.K.), inarudiwa mapaka leo hii na watu wa kiyahudi wakati wote wa asubuhi na jioni katika kila utaratibu wa kiibada. Ni ukiri wao wa imani.



NASB, NKJV	“Bwana ndiye mmoja”
NET, NIV	“Bwana ndiye mmoja”
NRSV, TEV	“Bwana ndiye mmoja”
NJB	“Bwana ndiye mmoja”
LXX	“Bwana ndiye mmoja”
JPSOA	“Bwana ndiye pekee”
REB	“Bwana wetu ndiye Mungu mmoja”

Hakuna KITENZI. Hii ni nguzo ya msingi ya ukiri wa kiyahudi wa imani moja kwa Mungu mmoja (Ingawa lazima ijulikane kwamba huu ukweli mkuu wa kithiolojia haujaainishwa kimuktadha). Israeli ilikuwa ya kipekee kabisa mbali na ibada za miungu wengi iliyofanywa na majirani zake na haswa msisitizo wa Wakanaani juu ya Mabaali wengi wa maeneo yao.

MADA MAALUM: IMANI KATIKA MUNGU MMOJA

Mwanadamu siku zote amekuwa akiishi kuna zaidi ya ukweli kuliko huu unaoonekana (yaani kuathiriwa na vitu nje ya uwezo, kama vile dhoruba, kupatwa kwa jua na mwezi, kuanguka kwa vimondo, hali ya hewa, matukio, vifo, n.k.). Wataalamu wa sayansi ya binadamu wanatwambia kuwa wanakutana na vitu katika makaburi ya wanyama wa kale waliowahi kuishi ambavyo yumkini ni viashiria ya maisha yajayo, ambayo yanaweza kuonekana kama mwendelezo wa maisha ya baadaye.

Tamaduni ya kwanza kuandikwa ilikuwa ni ya wakati wa kiangazi (Tigris Kusini, Mito Yufrati), ilianza miaka ya 10,000 - 8,000 K.K. Waliandika mashairi kuelezea mawazo yao kwa Mungu na namna wanavyojamiiana. Tena, zaidi kama wanadamu pamoja na madhaifu yao yote. Tamaduni zao zilikuwepo katika namna za midomo zamani hata kabla hazijaandikwa.

Kulikuwa na kukua kwa kithiolojia kutoka

1. kuabudu wanyama mpaka
2. kuabudu miungu wengi mpaka
3. mungu mkuu (kuabudu miungu wawili)

Dhana ya "Mungu mmoja" (mmoja na mmoja tu binafsi Mungu mwenye maadili asiye na asili ya kike), si tu "mungu mkuu" ya miungu wengi au mungu mzuri kama miungu ye upili ya kiashuru (wafuasi wa Zoroaster), ni pekee kwa israeli (Ibrahim na Ayubu, 2000 κ.κ.). ni mmoja tu wa pekee asiye patikana katika Misri (Amenhotep IV, pia akijulikana kama Akhenaten, 1367-1350 au 1386-1361 κ.κ., aliyeabudu *Aten*, mungu jua, kama mungu pekee). Angalia J. Assmann, *The Mind of Egypt*, kurasa za 216-217.

Dhana hii inaelezea katika tungo kadhaa katika Agano la Kale

1. "hakuna kama YHWH wetu Elohim," Kutoka 8:10; 9:14; Kumbukumbu la Torati 33:26; 1 Wafalme 8:23
2. "Hakuna mwingine zaidi Yake," Kumbukumbu la Torati:30; 1 Kor. 8:4,6; 1 Tim. 2:5; Yakobo 2:19
3. "Hakuna kama wewe," 2 Samweli 7:22; Yeremia 10:6
4. "wewe pekee ndiwe Mungu," Zaburi 86:10; Isaya 37:16
5. "Kabla yangu hakukuwa na Mungu na baada yangu hatotokea," Isaya 43:10 adherence
6. "hakuna mwingine; zaidi yangu. . .hakuna mwingine," Isaya 45:5,6,22
7. "Yeye ni chanzo cha vitu vyote," Isaya 45:7 (kama vile Amosi 3:6)
8. "hakuna mwingine, hakuna Mungu mwingine," Isaya 45:14,18
9. "hakuna mwingine isipokuwa," Isaya 45:21
10. "hakuna kama mwingine;. . .hakuna kama mimi," Isaya 46:9

Lazima kukiri kuwa fundisho hili muhimu limefunuliwa katika maendeleo katika njia. Kauli ya mwanzo ingeweza kueleweka "utii kwa mungu mmoja kati ya wengi" au kuabudu mungu mmoja kwa kimatendo (kuna miungu mingine, yani Joshua 24:15; 1 Wafalme 18:21), lakini Mungu mmoja tu kwa ajili yetu (kama vile Kutoka 15:11; 20:2-5; Kumbukumbu la Torati 5:7; 6:4,14; 10:17; 32:12; 1 Wafalme 8:23; Zaburi 83:18; 86:8; 136:1-9).

Maandiko ya kwanza ambayo yalianza kuonesha umoja (Hali ya Kifalsafa ya Mungu mmoja) ni mapema (kama vile Kutoka 8:10; 9:14; 20:2-3; Kumbukumbu la Torati 4:35,39; 33:26). Madai yaliyokamili na yashinda nayo yanapatikana katika Isaya 43-46 (kama vile 43:10-11; 44:6,8; 45:7,14,18,22; 46:5,9).

Agano la Kale linapunguza miungu ya mataifa kama

1. Uumbaji wa kibinadamu – Kumbukumbu la Torati 4:28; 2 Wafalme 19:18; Zaburi 115:4-8; 135:15-18; Isaya 2:8; 17:8; 37:19; 40:19; 41:7,24,29; 44:10,12; 46:6-7; Yeremia 10:3-5; Ufunuo 9:10
2. mapepo – Kumbukumbu la Torati 32:17; Zaburi 106:37; Isaya 8:19; 19:3c; 1 Kor. 10:20; Ufunuo 9:20
3. ubatili, utupu – Kumbukumbu la Torati 32:21; 2 Wafalme 17:15; Zaburi 31:6; Isaya 2:18; 41:29; Yeremia 2:5; 10:8; 14:22; Yeremia 2:5; 8:19
4. hakuna miungu – Kumbukumbu la Torati 32:21; 2 Nyakati 13:9; Isaya 37:19; Yeremia 2:11; 5:7; 1 Kor. 8:4-5; 10:20; Ufunuo 9:20

Agano Jipya linaelezea katika Kumbukumbu la Torati 6:4 katika Warumi 3:30; 1 Kor. 8:4,6; Efe 4:6; 1 Tim. 2:5; na Yakobo 2:19. Yesu alinukuu kama amri ya kwanza katika Mt. 22:36-37; Marko 12:29-30; Luka 10:27. Agano la Kale pia kama Agano Jipya, linaelezea ukweli wa viumbe vingine vya kiroho (mapepo, malaika), lakini muumbaji mmoja tu/Mungu mkombozi (YHWH, Mwanzo 1:1).

Hali ya kuwepo kwa Mungu mmoja kibiblia kunatabia zifuatazo

1. Mungu ni mmoja na wa pekee ((ontology) nadharia inayojishughulisha na asili ya uhai inadhaniwa, haijawekwa bayana)
2. Mungu ni wa binafsi (kama vile Mwanzo 1:26-27; 3:8)
3. Mungu ni mwadilifu (kama vile Mwanzo 34:6; Nehemia 9:17; Zaburi 103:8-10)
4. Mungu aliwaumba wanadamu katika sura yake (Mwanzo 1:26-27) kwa ajili ya ushirika (yaani #2). Ni Mungu mwenye wivu (kama vile Kutoka 20:5-6)

Kutoka katika Agano Jipya

1. Mungu ana milele tatu, udhihirisho wa nafsi (angalia Mada Maalum: Utatu)
2. Mungu kwa ukamilifu wake amefunuliwa kikamilifu ndani ya Yesu (kama vile Yohana 1:1-14; Kol. 1:15-19; Ebr. 1:2-3)
3. Mpango wa milele wa Mungu kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka ni sadaka ya Mwanawe wa Pekee (Isaya 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; Fil. 2:6-11; Waebrania)

6:5 “Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote”Huu ni msisitizo mkuu ambao unaelezea kwamba mwitikio wetu kwa Mungu unatakiwa kujumuisha utu wote. Yesu aliutumia mstari huu katika kuunganisha na Law. 19:18 kukiri umuhimu mzima wa sheria(kama vile Mt. 22:36-38; Marko 12:29-34; Luka 10:27-38).

“Upendo” wa Waaminio (BDB 12, KB 17 Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kudhaniwa. Ni tabia ya Kumbukumbu la Torati kuunganisha utii kwa agano la YHWH kama ushahidi wa upendo wa mtu kwake (kama vile 5:10; 6:5; 7:9; 10:12; 11:1,13;13:3; 19:9; 30:6,16,20). Angalia dokezo kamili 5:10.

Maneno “moyo” na “nafsi” mara kwa mara yanatumika kwa pamoja kuonyesha mtu kamili (kama vile 4:29; 10:12;11:13; 13:3; 26:16; 30:2,6,10).

Neno “nafsi” (BDB 659) huelezea nguvu ya uhai (yaani, pumzi) kwa wote wanadamu na wanyama (mfano Mwa.1:20-30; 2:7,19; 7:22; Ayubu 34:14-15; Zab. 104:29,30; 146:4; Mhubiri. 3:19-21). Hapa huashiria shauku kali.

“Nguvu” (BDB 547) humaanisha “utele” au “nguvu” (kama vile II Wafalme 23:25). Maneno haya matatu “moyo,”“nafsi,” “nguvu,” yanawakilisha mtu kamili na hivyo kufanana na kifungu cha maneno, “kwa moyo wako wote.”Tazama maneno “yote” (BDB 481) linarudiwa mara tatu kwa ajili ya msisitizo.

Amri hii inawekwa wazi na Yesu kama amri kuu (kama vile Mt. 22:34-40;Marko 12:29-30; Luka 10:25-37). Kila mojawapolinaelezea aina tofauti ya viongozi wa kiyahudi. Hata hivyo lazima ieleweke kwamba maisha ya Yesu na Mitume yalikuwa ya kipindi cha mpito kutoka Agano la Kale kwenda Agano Jipya.Sheria hizi mbili, upendo kwa Mungu (Kumb. 6:5) mpende jirani yako (Law. 19:18) pia ni muhtasari wa agano Jipya!

Kwa ajili ya maswali, “ni kwa namna gani waaminio wa Agano Jipya wanaweza kuitikia?” kwa sheria za Agano la Kale angalia:

1. *How to Read the Bible for All Its Worth*, Douglas Stuart, kur. 165-169
2. *Cracking Old Testament Codes*, D. Brent Sandy and Ronald L. Giese, kur. 123-125.

6:6 “maneno haya” “Maneno haya” yanarejerea kwa agano la YHWH ambalo lilitolewa kupitia Musa.

▣**“utayaweka moyoni”**Neno moyo (BDB 523), katika Kiebrania linaashiria kuelekezwa katika shabaha ya maisha ya mtu mmoja mmoja. Msisitizo uliopo katika Agano la Kale pia ulimaanisha uaminifu wa ndani kama ulivyo katika Agano Jipya (kama vile Kumb.4:29; 6:5, 6; 10:12; 11:13,18; 13:3; 26:16; 30:2, 6, 10; Agano Jipya, “kwa akili zako zote,” Marko 12:30; Luka 10:27).Wakati mwingine tunakuwa na madhanio mabaya ya uongo kwa kuleta utofautisho kati ya Agano la Kale kuwa sheria ya mwili na Agano Jipya kuwa imani ya ndani. Yawezekana tunapata makosa haya kutoka katika Yer. 31:31-34, ambayo inasisitiza “moyo mpya.” Hata hivyo hata katika Agano la Kale mwamini mmoja mmoja alitarajiwa kuelekeza utu wake wote, matendo na nia kwa Bwana Mungu wake.

6:7 “mtawafundisha kwa bidii watoto wenu”KITENZI(BDB 1041, KB 1606, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) humaanisha“kuchonga” na katika *Piel* haya ni matumizi pekee. Neno katika lugha ya ugaritiki humaanisha “kurudia.” Hiyo inaonekana kuwa msisitizo wa msingi wa mstari huu. Walimu wa Kiyahudi wanatumia mstari huu kuelezea kwambaShemalinatakiwa “kurudiwa”asubuhi na jioni. Tunatakiwa kuzungumzia mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu wakati wote wa shughuli zetu za kila siku. Ni jukumu la wazazi kurithisha mtindo wa maisha ya imani (kama vile Kumb. 4:9; 6:20-25; 11:19; 32:46,Angalia dokezo kamili katika 4:9). Inafurahisha kwamba mtiririko wa nyakati hizi tofauti kwa ajili ya mafundisho yanaangukia katika utaratibu ule ule wa kifasihi kama ilivyo katika Zab. 139:2-6 na Mithali6:20-22. Msisitizo huu unarudiwa katika Mithali 22:6. Shule ya Kanisa letu la kisasa haiwezi kuchukua nafasi ya mafunzo ya kimaadili ya wazazi lakini hakika inaweza ikasaidia kwa kurutubisha makuzi!

6:8 “nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako”Kiasili tungo hii inaonekana kutumika kama stiari (kama vile LXX). Muktaadha ni fursa ya mtindo wa mafundisho ya maisha kwa kutumia neno la Mungu. Hata hivyo walimu wa sheria waliuchukua mstari huu kihalisia kwa kufunga kitambaa cha ngozi katika mkono wao wa kushoto kikiwa na kasanduku kadogo (*tefillin*) kalikoandikwa maandiko yalichochaguliwa kutoka katika Torati. Kisanduku hicho hicho pia walikifunga katika mapaji yao ya uso. Hivi “vifungio” au“vifungavyo katika mapaji ya uso” (BDB 377) vinatajwa katika Kumb. 11:18 na Mt. 23:5.

6:9 “yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako.”Hii tena ni ishara ya kiuwakilishi ambayo Mungu anatakiwa awe na sehemu ndani yake, sio tu katika maisha yetu ya nyumbani lakini katika maisha yetu ya kijamii (yaani malango, kama vile.21:19; 22:15,24). Kama lango (BDB 265) la nyumba mara nyingililionekana kuwa mahali pa kipepo katika ulimwengu wa Warumi na Wayunani, katika ulimwengu wa kiyahudi liliwakilisha uwepo wa Mungu (yaani mahali ambapo damu ya Pasaka iliwekwa, kama vile Kut. 12:7,22,23).

Neno “Malango yako” (BDB 1044) linaweza kurejelea sehemu ya makutano ya kijamii na kutolea haki (yaani, kama malango ya mjini).Siku zote visanduku hivi vidogo na alama kwenye vizingiti vya malango (*mezuz*) vilikuwa na vifungu mbalimbali vya maandiko: Kumb. 6:4-9; 11:13-21 na Kut. 13:1-10,11-16.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 6:10-15

¹⁰Tena itakuwa atakapokwisha Bwana, Mungu wako, kukuleta katika nchi aliyowaapia babu zako, Ibrahimu na Isaka na Yakobo, ya kuwa atakupa; miji mikubwa mizuri usiyojenga wewe, ¹¹na nyumba zimejaa vitu vyema vyote usizojaza wewe, na visima vimefukuliwa usivyofukua wewe, mashamba ya mizabibu na mizeituni usiyopanda wewe, nawe utakula na kushiba; ¹²ndipo ujitunze, usije ukamsahau Bwana aliyekutoa nchi ya Misri, nyumba ya utumwa. ¹³Mche Bwana, Mungu wako; ndiye utakayemtumikia, na kuapa kwa jina lake. ¹⁴Msifuute miungu mingine katika miungu ya mataifa wawazungukao; ¹⁵kwani Bwana, Mungu wako, aliye katikati yako ni Mungu mwenye wivu; isije ikawaka juu yako hasira ya Bwana, Mungu wako, akakuangamiza kutoka juu ya uso wa nchi.

6:10-11Hii inaonyesha kwamba Israeli ilikuwa inaenda kumiliki ardhi ya Wakanaani (kama vile Mwa. 15:16). Walitakiwa kumiliki nyumba zao, mashamba yao ya mizabibu na viwanja. Japo, mstari wa 12 unasisitiza kwamba hakutakiwa kusahau kwamba ni Bwana aliyempatia hivi vyote na sio mali zake mwenyewe (kama vile 4:9; 8:11-20; Zab. 103:2). Ikiwa wangemsahau YHWH kinyume chake wangepoteza vyote. Wangepoteza nyumba, viwanja na mashamba ya mizabibu (kama vile 28:27-48). Upendo wa Kimungu ulianzisha uhusiano wa kiagano, lakini utii wa kibinadamu uliyaendeleza.

6:12 “jiangalieni”KITENZI(BDB 1036, KB 1581, *Niphal* KAULI SHURUTISHI) kinatumika mara kwa mara katika Kumbukumbu la Torati, lakini mara nyingi katika *Qalstem*. *Niphal* inapatikana katika 2:4; 4:9,15,23; 6:12; 8:6,11; 11:16; 12:13,19,30; 15:9;23:9; 24:8 na siku zote kwa maana ya “kuwa waangalifu”!

☐**“msije kusahau”**KITENZI(BDB 1013, KB 1489, *Qal* WAKATI USIO TIMILIFU) Ni onyo linalojirudia rudia katika Kumbukumbu la Torati (kama vile4:9,23,31; 6:12;8:11,14,19[mara mbili]; 9:7; 25:19).

☐**“BWANA aliyekutoa katika nchi hii ya Misri, kutoka katika nyumba ya utumwa”**Huu ni msisitizo endelevu wa kitabu cha Kumbu kumbu la Torati (kama vile Kumb. 4:10; 5:29;6:2). Si sawa kuainisha tabia za Agano la Kale kama sheria na Agano Jipya kama neema (Martin Luther).

6:13Mstari huu una mambo kadhaa kwamba Israeli wanatakiwa kuyatenda kwa YHWH wanapoingia nchi ya ahadi kwa ushindi:

1. “mche Bwana Mungu wako tu” - BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILFU
2. “mwabudu Yeye” - BDB 712, kutumia” KB 773, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. “kuapa kwa jina langu” - BDB 989, KB 1396, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU. Tazama dokezo kamili katika 5:11.

Mambo haya yote yanajumuisha kuabudu na kutumika mara kwa mara katika maandiko ya Musa.Sehemu ya ibada ya kipagani ya Israeli walitakiwa kutamka kwa jina la YHWH. Yesu anaonekana kunukuu mstari huu katika Mt. 4:10 wakati wakikabiliana na yule Mwovu. Anabadilisha neno “kumcha” katika mstari wa 13 kuwa neno “kuabudu,” ambalo linatuonyesha sisi kwamba maneno haya mawili kimsingi yanafanana. Jina la Mungu linaaksiwa na tabia Yake na Utu wake.

6:14 Mstarihuu unaongeza matakwa mengine kwenye orodha ya mstari wa 13:

4. “hutaabudu miungu mingine” - BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
Hapa ibada ya kuabudu miungu ya ustawi ya Wakanaani inakatazwa kata kata.

☐“miungu. . .miungu”Haya ni maneno *Elohim*(BDB 43) na *El*(BDB 43). Tazama Mada Maalum katika 1:3.

6:15 “kwa maana BWANA Mungu wako yu kati kati yenu”Hili lilikuwa ni kusudi la uumbaji. Mungu anataka kukaa na wale walioumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwa.1:26-27). Hii ni dhana ya kimasihya ya Immanuel, ambayo inamaanisha “Mungu pamoja nasi” (kama vile Isa. 7:14 na Mt. 28:20).

☐“Mungu mwenye wivu”Neno hili la Kiebrania linaweza kumaanisha“wivu” au “upendo uzidio” (BDB 888, kama vile Kumb. 4:24; 5:9; tazama dokezo katika 4:24). Wivu ni neno la upendo. Tunakuwa na wivu kwa wale tunawapenda sana.Huu ni ukiri mwingine wa upendo wa Mungu kwa lugha ya kibinadamu, kwa neno la kifamilia. Tazama Mada Maalum katika 2:15.

☐“isije ikawaka juu yako hasira ya Bwana, Mungu wako, akakuangamiza kutoka juu ya uso wa nchi”Kama ufunuo wa upendo wa Mungu ulivyo, kitabu kile kile kinafunua ghadhabu ya Mungu. Kitabu kile kile chenye maneno yanayotufunika na upendo Wake kinatushangaza na hasira Yake (“kuwaka” BDB 354, KB 351, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile11:16-17; 31:16-17; Waamuzi. 2:14; 6:13, na “kuwaondoa” au “kufuta” BDB 1029, KB 1552, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 1:27; 2:22; 9:20; Yosh. 9:24). Njia nzuri ya kuelewa mahusiano kati ya upendo wa Mungu na gadhabu yake ni kulinganisha Kumb. 5:9 pamoja na 7:9. Kama Mungu anavyoyapatiliza maisha ya watu, hupatiliza ouvu wa baba kwenda kwa mwana hata kizazi cha tatu na cha nne, huwabariki maelfu wampendao kwa imani. Upendo wa Mungu uliokataliwa ni ghadhabu ya Mungu. Isaya huiita ghadhabu ya Mungu “kazi yake ya ajabu” (kama vile Isa. 28:21).

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 6:16-19

¹⁶Msimjaribu Bwana, Mungu wenu, kama mlivyomjaribu huko Masa. ¹⁷Zishikeni kwa bidii sheria za Bwana, Mungu wenu, na mashuhudizo yake, na amri zake alizokuagiza. ¹⁸Nawe fanya yaliyo sawa, na mema, machoni pa Bwana; ili mpate kufanikiwa, nawe upate kuingia na kuimiliki nchi nzuri Bwana aliyowaapia baba zako, ¹⁹ya kuwa atawasukumia nje adui zako wote mbele yako, kama alivyosema Bwana.

6:16 “Msimjaribu Bwana, Mungu wenu, kama mlivyomjaribu huko Masa”Sehemu yenyewe iliitwa *Masa*“walikomjaribu,” (BDB 650). Hii ni rejea kwa tukio ambalo lilitukia katika Kut. 17:1-7 (“mlivyomjaribu”BDB 650, KB 702, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU),pale watu walivyomnug’unikia Mungu juu ya upataji wao wa mahitaji na uwepo wake (kama vile Kumb. 9:22; 33:8). Walionyesha hali ya kutokuwa na imani (kama vile Zab. 95:8; Waebrania 3-4). Msifanye tena (“jaribu” *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)! Pia mstari huu unatumiwa na Yesu kwenye majaribu yake na shetani (kama vile Mt. 4:7; Luka4:12).

6:17 “Zishikeni kwa bidii sheria za Bwana, Mungu wenu”Tazama maelezo katika 6:3. Mwendelezo huu wa msisitizo juu ya utii (angalia katika dokezo 5:1) ni mkubwa na unaweka hatua kwa ajili ya mahusiano ya kiagano. Maagano yote ya Mungu na mwanadamu yanaanzishwa na Mungu Mwenyewe bila masharti, lakini ni lazima waitikie kwa namna ya masharti (kama vile 5:32, 33; 6:1, 2, 3, 17, 24, 25).

☐“sheriamashuhudizo yake, na amri zake”Tazama Mada Maalum katika 4:1.

6:18Kuna maneno matatu yanayofaa kuendana na matukio ya Israeli:

1. “mtaenenda sawasawa” - KITENZI, BDB 793 I, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, “kufanya”

- a. “haki” - BDB 449 maana yake “kinachotakiwa kufanywa” au “cha kupendeza,” kama vile Kut.. 15:26; Kumb. 6:18; 12:25,28;13:18; 21:9
 - b. “vyema” - BDB 373 II, linatumika mara mbili, “kile kinachopendeza,” kama vile Mwa. 16:6; Kumb. 12:28 (BDB 375III, mstari wa 24)
2. “ili mkafanikiwe” - BDB 405, KB 408, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, “mkatende vyema,” kama vile 4:40;5:16,29,33; 6:3,18; 12:25,28; 22:7

Tazama kwamba yote matatu yanapatikana katika 12:25,28. Ikiwa Israeli itatunza kile kinachotakiwa katika maagano, YHWH ataleta utajiri na maisha marefu!

6:19 “atawasukumia nje adui zako wote mbele yako”Mungu aliwapa nchi ya ahadi (“kuwaondoa,” BDB 213, KB 239, *Qal* KITENZIJINA HALISI, kama vile Mwa. 15:16-21). Aliwapa ushindi wa kijeshi lakini Israeli walitakiwa kujiandaa na kwenda kupigana. Yumkini huu ni muunganiko mzuri kuonyesha utoaji wa Mungu na mwitikio wa uamiifu wa kiagano (kama vile Yosh. 1-12).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 6:20-25

²⁰Na zamani zijazo atakapokuuliza mwanao, akikuambia, N'nini mashuhudizo, na amri, na hukumu, alizowaagiza Bwana, Mungu wetu? ²¹Ndipo umwambie mwanao, Tulikuwa watumwa wa Farao huko Misri; Bwana, akatutoa kutoka Misri kwa mkono wa nguvu; ²²Bwana akaonya ishara na maajabu, makubwa, mazito, juu ya Misri, na juu ya Farao, na juu ya nyumba yake yote, mbele ya macho yetu; ²³akatutoa huko ili kututia huku, apate kutupa nchi aliyowaapia baba zetu. ²⁴Bwana akatuamuru kuzifanya amri hizi zote, tumche Bwana, Mungu wetu, tuone mema sikuzote ili atuhifadhi hai kama hivi leo. ²⁵Tena itakuwa haki kwetu, tukitunza kufanya maagizo haya yote mbele ya Bwana, Mungu wetu, kama alivyotuagiza

6:20Huu ni msisitizo endelevu wa mafunzo ya kiroho na ya watoto (angalia dokezo kamili katika4:10).Sehemu ya kipengele cha muktadha kisichokuwa cha kawaida (yaani mistari ya 20-33) ni kwamba mashuhuda walikuwa wamekufa na wazao wao walikuwa wakihadithia. Hivyo hii inaweza kufanyika kuwa utaratibu wa kiruturujia (yaani, “wakati watoto wanapoomba. . .mtawaambia. . .,” Kut. 12:26,27; 13:14-15; Kumb. 6:20-25; Yosh. 4:6-7,21-24).

Inawezekana kwamba 6:20-24 ni moja ya vifungu kadhaa ambavyo vinazungumzia safari ya imani ya Israeli pamoja na YHWH, kutokea kwenye wito wa Ibrahimu hadi kwenye ushindi wa safari ya Kutoka Misri (kama vile 26:5-9; Yosh. 24:2-13; Zab. 77; 78; 105; 136).

6:21 “kwa mkono wenye nguvu”Tazama maelezo katika 4:34.

6:22Hii inarejelea yale mapigo kumi ya Misri. Kila moja ya mapigo lilikuwa ni hukumu dhidi ya miungu wa kimisri. Inavyoonekana haya mapigo yalidumu kipindi cha miezi kumi na nane, ikiwa mtu atadhania kulikuwa na namna ya majanga ya asili yaliyokuwa yakihusika. Mungu angeweza kuwakomboa kwa haraka zaidi lakini ni fikra zangu binafsi kuwa alikuwa akishughulikia imani ya wamisri kama alivyokuwa akishughulikana ya Waisraeli pia.Kundi lililochanganyika kiasi kwamba kuliacha Misri ikiwa na baadhi ya Wamisri waaminio.

6:24Mstari huu unaelezea faida za Israeli kuzitii amri za Mungu (1) kwa ajili yao(BDB 375 III, kama vile mstari wa 18) siku zote na (2) kwa ajili ya kuendelea kwao kuishi (BDB 310, KB 309, *Piel* KITENZIJINA HALISI)kama watu (mfano, 4:1; 8:1; 30:16,19).



NASB, NKJV

TEV “siku zote”

NRSV “bila kukoma”

NJB “milele”

Kiuhalisia huu ni muundo wa maneno wa neno “yote” (BDB 481) na “siku” (BDB 398) ukitumika kama stiari ya kudumu (kama vile 5:29; 28:33; Mwa. 6:5; Zab. 52:1, angalia Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, ukur. 316).

6:25 “na Itakuwa haki kwetu” Kama imani ya awali ya Ibrahimu na utii ilivyokubaliwa na YHWH (kama vile Mwa. 15:6) kama “haki,” vivyo hivyo utii wa kiagano juu ya sehemu ya Israeli (kama vile 24:13). Tazama Mada Maalum: Haki katika 1:16.

☐ **“kufanya bidii kutenda amri hizi zote”** Tazama asili ya kimasharti yenye kujirudia ya ahadi hizi:

1. “ikiwa mtakuwa waangalifu” - BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 4:6,9,40; 5:1,10,12,29,32; 6:2,3,17 (mara mbili)
2. “kutenda” - BDB 793, KB 889, *Qal/TUNGO* JINA, kama vile 4:6; 5:1,15,27,32; 6:1,3,18,24,25. Tazama dokezo katika 5:1.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani sura ya 6 inahusiana na Amri Kumi?
2. Kwanini kunakuwepo msisitizo mkubwa katika utii katika agano?
3. Ni nini umuhimu wa Kumb. 6:4-6 na kwa namna gani inahusiana na imani katika miungu wengi, kutokuwepo na miungu na imani katika Mungu mmoja?
4. Ni nini wajibu wa wazazi waaminio kuelekea kwa watoto wao?
5. Elezea chimbuko na matumizi ya kibiblia ya neno “haki” vyote katika shabaha yake ya Agano la Kale na Agano Jipya.

KUMBUKUMBU LA TORATI 7

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Watu waliochaguliwa	Maisha ndani ya Kanaani	Watu wa Bwana	Watu wa Israeli Waliotengwa
7:1-5	7:1-6	7:1-6	7:1-6
7:6-11			Uchaguzi wa Mungu na Upendeleo wake
	7:7-11	7:7-11	7:7-11
Baraka zitokanazo na Utii		Baraka zitokanazo na Utii	
7:12-16	7:12-16	7:12-16	7:121-15 7:16
Uweza wa Yhwh			
7:17-26	7:17-26	7:17-26	7:17-20 7:21-24 7:25-26

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi”) *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (mzunguko #3, uk viii) Linganisha mgawanyo wa somo lako na tafsiri nne hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 7:1-5

¹Bwana, Mungu wako, atakapokutia katika nchi uendayo kuimiliki, atakapoyang'oa mataifa mengi watoke mbele yako, Mhiti, na Mgirgashi, na Mwamori, na Mkanaani, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi, mataifa saba

makubwa yenye nguvu kukupita wewe; ²wakati Bwana, Mungu wako, atakapowatoa mbele yako, nawe utawapiga; wakati huo ndipo uwaondoe kabisa; usifanye agano nao, wala kuwahurumia; wala usioane nao; ³binti yako usimpe mwanawe mume, wala usimtwalie mwanao mume binti yake. ⁴Kwa kuwa atamkengeusha mwanao mume asinifuuate, ili wapate kuabudu miungu mingine; ndipo itakapowaka hasira ya Bwana juu yenu, naye atakuangamiza upesi. ⁵Lakini watendeni hivi; zivunjeni madhabahu zao zibomosheni nguzo zao, yakateni maashera yao, ziteketezeni kwa moto sanamu zao za kuchonga.

7:1 “Mhiti” Tazama Mada Maalum: Makazi ya Waisraeli ya Kanaani ya awali katika 1:4.

☐ **“mataifa saba”** Orodha ya mataifa tofautitofauti kutoka 10, 7, 5, 3, au 1 (yaani, Mkanaani au Mwamori).

7:1-5 Kuna VITENZI kadhaa vilivyotumikakuamrisha mwitikio waisraeli kwa makundi ya makabila yaishio Kanaani:

1. “atakapoyang'oa” - mst. 1, BDB 675, KB 730, *Qa* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kifasihi hiki kinamaanisha “kupungua,” kama vile II Fal. 16:6; hapa, kistiari “atakapoyang'ao,” kama vile mst. 2.
2. “Mungu wako, atakapowatoa mbele yako” – mst. 2, BDB 678, KB 733, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile mst. 23; Hes. 21:3 na Mungu atalifanya hili kwa Israeli kwa sababu ya dhambi zake zilizo katika I Fal. 14:16
3. “utawapiga” - mst. 2, BDB 645, KB 697, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, “kuadhibu,” kama vile Kut. 9:25; 21:20
4. “uwaondoe kabisa” - mst. 2, BDB 355, KB 353, *Hiphil* ya KAULI YA KITENZI JINA HALISI, kama vile 2:34; 3:6 (mara mbili); 7:2 (mara mbili)
5. “usifanye agano nao” - mst. 2, BDB 503, KB 500, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, “usije ukafanya agano,” kama vile Kut. 23:32; 34:12
6. “wala kuwahurumia” – mst. 2, BDB 335, KB 334, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile mst. 16; 13:8
7. “wala usioane nao” - mst. 3, BDB 368, KB 364, *Hithpael* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kifasihi “na kuoana nao,” kama vile Mwa. 34:9; Yosh. 23:12
8. “zivunjeni madhabahu zao” - mst. 5, BDB 683, KB 736, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 12:3; Kut. 34:13(23:24); II Fal. 23:12; II Nya. 31:1
9. “zibomosheni nguzo zao” - mst. 5, BDB 990, KB 1402, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile II Fal. 11:18, wakabomoa mahali pa juu na madhabahu, *Ba'al*, kama vile II Nya. 31:1
10. “yakateni maashera yao” - mst. 5, BDB 154, KB 180, *Piel* ya WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile mst. 25; 12:3; II Nya. 14:3; 31:1; 34:4,7
11. “ziteketezeni kwa moto sanamu zao za kuchonga” - mst. 5, BDB 976, KB 1358, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile I Nya. 14:12 katika Mika 1:7, vitu vya sanamu za miungu vinachomwa

7:2 “uwaondoe kabisa” Hili ni *nenohere*m (BDB 355, KB 353, *Hiphil* ya KITENZI JINA HALISI) Hili lilimaanisha kwamba kitu fulani kilitolewa kwa ajili ya Mungu ili kiangamizwe. Neno la Agano Jipya kuhusiana na dhana hii ni *corban*. Hili lilihusiana na dhana ya utakatifu au kitu fulani kilichotengwa kwa ajili ya matumizi ya Mungu. Kwa kuwa kitu hicho kilikuwa kitakatifu sana kisingeweza kutumiwa na wanadamu, njia pekee ya kuhakikisha kutotumika kwake ilikuwa ni kukiharibu. Hivyo, ndani ya mipaka ya Israeli, wakati miji ilipochukuliwa, watu, na wakati mwingine wanawake, watoto, na wanyama pia waliuawa. Kwa hizi siku zetu za leo huu unaonekana kuwa ukatili sana, lakini hili lilikuwa tendo la kawaida katika siku zile. Mfano mzuri wa hili unaweza kuwa mji wa Yeriko katika Yoshua 6 au Lakishi katika Yosh. 10:28,35. Mwanzo 15:16; Hes. 33:55; Yosh. 23:13 unaoeleza sababu za kithiolojia za maangamizi ya Wakanaani ya jumla.

☐ **“usifanye agano nao”** Yoshua 9 inatupa mfano wa kihistoria wa Waisraeli kushindwa kuishika amri hii.

☐
NASB “wala kuwahurumia”
NKJV “wala kuwaonyesha msamaha”

NRSV “usionyeshe kuwasamehe”

TEV “usi. . .msamaha wo wote”

NJB “usi. . .masikitiko yo yote”

KITENZI kikanushi (BDB 335 I, KB 334, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinamaanisha “kuonyesha huruma” au “kuwa mwenye neema.”

Hata hivyo, Israeli haikuwa na nafasi hii (kama vile mst. 16; 13:11-16; 19:13,21; 25:12). Msamaha ungeichafua nchi kwa dhambi; msamaha ungeachilia kile ambacho YHWH asingekifanya!

7:3 “usioane nao” Hili halikuwa na vidokezo vihusivyo rangi hata kidogo; hili lilikuwa la sababu za kidini (kama vile Kut. 34:12-17). Vifungu vikuu vinavyohusiana na hili ni adimu katika Ezra 10 na Nehemia 13. Mungu hakuwataka watu wake waoane na Wakanaani kwa sababu ya kuabudu sanamu, tendo ambalo lingeisukuma mbali mioyo yao kutoka kwake na kuupotosha ufunuo wake mwenyewe kwa ulimwengu.

7:4 “Kwa kuwa atamkengeusha mwanao mume asinifuata” Tazama. 33:55; Yosh. 23:13. Hapa ndipo dhana ya Kiyahudi ya mama kuwa msingi wa uimarifu wa sheria za Kiyahudi ulipoanzia.

7:5 “zivunjeni . . .zibomosheni . . .yakatani . . . ziteketezeni” Tazama orodha kamili katika 7:1-5.

☐ **“maashera”** Tafsiri ya toleo la KJV lina neno “misitu.” Maana yake halisi ilikuwa “alama za mungu wa kike aliyechongwa kwa mbao” (BDB 81). Hii ilikuwa nguzo ya mbao ambayo ilikuwa imesimamishwa pembeni mwa nguzo ya jiwe la Baali lilokuwa limeinuka, mungu wa ustawi. Ashera au Astartes alikuwa mwenza wa kike na aliwakilishwa kwa nguzo iliyochongwa kwa mbao. Haijulikani kama hii ilikuwa miti ya moja kwa moja nguzo iliyochongwa.

ANDIKO LA NASB (LILOBORESHWA) KUMBUKUBU LA TORATI 7:6-11

⁶Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako; Bwana Mungu wako, amekuchagua kuwa watu wake hasa, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi. ⁷Bwana hakuwapenda ninyi, wala hakuwachagua ninyi, kwa sababu mlikuwa wengi kuliko mataifa yote, maana mlikuwa wachache kuliko watu wote; ⁸ bali kwa sababu Bwana anawapenda, na kwa sababu alitaka kuutimiza uapo wake aliowaapia baba zenu, ndiyo sababu Bwana akawatoa kwa mkono wa nguvu, akawakomboa katika nyumba ya utumwa, katika mkono wa Farao, mfalme wa Misri. ⁹ Basi jueni ya kuwa Bwana, Mungu wenu, ndiye Mungu; Mungu mwaminifu, ashikaye agano lake na rehema zake kwao wampendao, na kushika amri zake, hata vizazi elfu; ¹⁰naye huwalipa wamchukiao mbele ya uso wao, kuwaangamiza. Hatakuwa mlegevu kwake yeye amchukiaye, atamlipa mbele ya uso wake. ¹¹Basi zishike amri, na sheria, na hukumu ninazokuamuru leo, uzitende.

7:6 “u taifa takatifu . . . Mungu wako, amekuchagua” Uchaguzi wa Agano la Kale (yaani, “chaguliwa” - BDB 103, KB 119, *Qal*, ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ulikuwa kwa ajili ya huduma, ambapo huu mara nyingi haukuhusisha wokovu (kama vile Koreshi katika Isa. 44:28; 45:1). “Waliokuwa wakichaguliwa,” kama “watakatifu,” walikuwa na mengi ya kufanya zidi kwa uhusiano wao na YHWH kuliko uchaji binafsi, kama matunizi ya Agano Jipya ya neno “mtakatifu” kwa waaminio. Mugu aliichagua Israeli ili kulichagua taifa ili kuuchagua ulimwengu (kama vile Kut. 19:5-6). Yeye aliwataka “watu walio watakatifu” (BDB 872) kuuonyesha ulimwengu tabia na shauku ya kuwajua. Lakini, hata taifa hilio, mara nyingi lilikuwa tendo binafsi la imani ambayo ilimfanya mtu kuwa na haki pamoja na Mungu, si kwa sababu ya kuwa sehemu ya jumuiya ya agano (kama vile Ezekiel 18). Jumuiya ya agano ilikuwa na wale waliojitoa, kwa imani, kwa ajili ya Sheria ya Mungu. Hii ilikuwa na zaidi ya Wayahudi; wageni kati yao, wasiojulikana nchini mwao, na watumwa wa kigeni majumbani kwa wema wote alikubalika na waliruhusiwa kushiriki agano la uchaguzi (kama vile Kut. 12:38).

☐

NASB “watu wake hasa”

NKJV, Tanib ya NASB “hazina ya kipekee”

NRSV, NIV "umiliki wa hazina yake"

TEV -----

NJB "watu wake mliowekwa hazina"

JPSOA, REB "umiliki wa kipekee"

NET Bible "wa thamani"

Kiuhalisia hii ni "watu wa milki" (BDB 766 I na 688, kama vile Kut. 19:5) au "hazina ya kipekee." Neno hili lenye kumaanisha mali iliyothamanishwa, limetumika kistiari kumanaanisha watu wa agano la Mungu (kama vile 7:6; 14:2; 26:18; Zab. 135:4; Tito 2:14; I Pet. 2:9). Pengine kwa siku hizi zetu tungeweza kusema kuwa Israeli ilikuwa taji la YHWH lililopambwa (yaani, kuyaeneza maarifa yake na ufunuo kwa mataifa yote). Tazama Mada Maalum:Upendeleo wa Kiinjilisti wa Bobkatika 4:6.

7:7 "Bwana hakuwapenda ninyi, wala hakuwachagua ninyi, kwa sababu mlikuwa wengi kuliko mataifa yote, maana mlikuwa wachache kuliko watu wote" KITENZI asilia(BDB 365 I, KB 362, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha "kubana kwa pamoja" au "kuunganisha" kama vile 10:15 (neno tofauti na upendo [kama vile mst. 8], bali kweli ile ile i katika 4:37) na huenda Isa. 38:17. Hiki KITENZI kinatumika kumaanisha shauku katika Mwa. 34:8; Kmb. 21:11).

Mstari huu unakazia juu ya kutokustahili, huruma isiyostahili, neema, na pendo la Mungu! Tazama Mada Maalum: Tendo la Neema ya YHWH katika Israeli katika 9:4-6. Kwa kawaida, ilikuwa vigumu Israeli kupenda kwa sababu ya ugumu na ukaidi (kama vile 9:6,13; 31:27). Neema ya Mungu inaonyeshwa vema zaidi kwa sababu ya uasi wa Israeli!

7:8 "sababu Bwana anawapenda" Mara nyingi Agano la Kale linakazia kwambaMungu atazitimiza ahadi zake juu ya baba zetu, Ibrahimu, Isaka, na Yakobo (kama vile Mwanzo 12, 15, 18, 26, 28). Lakini hapa Mungu anaonyesha kwamba alilifanya hili kwa sababu anakipenda kizazi hiki, pia!

☐**"akawatoa"** Hiki KITENZI(BDB 422, KB 425, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ni cha kawaida sana na kinatumika katika maana (mifano kutoka katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati):

1. halisi
 - a. jeshi lilijitokeza kwa ajili ya mapigano, 1:44; 2:32; 3:1; 20:1,10; 24:5; 29:7
 - b. chemchemi za maji zibubujikazo, 8:7
 - c. uliotoka, 9:7; 16:3,6
 - d. utazichukua nje shambani, 14:22; 28:38
 - e. akuletee nje ile rehani, 24:11
2. kistiari
 - a. akatutoa katika, 1:27; 4:20; 5:6,15, n.k.
 - b. katika vijiji, 2:23
 - c. akawakomboa, 7:8
 - d. kumzushia jina baya, 22:14
 - e. akawa mke wa mtu, 22:19; 24:2
 - f. utokapo, 28:6,19; 33:18
 - g. Hutavuka, 31:2

Ni muktdha pekee uwezao kudhihirisha maana halisi. Hii ndiyo kweli ya maneno yote!

☐**"akawakomboa"** Hiki KITENZI(BDB 804, KB 911, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinamaanisha "kununua kwa gharama." Hiki kilitumika katika tendo la kununua au kupata (1) mzaliwa wa kwanza (kama vile Kut. 13:1-22; Hes. 18:15-17) Walawi (Hes. 3:44-51) au (2) mtumwa (kama vile 15:15; 24:18, yaani, Israeli).

MADA MAALUM: FIDIA/KOMBOA

- I. AGANO LA KALE

- A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).
 2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
 - a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
 - b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozi wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
 - c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)
- B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
 - a. Kimaumbile
 - b. Kijamii
 - c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
 2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
 - a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
 - b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
 3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (i.e., *go'el*, BDB 145).
 4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
 - a. Baba
 - b. Mme
 - c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupitia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

II. AGANO JIPYA

- A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisi ni wa Kristo.
 2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laana" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenye dhambi wasingaitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!
 3. *Luō*, "kuweka huru"
 - a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
 - b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
 - 1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
 - 2) kujitoka mwenyewe kwa ajili ya kuwatakaswa watu (Tito 2:14)
 - 3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
 - c. *Lutrōsis*, "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
 - 1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68

- 2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
- 3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
4. *Apolytrōsis*
 - a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
 - 1) Luka 21:28
 - 2) Warumi 8:23
 - 3) Waefeso 1:14; 4:30
 - 4) Waebrania 9:15
 - b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
 - 1) Warumi 3:24
 - 2) 1 Wakorintho 1:30
 - 3) Waefeso 1:7
 - 4) Wakolosai 1:14
5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoka kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhambi pekee iliyokubaliwa, yeye aliyewafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).
- B. Dhana ya kitheolojia katika Agano Jipya.
 1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
 2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
 3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenuuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
 4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
 5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, theolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoka kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!
 6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufafanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbangu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

7:9 "jueni" Tazama maelezo kamili katika 4:35.125

■ Tambua ya kuwa iliwapasa Waisraeli "kujua" (BDB 393, KB 390, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kuhusu Mungu:

1. "Bwana ndiye Mungu" – NOMINO zote, kama vile 4:35,39 pamoja na KIBAINISHI CHA WAZI kabla ya neno *Elohim* la mwisho
2. "Bwana aliye mwaminifu" - BDB 52, *Niphal* ya WAKATI ENDELEVU, kama vile Isa. 49:7. Hili ndilo dai kuu la kithiolojia (kama vile Zaburi 89)! Hili linafasiliwa kupitia vipengele vinavyofuatia.
3. "mwazisikiliza hukumu hizi" - KITENZI, BDB 1036, KB 1581, *Qal* ya KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU, kama vile mst. 12; Mwa. 28:15,20; Yosh. 24:17; Zab. 146:6

4. “na rehema zake” - NOMINO, BDB 338, kama vile mist. 9,12; I Fal. 8:23; II Nya. 6:14; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4

Katika mwangaza wa hili iliwapasa:

1. wampendao, mst. 9, BDB 12, KB 17, *Qal* ya KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPO (kama vile 6:5; 7:13; 11:1,13,22; 13:3). Tazama maelezo kamili katika 5:10.
2. kushika amri zake, mst. 9, BDB 1036, KB 1581, *Qal* ya KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU. Tazama maelezo katika 5:1.

Ufahamu usawa uliopo kati ya uaminifu wa Mungu na uaminifu wa Israeli! Baraka toka kwenye uhusiano binafsi pendwa, wenye utii pamoja na YHWH zilibubujika kwa “kizazi cha maelfu. Neno maelfu ni stiari yenye kumaanisha utele mwingi, mara nyingi si halisi (kama vile Zab. 90:4; Ufu. 20:2,3,4,7). Tazama maelezo katika 5:9.

☐“Mungu mwaminifu” Tazama Mada Maalum katika 1:32.

7:10-11 Utambue mwitikio waYHWH kwa wale “wamchukiao” - BDB 971, KB 1338, *Qal* ya KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU, kama vile 5:9; Kut. 20:5; Hes. 10:35; II Nya. 19:2; Zab. 68:1; 81:15; 83:2; 139:21:

1. “nawapatiliza” - BDB 1, KB 2, *Hiphil* ya KITENZIJINA HALISI
2. “mbele ya macho yenu” - BDB 1022, KB 1532, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, yenye kumaanisha “fidia,” “lipiza,” kama vile Yer. 51:24

7:11 “amri, na sheria, na hukumu” Tazama Mada Maalum katika 4:1.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 7:12-16

¹² Na itakuwa, kwa sababu mwazisikiliza hukumu hizi, na kuzishika na kuzitenda, basi Bwana, Mungu wako, atakutimilizia agano na rehema aliyowaapia baba zako; ¹³ naye atakupenda na kukubarikia na kukuongeza tena atabarikia uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, nafaka zako na divai yako, na mafuta yako, maongeo ya ng'ombe zako, na wadogo wa kondoo zako, katika nchi aliyowaapia baba zako kuwa atakupa. ¹⁴ Utabarikiwa kuliko mataifa yote; hakutakuwa na mtu mume wala mke aliye tasa kati yenu; wala kati ya wanyama wenu wa mifugo. ¹⁵ Na Bwana atakuondolea ugonjwa wote; wala hatatia juu yako maradhi yo yote mabaya uyajuayo ya Misri, lakini atayaweka juu ya wote wakuchukiao. ¹⁶ Nawe angamiza mataifa yote atakayokupa Bwana, Mungu wako; jicho lako lisiwahurumie, wala usitumikie miungu yao; kwani litakuwa ni mtego kwako jambo hilo.

7:12 Utambue uhusiano wakimakubaliano (yaani, majukumu ya agano la pande mbili). Tambua kuwa “agano lake” na “wema wake” vinaanana.

7:13-15 Zitambue baraka za kiagano zaYHWH:

1. atakupenda
2. kukubariki
3. kukuongeza
4. atabariki uzao wa tumbo lako
5. atabariki uzao wan chi yako
 - a. nafaka zako
 - b. divai yako
 - c. mafuta yako
6. maongeo ya ng'ombe zako
7. hakutakuwa na tasa (kama vile Kut. 23:26)
 - a. mwanadamu (kama vile Mwa. 11:30; 16:1; 25:21; 29:31)
 - b. mifugo (kama vile 28:4; 30:9)
8. hapatakuwa na magonjwa (hili ni neno adimu lililotumika hapa tu na katika 28:10)
9. utawaangamiza adui zako

Hizi baraka tele (kama vile Kut. 23:25-26) pia zimwekwa bayana katika Kumbukumbu la Torati 28, lakini zimezungukwa na athari za kutokutii (kama vile Kumbukumbu la Torati 27 na 28:15-58). Asili ya amri ya agano la Musa ni dhahiri. Historia ya iliyobakia kuhusu Israeli inaweza kueleweka vema katika mwangaza wa Kumbukumbu la Torati 27-29. Ahadi na baraka za Mungu zinapatikana katika uaminifu, tumaini, utii wa Israeli pekee. Kamwe Israeli haikuweza kuhimili kiwango hiki cha utendaji, hivyo kulikuwa na hitaji la agano jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38; Wagalatia 3), lenye kujikita katika matendo ya YHWH.

Wafuasi wote wa Yesu walipendao Agano la Kale huomba na kutarajia uamsho wa wakati wa mwisho (kama vile Warumi 9-11). Lakini lazima ielezwe kwa usahihi, bila Yesu hakuna tumaini la agano (kama vile Yohana 14:6; 1:12; 3:16; 20:31).

7:16 “mtego” Ilikuwa lazima kuiepuka miungu ya Kikanaaniili wasiingie mtegoni (BDB 430, kama vile Kut. 23:33; Hes. 33:55; Yosh. 23:13; Amu. 2:3; 8:27; Zab. 106:36), ambao kifasihi ni “chambo cha mtego wa mnyama”!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LATORATI 7:17-26

¹⁷Nawe kama ukisema moyoni mwako, Mataifa haya ni mengi kunipita mimi; nitawatoaje katika milki yao?
¹⁸Usiwaogope; kumbuka sana Bwana, Mungu wako, alivyomfanya Farao na Misri yote; ¹⁹uyakumbuke hayo majaribu makuu yaliyoyaona macho yako, na hizo ishara, na maajabu, na mkono wa nguvu, na mkono ulionyoka, aliokutolea nje Bwana, Mungu wako; ndivyo atakavyowafanya Bwana, Mungu wako, mataifa yote unaowaogopa. ²⁰Tena Bwana, Mungu wako, atampeleka mavu kati yao, hata hao watakaosalia, hao wajifichao, waangamie mbele zako. ²¹Usiingiwe na kicho kwa sababu yao; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu katikati yako, Mungu mkuu, mwenye utisho. ²²Naye Bwana, Mungu wako, atayatupia nje mataifa yale mbele yako kidogo kidogo; haikupasi kuwaangamiza kwa mara moja, wasije wakaongezeka kwako wanyama wa mwitu. ²³Ila Bwana, Mungu wako, atawatoa mbele yako, atawatia mashaka, mashaka makuu, hata waishe kuangamizwa. ²⁴Na wafalme wao atakutilia mkononi mwako, nawe utalipoteza jina lao litoke chini ya mbingu; hapana mtu atakayeweza kusimama mbele yako, hata utakapokwisha kuwaangamiza. ²⁵Sanamu za kuchonga za miungu yao mtaziteketeza kwa moto; usitamani fedha wala dhahabu iliyo juu yao, wala usitwae iwe yako usije ukanaswa nayo; kwa maana ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako; ²⁶na machukizo usitie ndani ya nyumba yako, usije wewe kuwa kitu cha haramu mfano wake; ukichukie kabisa, na kukikataa kabisa; kwa kuwa ni kitu kilichoharimishwa.

7:17 “kama ukisema moyoni mwako” Hii ni nahau ya Kiebania ya kifungu “kama unafikiri au unamashaka” (kama vile mst. 21; 9:23; Zab. 95:8). Hoja kuu ya aya hii ni kuitia moyo Israeli:

1. kwa matendo ya YHWH dhidi ya Misri (yaani, mapigo), mist. 18-19
2. kwa matendo ya HWH yaliyoahidiwa dhidi ya Kanaan (yaani, mavu), mist. 20-24

7:18 “kumbuka sana” Hiki KITENZI (BDB 269, KB 269, *Qal* ya KITENZI JINA HALISI na *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinatumika mara kwa mara kwa ajili ya msistizo (kama vile 5:15; 7:2[mara mbili]; 8:18; 9:7,27; 15:15; 16:3,12; 24:9,18,22; 25:17;32:7). Yawapasa waamini kurejea nyuma ili kuuona mkono wa Mungu kwa wakati huu. Kama alivyokuwa katika wakati uliopita, hivyo atakuwa hivyo (“wale wanaompenda na kuzishika amri zake”). YHWH ametenda na atatenda katika historia badala ya watu wake!

7:19 Yatambue maneno ya kuyafasilimatendo ya YHWH ya kiukombozi katika Misri:

1. “yale majaribu makuu” BDB 152 na 650 II, kama vile 4:34; 29:3 (asili yenye kufanana [III] inatumika katika Israeli “kujaribu” YHWH kipindi cha kutangatanga jangwani, kama vile 6:16, 9:22)
2. “ishara” BDB 16, kama vile 4:34; 7:19; 26:8; 29:2; 34:11; Zab. 28:43; 105:27; 135:9
3. “maajabu” BDB 68, kama vile 4:34; 6:22; 7:19; 26:8; 34:11; Zab. 78:43; 105:27; 135:9
4. “mkono hodari” BDB 305 na 388, kama vile 4:34; 5:15; 6:21; 7:8,19; 9:26; 11:2; 26:8; 34:12, tazama maelezo katika 4:34
5. “mkono ulionyoshwa” BDB 283 na 639 (*Qal* ya KAULI TENDWA YA WAKATI ENDELEVU), kama vile 4:34; 5:15; 7:19; 9:29; 11:2; 26:8

Nimeweza kuonyesha ufanano ulio katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Pia huu unajitokeza katika kitabu cha Kutoka. Haya matendo ya YHWH ya kiukombozi ndilo tumaini kuu la Israeli! Huu ni ukamilifu wa ahadi juu ya Ibrahimu (kama vile Mwa.15:12-21). Huu ndiyo msingi wa agano la kitaifa.

7:20 “Mungu wako, atampeleka mavu” Kuna maana mbili za neno “mavu” (BDB 864): (1) kwa vyo vyote vile ni la kitamathali (kama vile Kumb. 1:44, lililoeleza juu ya jeshi kama kundi la nyuki) au (2) halisi (kaa vile Kut. 23:28; Yosh. 24:12, ambapo mavu waliagizwa na Mungu ili kuyatawanya majeshi ya kigeni). Mungu anawaonyesha watu wake kwamba anawapigania badala yao!

7:21 “Usiingiwe na kicho kwa sababu yao” Hiki KITENZI (BDB 791, KB 888, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinarudiwarudiwa mara kadhaa (kama vile 1:29; 7:21; 20:3; 31:6; Yosh. 1:9).

☑ **“Bwana, Mungu wako, yu katikati yako”** Hii ni kweli ya ajabu. Mungu mkuu, Aliye Mtakatifu, hukaa na watu wake (kama vile Kut. 29:45; Hes. 5:3; 35:34). Hivi ndivyo jina *Emmanuel* linavyomaanisha (kama vile Isa. 7:14; 8:8,10).

☑ **“Mungu mkuu, mwenye utisho”** Kifungu hiki kinaundwa na:

1. KIELEZI - “mkuu” BDB 42
2. *Niphal* ya WAKATI ENDELEVU - “utisho” BDB 431, KB 432

Wasifu huu wa YHWH (wenye kutumia shina la neno *Niphal*) pia unapatikana katika 10:17; Neh. 1:5; 4:14; 9:32; Dan. 9:4.

7:22 Mstari huu unaonyesha usawa kati ya nguvu ya YHWH (yaani, “atayatupia nje” BDB 675, KB 730, *Qal* ya WAKATI TIMILIFU) na mipaka ya mwanadamu:

1. “haikupasi kuwaangamiza kwa mara moja”
2. “wasije wakaongezeka kwako wanyama wa mwitu”

7:23 Matendo ya Mungu yanaelezwa kama:

1. “Bwana, Mungu wako, atampeleka mavu kati yao,” mst. 20
2. “Bwana, Mungu wako. . . atawatia mashaka, mashaka makuu, mst. 23 (NOMINO na KITENZI kinachotokana na asili ile ile), mst. 23, kama vile Kut. 23:27 (huu ni msamiati wa neno vita takatifu)
3. “Na wafalme wao atakutilia mkononi mwako,” mst. 24

7:24 “nawe utalipoteza jina lao litoke chini ya mbingu” Hiki KITENZI (BDB 1, KB 2, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI ULIOPO) kinatumika hapa katika mfumo wa na nahau ya ukamilifu na maangamizi ya jumla na kifo ili pasiwepe na vizazi (yaani, vita takatifu).

☑ **“hapana mtu atakayeweza kusimama mbele yako”** Hii ni nahau ya Kiebrania yenye kumaanisha mapigano ya kijeshi (yaani, majeshi mawili, kama vile 11:25; Yosh. 1:5; 10:8; 23:9).

7:25-26 Mistari hii inaelza namna Israeli ilivyopaswa kuitenda miungu ya Kikanaani (yaani, “Sanamu za kuchonga” (BDB 820 ya MUUNDO WA MANENO 43; tazama maelezo kamili katika 12:3):

1. “mtaziteketeza kwa moto” - BDB 976, KB 1358, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile mist. 5,25; 12:3
2. “usitamani fedha wala dhahabu”
 - a. usiitwae iwe yako usije, mist. 25,26
 - b. usije ukanaswa (BDB 430) nayo
 - c. na machukizo (BDB 1072, kama vile 12:3)
 - d. ni kitu kilichoharimishwa (yaani, “kitu kilicholaaniwa,” BDB 214)
 - e. usije wewe kuwa kitu cha haramu mfano wake (BDB 1055, vyote NOMINO na KITENZI), chenye (BDB 1073) kuchukiza

7:26 “kitu cha haramu” Kifungu hiki kililihusianishwa na neno *herem*, ambalo lilimaanisha “kujitoka kwa Mungu kwa ajili ya maangamizi ya jumla.” Mara nyingi hili linatafsiriwa kama “kwa chini ya zuio.” Matumizi mengine ya dhanana ya chini ya katazo yangukuwa kukufuru, hivyo, ilipaswa kuangamizwa jumla.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mungu alikuwa akichukua nchi ya taifa moja na kuligawia taifa lingine?
2. Je! Biblia inasema, “Hakuna” kuoana watu wa jamii tofautitofauti?

Je! inamaanisha nini kwamba Mungu aliichagua Israeli kama watu wa kipekee

KUMBUKUMBU LA TORATI 8

MIGAWANYO YA AYA KATIKA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Mkumbuke Bwana, Mungu wako	Jaribu la kiburi na kujiona kuwa wanaweza	Nchi nzuri inamilikiwa	Majaribu jangwani
8:1-10	8:1-10	8:1-10	8:1-4 8:5-6 Nchi ya ahadi na majaribu yake
		Onyo dhidi ya kumsahau Bwana	8:7-10
8:11-20	8:11-20	8:11-20	8:11-16 8:17-20

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi) *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozokwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiyaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. Nk.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 8:1-10

¹Amri hii ninayokuamuru leo mtaishika kuitenda, mpate kuishi na kuongezeka, na kuingia katika nchi ile ambayo Bwana aliwaapia baba zenu; nanyi mtamiliki. ²Nawe utaikumbuka njia ile yote Bwana, Mungu wako aliyokuongoza miaka hii arobaini katika jangwa, ili akutweze, kukujaribu kuyajua yaliyo moyoni mwako, kwamba utashika amri zake, au sivyo. ³Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiojua wewe wala baba zako hawakujua; apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana. ⁴Mavazi yako hayakuchakaa, wala mguu wako haukuvimba, miaka hiyo arobaini. ⁵Nawe fikiri moyoni mwako, ya kuwa kama vile baba amrudivyo mwanawe, ndivyo Bwana, Mungu wako, akurudivyo. ⁶Nawe uzishike amri za Bwana, Mungu wako, upate kwenda katika njia zake, na kumcha. ⁷Kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yuakingiza katika nchi nzuri, nchi yenye vijito vya maji, na chemchemi, na visima, vibubujikavyo katika mabonde na milima; ⁸nchi ya ngano na shayiri, na mizabibu, na mitini, na mikomamanga; nchi ya mizeituni yenye mafuta, na asali; ⁹nchi utakayokula mikate humo, pasina

shida, hutapungukiwa na kitu ndani yake; nchi ambayo mawe yake ni chuma, na milima yake yafukuka shaba.
¹⁰Nawe utakula ushibe, utamshukuru Bwana, Mungu wako, kwa nchi nzuri aliyokupa.

8:1 “Amri hii ninayokuamuru leo” Tambua NOMINO hii (BDB 846, tazama Mada Maalumu katika 4:1) na KITENZI (BDB 845, KB 1010, *Piel* KAULI ENDELEVU) ni SHAMIRISHO (kutoka asili ile ile).

☐“**mtaishika kuitenda**” KITENZI hiki (BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, tazama muhtasari katika 6:12) kimetumika mara nyingi katika Kumbukumbu la Torati (kama vile *Qal*, 4:2,6,9,40; 5:1,10,12,29,32; 6:2,3,17[mara mbili],25; 7:8,9,11,12[mara mbili]; 8:1,2,6,11; 10:13; 11:1,8,22[mara mbili],32; *Niphal* 2:4; 4:9,15,23; 6:12; 8:11; 11:16). Kifungu hiki kinaonyesha kwamba uhusiano wa kupenda agano na utiifu ni njia ya Mungu ya kumbariki mwanadamu na kuzitimiliza ahadi zake (kama vile mist. 2,6,16, 18; 4:1).

☐“**mtaimiliki nchi**” Tazama Mada Maalumu chini.

MADA MAALUM: KUIMILIKI NCHI (katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati

KITENZI hiki (BDB 439, KB 441, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinarumika kwa kurudiwarudiwa katika uhusiano na

1. Ahadi/kiapo cha YHWH/ kwa Mababa wa Imani (kama vile Kumb. 1:8; 10:11)
2. Israeli ikitembea katika ahadi hizi na kuingia ndani ya nchi (kama vile Kumb. 2:24; 3:18-20)
3. Hii inafanana na neno "urithi" (Kumb. 3:28)
4. Lazima Israeli ilitii agano ili kuulinda umiliki wa agano (kama vile Kumb. 4:1,5,14; 6:1; 8:1; 11:8-9,26-32; tazama Mada Maalum: Shika)

Katika ahadi ya YHWH kwa Ibrahimu (Mwanzo 12) alijikita katika mambo mawili: (1) uzao wa Ibrahimu na (2) Nchi ya Ahadi (yaani, Kanaani, kama vile Mwa. 15:12-21). Agano la Kale linajikita katika #2 na Agano Jipya linajikita katika #1. Lazima ikumbukwe kuwa nchi iliyoahidiwa kwa Israeli ilikuwa na amri ya ulitii wa agano (kama vile Kumbukumbu la Torati 27-30). Tendo la kutolitii agano ndilo lililosababisha uhamisho wa Ashuru na Babeli.

Sina uhakika kwamba utawala wa sasa wa Israeli (yaani, 1947) ni utimilifu wa nabii za Agano la Kale kwa sababu si taifa la toba, utii. Ni asilimia 5% ya raia wake wanajiudhulisha katika sinagogi mara kwa mara. Hii ni demokrasia ya kisiasa, ya kidunia, ni ya Ulaya. Hawa ni wafuasi wa kisheria lakini si haki za Israeli za ahadi za Agano la Kale.

Wengi wamejaribu kuzifanya ahadi hizi kuwa za watu wa jamii moja (yaani, Mwa. 12:1-3) lakini Wayahudi wengi wa sasa si uzao wa kimwili wa Ibrahimu (yaani, Kiksemiti) bali ni wale waliobadili itikadi za kisiasa na kidini toka Ulaya (yaani, Khazars wa asili ya Turkish, waliobadili itikadi zao na kuwa katika Dini ya Kiyahudi mnamo B.K. 740) au Afrika (yaani, Wayahudi wa ki-Ethiopia).

Agano la YHWH (tazama Mada Maalum: Agano) la ki-masharti!

8:2 “utaikumbuka” KITENZI hiki (BDB 269, KB 269, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, Kama vile 5:15; 7:18[mara mbili]; 8:2,18; 9:7,27; 15:15; 16:3,12; 24:9,18,22; 25:17; 32:7), “utaikumbuka,” kimetumika katika njia mbili katika Agano la kale. Linahitajika agano la mwanadamu ili kukumbuka matendo ya Mungu na sheria zake. Hii ilikuwa ni Nahau ya Kiebrania, “mkumbuke Mungu kama kumtanguliza.” Ni maombi ya mwanadamu kwamba Mungu hazikumbuki dhambi zetu.

☐“**katika jangwa**” Israeli (yaani, walimu wake) aliangalia nyuma katika kipindi cha kutangatanga jangwani kama “fungate la wanandoa” kati ya YHWH na Israeli. Mungu hakuwahi kamwe kuwa karibu zaidi na watu wake kama katika wakati huu mgumu kwa sababu wao walimtegemea yeye kwa kila kitu. Na sasa walikuwa na utele na Baraka katika nchi ya ahadi. Mungu aliwaonya waendele kumtegemea yeye kwa sababu yeye alikuwa chanzo cha kila kitu (kama vile mst. 18).

☐“miaka arobaini” Namba hii mara nyingi imetumika katika njia ya stiari ili kuonyesha kipindi kirefu cha muda, muda mrefu zaidi ya mzunguko wa mwezi (yaani, siku 28). Hata hivyo, kwa nyakati zingine ilikuwa dhahili. Mara nyingi ni vigumu kujua ni kipi cha kuchagua pasipo taarifa nyingine za kihistoria au kimaandiko. Mwisho wa kipindi cha kutangatanga jangwani ni miaka 38.

☐“ili akutweze, kukujaribu” Tambua mfuatano:

1. KIUNGANISHI, “ ili ” (BDB 775)
2. vitatu *Piel* ya VITENZI JINA HALISI CHA MUUNDO WA MANENO:
 - a. “ili akutweze” (BDB 776, KB 853, kama vile mist. 2,3,16)
 - b. “ili kukujaribu” (BDB 650, KB 702, kama vile mst. 16)
 - c. “ili kuyajua” (BDB 393, KB 390, kama vile mist. 2[mara mbili],3,[mara tatu],5,16)

Mungu anataribu (BDB 650, KB 702, *Piel* ya KITENZIJINA HALISI CHA MUUNDO WA NANENO, mst. 16; 13:3; Amu. 2:22; 3:1,4) sisi na mtazamo wa kuendelea kuimarisha imani yetu (mf. Mwa. 22:1; Kut. 15:25; 16:4; 20:20; Kumb. 8:2,16; 13:3; Amu. 2:22; II Nya. 32:31 na Mt. 4:1; Ebr. 12:5-13). Ikiwa sisi ni wana wa Mungu tutajaribiwa! Zaidi tunajaribiwa katika eneo la maisha yetu ambacho ndiyo kipaumbele kwetu. Kujaribiwa kunamaanisha kutufanye sisi tufanane zaidi na Kristo.

Neno “akutweze” (BDB 776, KB 853, *Piel* ya KITENZIJINA HALISI CHA MUUNDO WA MANENO) limetumika katika mist. 2,3,16. Agano la Kale pekee linamuita Musa mtu mpole (kama vile. Hes. 12:3; na muda mwingi katika Zaburi) na Agano Jipya linamuita Yesu mpole (kama vile Mt. 11:29). Mungu anatamani dhamira ya upole na kuaminika kwa watu wake (mf, 10:3; Ezra 8:21).

Neno “moyo” limetumika kitamathari kwa ajili ya nia zetu (kama vile mst. 2,5,14, na 17). Tazama Mada Maalumu katika 2:30.

MADA MAALUMU: MUNGU ANAWAJARIBU WATU WAKE (AGANO LA KALE)

Neno "jaribu" (BDB 650, KB 702, *Piel* kauli ya wakati uliopo; Mwa. 22:1) ambalo linatumika katika namna ya "kufanya jaribio." Linatumika katika namna ya kumleta mtu katika sehemu ambapo wanatambua na kufanyia kazi vipaumbele vyao walivyojiwekea wenyewe. Ni wazi kutoka Mwanzo 12 mpaka 22 kwamba Mungu anampatia Ibrahimu mfululizo wa mazingira (walimu wa Kiyahudi wanasema ni kumi) ili aweke shabaha ya upendo wake na tumaini katika Mungu na Mungu tu (yawezekana pia Ayubu). Majaribu haya hayakuwa sana kwa ajili ya Mungu, lakini kwa ajili ya Ibrahimu na uelewa wake kwa Mungu aliyemuita kutoka Uru ya Wakaldayo. Ibrahimu anaamriwa aache familia yake, nyumba, marafiki, urithi, desturi na hata maisha yake ya baadaye (mwana wake aliyehaidiwa katika Mwanzo 22) kumfuata Mungu kwa Imani. Mungu anawajaribu watoto wake wote katika eneo la vipaumbele vyao (kama vile Mt. 4: na kuendelea; Ebr. 5:8; 12:5-13).

Mungu anajaribu (BDB 650) ili aweze kujua (BDB 393; tazama Mada Maalumu: Kujua). Israeli mara kwa mara walimjaribu Mungu kwa kutotii kwao na Mungu alithibitisha kuwa kweli kwa neno lake. Sasa Mungu atawapa Israeli na watu wake nafasi ya kuonesha uaminifu wao unaotajwa na imani.

1. Mungu aliwajaribu watu wake kwa pamoja
 - a. Kutoka 15:25; 16:4; 20:20
 - b. Kumbukumbu la Torati 8:2,16; 13:3
 - c. Waamuzi 2:22; 3:1,4
2. Mungu aliwajaribu Waisraeli mmoja mmoja
 - a. Ibrahimu, Mwanzo 22:1-12
 - b. Hezekia, 2 Nyakati 32:31
3. Waandishi wa Zaburi wanalia kwa Mungu kuwajaribu ili aondoe uchafu uliojificha (kama vile Zab. 26:2; 139:23)
4. Watu wa Mungu wa Agano Jipya pia wanajaribiwa, kama ilivyokuwa kwa Yesu (Mathayo 4; Luka 4; Ebr. 5:8). Angalia Mada Maalumu: Maneno ya Kiyunani kwa Kujaribiwa na Visawe Vyake.

Tazama [Mada Maalumu: Istirahi za Kujaribu na Visawe vyake](#)

8:3 “mana” Hiki (BDB 577 I, watu walikiita “mana” [Kut. 16:31] toka katika swali la kwenye kitabu cha Kut.16:15, “Nini hiki?” Musa alikiita “mkate kutoka mbinguni,”Kut. 16:4) kilikuwa ni chakula maalumu kilichotolewa na Mungu kipindi cha wakati wa kutangatanga jangwani. Kimeelezwa katika Kut. 16:4, 14-15; 31; Hes. 11:7-8, lakini kiini chake halisi hakijulikani kwetu (BDB inasema kinafahamika kwa Mabedui huko Sinai na kwamba hasa hasa ni juisi kutoka katika tawi la mti fulani, lakini hii haifai kwa maelezo ya Kibiblia). Mungu alitoa kile walichohitaji kwa kila siku, sio kwa ajili ya muda mrefu ili watu waweze kujifunza kumwamini Yeye kwa ajili ya mahitaji ya kila siku. Alitenda hivi pia kwa ajili ya waaminio wa agano jipya (kama vile Mt. 6:11).

☐“**usiyojua**” Hii (BDB 393, KB 390) asili imetumika mara tatu katika kifungu hiki (tazama muhtasari kamili katika 4:35):

1. “usiyojua wewe” - *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
2. “wala baba zako hawakujua” - *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
3. “apate kukujulisha” - *Hiphil* ya KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO

Pia tambua baadhi ya sehemu katika sura hii:

mst. 2 “ili kuyajua” - *Qal* ya KITENZIJINA CHA MAUUNDO WA MANENO

mst. 5 “fikiri” - *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU

mst. 16 imerudiwa #2

☐“**kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu**” Hiki ni mojawapo ya vifungu ambavyo Yesu alikitumia kwa shetani katika majaribu yake (kama vile Mt. 4:14; Luka 4:4). Wanadamu wanahitaji, uhusiano binafsi wa kuaminika na Mungu zaidi kuliko kitu chochote (mf. Zab. 42:1-4; 63:1; 143:6, Augustino anasema katika kila mtu kuna umbo la mungu)! Mwili hautoshi kwa ajili ya uzima halisi (yaani, “kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana”).

8:4 “Mavazi yako hayakuchakaa” Rashi (mtoa maoni wa Kiyahudi wa zama za kati) na shahidi Justini (baba wa kanisa la awali) wotewanadai kwamba mavazi ya watoto yalikuwa kadri watoto walivyokua na kamwe hayakuzeeka (kama vile Kut. 29:5 inaongeza hata viatu vyao; Neh. 9:21)! Maelezo ya ajabu kiasi gani ya usimamizi wa Mungu kwa ajili kila hitaji.

☐“**wala mguu wako haukuvimba**” Hiki ni KITENZI adimu cha Kiebrania (BDB 130, KB 148, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Neh. 9:21) kinachomaanisha “kuvimba.” Asili ile ile kama ya NOMINO inayorejelea ongezeko la mkate. Hii inadai kwamba maumbo yao kimwili yalikuwa pia imara ili kuhimili safari ndefu, na ngumu.

8:5 “kama vile baba amrudivyo mwanawe, ndivyo Bwana, Mungu wako, akurudivyo” Hapa ni mfanano maalumu wa YHWH kama baba mwenye upendo (kama vile Mit. 3:15). Anaturudi sisi kwa ajili ya mema yetu (Ebr. 12:5-13). Tazama Mada Maalumu katika 2:15. Tazama Mada Maalumu chini.

MADA MAALUM : UBABA WA MUNGU

- I. Agano la Kale
 - A. kuna maana kuwa Mungu ni Baba kwa maana ya uumbaji.
 1. Mwa. 1:26-27
 2. Mal. 2:10
 3. Mdo. 17:28
 - B. Baba ni ushabihiano uliotumika katika maana mbalimbali.
 1. baba wa Israeli (kwa kuchaguliwa)
 - a. "Mwana" – Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 3:19; 31:9,20; Hosea 1:10; 11:1; Mal. 1:6
 - b. "mzaliwa wa kwanza" – Yer. 31:9
 2. baba wa mfalme wa Israeli (kwa maana ya Kimasihi)
 - a. 2 Sam. 7:11-16
 - b. Zab. 2:7; Mdo. 13:33; Ebr. 1:5; 5:5

- c. Hosea 11:1; Mt. 2:15
- 3. mshabihiano wa kuwapenda wazazi
 - a. baba (stiari)
 - 1) abebavyo mwanae – Kumb. 1:31
 - 2) kumwadibisha – Kumb. 8:5; Mith. 3:12
 - 3) mtoaji (yaani., Kutoka) – Kumb. 32:6
 - 4) hatawasahau – Zab. 27:10
 - 5) huwapenda – Zab. 103:13
 - 6) rafiki/mlinzi – Yer. 3:4
 - 7) mponyaji/mwenye kusamehe – Yer. 3:22
 - 8) hukupa rehema – Yer. 31:20
 - 9) mfundishaji – Hosea 11:1-4
 - 10) mwana wa pekee – Mal. 3:17
 - b. mama (stiari)
 - 1) hatawasahau – Zab. 27:10
 - 2) upendo wa mama aleaye – Isa. 49:15; 66:9-13 na Hosea 11:4 (pakiwepo na mpango wa marekebicho ya kimuktadha wa neno "nira" kwenda "mtoto mchanga")

II. Agano Jipya

A. Utatu (maandiko yote matatu yametaja)

- 1. Injili
 - a. Mt. 3:16-17; 28:19
 - b. Yohana 14:26
- 2. Paulo
 - a. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
 - b. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
 - c. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
 - d. Gal. 4:4-6
 - e. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4
 - f. 1 The. 1:2-5
 - g. 2 The. 2:13
 - h. Tito 3:4-6
- 3. Petro – 1 Pet. 1:2
- 4. Yuda – Mistari ya 20-21

B. Yesu

- 1. Yesu kama "mwana apendezwaye nae" – Yohana 1:18; 3:16,18; 1 Yohana 4:9
- 2. Yesu kama "Mwana wa Mungu" – Mt. 4:3; 14:33; 16:16; Luka 1:32,35; Yohana 1:34,49; 6:69; 11:27
- 3. Yesu kama mpendwa – Mt. 3:17; 17:5
- 4. Matumizi ya Yesu ya neno *abba* kwa ajili ya Mungu – Marko 14:36
- 5. matumizi ya Yesu ya VIHISISHI kuonyesha vyote kuhusu Yeye na uhusiano wetu na Mungu
 - a. "Baba Yangu," mf., Yohana 5:18; 10:30,33; 19:7; 20:17
 - b. "Baba yako," mf., Mt. 5:16,45,48; 6:1,4,6,8,9,14,15,18,26,32; 7:11; 10:20,29; 18:14
 - c. "Baba yetu," mf., Mt. 6:9,14,26

C. moja ya stiari nyingi za kifamilia kuelezea ushirika wa ndani kati ya Mungu na mwanadamu:

- 1. Mungu kama Baba
- 2. waamini kama
 - a. wana wa Mungu
 - b. watoto
 - c. wamezaliwa na Mungu
 - d. wamezaliwa mara ya pili

- e. wameasiliwa
- f. wamezaliwa
- g. familia ya Mungu

8:6 “upate kwenda katika njia zake” Hiinistiari iliyozeleka kibiblia kwa ajili ya mtindo wa maisha (mf. 5:33; 8:6; 10:12; 11:22; 19:9; 26:17; 28:9; 30:16). Mungu anatumia sisi tuishi kwa ajili yake kila siku. Imani ya kibiblia sio kanuni ya imani, wala tendo la sakramenti, wala fundisho la somo wala utaratibu wa kithiolojia, lakini ni uhusiano wa kila siku na Mungu.

☐**“na kumcha”** Hiki *Qal* KITENZI CHA MUUNDO WA MANENO kinafanana na neno “kudembea.” Hii ni dhana ya hofu na heshima (kama vile 4:10; 5:29; 6:2,13,24; 7:19; 8:6; 10:12,20; 13:4; 14:23; 17:19; 31:12-13).

8:7-10 Huu ni msisitizo juu ya thamani ya maji kwenye jamii ya watu walimaji na aridhi isiyo na rutuba ya nchi ya ahadi. Katika makala za kale za Mesotamia, Palestina ilikuwa inafahamika kama “nchi itoayo maziwa na asali” (kama vile Kut. 3:8,17; 13:5; 33:3; Kumb. 6:3; 11:9; 26:9; 27:3; 31:20). Pia ilikuwa na madini mengi sana, mst. 9. Baraka za Mungu kwa Israeli zilimaanisha kuanzisha mwikio wa furaha (kama vile mst.10). Mungu anatamani sisi tufurahie uumbaji wake lakini kwa ajili ya kukumbuka kwamba ndiye aliyetupatia.

8:10 sehemu ya kwanza ya kifungu hiki ni chanzo cha mamlaka ya walimu wa Kiyahudi ya kunawa baada ya kumaliza kula. Hii ni aina ya uandishi usio wa kimkutadha, ijapokuwa ni wa Mungu, hauhusiani na “kusudi la mwandishi”!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 8:11-20

¹¹Jihadhari, usije ukamsahau Bwana, Mungu wako, kwa kutozishika amri zake, na hukumu zake, na sheria zake, ninazokuamuru leo. ¹²Angalia, utakapokuwa umekula na kushiba, na kujenga nyumba nzuri na kukaa ndani yake; ¹³na makundi yako ya ng'ombe na kondoo yatakapoongezeka, na fedha yako na dhahabu yako itakapoongezeka, na kila kitu ulicho nacho kitakapoongezeka; ¹⁴basi hapo moyo wako usiinuke, ukamsahau Bwana, Mungu wako, aliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa; ¹⁵ aliyekuongoza katika jangwa lile kubwa lenye kitisho, lenye nyoka za moto na nge, nchi ya kiu isiyokuwa na maji; aliyekutolea maji katika mwamba mgumu, ¹⁶ aliyekulisha jangwani kwa mana, wasioyijua baba zako; apate kukutweza, apate kukujaribu, ili kukutendea mema mwisho wako. ¹⁷ Hapo usiseme moyoni mwako, Nguvu zangu na uwezo wa mkono wangu ndio ulionipatia utajiri huo. ¹⁸ Bali utamkumbuka Bwana, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo. ¹⁹ Lakini itakuwa, kama ukimsahau Bwana, Mungu wako, na kuiandama miungu mingine, na kuitumikia na kuiabudu, nawashuhudia leo ya kuwa mtaangamia bila shaka. ²⁰ Kama vile mataifa yale ambayo Bwana anawaangamiza mbele yenu, ndivyo mtakavyoangamia; kwa sababu hamkutaka kuisikiliza sauti ya Bwana, Mungu wenu.

8:11 “Jihadhari” KITENZI hiki (BDB 1036, KB 1581, *Niphal* KAULI SHURUTISHI, kama vile 5:12; ;8:6; 11:8; 16:1) kinatafsiriwa “tunza,” “angalia,” “kuwa makini kutenda” (tazama muhtasari katika 6:12). Kinaitwa kuwa mtiifu.

☐**“ukamsahau”** KITENZI hiki (BDB 1013, KB 1489, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, kama vile 4:9,23,31; 6:12; 8:11,14,19[mara mbili]; 9:7; 25:19) ni kinyume cha neno “kumbuka” (kama vile 5:15; 7:18; 8:2,18; 9:7,27; 15:15; 16:3,12; 24:9,18; 25:17; 32:7). Huu ni mwelekeo wa kuridhisha, anguko la mwanadamu, hata mwanadamu wa kidini. Tunaposahau Baraka za Mungu tunajidanganya katika kufikiri kwamba tunatenda wenyewe kwa uwezo wetu! Mtoaji lazima apewe kipaumbele, sio zawadi (kama vile Zab. 103:20)!

☐**“Bwana, Mungu wako”** Tambua walikuwa wanamkumbuka Mungu na njia sahihi ya kutenda ni utiifu (kama vile Luka 6:46). Kwa ajili ya majina ya Uungu, tazama Mada Maalumu katika 1:3.

☐ **“amri zake, na hukumu zake, na sheria zake”** Tazama Mada Maalumu: Maneno kwa ajili ya ufunuo wa Mungu katika 4:1.

8:13 “yatakapoongezeka” Hiki KITENZI (BDB 915, KB 1176, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kimerudiwa mara tatu ili kuonyesha aina tofauti za Baraka za Mungu.

8:15 “nyoka wakali” Inatia mashaka ikiwa (KIVUMISHI, BDB 977 I na NOMINO BDB 638) walikuwa na jina hili kwa sababu ya rangi yao (kutoka KITENZI) au maumivu (kutoka katika sumu) ya kuumwa kwao (kama vile Hesabu 21).

☐ **“aliyekutolea maji katika mwamba mgumu ”** Tukio hili limeandikwa katika kitabu cha Kut. 17:6 na tena katika kitabu cha Hes. 20:11. Paulo, katika kitabu cha I Kor. 10:4, anasema mwamba huu ulikuwa ni kielelezo cha utoaji wa kimasihwa wa Mungu.

8:16 YHWH analeta jaribu ili kubariki (mf. Ibrahimu katika Mwanzo 22; Israeli katika Kut. 20:20; mana katika Kut. 16:4). kujukaribu (BDB 650, KB 702) hata katika maombi kwenye Zab. 26:2 na katika maneno tofauti, lakini fikra ile ile, katika Zab. 139:1,23.

8:17 “Nguvu zangu na uwezo wa mkono wangu ndio ulionipatia utajiri huo” Angalia maneno ya kujitapa na kiburi (kama vile mst. 18; Yakobo 4:13-17). Tazama Mada Maalumu: Matendo ya Rehema za YHWH kwa Israeli katika 9:4-6.

8:18 “Bali utamkumbuka ” tazamamuhtasari katika 7:18.

☐ **“alifanye imara agano lake alilowapa baba zako ”** Ushindi wa YHWH ulikuwa unafikia kilele cha mpango wa ukombozi uliorudi nyuma kwenye kitabu cha Mwa. 3:15; 12:1-3; 26:24; 28:13-15. Tungo hii imekuwa uthibitisho uliojirudia katika kitabu cha Kumbukumbu (kama vile 1:8; 6:10; 8:18; 9:5,27; 29:13; 30:20; 34:4). KITENZI (BDB 989, KB 1396) ni *Niphal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, ambacho katika ahadi za agano kinaweza kuwa KAULI TENDWA au YENYE KUJIREJEA (mf, Mwa. 12:3).

8:19 Matokeo ya kutokutii ni dhahili kama matokeo ya utiifu! Tambua VITENZI “kuiandama” (BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU), “kuitumikia” (BDB 712, KB 773, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU), na “kuiabudu” (BDB 1005, KB 295, *Hishtpaphel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) vinafanana.

☐

NASB “kama ukimsahau Bwana”

NKJV “ikiwa kwa maana yeyote umemsahau Bwana”

NRSV “ikiwa umemsahau Bwana”

TEV “kamwe usimsahau Bwana”

NJB “jihadhari, kama umemsahau Yahweh”

Muundo ni KITENZI “kusahau” (BDB 1013, KB 1485) chenye kujirudia, KITENZI JINA HALISI kinafuatiwa na *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU. Uundaji huu ni mbinu ya kiebrania ya kutilia mkazo. Muundo huu huu unaonekana na neno “kuangamia” katika mst. 19.

8:20 “mtaangamia” Tambua kwamba katika mist. 19 na 20 KITENZI “kuangamia” (BDB 1, KB 2) kimetumika mara nne (KITENZI JINA HALISI katika mst. 19; *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU mara mbili katika mist. 19 na 20, na *Hiphil* KAULI ENDELEVU katika mst. 20).

Haya ni maneno ya maonyo yaliyozoeleka katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Yametumika katika njia kadhaa:

1. Mungu atawaangamiza wana wa Israeli ikiwa hawatatii agano lake - 4:26 (mara mbili); 8:19,20; 9:3; 11:17; 28:20,22,51,63; 30:18(mara mbili).
2. Mungu anawaamuru Israeli kuwaangamiza kabisa Wakanaani - 7:24; 8:20; 12:2,3.

3. Mungu atawaangamiza wale wanaomchukia yeye - 7:10.

4. Mungu ataliangamiza jeshi la Wamisri - 11:4

Israeli watawekwa chini ya matokeo ya “vita takatifu” ikiwa wataliacha agano (Kumbukumbu la Torati 27-29)! Mungu hawaheshimu watu!

Kuna matokeo ya hatari kwa ajili ya kutokutii kama vile faida kubwa kwa ajili ya utiifu. Haki hureta kuwajibika ! “na kila aliyepewa vingi, kwake vitatakwa vingi” (kama vile Luka 12:48)!

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha miujiza ya Mungu ambayo aliitenda kwa watu wake jangwani ambayo imetajwa katika sura ya 8.
2. Je! Mungu aliwajaribu watu wake? Kwa nini?
3. Kwa nini shida ya kutokuwa wanyenyekevu imetokea mara nyingi kati

KUMBUKUMBU LA TORATI 9

MIGAWANYO YA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Uasi wa Israel unahakikiwa	Jaribu la kujihesabia haki	Ukaidi wa watu	Ni Yahwe, na sio Israel, Anapata ushindi
9:1-12	9:1-3 9:4-5	9:1-3 9:4-6	9:1-6
	9:8-14	9:7-11	Mwenendo wa Israel huko Horeb; Musa anaingilia kati 9:7-14
9:13-24	9:15-21	9:12 9:13-14 9:15-21	9:15-21
Israel imetenda dhambi			Tena. ombi la Musa
	9:22-24	9:22-24	9:22-24
9:25-29	9:25-29	9:25-29	9:25-29

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Taz. uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu nimwongozokwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (ukisoma mzunguko wa #3, uk. viii).linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 9:1-6

¹Sikiza, Ee Israeli; hivi leo unataka kuvuka Yordani uingie kwa kuwamiliki mataifa yaliyo makubwa, na yenye nguvu kukupita wewe, miji mikubwa iliyojengewa kuta hata mbinguni, ²watu wakubwa, warefu, wana wa Waanaki, uwajuao, uliokuwa ukisikia wakitajwa hivi, Ni nani awezaye kusimama mbele ya wana wa Anaki? ³Basi jua siku hii ya leo kuwa Bwana, Mungu wako, ndiye atanguliaye kuvuka mbele yako kama moto uteketezao; atawaangamiza, tena atawaangusha mbele yako; ndivyo utakavyowafukuza na kuwapoteza upesi, kama alivyokuambia Bwana. ⁴ Usiseme moyoni mwako, Bwana, Mungu wako, atakapokwisha kuwasukumia nje mbele yako, ukasema, Ni kwa haki yangu alivyonitia Bwana niimiliki nchi hii; kwani ni kwa ajili ya uovu wa mataifa haya Bwana awafukuza nje mbele yako. ⁵ Si kwa haki yako, wala kwa unyofu wa moyo wako, hivi uingiavyo kuimiliki nchi yao; lakini ni kwa uovu wa mataifa haya Bwana, Mungu wako, awafukuza nje mbele yako; tena apate kuliweka imara hilo neno Bwana alilowaapia baba zako Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo. ⁶ Basi jua ya kuwa Bwana, Mungu wako, hakupi nchi hii nzuri uimiliki kwa ajili ya haki yako,

9:1 “Sikia” Hili ni neno la Kiebrania *shema* (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI, k.v. 4:1; 5:1; 6:3,4; 9:1; 20:3; 27:9), lenye kumaanisha “kusikia ili kutenda.” Tazama maelezo katika 4:1.

☐“**Ee, Israel**” Tazama Mada Maalum katika 1:1.

☐“**yaliyo makubwa, na yenye nguvu kukupita wewe**” Hii ni dhamira inayojirudia (tazama maelezo katika 1:28). Wazo la kithiolojia (yaani., uchaguzi wa YHWH mwenye Enzi na ahadi Yake kwa wazee wa imani) ipo katika 7:6-9. Ni mwaminifu na mkweli. Tabia yake ni ya ajabu kwa Israel iliyokaidi na yenye shingo ngumu (k.v. mistari ya 6,7,13,24,27; 10:16; 31:27).

9:2 “Waanaki. . wana wa Anaki” Kiuasili wa neno, hili neno linamaanisha “shingo ndefu” na, hivyo basi, linarejelea kwenye majitu. Katika Kumb. 2:10-11 linahusiana na *Rephaim* na katika Hes. 13:33 linahusiana na *Nephilim*. Tazama Mada Maalum katika 1:28.

☐“**jua**” Tazama maelezo kamili katika 4:35.

9:3 “siku hii ya leo” KITENZI(BDB 393, KB 390, *Qal* KAULI YA WAKATI ULITIMILIFU) kinatumika mara kadhaa na kwa maana mbalimbali. Tazama Mada Maalum katika 4:35.

☐“**moto uteketezao**” Hii ni BDB 77 pamoja na BDB 37. Hii stiri inaelezea hukumu ya Mungu juu ya watu wake walioko katika nchi kwa sababu ya uovu wao (k.v. mst.4-5; Mwa. 15:16). Tazama maelezo katika 4:24. Kwa ajili ya mjadala mzuri wa maelezo yaliyotumika kumweleza Mungu tazama *The Dictionary of Biblical Imagery*, kur.332-336.

☐“**atawaangamiza, tena atawaangusha mbele yako**” Hivi VITENZI viwili vya ushindi vinafanana na kuyaelezea matendo ya YHWH kwa niaba ya Israeli:

1. “atawaangamiza” - BDB 1029, KB 1552, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU
2. “atawaangusha” - BDB 488, KB 484, *Hiphil* KAULI ISITIMILIFU

Pia tambua kuwa Israeli lazima itende kwa imani na kushambulia:

1. “utakavyowafukuza” - BDB 439, KB 441, *Hiphil* KAULI ILIYO TIMILIFU
2. “kuwaangamiza upesi” - BDB 1, KB 2, *Hiphil* KAULI ILIYO TIMILIFU pamoja na KITENZI(BDB 555 II)

Tambua mlinganyo uliopo wa kimaagano na kithiolojia kati ya kitendo cha ahadi cha Mungu mwenye Enzi na mamlaka waliopewa viongozi na jeshi la Israeli kuwajibika kwa uaminifu. Yote ni ya muhimu! Pia itambulike kuwa YHWH alimaliza kazi Yake, lakini Israeli haikumaliza kazi ya kuwaondoa moja kwa moja wale wakazi wa asili waliokuwepo katika nchi (k.v. Waamuzi 1-2). Israeli walipaswa kuwaangamiza upesi (. 7:22), lakini haikufanya hivyo!

9:4-6 “moyoni mwako, Bwana, Mungu wako, atakapokwisha kuwasukumia nje mbele yako, ukasema, Ni kwa haki yangu” Hii inafanana na 8:11-20. Mungu anawaonyesha watu wake tena kuwa anatenda, sio kwa sababu kuwa wao ni wema, bali kwa sababu ya (1) uovu wa watu katika nchi (k.v. Mwa. 15:12-21; Law. 18:24-25; 20:13-14) na (2) ahadi Yake kwa wazee wa imani iliyoanzia katika Mwa. 12:1-3. Aliwataka wakumbuka kuwa Yeye yupo kamili kwenye utendaji kazi.

KITENZI cha awali“ukasema” (BDB 55, KB 65) ni *Qal* KAULI ISITIMILIFU, kikitumika katika maana ya KUSIHI. Roho ya mwanadamu aliyeanguka bado inaendelea kuwepo na kwa habari ya kiroho ni hatari.

KITENZI cha pili “kuwasukumia nje” (BDB 213, KB 239, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO) kinaonyesha uhusika wa kiutendaji wa YHWH kwenye ushindi (k.v. 6:19; Yosh. 23:5).

MADA MAALUM: MATENDO YA NEEMA YA YHWH KWA ISRAELI

Lazima ielezewa kwa uwazi kuwa safari ya kutoka Misri, kipindi cha kutangatanga jangwani, na ushindi yalikuwa ni matendo ya huruma ya YHWH (yaani., Mwa. 15:12-21), na sio zawadi za thamani kwa sababu ya matendo ya Israel:

1. Ulikuwa ni upendo wa YHWH kwa ajili ya "mababa" – Kumb. 4:37-38; 7:8; 10:15 (yaani., mababa wa imani)
2. Haikuwa ni idadi ya Waisraeli – Kumb. 7:7
3. Haikuwa nguvu wala uweza wa Israeli – Kumb. 8:17
4. Sio kwa haki yako ua unyofu wa moyo wako – Kumb. 9:5-6
5. YHWH anaendelea kuipenda Israeli hata katikati ya hukumu – Yer. 31:3

9:5 “Si kwa haki yako, wala kwa unyofu wa moyo wako” NOMINO hizi mbili zinfanana katika muktadha huu:

1. “haki” - BDB 842, kama vile 6:25; 9:4,5,6; 24:13; 33:21, tazama Mada Maalum katika 1:16
2. “unyofu” - BDB 449, ikimaanisha uaminifu au muundo wa maisha ya kiuadilifu, k.v. I Nya. 29:17; Zab. 119:7

Israeli sio kwamba inapewa nchi ya Kanaani kwa sababu ya uchaji wake wa Mungu, bali ni Wakanaani kutokuishi maisha ya Kimungu (k.v. mst. 4; Mwa. 15:12-21; Law. 18:24-28, tazama maelezo katika 3:6).

☐ **“tena apate kuliweka imara hilo neno Bwana alilowaapia baba zako Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo”** Tambua VITENZI:

1. “kuliweka imara” - BDB 877, KB 1086, *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO
2. “BWANA alilowaapia” - BDB 989, KB 1396, *Niphal* KAULI ILIYO TIMILIFU

MADA MAALUM: AGANO LILILOAHIDIWA KWA MABABA WA IMANI

Huu uhusiano wa ahadi maalumu ya agano la mwanzo ulifanyika kwa

1. Ibrahimu, Mwa. 12:1-3
 - a. Ardhi, Mwa. 12:7; 13:4-15; 15:18-21
 - b. Watu, Mwa. 13:16; 15:4-5; 17:2-6; 22:18
 - c. Baraka kwa ulimwengu, Mwa. 18:18; 22:18
2. Isaka, Mwa. 26:2-4
 - a. Ardhi
 - b. Watu
 - c. Kuubariki ulimwengu
3. Yakobo, Mwa. 28:2-4,13; 35:9-12; 48:3-4
 - a. Ardhi
 - b. Watu

Taifa la Israeli (nchi), Kut. 3:8,17; 6:8; 13:5; 33:1-3; Kumb. 1:7-8,35; 4:31; 9:3; 11:25; 31:7; Yosh. 1:6

☐ **“haki”** Tazama Mada Maalum katika 1:16.

9:6, 13 “u mwenye shingo ngumu” Mwanzoni kabisa hiki kilikuwa ni kifungu cha maneno kwa ajili ya mambo ya kilimo kikirejelea ng’ombe mkaidi. Kiuhalisia hili linamaanisha “ugumu wa shingo” au “shingo ngumu” (BDB 904 MUUNDO WA MANENO BDB 791, k.v. 6,7,13,24,27; 10:16; 31:27; Kut. 32:9; 33:3,5; 34:9).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 9:7-21

⁷Kumbuka, usisahau ulivyomtia Bwana, Mungu wako, kasirani jangwani; tangu siku uliyotoka nchi ya Misri hata mlipofika mahali hapa, mmekuwa na uasi juu ya Bwana ⁸Tena mlimkasirisha Bwana katika Horebu, Bwana akakasirika nanyi hata akataka kuwaangamiza. ⁹Na hapo nilipokwea mlimani kwenda kuzipokea

mbao za mawe, nazo ni mbao za agano Bwana alilofanya nanyi, ndipo nikakaa mle mlimani siku arobaini usiku na mchana; sikula chakula wala kunywa maji. ¹⁰Bwana akanipa zile mbao mbili za mawe zimeandikwa kwa kidole cha Mungu; na juu yake yameandikwa maneno mfano wa yote aliyosema nanyi Bwana mle mlimani toka kati ya moto siku ya mkutano. ¹¹Ikawa mwisho wa siku arobaini usiku na mchana, Bwana alinipa zile mbao mbili za mawe, nazo ni mbao za agano. ¹²Bwana akaniambia, Ondoka huko, shuka upesi; kwa kuwa watu wako uliowatoa Misri wamejiharibu; wamekengeuka mara katika njia niliyowaamuru; wamejifanyia sanamu ya kusubu. ¹³Tena Bwana akasema nami zaidi, akaniambia, Nimeliona taifa hili; na tazama, ni taifa lenye shingo ngumu; ¹⁴niache, nipate kuwaangamiza, na kulifuta jina lao chini ya mbingu; nami nitakufanya wewe uwe taifa kubwa lenye nguvu kuwapita wao. ¹⁵Basi nikageuka nikashuka mle mlimani, mlima ukawaka moto; na zile mbao mbili za agano zilikuwa katika mikono yangu miwili. ¹⁶Nikaangalia, na tazama, mlikuwa mmefanya dhambi juu ya Bwana, Mungu wenu; mmefanya ndama ya ng'ombe ya kusubu; mmekengeuka upesi katika njia aliyowaamuru Bwana. ¹⁷Nikazishika zile mbao mbili, nikazitupa kutoka katika mikono yangu miwili, nikazivunja mbele ya macho yenu. ¹⁸Nikaanguka nchi mbele za Bwana siku arobaini usiku na mchana, kama pale kwanza; sikula chakula wala kunywa maji; kwa sababu ya makosa yenu yote mliyokosa, kwa kufanya yaliyo maovu machoni pa Bwana, kwa kumkasirisha. ¹⁹Kwa kuwa niliogopa hasira na makamio aliyowakasirikia Bwana kutaka kuwaangamiza. Lakini Bwana alinisikiza wakati huo nao. ²⁰Bwana akamkasirikia sana Haruni akataka kumwangamiza; nikamwombea Haruni naye wakati huo. ²¹Kisha nikaitwaa ile dhambi yenu, huyo ndama mliyemfanya, nikamteketeka kwa moto, nikamponda, nikamsaga tikitiki, hata akawa laini kama vumbi; nikalitupa vumbi lake katika kijito kilichoshuka kutoka mlimani.

9:7 “Kumbuka, usisahau” VITENZI viwili vya mwanzo(BDB 269, KB 269, *Qal* KAULI SHURUTISHI, k.v. 5:15; 7:18[mara mbili]; 8:2; 9:7,27; 15:15; 16:3,12; 24:9,18,22; 25:17; 32:7 na BDB 1013, KB 1489, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, vikitenda kazi kama KITENZI AMRISHI, k.v. 4:9,23; 6:12; 8:11,14,19[mara mbili]; 9:7) ni kuisaidia Israeli kukumbuka (tazama maelezo katika 7:18) na kutokurudia kupungukiwa imani katika YHWH, ahadi zake na nguvu Zake kama walivyofanya mara kadhaa wakati wa kutoka Misri na kipindi cha kutangatanga jangwania. Musa aliyataja matendo yao ya kuabudu sanamu na uasi mwanzoni mwa Mlima Horebu katika mst. 8, ambapo Haruni alichonga sanamu ya ndama kwa madai ya watu!

9:7-8 “ ulivyomtia Bwana, Mungu wako, kasirani” Tazama Kutoka 16; 32; na Hesabu 13-14; 16:21,25 kama baadhi ya mifano.

9:7-22 Mistari hii inarejelea matendo ya Israeli wakati Musa alipokuwa katika Mlima Horebu/Sinai akipokea sheria (k.v. Kutoka 32).

9:9 “mbao za mawe, nazo ni mbao za agano Bwana alilofanya nanyi” Dhahiri kifungu cha maneno “mbao za mawe, na mbao za agano” vinafanana. Tazama Mada aalum: Agano katika 4:13. Haya yalikuwa ni maneno ya YHWH, na sio Musa'. Ufunuo huu, sio ugunduzi wala maoni yake.

9:9,11,18 “siku arobaini” Hesabu hii mara nyingi ni alama ya kipindi kirefu cha muda, kisichoelezeka, kirefu kuliko mzunguko wa mwezi (yaani., siku 28) lakini pungufu kuliko mabadiliko ya msimu. Muda wa kutoka Mlima Horebu/Sinai kuingia nchi ya Kanaani ulikuwa ni miaka therathini na nane.

9:9, 18 “Sikula chakula wala kunywa maji” Hili linarejelea kwenye siku 40 tofauti na za kufunga zikimaanisha huenda (1) kuilinda miujiza (k.v. Kut. 24:18; 34:28) au (2)nahau zenye kutiwa chumvi kwa ajili funga ya muda (hakuna chakula, lakini unakunywa maji).

9:10 “mbao mbili za mawe” Kwa sababu ya mikataba ya Wahiti huko Suzeraini kama muundo wa kihistoria uliofikiwa, hili laweza kurejelea kwenye nakala kamili mbili za sheria. Tazama kwenye sehemu ya utangulizi wa kitabu, VII.

☐“zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu” Hii ni nahau kwa ajili ya asili ya amri kumi za Mungu na maelezo yake (k.v. Kut. 31:18; 32:15-16; Kumb. 4:13). Tazama Mada Maalum: Mungu Kuelezewa kama Mwanadamu (Lugha za kibinadamu) katika 2:15.

☐“maneno mfano wa yote aliyosema nanyi Bwana mle mlimani toka kati ya moto siku ya mkutano” Hii ni dhamira yenye kujirudia (k.v. 4:12,15,33,36; 5:5,22,24,26; 9:10; 10:4). Kifungu kinasisitiza matendo ya Mungu na ufunuo binafsi wa agano lililomo katika Mlima Horebu/Sinai.

9:12-14 Kama Musa alivyoyashuhudia mazungumzo yake akiwa na Mungu katika Mlima Horebu/Sinai YHWH alitumia amri kadhaa:

1. “ondoka,” mst. 12 - BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. “shuka upesi,” mst. 12 - BDB 432, KB 434, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. “niache,” mst. 14 - BDB 951, KB 1276, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
4. “nipate kuwaangamiza,” mst. 14 - BDB 1029, KB 1552, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU ikitumika katika maana ya KUSIHI
5. “kulifuta jina lao,” mst. 14 - BDB 562, KB 567, *Qal* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU ikitumika katika maana ya KUSIHI

☐“kwa kuwa watu wako uliowatoa Misri” KITENZI hiki (BDB 422, KB 425, *Hiphil* KAULI YA WAKATI ULIOTIMILIFU) kinatumika na YHWH mara nyingi, lakini hapa kinatumiwa na Musa.

☐“wamejifanyia sanamu ya kusubu” Hii ilikuwa sio ibada ya sanamu, bali ni uwasilisho halisi wa YHWH. Huu ulikuwa uvunaji wa amri ya pili. Walitaka mungu wanayeweza kumwona na kumgusa kama ilivyokuwa kwa watu wa Misri na kule Kanaani waliyekuwa naye.

9:14 je huu ni mfano wa ghadhabu ya Mungu au ni jaribu juu ya uongozi wa Musa (k.v. mst. 25 na kuendelea, Kut. 32:30-35)?

☐“kulifuta jina lao chini ya mbingu ” Hii ni nahau ya Kiebrania (k.v. 25:5; Zab. 41:5) kwa ajili ya mauaji kamili ya Israel!

9:15 “mlima ukawaka moto ” Kuwaka kwa moto au mwanga mwangavu ilikuwa ni alama ya uwepo wa Mungu (k.v. 1:32-33; Isa. 66:15). Tazama Mada Maalum : Moto katika 4:11.

9:16 “mmefanya ndama ya ng'ombe ya kusubu ” KITENZI kile kile(BDB 793 I, KB 899, *Qal* KAULI YA WAKATITIMILIFU) kinatumika katika mistari ya 12 na 21. Hapa sanamu hii inaitwa (1)“ndama ya ng'ombe wa kusubu” (BDB 722, k.v. Kut. 32:4,8) (2) katika mst. 21, “ndama,” lakini (3) katika mst 12 “sanamu ya kusubu” (k.v. Kut. 34:17; Law. 19:4).

9:17 “nikazivunja mbele ya macho yenu ” Siku ile ile agano lilipoandikwa na Mungu lilivunjika (yote kwa pamoja kiuhalisia na kimethali).

9:19 “Bwana alinisikiza ” Tazama Kutoka 34. Tambua asili ya hofu ya Musa (BDB 388, KB 386, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. 28:60):

1. Hasira ya YHWH - BDB 60, k.v. Kut. 32:12
2. Hasira kali ya YHWH - BDB 404, k.v. 29:23
3. Ghadhabu ya YHWH - BDB 893, KB 1124, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. 1:34; Law. 10:6; Hes. 16:22
4. Ili niwaangamize ninyi - BDB 1029, KB 1552, *Hiphil* KITENZI CHA MUUNDO WA MANENO, k.v. 6:15; 9:20

Namba 1 na 2 zaweza kutenda kama wazo moja lenye kuunganishwa na maneno mawili (k.v. TEV, NET Bible).

9:20 “Haruni” Musa wakati akimwomba Haruni haikuandikwa katika kitabu cha Kutoka 32.

9:21 Tazama Kutoka 32:20. Tazama VITENZI vingapi vimetumika kuelezea kile Musa alikifanya kwenye sanamu ya ndama, dhambi mbaya:

1. “nikamteketeza kwa moto,” BDB 926, KB 1358, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU
2. “nikamponda,” BDB 510, KB 507, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, k.v. II Fal. 18:4; Mika 1:7
3. “nikamsaga tikitiki,” BDB 377, KB 374, *Qal* KITENZIJINA HALISI
4. “akawa laini kama mavumbi,” BDB 200, KB 229, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
5. “nikalitupa vumbi lake katika kijito,” BDB 1020, KB 1527, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 9:22-24

²²Tena huko Tabera, na Masa, na Kibroth-hataava mlimtia Bwana hasira. ²³Na wakati alipowatuma Bwana kutoka Kadesh-barnea, akiwaambia, Kweeni mkaimiliki nchi niliyowapa; ndipo mkaasi juu ya maagizo ya Bwana, Mungu wenu, hamkumsadiki wala hamkusikiza sauti yake. ²⁴Mmekuwa na uasi juu ya Bwana tokea siku nilipowajua ninyi.

9:22 “Tabera” Jina la sehemu hii linatokana na mchezo wa maneno wa KITENZI “teketeza kwa moto” (BDB 129). Hili lilikuwa ni eneo la kijiografia mahali ambapo YHWH aliyajibu malalamiko yao kwa hukumu ya moto (k.v. Hes. 11:1-3,34-35). Ilikuwa yapata safari ya siku tatu kaskazini mwa Mlima Horebu/Sinai.

☐ **“Masa”** Hii ilikuwa ni sehemu nyingine iliyokuwa na mgogoro kati ya YHWH na Israeli kipindi cha kutoka Misri (k.v. Kut. 17:7). Mara nyingi inahusishwa na Meriba (k.v. Kumb. 33:8), lakini sio kila mara (k.v. 6:16; 9:2). Yote kwa pamoja yanamaanisha “jaribu (BDB 650 III, k.v. 6:16; 9:22; 33:8; Kut. 17:7; Mit. 95:8) na migongano.”

☐ **“Kibroth - Hattaava”** Jina linamaanisha “walipozikwa watu waliotamani” (BDB 869, k.v. Hes. 11:31-35). Katika kitabu cha Hesabu 11 hakuna safari yeyote ya kusonga mbele iliyoenezwa kati ya Tabera na Kibroth-Hattaava, lakini hapa katika Kumbukumbu la Torati maeneo yote mawili yanaonekana kuwa mbali na mwenzake.

9:23 “Kweeni mkaimiliki nchi niliyowapa” Hizi zote ni *Qal* KAULI SHURUTISHI na zinadhihirisha maneno ya moja kwa moja ya Musa kwa Israel:

1. “kweeni” - BDB 748, KB 828
2. “mkaimiliki” - BDB 439, KB 441

Tazama tena amri ya YHWH kwa ajili ya Israeli kutenda sawa sawa juu ya kuamini kwao katika ukuu na ahadi Zake. Lakini badala ya imani Israeli wakaonyesha kutokuamini:

1. “wakaasi kinyume cha neno lake” - BDB 598, KB 632, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, k.v. Hes. 20:24; 27:14; Kumb. 1:26,43; 9:23; Zab. 107:11
2. “hamkuamini katika Yeye” - BDB 52, KB 63, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (Tazama Mada Maalum katika 1:32)
3. “wala kusikiliza sauti Yake” - BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (hizi *Qal* KAULI ZA WAKATI TIMILIFU). Hakika hii ni kinyume cha utii wa agano na uajibikaji.

☐ **“ndipo mkaasi”** Tazama maelezo katika 1:26

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 9:25-29

²⁵Ndipo nikaanguka nchi mbele za Bwana siku zile arobaini usiku na mchana nilizokuwa nimeanguka nchi; kwa kuwa Bwana alisema atawaangamiza. ²⁶Nikamwomba Bwana, nikasema, Ee Bwana Mungu, usiwaangamize watu wako, urithi wako, uliowakomboa kwa ukuu wako, uliowatoa Misri kwa mkono wa nguvu. ²⁷Wakumbuke watumwa wako, Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo; usiangalie upotofu wa watu hawa,

wala uovu wao, wala dhambi yao; ²⁸ isije nchi uliyotutoa ikasema, Ni kwa sababu Bwana hakuweza kuwaleta katika nchi aliyowapa ahadi, tena ni kwa kuwa aliwachukia, alivyowatoa nje ili kuwaua jangwani. ²⁹ Nao ni watu wako, urithi wako, uliowatoa kwa nguvu zako kuu na mkono wako ulionyoka.

9:25 Maombi ya kusihhi ya Musa yanatumia VITENZI viwili:

1. “nikaanguka chini” - BDB 656, KB 709
 - a. *Hithpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, mst. 25
 - b. *Hithpael* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, mst. 25
2. “nikamwomba” - mst. 26 - BDB 813, KB 933, *Hithpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

9:26-29 Mistari ya 26-29 inaonyesha sababu tatu Musa alizompa Mungu ili kupata majibu ya swali lake, ni kwa nini aihurumie Israel?”:

1. Ahadi yake kwa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo (k.v. Kut. 32:13)
2. Kanaani kuelewa visivyo tabia ya YHWH
3. Kanaani hawataelewa hukumu ya YHWH juu ya Israeli

Aya inajumuisha VITENZI vitatu vya hoja za maombi:

1. “usiwaangamize,” mst. 26 - BDB 1007, KB 1469, *Hiphil* KITENZI AMRISHI
2. “kumbuka,” mst. 27 - BDB 269, KB 269, *Qal* KITENZI SHURUTISHI
3. “usiangalie” (yaani, “geuka”), mst. 27 - BDB 815, KB 937, *Qal* HALI YA KUSIHI

Musa anamsihi YHWH na mpango wake wa ukombozi wa milele kwa ajili ya watu wote kama msingi wa kutokuangamiza watu wake wa agano waliokaidi. Zaidi ni katika ahadi kuliko kikundi cha watu! Tazama Mada Maalum: Mapendeleo ya Bob ya Kiinjilisti katika 4:6.

9:26 Tazama namna ombi la Musa linavyomkumbusha YHWH juu ya uhusiano wake wa agano:

1. “Bwana Mungu” (kiuhalisia, “*adon* YHWH,” k.v. 3:24. Tazama Mada Maalum katika 1:3.
2. “watu wako” – jina la agano, k.v. mst. 29
3. “urithi wako” – zawadi ya agano, k.v. mst. 29
4. “uliwakomboa - BDB 804, KB 911, *Qal* KAULI YA WAKATI ULITIMILIFU, tendo la neema la agano (tazama Mada Maalum: Fidia/Komboza katika 7:8). YHWH aliwaokoa toka utumwani hadi kuishi kifamilia (k.v. 7:8; 9:26; 13:5)
5. “uliwaokoa toka Misri” - BDB 422, KB 425, *Hiphil* KAULI YA WAKATI ULITIMILIFU, ahadi ya agano kwa Ibrahim (k.v. mst. 29; Mwa. 15:16-21)

Mungu anatenda kutokana na Yeye alivyo! Anafuata mpango wake wa ukombozi! Tumaini kubwa la wanadamu wote ni tabia ya YHWH isiobadilika, ya rehema, neema, na upendo (mf., Kut. 34:6; Mal. 3:6). Tazama maelezo katika 4:31 na 10:17.

☐“**kwa mkono wa nguvu**” Kifungu cha maneno “kwa mkono wa nguvu” katika mst 29 kwa pamoja kimepatikana katika maandiko ya Kimisri kikimrejelea mfalme wa Misri. Musa alivichagua vifungu vya maneno ambavyo Israeli ilikwisha kuvisikia kabla vikihusiana na Farao. YHWH alikuwa mfalme wao wa kweli!

9:27 Tazama tabia ya Israeli:

1. “upotovu wao” - BDB 904, k.v. mistari ya. 6,7,13,24,27
2. “uovu wao” - BDB 957, k.v. Yer. 14:20; Ezek. 3:19; 33:12
3. “dhambi zao” - BDB 308, k.v. Kut. 32:30; Kumb. 9:18; Zab. 32:5; 51:5; Mith. 5:22; 13:6; 14:34; 21:4; 24:9
4. (Kumbukumbu la Torati linachangiana matumizi ya msamiati)

9:28 “**isije nchi uliyotutoa ikasema**” Mungu, kwa sababu ya sifa zako njema na kusudio la ukombozi kwa ulimwengu wote, irehemu Israeli. Kifungu kingine kilichotumika kwa maana ile ile ni, “kwa ajili ya jina la Mungu” (k.v. Isa. 48:9-11; Ezek. 20:9,14,22,44; 36:21-23; Dan. 9:17-19).

9:29 “**kwa nguvu zako kuu na mkono wako ulionyoka**” Tazama maelezo kamili katika 4:34.

MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozowa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mungu aliichagua Israel?
2. Je! mst. wa 14 unaaksi asili ya kweli ya Mungu? Kama sivyo, asili yake ni ipi?
3. Orodhesha na kujadili sababu tatu Musa alizotoa kwa YHWH ili asiingamize Israeli.

KUMBUKUMBU LA TORATI 10

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Jozi ya pili ya mbao	Jaribu la kujihesabia haki	Musa anapokea Amri tena	Sanduku la Agano:chaguo La Lawi
	(9:1-10:11)		
10:1-5	10:1-5	10:1-5	10:1-5
10:6-11	10:6-9	10:6-9	10:6-9
	10:10-11	10:10-11	10:10-11
Umaana wa Sheria	Bwana akitakacho	Mungu anachohitaji	Tohara ya Moyo
	(10:12-11:32)		
10:12-22	10:12-22	10:12-22	12:12-13 10:14-22

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi) **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiyaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 10:1-5

¹ Wakati ule Bwana akaniambia, Chonga mbao mbili za mawe mfano wa zile za kwanza, kisha uje kwangu huku mlimani, ukajifanyie na sanduku la mti. ²Nami nitaandika juu ya hizo mbao maneno hayo yaliyokuwa juu ya mbao za kwanza, ulizozivunja, nawe uzitie ndani ya hilo sanduku. ³Basi nikafanya sanduku la mti wa mshita, nikachonga mbao mbili za mawe mfano wa zile za kwanza, nikakwea mle mlimani, na zile mbao mbili mkononi mwangu. ⁴Naye akaandika juu ya mbao mfano wa maandiko ya kwanza, zile amri kumi, alizowaambia Bwana huko mlimani toka kati ya moto siku ya mkutano; Bwana akanipa. ⁵Basi nikageuka nikashuka kutoka mlimani, nikazitia mbao ndani ya sanduku nililofanya; nazo zimo humo kama alivyoniama Bwana.

10:1 “mlimani” Hii inarejerea kwa Mlima Horebu/Mlima Sinai. Angalia Mada maalum katika 1:2.

☐ Musa anatakiwa kuandaa kwa ajili ya kukutana kwake tena na YHWH:

1. “kata kwa ajili yako mbao mbili za mawe” - BDB 820, KB 949, *Qal* KAULI SHURUTISHI, kama vile kut. 34:1,4
2. “Unijie” - BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. “ufanye sanduku” - BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kut. 25:10

Mikataba ya Wahiti pia ilitakikana iwe na nakala mbili za makubaliano. Moja alipewa mfalme mdogo kusoma kila mwaka na nyingine ilibandikwa katika hekulu la mungu wa mfalme mwenye nguvu. Tazama utangulizi wa kitabu,VII.

☐“**sanduku la mti**”Kutoka 37:1 inasema Bezalel alitengeneza sanduku la agano. Rashi anasema maelezo ya sanduku hayakutolewa mpaka Musa aliposhuka chini mara ya pili kutoka Mlima Sinai. Hivyo Musa lazima alikuwa ametengeneza sanduku la mpito kwanza na baadaye Bezaleli akatengeneza lingine zuri zaidi (kama vile Kut. 25:10-22). Hili sanduku la kwanza lililotengenezwa haraka haraka na Musa lilibeba Amri Kumi tu (kama vile I Wafalme 8:9). Sanduku lililokuja kutengenezwa baadaye lilikuwa na: Amri Kumi, mfano wa mana na fimbo ya Haruni. Kwa mjadala mzuri tazama Roland de Vaux, *Ancient Israel*, juzuu 2, kur. 292-303.

10:2 “Nami nitaandika”YHWH aliandika sheria, mstari wa 4 na Kut. 34:1. Hata hivyo Kut. 34:27 inazungumzia maandiko ya Musa. Yawezekana Mungu aliandika Amri Kumi lakini Musa aliandika maelezo na matamko ambayo yanaelezea na kufanyiwa kazi. Haikuwa akili na ufahamu wa Musa wala mazingira yake ya kidesturi bali Mungu Mwenyewe ndiye aliyeanzisha sheria. Mungu alitumia mifano ya kidesturi na miundo ambayo Musa angeweza kuifahamu kirahisi. Kwa namna nyingi muundo wa sheria ni sawasawa na sheria ya kibabeli lakini maudhui ni tofauti.

☐“**hilo sanduku**”Kuwekwa huku kwa nyaraka maalum mbele ya Mungu ni tabia ya Mashariki ya Karibu. Linganisha *Egyptian Book of the Dead*(katika sanduku chini ya miguu ya Thot) na Mikataba ya Wahiti ya Suzeria ya Milenia ya pili K.K.tazama utangulizi wa kitabu,VII.

10:3 “mti wa mshita”Huu ulikuwa mti wa mshita mgumu, wenye rangi ya udhurungi ya chungwa (BDB 1008) unaomea katika jangwa. Ulikuwa mti mdogo wa jangwani uliozoeleka (kama vile Isa. 41:19). Mti huu ulihusianishwa na aina zote za samani za hema la kukutanikia. Unatokea hapa tu nje ya kitabu cha Kutoka.

10:4 “Amri Kumi” Kiuhalisia hii ni “amri kumi” (BDB 796 MUUNDO WA MANENO BDB 182). Tabia hizi za msingi, sheria za kimsingi ni sawia na zenye kuelezewa katika kanuni za pamoja. Zinaweka msimamo wa kimamlaka wa mahusiano ya ukaribu na YHWH (kama vile mstari wa 20), zikifunua ibada na utii ambao unageuza na kukataa kutokuwa na mahusiano mengine yasiyofaa ya kiagano na kitu kingine (na pia kingine kisicho cha ushirika, kama vile 10:17-19). Ili kujua YHWH ndiye anayethiri maisha yote na vipaumbele vyake!

☐“**huko mlimani toka kati ya moto**”Hii inarejerea uwepo wa Mungu juu ya Mlima Horebu/Sinai, ulio andikwa katika Kut. 19:16-20. Uwepo wake una elezwa kama “moto ulao juu ya mlima” (kama vile Kut. 24:17). Kifungu hiki kinatumika mara kadhaa (kama vile 4:12,15,33,36; 5:4,24,26).

Moto (BDB 77) ilikuwa ishara ya wa uwepo wa utukufu wa YHWH:

1. mwanga katika Mwa. 15:17
2. kijiti kinachowaka bila kuteketea katika Kut. 3:2
3. moto juu ya mlima Horebu, Kut. 19:18; Kumb. 4:11,12,15,33,36
4. nguzo za moto ya *Shekinah* katika Kut. 13:21,22; 14:24; Hes. 9:15,16; 14:14; Zab. 78:14
5. makaa yamoto ya gari lafarasi libebalo kiti cha enzi cha YHWH katika maono ya Ezekiel katika Ezek. 1:13; 10:2

Amri Kumi zinarudiwa kusemwa kutoka katikati ya moto (kama vile 4:12,15,33; 5:4,22,24,26; 9:10; 10:4). Amri hizi zilikuwa ufunuo binafsi wa kiagano kutoka kwaYHWH, na sio akili za Musa.

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 10:6-9

⁶(Wana wa Israeli wakasafiri kutoka visima vya Bene-Yaakani kwenda Mosera; Haruni akafa huko, akazikwa huko; na Elezari mwanawe alitumika utumishi wa ukuhani badala yake. ⁷Wakasafiri kutoka huko kwenda Gudgoda; wakatoka Gudgoda wakaenda Yotbatha, nayo ni nchi ya vijito vya maji. ⁸Na wakati huo Bwana aliitenga kabila ya Lawi ili walichukue lile sanduku la agano la Bwana, wasimame mbele ya Bwana kwa kumtumikia, na kuwabarikia watu kwa jina lake, hata hivi leo. ⁹Ndipo asiwe na fungu Lawi, wala urithi

MADA MAALUM: NYONGEZA ZA BAADAYE KWENYE KUMBUKUMBU LA TORATI

Aya hii (10:6-9) inaonekana na wanazuoni wengi wa kisasa kuwa moja ya nyongeza kadhaa za baadaye za kiuhariri kwenye maandiko ya Musa. Ingawa haiwezi kuthibitishwa kwamba muhtasari huu hautoki katika kipindi cha Musa, ni wazi kwamba kulikuwa na maingizo kadhaa ya kiuhariri. Israeli ilikuwa Misri kwa karne na waandishi wa Kimisri walikuwa wamepeva mafunzo kuyaboresha maandiko wakati wanapopenda. Kwa wale wengio wetu ambao tunaamini katika uvuvio na ulinzi wa ufunuo wa kiungu tunaweza msisitizo katika kuongozwa na Roho katika nyongeza zote zinazosadikiwa zinahusiana na Agano la Kale. Hayaathiri mafundisho makuu au kuleta wasiwasi katika historia ya maandiko yanayozunguka. Lazima ichukuliwe na watu wa kisasa kwamba hatujui bado:

1. muda
2. mwandishi
3. mbinu ya ukusanyaji na upangaji wa Agano la Kale katika hatua zake za mwanzoni. Tunaamini kwa kukubali MT kama maneno yanayohifadhi ya Mungu!

Nadharia mpya kwa baadhi ya nyongeza za kiuhariri zimependekezwa na R. H. Polzin, *“Deuteronomy” in The Literary Guide to the Bible*. Kinapendekeza maoni ya nyongeza kuwa yanatoka kwa msimulizi, sio mhariri. Anaonelea kwamba maoni haya ya msimuliaji yanaweza kuonekana katika 1:1-5; 2:10-12, 20-23; 3:9, 11, 13b-14; 4:4-5:1a; 10:6-7, 9; 27:1a, 9a, 11; 28:69; 29:1; 31:1, 7a, 9-10a, 14a, 14c-16a, 22-23a, 24-25, 30; 32:44-45, 48; 33:1; 34:1-4a, 5-12. Polzin anaeleza kwamba huyu msimulizi anayeonekana anadaiwa kuwa na malaka ya kutegemewa kama Musa, ambaye anaandaa jukwaa kwa “Historia ya Kumbu kumbu la ki-torati” ya Yoshua - Wafalme. Nadharia hii inaeleza ufanano kati ya Vitabu vitano vya Musa na Manabii waliotangulia.

10:6 “Bene-Yaakani kwenda Mosera”Maneno mawili ya kwanza (BDB 91,122) yanafasiri kwa uhalisia, “visima vya wana wa Yaakani” (kama vile Hes. 33:31). Jina Mosera linamaanisha “kukemewa/kuadhibiwa” (BDB 64). Mosera (yawezekana ni jimbo), laweza kuwa jina sawa na Mlima Hori (kama vile Hes. 20:22-29; 33:38), ni eneo ambalo Haruni alifia. Haya Yote yanarejelea maeneo ya kijiografia ambapo Wana wa Israeli walitangatanga.

☐**“Haruni alifia pale”**Hesabu 20:27-28 inasema kwamba hili lilitokea katika mlima Hori. Haruni kama Musa hakuingia Nchi ya Ahadi kwa sababu ya kutokutii (kama vile Hes. 20:8,12).

☐**“Eliezari”**Jina lake linamaanisha “Mungu amesaidia” (BDB 46). Huya alikuwa mwana wa tatu wa Haruni (kama vile Kut. 6:23). Wana wawili wa kwanza waliuwawa kwasababu hawakuzitilia maanani sheria za Mungu (kama vile Law. 10:1-7; Hes. 3:4). Waalimu wa sheria za Kiyahudi wanasema kwamba kwasababu ya Law. 10:9 inakataza vileo kwa makuhani siku wanapokuwa katika zamu zao, Nadabu na Abihu walikuwa wamelewa. Ukuhani Mkuu ulitakiwa kutokea katika familia ya Haruni (kama vile Kut. 29:9; 40:15; Hes 3:5-10; 25:13).

10:7 “Gudgoda”Maana ya jina hili haina haijulikani (BDB 151). Hii inaonekana kutambuliwa na Horhaggidgad katika Hes. 32:32. Maeneo yote mawili yalikuwa ni mahali ambapo Israeli waliweka kambi katika safari yao juu ya mlima Horebu/Sinai kuelekea Kadesh-barnea. Toleo la JPSOA lina jina “Gudgod.”

☐**“Jotbatha”**Neno hili linamaanisha “ipendezayo” (BDB 406, yawezekana ni kwa sababu ya uwepo wa maji). Pia inatajwa kama sehemu ya kambi katika Hes. 33:33-34. Toleo la JPSOA lina neno “Jotbath.”

10:8 “BWANA akawatenga kabila la Lawi”KITENZI“akawatenga” (BDB 95, KB 110, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Hes. 8:14; 16:9; I Nyakati 23:13) kinamaanisha “kugawanya.” Hapa kutenga ni kwa ajili ya

- (1) huduma maalum za kiibada zinazohusiana na hema la kukutanikia na baadaye hekalu;
- (2) baraka za watu (kama vile 10:8; Law.9:22-23; Hes. 6:22-27);
- (3) kuhukumu kesi na migogoro ya watu (kama vile 21:5); na

(4) kuhukumu vitu najisi na visivyo najisi (kama vile Law. 10:10). KITENZI hiki ni sawa na “chagua” (BDB 103, KB 119, kama vile 18:5; 21:5).

Israeli lilitakiwa kujitenga na mataifa mengine (kama vile Law. 20:24-26; I Wafalme 8:53; yaani, “taifa takatifu,” kama vile Kut. 19:6), Hivyo kabila la Lawi lilitakiwa kutegwa na makabila mengine kama watumishi wa kiibada wa YHWH. Hawa walichaguliwa kwasababu

(1) Lawi lilikuwa ndilo kabila ambamo Musa na Haruni wametokea;

(2) Walawi walichukua nafasi ya “mzaliwa wa kwanza” kwa Waebrania (kama vile Kut.13; Hes. 3:12; 8:14-19); au

(3) Kwa uaminifu Lawi iliitikia wito wa Musa wa kuiadhibu Israeli (kama vile Kut. 32:25-29). Katika Mwa. 29:34, Lea anamwita mwanawe wa tatu Lawi kwasababu mume wake hakumpenda, japo jina la mtoto lilimaanisha, “Yakobo ameungamanishwa (au kuungana) kwangu” (BDB 532).

Kama kabila la kikuhani, wangepanya haya

(1) kubeba sanduku la agano

(2) kusimama mbele za Bwana ili kumtumikia (yaani, majukumu yote katika hema ya kukutanika na baadaye hekalunihuko Yerusalemu, kama vile 18:5; Hes. 18:1-7

(3) kubariki katika jina Lake (mfano, Hes. 6:24-27)

Baadaye kungekuwepo majukumu ambayo yangekabidhiwa kwa baadhi ya familia za Lawi kufanyika kuwa makuhani na wengine kufanyika kama Walawi. Hata hivyo katika Kumbukumbu la Torati Walawi wote wanaweza kutenda kama makuhani (linganisha 31:9 na 25). Tazama Roland deVaux, *Ancient Israel*, juzuu 2, kur. 358-371.

10:9 “Lawi hana seemu au urithi” Ingawa kabila la Lawi halikuwa limepewa sehemu yoyote ya ardhi, sehemu ya miji arobaini na nane iligawiwa kwao pamoja na maeneo ya kulishia wanyama iliyowazunguka (kama vile Hes. 35:1-8; Yosh. 21).

☐ **“BWANA ndiyo urithi wake”** Hii iliashiria mahali pake maalumu pa huduma (kama vile Hes. 18:20; Kumb. 10:9; 18:1,2; Yosh. 13:33; Ezek. 44:28)! Ahadi hii ya kupendeza kwa kabila la Lawi ilifanyika kilio kutoka ndani ya moyo wa kila mwamini wa kweli (kama vile Zab. 16:5; 73:23-28; 119:57; 142:5; Maombolezo 3:24).

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 10:10-11

¹⁰Nikakaa mle mlimani kama hapo kwanza, siku arobaini usiku na mchana; Bwana akanisikiza wakati huo nao; asitake Bwana kukuangamiza. ¹¹Bwana akaniambia, Ondoka, ushike safari yako mbele ya watu; nao wataingia waimiliki nchi, niliyowaapia baba zao ya kuwa nitawapa.

10:10 “hapo kwanza, siku arobaini usiku” Tazama Kut. 34:28; Kumb. 9:18.

☐ **“asitake Bwana kukuangamiza”** Hii ilikuwa ni huduma ya kimaombi ya Musa (kama vile 9:25-29; Kut.32:9-14).

10:11 YHWH aliamuru Israeli kutenda kile ambacho alikuwa amekiahidi tayari—kutawala Nchi ya Ahadi:

1. “inuka” - BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI SHURUTISHI YENYE HALI YA UMOJA, kama vile 2:13,24, ambayo ni HALI YA WINGI na inarejerea kwa Israeli. Hapa HALI YA UMOJA unarejerea kwa Musa.
2. “endelea” - BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI SHURUTISHI YENYE HALI YA UMOJA, kiuhalisia inamaanisha “kuvunja kambi na kuanza hatua ya pili ya safari” (kama vile Kut. 17:1; 40:36,38; Hes. 10:2,12; 33:1,2). Musa alitakiwa kuongoza watu mbele.
3. “waingie” - BDB 97, KB 112, *Qal* KAULI SHURUTISHI YENYE HALI YA WINGI, ambayo inaweza kufanya kazi kama HALI YA KUSIHI.
4. “na kumiliki ardhi” - BDB 439, KB 441, *Qal* KAULI SHURUTISHI YENYE HALI YA WINGI, ambayo inaweza kufanya kazi kama HALI YA KUSIHI ambapo Israeli inaitwa kutimiza kiapo cha YHWH kwa Mababa wa Imani (kama vile 1:8; Yosh. 21:43). Mungu anamtumia mwanadamu kama chombo (mfano, Kut. 3:7-12)! Ni nguvu Zake na makusudi lakini watu wake lazima watende kazi katika imani na kutumaini!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 10:12-22

¹²Na sasa, Israeli, Bwana, Mungu wako, anataka nini kwako, ila umche Bwana, Mungu wako, na kwenda katika njia zake zote, na kumpenda, na kumtumikia Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote; ¹³kuzishika amri za Bwana na sheria zake, ninazokuamuru leo, upate uheri? ¹⁴Tazama, mbingu ni mali za Bwana, Mungu wako, na mbingu za mbingu, na nchi, na vitu vyote vilivyomo. ¹⁵Tena, Bwana aliwafurahia baba zako, na kuwapenda, akawachagua wazao wao baada yao, naam, na ninyi zaidi ya mataifa yote kama hivi leo. ¹⁶Basi, zitahirini govi za mioyo yenu, wala msiwe na shingo ngumu. ¹⁷Kwa maana Bwana, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa mabwana, Mungu mkuu, mwenye kuogofya, asiyependelea nyuso za watu, wala hakubali rushwa. ¹⁸Huwafanyia yatima na mjane hukumu ya haki, naye humpenda mgeni, akimpa chakula na mavazi. ¹⁹Basi, mpendeni mgeni, kwa sababu ninyi wenyewe mlikuwa wageni katika nchi ya Misri. ²⁰Mche Bwana, Mungu wako, umtumikie yeye; ambatana naye, na kuapa kwa jina lake. ²¹Yeye ndiye fahari yako, na yeye ndiye Mungu wako, aliyekutendea mambo haya makubwa, ya kutisha, uliyoyaona kwa macho yako. ²²Baba zako walishukia Misri na watu sabini; na sasa Bwana, Mungu wako, amekufanya kama nyota za mbinguni kwa wingi.

10:12-13 Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: MAHITAJI YA AGANO LA YHWH KWA ISRAELI

Mahitaji ya YHWH (BDB 981, KB 1371, *Qal* KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPO ENDELEVU) yanawekwa wazi katika mfululizo wa *Qal* KITENZIJINA HALISI:

1. "kumcha BWANA" - BDB 431, KB 432, kama vile 4:29; 10:20
2. "kutembea katika njia zake zote" - BDB 229, KB 246, k.v. 4:29
3. "kumpenda" - BDB 12, KB 17, kama vile 6:5; 10:15; atazama maelezo kamili katika 5:10
4. "kumtumikia BWANA Mungu wako kwa moyo wako wote na roho yako yote" - BDB 712, KB 773, kama vile 4:29; 6:5; 10:12; 11:13; 13:3; 26:16; 30:2,6,10
5. "kutunza amri za BWANA na sheria Zake" - BDB 1036, KB 1581

Kifungu hiki ni sawasawa na Mika 6:6-8. Vyote vinazungumzia ju ya imani inayogusa maisha ya kila siku!

10:13 "kwa ajili yenu" Utii unaleta Baraka; kutotii kunaleta hukumu (kama vile sura za 27-29).

10:14 Mstari huu unamaanisha imani ya Mungu mmoja. Hii inayarejelea mazingira ya sayari hii, ulimwengu wote (anga la juu la nyota), na enzi ya Mungu (yaani, mbingu tatu).

10:15 Tazama njia zinazofanana za kuelezea uchaguzi wa YHWH kwa Israeli kama watu wake maalum (yaani "hata muwe juu ya watu wote," kama vile Kut. 19:5-6; Kumb. 7:6; 14:2):

1. "kuweka upendo Wake" - BDB 365 I, KB 362, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile 7:7. Katika 4:37 neno lingine kwa upendo (BDB 12, KB 17) linatumika.
2. "Alichagua wazao wao" - BDB 103, KB 119, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 4:37.

☐ "kama ilivyo leo hii" Tazama maelezo katika 3:14.

10:16 Israeli ilitakiwa kuitikia uchaguzi huu wa YHWH kwa:

1. "kuifanyia tohara mioyo yao" - BDB 557, KB 555, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU. Hii ni stiari ya kuwa tayari kwa ajili ya Mungu (kama vile Law. 26:41; Kumb. 10:16; 30:6; Yer. 4:4; 9:25-26). Inaelezewa kwa njia kadhaa:
 - a. fanyeni tohara ya miili yenu - Mwa. 17:14 (ishara ya agano)
 - b. fanyeni tohara ya midomo - nahau katika Kut. 6:12,30
 - c. fanyeni tohara ya masikio yenu - Yer. 6:10
 - d. Inahusiana na moyo wa kweli, sio tu tohara ya mwili - 30:6; Yer. 4:4; 9:25-26; Ezek. 44:9; Rum. 2:28-29
2. "kutokuzifanya shingo zao kuwa ngumu" - BDB 904, KB 1151, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 9:6,7,13,24,27; 31:27. Angalia dokezo katika 2:30.

10:17Tazama sifa zinazotumika kumuelezea YHWH:

1. Mungu wa miungu - BDB 43, kama vile Zab. 136:2
2. Bwana wa mabwana - BDB 10, kama vile Zab. 136:3
3. Mungu Mkuu - BDB 152, kama vile 3:24; 5:24; 9:26; 11:2; 32:3; Neh. 1:5; 9:32
4. Mungu mwenye nguvu - BDB 150, kama vile Neh. 9:32; Zab. 24:8; Isa. 10:21
5. Mungu wa kushangaza - BDB 431, KB 432, *Niphal* KAULI YA WAKATI ULIOPO ENDELEVU, kama vile 7:21; Neh. 1:5; 9:32

☐“**asiye na upendeleo**”Kifungu cha kiebrania kinamaanisha “asiyechagua kwa sura” (BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU pamoja naBDB 815). Hili mara nyingi linatumika kwa waamuzi (kama vile 1:17; 16:19; 24:17; Law. 19:15). Hililinaamaanisha kwamba Mungu ni Mungu wa hukumu ya haki (kama vile Kumb. 10:17; II Nyakati. 19:7).

☐“**hachukui rushwa**”Tabia ya YHWH inaelezewa kwa maneno ya sheria za kibinadamu (kama vile mistari ya 18-19). Hii mara nyingi inahusianishwa na kifungu hapo juu.

10:18-19Tazama namna tabia za kisheria za Mungu zilivyo katika mistari wa 18 zivyofafanuliwa katika matendo:

1. “Anahukumu (BDB 793 I, KB 889, *Qal*/ENDELEVU) kwa haki kwa ajili ya”:
 - a. yatima
 - b. wajane (kama vile 24:17; 26:12-13; 27:19; Zab. 68:4-5)
2. “huonesha upendo wake (BDB 12, KB 17, *Qal*/YA WAKATI ULIOPO ENDELEVU) kwa wageni kwa kuwapa” (BDB 678, KB 733, *Qal*/KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO):
 - a. chakula
 - b. mavazi

Wana wa Israeli wanatakiwa kufanya vitu hivi kwa sababu mbili

1. Itaifunua tabia ya Mungu (mistari wa 17; Isa. 58:6-7,10).
2. Wanajua namna wanavyojisikia pale wanapotendewa vibaya (mistari wa 19; 24:18,22; Kut. 22:21; 23:9).

Kut. 22:22-23 pia inataja kwamba Mungu atasikia maombi ya watu hawa ambao kijamii hawana nguvu na atawatendea kwa niaba yao (kama vile Zab. 146:9; Mal. 3:5; kama apendavyo Masihi, kama vile Isa. 11:4).

10:20Kwa namna vigezo vilivyowekwa na Mungu katika mistari ya 12-13 kwa VITENZIJINA VYA MUUNDO WA MANENO kadhaa, hapa vinawekwa kwetu tena*Qal* VITENZI VYA WAKATI USIO TIMILIFU:

1. “kumcha BWANA” - BDB 431, KB 432, kama vile 5:29; 6:13; 13:4
2. “mtumikie” - BDB 712, KB 773, kama vile 13:4
3. “shikamaneni naye” - BDB 179, KB 209, kama vile 11:22; 13:4
4. “apa kwa jina Lake” - BDB 989, KB 1396, kama vile 5:11; 6:13. Tazamamaelezo kamili katika 5:11.

Vyote hivi vinahusiana na nia sahihi na matendo ya ibada.

10:21 “Yeye ni sifa yako”Lugha ya Kumbukumbu la Torati inaufanano sana na Fasihi ya Hekima. Kifungu hiki kinaonekana katika Zab. 109:1.Hakuna KITENZI kilicho na kifungu hiki au kinachofuata. Ni ukiri wa nguvu ambao unasifu matendo ya YHWH ya ukombozi wakati wa safari ya kutoka Misri na kutanga tanga jangwani:

1. sifa yao (BDB 239)
2. *Elohim* wao (BDB 43)

☐“**aliyefanya haya na vitu vingi vya kushangaza ambavyo mmeviona**”Hii inarejerea kwa matendo ya YHWH na utoshelevu wakati wa safari ya kutoka Misri, kipindi cha kutanga tanga jangwani (kama vile 11:2), na hayo ambayo yatajirudia wakati wa mapambano!

10:22 “watu sabini katika wote”Sabini ni hesabu inayojirudia iliyotumika kwa ajili ya watu. Tazama 46:27; Kut. 1:5. Andiko moja la Kut. 1:5, lililopatikana katika maeneo ya elimukale Qumran (yaani magombo ya Bahari ya

Chumvi) lina idadi ya 75, ambalo linafanana na Mdo. 7:14-15. Kwa mjadala mzuri wa idadi tofauti tofauti, tazama *Hard Sayings of the Bible*, uk. 521 au Gleason L. Archer, *Encyclopedia of Bible Difficulties*, uk. 378-379.

☛“kama nyota za mbinguni”Huu ni utimilifu wa ahadi za Mungu. Tazamamaelezo kamili katika 1:10.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini kusudi la sheria ya Mungu (kwa maana ya Agano la Kale)?
2. Je! sura hii inaifunua imani katika Mungu mmoja? Wapi na kwa namna gani?
3. Kwa namna gani kitabu cha KumbuKumbu la Torati kinaelezea upendo wa Mungu kwa mwanadamu?

KUMBUKUMBU LA TORATI 11

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Upendo na Utii Vinapewa taji	Anachokihitaji Bwana (10:12-11:32)	Ukuu wa Bwana	Matendo ya Israeli yaliyopita
11:1-7	11:1-7	11:1-7	11:1-7
		Baraka za Nchi ya Ahadi	Ahadi na Maonyo
11:8-12	11:8-12	11:8-12	12:8-9 11:10-17
11:13-17	11:13-17	11:13-17	Hitimisho
11:18-21	11:18-21	11:18-21	11:18-21
11:22-25	11:22-25	11:22-25	11:22-25
11:26-32	11:26-28 11:29-30 11:31-32	11:26-32	11:26-32

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi’') *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (mzunguko #3, uk viii) Linganisha mgawanyo wa somo lako na tafsiri nne hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 11:1-7

¹Kwa ajili hii mpende Bwana, Mungu wako, na kushika sikuzote mausia yake, na amri zake, na hukumu zake, na maagizo yake. ²Nanyi leo jueni; kwa kuwa sisemi sasa na vijana vyenu, ambao hawakujua, wala hawakuona adhabu ya Bwana, Mungu wenu, ukuu wake, na mkono wake wa nguvu, na mkono wake

ulionyoka, ³ na ishara zake, na kazi zake alizomfanya Farao mfalme wa Misri, na nchi yake yote, katikati ya Misri; ⁴ na alivyolifanya jeshi la Misri, farasi zao, na magari yao; na aliyowafunikiza maji ya Bahari ya Shamu walipokuwa wakiwaandamia, na aliyowaangamiza Bwana hata hivi leo; ⁵ na mambo aliyowafanyia ninyi barani, hata mkaja mahali hapa; ⁶ na aliyowafanya Dathani, na Abiramu, wana wa Eliabu mwana wa Reubeni; nchi ilivyofunua kinywa chake, ikawameza, na walio nyumbani mwao, na mahema yao, na kila kitu kilichokuwa hai kikiwafuata, katikati ya Israeli yote; ⁷ lakini macho yenu yameiona kazi kubwa ya Bwana aliyoifanya, yote.

11:1 Tambua namna VITENZI viwili vya mstari huu vinavyohusiana. Kithiolojia hivi vinafanana. Lazima kimoja kilete matokeo ya kingine!

1. “mpendeBwana” - BDB 12, KB 17, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile mist. 13,22. Tazama maelezo kamili katika 5:10.

2. “sikuzote mausia yake” - BDB 1036, KB 1581, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

Huku ni kujirudia kwa 6:2,4-5; 10:12. Upendo ni vyote tendo (utii) na hisia (“kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa nguvu zako zote,” kama vile 13:3)

☐“mausia yake, na amri zake, na hukumu zake, na maagizo yake” Tazama Mada maalum katika 4:1.

11:2 “Nanyi leo jueni; kwa kuwa sisemi sasa na vijana vyenu, ambao hawakujua, wala hawakuona” Musa anajitokeza kwa wale waliokuwa shahidi wa macho (kama Walawi na watoto walio na umri wa chini kujiunga na jeshi, chini ya miaka 20, kama vile 1:6,9,14; 5:2,5; 11:2,7) wa matukio ya kutoka Misri na kipindi cha kutangatanga jangwani (kama vile 4:34; 7:19).

☐“jueni” Tazama maelezo kamili katika 4:35.

☐“adhabu ya Bwana” Adhabu ya Mungu(BDB 416) ni njema, mst. 3; na wakati mwingine ina madhara, mst. 6. Kumfundisha mtoto ndiyo tabia ya Mungu baba yetu (kama vile Heb. 12:5-13). Hili ni neno lingine la hekima linalotumika mara nyingi sana katika kitabu cha Mithali.

☐“ukuu wake” Tazama maelezo katika 10:17 na 4:31.

☐“na mkono wake wa nguvu, na mkono wake ulionyoka” Hiki ni kifungukinachotumika kumaanisha uweza wa Mungu (kama vile 4:34; 5:15; 6:21; 9:29). Tazama maelezo katika 4:34.

11:4 “Bahari ya Shamu walipokuwa wakiwaandamia” Hapa neno la Kiebrania ni “Bahari ya Shamu” (BDB 410 ya MUUNDO WA MANENO 693 I). Tazama Mada Maalum katika 1:40. Neno wakiwaandamia kifasihi ni “wakizamisha nyuso zao” (BDB 847, KB 1012, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kut. 14:23-31), ambayo ni nahau nyene kumaanisha kuzama chini.

11:5 Huu ni ukumbusho wa nuujiza wa Mungu wa utoaji wa mana kipindi cha kutangatanga jangwani. Tazama maelezo kamili katika 8:4.

11:6 “Dathani, na Abiramu” Tazama Hesabu 16:1-35; 26:9-10; Zab. 106:16-18.

☐“katikati ya Israeli” Tazama Mada Maalum katika 1:1.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 11:8-12

⁸Kwa hiyo yaangalieni maagizo yote niwaagizayo leo, mpate kuwa na nguvu, na kuingia mkaimiliki nchi mwivukiayo kuimiliki; ⁹ nanyi mpate kuzifanya siku zenu kuwa nyingi juu ya nchi Bwana aliyowaapia baba zenu, ya kuwa atawapa wao na kizazi chao, nchi imiminikayo maziwa na asali ¹⁰Kwa kuwa nchi mwingiayo kuimiliki, si mfano wa nchi ya Misri mlilotoka, uliyokuwa ukipanda mbegu zako humo na kuinywesheleza

kwa mguu wako, kama shamba la mboga; ¹¹lakini nchi mwivukiayo kuimiliki ni nchi ya vilima na mabonde, nayo hunyweshwa maji ya mvua ya mbinguni; ¹²nayo ni nchi itunzwayo na Bwana, Mungu wako; macho ya Bwana Mungu wako, ya juu yake, tangu mwanzo wa mwaka hata mwisho wa mwaka.

11:8 “Kwa hiyo” Aya hii inayarejelea madokezo yote ya kihistoria ya kipindi kilichopita yanayopatikana katika sura 11 au pengine kurejea nyuma. Mengi yaliyo ndani ya kitabu cha Kumbukumbu la Torati, hadi kufikia wakati huu, yamesimuliwa tena na tena kwa makaripio yale yale.

11:9 “nanyi mpate kuzifanya siku zenu kuwa nyingi juu ya nchi” Linganisha mst. 21 Kumb. 5:16. Hii si ahadi binafsi ya kudumu bali ni ahadi ya kitamaduni yenye uhimarifu wa jamii yenye kuiheshimu Sheria ya Mungu (kama vile 4:1; 8:1) na ambapo huiheshimu jamii (kama vile 4:40; 5:16,33; 6:2). Tazama maelezo kamili katika 4:40.

☐ **“Bwana aliyowaapia baba zenu, ya kuwa atawapa”** Tazama Mada Maalum: Ahadi za Agano kwa Mababa wa Imani katika 9:5.

☐ **“nchi imiminikayo maziwa na asali”** Haya si maelezo ya mwonekano wake bali ni wasifu wa kiufundi wenyekuonyesha namna ilivyo nchi ya Palestina iliyo katika Ugariti na kumbukumbu za ki-Misri. Tazama maelezo katika 6:3.

11:10 “si mfano wa nchi ya Misri” Ulimaji wa mazao ulikuwa tofauti sana humo Misri kuliko Palestina. Palestina ilikuwa na mvua za misimu (kama vile mst.11), Misri ilianzisha kilimo cha umwagiliaji toka Mto Nile na mafuriko yake ya kila mwaka.

☐ **“kuinyweshweleza kwa mguu wako”** Huenda kifungu hiki kinaurejelea (1) mfumo wa umwagiliaji ambapo shamba lilifurika na kisha mguu ulitumika kulikandamiza shimo kuelekea ndani ya mfereji ili kuyaruhusu maji kutoka nje au (2) kinu cha kuendesha kwa miguu kilitumika ili kuyaruhusu maji yatokeze kwa ajili ya umwagiliaji.

11:11 “nchi. . . hunyweshwa maji ya mvua ya mbinguni” Kwa watu wa jangwani hakuna baraka iliyo kuu kuliko maji ya kutosha, ya mara kwa mara (kama vile 8:7-9). Nchi hii nzuri inapatikana kwa sharti la utiii wa agano (kama vile mist. 16-17; Law. 26:14-20; Kumb. 28:12,23-24; I Fal. 8:35; 17:1; II Nya. 7:11-14; Isa. 5:6; Yer. 14; Amosi 4:7-8).

11:12 “macho ya Bwana” Hii ni sifa bainifu ya lugha ya kibinadamu ya Bwana ya mst. 2. Hii inaeleza juu ya kujali kwake kwa kipekee na kuwepo kwake katika Nchi ya Ahadi. Tazama Mada Maalum katika 2:15.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 11:13-17

¹³Tena itakuwa, mtakaposikiza kwa bidii maagizo yangu niwaagizayo leo, kwa kumpenda Bwana, Mungu wenu, na kumtumikia kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote, ¹⁴ndipo nitakapowapa mvua ya nchi yenu kwa wakati wake, mvua ya masika, na mvua ya vuli, upate kuvuna nafaka yako, na divai yako, na mafuta yako. ¹⁵Nami nitakupa nyasi katika mavue yako kulisha wanyama wako wa mifugo, nawe utakula na kushiba. ¹⁶Jitunzeni nafsi zenu, mioyo yenu isije ikadanganywa, mkageuka na kutumikia miungu mingine na kuiabudu; ¹⁷hasira za Bwana zikawaka juu yenu, naye akafunga mbingu kusiwe na mvua, wala nchi isitoe matunda yake; mkaangamia kwa upesi mtoke katika nchi nzuri awapayo Bwana.

11:13 Utambue ushurutishi (“mtakaposikiliza” BDB 49, kama vile mst. 22; na “kutii” BDB 1033, KB 1570, *Qal* ya KITENZIJINA HALISI na *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU kutokana na mzizi ule ule, wenye kuonyesha msistizo na kumaanisha “kusikia ili kutenda”) asili ya baraka za YHWH ni:

1. “kumpenda” - BDB 12, KB 17, *Qal* ya KITENZIJINA HALISI
2. “kumtumikia” - BDB 712, KB 773, *Qal* ya KITENZIJINA HALISI. Katika lgha ya Kiarabu asili hii inamaanisha kumwabudu na kumtii Mungu, kama vile Kut. 3:12; 4:3; 7:16; 8:1

3. “kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote,” kama vile 4:29; 6:5; na hasa 10:12. Musa anayarudia maombi haya ya kusihhi tena na tena kwa ajili yamsistizo.

☐“**mioyo**” Kwa Kiebrania cha kaleneno“mioyo” lilisimamia fikra na lengo, akili na nia ya mtu. Tazama Mada Maalum katika 2:30.

☐“**roho**” Neno hili linamaanisha“nguvu ya uhai iliyotolewa na Mungu” (BDB 659). Hili linaweza kuwarejelea wanadamu au wanyama walio katika kitabu cha Ufunuo.

11:14 “nitakapowapa mvua” Neno“nitakapowapa mvua” (BDB 678, KB 733) linaeleza juu ya baraka za agano la YHWH na laana:

1. mst. 9 – *Qal* ya KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO (baraka)
2. mst. 14 - *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU (baraka)
3. mst. 15 - *Qal* yaKAULI YA WAKATI TIMILIFU (baraka)
4. mst. 17 - *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (laana)
5. mst. 17 - *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU(laana)
6. mst. 21 - *Qal* yaKITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO (baraka)
7. mst. 25 - *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (baraka)
8. mst. 26 - *Qal* ya KAULI ENDELEVU (baraka/laana)
9. mst. 29 - *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU (baraka/laana)
10. mst. 31 - *Qal* ya KAULI ENDELEVU (baraka)
11. mst. 32 - *Qal* ya KAULI ENDELEVU (baraka/laana)

YHWH huwa na nia ya kubariki, lakini utii wa agano la Israeli ndiyo udhihirisho wa mwitikio wa namna gani (baraka au laana, kama vile sura 27-29) aliyoupokea.

Mungu amejitenga na asili yake lakini bado yuko katika udhibiti wake. Anautumia huu kujifunua kwa mwanadamu (kama vile Kumb. 27-28; Zab. 19:1-6; Rum. 1:19-25; 2:14-15).

☐“**wakati wake**” Eneo laPalestina lilikuwa na aina mbili za majira ya mvua kwa mwaka. Mvua za wakati (kwa ajili ya kupanda) zilizokuwa zikianza Mwezi wa Kumi – Mwezi wa Kumi na Moja (BDB 435, kama vile Yer. 5:24; Hos. 6:2; Yoeli 2:23).

☐“**mvua ya vuli**” Mvua za vuli (za kukuza mazao) zilizokuwa zikianza Mwezi wa Pili – Mwezi wa Nne (BDB 545, kama vile Yer. 3:3; Yoeli 2:23). Kwa wakati mwingine wingi wa umande ndiyo chanzo pekee cha unyevu. Hosea 6:3 inatumia stiari hii ya matengenezo mapya ya kiroho wakati wa mwisho.

☐“**nafaka yako, na divai yako, na mafuta yako**” Haya yalikuwa mazao makuu ya mlo wao (kama vile 7:13).

11:15 “wanyama wako wa mifugo” Hili neno“mifugo” (BDB 96) linarejelea:

1. viumbe hai vyote kuliko wanadamu, Mwa. 8:1; Kut. 9:9,10,22
2. wanyama wafugwao, Mwa. 47:17; Kut. 20:10; Law. 19:19; 26:22; Hes. 3:41,45; Kut. 2:35

☐“**nawe utakula na kushiba**” KITENZI hiki ni ahadi yenye kurudiwarudiwa katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 6:11; 8:10; 11:15; 14:29). Hii imeundwa na VITENZI viwili:

1. “utakula” - BDB 37, KB 46, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

2. "kushiba" - BDB 959, KB 1302, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

11:16-17 Mistari hii ni ya kimaonyo ("iweni macho," BDB 1036, KB 1581, *Niphal* ya KAULI SHURUTISHI, kama vile 4:9,15,23; 6:12; 8:11; 11:16; 12:13,19,28,30; 15:9; 24:8, tazama maelezo katika 6:12) kuhusu kuabudu sanamu na madhara yake.

MADA MAALUM: MADHARA YA KUABUDU SANAMU (kama vile Kumb. 11:16-17

A. "Jihadharini, msiiache mioya yenu ikadanganyika" – BDB 834, KB 984, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Ayubu 31:27

1. "geukeni" – BDB 693, KB 747, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kut. 32:8; 9:12; 17:11,17; Yer. 5:23

2. "kuitumikia miungu mingine" – BDB 712, KB 773, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kumb. 7:4,26; 8:19; 11:16; 13:6,13; 17:3; 28:14,36,64; 29:26; 30:17; 31:20; Yos. 23:16; 24:2,16; Yer. 11:10; 13:10; 16:11,13; 22:9; 25:6; 35:15

3. "kuiabudu" – BDB 1005, KB 295, *Hithpael* (Owens, uk. 805) na *Hishtaphel* (Parsing Guide, uk. 146)

Mara nyingi hii ilikuwa tabia ya mara kwa mara kwa upande wa Israeli! Madhara ya kuabudu sanamu yalikuwa makubwa.

B. "Hasira ya Bwana ikawaka juu yenu" – BDB 354, KB 351, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kut. 4:14; 22:24; 32:10; Hes. 11:1,10; 12:9; 32:10; Kumb. 6:15; 7:4; 11:17; 29:27; Yos. 23:11

1. "Naye atazikomesha mvua za mbingu hata zisinyeshe." Hiki ni kipengele cha laana kwa sababu ya kutoliitii agano, kama vile Kumb. 28:24; 2 Nya. 6:26-28; 7:13

2. "nchi haitatoa matunda yake" – matokeo ya kutokuwa na mvua

C. "mtafia katika katika nchi iliyo nzuri upesi" – BDB 1, KB 2, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kumb. 4:26; 7:4; 8:19,20; 28:20,22; 30:18; Yos. 23:13,16

Hakuna uchaguzi wa kati! Mungu analitoa agano lake kama utii halisi au lenye kupuuzwa. Mwanadamu aliyeanguka hawezi kukipata kiwango hiki cha uaminifu au utii kamili (kama vile Yos. 24:19). Kwa hiyo, kulikuwa na/huo unahitajika kwa ajili ya agano jipya unajikita katika huruma za Mungu na matendo yake (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38; Rum. 3:9-18,23; Wagalati 3)!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 11:18-25

¹⁸ Kwa hiyo yawekeni maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu; yafungeni yawe dalili juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu. ¹⁹Nayo wafunzeni vijana vyenu kwa kuyazungumza uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. ²⁰Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako; ²¹ili siku zenu zifanywe nyingi, na za vijana vyenu nao, juu ya nchi Bwana aliyowaapia baba zenu kuwa atawapa, kama zilivyo siku za mbingu juu ya nchi. ²²Kwa kuwa kwamba mtayashika kwa bidii maagizo haya yote niwaagizayo, kuyafanya; kumpenda Bwana, Mungu wenu, na kutembea katika njia zake zote, na kushikamana naye; ²³ndipo Bwana atakapowafukuza mataifa haya yote mbele yenu, nanyi mtamiliki mataifa makubwa yenye nguvu kuwapita ninyi. ²⁴Kila mahali mtakapokanyaga kwa nyayo za miguu yenu patakuwa penu; tokea hilo jangwa, na Lebanoni, na tokea mto wa Frati, mpaka bahari ya magharibi, itakuwa ndiyo mipaka yenu. ²⁵Hapatakuwa na mtu atakayeweza kusimama mbele yenu; Bwana, Mungu wenu, ataweka utisho wenu na kuhofiwa kwenu juu ya nchi yote mtakayoikanyaga, kama alivyowaambia.

11:18-20 Mistari hiini muhtasari wa sura ya 6:6-9. Hii inamaanisha hitaji la kuyatunza maneno kwa ajili ya uaminifu wa kuishi maisha ya ndani ya mwangaza wa maneno ya Mungu!

☛ **"yawekeni maneno yangu"** Kifungu hiki ni cha kistiari, BDB 962, KB 1321, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile 32:46. Hivi ndivyo stiazi za 6:8 na Kut. 13:9,16 zinavyoamaanisha. Lishike neno la Mungu siku zote na

kuliweka akilini mwenu. Lichunguze kila tendo katika mwangaza wake!

11:19 “wafunzeni vijana vyenu” Tazama maelezo katika 4:9.

11:20 “yaandike” Katika kipindi kilichopita baadhi ya wanazuoni walijiuliza juu ya uwezo wa Musa na Waisraeli wa kale kuweza kuandika. Kama ushahidi mambo ya siku za mwisho ulivyoboreshwawa, kwa siku za leo hakuna awezaye kulipinga hili. Tazama “The Question of Israelite Literary” in *Approaches to the Bible*, juzuu. 2, kr. 142-53 (kutooka Biblical Archaeology Society, 1995).

11:21

NASB “kama zilivyo siku za mbingu juu ya nchi”

NKJV “ziwavyo siku za mbingu juu ya nchi”

NRSV “kama zilivyo mbingu juu ya nchi”

TEV, NJB “kama lilivyo anga juu ya nchi”

Huu ni usemi wenye kufanana na kifungu “kanuni ya milele” (yaani, Ku. 12:14,17,24,25; 13:10). Hii ni stiari ya hali ya kudumu.

11:22 Asili ya sheria ya agano (kama vile mst. 13) na mahitaji yake ni ya mata kwa mara:

1. sheria hii ni sawa na mst. 13, lakini inatofauti ndogo tu:
 - a. “Kwa kuwa” na, BDB 49
 - b. “mtayashika” BDB 1036, KB 1581, *Qal* ya KITENZIJINA HALISI na *Qal* ya KITENZI CHA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (tungo ya kisarufi inatumika ili kuleta msistizo)
2. mahitaji (mtiririko wa *Qal* ya KITENZIJINA cha MIUNDO YA MANENO, kama mst. 13):
 - a. “kuyafanya” - BDB 793, KB 889
 - b. “kumpenda” - BDB 12, KB 17
 - c. “kutembea” - BDB 229, KB 246, kama vile 8:6
 - d. “kushikamana” - BDB 179, KB 209, kama vile 10:20; 13:4

11:23-25 Haya ni matokeo yaliyoahidiwa (yaani, “kama alivyowaambia,” mst. 25) ya sheria ya agano:

1. “Bwana atakapowafukuza mataifa haya yote mbele yenu,” mst. 23, BDB 439, KB 441, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kut. 34:24; Hes. 32:21; Kumb. 4:37-38; 9:4-5; Yosh. 23:5,13
2. “nanyi mtamiliki mataifa makubwa yenye nguvu kuwapita ninyi,” mst. 23, BDB 439, KB 441, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile 7:17; 9:3; Hes. 33:52
3. “Kila mahali mtakapokanyaga kwa nyayo za miguu yenu patakuwa penu,” mst. 24, BDB 201, KB 231, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Yosh. 1:3. Mipaka yao inaelezwa katika Mwa. 15:18; Kut. 23:31; Kut. 1:7; 3:12-17; Yosh. 1:1-4; 13:8-12
4. “Hapatakuwa na mtu atakayeweza kusimama mbele yenu,” mst. 25, BDB 426, KB 427, *Hithpael* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 7:24; Yosh. 1:5; 10:8; 23:9
5. “Bwana, Mungu wenu, ataweka utisho,” BDB 678, KB 733, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - a. “hofu” - BDB 808, kama vile 2:25
 - b. “woga” - BDB 432, kama vile Mwa. 9:2.

Hii ni kweli yenye kufanana, lakini ni tofauti katika maneno yaliyo katika Kut. 23:27 na Yosh. 2:9.

11:24 Kwamaelezo kamili yahasuyo mipaka ya Nchi ya Ahadi tazama 1:8.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 11:26-28

²⁶ Angalieni, nawawekea mbele yenu hivi leo baraka na laana; ²⁷ baraka ni hapo mtakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wenu, niwaagizayo leo; ²⁸ na laana ni hapo msiposikiza maagizo ya Bwana, Mungu wenu, mkikengeuka katika njia niwaagizayo leo, kwa kuandama miungu mingine msiojua

11:26-28 Mistari hii inaendeleza matokeo ya sheria ya agano kati ya YHWH na watu wake. Haya yanawekewa upanuzi katika Kumbukumbu la Torati 27-29. Mistari inaeleza sana historia ya Wayahudi.

Aya hii inaanza kwa wito wa angalizo, "Tazama" - BDB 906, KB 1157, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 1:8,21; 2:24; 4:5; 11:26; 30:15; 32:39. Hili neno "leo" (BDB 398) ni njia ya kuupinga ulaghai, tendo la muda mfupi (kama vile 4:39).

1. "baraka" - BDB 139
 - a. "mtakapoyasikiza" - BDB 1033, KB 1570, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, "niwaagizayo," kama ilivyoamriwa katika 4:1; 5:1; 6:3,4; 9:1; 20:3; 27:10; 33:7; ilivyoamriwa katika 7:12; 11:13(mara mbili); 15:5(mara mbili); 28:1(mara mbili),13; 30:10,17
2. "laana" - BDB 887
 - a. "msiposikiza," sawa na hapo juu, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - b. "mkikengeuka" - BDB 693, KB 747, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU
 - c. "kwa kuandama miungu mingine" - BDB 229, KB 246, kiuhalisia, "kutembea na," kama vile 6:14; 8:19; 11:28; 13:2; 28:14; Amu. 2:12; Yer. 7:6,9; 11:10; 13:10

Tofauti hii ya hatma mara nyingi inaitwa "njia mbili" (kama vile sura 28 na 30:1,15-20; Zab. 1; Yer. 21:8; Mt. 7:13-14).

11:28 "msiojua" Kiuhalisia hili ni neno "kujua." Tazama maelezo katika 4:35.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 11:29-32

²⁹Tena itakuwa, atakapokuleta Bwana, Mungu wako, na kukutia katika nchi uendeayo kuimiliki, ndipo uiweke baraka juu ya mlima wa Gerizimu, na laana uiweke juu ya mlima wa Ebali. ³⁰Je! Haiwi ng'ambo ya Yordani? Nyuma ya njia ya machweo ya jua, katika nchi ya Wakanaani waketi katika Araba kuelekea Gilgali, kando ya hiyo mialoni ya More? ³¹Kwani ninyi mtavuka Yordani mwingie kuimiliki nchi awapayo Bwana, Mungu wenu, nanyi muimiliki na kuketi humo. ³²Nanyi angalieni mzifanye amri na hukumu zote niwawekeazo leo mbele yenu.

11:29 "baraka. . . laana" Mistari huu unaeleza juu ya taratibu zakulifanya agano upya zilizofanywa na Yohana huko Shekemu (kama vile sura 27-28 na ya Yosh. 8:30-35). Kwa uwazi kabisa makundi mawili ya waimbaji wa Kilawi yaliimba au kuzisifia baraka toka MI. Gerezimu na laana toka kwa bwana Ebali. Hii milima miwili ilikuwa pembezoni mwa Shekemu (yaani, yenye maana ya kingo za mabega, BDB 1014). Utafiti wa mambo ya kale umegundua jiwe kubwa la madhabahu juu ya MI. Ebali ambalo linaendana na maelezo ya madhabahu hii ndani ya Talmud. Tazama Utangulizi wa kitabu VII.

Mstari huu unaifuatisha Mikataba ya Suzerain Hittite, ambayo inamhusianisha mfalme na dhima inayozungumziwa (kama vile Kumb. 27: Yosh. 24 kwa mpangilio ule ule).

11:30 "Araba" Hili ni Bonde la Yordan kusini mwa Bahari ya Shamu. Tazama maelezo katika 1:1.

☐ **"Gilgali"** Neno hili linamaanisha "mzunguko wa mawe" (BDB 166 II), ambalo lilikuwa jina la kambi ya kwanza ya Waisraeli humo Kanaani (kama vile Yosh. 4:19). Hata hivyo, hii inaweza kuwa mbele ya kaskazini karibu na

Shekemu (tazama *The IVP Bible Background Commentary, OT*, uk. 181).

▣ **“mialoni More”** Huu ni mti uliokuwa umejitenga aukichaka. Tunafahamu kuwa eneo hili lilikuwa limejitenga karibu na Shekemu kwa sababu ya Mwa. 12:6 na 35:4. Jina More linamaanisha “mwalimu” (BDB 435).

11:31-32 Mistari hii ya kimhutasari yenye kueleza kile kilichokuwa kimeelezwa mara nyingi kabla.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwani kitabu cha Kumbukumbu la Torati kinarudia sana vifungu vile vile na matukio ya kihistoria?
2. Ni kwa namna gani misingi ya amri au uchaguzi wa Agano unasistizwa?
3. Ni kwa namna gani ukuu wa YHWH unasistizwa?

KUMBUKUMBU LA TORATI 12

MIGAWANYO YA AYA KATIKA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Agizo la mahali pa Kuabudu	Mahali pa kuabudu	Eneo moja kwa ajili ya kuabudu	Muundo wa sheria (12:1-26:15)
12:1-28	12:1	12:1-3	12:1
	12:2-7		Mahali pa kuabudu 12:2-3
	12:8-12	12:4-7 12:8-14	12:4-7 12:8-12
	12:13-14		Utaratibu wa sadaka 12:13-14
	12:15-19	12:15-19	12:15-16 12:17-19
	12:20-27	12:20-28	12:20-28
Kujihadhari na Miungu ya uongo		Onyo dhidi ya ibada ya sanamu (12:29-13:18)	Dhidi ya imani za Wakanaani
12:29-32	12:29-32	12:29-31	12:29-13:1
(12:32-13:18)	Onyo dhidi ya ibada Ya sanamu	12:32	

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI(tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi) **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. Nk.

UTANGULIZI

- A. Hili limeanza na ukuzaji wa amri kumi katika sheria za kila siku (yaani, sura 12-26), ambalo linaifunika Israeli na maisha ya kiulimwengu na utakatifu. Ikiwa mmoja atafuata muhtasari wa mikataba ya Wahiti, hivyo (1) 4:1-11:32 inajumuisha misingi ya sheria na (2) 12:1-26:19 ni sifa panuzi na ufafanuzi wa sheria hizo.

Wanazuoni wameonyesha kwa kuzielezea nne “mkusanyiko wa sheria zilipangwa kwa mfumo maalumu” katika vitabu vitano vya kwanza vya Biblia:

1. Kitabu cha agano, Kut. 20:22-23:33

2. Kanuni za kuhani, Kut. 25-31 na 34:29 kupitia katika Mambo ya Walawi 16
3. Kanuni za Patakatifu, Mambo ya Walawi 17-26
4. Kanuni za kitorati, Kumbukumbu la Torati sura 12-26 na 28

Hata hivyo, orodha hii imeathiriwa na chanzo hatari kilichojitokeza cha Julius Wellhausen (yaani, waandishi J=YHWH; E=*Elohim*; D=Deuteronomy; na P=priestly) katika vitabu vitano vya kwanza vya Biblia zaidi kuliko sasa, millennia ya pili K.K vinafanana (kama vile R. K. Harrison, *Old Testament times* na John H. Walton, *Ancient Israelite Literature In Its Cultural Context*).

- B. Sura hii ilikuwa ni mabishano yaliyohusu tarehe ya ghadhabu za Kumbukumbu la Torati. Kiini chake mist. 1-7 ambacho kiliita eneo moja muhimu la madhabahu ya kuabudu (baadaye Yerusalemu).
- C. Inaonekana kwamba andiko hili linasimulia vipindi viwili tofauti na makusudi: (1) katika jangwa (yaani, hema la kukutania) na (2) katika nchi ya ahadi. Kusudi la sheria yote ni kumwabudu YHWH
Kwa heshima katika mahali, shauku na muundo. Ibada ya sanamu na mahali pao pa kuabudu ilikataliwa. Mashaka yanaonekana kati ya uhalali wa mahali maalumu pa kuabudu (Kut. 20:24; Kumb. 16:21) na sehemu maalumu ya Israeli ya kuabudu. Mahali maalumu na madhabahu maalumu (kama vile Kumbukumbu la Torati 27) palipo ruhusuwa (mf. I afal. 3:3-5), lakini saduku la agano, hema la kukutania na baadae hekalu zilitiliwa mkazo.
- D. Kihistoria lazima itambulike kwamba mageuzi ya Hezekia yalilenga eneo maalumu la kuabudu zaidi kuliko mageuzi ya Yosia, ambayo kawaida yalitumika kama tukio lililoaminika kihistoria kwa ajili ya maandiko ya Kumbukumbu la Torati (yaani, 621 K.K., kama vile II Fal. 18:22; II Nya. 32:12 na Isa. 36:7). Mageuzi ya Yosia awali yalikusika na ibada ya sanamu sio mahali pa kuabudu! Binafsi nakataa nadharia ya chanzo cha shutuma ya vitabu vitano vya kwanza vya Biblia JEDP (kama vile Josh McDowell *More Evidence That Demands A Verdict*).

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 12: 1-7

¹ Hizi ndizo amri na hukumu mtakazotunza kuzifanya katika nchi aliyokupa Bwana, Mungu wa baba zako, uimiliki, siku zote mtakazoishi juu ya nchi. ² Vunjeni kabisa mahali pote walipokuwa wakiitumikia miungu yao mataifa mtakayoyamiliki, juu ya milima mirefu, na juu ya vilima, na chini ya kila mti wenye majani mabichi; ³ nanyi zivunjeni madhabahu zao, zibomoeni nguzo zao, na maashera yao yateketezeni kwa moto, na sanamu za kuchonga za miungu yao zikateni; na jina lao lifutilieni mbali na mahali hapo. ⁴ Wala msimfanyie hivyo Bwana, Mungu wenu. ⁵ Lakini mahali atakapochagua Bwana, Mungu wenu, katika kabila zenu zote, apaweke jina lake, maana, ni makao yake, elekezeni nyuso zenu hapo, nawe wende huko; ⁶ pelekeni huko sadaka zenu za kuteketewa, na dhabihu zenu, na zaka zenu, na sadaka ya kuinuliwa ya mikono yenu, na nadhiri zenu, na sadaka zenu za hiari, na wazaliwa wa kwanza wa makundi yenu ya ng'ombe na ya kondoo; ⁷ na huko mtakula mbele za Bwana, Mungu wenu, nanyi furahini katika yote mtakayotia mikono yenu, ninyi na wa nyumbani mwenu, aliyokubarikia Bwana, Mungu wako.

12:1 “amri na hukumu” Tazama Mada Maalumu katika 4:1.

☐ “**mtakazotunza**” Huu ni muunganiko wa KITENZI, “linda” (BDB 1036, KB 1581, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) na *Qal* ya KITENZI JINA HALISI CHA MUUNDO WA MANENO, (BDB 793, KB 889). Hii ni dhamira inayojirudia (mf. Kut.23:13,21; 34:11-12; Law. 18:4-5,26,30; Kumb. 4:6,9,15,23,40; na mara nyingi zaidi hasa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati na fasihi ya hekima).

☐ “**aliyokupa Bwana, Mungu wa baba zako**” KITENZI kinaonyesha tendo lililokamilika (BDB 678, KB 733, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU), bado matukio ni ya wakati ujao. Ni njia ya Kiebrania ya kuonyesha imani (yaani,

ukamilifu wa kinabii). Hii ni dhamira iliyojirudia katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 1:8,20,21,25,35,36,39; 2:29; 3:18,20; 4:1,21,38,40; 5:16,31; 6:10,23; 7:13,16; 8:10; 9:6,23; 10:11; 11:9,17,21,31; 12:1,9; 15:4; 17:14; 18:9; 19:1,2,8,14; 21:23; 24:4; 25:15,19; 26:1,2,3,6,9,10,15; 27:3; 28:8,11,52; 31:7; 32:49; 34:4). Inaonyesha chaguo la rehema za YHWH na utoaji kwa ajili ya Israeli.

☐ **“uimiliki”** KITENZI hiki (BDB 439, KB 441, *Qal* ya KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO) ni ahadi inayojirudia. Tazama Mada Maalumu: Kuimiliki Nchi katika 8:1.

☐ **“juu ya nchi”** Kifungu “juu ya nchi” ni njia nyingine ya kusema “katika nchi” (kama vile mst. 19). Kwa kadri wana wa Israeli watakvoyozitunza amri za Mungu, ndivyo watakvoyoishi katika nchi ya ahadi. Tazama muhtasari katika 4:40.

Kifungu hiki kina tofauti mbili za maneno “nchi”:

1. “katika nchi” - BDB 75
2. “juu ya nchi” - BDB 9

Yote yanarejelea kwa dunia nzima au kwa nchi ya Kanaani. Hivyo kwa kawaida ni visawe (kama vile. 4:38-40; 11:8-9; 12:1; 26:2,15).

12:2 “Vunjeni kabisa mahali pote” Kifungu “vunja kabisa” linatokana na neno la Kiebrania lenye maana ya “sababisha maangamizi” (BDB 1, KB 2, *Piel* KITENZIJINA HALISI na *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, ambalo linaonyesha mamlaka, kama vile mst. 3; Hes. 33:52[mara mbili]; II Fal. 21:3). Mungu alikuwa anawaonya wana wa Israeli ili kuiangamiza madhabahu ya wapagani ili kwamba isije kuwa sehemu yao ya ibada ya ustawi (kama vile Kut. 23:24; 34:13).

☐ **“juu ya milima mirefu, na juu ya vilima, na chini ya kila mti wenye majani mabichi ”** haya ni maeneo maalumu ya madhabahu ya *Ba'al* na *Asherah* ambapo taratibu za ibada ya ustawi zilifanyika (kama vile Yer. 2:20; 3:2,6; 17:2; Isa. 57:5,7; Hosea 4:13).

12:3 “nguzo takatifu” Tazama Mada Maalumu hapa chini.

MADA MAALUM : Kushawishika kwa Israeli kwenye Ibada ya Ustawi wa Wakanaani

Kumbukumbu la torati 12:3 linaorodhesha vipengele mbalimbali vya dhehebu la kumwabudu *Ba'al* na namna ilivyompasa Israeli kuviangamiza vitu vihusianavyona dhehebu hilo.

1. "zivunjeni madhabahu zao"
 - a. hiki KITENZI, BDB 683, KB 736, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kumb. 7:5; 2 Nya. 31:3; 34:4
 - b. kipengele cha, "madhabahu," BDB 258, *Ba'al's* madhabahu yalikuwa majukwaa ya kipande cha jiwe pamoja na jiwe kubwa lililo inuka (nguzo) na kuwekewa shimo la kupanda mti au kifungio cha ubao, nguzo iliyochongwa (*Asherah*)
2. "zibomosheni nguzo zao"
 - a. hiki KITENZI, BDB 990, KB 1402, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kumb. 7:5; 2 Fal. 3:2; 10:27
 - b. kipengele cha, "nguzo," BDB 663. Haya yalikuwa mawe yaliyo inuka yenye kutumika kama ishara ya mungu wa ustawi wa nguvu za uzazi wa mwanamme (kama vile Kumb. 16:22).
3. "yakateni maashera yao, ziteketezeni kwa moto"
 - a. hiki KITENZI, BDB 976, KB 1358, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Kut. 7:5, katika 2 Nya. 31:1 na 34:4, iliwapasa "kukatwakatwa."
 - b. kipengele cha, *Asherim*, BDB 81. Hii iliashiria mti wa uzima. *Asherah* (kama vile ABD, juzuu 1, kr. 483-87, ambapo mti huu u katika mashairi ya kifasihi toka Ugarit, *Anath* is *Ba'al's* consort, kama vile ABD, juzuu. 1, kr. 225-26) ambaye alikuwa mwenza wa kike wa *Ba'al*. Huu unaweza kuwa mti wa moja kwa moja au nguzo iliyochongwa

4. "ziteketezeni kwa moto sanamu zao za kuchonga"
 - a. hiki KITENZI, BDB 154, KB 180, *Piel* YA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Kumb. 7:5; 2 Nya. 14:2; 31:1; 34:4,7
 - b. kipengele cha, "ziteketezeni kwa moto sanamu zao za kuchonga," BDB 820 TUNGO 43. Kumb. 7:5; na 2 Nya. 34:7 inatengeneza tofauti kati ya *Asherim* na sanamu.
5. "Vunjeni kabisa mahali pote"
 - a. hiki KITENZI, BDB 1, KB 2, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Kumb. 12:2 (mara mbili)
 - b. kipengele, "jina," BDB 1027. Neno hili linaonekana kuwakilisha jina la mungu kama mmiliki wa eneo, ambalo sasa linaharibiwa na, hivyo, majina yao yanatoweka. Ni jina la YHWH lenye jina/linaloabudiwa katika eneo hili sasa (kama vile Kumb. 12:5,11).

12:5 "mahali atakapochagua Bwana" Mungu alichagua (BDB 103, KB 119, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, Kama vile mist. 11,14,18,21,26; 14:23-25; 15:20; 16:2,6,11,15; 17:8,10; 18:6; 26:2; 31:11) sehemu ya kuabudia (kama vile Kut. 20:24).

Hema la kukutania (sanduku la agano) lilisafiri na Israeli:

1. Gilgali, Yosh. 4:19; 10:6,15
2. Shekemu, Yosh 8:33
3. Shilo, Yosh 18:1; Amu. 18:31; I Sam. 1:3
4. Betheli, (inawezekana) Amu. 20:18,26-28; 21:2
5. Kiriath-yearimu, sanduku la agano, I Sam. 6:21; 7:1-2 (makuhani huko Nobu, kama vile I Samueli 21-22)
6. Yerusalemu
 - a. Daudi anautwaa mji wa Wayebusi (kama vile II Sam. 5:1-10)
 - b. Daudi analireta sanduku la agano Yerusalemu (kama vile II Samuel 6)
 - c. Daudi ananunua eneo la hekalu (II Sam. 24:15-25; II Nya. 3:1)

Wanazuoni wengi wa leo wanajaribu kutetea kwamba kitabu cha Kumbukumbu la Torati kiliandikwa baada ya kupata nafasi ya mageuzi ya Hezekia na Yosia ya mahali maalumu pa kuabudia. Hata hivyo, Kumbukumbu la Torati halitaji Yerusalemu kama eneo maalumu ambalo YHWH atalichagua. Katika muktadha wa kitheolojia ni kinyume kati ya:

1. Eneo takatifu la *Ba'al* na mojawapo ya eneo takatifu la Israeli
2. Imani ya Mungu mmoja wa Israeli dhidi ya miungu wengi wa Wakanaani (na mwisho mashariki ya karibu ya kale)



NASB "apaweke jina lake, maana, ni makao"
NKJV "ili aliweke jina kwa ajili ya maskani yakelake"
NRSV "kama maskani yake ili aliweke jina lake huko"
TEV "ambapo watu watakuja katika uwepo wake"
NJB "huko ataliweka jina lake na kupata maskani"

Tafsiri ya kifungu hiki inaathiriwa na mst. 11. Kifungu cha 5 kina neno "ni makao yake" (BDB 1015), ambapo mst. 11 una "alikalisha jina" (BDB 1014, KB 1496, *Piel* ya KITENZI CHA MUUNDO WA MANENO). Kwa maana ya kufanana sana na hapakuwa na tofauti kitheolojia au kividokezo.

Wayahudi walibadilisha jina la Mungu kwa ajili ya uwepo wa Mungu. Hii ni rejea iliyolenga Hema la kukutania katika siku za awali.

MADA MAALUM: "JINA" LA YHWH (AGANO LA KALE)

Matumizi ya "jina" kama neno mbadala wa YHWH Yeye mwenyewe ni usambamba wa Kut. 23:20-33 matumizi ya "malaika," anayesemekana kuwa "Jina langu li ndani Yake." Huu mbadala pia unaweza kuonekana katika matumizi ya "utukufu Wake" (mfano Yohana 1:14; 17:22: Angalia Mungu anaelezewa kama mwanadamu). Majaribio yote ni kulainisha tabia yake binafsi ya kupewa sifa za kibinadamu ya uwepo wa YHWH

(kama vile Kut. 3:13-16; 6:3). YHWH hakika anazungumzwa juu ya namna ya kibinadamu, lakini pia ilijulikana kama alikuwepo kiroho katika uumbaji wote (kama vile I Wafalme 8:27; Zab. 139:7-16; Yer. 23:24; Mdo. 7:49 ananukuu Isa. 66:1).

Kuna mifano kadhaa ya “jina” ikiwakilisha maana ya uungu wa YHWH na uwepo wake binafsi.

1. Kumb. 12:5; II Sam. 7:13; I Wafalme 9:3; 11:36
2. Kumb. 28:58
3. Zab. 5:11; 7:17; 9:10; 33:21; 68:4; 91:14; 103:1; 105:3; 145:21
4. Isa. 48:9; 56:6
5. Ezek. 20:44; 36:21; 39:
6. Amosi 2:7
7. Yoh. 17:6,11,26

Dhana ya “kuita” (yaani kuabudu) jina la YHWH linaonekana mwanzoni katika Mwanzo.

1. Mwa. 4:26, uzao wa Sethi
2. Mwa. 12:8, Ibrahimu
3. Mwa. 13:4, Ibrahimu
4. Mwa. 16:13, Hajiri
5. Mwa. 21:33, Ibrahimu
6. Mwa. 26:25, Isaka

na katika Kutoka:

1. 5:22-23, inaongea katika jina Lako
2. 9:16, tangaza jina langu katika dunia yote (kama vile Rum. 9:17)
3. 20:7, usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako (kama vile Law. 19:12; Kumb. 5:11; 6:13; 10:20)
4. 20:24, ambapo nitasababisha jina langu kukumbukwa (kama vile Kumb. 12:5; 26:2)
5. 23:20-21, malaika (“kwakuwa jina langu li ndani yake”)
6. 34:5-7, Musa anaita (au “kuliitia”) jina la Bwana. Hili ni kati ya maandiko machache kwamba yanayoelezea tabia ya YHWH (kama vile Neh. 9:17; Zab. 103:8; Yoeli 2:13)

Kumfahamu mtu kwa jina kunamaanisha ukaribu (kama vile Kut. 33:12); Musa analijua jina la YHWH na katika 33:17, YHWH analijua jina la Musa. Huu ni muktadha ambapo Musa anataka kuona utukufu wa Mungu (kama vile mstari wa 18), lakini Mungu anaruhusu yaya kuona “Wema Wake” (mstari wa 19), ambao ni sambamba na “jina” (mstari wa 19).

Waisraeli wanatakiwa kuharibu “majina” ya miungu ya Kanaani (kama vile Kumb. 12:3) kumuita Yeye (kama vile Kumb. 6:13; 10:20; 26:2) katika mahali maalumu Anasababisha jina lake kukaa/kudumu (kama vile Kut. 20:24; Kumb. 12:5,11,21; 14:23,24; 16:2,6,11; 26:2).

YHWH anakusudi la kiulimwengu likiwemo jina lake

1. Mwa. 12:3
2. Kut. 9:16
3. Kut. 19:5-6
4. Kumb. 28:10,58
5. Mika 4:1-5

12:6 kifungu hiki kinataja aina kadhaa za matoleo:

1. **“sadaka za kuteketezwa”** hii ilimaanisha sadaka zote za kuteketezwa (BDB 750 II). Hii ilikuwa njia ya kuonyesha kujitoa kwa dhati mbele za Mungu. Ilikuwa ni sadaka ya hiari (kama vile Mambo ya Walawi 1).
2. **“dhabihu”** hii inarejelea sehemu za kuteketezwa, sehemu ya matoleo ya kuteketezwa (BDB 257). Hizi zilikuwa sadaka za dhambi, sadaka za amani, sadaka za shukrani, nk. Hizi zilikuwa ni sadaka zozote zilizohusisha damu (kama vile Mambo ya Walawi 7).
3. **“zaka”** zaka ilikuwa njia ya Waisraeli kuwategemeza makuhani, ambao hawakupata urithi wa nchi. Inaonekana kuna zaka aina tatu (BDB 798):
 - a. Kwa ajili ya mahali patakatifu
 - b. Kwa ajili ya mahali pa Walawi, wenye kuwajibika

- c. Kila baada ya miaka mitatu kwa ajili ya masikini (Law. 27:30-33; Hes. 18:21-22)
4. **“sadaka ya kuinuliwa ya mikono yenu”** Hili ni neno la Kiebrania kwa ajili ya “sadaka ya kuinuliwa” (BDB 929, kama vile Law. 7:32). Hii inarejelea sadaka ambayo sehemu ya mnyama ilitolewa kwa ajili ya kula makuhani.
 5. **“sadaka za nadhiri”** Huu (BDB 623) ni mfano wa hali ya kiapo kwa Mungu, “nitafanya hivi, ikiwa utafanya hivyo.” Hii ni sehemu ya Wayahudi kutunza kiapo chao (Law. 7:16-18).
 6. **“sadaka zenu za hiari”** Hizi (BDB 621) zinarejelea shukrani ya mtoaji au sifa kutokana na kuzidi kwa mema ya Mungu (kama vile Law. 22:18nakuendelea).
 7. **“mzaliwa wa kwanza”** Hizi (BDB 114) zinarejelea kwa malaika wa kifo aliyepita kati ya Wamisri na kuua mzaliwa wa kwanza wa mnyama na wa mwanadamu. Kwa ufahamu wa tukio hili wazaliwa wa kwanza wote wa mnyama na wa wanadamu walikuwa wa kipekee kwa Mungu (kama vile Kut.13; Law. 27:26-27)!

12:7 “huko mtakula mbele za Bwana” Hii inarejelea chakula cha ushirika, ambacho kitheolojia kinatangulia mbele ya Pasaka na Ekaristi zote (kama vile mist. 12,18; 14:26; Ufu. 3:20). Watu wa Mungu waliumbwa ili kufurahi (BDB 970, KB 1333, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) pamoja nae katika uumbaji wa kimwili na kuabudu kwa urafiki wa karibu sana (kama vile Law. 23:40; Hes. 10:10; Kumb. 12:7,12,18; 14:26; 16:11; 26:11; 27:7; 28:47).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 12: 8-12

⁸ Msifanye kwa kufuata mambo yote tuyafanyayo hapa leo, kila mtu kama aonavyo vema machoni pake; ⁹kwani hamjafikilia bado katika raha na urithi akupao Bwana, Mungu wako. ¹⁰Lakini mtakapovuka Yordani na kukaa katika nchi anayowarithisha Bwana, Mungu wenu, akawapeni raha, akiwaokoa na adui zenu pande zote, mkakaa salama; ¹¹wakati huo itakuwa kwamba mahali pale atakapopachagua Bwana, Mungu wenu, alikalishe jina lake, hapo ndipo mtakapoleta kila kitu ninachowaamuru; sadaka zenu za kuteketezwa, na dhabihu zenu, na zaka zenu, na sadaka ya kuinuliwa ya mikono yenu, na nadhiri zenu zote teule mtakazoweka kwa Bwana. ¹²Nanyi mtafurahi mbele za Bwana, Mungu wenu, ninyi, na wana wenu, na binti zenu, na watumishi wenu wanawaume na wanawake, na Mlawi aliyemo malangoni mwenu; kwa kuwa hana sehemu wala urithi kwenu.

12:8 “Msifanye kwa kufuata mambo yote tuyafanyayo hapa leo” Mambo yatakuwa ya mfano mmoja katika nchi ya ahadi. Utekelezaji wa kidini kipindi cha wakati wa kutangatanga jangwani ulikua rahisi zaidi kuliko maandalio ya utekelezaji katika nchi ya ahadi, hasa kwenye hekalu, lililowekwa baadae huko Yerusalemu.

☑ **“kila mtu kama aonavyo vema machoni pake”** tungo hii hapa ina kidokezo kisicho pendelea upande wowote, lakini katika kitabu cha Waamuzi kuna kidokezo kibaya cha madai ya uhuru wa kila mmoja kutoka katika masharti ya agano kama kupitia chaguo la dhambi au agano la ujinga (kama vile. 17:6; 21:25).

12:9 Tazama muhtasari katika 12:1

12:10 “akawapeni raha . . . salama” YHWH anakupa raha (BDB 628, KB 679, *Hiphil* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU) kutoka kwa maadui zako. Usalama huu (BDB 442, KB 444, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) haukufanikiwa kwa sababu ya jeshi kubwa la Israeli, bali kwa sababu ya uwepo wa YHWH.

12:11 “mahali pale atakapopachagua Bwana Mungu wenu” Hii inarejelea kwa sehemu maalumu ya kuabudia (yaani, hema la kukutania na sanduku la agano, kama vile mist. 5,14), ambalo kwanza lilikuwa huko Shilo. Tazama muhtasari kamili katika 12:5.

12:12 “Nanyi mtafurahi” Hili ni kusudi la sheria za Mungu (kama vile mist. 7,18; 14:26; 28:47).

☑ **“ninyi, na ”** tambua ni kwa namna gani kila mtu katika familia pamoja na watumishi na Walawi wa mahali (kama vile mst. 19) walikuwa wanajumuishwa! Katika maana hii ilikuwa ni wahusika wa familia nzima. Walikuwa

wanapendwa na kuandaliwa kwa ajili ya, mahitaji muhimu katika maisha na kwa ajili ya uzima ujao (yaani, kuabudu).

12:12, 19 “Mlawi aliyemo malangoni mwenu” Makuhani wote walikuwa Walawi, lakini Walawi hawakua makuhani wote. Hapa “Mlawi” inarejelea familia isiyo kuwa ya makuhani wa Mlawi ambae ni kielelezo cha masikini na mhitaji (kama vile mist. 18,19; 14:27,29; 16:11,14; 26:12-13), kwa sababu Walawi hawakupewa nchi. Waalimu wa sheria wa mahali walikua wanaheshimiwa.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 12:13-14

¹³ Ujihadhari usitoe sadaka zako za kuteketezwa katika kila mahali upaonapo; ¹⁴ bali katika mahali atakapopachagua Bwana katika kabila zako mojawapo, ndipo utakapotoa sadaka zako za kuteketezwa, ndipo utakapotenda yote nikuamuruyo.

12:13 “Ujihadhari usitoe sadaka zako za kuteketezwa katika kila mahali upaonapo ” Mungu atakuonyesha wewe sehemu maalumu kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa (kama vile mist. 5,11,14). Usitumie kwenye madhabahu nyingi za Wakanaani kwa sababu ziko huko. Usimtotee YHWH sadaka za kuteketezwa kwenye madhabahu iliyosimamishwa kwa ajili ya *Ba'al*. Hata hivyo, kuna baadhi ya madhabahu za mahali zilizotengenezwa kwa ajili ya YHWH (kama vile Kumb. 16:21; I Fal. 3:4).

Kifungu hiki kina VITENZI vitatu:

1. “ujihadhari ” - BDB 1036, KB 1581, *Niphal* KAULI SHURUTISHI
2. “usitoe sadaka” - BDB 748, KB 828, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. “upaonapo” - BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 12: 15-19

¹⁵Pamoja na haya waweza kuchinja nyama na kula ndani ya malango yako yote, kwa kufuata yote yatamaniwayo na roho yako, kwa mfano wa baraka ya Bwana, Mungu wako, aliyokupa; aliye tohara na asiye tohara ana ruhusa kula katika nyama hiyo, kama ya paa na ya kulungu. ¹⁶Lakini msiile damu; imwageni juu ya nchi kama maji. ¹⁷Usile ndani ya malango yako zaka ya nafaka zako, wala ya divai yako, wala ya mafuta yako, wala wazaliwa wa kwanza wa makundi yako, ya ng'ombe wala ya kondoo, wala nadhiri zako uwekazo zo zote, wala sadaka zako za hiari, wala sadaka ya kuinuliwa ya mkono wako; ¹⁸lakini hivyo mtakula mbele za Bwana, Mungu wako, mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako, wewe, na mwanao mume na mke, na mtumwa wako mume na mke, na Mlawi aliye ndani ya malango yako; nawe furahi mbele za Bwana, Mungu wako, katika yote utakayotia mkono wako. ¹⁹Jilinde nafsi yako usimwache Mlawi siku zote uishizo katika nchi yako.

12:15, 20-24 “waweza kuchinja” Hii inaonyesha upana wa sheria (kama vile Law. 17:1na kuendelea) ikiwa mnyama ameuawa (BDB 256, KB 261, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kwa ajili ya chakula na sio kwa ajili ya sadaka, anaweza kuuawa popote pale.

12:15 “aliye tohara na asiye tohara” Hii hairejelei kwa wanyama safi mbali na chakula (kama vile mist. 20-22; Law.11), lakini wanyama wasio safi kama mbali na sadaka. Kondoo mwenye dosari anaweza kuliwa na wanadamu kama inavyoweza kuwa kwa wanyama wa mwituni kama Kulungu, lakini sio nguruwe, nk.

12:16 “msiile damu ” Hii inasimulia kutoa heshima kwa Waebrania kwa ajili ya damu kama kielelezo cha uzima. Hata walipoua wanyama, kwa ajili ya kula au sadaka, waliimwaga chini damu (kama vile 15:23; Law. 17:13) na hawakuila, kwa sababu uzima ni wa Mungu. Damu iliwakilisha uzima, na uzima ni wa Mungu (kama vile mist. 23-25; Mwa. 9:4; Law. 7:11-12; 17:10-11)!

12:17-18 Hili ni onyo lingine juu ya kutumia mahali patakatifu kwa ajili ya kuabudu (kama vile mst. 26).

12:17 “zaka” Kifungu hiki kinataja mambo kadhaa ambayo yalikuwa yanhusu zaka (BDB 798 kama vile 14:23; 18:4; Hes.18:12):

1. “nafaka” - BDB 186
2. “divai” - BDB 440
3. “mafuta” - BDB 850

Hii ilikuwa jamii ya wakulima.

12:19 Tazama muhtasari katika mst. 12.

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 12: 20-28

²⁰Bwana, Mungu wako, atakapongeza mpaka wako, kama alivyokuahidi, nawe utakaposema, Nataka kula nyama, kwa kuwa roho yako yatamani kula nyama; waweza kula nyama, kwa kufuata yote inayotamani roho yako.²¹ Na mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako, apaweke jina lake, pakiwa mbali nawe mno, ndipo utakapochinja katika kundi lako la ng'ombe na kondoo alilokupa Bwana kama nilivyokuagiza, nawe utakula ndani ya malango yako, kwa kufuata yote inayotamani roho yako. ²² Kama vile aliwavyo paa na kulungu, ndivyo utakavyoila nyama hii; asiyekuwa tohara na aliye tohara wataila pia. ²³ Ila ujidhadi kwamba usile damu, kwani ile damu ndiyo uhai; na uhai usile pamoja na nyama. ²⁴ Usiile; imwage juu ya nchi kama maji. ²⁵ Usiile; ili upate kufanikiwa, na watoto wako baada yako utakapofanya yaliyoelekea machoni pa Bwana. ²⁶ Ila vitu vyako vitakatifu ulivyo navyo, na nadhiri zako, uvitwae ukaende mahali atakapochagua Bwana; ²⁷ nawe zisongeze sadaka zako za kuteketezwa, nyama na damu, juu ya madhabahu ya Bwana, Mungu wako; na damu ya dhabihu zako uimwage juu ya madhabahu ya Bwana, Mungu wako, na wewe utakula nyama yake. ²⁸ Maneno haya nikuagizayo yote yatunze na kuyasikiza, ili upate kufanikiwa na watoto wako baada yako milele, hapo uyafanyapo yaliyo mema na kuelekea machoni pa Bwana, Mungu wako.

12:20 “Nataka kula nyama” KITENZI hiki (BDB 37, KB 46) kimerudiwa mara tatu:

1. *Qal* HALI YA KUSIHI
2. *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO
3. *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

Ikiwa watatamani kula nyama katika nchi ya ahadi yumkini wanaweza kulitenda hili:

1. Aina ya nyama ya kufaa (mist. 17,22)
2. Aliyeuawa katika sehemu sahihi (mist. 15,18,21,27)
3. Aliyeuawa katika njia sahihi (mist. 16,23-25)

12:23 “ila ujidhadi” KITENZI hiki (BDB 304, KB 302, *Qal* KAULI SHURUTISHI) kinamaanisha “iweni hodari” (kama vile. 31:6,7,23) katika maana ya kiitikio imara kutoka katika kitu fulani (kama vile I Nya. 28:7).

12:26 “vitu vyako vitakatifu” Hii inarejelea vitu vilivyotajwa katika mst. 17.

12:28 “yatunze” KITENZI hiki (BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI SHURUTISHI) kimetumika kwa kurudiwa rudiwa katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 4:9,15,23; 6:12; 8:11; 11:16; 12:13,19,28,30; 15:9; 24:8) ili kutia moyo utiifu kwa agano la YHWH.

☐“ili upate kufanikiwa na watoto wako baada yako milele” KITENZI (BDB 405, KB 408, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kimetumika mara kadhaa katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 4:40; 5:16,29,33; 6:3,18; 12:25,28; 22:7) na katika Yeremia (kama vile 7:23; 38:20; 42:6) na kurejelea maisha yote kwa ujumla ya watu wa YHWH yaliyobarikiwa na ya furaha. Tena, utiifu wa agano unahusishwa na Baraka na maisha marefu katika nchi. Utiifu huu mzima ni onyo kwa vizazi vilivyofanikiwa yaani, milele). Tazama Mada Maalumu: Milele (*’Olam*) katika 4:40.

☐“hapo uyafanyapo yaliyo mema na kuelekea ”

1. "mema" BDB 373 II
 - a. Machoni pa Mungu, 6:18; 13:18; II Nya. 14:2
 - b. Machoni pa wanadamu, Yosh. 9:25; Amu. 19:24; Yer. 26:14
2. "kuelekea" BDB 449, ile ile kama juu, lakini pia Kumb. 12:25; 13:18; I Fal. 11:38; 14:8; 15:11; 22:43; II Fal. 12:2 (kwa ufanano na 1. b. hapo juu, tazama 12:8).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 12: 29-31

²⁹Bwana, Mungu wako, atakapoyakatilia mbali hayo mataifa mbele yako, huko uingiako kuyamiliki, nawe ukawatwaa, na kuketi katika nchi yao; ³⁰ujiangalie, usije ukanaswa ukawafuata, wakiisha kuangamizwa mbele yako; wala usije ukauliza habari za miungu yao, ukisema, Mataifa haya waitumikiaje miungu yao? Nami nifanye vivyo. ³¹Usimtende kama haya Bwana, Mungu wako; kwani kila yaliyo machukizo kwa Bwana, ayachukiayo yeye, wameifanyia miungu yao; kwa maana hata wana wao na binti zao huiteteketeza hiyo miungu yao ndani ya moto.

12:29 "Bwana, Mungu wako, atakapoyakatilia mbali hayo mataifa mbele yako" KITENZI hiki (BDB 503, KB 500, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinamaanisha YHWH atawaondosha watu kwa kuwaua (kama vile 19:1; Yosh. 23:4; II Sam. 7:9; Yer. 44:8). Hii inaonyesha kwamba YHWH anapigana vita vya Israeli.

12:30 "ujiangalie" Tazama muhtasari katika mstr. 28.

☐ **"usije ukanaswa"** KITENZI (BDB 669, KB 723, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU), ni katika *Qal* tawi, ni dhahili kinamaanisha, "Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake" (kama vile Zab. 9:16). tawi *Niphal*, limetumika tu hapa, ni dokezo pana la kistiari la "kulenga shabaha."

☐ **"usije ukauliza habari za miungu yao"** KITENZI (BDB 205, KB 233, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinamaanisha "kutafuta habari":

1. YHWH katika 12:5; 4:29; Yer. 10:21; 29:13
2. miungu ya Wakanaani katika 12:30; II Nya. 25:15,20; Yer. 8:2

12:31 YHWH amesema dhahili kwa Israeli kwamba ikiwa watakuwa na mazoea yale yale ya ibada za machukizo, atawaondoa watoke katika nchi (kama vile 7:4; Law. 18:24-30) kama Wakanaani walivyotenda (kama vile Mwa. 15:16-21). YHWH "anachukia" (BDB 971, KB 1338, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ibada ya sanamu (kama vile 12:31; 16:22; tazama Mada Maalumu: Mungu anaelezewa kama mwanadamu [lugha za kibinadamu] katika 2:15). Tazama Mada Maalumu chini.

MADA MAALUM: MOLECH

Hili neno (BDB 574, KB 592) halina uyakinifu. Kumekuwa na nadharia kadhaa.

1. zinazohusianana miungu iliyo ulimwenguni
 - a. "*Malik*" kutokana na bamba za Ebla (± 2,300 B.C. kutoa Shamu ya kaskazini)
 - b. "*Maliku*" au "*Muluk*" kutokana bamba za huko Mari (± 1800-1750 K.K. kutoka mji wa Sumeria ulio kandokando ya Mto Frati)
2. zinazohusiana na aina ya dhabihu kutokana na matumizi ya neno lenye kuhofisha "*molk*" kutokana na nguzo ya mawe ya afrika Kaskazini kuanzia karne ya 4 hadi karne ya 1 K.K.). Hili linaweza kuwa limemuhusisha kondoo mbadala aliyeteketezwa kwa niaba ya mtoto (Eissfeldt). Toleo la N. H. Snaith theorizes lilimaanisha kwamba watoto walitokana na mapenzi ya kikahaba, yaliyojikita juu ya
 - a. Law. 18:19-23 yenye kuhusika na dhambi za uzinzi, hivyo mstari wa 18 pia unaweza kuwa hivyo
 - b. Hivi ndivyo Kitabu cha Sheria za Kiyunani kinavyolichukulia neno hili pia
3. huenda mkanganyiko uliopo katika neno *Milcom* (kama vile *Molech* katika 1 Fal. 11:7, lakini tambua

kuwa neno *Milcom* linatajwa kama 1 Fal. 11:5,33. Hata hivyo, hawa miungu wote wanarejelewa katika Zab. 106:35-39).

4. Hili neno ni uchezeaji wa neno la Kiebrania unaotokana na konsolnanti za neno "Mfalme" (MLK, BDB 591) zilizounganishwa pamoja na irabu zinazotokana na neno "aibu" (BDB 101 or 102). Hata kama suala hili ni kweli, hili halimwelezi mungu au dhehebu.

Dhehebu la *Molech* linaelezwa kama dhabihu ya mwanadamu kuwatoa watoto kama dhabihu, kwa moto (kwa vyovyote vile waliteketezwa wakiwa hai au walitolewa sadaka baada ya kuuawa kwa namna nyingine, haijulikani). ikiwa hili ni la kweli hii ilikuwa

1. aina ya dhehebu la ustawi
2. dhehebu ambalo lilimwabudu mungu wa ulimwenguni

Huyu mungu alikuwa akiabudiwa humo Yerusalemu katika bonde la wana wa Hinomu, bonde ambalo lilikuja kujulikana kama "Tofethi" (kama vile Isa. 30:33; 57:5; Yer. 7:31; 32:35). Ibada ilikuwa ikibainishwa kwa kutumia wana na mabinti zao kuwateketeza motoni (kama vile Kumb. 12:31; 18:10; 2 Fal. 16:3; 17:17,31; 21:6; Zab. 106:37; Yer. 7:31; 19:5; Eze. 16:20-21). Neno lenyewe linajitokeza katika Law. 18:21; 20:2,3,4,5; 1 Fal. 11:7; 2 Fal. 23:10; Yer. 32:35; huenda Amosi 5:26; Matendo 7:43. Hili dhehebu lilihusiana zaidi na Wafalme wa Yuda, Ahabu na Manase, ingawa linaonekana katika uhusiano wa kale wa Kiyahudi na ibada za ustawi za wapagani walioizunguka.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 12: 32

³²Neno niwaagizalo lo lote liangalieni kulifanya; usiliongeze, wala usilipunguze.

12:32 "usiliongeze, wala usilipunguze" Mungu yuko makini juu ya utiifu wa neno lake (tazama muhtasari katika 4:2). Hata hivyo, Kumbukumbu la Torati linaonyesha baadhi ya sheria za mabadiliko ya kipindi cha jangwani. Ni lazima tuutumie ukweli wa Biblia kwa kila kizazi kipya na utamaduni. Mungu alijifunua mwenyewe kwa utamaduni maalumu katika muda maalumu. Baadhi yake pekee zinasimulia muda na watu (mf, vita takatifu, mitala, utumwa, kutumikisha mwanamke), lakini zaidi ni ukweli wa milele utumike kwa kila kipindi (ili kujadili namna ya kutofautisha kati umilele na utamaduni, tazama Fee na Stuart, *How To Read the Bible For All Its Worth*, kr. 149-164 na Gordon Fee, *Gospel and Spirit*, kr. 1-36).

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembele katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini kuna mkazo zaidi wa eneo maalumu la kuabudu?
2. Kwa nini baadhi ya sheria zimebadilika?
3. Kwa nini damu ilikua ni ya muhimu kwa Waebrania?
4. Kwa nini sheria hizi zimeelezea kila kitu kwa ukamilifu?

KUMBUKUMBU LA TOTARI 13

MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Adhabu kwa wale walioasi	Onyo juu ya ibada ya sanamu (12:32-13:19)	Onyo juu ya ibada ya sanamu (12:29-13:18) 12:32-13:5	Juu ya ushirikina wa Wakanaani (12:29-13:1)
13:1-5	13:1-5		Juu ya ushawishi wa Ibada ya sanamu
13:6-11	13:6-11	13:6-11	13:2-6 13:7-12
13:12-18	13:12-18	13:12-18	13:13-19

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Taz. uk. vii katika kipengele cha utangulizi) *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (ukisoma mzunguko wa #3, uk. viii).linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA HISTORIA YA NYUMA

- A. Hiki ni kifungu kigumu cha maandiko kuweza kukitafasiri na kukielewa. Sio kifungu ambacho mtu anaweza kukitumia ili kuelezea upendo wa Mungu.
- B. Sura hii ni mabishano kati ya ibada ya sanamu katika viwango vyote vya dini, vile vile pia, maisha ya kawaida.
 1. Mistari ya 1-5 inazungumzia kuhusu manabii wa uongo (k.v. 18:20).
 2. Mistari ya 6-11 inazungumzia kuhusu wanafamilia wanaojaribu kuivuta familia nyingine kuingia kwenye ibada ya sanamu.
 3. Mistari ya 12-18 inazungumzia kuhusu jamii nzima inayokumbatia ibada ya sanamu (k.v. 29:18).
- C. Panaonekana kuwepo na utofauti kwenye Agano la Kale kati ya nabii na mwotaji wa ndoto. Maono yanaonwa na mtu ambaye hajalala na mwenye kuzidhibiti fahamu zake. Ezekiel, akiwa katika Mto Kebari, ni mfano wa hayo maono. Daniel pia ni mfano wa mtu anayetafasiri ndoto. Yote haya ni maono toka kwa Mungu. Namna mojawapo ya kawaida kwa ajili ya Mungu ili kuzungumza na watu siku za leo sio kupitia katika maono na ndoto, na bado anauwezo wa kufanya mojawapo.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 13:1-5

¹Kukizuka katikati yako nabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ²ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, Na tuiquate miungu mingine usiyojua, tuitumikie hiyo; ³wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa Bwana, Mungu wenu, yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda Bwana, Mungu wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. ⁴Tembeeni kwa kumfuata Bwana, Mungu wenu; mcheni na kushika maagizo yake na kuisikia sauti yake, nanyi mtumikieni na kushikamana naye. ⁵Na yule nabii, au yule mwotaji wa ndoto, na auawe, kwa kuwa amesema yaliyopotoka juu ya Bwana, Mungu wenu, aliyewatoa katika nchi ya Misri, akakukomboza katika nyumba ya utumwa, apate yule mtu kukupotoa katika njia aliyokuamuru Bwana, Mungu wako, uiendee. Ndivyo utakavyouondoa uovu uotoke katikati yako.

13:1 Sio watu wote wanaodai kuongea na Mungu wanaweza kuaminiwa. Lazima tuwajaribu (k.v. Kumb. 18:20-22; Mathayo 7; 24:24; I Yohana 4:1-6; II Pet. 3:15-16).

13:1,3 “Nabii” Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: UNABII WA AGANO LA KALE

UTANGULIZI

A. Maelezo ya Ufunguzi

1. Jamii ya waaminio haikubaliani kuhusu namna ya kufasiriri unabii. Baadhi ya kweli zingine zimehimarishwa kama sehemu ya imani halisi kwa karne zote, lakini si hii.
2. Kuna hatua kadhaa za unabii wa Agano la Kale zilizoielezwa vizuri
 - a. Kabla ya utawala wa wafalme na malkia
 - (1) Watu binafsi walioitwa manabii
 - (a) Ibrahimu - Mwa. 20:7
 - (b) Musa – Hes. 12:6-8; Kumb. 18:15; 34:10
 - (c) Haruni – Kut. 7:1 (msemaji wa Musa)
 - (d) Miriamu – Kut. 15:20
 - (e) Medadi na Eldadi Hes. 11:24-30
 - (f) Debora – Amu. 4:4
 - (g) Wasiotajwa – Amu. 6:7-10
 - (h) Samweli – 1 Sam. 3:20
 - (2) marejeleo kuhusu manabii kama kundi – Kumb. 13:1-5; 18:20-22
 - (3) Kundi la manabii au waongozaji 1 Sam. 10:5-13; 19:20; 1 Fal. 20:35, 41; 22:6, 10-13; 2 Fal. 2:3, 7; 4:1, 38; 5:22; 6:1, nk.
 - (4) Masihi aliyetwa nabii – Kumb. 18:15-18
 - b. Utawala wa kifalme usioandikwa (ulijishughulisha na mfalme):
 - (1) Gadi – 1 Sam. 22:5; 2 Sam:24:11; Nya. 29:29
 - (2) Nathani – 2 Sam. 7:2; 12:25; 1 Fal. 1:22
 - (3) Ahija – 1 Fal. 11:29
 - (4) Yehu – 1 Fal. 16:1, 7, 12
 - (5) wasiotajwa 1 Fal. 18:4, 13; 20:13, 22
 - (6) Eliya – 1 Fal. 18-2 Fal. 2
 - (7) Mika – 1 Fal. 22
 - (8) Elisha- 2 Fal. 2:9, 12-13
 - c. Manabii wa sasa walioandikwa (wanatumikia taifa na mfalme): Isaya – Malaki (isipokuwa Danieli)

B. Maneno ya Kibiblia.

1. *Ro'eh* = "muonaji" (BDB 906, KB 1157), 1 Sam. 9:9 Marejereo yenyewe yanaonesha mabadiliko kuelekea neno nabi *Ro'eh* linatokana na neno la jumla "kuona." Mtu huyu alielewa njia za Mungu na mipango na alikuwa akiona kuhusu kuelewa kusudio la mapenzi ya Mungu kwa jambo fulani.
2. *Hozeh* = "muonaji" (BDB 302, KB 3011), 2 Sam 24:11. Kimsingi ni neno sawa na *Ro'eh*. Linatokana na neno adimu "kuona." Muundo uliobadilishwa unatumika mara nyingi sana kurejea juu ya linatumika kuwarejelea manabii. (yaani "kutazama").
3. *Nabi'* = "nabii" (BDB 611, KB 661), sawa na KITENZI cha Lugha ya Mesopotamia ya Kale *Nabu* = "kuita" na Kiarabu *Naba'a* = "kutangaza". Hili ni neno la kawaida sana katika Agano la Kale kumaanisha nabii. Limetumika zaidi ya mara 300. Asili na maana yake halisi haifahamiki vizuri lakini "kuita" kwa sasa inaonekana ndiyo sahihi. Bila shaka uelewa wa uhakika unatokana na maelezo ya Musa kuhusu YHWH na uhusiano wa Musa na Farao kupitia kwa Aruni (kama vile Kut. 4:10-16; 7:1 Kumb. 5:5). Nabii ni yule mtu ambaye huzungumza na Mungu kwa ajili ya watu Wake (Amosi 3:8; Yer. 1:7, 17; Ezek. 3:4).
4. Maneno yote matatu yanatumika katika huduma ya nabii katika 1Nya. 29:29; Samweli- *Ro'eh*; Nathani – *Nabi'* na Gadi - *Hozeh*.
5. Fungu '*ish ha – 'elohim*, "Mwana wa Mungu," pia ni neno pana kwa mtu yule anayezungumza na Mungu. Limetumika takribani mara 76 katika Agano la Kale kwa maana ya "nabii."
6. Neno "nabii" ni Kiyunani kwa asili yake. Linatokana: (1) *pro* = "kabla" au "kwa ajili ya" na (2) *phemi* = "kuzungumza"

MAANA YA UNABII

- A. Neno "nabii" lina elimu-maana pana katika Kiebrania kuliko kiingereza vitabu vya kihistoria vya Yoshua mpaka wafalme (isipokuwa Ruthu) imeandikwa na Wayahudi kama "manabii wa mwanzo" wote wawili Ibrahimu (Mwa. 20:7 Zab. 105:15) na Musa (Kumb. 18:18) wametambuliwa kama manabii (pia Miriamu, Kut. 15:20). Kwa hiyo kuwa makini na maelezo ya kiingereza yanayobashiri
- B. "kutoa unabii kwaweza kuelezewa kama kuelewa historia inayokubaliana na maana ya maneno yanayohusika ki-Uungu, yenye kusudi la ki-Uungu, na ushiriki wa ki-Uungu." *Interpreter's Dictionary of the Bible*, vol. 3, ukurasa wa 896
- C. Nabii sio mwana falsafa wala mwana theolojia, bali ni mtu mpatanishi wa agano ambaye huchukua neno la Mungu kulipeleka kwa watu wake ili kuyatengeneza maisha yao ya mbele kwa kurekebisha maisha waliyonayo sasa" Nabii na unabii, *Encyclopedia judaica* juzuu 13 ukurasa wa 1152.

KUSUDI LA UNABII

- A. Unabii ni njia ya Mungu ya kuongea na watu wake, kuwapa mwongozo katika mipango yao mipya na matumaini katika uhibitaji wake juu ya maisha yao na matukio ya ulimwengu. Ujumbe wao kimsingi ulikuwa wa kiushirikiano. Ulikusudia kukemea, kuhamasisha, kusababisha imani na toba na kuwajulisha watu wa Mungu kuhusu Mungu mwenyewe na mipango yake. Kuwafanya watu wa Mungu kuwa waaminifu kwenye maagano ya Mungu. Kwa hili yapaswa kuongezewa kuwa daima inatumika kubainisha wazi uchaguzi wa Mungu na msemaji wake (Kumb. 13:1-3; 18:20; 22). Hii ingalirejea juu ya Masihi.
- B. Daima nabii anachukulia mgogoro wa kihistoria na kithiolojia nyakati zake na kuuendeleza katika muundo wa siku za kiamama. mtazamo huu wa siku za mwisho wa historia si wa kawaida katika Israeli na maaana yake ya uteuzi wa kiungu na ahadi za maagano.
- C. Ofisi ya nabii inaonekana kuweka usawa (Yer.18:18) na kujitwalia ofisi ya kuhani mkuu kama njia ya kujua mapenzi ya Mungu. Urimu na Thumamu wanazidi kuingia katika ujumbe wa mdomo toka kwa mnenaji wa Mungu. Ofisi ya nabii inaonekana pia kutoweka katika Israeli baada ya malaki. Haionekani tena mpaka miaka 400 baadaye ikisemwa na Yohana mbatizaji. Haijulikani ni kwa namna gani kipawa cha Agano Jipya cha "unabii" kinahusishwa na agano la kale. Manabii wa Agano Jipya (Matendo 11:27-28; 13:1; 15:32; 1 Kor. 12:10; 28-29; 14:29, 32,37; Efe. 4:11) sio wadhilishaji wa ufunuo mpya au maandiko, bali wanenaji wa mambo yajayo ya mapenzi ya Mungu katika hali ya Agano.

- D. Unabii sio hasa utabiri kiasili. Utabiri ni njia mojawapo ya kuthibitisha ofisi yake na ujumbe wake, lakini itambuliwe kuwa “chini ya 2% ya unabii wa Agano la Kale ni wa ki-Umasihi. Chini ya 5% hasa inaelezea enzi mpya ya patano. “chini ya 1% inahusu matukio ambayo bado hayajatokea.”(Fee and Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa wa 166).
- E. Manabii wanamwakilisha Mungu kwa watu, wakati kuhani anawakilisha watu kwa Mungu. Huu ni usemi wa jumla. Kulikuwepo na wenye dharura kama Habakuki, ambaye alijitetea kwa Mungu.
- F. Sababu inayosababisha kutowaelewa manabii ni kwamba hatujui ni vipi vitabu vyao viliandikwa. Havina mfuatano mzuri. Vinaonekana kuwa na mrejea lakini sio mara zote kile mtu angekitarajia. Mara zote havina muundo wa kihistoria ulioko wazi, muda muafaka, au mgawanyo wa wazi kati ya mafanikio. Vitabu hivi ni vigumu:
 1. Kusoma katika mkao mmoja
 2. Kuchambua ki mada au mada kwa mada
 3. Kutambua kiini cha ukweli au kusudio la manabii katika kile kipindi.

TABIA ZA UNABII

- A. Katika Agano la Kale kunaonekana kuwepo na mwendelezo wa dhana ya “Nabii” na “unabii.” katika Israeli ya mwanzo kulianzishwa ushirika wa manabii, ukiongozwa na kiongozi mwenye haiba kubwa kama Eliya au Elisha. Wakati mwingine kifungu “wana wa manabii” kilitumika kumaanisha kundi hili (2 Falme 2). manabii walikuwa wanaainishwa na upeo wa hisia (1 Sam. 10:10-13; 19: 18-24).
- B. Hata hivyo kipindi hiki kilipita haraka sana kuingia katika kipindi cha nabii mmoja mmoja. palikuwepo na wale manabii (wa ukweli na wa uongo) waliotambuliwa na mfalme na waliishi katika nyumba ya mfalme (Gad na, Nathan). Pia, palikuwa na wale waliokuwa wanajitegemea, wakati mwingine hawakuhusiana na jamii ya watu wa Israel wenye hadhi (Amosi). Wakijumuisha wote wanaume na wanawake (2 Fal. 22:14)
- C. Nabii daima alikuwa muonaji wa nyakati zijazo, kwa sharti la mwitikio wa mtu mmoja. Daima wajibu wa nabii ulikuwa kuweka wazi mpango wa Mungu kwa watu wote kuhusu uumbaji wake usioathiriwa na mwitikio wa Mwanadamu. Mpango wa kiamu kwa watu wote ni wa kipekee kati ya manabii wa kake wa Mashariki. Utabiri na itii wa agano ni pacha ya ujumbe wa kinabii (kama vile Fee na Stuart, uk. 150). Hii inaonesha kuwa manabii kimsingi walikuwa na mtazamo wa pamoja. Kwa kawaida walihudumia taifa japo sio taifa pekee bali na mengine.
- D. Mambo mengi ya kinabii yaliwasilishwa kwa mdomo. Baadaye yaliwekwa pamoja kwa namna ya dhamira, mfuatano, au mpangilio mwingine wa fasihi za Mashariki ambazo zimepotea kwetu. Kwa sababu ilikuwa kwa njia za simulizi hazikupangiliwa kama maandiko yaliyoandikwa. Hii inasababisha kuwepo na ugumu wa kukisoma kitabu chote moja kwa moja na kuwepo ugumu wa kuelewa pasipo muundo maalumu wa kihistoria.
- E. Manabii wanatumia mipangilio kadhaa kufikisha ujumbe wao.
 1. Mazingira ya kimahakama – Mungu anawapeleka watu wake katika mahakama, daima ni suala la talaka ambapo YHWH anamkataa mke wake (Israeli) kwa kutokuwa mwaminifu (Hosea 4; mica 6).
 2. Maombolezo ya msiba –kipimo halisi cha aina ya ujumbe huu na tabia yake ni “huzuni” iliyoondolewa kama kitendo maalumu(Isaya 5; Habakuki2).
 3. Tamko la Agano la Baraka- asili ya kimasharti ya agano limesisitizwa na madhara yake yote, hasi na chanya, yametajwa kwa ajili ya siku za mbeleni (Kumb 27:28).

MIONGOZO INAYOSAIDIA KATIKA KUTAFSIRI UNABII

- A. Tafuta kusudio la awali la nabii (mwandishi) kwa kutambua muundo wa kihistoria wa kitabu na uelewa wa kifasihi wa kila kitabu. Bila shaka kitahusu Waisraeli kuvunja agano la Musa kwa namna Fulani.
- B. Soma na kutafsiri unabii wote, na sio sehemu tu, elezea kwa mhutasari kama ulivyo ujumbe. Tazama namna unavyohusiana na habari iliyopo. Jaribu kuelezea kwa muhtasari kitabu chote.
- C. Chukua tafasili ya fasihi ya habari hadi kitu fulani katika andiko lenyewe likupeleke kwenye matumizi ya kitamathari; kasha weka lugha ya kitamathari katika nadharia.
- D. Chambua vitendo vyenye alama katika uwazi wa mpangilio wa kihistoria na aya zinazofanana. Kumbuka

hili kuwa fasihi za mashariki ya mbali sio fasihi za magharibi au zile za kisasa.

- E. Zingatia utabiri wako kwa makini.
1. Je! unajitenga na siku zile za mwandishi?
 2. Je! ni wapi baadaye unatekelezwa katika historia ya Israeli?
 3. Je! bado ni matukio yajayo?
 4. Unanahitajika kukamilishwa sasa au siku zijazo?
 5. Ruhusu waandishi wa biblia, sio wa sasa, kuongoza majibu yako.
- F. Jambo maalumu
1. Je! utabiri umewezeshwa na mwitikio wenye masharti?
 2. Je! ni kwa yupi unabii huu umeelekezwa (na kwa nini?)
 3. Kuna uwezekano, wa kibiblia au kihistoria, kwa utekelezwaji wa pamoja?
 4. Waandishi wa Agano Jipya, wakiwa chini ya uvuvio, walikuwa na uwezo kumuona masihi sehemu mbalimbali katika Agano la Kale ambazo hazikudhihilishwa kwetu. hili halina uhakika, wanaonekana kutumia mfumo wa kugawanya vitu. Kwa vile sisi hatukuvuwiwa bora tuwaachie wenyewe.

VITABU VITAKAVYOKUSAIDIA

- A. *A Guide to Biblical Prophecy* cha Carl E. Amending and W. ward Basque
- B. *How to read the Bible for All its Worth* by Gordon Fee and Douglas Stuart
- C. *My servants the Prophets* cha Edward J. Young
- D. *Plowshares and Pluning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Profecy and Apocalyptic* cha D. Brent Sandy
- E. *New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, vol. 4, pp. 1067-1078
- F. *The Language and Imagery of the Bible* cha G.B Caird



NASB, NKJV,

NJB "mwotaji wa ndoto"

NRSV "wale wanaobashiri ndoto"

TEV "mtafasiri wa ndoto"

JPSOA "mtabiri wa ndoto"

Hili neno ni muundo wa KITENZI (BDB 321, *Qa/ KAULI TENDAJI YA WAKATI ENDELEVU*) na NOMINO HALI YA UWINGI (BDB 321). Ubashiri (k.v. 18:14-15) au kujaribu kuelewa, kutambua kabla, au kuathiri mapenzi ya mungu/miungu kilikuwa ni kitu cha kawaida huko Mashariki ya Karibu ya Mbali. Palikuwepo na namna nyingi za ubashiri:

1. Kwa ndoto/kupagawa (hali ya kiufahamu)
2. Bahati na sibu, fimbo (vitu vilivyotengenezwa na mwanadamu)
3. Mawingu/dhoruba/ukame (hali ya hewa)
4. ndege (aina ya mruko na aina ya ndege)
5. Ishara katika anga (kuonekana kwa vimondo, kupatwa kwa jua na mwezi, n.k)
6. Hali ya ini la kondoo (na wanyama wengine wanaotolewa kidhabihu)

13:1, 2 "ishara" inavyoonekana kwangu ni kuwa neno "ishara" (BDB 16) katika biblia linatumika pindi unapooonea kuhusu kitu kingine ambacho kilitabiriwa na hatimaye kutimia. Hili neno linatumika kwa maana mbalimbali tofauti kwenye Kitabu cha Kumbukumbu la Torati:

1. Miujiza/mapigo ambayo YHWH aliyafanya kupitia Musa huko Misri kumlazimisha Farao awaachie wana wa Israeli waondoke, 4:34; 6:22; 7:18-19; 11:3; 26:8; 29:2-3; 34:11.
2. Vyombo vidogo vidogo vilivyokuwa na maneno ya maandiko, 6:8; 11:8
 - a. Mkono wa kushoto
 - b. Paji la uso
 - c. Miimo ya milango

3. Miujiza/ubashiri wa manabii wa uongo kuwapotosha Israel wasimwabudu YHWH, 13:1-2.
4. Hukumu ya YHWH juu ya Israel iliyokaidi itatenda kazi kama onyo la baadaye kwa vizazi vya Waisraeli, 28:46.

☞“**au maajabu**” Neno “maajabu” (BDB 65) linaonekana kurejelea kwenye matendo ya miujiza yaliyofanyika mbele ya mashuhuda. Mara nyingi linatumika kwenye baiskeli ya watu wawili kukiwa na “ishara.”

13:2 “**ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia**” Miujiza haiji yenyewe toka kwa Mungu (k.v. Kut. 7:11,22; Mt. 24:24; II Thess. 2:9). Hili pia ni kweli juu ya ubashiri ulio sahihi (k.v. 18:22). Kama “nabii” wa Kumb. 18:18-19 anatabiri mbele ujio wa Masihi, hivyo huyu nabii wa uongo anamtabiri mpinga Kristo ajae (k.v. 18:20). “uongo” unadhihirishwa kama:

1. Neno lisilo la kweli
2. Neno lisilo la YHWH

☞“**Na tuifuate miungu mingine..... tuitumikie**” Hivi VITENZI viwili vinaandika tofauti iliyopo toka ibada maalum ya YHWH:

1. “tuifuate” - BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI YENYE HALI YA KUSIHI. Hili ni onyo lenye kujirudia, k.v. 6:14; 8:19; 11:28; 13:2,6,13; 28:14; 29:18,26
2. “tuitumikie” - BDB 712, KB 773, *Hophal* KAULI ISIO TIMILIFU, ikitumika kwa maana ya KUSIHI. Hili pia ni onyo lenye kujirudia, k.v. 5:9; 7:4,16; 8:19; 11:16; 13:2,6,13; 17:3; 28:14,36,64; 29:18,26; 30:17; 31:20. Kifungu cha maneno “tuitafute miungu mingine” ni onyo lenye kujirudia, sio tu katika kitabu cha
3. Kumbukumbu la Torati, bali hata katika kitabu cha Yeremia.

☞“**miungu (mingine msioijua)**” Suala zima hapa sio uwezo wa kufanya ishara, bali ni ibada maalum ya YHWH. Tazama Mada Maalum : kujua katika 4:35.

13:3 “**usiyasikize maneno ya nabii yule**” KITENZI (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) ni neno la imani ya Kiyahudi lenye kujirudia mara kwa mara (*shema*), linalomaanisha “kusikia kwa ajili ya kutenda.” Tazama maelezo katika 4:1.

☞“**kwa kuwa Bwana, Mungu wenu, yuawajaribu**” KITENZI (BDB 650, KB 702, *Piel* KAULI ENDELEVU) kinaelezea ukweli kwamba Mungu huwaweka wanadamu katika hali ya kujaribiwa au ili kujua na kuimarisha imani/utii ndani yake (k.v. Mwa. 22:1-12; Kut. 15:25; 16:4; 20:20; Kumb. 8:2,16; Amu. 2:22; 3:1,4; II Nya. 32:31). Hata uwepo wa manabii wa uongo kati ya watu ni njia ya Kiungu ya kutenganisha waamini wa kweli toka kwa waamini wa vipindi. Mungu hutumia uovu kwa makusudi yake Mwenyewe (k.v. Mwanzo 3)!

☞“**kwa moyo wako wote na roho yako yote**” tazama maelezo katika 4:29. Hii ni stiari kwa ajili ya moyo kamili wa ibada. Israeli mara kadhaa imeelezewa kumpenda YHWH kwa moyo kamili wa ibada (k.v. 6:5; 7:9; 10:12; 11:1,13,22; 13:3; 19:9; 30:6,16,20).

13:4 Huu mstari unajumuisha mfuatano wa *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, ambao unatoa mwongozo kwa ajili ya ibada maalum ya YHWH:

1. “fuata,” BDB 229, KB 246, k.v. 8:6
2. “mcheni,” BDB 431, KB 432
3. “kushika,” BDB 1036, KB 1581, k.v. 5:29; 6:2
4. “kuisikia,” BDB 1033, KB 1570
5. “tumikieni,” BDB 712, KB 773
6. “shikamana,” BDB 179, KB 209

Mstari huu unafanana na 6:13 na 10:20.

13:5 “Na yule nabii, au yule mwotaji wa ndoto, na auawe” YHWH anahusika na uchafuzi wa ibada yake kama ambavyo Kumbukumbu la Torati 12 linavyoonyesha kwa wazi. Ikiwa ibada ya YHWH imekwisha kuchafuliwa hapa, Agano Jipya lisingekuwa kweli. Mungu alihofu kuwa watu wake wapate kutenda ibada zao katika namna ile ile aliyo waamuru (k.v. 4:2; 12:32). Kama haikuwa ibada safi, madhara yake ni kifo, ikiwajumuisha Wakanaani na manabii wa uongo ndani ya Israel (k.v. 13:5,9,15). Upotofu ulifanyika kwa ajili ya watu binafsi ndani ya jamii (k.v. 4:19; 13:5,10).

☐ **“akakukomboa”** Neno hili (BDB 804, KB 911, *Qal* KAULI ENDELEVU) ni namna ya kuelezea gharama iliyolipwa kumkomboa mtu toka utumwani au kifungoni. Tazama Mada Maalum katika 7:8.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 13:6-11

⁶Atakapokushawishi kwa siri ndugu yako, mwana wa mamaako, au mwana wako, au binti yako, au mke wa kifuani mwako, au rafiki yako aliye kama moyo wako, akikuambia, Twende tukaabudu miungu mingine usiyojua wewe wala baba zako; ⁷katika miungu ya mataifa yaliyo kando-kando yenu karibu nawe au mbali nawe, tokea ncha moja ya dunia hata ncha ya pili ya dunia; ⁸usimkubalie wala usimsikize; wala jicho lako lisimwonee huruma, wala usimwache, wala usimfiche; ⁹mwue kweli; mkono wako na uwe wa kwanza juu yake katika kumwua, na baadaye mikono ya watu wote. ¹⁰Nawe mtupie mawe hata afe; kwa kuwa alitaka kukupotoa na Bwana, Mungu wako aliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. ¹¹Na Israeli wote watasikia na kuogopa, wasifanye tena uovu mfano wa huo katikati yako.

13:6, 8 “ndugu yako..... au mwana wako.... au binti yako....au mke wa kifuani mwako..... au rafiki yako” Ikiwa hata mtu alikuwa mpendwa wa karibu sana nawe, ndugu, au rafiki akijaribu kukupotoa kuabudu mungu mwingine, basi Mwisraeli mwaminifu awarejeshe ili jamii iwarushie mawe (k.v. mistari ya 9-10). Hiki ndicho kitovu cha uwajibikaji wa agano binafsi. Haya ni maelezo muhimu ndani ya muktadha wa muundo wa kitamaduni ambapo familia ilikuwa ni ya muhimu (k.v. Mt. 10:34-39; Luka 14:25-27).

13:6 “Twende tukaabudu miungu mingine ” VITENZI hivi vyote ni vya *Qal* HALI YA KUSIHI:

1. “twende” - BDB 229, KB 246
2. “tukaabudu” - BDB 712, KB 773

Vinatumika kama stiari ya pamoja kwa ajili ya kuabudu.

13:7 “miungu ya mataifa yaliyo kando-kando yenu karibu nawe au mbali nawe, tokea ncha moja ya dunia hata ncha ya pili ya dunia ” Hili andiko lina tafasiri mbalimbali zenye kuwezekana. Kifungu chaweza kurejelea kwa:

1. Miungu ya Wakanaani, ikiwa ni kaskazini au kusini mwa Kaanani (“dunia” = “nchi”)
2. Miungu ya kigeni, ikiwa ni Mesopotamia au Palestina (“karibu yako au mbali nawe”)
3. Onyo pekee dhidi ya ibada ya kuiabudu miungu toka kwenye nyota, ikiwa ni jua, mwezi, nyota, sayari,
4. vimondo, kupatwa kwa mwezi au jua n.k (vitu vinavyochwea na kuzama)

13:8 Huu mstari unaorodhesha (mfuatano wa *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU kanushi) namna mfuasi wa kweli wa YHWH anavyolazimika kumtendea mfuasi wa miungu mingine:

1. Usimkubalie - BDB 2, KB 3
2. usimsikize - BDB 1033, KB 1570
3. wala jicho lako lisimwonee huruma - BDB 299, KB 298, k.v. 7:2,16
4. wala usimwache- BDB 328, KB 328, k.v. I Sam. 15:3
5. wala usimfiche - BDB 491, KB 487 (kiuhalisia ni “kumfunika”) ni maoni mafupi tu juu ya #3.

Muundo huu ni nahau kwa ajili ya kifungu cha maneno “usiiruhusu mihemuko yako ya kibinadamu iathiri matendo yako yanayohitajika na Mungu.” Unapatikana mara kadhaa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati 7:16; 13:8; 19:13,21; 25:12 (k.v. NIDOTTE, vol. 2, uk. 50).

13:9 “kweli; mkono wako na uwe wa kwanza juu yake katika kumwua ” MAANDISHI YA KIMASORETI hayana neno “kumpiga jiwe” katika mstari huu, ingawa kwamba ndiyo namna ya kifo kilichodokeza kutendeka (k.v. mst.

10). ANDIKO LA KIMASORETI (MT) lina *Qal* KITENZIJINA HALISI na *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU ya KITENZI“kuua” BDB 246, KB 255 (yaani., “mwue kweli”), lenye kumaanisha msisitizo. Mikono ya wale mashahidi na iwe ya kwanza kumpiga kwa mawe (kama vile mst. 10; 17:7). Ikiwa mtu atamnenea uongo mshitakiwa, hivyo atakuwa ametenda mauaji ya kimakusudi (k.v. 5:20).

13:10 “mtupie mawe hata afe ” ANDIKO LA KIMASORETI (MT) lina KITENZI “mtupie mawe hata kufa” (BDB 709, KB 768, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU) na neno kwa ajili ya “kumtupia mawe” (BDB 6), ambalo kiuhalisia lingekuwa“kumpiga kwa mawe.” Kutupiwa mawe ilikuwa ni adhabu nzito ambayo ilitendwa na jamii nzima ya kimaagano (k.v. Law. 20:2,27; 24:13-23; Hes. 15:32-36; Kumb. 13:10; 21:21; Yosh 7:22-26). Hili sio neno la kwaida litumiwalo kwa ajili ya adhabu ya kifo. Hili neno linazungumzia uharaka wa kutokomeza uovu (k.v. Kut. 32:27; Law. 20:15,16; Hes. 25:5; Kumb. 13:10; Ezek. 9:6). Watu walipigwa mawe na jamii kwa sababu ya:

1. kuiabudu sanamu, Law. 20:2-5 (pia yumkini 6-8); Kumb. 13:1-5; 17:2-7
2. kukufuru, Law. 24:10-23; I Fal 11-14; Luka 4:29; Mdo. 7:58 (yote yanalenga Kut. 22:28); pia angalia Yohana 8:59; 10:31; 11:8
3. Ukaidi wa kutotii wazazi, Kumb. 21:18-21 (yumkini Law. 20:9)
4. Kutokuwa mwaminifu kwenye ndoa, Kumb. 22:22,23-27 (yumkini Law. 20:10-16)
5. Kufanya uhaini (ikijulikana kama kumwasi YHWH), Yoshua 7



NASB “kukupotosha”

NKJV “kukupotoa”

NRSV “akijaribu kukugeza”

TEV “akijaribu kukupotosha”

NJB “akijaribu kukupotosha”

Hiki ni KITENZI(BDB 623, KB 673, *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO) chenye kumaanisha “kukuondoa.” Hawa ni manabii wa uongo (mst. 1) na wakionekana kuwa ndugu wa agano (mst. 6) wakijaribu kuwaondoa wapendwa toka kwa YHWH kwa kuwaelekeza kwa miungu wengine. KITENZI(k.v. mistari 5,12; 4:19; II Fal. 17:21) kinafanana na neno “kushawishi” (BDB 694, KB 749, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU) ya mst. 6. Inafurahisha kwamba mzizi ule ule wa neno la Kiebrania unatumika kuelezea safari ya kutoka utumwani Misri (yaani ., kutawanyika).

13:11 kuna wengi walihusika kwenye adhabu kuliko kuadhibiwa. Na mtu Yule aliyetenda uasi aliweza kupata madhara makubwa (yaani., kupigwa mawe),lakini pia kuna zuio kwa wale wote washuhudia au kusikia kuhusu suala la adhabu (k.v. 17:12-13; 19:15-21; 21:18-21; Rum. 13:4).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA):13:12-18

¹² Ukisikia yasemwa habari ya miji yako mmojawapo, akupayo Bwana, Mungu wako, ukae humo, ukiambiwa, ¹³ Kumetoka katikati yako mabaradhuli kadha wa kadha, wamewapotoa wenyeji wa mji wao, wakisema, Twendeni tukaabudu miungu mingine msiojua; ¹⁴ ndipo nawe uulize na kutafuta, ukiuliza kwa bidii; nawe angalia, ikiwa kweli, na jambo lile halina shaka, kwamba machukizo mfano wa haya yafanyika katikati yako; ¹⁵ hakika yako uwapige wenyeji wa mji ule kwa makali ya upanga, kwa kuwaangamiza kabisa, pamoja na vitu vyote vilivyomo, na wanyama walio humo, kwa makali ya upanga. ¹⁶Na nyara zake zote uzikusanyie katikati ya njia yake; na mji uuteketeze kwa moto, na nyara zake zote, kuwe sadaka kamili ya kuteketezwa kwa Bwana, Mungu wako; nao utakuwa magofu milele; usijengwe tena. ¹⁷ Kisishikamane na mkono wako kitu cho chote katika kitu kilichoharimishwa; ili ageuke Bwana na ukali wa hasira zake akurehemu, akuonee huruma, na kukufanya kuwa wengi, kama alivyowaapia baba zako; ¹⁸utakaposikiza sauti ya Bwana, Mungu wako kwa kushika maagizo yake yote nikuagizayo leo, ufanye yaliyoelekea machoni pa Bwana, Mungu wako.

13:13 “mabaradhuri” Kiuhalisia hili linamaanisha “wana wa *Beliali*” (BDB 116). Neno la Kiebrania linamaanisha “baradhuri” au “wasio na faida” (k.v. Amu. 19:22; 20:13; I Sam. 10:27; 30:22; I Fal. 21:10,13; Mit. 6:12). Kwenye kipindi cha Agano Jipya, neno *Beliali* likajakuwa ni kisawe cha neno shetani (k.v. II Kor. 6:15).

☐“wamewapotoa” Tazama maelezo katika mst. 10.

13:14 Mstari huu unaorodhesha mfuatano wa VITENZI vyenye kuuliza (vyote ni *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU):

1. NASB “uliza”
NKJV, NRSV “tafuta”
NJB “nawe angalia”
KITENZI ni BDB 205, KB 233, kikimaanisha “uliza,” k.v. 17:4,9; 19:18
2. NASB, NKJV “nawe angalia”
NJB “ikiwa ni kweli”
KITENZI ni BDB 350, KB 347, kikimaanisha “angalia,” k.v. Zab. 139:1,23; Mith. 18:17
3. NASB “uliza kwa undani”
NKJV “uliza kwa bidii”
NJB “uliza kimakini”

Huu ni muunganiko wa BDB 981, KB 1371, *Qal* KAULI ILIO TIMILIFU, neno“uliza” na BDB 405, KB 408, *Hiphil* KITENZIJINA HALISI, neno“kwa bidii,” k.v. 17:4; 19:8

13:15 “hakika. . .kwa kuwaangamiza” Kifungu hiki cha maneno “kwa kuwaangamiza” (BDB 355) kinamaanisha “moja kwa moja kuwatoa kwa Mungu kwa ajili ya kuwaangamiza.” Tazama maelezo kamili katika 3:6. Madhara ya aina ile ile yaliyopimiwa wapagani yatawapata Wayahudi ikiwa wataiabudu miungu wengine.

13:16

NASB “utakuwa magofu milele”
NKJV “utakuwa rundo milele”
NRSV “utabaki kuwa magofu milele”
TEV “lazima ubaki kuwa magofu milele”
NJB “lazima ubaki chini ya laana ya maangamizi”

Hiki kifungu cha mwisho kilikuwa ni nahau ya Kiebrania kuhusiana na laana (mf., Yosh. 8:28; Yer. 49:2). Kwa ajili ya dhana ya neno “milele” tazama Mada Maalum katika 4:40.

13:16 “uuteketeze kwa moto” Hii ni dhana ya Kiebrania ya kuwakabidhi mateka wote wa “vita takatifu” kwake (BDB 356). Kitu kilichofanyika hapa (na mst. 17) kinatokea katika Yohua 6-7!

13:17-18 Tazama mtiririko wa mawazo:

1. Wenye kuabudu ibada ya sanamu walistahili hukumu (yaani., vita takatifu, wote waliokuwa wakipumua, waliokufa), mistari ya 12-15.
2. mateka wote wa mji walitolewa kwa YHWH kama sadaka ya kuteketezwa (yaani., kwenye vita takatifu, vitu vyote vya thamani vilitolewa kwa YHWH), mistari ya 16-17
3. utii huleta baraka, mistari ya 17-18:
 - a. aliighaili hasira yake kali
 - b. huonyesha huruma, k.v. 30:3
 - c. ana rehema (mzizi ule ule kama hapo juu, BDB 933)
 - d. huleta utele
 - e. hutimiza kiapo kwa mababa
4. Baraka ni razima kwa wenye utii, mst. 18

☐“ufanye yaliyoelekea machoni pa Bwana Mungu wako” Hiki kifungu kinajitokeza mara kadhaa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (k.v. 6:18; 12:28; 13:18). Pia kinajitokeza katika I Fal. 11:38; 14:8;15:11; 22:43; II Fal. 12:3. YHWH ni kipimo cha utu na haki ambapo yote huhukumiwa. Tazama Mada Maalum: Haki katika 1:16.

MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozowa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini sura hii ni kali kwa utendaji wake wa imani zingine?
2. Je! sura hii yawezakuwa ni msingi wa yale tuyafanyayo kwa imani zingine katika siku zetu za leo?
3. Unamtambua mtu anayenena uongo kwa ajili ya Mungu? Vipi kuhusu miujiza?
4. Elezea dhana ya Agano la Kale kuhusu ushirika (yaani. Mmoja anaathiri wote), ambao hujibu wingi wa maswali kuhusu Agano Jipya.

KUMBUKUMBU LA TORATI 14

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Kuomboleza kusiko sahihi	Mtindo wa maisha ya mtu	Matendo yanayokatanzwa ya	Dhidi ya tendo la ibada
14:1-2	Mtakatifu	kuomboleza	ya miungu mingine
Nyama najisi na isiyo	14:1-2	14:1-2	14:1-2
Najisi		wanyama najisi na wasio	Wanyama wasio najisi na
14:3-8	14:3-8	najisi	walio najisi
14:9-10	14:9-10	14:3-8	14:3-8
14:11-20	14:11-20	14:9-10	14:9-10
		14:11-18	14:11-20
		14:19-20	
14:21	14:21a	14:21a	14:21a
	14:21b	14:21b	14:21b
Kanuni za Fungu la Kumi		Sheria ya Fungu la Kumi	Fungu la Kumi la mwisho
14:22-27	14:22-27	14:22-26	wa Mwaka
		14:27-29	14:22-23
			14:24-27
			Fungu la Kumi la mwaka
14:2-29	14:28-29		wa tatu
			14:28-29

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Tazama uk. wa viii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika kiyaya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA 14:1-16:17

- A. Kumbu kumbu la Torati 14:1-2 ni ukiri wa mwanzo kwamba Israeli, ni watu wa kipekee wa YHWH (kama vile Kut.19:5-6), lazima waliishi hilo!
- B. Kumbu kumbu la Torati 14:3-16:17 ni muhtasari wa baadhi ya mahitaji makuu ya agano ya watu wa Mungu yaliyowekwa mbele katika Kutoka - Hesbau
 1. Vyakula vilivyo najisi na visivyo najisi 14:1-21 kiasili vinapatikana katika Mambo ya Walawi 11:1-23.
 2. Zaka katika 14:22-29 kiasili imetolewa katika Hes. 18:21-29.
 3. Kufutiwa madeni katika 15:1-11 kiasili imetolewa katika Law. 28:8-38.
 4. Kuachiliwa kwa watumwa wa Kiebrania katika 15:12-18 kiasili imetolewa katika Law. 25:38-55.
 5. Ukombozi wa wazaliwa wa kwanza 15:19-23 kiasili imetoka katika Kut. 13:1-16.

6. Karamu tatu za kila mwisho wa mwaka za hija katika 16:1-17 zimetolewa kiasili katika kitabu cha Law. 23:4-8 na pia katika Hes. 28:16-29:40.
(Ainicho kutoka *Old Testament Theology*, cha Paul R. House, ukur. 184)
7. Asili ya muhtasari wa Kumbukumbu la Torati inaonekana dhahiri. Mara kwa mara sheria zinabadilikakwa ajili ya mazingira mapya.
Lazima ielezewe tena kuwa watu wa leo hawajui namna gani, lini, au kwanini kuwepo na muundo wa vitabu hivi vya Agano la Kale.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:1-2

¹ Ninyi mmekuwa wana wa Bwana, Mungu wenu; msijitoje miili yenu, wala msifanye upaa katikati ya macho yenu kwa ajili ya aliyekufa. ² Kwa kuwa u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako, na Bwana amekuchagua kuwa watu wake hasa, kuliko mataifa yote yaliyo juu ya uso wa nchi.

14:1 “Ninyi mmekuwa wana wa Bwana”Tazama stiari za kifamili zitumikazo kama misamiati ya kiagano (kama vile 1:31;8:5; 32:5). Angalia Mada Maalum:Ubaba wa Mungu katika 8:5. Tazama majina matatu maalumu kwa ajili ya Waisraeli yanayotumika katika mistari ya 1-2.

☐ **“kujikata”**KITENZI ni BDB 151, KB 177, *Hithpoel* (aina nadra ya shina la *Hithpael*) KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU na mara nyingi kinapatikana katika maandiko ya neno “kufyeka” au “kukata.” Hili lilikuwa ni tendo la ibada la kipagani (aidha ili kuweza kuvuta miungu au kusababisha hisia za maombolezo kwa wafu, kama vile Law. 19:28; 21:5; I Wafalme 18:28; Yer. 16:6; 41:5; 47:5; 48:37).

MADA MAALUMU: IBADA KWA WALIO KATIKA HUZUNI

Waisraeli walieleza huzuni kwa mpendwa wao aliyefariki na toba binafsi, pamoja na makosa ya jinai yaliyofanyika kwa ujumla kwa njia kadhaa:

1. Kurarua mavazi, Mwa. 37:29,34; 44:13; Waamuzi. 11:35; 2 Sam. 1:11; 3:31; 1 Fal. 21:27; Ayubu 1:20
2. Kuvaa gunia, Mwa. 37:34; 2 Sam. 3:31; 1 Fal. 21:27; Yer. 48:37
3. Kuvua viatu, 2 Sam. 15:30; Isa. 20:3
4. Kuweka mikono kichwani, 2 Sam. 13:19; Yer. 2:37
5. Kuweka vumbi kichwani, Yos. 7:6; 1 Sam. 4:12; Neh. 9:1
6. Kuketi sakafuni, Omb. 2:10; Ezek. 26:16 (kulala chini, 2 Sam. 12:16); Isa. 47:1
7. Kupiga kifua, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26; Nah. 2:7
8. Omboleza, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26
9. Kata mwili, Kumb. 14:1; Yer. 16:6; 48:37
10. Kufunga, 2 Sam. 1:12; 12:16,21; 1 Fal. 21:27; 1 Nya. 10:12; Neh. 1:4
11. Kuimba na kusifu katika maombolezo, 2 Sam. 1:17; 3:31; 2 Nya. 35:25
12. Upara (nywele zilikatwa), Yer. 48:37
13. Kunyooa ndevu, Yer. 48:37
14. funika kichwa au uso, 2 Sam. 15:30; 19:4

Hizi zilikuwa ishara za nje kutokana na hisia za ndani

☐ **“msifanye upaa”**Hii (“kufanya upaa, BDB 901) pia inarejerea kwa ibada ya maombolezo ya mataifa jirani yalioizunguka (kama vile Yer. 16:6; 41:5; Ezek. 27:31; 44:20). Kwa kutofautisha (1) Makuhani wa Israeli hawakuruhusiwa kunyooa kabisa (kama vile Law. 21:5) na (2) Waisraeli hawakuruhusiwa hata kunyooa ndevu zao (kama vile Law. 19:27). Sheria nyingi za Israeli zilitolewa zikiwa katika hali ya kupingana na zile za Wakanaani!

☐ **“kwa ajili ya aliyekufa”**Ibada za maombolezo zinazoelezewa zinaunganishwa na:

1. kuabudu watu wa kale

2. kuabudu Baali (kufa [kipupwe] na kuinuka [masika] asili ya mungu wa Wakanaani)

14:2 “watu watakatifu” Dhana inahusiana na jukumu la Israeli la kumfunua YHWH na Masihi Wake (kama vile Kut.19:6;Kumb. 7:6). Angalia Mada Maalum katika 4:6.

Kumbu kumbu la Torati linatumia lugha ya kiagano, ambayo inaelezea uungu kama “BWANA Mungu wako” na watu Wake“watakatifu,” “waliochaguliwa,” “hazina maalum” (kama vile 4:20; 7:6; 14:2; 26:18; 28:9;29:12-13). Pia tazama Yeremia (kama vile 7:23; 11:4; 13:11; 24:7; 30:22; 31:1,33; 32:38). Na pia nani anaweza kusahau Hosea 1-3!

☐**“Bwana amekuchagua”KITENZI** (BDB 103, KB 119, *Qa/ KAULI YA WAKATI TIMILIFU*) kinatumika juu ya uchaguzi wa Mungu mwenye uweza:

1. Ibrahimu, Mwa. 12:1; Neh. 9:7
2. Mababa wa imani, Kumb. 7:8
3. wazao wa mababa wa imani, Kumb. 4:37; 10:15
4. Israeli, Kumb. 7:6; Zab. 135:4; Isa. 44:1,8; 43:10; Ezek. 20:5
5. Yeshuruni (Israel au Yerusalem), Kumb. 32:15; 33:5,26; Isa. 44:2
6. mfalme wa Israeli (uwakilishi wa utawala wa YHWH, ambao ungetabiri juu ya Daudi [kama vile I Sam. 10:24;16:8,9,10; II Sam. 6:21], aliyekuwa mfano wa Masihi), Kumb. 17:14-17
7. nafasi ya jina lake kukaal (yaani madhabahu kuu), Kumb. 12:5,11,14,18,21,26; 14:24; 15:20;16:2,6,7,11,15; 17:8,10; 31:11

Uweza wa Mungu na kusudi linaelezewa katika uchaguzi wake kwa Israeli.“Uchaguzi” wa Mungu katika Agano la Kale siku zote unahusianishwa na huduma, sio lazima wokovu kama ilivyo katika Agano Jipya. Israeli ilitakiwa kumfunua YHWH kwa ulimwengu wote ili kwamba ulimwengu uweze kuokolewa (kama vile Mwa. 12:3 ikinukuliwa katika Mdo. 3:25 na Gal. 3:8). Tazama Mada maalum katika 4:6.

☐**“kuwa watu wake hasa, kuliko mataifa yote yaliyo juu ya uso wa nchi”**Neno“umiliki” (BDB 688) linamaanisha hazina maalum (kama vile Kut. 19:5; Zab. 135:4; Mal.3:17). Kifungu hiki kinachojirudia katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 7:6; 14:2; 26:18). Tafadhali soma Mada Maalum: Upendeleo wa Kiinjili wa Bob 4:6! Kutoka katika hili utaona namna ninavyotazama ufasiri wa maandiko! Inaonesha kituo cha uunganishi cha mtazamo wangu wa kiulimwengu (yaani Agizo Kuu)!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 14:3-8

³Usile kitu cho chote kichukizacho. ⁴Wanyama mtakaokula ni hawa ng'ombe, na kondoo, na mbuzi, ⁵kulungu, na paa, na kongoni, na mbuzi wa mwitu, na paa mweupe, na pofu, na mbuzi wa mlima; ⁶na kila mnyama aliyepasuliwa ukwato, ukapasuka ukwato wake zikawa mbili, naye ni mnyama mwenye kucheua akatafuna tena, katika wanyama wote, ndiye mnyama mtakayemla. ⁷Lakini, hawa msile katika wale wenye kucheua, na hao waliopasuliwa ukwato; ngamia, na sungura, na kwang'a, kwa kuwa hucheua, lakini hawakupasuliwa kwato, ni najisi kwenu; ⁸na nguruwe, kwa kuwa amepasuliwa ukwato lakini hacheui, huyu ni najisi kwenu msile nyama zao, wala mizoga yao msiiguse.

14:3 “Usile”Mistari ya 3-21 inaaksi Mambo ya Walawi 11:2-19, lakini kukiwa na utofauti. Tofauti kama hii ambayo ni ngumu kuelezea imesababisha matazamio ya vyanzo kadhaa. KITENZI“kula” (BDB 37, KB 46) kinatumika mara 17 katika sura hii. Tazama Mada Maalum.

MADA MAALUM: SHERIA ZA CHAKULA ZA AGANO LA KALE

Kwa mawazo yangu vyakula hivi (Mambo ya Walawi 11; Kumbukumbu la Torati 14) hayatolewi kimsingi kwa ajili ya afya au sababu za kiusafi (yaani, *Maimonides*, Guide 3:48; *Kiddushin* 49b [*Talmudic tractate*]), lakini kwa sababu za kithiolojia. Waisraeli hawakutakiwa kuchangamana na Wakanaani (kama vile Isa. 65:4; 66:3, 17). Taratibu nyingi zinazotolewa kwa Israeli kupitia Musa zinahusiana na matendo ya kijamii na ibada na chakula ya Wakanaani (mfano Kutoka. 8:23).

Katika swali la “je sheria hizi za chakula hizi ni za kufuata au hata kusaidia kwa waaminio wa Agano Jipya,” Naweza kusema Hapana! Hapana!

Hapana! Hapa ni sababu zangu:

1. Yesu alikataa sheria za vyakula kama njia ya kujongea kwa Mungu na kumpendeza, Marko 7:14-23 (hakika maoni ya kiuhariri yaliyoandikwa aidha na Petro au Yohana Marko katika mstari wa 19 yana uvuvio ule ule pia)
2. Swali hili muhimu linaweza likawa jambo la Baraza la Yerusalemu la Mdo. 15, ambapo liliamua kwamba Mataifa hayakutakiwa kufata sheria za kiibada za Agano la Kale (kama vile, hasa mstari wa 19). Mstari 20 sio sheria ya chakula lakini makubaliano ya ushirika kwa Wayahudi waaminio ambao wanaweza kuwa makanisa yao ya Mataifa.
3. Uzoefu wa Petro, Mdo. 10 katika Joppa haihusiani na chakula bali juu ya ukubalifu wa watu wote, bado Roho alitumia jambo lisilo la hapo la sheria za chakula kama ishara ya kumfundisha Petro!
4. Mjadala wa Paulo wa “udhaifu” na “wenye nguvu” waaminio unatutahadhalisha kutolazimisha ufasiri wetu wenyewe (kama vile Rom. 14:1-15:13; I Wakorintho 8-10).
5. Maonyo ya Paulo juu ya ushikiliaji dini na kuhukumiana kwa kuhusianisha na mafundisho ya uongo yanayoandikwa katika Kol. 2:16-23 yanatakiwa kuwa onyo kwa waaminio wote wa kila kizazi!

MADA MAALUM: CHUKIZO (AGANO LA KALE)

Maana ya msingi ni "kuchukiza" au "yenye ubaya." Hili ni tendo la kukiuka mipaka.

Neno "Chukizo" (BDB 1072, KB 1702) linaweza kurejelea mambo kadhaa:

1. Mambo yaliyohusiana na Wamisri:
 - a. hawa walichukizwa kwa tendo la kula na Waebrania, Mwa. 43:32
 - b. walichukizwa kwa tendo la kuchangamana na wachungaji, Mwa. 46:34
 - c. walichukizwa nkwa tendo la Waebrania kutoa dhabihu, Kut. 8:26
2. mambo yaliyohusiana na fikra za YHWH kuyahusu matendo ya Israeli:
 - a. chakula kisicho safi, Kumb. 14:3-20
 - b. miungu, Kumb. 7:25; 27:15
 - c. roho za kiapagani, Kumb. 18:9,12
 - d. kutoa dhabihu (kuteketeza) ya watoto kwa Moleki, Law. 18:21; 20:2-5; Kumb. 12:31; 18:9,12; 2 Fal. 16:3; 17:17-18; 21:6; Yer. 32:35
 - e. miungu ya Mkanaani, Kumb. 13:14; 17:4; 20:17-18; 32:16; Isa. 44:19; Yer. 16:18; Eze. 5:11; 6:9; 11:18,21; 14:6; 16:50; 18:12
 - f. kuwatoa dhabihu wanyama wenye makufuru, Kut. 17:1 (kama vile Kumb. 15:19-23; Mal. 1:12-13)
 - g. kutoa dhabihu kwa miungu, yer. 44:4-5
 - h. kujitwalia mwanamke aliyetarakishwa, Kumb. 24:1-4
 - i. wanawake kuvaa mavazi ya wanaume (huenda ni idada za ki-Kanaani), Kumb. 22:5
 - j. Usilete ujira wa kahaba (ibada za ki-Kanaani), Kumb. 23:18
 - k. miungu ya Israeli, Yer. 2:7
 - l. Kujamiina kwa jinsia (huenda ni ibada za ki-Kikanaani), Law. 18:22; 20:13
 - m. kutumia vipimo visivyo sahihi, Kumb. 25:15-16; Mit. 11:1; 20:23
 - n. sheria za vyakula ziilikiukwa (huenda ni ibada za ki-Kanaani), Kumb. 14:3
3. Mifano iliyo katika Fasihi ya Vitabu vya Hekima:
 - a. Ayubu 30:10 – Ayubu juu ya jamii yake
 - b. Zaburi 88:8 – wanazaburi katika umoja wao
 - c. Mithali
 - 1) Mit. 3:32 – mtu mkaidi
 - 2) Mit. 6:16-19
 - a) macho ya kiburi, Mit. 6:17a
 - b) ulimi wa uongo, Mit. 6:17a

- c) mauaji, Mit. 6:17b
- d) mshauri mbaya, Mit. 6:18a; 15:26
- e) wepesi wa kukimbilia uovu, Mit. 6:18b
- f) shahidi wa uongo, Mit. 6:19a
- g) Naye apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu, Mit. 6:19b
- 3) Mit. 11:1; 20:10,23 – vipimo visivyo sawa
- 4) Mit. 11:20 – moyo wenye uhalifu
- 5) Mit. 12:22 – midomo ya uongo
- 6) Mit. 15:8; 21:27 – sadaka za mtu mbaya
- 7) Mit. 15:9 – njia za mtu mbaya
- 8) Mit. 16:5 – moyo wa majivuno
- 9) Mit. 17:15
 - a) asemaye kwamba asiye haki ana haki
 - b) asemaye kwamba mwenye haki

(10) Mit. 28:9 – aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria

4. Kuna kifungu cha matukio ya siku ya mwisho, "chukizo la huzuni," ambacho kinatumika katika Danieli (kama vile Dan. 9:27; 11:31; 12:11). Hiki kinaonekana kuayarejelea matukio matatu tofauti tofauti (utimilifu mwingi wa unabii):
 - a. Antiochus IV Epiphanes wa kipindi Wamakayo cha uwazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya (kama vile 1 Mak. 1:54,59; 2 Mak. 6:1-2)
 - b. Jemedari wa Kirumi (Mfalme wa aliyefuatia), Tito, aliyeitawanya Yerusalemu na kuliharibu hekalu mnamo 70 B.K (kama vile Mt. 24:15; Marko 13:14; Luka 21:20)
 - c. Kiongozi wa ulimwengu wa nyakati za mwisho aliyeitwa "mtu wa sheria" (kama vile 2 The. 2:3-4) au "Mpinga Kristo" (kama vile 1 Yohana 2:18; 4:3; Ufunuo 13)

☐ **“cho chote kichukizacho”**Tungo hii (BDB 481 MUUNDO WA MANENO 1072) inatumika pia katika Kumb. 14:3.

14:5 “na paa, na kongoni, na mbuzi wa mwitu”Hawa ni wanyama najisi wa mwituni wasiofaa kwa ajili ya sadaka lakini si kwa chakula.Hawatajwi katika Mambo ya Walawi 11 kwasababu hawakuwa wanajulikana katika nchi ya Misri. Baadhi ni ngumu kwa watu wa sasa kuwatambua.

14:6 “na kila mnyama aliyepasuliwa ukwato.....mwenye kucheua akatafuna tena”Huu ni mwongozo wa msingi kwa ajili ya utoaji wa sadaka unaotolewa katika Mambo ya Walawi 11:4. Kifungu hiki, “kupasuliwa ukwato,” ipo katika namna ya upanuzi (KITENZI BDB 828, KB 969, *Hiphil* WAKATI TIMILIFU pamoja na NOMINO BDB 828) kama katika mstari wa 7. Kwa maelezo haya yanaunganishwa na muundo wa upanuzi wa pili (KITENZI BDB 1042, KB 1608, *Qal* KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPO ENDELEU pamoja na NOMINO (BDB 1043). Maelezo haya ni ya kibainishi na ya wazi.

☐Baadhi ya wanyama ambao kwa sehemu tu hutimiza matakwa mawili (“kupasuka nyayo” na “kucheua”) wanatajwa katika mstari wa 7.

14:7

NASB “kwang'a”
NKJV “kwang'a”
NRSV, TEV “kwang'a”
LXX, NJB
NJB, NIV “kwang'a”
JPSOA “kwang'a”

Huyu mnyama (BDB 1050 I) inavyoonekana kataja katika kitabu cha Law. 11:6 kama “sungura pori” au “sungura wa kufugwa.” Inafurahisha kwamba Mambo ya Walawi inasema (kama inavyodhaniwa hapa) kwamba sungura

wanacheua. Hii ni sehemu nzuri kuwakumbusha wasomaji kwamba Waisraeli walijikita ufahamu wao wa asili juu ya uchunguzi wa kitabia (lugha ya kimatukio). Sungura, kiuhalisia hawacheui, bali kucheza kwa pua zao kunawafanya waonekane kana kwamba wanacheua. Hili si kosa katika Biblia bali utambuzi kwamba watu wa kale walikita ufahamu wao katika uchunguzi wa nje na sio mbinu za kisasa za kisayansi.

14:18 “nguruwe” Nguruwe aliliwa na kutumika katika ibada za kutoa sadaka za Wakanaani (kama vile Isa. 65:4; 66:3,17). Ilichukuliwa kama najisi kwasababu ya tabia yake ya ulaji (kama mbwa wafanyavyo) na maeneo anayopendelea kupumzika (mashimo yenye tope). Nguruwe walikuwa wakitolewa sadaka mara kwa mara katika desturi za Wahiti, Wayunani na Warumi. Pia waliliwa (na baadhi ya makundi) na desturi za Mediterania. Kwa mjadala mpana wa vyakula na sadaka za Mashariki ya Karib ya Kale ABD, juzuu 6, “Zoology,” kur. 1109-1167, kwa nguruwe, tazama uk. 1130-1135.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:9-10

⁹Mtakula hawa katika wote walio majini; kila kilicho na mapezi na magamba mtakula; ¹⁰na kila kisichokuwa na mapezi na magamba msile; ni najisi kwenu.

14:9 “kila kisichokuwa na mapezi na magamba”Huu ni mwongozo wa msingi wa Law. 11:9-12. Tena sababu za msingi kwa makatazo hayatolewi popote katika Agano la Kale. Angalia dokezo katika 14:3.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:11-20

¹¹Mna ruhusa kula katika nyuni wote walio safi. ¹²Lakini hawa msiwale; tai, na furukombe, na kipungu; ¹³na kengewwa, na kozi, na mwewe kwa aina zake; ¹⁴na kila kunguru kwa aina zake; ¹⁵na mbuni, na kirukanjia, na dudumizi, na kipanga kwa aina zake; ¹⁶na bundi, na mumbi, na bundi mkubwa; ¹⁷na mwari, na nderi, na mnanzi; ¹⁸na membe, na koikoi, kwa aina zake; na hudihudi, na popo. ¹⁹Na wadudu wote watambao wenye mabawa ni najisi kwenu; msiwale. ²⁰Mna ruhusa kula katika nyuni wote walio safi.

14:11Hii ni sawasawa na Law. 11:13-19. Sababu ya “unajisi” haitolewi lakini inaonekana wazi kwamba ndege wanaoorodheshwa wanakula nyama.

14:18 “koikoi” Aina hii ya ndege (BDB 189) hula aina zote za wadudu mpaka wale kombamwiko. Ilikuwa kujulikana kwa kula kwake katika maeneo machafu na kuwa na maeneo ya kupumzika, hivyo alikuja kuwa ndege “najisi” mwenye kuhamahama.

14:19 “watambao wenye mabawa”Kifungu hiki (BDB 481 TUNGO 1056 & 733, kama vile Mwa. 7:14,21) kinarejerea wadudu watambao. Hii inafanana na Law. 11:20-23, ambapo baadhi ya wadudu sio najisi kuliwa (yaani nzige, kama vile Mt. 3:4; Marko 1:6). Wadudu hawa ni chakula cha ndege wengi walio najisi.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 14:21

²¹Msile nyamafu yo yote; waweza kumpa mgeni aliye ndani ya malango yako, ili apate kula; au kumliza mtu wa mataifa; kwa kuwa wewe u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako. Usimtokose mwana-mbuzi katika maziwa ya mamaye.

14:21 “Msile nyamafu yo yote”Hili linaweza kuthibitishwa katika kitabu cha Kut. 22:31. Moja ya sababu ilikuwa ni kwasababu damu ilikuwa bado iko ndani yake (kama vile 12:16,23-25; Mwa. 9:4). Sheria hii haikumuhusu kila mtu katika Nchi ya Ahadi (yaani, wageni na watu wa mataifa mengine haikuwahusu, lakini tazama Law. 17:15). Sheria hizi za vyakula zilikusudiwa kuwatenganisha Israeli kutoka katika matendo ya jamii ya Wakanaani na ibada zao. “Hutachemsha maziwa ya mtoto ana mama yake” *The Ras Shamra* (angalia Cyrus H. Gordon, *Ugaritic Handbook*, ukur. 174) maandiko yanaonesha kwamba hii ilifanyika katika desturi zingine kama uwakilishi wa ustawi. Dini ya Kiyahudi ilikuza sheria za vyakula kwa uzingativu mkubwa sana (walitenganisha vyombo vya kupikia na sahani kwa ajili ya nyama na bidhaa za maziwa na siagi) kwa kuzingatia mstari huu. Hata hivyo msukumo unaonekana

kuhusiana na ibada ya Wakanaani ya utoaji sadaka (kama vile Kut. 23:19; 34:26). Haihusiani na jambo lolote juu ya ugonjwa au usafi.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) 14:22-27

²²Usiache kutoa zaka ya fungu la kumi katika maongeo yote ya mbegu zako, yatokayo shamba mwaka baada ya mwaka. ²³Nawe utakula mbele za Bwana, Mungu wako, mahali atakapochagua apakalishe jina lake, zaka ya nafaka zako, na divai yako, na mafuta yako, na wazaliwa wa kwanza wa makundi yako ya ng'ombe na ya kondoo; ili upate kujifunza kumcha Bwana, Mungu wako, daima. ²⁴Na njia ikiwa ndefu mno nawe, usiweze kuzichukua kwa kuwa mahali ni mbali nawe mno atakapochagua Bwana, Mungu wako, apakalishe jina lake, hapo atakapokubarikia Bwana, Mungu wako; ²⁵ndipo uzibadili ziwe fedha, na kufunga zile fedha uende nazo mkononi mwako, hata mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako; ²⁶na zile fedha zitumie kwa cho chote itakachotamani roho yako, ng'ombe, au kondoo, au divai, au kileo, au roho yako itakacho kwako cho chote; nawe utakula huko mbele za Bwana, Mungu wako; tena furahi, wewe na nyumba yako; ²⁷na Mlawi aliye ndani ya malango yako usimwache, kwani hana fungu wala urithi pamoja nawe.

14:22 “fungu la kumi”Hesabu 18 inazungumzia fungu la kumi kwa ajili ya Walawi na pia makuhani kwenye madhabahu.Hata hivyo kifungu hiki kinafanana na sura ya 12 na kuzungumzia zaidi fungu la kumi la mazao yatokananyo na kilimo. Tazama dokezo katika sura ya 12.

14:23 “mahali atakapochagua apakalishe jina lake.” Tazama dokezo kamili katika 12:5.

14:26 “na zile fedha zitumie kwa cho chote itakachotamani roho yako”Hii inarejerea vitu vya kutolewa zaka katika madhabahu kuu. Hii ni sawa na 12:20. Kifungu hiki kinawafanya “washika dini” wachanganyikiwe! YHWH anataka furaha yetu! Anataka atushirikishe na tushirikiane nae (kama vile 12:7,18; 16:14; 27:7; I Nyakati. 29:22; Zab. 104:15; Mhubiri2:24; 3:12,13,22; 5:18; 8:15; 9:7-9; Isa. 22:13). Hata Agano Jipya linaipanua dhana hii kwa kutaja kwa uwazi kwamba katika uumbaji hakuna kinachoonekana kuwa najisi kwacho chenyewe (mfano, Mdo. 10:15; Rom. 14:2,14,20; I Kor. 6:12;10:23-33; I Tim. 4:4). Hii haimaanishi kuwapa wanadamu kibali cha kutenda dhambi bali kutia moyo uhuru wa Mkristo kutoka katika nadharia za kidini na kuhukumiana (kama vile Kol. 2:16-23). Hata hivyo, mwamini mkomavu atakuwa makini akiwa katika ulimwengu huu ulioanguka kutofanya kitu ambacho kitamkwaza ndugu dhaifu ambaye Kristo alimfia (kama vile Rom. 14:1-15:13)!

☉**“au kileo”**Hiki (BDB 1016) kilikuwa ni kileo ambacho kilikuwa kinatengenezwa kwa kuchachuliwa kiasili na kuongezwa asilimia ya kilevi kuwa kubwa (yaani, kiwe kikali zaidi). Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: MTAZAMO WA KIBIBLIA KUHUSIANA NA ULEVI NA KILEO

I. Maneno ya Kibiblia

A. Agano la Kale

1. *Yayin* – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hiii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
2. *Tirosh* – Hiii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unaanza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
3. *Asis* – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya," BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
4. *Sekar* – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mziziz wa Kiebrania unatumika ndani

ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi huu unaongezwa katika ndani yake ili kukifanya kileweshe zaidi. Hiki ni sawa na *yayin* (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).

B. Agano Jipya

1. *Oinos* – neno lililo sawa kimaana na *yayin*
2. *Neos oinos* (divai mpya) – neno linalofanana la Kiyunani sawa na *natiros* (kama vile Marko 2:22).
3. *Gleuchos vinos* (divai mpya, *asis*) – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).

II. Matumizi ya Kibiblia

A. Agano la Kale

1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
2. Divai ni swehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
3. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2; Mit. 31:6-7).
4. Divai inaqweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu – Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uriah – 2 Sam. 11:13; Amnon – 2 Sam. 13:28; Ela – 1 Fal. 16:9; Ben-hadad – 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amos 4).
5. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
6. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mit. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
7. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).
 1. Kipindi cha uwazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya
 2. Divai katika upatanisho ina msaada (Ecclesiasticus 31:27-33).
 3. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa yalevyayo yanahitajika." (BB 58b).

C. Agano Jipya

1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji katika divai (Yohana 2:1-11).
2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima molja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1 na kuendelea; Ufu. 19:9).
7. Divai ililaaniwa (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).

III. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia

A. Mkazo wa Kiupembuzi

1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
2. Ulevi ni tatizo kubwa.
3. Waamini katika baadhi ta tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1-23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).

B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka

1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote.
 - a. chakula – Marko 7:19; Luka 11:44; 1 Kor. 10:25-26
 - b. mambo yote yasiyo najisi – Rum. 14:14,20; 1 Tim. 4:4
 - c. mambo yote ya halali – 1 Kor. 6:12; 10:23
 - d. mambo yote yaliyo safi – Tito 1:15

2. Mwanadamu aliyeanguka ametumia vibaya zawadi ya Mungu kwa kuzitumia nje ya mipaka ya Mungu aliyoitoa.
- C. Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uuumbaji wa vitu vinayoonekana (tazama B. 1. Hapo juu).
- IV. Utamaduni wa Karne ya kwanza ya Kiyahudi na Chachu
- A. Chachu hunza ndani ya muda mfupi, takribani ndani ya masaa 6 baada ya barungi kusagwa
- B. Desturi ya Kiyahudi inasema kwamba povu linapoonekana juu yake (dalili ya uchachu), hii huelekea kuwa sehemu ya divai iliyo na uchachu (Ma aseroth 1:7). Hii iliiitwa "divai mpya" au "divai tamu."
- C. Chachu ya kwanza iliyo kali uilikamilishwa baada ya juma moja.
- D. Chachu ya pili ilichukuwa sku zipatazo 40 . Katika hatua hii tendo hili lilifikiriwa kama "divai kukuu" na ingweza kutolewa madhabahuni (Edhuyyoth 6:1).
- E. Divai ambayo iliyobakizwa ndani ya machicha (divai kongwe) ilifikiriwa kuwa nzuri, lakini ilitakiwa kuchujwa vizuri kabla ya kutumiwa.
- F. Divai ilifikiriwa kuwa kuukuu kwa usahihi baada ya kutunzwa vema kwa ajili ya kuchachushwa. Miaka mitatu kilikuwa kipindi cha muda mrefu ambapo divai ingetunzwa kwa usalama. Hii iliiitwa "divai kuuku" na ilitakiwa kuchanganywa na maji.
- G. Ni katika miaka 100 ya mwisho pekee ya ukame wa mazingira na ongezeko la madawa uchachu umetoweka. Ulimwengu wa kale usingeweza kustisha tendo la asili la kuchachusha.
- V. Maelezo ya Kiufungaji
- A. Hakikisha uzoefu wako, thiolojia, na fasiri ya kibiblia havimkashifu Yesu na ile karne ya kwanza ya Kiyahudi/Utamaduni wa ki- Kristo! Hawa kwa uwazi hawakujinyima moja kwa moja.
- B. Mimi sitetei matumizi haya ya kilevi kwa jamii. Hata hivyo, wengi huchochea nafasi ya Biblia juu ya somo hili na sasa wanadai keki kuu iliyojikita katika utamaduni/ubaguzi wa kimadhehebu.
- C. Kwangu mimi, Warumi 14 na 1 Wakorintho 8-10 zimetoa utambuzi na mwongozo uliojikita katika upendo na heshima kwa waamini wenetu na kuieneza injili ndani ya utamaduni wetu, si uhuru binafsi au ukosoaji wa hukumu. Ikiwa Biblia ni chanzo pekee cha imani na matendo, bila shaka yatupasa wote kufikiria upya juu ya jambo hili.
- D. Ikiwa tunahimiza kujinyima moja kwa moja kama mapenzi ya Mungu, nini tunachokimaanisha juu ya Yesu, pamoja na zile tamaduni za sasa ambazo kwa hali ya mazoea hutumia divai (m.f. Ulaya, Israeli, Argentina).

☐“nawe utakula huko mbele za Bwana”Hii inarejerea sadaka ya amani ambapo Mungu na Mtoa sadaka na familia yake walikula pamoja. Katika Mashariki ya Kale ya Karibu kula pamoja ilikuwa ishara ya agano.

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 14:28-29

²⁸Kila mwaka wa tatu, mwisho wake, toa fungu la kumi lote la maongeo yako ya mwaka huo, uliweke ndani ya malango yako; ²⁹na Mlawi kwa kuwa hana fungu wala urithi pamoja nawe, na mgeni, na yatima, na mjane aliyefiliwa na mumewe, walio ndani ya malango yako, na waje wale na kushiba; ili kwamba Bwana, Mungu wako, akubarikie katika kazi yote ya mkono wako uifanyayo.

14:29 “na mgeni, na yatima, na mjane”Kumbu Kumbu la Torati liko makini katika kujali kwake wale wote walioishi katika Nchi ya Ahadi (kama vile 10:18; 26:12-15)! Fungu la kumi la mwaka wa tatu lilikuwa kwa ajili ya walawi na masikini waliopo katika maeneo ya mji.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kigezo gani kilichotumika kuamua kipi kiwe najisi na kipi kisiwe?
2. Je! sheria hizi zimetoka kwa Mungu? Ikiwa ndivyo, kwanini hatuzishiki leo hii?
3. Nini ilikua kusudio la fungu la Kumi?

KUMBUKUMBU LA TORATI 15

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Madeni Yanafutwa Kila baada ya Miaka Saba	Maisha ya watu walio Watakatifu (14:1-15:23)	Mwaka wa Saba	Mwaka wa Sabato
15:1-6	15:1-6	15:1-3	15:1-6
Wema kwa Masikini		15:4-6	
15:7-11	15:7-11	15:7-11	15:7-11
Sheria Kuhusu Utumwa wa Watumishi		Namna ya kuwatenda Watumwa	Watumwa
15:12-18	15:12-17a	15:12-15	15:12-15
		15: 16-18	15:16-17
	15:17b		15:18
Sheria Kuhusu Mzaliwa wa Kwanza wa Wanyama		Mzaliwa wa kwanza Ng'ombe na Kondoo	Mzaliwa wa Kwanza
15:19-23	15:19-23	15:19-23	15:19-23

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi’') *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozokwa kujisomea fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (mzunguko #3, uk viii) Linganisha mgawanyo wa somo lako na tafsiri nne hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA SURA YA 15

- A. Sura ya 15 ni mwendelezo wa amri maalum ambazo zilishughulika na baadhi ya mahitaji pekee ya kilimo na kweli za kiishara za kimahusiano ambazo YHWH alihitaji kuzijenga ndani ya watu wake.
- B. Sura hii imegawanyika vema katika vipengele vitatu tofauti tofauti:

1. Mistari 1-11 inashughulika na upanuzi wa miaka ya Sabato iliyosalia ya Kipindi cha wana wa Israeli kutoka Misri. 23:10-13 na Law. 25:1-7 kwa wadaiwa na maskini wa eneo lile. II Nyakati 36:21 inasema kwamba uhamisho ulikuwa matokeo ya Wayahudi kushindwa kuishika Amri hii.
 2. Mistari 12-18 inashughulika na jamii ya utumwa, Mwebrania (mwanamume au mwanamke) ambaye alikuwa akimfanyia mtu fulani kazi kwa ajili ya kulipa madeni.
 3. Mistari 19-23 inashughulika na mzaliwa wa kwanza wa mifugo, au sadaka ya mzaliwa wa kwanza wa wanyama.
- C. Sura hii inabainishwa na matumizi ya VITENZI viwili:
1. Baadhi ni VITENZI HALISI na VITENZI VYA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU vya asili ile ile (ambavyo ni vya muundo wa kisarufi wa kukuza maana):
 - a. “Bwana atakubarikia kweli,” mst. 4, *Piel* yaof BDB 138, KB 159
 - b. “utaisikiza tu kwa bidii,” mst. 5, *Qal* ya BDB 1033, KB 1570
 - c. “mfumbulie mkono wako kwa kweli,” mst. 8, *Qal* ya BDB 834 I, KB 986
 - d. “umkopeshe kwa kweli,” mst. 8, *Hiphil* ya BDB 716, KB 778
 - e. “Mpe kwa kweli,” mst. 10, *Qal* ya BDB 678, KB 733
 - f. “Mfumbulie kwa kweli,” mst. 11, *Qal* ya BDB 834, KB 986
 - g. “umwangelie kwa wema,” mst. 14, *Hiphil* ya BDB 778, KB 858
 2. Vingine ni VITENZI vyenye kufanana, vimetumika mara mbili:
 - a. “utakopesha. . . lakini hutakopa,” mst. 6, a *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU na *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ya BDB 716, KB 778
 - b. “utayatawala. . . usitawaliwe,” mst. 6, a *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU na *Qal* ya WAKATI USIO TIMILIFU ya BDB 605, KB 647
 - c. “mwache huru . . . huru. . . usimwache aende zake,” mist. 12,13, zote tatu ni *Piel* ya KAULI za WAKATI USIO TIMILIFU wa BDB 1018, KB 1511
 - d. “watakula. . . usile,” mist. 22,23, zote ni *Qal* ya KAULI ZA WAKATI USIO TIMILIFU wa BDB 37, KB 46
Tambua kuwa kundi la pili ni yakinifu na lenye kufuatiwa na matumizi kanushi.
 3. Kuna marudio ya NOMINO na *Qal* ya KITENZI HALISI cha asili ile ile katika mst. 2 - “maachilio. . . imepigwa mbiu,” yote kutoka BDB 1030, KB 1557

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LATORATI 15:1-6

¹Kila miaka saba, mwisho wake, fanya maachilio. ² Na jinsi ya maachilio ni hii, kila mkopeshaji na akiache alichomkopesha mwenziwe, wala asimlipize mwenziwe wala nduguye; kwa kuwa imepigwa mbiu ya maachilio ya Bwana. ³Waweza kumtoza mgeni; lakini kila uwiacho kwa nduguyo mkono wako utamwachilia. ⁴ Lakini hawatakuwako maskini kwenu; (kwa kuwa Bwana atakubarikia kweli katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako, uimiliki, iwe urithi wako;) ⁵kwamba utaisikiza tu kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, uyatunze maagizo haya yote nikuagizayo leo, kuyafanya. ⁶Kwani Bwana, Mungu wako, atakubarikia, kama alivyokuahidi; nawe utakopesha mataifa mengi, lakini hutakopa; tena utayatawala mataifa mengi, usitawaliwe na wao.

15:1 “¹Kila miaka saba” Hapa mambo mawili yalitokea: (1) nchi ilipaswa kufuatisha jambo hili kama alama ya umiliki wa Mungu wa nchi pamoja na uangalizi wake kwa watu masikini (kama vile Kut. 23:10-13; Lev. 25:1-7). Katika Josephus’ *The Antiquities of the Jews*, XIII.8.1, tunabaini rejea za taratibu za Wayahudi za mapumziko ya nchi na (2) hapa Waisraeli pia waliachiliwa dhidi ya madeni (kama vile mst. 2; 31:10). Saba ilikuwa kama namba ya utimilifu kwa sababu siku saba za uumbaji na siku ya saba ya mapumziko katika Mwa. 1:1-2:3.

15:2 “maachilio” Neno hili (BDB 1030) limanaanisha “punguzo.” Katika Kut. 23:10-11 KITENZI kinatumika kumaanisha kuipumzisha nchi kwa kila miaka saba. Hii NOMINO imetumika mara mbili tu katika Agano la Kale,

hapa na katika 31:10. Hapa kitenzi kinatumika kistiari kwa maana ya kusamehe deni, kwa kuwa mgawanyo wa mazao usingeweza kulipa deni lake ndani ya mwaka ambao upandaji ulikuwa umezuiliwa na hapakuwa na kazi kwa mfanyakazi aliyekodishwa. Mgeni, kwa upande mwingine, angefanya kazi shambani mwake na kulipa madeni.

☐“**kila mkopeshaji na akiache**” Kwa vyo vyote kifungu hiki kilimaanisha kuweka huru kwa wakati wa kudumu au kuweka huru kwa muda tu haijulikani. Mukadha unaonekana kuendana na tendo la kuweka huru kwa wakati wa kudumu, lakini naamini kwamba inaweza kuwa ilikuwa kwa mwaka mmoja tu nchi kupumzishwa kwa ajili ya deni lililosamehewa (kama vile Biblia ya NET, uk. 368 #16). Msamaha wa Mungu juu yao ulikuwa kiini kwa hawa wamiliki wa ardhi kusamehe madeni (kiishara, kwa nuda tu).

15:3 “mgeni” Neno hili linawarejelea wale wasio Waisraeli ambao walikuwa na makazi ya kudumu humo Palestina (BDB 648, kama vile 14:21; 15:3; 17:15; 23:20; 29:22), ambao walipewa mipaka ya haki za kiraia na ulinzi wa kisheria kwa mujibu wa sheria ya Musa. Neno lingine “rafiki” (BDB 158) linamaanisha wapya au wasafiri ambao pia walipewa haki za kiraia na ulinzi (kama vile 1:16; 5:14; 10:18,19[mara mbili]; 14:21,29; 16:11,14; 23:7; 24:14,17,19,20,21; 26:11,12,13; 27:19; 28:43; 29:11; 31:12). Utangalizi huu kwa wale wasio Waisraeli kwa uwazi ulionyesha:

1. tabia ya YHWH
2. uwezekano wa mjumuiko
3. tendo la wakati uliopita kwa Israeli humo Misri

15:4 “hawatakuwako maskini kwenu” Mistari 4-6 inaeleza hali ya ubora (iliyoashiriwa ndani ya mahitaji ya Mwaka wa Sabato na Mwaka wa Yubilee). Hali ya ubora mara chache ni ya kihistoria. Waisraeli wengi walipotewa ardhi zao za kifamilia. Mara nyingi kulikuwa na masikini miongoni mwa Wayahudi (kama vile Mt. 26:11).

15:5 Hili ni onyo la mara kwa mara kuhusu utii wa agano.

1. “kwamba utaisikiza tu kwa bidii” – hii *Qal* ya KITENZIJINA HALISI na *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU wa BDB 1033, KB 1570 (chenye kuonyesha mkazo)
2. “uyatunze maagizo haya yote” - *Qal* mbili za KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO cha BDB 1036, KB 1581 na BDB 793, KB 889 agano la ahadi za YHWH ni amri endelevu kuwa na mwitikio wa utii.

15:6 Baraka za YHWH zilizozungumzwa/kuahidiwa (BDB 180, KB 210, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) zinaelezwa:

1. “Bwana, Mungu wako, atakubarikia,” *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU wa BDB 138, KB 159, kama vile mst. 4 (mara mbili); 1:11; 2:7; 7:13 (mara mbili); 12:7; 14:24,29; 15:10,14,18; 16:10,15.
2. “utayatawala mataifa mengi, usitawaliwe na wao.” Hii ni *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU na kisha *Qal* kanushi ya WAKATI USIO TIMILIFU wa BDB 716, KB 778.
3. “Hii ni *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU na *Qal* kanushi ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU wa BDB 605, KB 647.

Ahadi hizi zina vidokezi vya kimataifa na vya matukio ya siku za mwisho (kama vile Isa. 9:6-7; 11:1-10; Mika 5:1-5a).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 15:7-11

⁷Kama akiwapo mtu maskini pamoja nawe, nduguzo mmojawapo, ndani ya malango yako mojawapo, katika nchi yako akupayo Bwana, Mungu wako, usifanye moyo wako kuwa mgumu, wala usimfumbie mkono wako nduguyo maskini; ⁸lakini mfumbulie mkono wako kwa kweli, umkopeshe kwa kweli yatoshayo haja yake katika ahitajiayo. ⁹Jitunze, msiwe na neno lisilofaa moyoni mwako, kusema, Umekaribia mwaka wa saba, mwaka wa maachilio; jicho lako likawa ovu juu ya nduguyo usimpe kitu; naye akamlilia Bwana juu yako, ikawa ni dhambi kwako. ¹⁰Mpe kwa kweli, wala moyo wako usisikitike utakapompa; kwa kuwa atakubarikia Bwana, Mungu wako, kwa neno hili katika kazi yako yote, na katika kila utakalotia mkono wako. ¹¹Kwa maana maskini hawatacoma katika nchi milele; ndipo ninakuamuru na kukuambia, Mfumbulie kwa kweli mkono wako nduguyo, mhitaji wako, maskini wako, katika nchi yako.

15:7 “Kama akiwapo mtu maskini pamoja nawe” Ukweli unaelezwa katika mst. 11. Umaskini unaweza kufasiliwa kama upungufu wa staha na heshima. Hapa upungufu unasababishwa na kupoteza ardhi ya kifamilia kunakosababishwa na kukopa fedha kama ndugu.

☐ **“nduguzo mmojawapo”** Sheria ya Musa inaonyesha, masikitiko ya YHWH ya kipekee na huruma kwa:

1. ndugu wengine agano wasiojiweza wa kiume/kike
2. wajane
3. yatima
4. wasio na makazi
5. wageni

Ni huruma ya namna hii kupitia misingi ya kijamii yeye kuufanya mkusanyiko wa sheria za Israeli kuwa za kipekee. Mfumo mwingine wa sheria za kale uliwaegemea wasomi, wenye mali nyingi, na wa jamii ya kifalme. Israeli iliwaegemea wanyonge, waliotengwa kijamii na kiuchumi, wasio na msaada kisheria, na wasiothamaniwa!

☐ **“ndani ya malango yako mojawapo, katika nchi yako”** Tambua kuwa si maskini wenyeji tu, bali namna jamii inavyowachukulia maskini hawa. YHWH huwataka watu wake kuwatendea wahitaji wake kama na yeye anavyowatendea!

☐ **“usifanye moyo wako kuwa mgumu, wala usimfumbie mkono wako nduguyo maskini”** Vyote nia na matendo vinahusishwa (kama vile II Nya. 9:7):

1. “usifanye moyo wako kuwa mgumu,” *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 54, KB 65, kama vile II Nya. 36:13
2. “wala usimfumbie mkono wako,” *Qal* ya KALI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 891, KB 1118

15:8 Vitambue VITENZI JINA HALISI na KAULI ZA WAKATI USIO TIMILIFU zenye kufanana kwa ajili ya msistizo:

1. “mfumbulie mkono wako kwa kweli” - *Qal* ya KITENZI JINA HALISI na *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ya BDB 834, KB 986. Stiari hii inafanana na mst. 7.
 - a. ufungue moyo wako (usifanye moyo wako kuwa mgumu)
 - b. ufungue mkono wako (usiukunje moyo wako) kama vile mist. 11,13
2. “umkopeshe kwa kweli” - *Qal* ya KITENZI JINA HALISI na *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ya BDB 716, KB 778

☐ **“umkopeshe kwa kweli yatoshayo haja yake”** Hii ni BDB 191 ya MUUNDO WA MANENO pamoja na 341, yenye kudokeza vya kutosha juu ya hitaji la ndugu, si katika ishara tu ya wale wapitao (kama vile Yakobo 2:15-26; I Yohana 3:16-17).

15:9 “Jitunze” Hii ni *Niphal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 1036, KB 1581), ambayo ni dhamira ya mara kwa mara (kama vile 4:9,15,23; 6:12; 8:11; 11:16; 12:13,19,28,30; 15:9; 24:8). Kuna matokeo ya agano baada ya kutii na kutokutii.

☐ **“neni lisilofaa”** Neno “lisilofaa” linatokana na asili ile ile (BDB 116) kama *Belial*. Hili linarejelea neno “lisilo na maana,” “la upumbavu,” “mtu mwovu” (kama vile Mit. 6:12). Taza maelezo katika 13:14.

☐	
NASB	“jicho lako likawa ovu”
NKJV	“jicho kuwa ovu”
NRSV	“mtazamo. . .kwa uhasama”
TEV	-----
NJB	“ghadhabu”

Hili neno “uhasama” (BDB 949, KB 1269, *Qal* yaKAULI YA WAKATI TIMILIFU) linamaanisha “ubaya au “uovu.” Nahau sawa na hii inatumika katika 28:54,56. KITENZI kama hiki kinarudiwa katika mst. 10, ambapo kinatafsiriwa kama “huzuni.” Nahau hii inahusiana na fikra zilizotawala ndani ya mtu katika mambo fulani na /au kuwahusu watu fulani. Nia ni muhimu sana katika vitabu vyote vya Agano la Kale na Agano Jipya. Mungu huangalia mioyo!

☐ **“naye akamlilia Bwana juu yako, ikawa ni dhambi kwako”** Maombi ya mtu mnyonge hayafanyi kuwa dhambi(yaani, yasiyo halali), bali kwa YHWH inaonyesha dhambi ndani ya moyo wa mwanadamu ulio na ubinafsi, mtu wa mwenye ukaidi (kama vile 24:18; Kut. 22:23). Baraka za YHWH ni masharti juu ya agano sahihi la nia na matendo.

Yawapasa watu wake kuiga tabia yake!

15:10 Huu ni muhtasari wa muktadha unaotokana na mst. 7.

☐ **“Mpe kwa kweli”** Tazama Tambuzi za Kimuktadha, C, 1, e.

15:11 **“Mfumbulie kwa kweli mkono wako”** Tazama Tambuzi za Kimuktadha, C, 1, f.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 15:12-17

¹² Ikiwa nduguyo, mume wa Kiebrania, au mwanamke wa Kiebrania, akiuzwa kwako, naye amekutumikia miaka sita; basi mwaka wa saba mwache huru aondoke kwako. ¹³ Nawe utakapomwacha huru aondoke kwako, usimwache aende zake mikono mitupu; ¹⁴ umwangelie kwa wema katika kundi lako, na sakafu yako ya nafaka, na kinu chako cha divai; mpe kama alivyokubarikia Bwana, Mungu wako. ¹⁵ Nawe kumbuka kwamba ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri, akakukomboza Bwana, Mungu wako; kwa hiyo mimi nakuamuru neno hili hivi leo. ¹⁶ Hata itakuwa, akikuambia, Siondoki kwako; kwa sababu akupenda wewe na nyumba yako, kwa kuwa yu hali njema kwako; ¹⁷ ndipo utwae uma, uupenyeze katika sikio lake uingie katika ubao wa mlango, naye atakuwa mtumishi wako milele. Na kijakazi chako naye mfanye vivyo.

15:12 Kiuhaliasia hili ni neno “ndugu” (BDB 26), lakini linatumika katika maana ya kitaifa ya neno “mwenza wa agano” au “dugu wa damu” (kama vile Law. 19:17; 25:25,35,36,39,47; Kumb. 15:12; 17:15). Hili linasistiza juu ya umoja wa kitaifa dhidi ya tofauti za kikabila au kifamilia. Istilahi hii na theolojia hii ni sawa na ile ya Gal. 6:10.

☐ **“Kiebrania”** Hili neno “Kiebrania” (BDB 720, KB 782) ni neno adimu la Agano la Kale. Kwa vyo vyote hili linarejelea (1) uzao wa jamii moja ya Eberi, mjukuu wa Shemu (kama vile Mwa. 10:21; (2) ni neno lenye kueleza juu ya kundi kubwa la Wasemiti (*Habiru*) huko Mashariki ya Karibu ya Kale, waliohamia kandokando ya Mesopotamia kama wahama hamaji katika milenia ya pili K.K.; au (3) kundi la wafanyakazi maskini wa kigeni waliopoteza mali zao (neno hili linatumiwa na wageni kutoa maelezo juu ya nyumba ya Ibrahimu, Yakobo na Yusufu).

☐ **“mume au mwanamke”** Kifungu hiki kinaonyesha usawa wa kisheria (kama vile mst. 17, pia ichunguze Mwa. 1:26-27). Mfumo wa sheria ya hapo kale uliwatenga (yaani, wanaume - Kut. 21:2-6; wanawake - Kut. 21:7-11). Hili lilikuwa ondoleo muhimu toka katika Mfumo wa sheria za Hammurabi, kumbukumbu la sheria za Babeli ambazo zilikuwepo kabla ya Musa, na mfumo wa kisiasa wa mataifa ya Kanaani. Watu wa Mungu walikuwa tofauti!

☐ **“akiuzwa kwako”** Hiki KITENZI (BDB 569, KB 581, *Niphal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinarejelea mtu anayejiuza katika utumwa wa mkataba (kama vile Law. 25:39,47,48,50; Mwebrania kama huyu anajadiliwa katika mist. 39- 46; Kut. 21:2-6).

☐ **“naye amekutumikia miaka sita”** Kifungu hiki kinaonekana kutohusiana kimtiririko na mwaka wa Sabato unaotajwa katika mist. 1-11, bali ikiwa ni hivyo, basi maana ya mst. 9 haijulikani.

☐ **“mwache huru”** KITENZI hiki (BDB 1018, KB 1511, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ni cha muhimu sana na ya kwamba kinarudiwa mara tatu katika mist. 12-13.

15:14 Mtumwa alipoachiliwa huru baada ya miaka yake sita ya kutumika, ilimpasa kupewa vyote alivyovihitaji kwa ajili ya kuendeleza nyumba yake.

1. “umwangelie kwa wema,”
Hiki ni KITENZI HALISI kingine na KITENZI CHA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU. Hii ni nahau ya Kiebrania, kiuhalisia ni, “utamfungua mnyororo kwa wema.” Tazama Tambuzi za Kimuktdha C, 1, g.
2. Viatambue vitu alivyopaswa kupewa:
 - a. kutoka katika kundi
 - b. kutoka katika sakafu ya nafaka
 - c. kutoka katika kinu cha divai
 - d. miongozo ilioongozwa imetolewa katika Kut. 21:3-4; Law. 15:41
3. Utoaji huu ulipaswa kufanyika katika hali ya kiroho na katika uzito ambao YHWH ameuonyesha kwa Israeli, kama vile mist. 4,6,10,18 na sababu maalum katika mst. 15 na Law. 25:41.

15:15 “Nawe kumbuka kwamba ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri” Msingi wa wema kwa mmiliki wa mtumwa ulikuwa na maana kwamba nyumba yake ilikuwa moja ya watumwa katika Misri na Mungu alikuwa mwema kwa mtumwa huyu. Tazama maelezo kamili katika 5:15.

☐ **“akakukomboa Bwana, Mungu wako”** KITENZI hiki (BDB 804, KB 911, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinatumika mara kadhaa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati, mara nyingi kina lirejelea tendo la neema ya YHWH la kuikomboa Israeli kutoka katika utumwa wa Kimisri (kama vile 7:8; 9:26; 13:5; 15:15; 21:8; 24:18). Tazama Mada Maalum katika 7:8. Kitabu cha Agano la Kale kinashuhudia vema juu ya pendo la kwanza na huruma ya Mungu kama ilivyo katika Agano Jipya! Wanadamu hawamtafuti Mungu, Yeye aliwatafuta na kuwakomboa! Matendo yake ya kwanza na tabia ya kutobadilika ndilo tumaini letu! Matendo ya Masihi kwa wote yanaonyeshwa katika matendo ya YHWH juu ya Israeli!

15:16 Mstari huu unafanana na Kut. 21:5. Huu unaonyesha mfano wa uhusiano wa unyenyekevu wa kujitoa ambao unafunua imani/pendo/utii wa uhusiano ya agano kati YHWH na Israeli. Shabaha ya agano ni upendo, maisha yenye baraka yenye kufuatishwa na mwendelezo wa uhusiano wa karibu katika ulimwengu wa roho. Baraka hizi mara nyingi ni matokeo ya uhusiano, kamwe si lengo!

15:17 “uopenyeze katika sikio lake” Kifungu hiki kina ishara mbili: (1) sikio lilikuwa ishara ya utii na (2) mlango uliokuwa ishara ya upendo ndani ya nyumba (TEV). Utaratibu huu ulifanyika ndani ya nyumba si katika eneo takatifu au katika lango la mji, kutegemeana na yule *Elohim* anayerejelewa na Kut. 21:6. Tafsihi ya Maandiko ya Agano la Kale la Kiebrania, Peshitta, na Targums za Kiaramu hii ni kama “waamuzi”, ambapo hili ni badiliko la utaratibu wa kale (kama vile Kut. 21:1-6). Hili lilimfanya kuwa mtumwa wa kudumu.

☐ **“milele”** Neno la Kiebrania ni *’olam* (BDB 761). Matumizi haya yanaonyesha kwamba neno la Kiebrania lazima litafanuliwa kulingana na muktadha wake. Hili linaweza kumaanisha “daima” au “kwa wakati mrefu wenye mipaka iliyohimarishwa.” Waalimu wa sheria za Kiyahudi wanasema kuwa neno hili lilimaanisha “mpaka mwaka wa Yubilee,” bali katika muktadha huu linamaanisha maisha ya kipindi cha utumwa. Tazama Mada Maalum katika 4:40.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 15:18

¹⁸Wala usione ugumu, utakapomwacha huru kuondoka kwako; kwani amekutumikia miaka sita kwa ujira mara mbili wa mwajiriwa; na Bwana, Mungu wako, atakubarikia kwa yote utakayofanya.

15:18 “Wala usione ugumu, utakapomwacha huru” Hii inamaanisha kwamba mtu hapaswi kulalamika pindi mtumwa aachiwapo huru baada ya miaka sita ya kutumika.



- NASB** “ujira mara mbili”
NKJV “amekuwa mtumwa wa kukodi kwa thamani mara mbili”
NRSV “amekodiwa kwa ujira wa wafanyakazi”
TEV “kwa nusu gharama ya wafanyakazi wa kukodi”
NJB “amekodiwa mara mbili ya kile anacholipwa mfanya kazi”
NET Bible “alikuwa wa thamani mara mbili ya mfanyakazi wa kukodi

Kuna baadhi ya mashaka kama tafsiri sahihi (kiuhalisia, “kwa nusu gharama,” BDB 1041 MUUNDO WA MANENO 969 I). Kuna uwezekano wa aina tatu:

1. mtumwa alikuwa akitumika mchana na usiku
2. mtumwa alifanya kazi bure, ambapo mtu wa kukodi alikuwa akilipwa
3. Isa. 16:14 inaorodhesha miaka mitatu kama kipindi cha kazi ya mtu wa kukodi (kama ulivyo ufafanuzi wa mfumo wa Sheria za Hammurabi), hivyo, mtumwa alifanya kazi mara mbili ya hiyo.

☐“na Bwana, Mungu wako, atakubarikia kwa yote utakayofanya” Baraka za aganohufuata utii wa agano, hasa panapokuwepo pendo sahihi, msamaha, fikra za kusaidia!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 15:19-23

¹⁹Wazaliwa wa kwanza waume wote wazaliwao katika kundi lako la ng'ombe na la kondoo, uwatakase kwa Bwana, Mungu wako; usifanye kazi kwa mzaliwa wa kwanza wa ng'ombe wako, wala usimkate manyoya mzaliwa wa kwanza wa kundi lako la kondoo. ²⁰Utamla mbele za Bwana, Mungu wako, mwaka hata mwaka mahali atakapochagua Bwana, wewe na nyumba yako. ²¹Lakini akiwa na kilema, akichechea, au akiwa kipofu, au mwenye kilema kibaya cho chote, usimsongezee Bwana, Mungu wako, sadaka. ²²Utamla ndani ya malango yako; wasio tohara na wenye tohara pia watakula, kama unavyokula paa na kulungu. ²³Pamoja na haya usile damu yake; uimwage nchi kama maji.

15:19-23 Mistari hii inashughulika na matumizi sahihi na matumizi yasiyo sahihi ya mzaliwa wa kwanza wa mifugo. Kifungu hiki kinairejelea Kut. 13:2, ambapo muktadha wa mapigo ya malaika wa kifo aliyewaua wazaliwa wa kwanza wa mwanadamu na mnyama huko Misri na Gosheni ambao nyumba zao hazikupakwa alama ya damu. Hii ilikuwa njia ya kiishara ya kuonyesha umiliki wa Mungu juu ya kila kitu (kama vile Kut. 13:2; Law. 2:14-16).

15:19 “uwatakase . . . Wazaliwa wa kwanza waume wote. . . kundi lako la ng'ombe na la kondoo” Kutoka 13 inatupa chimbuko la Kibiblia, pia tazama Hes. 18:15-16. Hii ilikuja kuwa njia ya ongezeko la kipato cha Walawi.

15:20 Hii inaurejelea 12:17-19; 14:23. Tazama maelezo kamili katika 12:5.

15:21 “Lakini akiwa na kilema . . . usimsongezee Bwana, Mungu wako” Mnyama mwenye kilema (mwenye upungufu) cha aina yo yote ile, yaani., upofu, kufifia rangi, mgonjwa, kiwete, kasoro, nk. asingesongezwa, bali angeliwa ndani ya nyumba na marafiki katika mazingira ya wenyeji (kama vile 12:15-16).

15:22

- NASB** “wasio tohara na wenye tohara pia watakula”
NKJV “mtu safi na asiye safi kama hyuo anaweza kumla”
NRSV “asiye safi na aliye safi kamahuyo”
TEV “wote, iwe safi au isiwe kiroho, wanaweza kumla”
NJB “aliye safi na asiye safi”

Katika Kiebrania kifungu hiki kinaweza kurejelea juu ya :

1. wale wamlao
2. yule aliwaye

Uchaguzi #1 inaonekana kuwa bora (LXX).

15:23 “Pamoja na haya usile damu yake” Damu ilikuwa ishara ya uzima na uzima ni wa Mungu (kama vile Mwa. 9:4-6; Law. 1:17; 7:26-27; 17:10-16; 19:26; Kumb. 12:16, 23-25; I Sam. 14:32-34). Ishara zilizo katika mistari iliyotangulia zinaonyesha umiliki wa Mungu juu viumbe vyote, hasa vile vilivyo hai.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! kuna ushahidi wa kihistoria wa mwaka wa Sabato imetekelezwa?
2. Nini sababu ya msingi ya hizi sheria zilizo katika sura 15?
3. Nini chimbuko la neno “Mwebrania”?

KUMBUKUMBU LA TORATI 16

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Pasaka	Kalenda ya Sikukuu Inafaywa Upya	Pasaka	Sikukuu: Pasaka na mikate Isiyotiwa chachu
16:1-8	16:1-8	16:1-4	16:1-8
16:5-8			
Sikukuu ya Majuma		Sikukuu ya Mavuno Inafanywa Upya	Sikukuu Nyinginezo
16:9-12	16:9-12	16:9-12	16:9-12
Pitio la sikukuu ya Hema la kukutania		Sikukuu za Makazi	
16:13-17	16:13-15	16:13-15	16:13-15
	16:16-17	16:16-17	16:16-17
Haki Lazima Itekelezwe (16:18-17:13)	Sheria inahusu haki na dini (16:18-17:20)	Utekelezwaji wa Haki (16:18-17:13)	Waamuzi
16:18-20	16:18-20	16:18-20	16:18-20
Mateso katika Ibada (16:21-17:7)			
16:21-17:1	16:21-17:1	16:21-17:1	16:21-17:1

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI(tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi) **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 16: 1-8

¹Utunze mwezi wa Abibu, ukamfanyie pasaka Bwana, Mungu wako, kwa kuwa ilikuwa ni mwezi wa Abibu alipokutoa Misri usiku Bwana; Mungu wako. ²Nawe umchinje pasaka Bwana, Mungu wako, katika kundi la kondoo na la ng'ombe, mahali atakapochagua Bwana apakalishe jina lake. ³ Usimle pamoja na mikate iliyotiwa chachu; siku saba utakula naye mikate isiyotiwa chachu, nayo ni mikate ya mateso; (kwa maana ulitoka nchi ya Misri kwa haraka); ili upate kukumbuka siku uliyotoka nchi ya Misri, siku zote za maisha yako. ⁴Wala isionekane kwako chachu muda wa siku saba katika mipaka yako yote; wala katika hiyo nyama uchinjaye siku ya kwanza jioni, kisilale cho chote usiku kucha hata asubuhi. ⁵Usimchinje pasaka ndani ya malango yako yote akupayo Bwana, Mungu wako; ⁶ila mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako, apakalishe jina lake, ndipo mtakapomchinja pasaka jioni, katika machweo ya jua, kwa wakati kama uliotoka Misri. ⁷Nawe umwoke na kumla mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako; kisha asubuhi yake ugeuke uende hemani mwako. ⁸Siku sita utakula mikate isiyotiwa chachu; na siku ya saba na uwe mkutano mtukufu kwa Bwana, Mungu wako, usifanye kazi yo yote.

16:1 “Utunze” Hili ni neno linalorudiwa rudiwa (BDB 1036, KB 1581, *Qal* ya KITENZIJINA HALISI) katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati— mara 73! Sura hii imeandikwa katika aina ile ile ya Kiebrania kama Amri Kumi za sura ya 5.

☐ **“mwezi”** Hii ni asili ile ile ya neno “mwezi mpya” (BDB 294 I). Tazama Mada Maalumu: Kalenda ya Mashariki ya Karibu ya Kale katika 1:3.

☐ **“Abibu”** Neno hili linamaanisha “malimbuko” (BDB 1), ambalo linaweza kudokeza miganda ya shayiri ya awali iliyokomaa. Hili lilikuwa jina la ki-Kanaani la kipindi cha wakati wa mwezi wa Tatu- Nne. Baadaye katika maandiko ya Wababeli neno *Nisan* limetumika katika kipindi hiki cha wakati. Kut 12:2,6 inatoa tarehe maalumu zilizotajwa hapa kwa ujumla.

☐ **“ukamfanyie”** Hiki ni KITENZI kilichozoeleka, “tenda,” “fanya” (BDB 793, KB 1581) kimetumika mara kadhaa katika sura ya 16 na kutafsiriwa kwa njia kadhaa:

1. “ukamfanyie,” mst. 1,10,13
2. “utakula,” mst. 8
3. “tena zishike amri hizi kwa kuzifanya,” mst. 12
4. “usipande. . . utakayofanya,” mst. 21

MADA MAALUMU: PASAKA

- I. Maelezo ya awali
 - A. Tendo la Kiungu la hukumu ya Wamisri na ukombozi wa Waisrael ni muguso wa upendo wa YHWH na uimalishaji wa taifa la Israeli (yaani, kwa manabii).
 - B. Kutoka kwa Waisrael ni timizo maalumu la ahadi ya YHWH kwa Abraham katika Mwa. 15:12-21. Pasaka inafanya ukumbusho wa kutoka kwa wana wa Israeli.
 - C. Huu ulikuwa wa mwisho, uliosambaa (kijiografia, yaani., Misri na Gosheni) na uharibifu mkubwa (wazaliwa wa kwanza wa binadamu na wanyama waliuwawa) kwa mapigo kumi yalitumwa na YHWH kwenda Misri na Musa.
- II. Neno lenyewe (BDB 820, KB 947)
 - A. Maana ya nomino haijulikani
 - 1) Iliyohusishwa na “mapigo” pamoja na “kipigo cha maaafa” (yaani, Kut. 11:1); Malaika wa Mungu walipiga wazaliwa wa kwanza wa binadamu na mifugo.

- B. Maana ya kitenzi
- 1) “kuchechema” au “kuchopea” (kama vile 2 Sam. 4:4), likitumika katika maana ya “ruka juu ya nyumba zilizotiwa alama” (yaani., Kut. 12:13,23,27, BDB 619, maarufu kama maelezo ya asili ya neno)
 - 2) “kucheza” (kama vile 1Fal. 18:21)
 - 3) Muakkadia-“kuridhisha”
 - 4) Mmisri-“kupiga”
 - 5) Vitenzi vilivyo sambamba katika Isa. 31:5, “kusimama ili kumlinda” kama vile REB ya Kut. 12:13)
 - 6) Milio ya Wakristo wa mwanzo iliyozoeleka kati ya *pasha* ya Kiebrania na *paschō* ya Kiyunani, “kuumwa/kuumia”
- C. Uwezekano wa mambo ya kihistoria yaliyowekewa umuhimu wa kwanza
- 1) Sadaka ya mchungaji kwa mwaka mpya
 - 2) Sadaka ya bedui na chakula cha jumuiya wakati wa kuondoa mahema kwenda uwanda wa malisho kuepuka uovu.
 - 3) Sadaka ya kuijepusha na uovu dhidi ya wachungaji wanao hama hama
- D. Sababu ni ngumu kuwa nazo uhakika wa kujua maana ya neno lenyewe, lakini vile vile na asili yake ni kwamba mambo mengi yaliyotofautiana kuhusu pasaka pia yanapatikana katika matambiko mengine ya kale.
- 1) Tarehe za majira ya kuchepua
 - 2) Maelezo ya asili na historia ya neno haijulikani
 - 3) Limehusianishwa na walinzi wa usiku
 - 4) Utumiaji wa damu
 - 5) Michoro/sanamu za malaika na mapepo
 - 6) Chakula maalumu
 - 7) Dalili za kilimo (mikate isiyotiwa chachu)
 - 8) Hakuna kuhani, hakuna madhabahu, wala mtizamo wa mahali Fulani
- I. Matukio
- A. Tukio lenyewe limeandikwa katika kitabu cha Kutoka 11-12
 - B. Sikukuu za mwaka zimeelezwa katika Kutoka 12 na kujumuishwa ndani ya sherehe ya siku nane zikiwa na sikukuu za mikate isiyotiwa chachu.
 - 1) Mwanzoni kabisa yalikuwa ni matukio ya kawaida, kama vile Kutoka. 12:21-23; Kumbu. 16:5 (kama vile Hes. 9)
 - a. Hakuna kuhani
 - b. Hakuna madhabahu maalumu
 - c. Utumiaji uliobobea wa damu
 - 2) Lilikuja kuwa ni tukio la madhabahu iliyokuwa kuu
 - 3) Muunganikano huu wa kawaida wa utoaji sadaka (yaani., damu ya mwana kondoo kufanya ukumbusho wa kifo cha malaika) na sikukuu ya mavuno katika madhabahu kuu ilitimizwa kwenye mwezi wa karibu na mwezi wa tatu au nne 14 na 15-21
 - C. Mfano wa umiliki wa wazaliwa wote wa kwanza wa watu na wanyama na ukombozi wao umeelezwa katika Kut. 13
- II. Wajibu wa kihistoria wa kushikilia mila na desturi
- A. Pasaka ya kwanza ilisherehekewa huko Misri, Kutoka 12
 - B. Katika mlima Horeb/Sinai, Hesabu 9
 - C. Pasaka ya kwanza ilisherehekewa huko Caanan (Gilgal) Yosh. 5:10-12
 - D. Kipindi cha Sulemani cha kuwakufisha hekalu, 1 Fal. 9:25 na 2Nya. 8:12 (yamkini, lakini haijaelezwa rasmi)
 - E. Ile moja wakati wa kutawala kwa Hezekia
 - F. Ile moja wakati wa mageuzi ya Yoasi
 - G. Angalia 2 Fal. 23:22 na 2 Nya. 35:18 inatajwa wakati wa Israel kukataa kuitunza hii sikukuu ya

mwaka.

III. Umuhimu wake

- 1) Hii ni moja kati ya siku tatu za sikukuu ya mwaka iliyohitajika (kama vile Kut. 23:14-17; 34:22-24; Kumb. 16:16):
 - 2) Pasaka/ mikate iliyotiwa chachu
 - 3) Sikukuu za wiki
 - 4) Sikukuu za vibanda
- A. Musa alionyeshwa kabla siku itakayoangaliwa katika madhabahu kuu(kwa vile palikuwepo na sikukuu zingine mbili) katika kumbu kumbu la torati
- B. Yesu alitumia wasaa la chakula cha pasaka ya mwaka (au siku kabla) kuthihirisha Agano Jipya katika mfano wa mkate na divai, lakini hakutumia mwana kondoo.
- 1) Chakula cha pamoja
 - 2) Sadaka ya ukombozi
 - 3) Umuhimu wa kuendeleza katika kizazi kijacho.

☐ **“usiku”** Malaika wa Kifo alipopita usiku wa manane (BDB 538), Farao alisema, “ondokeni tokeni” (kama vile Kut.12:31-33). Wana wa Israeli waliondoka haraka.

16:2 “katika kundi la kondoo na la ng'ombe” Linganisha Kut. 12:5 na II Nya. 30:24; 35:7, ambayo inatoa mwanya wa kutoa sadaka ya kondoo au mbuzi kwa aina ya wanyama wafugwao wote.

☐ **“mahali atakapochagua Bwana apakalishe jina lake”** Katika Misri hii ilikuwa huduma ya kifamilia; katika Kumbukumbu la Torati ilitunzwa kwa ajili ya mahali patakatifu pa kuabudia (kama vile 12:5,11,13,14,18,21,26; 14:23,25; 15:20; 16:2,6,7,11,15,16; 17:8,10; 18:6; 23:16; 26:2; 31:11).

16:3 “mikate isiyotiwa chachu” Wana wa Israeli hawakusubiri hata asubuhi kwa ajili ya mkate ili kuondoka. Maelezo haya ya sikukuu ya Pasaka ya Safari yanaunganishwa na sikukuu ya kilimo (kama vile Kut. 12:15-20; 23:14-17; 34:18).

Mikate iliyotiwa chachu, ambayo kwa kawaida ilikuwa ikitumika katika mambo yahasuyo sadaka (kama vile Law. 7:13; 23:17), ilikuja kuwa kielelezo cha dhambi na uasi. Mkanganyiko ulionekana katika kielelezo cha sikukuu kama nafasi ya kila Mwisraeli kusisitiza kuyaangalia maisha yao kwa ajili ya dokezo lolote la uasi au kutomtii YHWH. Kama siku ya upatanisho (Mambo ya Walawi 16) ilifanya kazi kwa kiwango cha kitaifa, Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu ilifanya kazi kwa mmoja mmoja au kwa kiwango cha familia.

Sikukuu hizi zilizohitajika kila mwaka ziliunganishwa na sikukuu ya Pasaka ili kuutumia ukombozi wa neema ya YHWH hata kabla ya ufahamu na mioyo ya watu wake. Kama neema na ahadi ya ukombozi uliotolewa kutoka Misri, ndiivyo Israeli ilivyotegemea sifa za kiroho zisizobadilika ili kumtumikia kadri miaka ilivyozidi kusonga mbele (kama vile 4:9).

☐ **“mikate ya mateso”** Tazama Kut. 12:8.

☐ **“(kwa maana ulitoka nchi ya Misri kwa haraka)”** Wayahudi waliondoka haraka kwa maombi ya Farao (kama vile Kut.12:31-33).

☐ **“upate kukumbukaMisri”** Pasaka ina umuhimu kihistoria na kitheolojia. Katika Misri tendo la Pasaka lilijikita katika ngazi ya kifamilia; katika Kumbukumbu la Torati ilikuwa kivuli cha ujio wa huduma ya mahali patakatifu; katika siku za Yesu ilikuja kuwa muungano wa zote (sehemu katika hekalu na sehemu ya nyumbani au walipokaa mahujaji walipokuwa katika Yerusalemu).

16:4 Kumbuka, Musa anawaeleza, kwa sehemu kubwa, ni wana wa kizazi kilichotoka Misri. Mstari huu unadokeza kwamba lazima kila kizazi kijiweke sehemu ya kwanza ya kizazi ambacho kina uzoefu wa nguvu na uwepo wa

Mungu, bado waliasi na kufia jangwani. Kila sikuku za mwaka zilikuwa ni kwa ajili ya kuwasaidia Israeli kutumainia zaidi uwepo wa YHWH na utoaji. Yeye alikuwa pamoja nao na kwa ajili yao, kama alivyokuwa na baba zao.

16:5 “ndani ya malango yako yote” Kiuhalisia hilini neno “malango” (BDB 1044, kama vile 12:15,17,21), ambapo linarejelea wakati ujao baada ya Israeli kuishinda Kanaani (kama vile mst. 18).

16:6 “katika machweo ya jua” Kwa wana wa Israeli huu ulikuwa ni mwanzo wa siku mpya (kama vile Mwanzo 1, kama vile Kut. 12:6.).

16:7 “Nawe umwoke na kumla” Kwa Kiebrania kifungu hiki kinaweza kumaanisha “chemsha” au “pika” (BDB 143, KB 164, *Piel* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU), lakini kwa sababu ya Kut. 12:8-9, lazima kimaanishe “kuokwa.”

☐ **“ugeuke uende hemani mwako”** Hii inaweza kumaanisha: (1) mazingira ya kutangatanga jangwani (au hasa katika nyanda za Moabu); (2) mahujaji waliokwenda Yerusalemu walikaa katika mahema wakati wa siku hizi saba za sikukuu; au (3) ni nahau inayomaanisha “rudi nyumbani mwako.

16:8 “mkutano mtukufu kwa Bwana, Mungu wako” Sikukuu ilimalizika kwa mazingira ya kuabudu kwa ushirika (kama vile Kut. 12:16, “mkutano mtukufu”). Kusudi mojawapo la mahali patakatifu lilikuwa ni kuimarisha utambulisho wa ushirika na jamii.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 16:9-12

⁹Jihesabie majuma saba; tangu wakati uanzao kutia mundu katika mmea utanza kuhesabu majuma saba. ¹⁰Nawe sikukuu ya majuma umfanyie Bwana, Mungu wako, kwa kutoa sadaka ya hiari ya mkono wako, utakayotoa kwa kadiri akubarikiavyo Bwana, Mungu wako; ¹¹nawe utafurahi mbele ya Bwana, Mungu wako, wewe na mwana wako na binti yako, na mtumwa wako na mjakazi wako, na Mlawi aliye ndani ya malango yako, na mgeni, na yatima, na mjane aliyefiliwa na mumewe, walio katikati yako, katika mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako, apakalishe jina lake. ¹²Nawe kumbuka kwamba ulikuwa mtumwa huko Misri; tena zishike amri hizi kwa kuzifanya.

16:10 “sikukuu ya majuma” Hii pia iliitwa (1) sikukuu ya mavuno katika Kut. 23:16) na (2) sikukuu ya malimbuko katika Hes. 28:26. mwishowe, ikawa Pentekoste (waalimu wa Kiyahudi wanaiunganisha na kutolewa kwa Sheria juu ya Mlima Sinai), inayomaanisha “siku hamsini.” Ilikuwa ni sikukuu ya mavuno ya mwezi wa tano- sita au kipindi cha mavuno ya ngano. Mtoaji alikuwa ni YHWH, si *Ba'al* !

☐ **“sadaka ya hiari”** Hii iliwaruhusu watu kuleta sadaka kwa kadri namna Bwana alivyombariki kila mmoja (kama vile mst. 17). Hii ni kanuni ya kiulimwengu kuhusu utoaji (kama vile II Wakorintho 8-9).

16:11 YHWH anamtaka kila mmoja ayatambue matendo yake yaliyopita kwa Israeli na uangalizi wake maalumu kwa wale wahitaji (kama vile mst.14; 12:12,18,19; 14:27,29; 26:11-13).

16:12 “nawe kumbuka” Sababu ya kitheolojia kuhusu Sikukuu ya Majuma (mavuno ya kilimo) ilikuwa ni tukio la utumwa wa Israeli katika Misri.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 16:13-15

¹³Fanya sikukuu ya vibanda siku saba, utakapokwisha kuyakusanya yatokayo katika sakafu yako ya nafaka, na katika kinu chako cha divai; ¹⁴nawe utafurahi katika sikukuu yako, wewe, na mwanao, na binti yako, na mtumwa wako, na mjakazi wako, na Mlawi, na mgeni, na yatima, na mjane aliyefiliwa na mumewe, walio ndani ya malango yako. ¹⁵Siku saba mfanyie sikukuu Bwana, Mungu wako, mahali atakapochagua Bwana; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, atakubarikia katika maongeo yako yote, na katika kazi zote za mikono yako,

16:13 “Sikukuu ya vibanda” Sikukuu ya Vibanda ilikuja kukokosa nguvu na ilikuwa kipindi cha mavuno (kama vile Kut. 23:16; 34:22; Law. 23:33-43).

Maelezo ya awali ya neno “vibanda” yanaeleza kufunua uzoefu wa wana wa Israeli juu ya:

1. maisha ya kilimo katika Misri, ambapo vibanda vilijengwa mashambani wakati wa mavuno
2. kuishi katika nyumba za muda (yaani, mahema) wakati wa kutoka Misri na kipindi cha kutangatanga jangwani
3. makazi ya muda kwa ajili ya mahujaji kukaa mahali patakatifu (ina uwezekano mdogo)

16:15 YHWH anataka kuwabariki watu wake ili waweze kufurahia (BDB 970, KB 1333, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) mmoja mmoja, kama familia, na kama watu wa Mungu (kama vile 12:7,12,18; 14:26; 16:11,14; 26:11; 27:7).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 16:16-17

¹⁶ Mara tatu kwa mwaka na watokee wanawaume wako wote mbele za Bwana, Mungu wako, mahali atakapochagua; katika sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu, na katika sikukuu ya majuma, na katika sikukuu ya vibanda; wala wasitokee mbele za Bwana mikono mitupu. ¹⁷ Kila mtu na atoe kama awezavyo, kwa kadiri ya baraka ya Bwana, Mungu wako, alivyokupa.

16:16 “Mara tatu kwa mwaka na watokee wanawaume wako wote” Kifungu cha 16 na 17 ni maelezo ya vifungu ambavyo vinasimulia sikukuu zote tatu (kama vile Kut. 23:14,17). Kumbuka milo ilikuwa ni ya wakati maalumu wa urafiki na ushirika wa kifamilia. Sikukuu hizi ziliwaruhusu Waisraeli:

1. kuimarisha maana ya jamii za kitaifa
2. kufundisha matendo makuu ya Mungu kwa vizazi vipya
3. kuwasaidia masikini na wahitaji
4. kuufurahia wema wa Mungu wa Israeli na utimilifu wake wa agano la ahadi/baraka

Kwa nini wanaume pekee? Je! hili linaifunua tabia ya unyenyekevu wa wanamke? Hakika Mashariki ya Kale ya Karibu haikuwa huru, bali wanawake walikuwa wanaheshimiwa ndani ya Israeli (mf. Mithali 31).

Nafikiri kuna aina mbili za uwezekano mzuri:

1. wanawamke walikuwa wakihitajika nyumbani katika shamba la mifugo na katika mazingira ya kilimo, hasa pindi wanaume hawapo
2. utendaji pekee wa wanaume uliweza kutambuliwa kwa alama ya Ibada ya Israeli kama tofauti kutoka Ibada ya Ustawi kwa Wakanaani, ambapo wanawake walitarajiwa

Kwa mjadala mzuri, mfupi wa hizi sikukuu tatu za kila mwaka za mahujaji tazama Roland de Vaux, *Ancient Israel*, juzuu 2, kr. 484-502.

☐ **“sikukuu”** Neno hili la Kiebrania (BDB 290, KB 290), Vyote kwa pamoja KITENZI na NOMINO, vinarejelea moja ya siku tatu za ibada za kila mwaka katika mahali patakatifu. Inaweza kutafsiriwa “sikukuu ya hija.”

16:17 “atoe kama awezavyo” Hii inarejelea kanuni ya ulimwengu ya utoaji—kila mmoja atoe kama apendavyo (kama vile mst. 10; II Wakorintho 8-9).

ANDIKO LA NSAB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 16:18-20

¹⁸Weka waamuzi na maakida katika malango yako yote akupayo Bwana, Mungu wako, kwa hesabu ya kabila zako; nao wawaamue watu kwa maamuzi ya haki. ¹⁹ Usipotoe maamuzi; wala usipendeleo uso wa mtu; wala usitwae rushwa; kwa kuwa rushwa hupofusha macho ya wenye akili, na kugeuza daawa ya wenye haki. ²⁰ Yaliyo haki kabisa ndiyo utakayoyafuata, ili upate kuishi na kuirithi nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.

16:18-20 Hii ni sehemu inayotenganisha ambayo inaendana na sura ya 18. Inahusika na maongozi kwa ajili ya uongozi wa kiraia (waamuzi wa kikabila, waamuzi wa Kilawi, wafalme, makuhani, na manabii).

16:18 “Weka waamuzi na maakida katika malango yako yote” Hawa ni kama wale wazee wa malango (mf. 21:19; 22:15; Amosi 5:10,12,15). Musa alikuwa mwamuzi mkuu, lakini alichagua wasaidizi (kama vile Kumb. 1:9-18; Kut.18:13-27).

16:19 “usipotoe” Kifungu hiki kinataja miongozo mitatu kwa ajili ya waamuzi, wasaidizi wa Musa:

1. Usipotoe maamuzi (BDB 639, KB 692, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Kut. 23:6; 27:19; Kumb. 16:19; 24:17; 27:19)
2. Wala usipendeleo uso wa mtu (BDB 647, KB 699, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, hasa kwa kiebrania ni “usimtamame usoni”)
3. Wala usitwae rushwa (BDB 542, KB 534, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Kumb. 27:25).

☐ **“rushwa”** Rushwa hutenda mambo mawili:

1. “hupofusha macho ya wenye hekima” - BDB 734, KB 802, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Kut. 23:8; ni stiaji kwa ajili ya nguvu ya fedha
2. “hupotosha (dhahili ‘geuza’) maneno ya mwenye haki” - BDB 701, KB 758, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Kut. 23:8; kumbuka neno “adilifu” au “haki” linatokana na neno, “futi kamba” (tazama Mada Maalumu katika 1:16). Maneno makuu kwa ajili ya dhambi katika Biblia ni mchezo wa maneno kwenye dhana hii hii.

16:20 “haki” maneno “haki” katika mst. 20 na “haki” katika mst. 18 ni kutoka katika asili ile ile ya Kiebrania (BDB 841), ambayo inaongelea kiwango. Mwaamuzi anaongoza kufuatana na kiwango ambacho kimefunuliwa kwa mapenzi ya Mungu (“haki, *na haki pekee*”). Viongozi (mahali maalumu na waamuzi makuhani) walitakiwa kuonyesha rehema, kutopendeleakwa YHWH (kama vile Kut. 23:6-8).

☐ **“ndiyo utakayoyafuata”** KITENZI hiki (BDB 922, KB 1191, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kimetumika dhahili katika Kumb. 11:4; 19:6, lakini hapa ni utaratibu wa baraza la Israeli. Stiaji nyingine iliyotumika hapa inapatikana katika Zab. 34:14; Mit. 21:21; Isa. 51:5; na Hosea 6:3.

☐ **“ili”** umiliki wa Israeli katika nchi na ahadi/Baraka za YHWH zilitolewa (kama vile 4:1,25-26,40; 5:16,29,33; 6:18; 8:1; 11:8-9,18-21; 16:20; 32:46-47).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 16:21-22

²¹Usipande mti uwao wote kuwa Ashera kwako kando ya madhabahu utakayofanya ya Bwana, Mungu wako. ²²Wala usisimamishe nguzo; ambayo Bwana, Mungu wako, aichukia.

16:21 Kumbukumbu la Torati 16:21, 22 na 17:1 ni aya moja. Aya hii inahusika na njia zifaazo za sadaka za kuteketezwa. Kwa ajili ya maelezo mafupi ya ibada za Wakanaani tazama Alfred J. Hoerth, *Archaeology and the Old Testament*, kr. 219-222 na William Foxwell Albright, *Archaeology and the Religion of Israel*, kr. 67-92.

☐ **“Usipande mti..... uwao wote kuwa Ashera”** Huu “msitu” au Ashera unadokeza msitu wa miti au mashimo kwenye madhabahu za Wakanaani ambapo walichonga mihimili, au miti iliyo hai kuwakilisha mke wa miungu ya kiume ya ustawi, iliyowekwa. Hili linamaanisha ibada ya ustawi. Tazama muhtasari katika 12:3.

16:22 “Wala usisimamishe nguzo” Tazama muhtasari katika 12:3.

☐ **“Mungu wako aichukia”** Tazama muhtasari katika 12:31.

MASWALI YAMJADALA

Huu ni mwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Bwana alitaka wawe na mikutano mitatu kila mwaka?
2. Je sikukuu zote tatu zilisimulia kilimo? Je hii inadokeza kwamba Musa alichukua sikukuu zilizokuwepo tayali na kubadilisha makusudi yake?
3. Orodhesha na kuelezea sikukuu hizi.
4. Orodhesha sheria tatu kwa ajili ya waamuzi.
 - a.
 - b.
 - c.
5. Ni kwa namna gani 16:21-22 inahusiana na 17:1?

KUMBUKUMBU LA TORATI 17

MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Haki sharti isimamiwe (16:18-17:13)	sheria zinazoshughulikia haki Na dini (16:18-17:20)	Usimamiaji wa haki (16:18-17:13)	Matumizi mabaya ya ibada (16:21-17:7)
16:21-17:1	16:21-17:1	16:21-17:1	16:21-17:1
17:2-7	17:2-7	17:2-7	17:2-7
17:8-13	17:8-13	17:8-13	Waamuzi wa Kilawi 17:8-13
Kanuni zilizowaongoza Wafalme		Maelekezo kuhusiana na mfalme	Wafalme
17:14-17	17:14-20	17:14-20	17:14-15
17:18-20			17:16-20

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 17:1

¹Usimchinjie Bwana, Mungu wako, ng'ombe wala kondoo aliye na kilema, wala neno ovu lo lote; kwa kuwa hayo ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako.

17:1 “aliye na kilema” Kimuktadha huu mstari unahusiana na 16:21-22, ambao pia unashughulika na mahali sahihi na aina ya utoaji dhabihu. Katika agano la Kale neno “kilema” (BDB 548) linarejelea kitu chochote chenye kuwa na tatizo kwenye mwili wake (k.v. 15:21; Law. 22:20-25). Malaki 1:6-8 inaandika mfano wa Israel kumtolea Mungu kidogo kati ya vingi walivyokuwa navyo.



NASB “ni machukizo”
NKJV “ni chukizo”
NRSV “chukizo”
TEV “hayo ni machukizo ”
NJB “chukizo”

Neno hili (BDB 1072) limejadiliwa katika 14:3.

☐ **“Bwana, Mungu wako ”** Hiki ni kifungu cha kimaagano kilichozoeleka kitumikacho na YHWH na *Elohim*. Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 17:2-7

²Ikiwa ameonekana katikati yako, ndani ya malango yako mojawapo, upewayo na Bwana, Mungu wako, mtu mume au mke afanyaye yaliyo maovu machoni pa Bwana, Mungu wako, kwa kuvunja maagano yake, ³ naye amekwenda kutumikia miungu mingine na kuiabudu, au jua, au mwezi, au vilivyo katika jeshi la mbinguni vyo vyote, nisivyoagiza mimi; ⁴ukiambiwa hayo nawe umeyasikia, ndipo utafute kwa bidii, na tazama, ikiwa ni kweli lina hakika jambo lile, kuwa yafanywa machukizo kama hayo katika Israeli; ⁵ ndipo umchukue nje malangoni kwako, yule mtu mume, au yule mwanamke, aliyefanya jambo lile ovu; ukawapige kwa mawe, wafe. ⁶ Huyu atakayeua na auawe kwa midomo ya mashahidi wawili, au mashahidi watatu; asiua kwa mdomo wa shahidi mmoja. ⁷Mikono ya wale mashahidi na iwe juu yake kwanza kwa kumwua, kisha mikono ya watu wote.

Uondoe vivyo uovu katikati yako.

17:2-13 Mistari hii inashughulika na utoaji haki. Mistari ya 2-7 inashughulika na ibada ya sanamu na shuhuda za kisheria. Mistari ya 8-13 inashughulika na muundo wa kiutendaji wa mahakama.

17:2

NASB “afanyaye yaliyo maovu”
NKJV “atendaye uovu”
NRSV “afanyaye yaliyo maovu”
TEV “aliyetenda dhambi”
NJB “yeye atendaye yaliyo maovu”

Hiki kifungu ni *Qal* KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 793 I, KB 889) na YAMBWA TENDWA (BDB 948). Hizi ni asili mbili za konsonanti zilizo za kawaida , ער chenyeye kumaanisha “baya,” “ovu,” “majonzi,” “huzuni,” “jeraha,” au “majanga.” Hapa muhtadha unarielezea kama (1) “kulikosea agano Lake,” mst. 2 (BDB 716, KB 778, kiuhalisia ni “pasaka”) na (2) “wamekwenda kuitumikia miungu mingine na kuiabudu,” mst. 3:

1. “wamekwenda” - BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. “kuitumikia” - BDB 712, KB 773, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. “kuiabudu” - BDB 1005, KB 295, *Hishtaphel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

☐ **“kwa kuvunja maagano yake”** KITENZI hiki (BDB 716, KB 778, *Qal* KITENZI CHA MUUNDO WA MANENO) kimsingi kinamaanisha “kupita juu yake” au “kupita katikati.” Mara nyingi kimetumika kwa maana ya uwazi, lakini wakati mwingine kwa maana ya kithiolojia. Mwanzoni kabisa kingeweza kurejelea kwenye tendo la kumgawa mnyama vipande viwili kama tendo la kimaagano na kupita kati ya vile vipande (mf., Mwa. 15:17). Kulivunja agano matokeo yake yalikuwa kifo au maangamizi (yaani., kama mnyama kumgawa vipande viwili). Iliamaanisha ukiukaji wa matendo ya wazi yaliyoelezewa (yaani., mapatano ya agano, k.v. 26:13; Yosh. 7:11,15; Amu. 2:20; II Fal. 18:12; Yer. 34:18-19; Hos. 6:7; 8:1).

17:3 “au jua, au mwezi, au vilivyo katika jeshi la mbinguni vyo vyote” Babeli ya kale ilikuwa ya kwanza, lakini sio ya mwisho, kuviona vitu vya kimbungu vikiwakilisha miungu au miungu ya kike (k.v. 4:19; II Fal. 17:16; 21:3,5; 23:4-5; II Nya. 33:3,5; Yer. 8:2; 19:13). Walidhani kuwa nuru iliyoko angani yaweza kuidhibiti hatma ya mwanadamu

(kimwili na kiroho).

17:4 Huu mstari unafanana na ule wa 13:14. KITENZI “ndipo utafute kwa bidii” (BDB 205, KB 233, *Qal* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU) kinadokeza uchunguzi kamili (k.v. 13:14; 17:4,9; 19:18; Law. 10:16; Amu. 6:29). Shutuma na maarifa ya upande wa pili hayakutosha kumtia mtu hatiani. Muundo wa kimahama wa Israeli ulikuwa mkali (“kupigwa mawe hadi mauti,” mst. 5), lakini wenye maelezo ya kutosha.



NASB, TEV “ikiwa ni kweli”
NKJV “hakika ikiwa ni kweli”
NRSV “hukumu imethibitika kuwa kweli”
NJB “imepetikana kuwa kweli na kuthibitika”

Nahau ya Kiebrania (KIAMBATA cha kubuni, BDB 243 II, b na NOMINO BDB 54) kimerudiwa mara tatu katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (yaani., 13:14; 17:4; 22:20).



NASB “kitu kichukizacho”
NKJV “kuwa hivyo ni chukizo”
NRSV “ni kitu cha kukataliwa”
TEV “ni kitu kiovu”
NJB “ni kitu kichukizacho”

Neno lile lile (BDB 1072) limetumika katika 17:1, ambapo linarejelea sadaka iliyo na dosari. Hapa inarejelea kwenye ibada ya sanamu (yaani., “jeshi la mbinguni”).

☐ “Israeli” Tazama Mada Maalum katika 1:1.

17:5 “malangoni mwako” Kifungu hiki kinamaanisha “kwenye eneo lako.” Hapa ni mahali ambapo wazee waliweza kuketi.

☐ “wapigwe kwa mawe wafe” Huu ulikuwa ni muundo wa adhabu ya pamoja (k.v. mst. 7). Kila mwanakaya kwenye jumuiya alitenda ili kujiondoa kwenye uovu (tazama maelezo kamili katika 13:10).

☐ Andiko la Kiebrania lina mtiririko wa VITENZI vyenye kurejelea habari za kifo katika mistari ya. 5-7:

1. “mtupieni mawe hata afe” - BDB 709, KB 768, *Qal* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, mst. 5
2. hata afe - BDB 559, KB 562
 - a. mst. 5, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
 - b. mst. 6, *Hophal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - c. mst. 6, *Qal* KAULI YA WAKATI ENDELEU
 - d. mst. 6, *Hophal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - e. mst. 7, *Hiphil* KITENZI JINZ CHA MUUNDO WA MANENO

Ukiukaji wa agano ulisababisha madhara makubwa (k.v. Kumbukumbu la Torati 27-29)! Uovu ndani ya jamii ulipaswa kukomeshwa.

17:6 “kwa midomo ya mashahidi wawili” Hili lilikuwa ni sharti la Musa (k.v. Hes. 35:30 na Kumb. 19:15; pia tazama Mt. 18:16; Yohana 8:7; II Kor. 13:1; na I Tim 5:19).

☐ “asiuawe kwa mdomo wa shahidi mmoja” Tazama 19:15-21 na Hes. 35:30.

17:7 “Mikono ya wale mashahidi na iwe juu yake kwanza” Yule aliyetoa ushahidi alipaswa kuwa wa kwanza kumtupia mawe (k.v. 13:9; Law. 24:14). Hivyo, na kama shahidi alisema uwongo, ndivyo Mungu angewaadhibu kwa kumwaga damu isio na hatia (yaani., kuwaua).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 17:8-13

⁸Ikiwa limezuka neno lililo zito kukupita wewe, katika maamuzi kati ya damu na damu, na kati ya daawa na daawa, na kati ya pigo na pigo, nayo yashindaniwa katika malango yako; ndipo nawe uondoke, ukwee uende mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako; ⁹uwaendee makuhani Walawi, na mwamuzi atakayekuwako siku hizo; uwaulize; nao watakuonyesha hukumu ya maamuzi; ¹⁰nawe fanya sawasawa na hukumu watakayokuonyesha mahali hapo atakapochagua Bwana; nawe tunza kufanya kwa mfano wa yote watakayokufunza; ¹¹kwa mfano wa sheria watakayokufunza, na kwa mfano wa hukumu watakayokuambia, fanya vivyo; usigeuke katika hukumu watakayokuonyesha, kwenda mkono wa kuume wala wa kushoto. ¹²Na mtu afanyaye kwa kujikinai, kwa kutomsikiza kuhani asimamaye hapo kwa kumtumikia Bwana, Mungu wako, au mwamuzi, na afe mtu huyo; nawe utauondoa uovu katika Israeli. ¹³Na hao watu wote watasikia na kuogopa, wasifanye tena kwa kujikinai.

17:8 Kesi zote zilizo ngumu (BDB 810, KB 927, *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) zilipelekwa kwa makuhani sehemu alipopachagua Bwana (k.v. 12:5,11,13). Aina hii ya kesi ngumu za kimaamuzi zimeelezwa kama:

1. “damu kwa damu” (BDB 196), ikimaanisha mauaji
2. “hukumu kwa hukumu” (BDB 192)
 - a. NRSV, “aina moja ya haki ya kisheria na nyingine”
 - b. TEV, “madai Fulani ya haki za mali”
 - c. NJB, “mgogoro wa madai”
 - d. REB, “haki za raia”
 - e. JPSOA, “sheria za kiraia”
 - f. NET Bible, “madai ya kisheria”
 - g. NIV, “madai”
3. “fimbo kwa fimbo” (BDB 619), ikimaanisha aina fulani ya mashambulizi (k.v. 21:5)

The Jewish Study Bible, uk. 405, kinadai kuwa kesi ngumu zilizohusisha ukosefu wa ushahidi. Kwa kuzipeleka hizi kesi kwa makuhani patakatifu pa patakatifu, Musa alidhani kuwa mtizamo wa Kiungu utalitambua kosa au kutokuwa na kosa kwa pande zote mbili zilizohusika.

☐ **“mahali atakapopachagua Bwana”** Kitenzi hiki (BDB 103, KB 119) kimetumika katika kitabu cha Kumbukumbu la Totati kwa ajili ya mambo mbali mbali:

1. Chaguo la YHWH la mababa wa Israeli, 4:37
2. Chaguo la YHWH la Israeli, 7:6,7; 10:15; 14:2
3. Chaguo la YHWH la sehemu ya patakatifu pa patakatifu, 12:5,11,14,18,21,26; 14:23,24,25; 15:20; 16:2,6,7,11,15,16; 17:8,10; 18:6; 26:2; 31:11
4. Chaguo la YHWH la mfalme, 17:15
5. Chaguo la YHWH juu ya ukuhani wa wana wa Lawi, 18:5; 21:5

17:9 “kuhani wa Kilawi” Andiko la Kimasoreti (Kiebrania), tafasiri ya maandiko ya kale (Kiyunani), toleo la Peshitta (Kishamu) yana hali ya uwingi, “makuhani.” Hili linaonyesha kundi la makuhani (k.v. 19:17). Hili lilikuwa ni ushahidi wa andiko la sheria za Kiyahudi kwa ajili ya wakuu wa baraza la Sinagogi (lililoundwa na Ezra).

☐ **“mwamuzi”** Andiko la Kimasoreti lina hali ya umoja. Hili linarejelea kwa mwamuzi mmoja (k.v. II Nya. 19:11 kwa ajili ya mfano wa kihistoria kuhusiana na hili) au kiongozi wa kundi la waamuzi.

17:9-12 Israeli ilipaswa kuheshimu na kutii mazungumzo yote ya kimahakama kwa sababu wanayathibitisha maamuzi ya YHWH. Tazama VITENZI vilivyotumika:

1. “kutamka wazi” - BDB 616, KB 665
 - a. mst. 9, *Hiphil* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU
 - b. mst. 10, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - c. mst. 11, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. “fanya” - BDB 793, KB 889

- a. mst. 10, *Qal* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU
 - b. mst. 10, *Qal* KITENZIJINZ CHA MUUNDO WA MANENO
 - c. mst. 11, *Qal* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU
 - d. mst. 12, *Qal* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU
3. “wafundishe” - BDB 434, KB 436
 - a. mst. 10, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - b. mst. 11, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 4. “kutomsikiza” - BDB 1033, KB 1570, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO

17:11 “usigeuke katika hukumu..... kwenda mkono wa kuume wala wa kushoto” Hii ni nahau ya Kiebrania kwa ajili ya kutoyabadilisha maamuzi na adhabu iliyotolewa na waamuzi wa Kilawi. Stiari ya aina ile ile imetumika kwenye maneno ya YHWH katika 4:2; 12:32. Mara tu mapenzi ya YHWH yanapojulikana, kwenda kushoto au kulia maana yake ni ukaidi (k.v. 5:32; 17:20; 28:14; Josh. 1:7; 23:6; II Fal. 22:2; Mith. 4:27).

17:12 “kujikina!” Neno hili (BDB 268) limetumika kuhusu kutomsikiza (k.v. 1:43; 17:12,13; 18:20,22). Mwamuzi na kuhani walikuwa ni wawakilishi wa mamlaka ya YHWH. Kwa hiyo, kuyakataa maamuzi yao ilikuwa ni kumkataa YHWH! Katika 18:20-22, ni manabii wasiotambua YHWH akinena kwa jina lake, kwa kutumia mamlaka yake!

☐ **“kuhani asimamaye hapo kwa kumtumikia Bwana”** Hii ni stiari kwa ajili ya kuhani wa Kilawi.

- ☐
- NASB, NRSV** “*utauondoa uovu katika Israeli*”
NKJV “*utamwondoa mtu mbaya katika Israeli*”
TEV “*utauondoa uovu huu katika Israeli*”
NJB “*utalazimika kuuondoa uovu huu katika Israeli*”

KITENZI (BDB 128, KB 145, *Piel* KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU) kinamaanisha kuchoma au kuunguza (k.v. Hes. 11:3). Hapa linatumika kistiari kama kwenye 13:5; 17:7,12; 19:13,19; 21:21.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 17:14-17

¹⁴ Utakapokwisha kuingia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako ukaimiliki, na kukaa humo; nawe utakaposema, Nitaweka mfalme juu yangu mfano wa mataifa yote yaliyo kando-kando yangu; ¹⁵ usiache kumweka yule atakayechaguliwa na Bwana, Mungu wako, awe mfalme juu yako; umweke mmoja katika ndugu zako awe mfalme juu yako; usimtawaze mgeni juu yako, ambaye si ndugu yako. ¹⁶ Ila asifanye farasi wake kuwa wengi, wala asiwarudishe watu Misri, ili apate kufanya farasi kuwa wengi; kwa kuwa Bwana amewaambia, Tangu sasa msirudie tena njia ile. ¹⁷ Wala asijizidishie wake, ili moyo wake usikengeuke; wala asifanye fedha zake na dhahabu kuwa nyingi mno.

17:14-20 Hii ni moja ya mistari yenye mikanganyiko katika Agano la Kale, hasa katika vitabu vitano vya Musa. Mistari inazungumzia kuhusu mfalme ajae. Wasomi wengi wa agano la Kale wa zama zetu wanasema kuwa Kumbukumbu la Torati ni kitabu kilichopatikana wakati wa mageuzi ya Yosia miaka mamia iliyopita na baadaye wakati wa kipindi cha mfumo wa kifalme, na ndipo kikaandikwa na makuhani ili kuifanya ibada iwe Yerusalem (k.v. II Fal. 22:8; II Nya. 34:14-15). Wanadai kuwa huu ni ushahidi ambao haukuandikwa na Musa kwa sababu hapana sehemu yoyote kwenye vitabu vitano vya Musa panapotaja kuhusiana na mfalme. Ni jambo lililopitwa na wakati kumrejelea Suleiman, dhahili shairi ni lazima lingaliandikwa baadaye. Siamini lolote kwenye hili! Baadhi ya mistari inayoonyesha kuwa mistari ya 14-20 sio ya kipekee kwenye vitabu vitano vya Musa ni Mwa. 17:6, 35:11; 36:31; Hes. 24:7; Amu. 8:22,23; 9:6. Tazama Mada Maalum hapo chini.

MADA MAALUM: UANDISHI WA VITABU VITANO VYA MUSA

- A. Biblia yenyewe haimtaji mwandishi (kama ilivyo kweli kwenye viatbu vingi vya Agano la Kale). Kitabu cha Mwanzo hakina kipengele cha "Mimi" kama ilivyo kwa Ezra, Nehemiah, au kipengere cha "sisi" kama

ilivyo kwenye Matendo ya Mitume.

- A. Tamaduni za Kiyahudi
1. Waandishi wa kale wa Kiyahudi wanasema ni Musa ndiye aliandika
 - a. Bin Sira *Ecclesiasticus*, 24:23, kiliandikwa yapata mwaka wa 185 K.K.
 - b. *Baba Bathra* 14b, sehemu ya buki la sheria za Kiyahudi ambayo huelezea taratibu za kiuandishi wa vitabu
 - c. Filo wa Iskanderia huko, Misri, mwana falsafa wa Kiyahudi, aliyeishi yapata mwaka wa 20 K.K. hadi mwaka wa 42 B.K
 - d. Flavius Josephus, mwana historia wa Kiyahudi, aliyeishi yapata mwaka wa 37-70 B.K
 2. YHWH Mwenyewe anaufunua ukweli wa Musa
 - a. inasemekana Musa aliandika kwa ajili ya watu
 - 1) Kutoka 17:14
 - 2) Kutoka 24:4, 7
 - 3) Kutoka 34:27, 28
 - 4) Hesabu 33:2
 - 5) Kumbukumbu la Torati 31:9, 22, 24-26
 - b. Inasemekana Mungu aliongea na watu kupitia Musa
 - 1) Kumbukumbu la Torati 5:4-5, 22
 - 2) Kumbukumbu la Torati 6:1
 - 3) Kumbukumbu la Torati 10:1
 - c. Inasemekana Musa ndiye aliyeyasema maneno ya Torati kwa watu
 - 1) Kumbukumbu la Torati 1:1, 3
 - 2) Kumbukumbu la Torati 5:1
 - 3) Kumbukumbu la Torati 27:1
 - 4) Kumbukumbu la Torati 29:2
 - 5) Kumbukumbu la Torati 31:1, 30
 - 6) Kumbukumbu la Torati 32:44
 - 7) Kumbukumbu la Torati 33:1
 3. Wandishi wa Agano la Kale wanadai alikuwa ni Musa
 - a. Yoshua 8:31
 - b. 2 Wafalme 14:6
 - c. Ezra 6:18
 - d. Nehemia 8:1; 13:1-2
 - e. 2 Mambo ya Nyakati 25:4; 34:12; 35:12
 - f. Danieli 9:11
 - g. Malaki 4:4
- B. Taratibu za Kikristo
1. Yesu anaainisha nukuu toka kwenye Torati ya Musa
 - a. Mathayo 8:4; 19:8
 - b. Marko 1:44; 7:10; 10:5; 12:26
 - c. Luka 5:14; 16:31; 20:37; 24:27, 44
 - d. Yohana 5:46-47; 7:19, 23
 2. Wandishi wengine wa Agano Jipya wanaoainisha nukuu toka kwenye Torati ya Musa
 - a. Luka 2:22
 - b. Mdo. 3:22; 13:39; 15:1, 15-21; 26:22; 28:23
 - c. Warumi 10:5, 19
 - d. 1 Wakorintho 9:9
 - e. 2 Wakorintho 3:15
 - f. Waebrania 10:28
 - g. Revelation 15:3

3. Wengi wa Makaasisi wa kantsa la mwanzo waliukubali uandishi wa Musa. Hata hivyo, Ireneaus, Clement wa Iskanderia, Origen, na Tertullian wote walikwisha kujiuliza kuhusu uhusiano wa Musa kwenye muundo uliopo wa kanuni za kanisa za kitabu cha Mwanzo (cf. D. 2. on page 3).

C. Utafiti wa leo

1. Dhahili pamekuwepo na baadhi ya matoleo ya kiuhariri kuhusu Torati (inavyoonekana ni kuifanya kazi ya kale iweze kueleweka zaidi kwa wasomaji wa leo, ambayo ilikuwa ni tabia ya waandishi wa Misri):
 - a. Mwanzo 12:6; 13:7; 14:14; 21:34; 32:32; 36:31; 47:11
 - b. Kutoka 11:3; 16:36
 - c. Hesabu 12:3; 13:22; 15:22-23; 21:14-15; 32:33na kuendelea
 - d. Kumbukumbu la Torati 3:14; 34:6
2. Waandishi wa kale walikuwa wasomi na wenye elimu ya juu. Mbinu zao hata hivyo, zilitofautiana toka nchi moja na nyingine:
 - a. Huko Mesopotamia, walikuwa waangalifu kutobadilisha kitu chochote, na hata kuzihakiki kazi zao kwa usahihi zaidi. Hapa pana kiambishi tamati cha mwandishi wa kale wa Kisumeri toka mnamo mwaka wa 1400 K.K: "Kazi imekamiliwa toka mwanzo hadi mwisho, imenakiliwa, imepitwa, kulinganishwa, na kuthibitishwa alama kwa alama."
 - b. Huko Misri walikuwa huru kuyapitia maandiko na kuyabiresha kwa ajili ya wasomaji wa leo. Waandishi wa maeneo ya elimukale huko Qumran (yaani., Magombo ya Bahari ya Chumvi) waliufuata utaratibu huu.
3. Wasomi wa karne ya 19 walidhani kuwa Torati ni mkusanyiko wa nyaraka toka vyanzo mbali mbali zaidi ya kipindi kirefu (Graff-Wellhausen). Nadharia hii ilijikita juu ya:
 - a. majina tofauti ya Mungu
 - b. Dhahiri jozi ya maneno ya kufanana katika andiko
 - c. Muundo wa fasihi wa habari
 - d. Thiolojia ya habari
4. Vyanzo vya kubuni na tarehe
 - a. Chanzo J (matumizi ya neno YHWH toka Kusini mwa Israeli) – 950 K.K.
 - b. Chanzo E (matumizi ya neno Elohim toka kaskazini mwa Israeli) – 850 K.K.
 - c. Vyanzo JE kwa pamoja – 750 B.C.
 - d. Chanzo D – 621 K.K. (kitabu cha sheria, 2 Fal. 22:8, kiligunduliwa kipindi cha mageuzi ya Yosia alipokuwa akilitengeneza upya hekalu na ndiyo muda dhaniwa wa kitabu cha Kumbukumbu la Torati, kikiandikwa na kuhani asiyejulikana wa kipindi ya Yosia kuyaunga mkono mageuzi yake.).
 - e. Chanzo P (uandishi upya wa kikuhani wa Agano la Kale, hususani kanuni za ibada na taratibu) – 400 K.K.
5. Dhahiri pamekuwepo na matoleo ya kiuhariri kwenye Torati. wayahudi wanadai kuwa alikuwa ni
 - a. Kuhani Mkuu (au mwingine wa familia yake) kipindi cha uandishi
 - b. Nabii Yereimia
 - c. Mwandishi Ezra – IV Esdras anasema aliandika upya kwa sababu nyaraka za mwanzo ziliteteketwa wakati wa anguko la Yerusalemu katika mwaka wa 586 K.K.
6. Hata hivyo, nadharia za vyanzo J. E. D. P. vinasema zaidi kuhusu nadharia zetu za fasihi za leo na namna zake kuliko ushahidi toka kwenye Torati (R. K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, pp. 495-541 and *Tyndale's Commentaries*, "Mambo ya Walawi," kur. 15-25).
7. Tabia za fasihi za Kiebrania
 - a. Jozi ya kufanana, kama Mwanzo 1 na 2, ni za kawaida katika Kiebrania. Mara nyingi maelezo ya pamoja hutolewa, yakifuatiwa na habari maalum. Hili lingeweza kuwa ni namna ya kuusema ukweli au kusaidia usimuliaji wa kumbukumbu.
 - b. Waalimu wa sheria za Kiyahudi wa kale walisema majina mawili ya Mungu yaliyokuwa yamezoeleka yalikuwa na umuhimu wa kithiolojia:
 - 1) YHWH – Jina la agano kwa ajili ya Uungu lenye kuhusiana na Israel kama Mkombozi na Mwokozi (k.v. Zab. 19:7-14; 103).

2) Elohim – Mungu kama Muumbaji, Mtoaji, na Mwezeshaji wa maisha yote hapa duniani (k.v. Zab. 19:1-6; 104).

c. Ni kawaida kwenye fasihi isio ya kibiblia ya mashariki ya karibu kwa ajili ya aina mbali mbali ya mitindo na misamiati kutokea kwenye kazi za fasihi zilizowekwa pamoja (cf. R. K. Harrison, pp. 522-526).

8. Kuna nadharia inayojitokeza kuwa palikuwepo na waandishi (sehemu mbalimbali za Israeli) wakishughulikia sehemu tofauti za vitabu vitano vya Musa kwa wakati mmoja chini ya maongozi ya Samueli (k.v. 1 Sam. 10:25). Hii nadharia mwanzoni ilipendekezwa na E. Robertson's *The Old Testament Problem*.

D. Ushahidi toka fasihi ya kale ya Mashariki ya Karibu inadokeza kuwa Musa alitumia nyaraka zilizoandikwa kwenye vigae vya vyungu au mtindo wa Kimesopotamia wa simulizi za mdomo kukiandika kitabu cha Mwanzo. Hapakuwepo na namna ya kuipunguza hamasa, bali ni jaribio la kuelezea tabia ya fasihi ya kitabu cha Mwanzo (k.v. P. J. Wiseman's *New Discoveries in Babylonia about Genesis*). Ukianza mwanzo 37, panaonyesha mtindo wa ushawishi wa Kimisri, muundo, na msamiati unaonekana kuonyesha Musa alitumia huenda uundaji wa fasihi au simulizi za mdomo toka kwa Waisraeli wa siku hizo waliokuwepo Misri na Mesopotamia. Elimu rasmi ya Musa yote ilikuwa toka Misri! Uwepo halisi wa fasihi ya vitabu vitani vya Musa haujulikani. Naamini Musa ni mtunzi na mwandishi wa sehemu kubwa ya vile vitabu vitano, ingawa angeweza kutumia waandishi na/au simulizi za mdomo. Maandiko yake yameboreshwa na waandishi. Wanahistoria na hivi vitabu vichache vya kwanza vya Agano la Kale vyenye kuaminika vimekwisha elezwa kwa mifano na wana elimukale wa sasa.

17:14 “utakaposema, Nitaweka mfalme juu yangu mfano wa mataifa yote yaliyo kando-kando yangu” KITENZI ni cha *Qa/ HALI YA KUSIHI* (BDB 962, KB 1321). Kimejirudia mara nne katika mstari wa 14 na 15. Kile cha pili ni (*Qa/ KITENZIJIINA HALISI*) na cha tatu (*Qa/ KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*) vikitumika pamoja kama njia mojawapo ya upanuzi:

1. NASB, NKJV “usiache kumweka”
2. NRSV “waweza kumweka”
3. TEV “hakikisha unamweka”

Tatizo halikuwa ni mfalme, bali mfalme “kama yalivyo mataifa yote yaliyonizunguka”! mfalme alipaswa kumwakilisha YHWH (k.v. mst. 8), na wala sio mahakama za kipagani za Kimashariki. Hili suala linashughulika na pale Israel ilipomwomba Samweli kuwa mfalme katika kitabu cha I Samueli 8.

17:15 “yule atakayechaguliwa na Bwana” Mungu ni mwenye ukuu, Yeye (na sio Israeli, k.v. mst. 14) humchagua mtu, lakini Israeli inathibitisha chaguo lake kwa maelezo yao (mf., Amu. 11:11; Hos. 1:11). Tazama mwongozo kwa ajili ya ufalme:

1. Wakati Israeli ilipoimiliki nchi, mst. 14
2. Mtu ambaye YHWH humchagua, mst. 15
3. Asiye mgeni, mst. 15
4. Hataweka imani yake katika walinzi wa kijeshi (“kujizidishia farasi”), mst. 16
5. Hatahitaji msaada toka Misri, mst. 16
6. Hataiweka imani yake kwenye kazi za kisiasa (“kujizidishia wake”), mst. 17
7. Hataiweka imani yake katika mali (“kijiongezea fedha na dhahabu”), mst. 17

Namba 4-7 hapo juu zinaonyesha maneno machafu ya Suleiman! Ni namna ya ajabu katika sheria ya Mashariki ya Karibu ya Kale kuona kuwa mamlaka ya mfalme yanawekewa mipaka, lakini Israeli ni Mungu:

1. Anaandaa mahali na utaratibu wa haki
2. Anaandaa muundo wa ibada
3. Anaweka mipaka juu ya mamlaka ya Kifalme, mafanikio na mali
4. Mfalme ni mmoja kati ya ndugu wa agano (k.v. mst. 20)
5. Ni lazima mfalme ajifunze kila mara na kuziweka sheria za Mungu katika vitendo (kibinafsi na kwa utaratibu) (k.v. mstari ya. 18-19)

17:16 “Ila asifanye farasi wake kuwa wengi” Farasi walikuwa wakimilikiwa na watawala, na sio watu wa kawaida. Farasi ilikuwa ni silaha ya mapambano kwenye vita. Kwa maneno mengine, “usiweke imani yako katika uwezo wa jeshi lako, Mimi, Mungu wako ninakulinda.”

☐ **“msirudie tena njia ile”** Yumkini hili linarejelea kwenye utumiaji wa askari mamuluki wa Kiebrania kwa ajili ya farasi. Moja ya mfano wa kihistoria ni ile jamii kubwa. Hata hivyo, katika muktadha, tena inadai kuwa mfalme ajae lazima awe muumini wa YHWH!

17:17 “Wala asijidishie wake” Hili linarejelea (1) tamaa ya madaraka au yumkini zaidi (2) vikundi vya kisiasa na kidini. Hii ilikuwa ni namna ya Mashariki ya Karibu ya Kale kutengeneza mikataba ya kutoshambuliana.

☐ **“; wala asifanye fedha zake na dhahabu kuwa nyingi mno”** Mungu alimweka mfalme kuwa Wake chini ya mchungaji. Ili awe chini ya mchungaji kamwe asijitaabishe kwa ajili ya mali au mamlaka yake binafsi.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 17:18-20

¹⁸Tena na iwe, zamani aketipo juu ya kiti cha ufalme wake, ajiandikie nakala ya torati hii katika chuo, kufuata hicho kilicho mbele ya makuhani Walawi; ¹⁹ na awe nayo, asome humo siku zote atakazoishi; ili apate kujifunza kumcha Bwana, Mungu wake, ayashike maneno yote ya torati hii na amri hizi, kwa kuyafanya; ²⁰ moyo wake usije ukainuliwa juu ya ndugu zake, wala asikengeuke katika maagizo, kwa mkono wa kuume wala wa kushoto; ili apate kuzifanya siku zake kuwa nyingi katika ufalme wake, yeye na wanawe, katikati ya Israeli.

17:18-20 Hii mistari ni maelezo ya uhusiano wa mfalme kwenye mapenzi ya Mungu yaliyodhihirishwa kwao. (yaani., Walawi).

17:18 “ajiandikie nakala ya torati hii katika chuo ” Yumkini hili linarejelea kwa mtu fulani (yaani., kuhani wa Kilawi) kutengeneza nakala kwa ajili yake (k.v. II Fal. 11:12). Huu ni mistari ule ambao tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani yalipata jina kwa ajili ya kitabu cha Kumbukumbu la Torati (yaani., amri ya pili), lakini katika muktadha mistari huu unarejelea kwenye nakala ya pili ya sheria, na wala sio toleo la sheria lililofanyiwa maboresho.

17:19 Mistari huu una sheria zenye kufuatana *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO, yenye kutiririka toka kwenye usomaji wa mfalme (BDB 894, KB 1128, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU) na hali ya kijifunza (BDB 540, KB 531, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) toka kwenye ufunuo wa YHWH wa mapenzi yake kupitia Musa (yaani., vitabu vitano vya Musa):

1. Kuhofu (BDB 431, KB 432)
2. Kuishika (BDB 1036, KB 1581)
3. Kuitenda (BDB 793, KB 889)
4. Moyo usiinuke juu ya ndugu zake (BDB 926, KB 1202, cf. 8:14)
5. Usikengeuke katika maandiko (BDB 693, KB 747)

Nakala hii ya sheria za Mungu ilitakiwa kubaki kwa mfalme (hili linarejelea kwenye KITENZI cha kwanza katika mistari wa 19, BDB 224, KB 243, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU). Hili linaaksi ufanano wa mikataba ya Wahiti, pale nakala mbili za agano zilipotengenezwa. Nakala moja iliwekwa hekaluni mwa mungu wa ndugu wa agano (hapa ni hemani mwa YHWH) na nakala nyingine ilibaki na mfalme (yaani., kusomwa kila mara ili kwamba ipatwe kutunzwa).

☐ **“maneno yote ya torati hii na amri hizi”** Tazama Mada Maalum katika 4:1.

17:20 “kushoto wala kulia” Hii ni nahau ya Kiebrania kwa ajili ya utii. Mapenzi ya Mungu yalielezwa kama “njia” au “mwongozo.” Kwa wazi iliingaliwa (na sheria). Waisraeli walitakiwa kubaki katika mwongozo huo (mf., Zab. 119:105), yenye kurejelea stadi ya maisha (mf., Mith. 6:23).

☐ “ili apate kuzifanya siku zake kuwa nyingi katika ufalme wake” Ufalme, kama ule wa kuhani mkuu, ulikuwa ukirithiwa kiukoo. Ufalme (yaani., baadaye dhana ya umasihi) ulitabiriwa kuwa katika uzao wa Yuda (k.v. Mwa. 49:10; II Samuel 7).

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa namna gani sura ya 16:21-22 inahusiana na sura ya 17:1?
2. Ni kwa namna gani haki ilisimamiwa?
3. Kwa nini mistari ya. 14-20 ni yenye mkanganyiko?
4. Ni uhusiano upi uliokuwepo wa mfalme wa Israeli na sheria?

KUMBUKUMBU LA TORATI 18

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Sehemu ya makuhani na Walawi	Ibada sahihi ya Mungu	Gawio la Makuhani	Ukuhani wa Kilawi
18:1-5	18:1-2 18:3-5	18:1-2 18:3-5	18:1-2 18:3-5
18:6-8	18:6-8	18:6-8	18:6-8
Epuka Mila mbaya		Onyo dhidi ya matendo ya Kipagani	Manabii
18:9-14	18:9-14	18:9-13 Ahadi ya Kumtuma Nabii	18:9-12 18:13-20
Nabii mpya kama Musa		18:14-15	
18:15-22	18:15-22	18:16-20 18:21-22	18:21-22

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA — 16:18 - 18:22 inahusiana na uongozi wa Israeli

- A. Waamuzi - 16:18-20; 17:8-13
- B. Mfalme - 17:14-20
- C. Makuhani/Walawi - 18:1-8
- D. Manabii - 18:9-22
 1. uongo – sura za 9-13
 2. kweli – sura za 14-22
 - a. waliopo (Musa)
 - b. wa baadaye (kabla na baada ya uhamisho)
 - c. atakayekuja (Masihi)

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 18:1-2

¹ Makuhani Walawi, kabila yote ya Lawi, wasiwe na fungu wala urithi pamoja na Israeli; watakula sadaka za Bwana zifanywazo kwa moto, na urithi wake. ² Wala wasiwe na urithi kati ya ndugu zao; Bwana ndiye urithi wao, kama alivyowaambia.

18:1 “Makuhani Walawi, kabila yote ya Lawi” Kwa mujibi wa Roland de Vaux, *Ancient Israel*, juzuu. 2, uk. 358, jina Lawi linaweza kuwa na vyanzo vipatavyo vitatu:

1. “kuzunguka zunguka,” kucheza kiibada au taratibu za kiibada kwa kucheza (sawa na kucheza kwa manabii wa Ba’ali katika I Wafalme 18:26)
2. “kusindikiza mtu” au “kuunganishwa kwa mtu mwingine,” chanzo maarufu yumkini kinatolewa katika Mwa. 29:34, pia katika Hes. 18:2,4
3. “kuazima,” “kutoa nadhiri au ahadi,” huenda neno hili linarejelewa na ni sawa na “iliyotolewa” likimrejelea mzaliwa wa kwanza wa YHWH (Hes. 3:12; 8:16) au kwa Samweli kutolewa kwa YHWH katika I Sam. 1:28

Kuna hatua kadhaa za ukuaji zinazohusika:

1. wakati wa Safari ya kutoka Misri ni mzaliwa wa kwanza kutoka kila familia aliyetolewa kwa YHWH, kumtumikia (kama vile Kutoka 13)
2. hii ilibadilishwa (Agano la Musa) kwenda kwa kabila fulani (yaani, Lawi) lililofanya kazi kama watumishi wa kipekee wa YHWH (kama vile Hes. 3:12; 8:16)
3. hii ilirekebisha katika Historia ya Israeli:
 - a. baadhi ya familia za Kilawi zilitumika katika madhabahu kuu
 - b. wengine walitumika katika madhabahu ndogo ndogo katika maeneo yao
 - c. baadaye Dini ya Kiyahudi ilipanua dhana ya walimu wa Kilawi ya maeneo madogo madogo kwenda katika walimu wa Kilawi wa maeneo hayo au waandishi lakini si lazima kutoka katika kabila la Lawi
4. kwa mjadala mzuri wa nadharia nyingine tazama (1) Kitabu cha *The Language and Imagery of the Bible*, cha G. B. Caird, uk. 70 na (2) *Ancient Israel* cha Roland de Vaux, juzuu 2, kur. 360-371

☐ “wasiwe na fungu wala urithi” Urithi wa Walawi ulikuwa wa Mungu mwenyewe (kama vile 10:9; 12:12; 14:27, 29; Zab. 16:5; 73:23-26; Omb. 3:24; Eze. 28). Katika Yohua 20-21 Walawi wanapewa sehemu ya miji 48 na ardhi inayozunguka kama miliki yao. Kati ya hii miji 48 kulikuwa na miji mingine sita ya Makimbilio, mitatu kila upande wa Yordani ambapo mtu angeweza kukimbilia ikiwa angejikuta amemuua mwenza wa agano pasipo kukusudia ili kumkimbia “mlipa kisasi wa damu.” (kama vile 19:1-13; Hes. 35:9-15).

☐ “watakula sadaka za Bwana” Kiasili Walawi wote walishiriki katika sehemu za sadaka za Israeli (kama vile mist. 6-8). Baadaye makuhani walisaidiwa kwa chakula kutoka katika madhabahu na vipande vidogo vya ardhi ya mtu binafsi iliyokuwa imezunguka miji ya Kilawi. Pia Walawi walisaidiwa na fungu la kumi la mwaka wa tatu lililokuwa likitolewa katika maeneo yao (kama vile 14:27; Hes. 18: 25-29; Neh. 10:37, 38).

Kuna baadhi ya tofauti katika namna kabila lote la Lawi lilivyokuwa likisaidiwa. Huu sio mgongano bali ni maendeleo yanayohusiana na madhabahu kuu.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA):18:3-5

³ Na hii itakuwa haki ya makuhani kwa watu hao wasongezao sadaka, ikiwa ni ng'ombe au kondoo wampe kuhani mkono, na mashavu mawili, na tumbo. ⁴ Malimbuko ya nafaka zako, na divai yako, na mafuta yako, na manyoya ya kwanza ya kondoo zako, umpe. ⁵ Kwani Bwana, Mungu wako, amemchagua katika kabila zako zote, asimame atumike kwa jina la Bwana, yeye na wanawe milele.

18:3 Tazama Mambo ya Walawi 7:28-36; Hes. 18:8-19 ambapo sehemu tofauti tofauti za sadaka zinatolewa kwa makuhani.

☐ **“mashavu”** Hii (BDB 534 I) inarejerea juu ya taya (mfupa wa taya na nyama zake zilizogandana chini, zenye kutengeneza mashavu).

☐ **“tumbo”** Neno hili (BDB 867) kimsingi linamaanisha “sehemu ya wazi” au “sehemu ya wazi ya meno” na katika muktadha huu, linarejelea kwa moja ya matumbo, yawezekana tumbo la nne linalohusu ucheuaji wa majani. Kamusi ya *Webster’s Third International Dictionary*, uk. 1922, inasema kwamba ukuta wa tumbo la nne la mifugo ulitumika katika ucheuaji kwa wa kuzalisha maziwa. Utumbo wa ndani ulichakatwa mpaka kuwa unga wa njano ambao ulitumika kwa kutengeneza siagi.

18:4 “Malimbuko ya... mafuta yako” Sehemu ya kwanza ya zabibu zilizoiva ilikuwa zawadi za watu kwa YHWH na kutoka kwake mpaka kwa Walawi/Makuhani (kama vile Hes. 18:12; Kumb. 12:17; 14:23; 18:4)

☐ **“manyoya ya kwanza ya kondoo zako”** Hitaji hili linatajwa hapa tu.

18:3-5 Wale waliofanya kazi katika madhabahu ya YHWH walipata gawio la YHWH. Watu wa sasa wanahitaji kukumbushwa kwamba:

1. Sabato
2. malimbuko ya kwanza
3. mzaliwa wa kwanza
4. fungu la kumi

Zote ni njia za Kiebrania za kuelezea umiliki wa YHWH. Haimaanishi kwamba wanadamu wanapata siku sita, mazao mengine yote yanayobakia, au tisa ya kumi ya mapato yao! Wanadamu hawamiliki cho chote na ni mawakili wa kila kitu!

Sayari na zawadi ya maisha humilikiwa na Muumbaji wake na Mtoshelezaji wake.

☐ **“Mungu amechagua”** Katika 10:8 tendo hili hili linaitwa “kutenga” (NIDOTTE, juzuu. 1, uk. 604). Aina hii hii ya mifanano inawasaidia watu wa leo kupata maana ya visawe vya kale vya kuzungumzwa na uhusiano wa kimaana.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 18:6-8

⁶ Na akija Mlawi atokaye katika malango yako mojawapo, katika Israeli yote alipokuwa akikaa, akaja kwa mapenzi yote ya nafsi yake mahali atakapochagua Bwana; ⁷ na atumike kwa jina la Bwana, Mungu wake, kama wafanyavyo ndugu zake wote, Walawi wasimamao huko mbele za Bwana. ⁸ Wawe na fungu sawasawa la kula, pamoja na haya yaliyomfikilia kwa kuuzwa urithi wa baba zake.

18:6 Walitakiwa kuwa mbadala wa “mzaliwa wa kwanza” wa Kutoka 13. Hili lilikuwa limejikita katika uamuzi wa Mungu na sio vigezo vya kibinadamu ambavyo kiuhalisia vinatokana na dhambi za Lawi, Musa na Haruni.

18:6-7 Hii iliruwahusu Walawi/makuhani kuishi nje ya Yerusalemu na upatikanaji wao katika kufundisha na juu ya kuhukumu katika kila mji. Japo walikuwa na uwezo na haki ya kufanya kazi katika madhabahu kuu pia.

18:8

NASB “isipokuwa kile atakachopokea kutoka katika mauzo ya mashamba ya baba yake”

NKJV “kuacha kitokanacho na mauzo ya urithi wake”

NRSV “ingawa wana mapato yatokanayo na mauzo ya mali ya familia”

TEV “na aweze kutunza chochote ambacho familia yake wanamtumia”

NJB “pamoja na haya yaliyomfikilia kwa kuuzwa urithi wa baba zake”

JPSOA “bila kuzingatia zawadi zake binafsi na urithi”

LXX “kuacha mauzo ya mali yake ya urithi”

REB “kuacha kile anachokirithi kutoka kwa baba yake”

Tafsiri tofauti tofauti zinaonesha uchaguzi. Huu unarejerea kuuzwa kwa mali za familia (lakini sio ardhi).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 18:9-14

⁹ Utakapokwisha kuingia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako usijifunze kutenda kwa mfano wa machukizo ya mataifa yale. ¹⁰ Asionekane kwako mtu ampitishaye mwanawe au binti yake kati ya moto, wala asionekane mtu atazamaye bao, wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri, wala msihiri, ¹¹ wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu apandishaye pepo, wala mchawi, wala mtu awaombaye wafu. ¹² Kwa maana mtu atendaye hayo ni chukizo kwa Bwana; kisha ni kwa sababu ya hayo Bwana, Mungu wako, anawafukuza mbele yako. ¹³ Uwe mkamilifu kwa Bwana, Mungu wako. ¹⁴ Maana mataifa haya utakaowamiliki huwasikiliza wanaoshika nyakati mbaya na kutazama bao; bali wewe, Bwana, Mungu wako, hakukupa ruhusa kutenda hayo.

18:10-11 Kuna mfuatano wa KAULI ENDELEVU, ambazo zinaashiria kuabudu miungu kwa Wakanaani:

1. NASB, “yeye asababishaye mwanawe au bintiye kupita katika moto” - BDB 716, KB 778, *Hiphil* KAULI ENDELEVU
2. NASB, “yeye atumiaye uchawi” - BDB 890, KB 1115, *Qal* KAULI ENDELEVU (inatumia vyote KITENZI na NOMINO)
NKJV, NET, “yeye afanyaye uchawi”
NRSV, NJB, NIV, “yeye afanyaye ushirikina”
JPSOA, “mpiga ramli”
3. NASB, “afanyaye uchawi” - BDB 778 II KB 857, *Poel* KAULI ENDELEVU
NKJV, NRSV, NJB, JPSOA, “mchawi”
NIV, “ushirikina”
NET, “mpiga ramli”
4. NASB, NKJV, NIV, “atafsiriye ramli” - BDB 638 II, KB 690, *Piel* KAULI ENDELEVU
NRSV, NJB, “mpiga ramli”
JPSOA, “mshirikina”
NET, “mpiga ramli”
5. NASB, NKJV, NRSV, NJB, JPSOA, NET, “mshirikina” - BDB 506, KB 503, *Piel* KAULI ENDELEVU
NIV, “afanyaye uchawi”
NASB, “alogaye” BDB 287, KB 287, *Qal* KAULI ENDELEVU (ikitumia vyote ni KITENZI na NOMINO)
6. NKJV, “alogaye”
NRSV, JPSOA, NIV, “yeye alogaye”
NJB, “aendaye kuloga”
7. NASB, NKJV, “mpiga ramli” (yaani, chombo) BDB 981, KB 1371, *Qal* KAULI ENDELEVU
NRSV, JPSOA, “aulizaye mapepo”
NJB, “muaguzi”
NIV, “chombo”
NET, “aaguaye”
8. NASB, NKJV, NIV, “mpiga ramli” [kudhaniwa] (yaani, mwenye maroho) BDB 981, KB 1371, *Qal* KAULI ENDELEVU (kudhaniwa)
NRSV, “aulizaye roho zingine”
NJB, “vyanzo”

JPSOA,
NET,

“roho zijulikanazo”
“afanyaye uganga”

9. NASB, NKJV,

“aitaye waliokufa”

a. BDB 205, KB 233, *Qal* KAULI ENDELEVU

b. BDB 559, KB 562, *Qal* KAULI ENDELEVU

NRSV,

“amtafutaye mungu kupitia waliokufa”

NJB, NET,

“mganga wa mizimu”

JPSOA,

“aulizaye waliokufa”

NIV,

“aulizaye waliokufa”

Kama unavyoweza kuona kutokana na tafsiri tofauti tofauti za Kingereza kwa kiasi fulani maneno haya yana mwingiliano. Maneno haya yanaonekana kurejelea aina mbali mbali za matendo ya kiibada ya kipagani, lakini maana zake kamili hazijulikani kwa wanafunzi wa leo wa Biblia. Tazamagalia mjadala mfupi katika (1) *Dictionary of Biblical Imagery*, kur. 524-528 na 608-610 na pia *Synonyms of the Old Testament* cha Robert B. Girdlestone, kur. 296-302. Picha ya ujumla ni jaribio la kujua na kufanyia kazi wakati ujao kwa ajili ya faida binafsi. Watu wa YHWH wanatakiwa kumwamini yeye na kumtumikia. Dhambi ya kale ya asili ya kifungu “mimi kwanza” ni chanzo cha matatizo yote ya mwanadamu!

18:10 “amfanyaye kijana wake au bintiye kupita katika moto” Hii ni rejea ya ibada ya mungu wa ustawi, *Moleki*. Katika Israeli mzaliwa wa kwanza (kama vile Kut. 13) alitolewa kwa YHWH ili amtumikie. Katika Kanaani mzaliwa wa kwanza alitakiwa kutolewa sadaka kwa mungu *Moleki* kwa moto kwa ajili ya kuendeleza ustawi, (kama vile Kumb. 12:31; Law. 18:21). Hata kuna simulizi moja katika 2 Wafalme 21:6 ambapo watu wa Mungu walimwabudu mungu huyu wa uongo! Pia inawezekana kwa namna fulani hili linafanana na kuujua wakati ujao (kama vile II Wafalme 3:26-27). Tazama Mada Maalum: *Moleki* katika 12:31.

☐ **“uganga”** Hii inatokana na asili ya Kiebrania ya neno “uaguzi” (BDB 890, kama vile Hes. 22:7; 23:23; Ezek. 21:21; II Wafalme 17:17). Hili ni neno la jumla linaloelezea mbinu kadhaa tofauti tofauti lakini makusudio yote katika kuamua mapenzi ya uungu kwa namna ya mwili au asili kama vile kuchunguza maini ya kondoo au kurusha mishale. Hili limejikita katika mtazamo wa kipagani kwamba kuna taarifa kuhusu ubaadaye uliofichwa katika matukio ya asili na wanadamu wenye vipawa (yaani manabii wa uongo, mfano, Yer. 27:9; 29:8; Ezek. 13:9; 22:28) kujua na kuamua juu ya ubaadaye huu.

☐ **“yeye alogaye”** Neno hili (BDB 778 II, KB 857) linafanana na neno “wingu” (BDB 777). Wataalamu wa lugha na wanafikiri kuwa neno hili linahusiana na sauti inatokana na:

1. milio ya wadudu
2. sauti ya upepo katika miti
3. asili isiyojulikana (ikiwa wingu, basi itakuwa inanahusiana na kuona)

Kifungu mfanano katika maandiko ya Musa ambacho kinakatiza matendo haya ya kipagani. 19:26-20:8 (tazama hasa 19:26). Neno hilo hilo pia linapatikana katika Waamuzi 9:37; II Wafalme 21:6; II Nyakati 33:6; Isa. 2:6; 57:3; Yer. 27:9; Mika 5:12.

☐ **“yeye apigaye ramli”** Maana ya neno hili (BDB 638 II, KB 690) haijulikani. Katika Kiashuru hili linamaanisha “kunong’ona na kutaja maneno ya kuloga” (KB 690). Mzizi huu una matumizi kadhaa:

1. nyoka - BDB 638 I
2. KITENZI katika *Piel* tu, (BDB 638 II) chenye maana:
 - a. Tendo la kuloga
 - b. atazamaye ramli
3. shaba - fedha - BDB 638 III
4. isiyojulikana - BDB 638 IV

☐ **“mchawi”** Neno hili (BDB 506, KB 503) kimsingi linamaanisha “kukata” (1) kama ilivyo katika kukatakata vipande vidogo vidogo vya viungo kwa ajili ya kutengeneza dawa ya miujiza (2) kujikata mwenyewe kama miji ya kumfanya mungu aitikie kwa haraka (yaani, matumizi ya kiashuru, kama vile I Wafalme 18:28). Neno hili lilitumika kuelezea wasaidizi wa Farao katika Kutoka 7:11 na wasaidizi wa Nebukadreza katika Dan. 2:2.

18:11 “apigaye fundo” Hii kibayana ni “kufunga vifundo,” “kuungana na,” au “kujiunganisha” (BDB 287, KB 287). Katika Zab. 58:5 na Muh. 10:11 inarejerea kufanya uchawi kwa kutumia nyoka. Utofauti kidogo unaelezea wabashiri wa Kibabeli wa uongo katika Isa. 47:8-11.

☐ **“apandishaye”** Maana ya msingi ya KAULI ENDELEU (BDB 981, KB 1371) ni “kuuliza” au “kutaka kujua.” Hapa humaanisha kuuliza kutoka katika ulimwengu wa roho (mfano, YHWH, Yosh. 9:14 au sanamu, Hosea 4:12).

NOMINO ya kwanza, “kupandisha” (BDB 15) ni ngumu kutoa maana. Baadhi wanaona ni kama ile iliyotumika katika Law. 19:31; 20:6,27 kama (1) shimo, au sehemu ya kutolea sadaka au (2) muundo wa neno “baba” ambao unarejelea ibada kwa wahenga wa kale. Huu unatafsiriwa katika LXX katika Isa. 8:19 kama “mpandisha pepo.” Kwa sababu ya hili na Isa. 29:4 baadhi wanafikiri kuwa hili linamaanisha “kuimba kwa sauti ya chini” au “kunong’onezana.” Hii inamaanisha “kuzungumza kwa sauti ya tofauti.” Hata hivyo kutokana na I Sam. 28:7-9, hii inafanana na uwezo wa kumuita mtu au kuzungumza na mtu aliyepo chini ya ardhi au kuzungumza na waliokufa au roho zilizo kuzimu, yaani kupandisha pepo.

Nomino ya pili, “mpandisha pepo” (BDB 396) ililikuwa muundo wa neno la Kiebrania “kujua” (BDB 395). Hii inamrejelea yule aliye na maarifa ya ulimwengu wa roho au aliye na mawasiliano na wale walio na maarifa ya ulimwengu wa roho (kama vile Isa. 8:19; 19:3).

☐ **“aombaye wafu”** Kifungu hiki ni muunganiko wa KAULI ENDELEU mbili za aina ya *Qal* (BDB 205, KB 233, “kuuliza” na BDB 559, KB 562, “waliokufa”). Katika muktadha huu hiki kinarejerea kuamsha pepo “waamsha mapepo.” Watu hawa ambao wanatakiwa kuwa na kipawa, watu wenye mawasiliano na wafu kwa ajili ya taarifa juu ya wakati ujao na nguvu ya kuiathiri.

Desturi zote za Kale zialiamini katika maisha baada ya kifo. Kwa muda mrefu katika Mashariki ya Karibu ya Kale hii ilikuwa na namna mbili:

1. kuabudu watu wa kale ambapo roho za wanafamilia zingeweza kuathiri wakati uliopo na ujao
2. nguvu ya vionekavyo (nyota, nguvu za asili) au ya ulimwengu wa roho (mapepo, miungu) ingeweza kutumika kujua na kuathiri hatma binafsi

18:12 “chukizo” Neno hili (BDB 1072) linatumika mara nyingi mara katika Kumbu umbu la Torati, Mithali na Ezekieli. Tazama Mada Maalum katika 14:3.

☐ **“Bwana, Mungu wako, anawafukuza mbele yako”** Hiki ni kipengele cha “vita vitakatifu.” Hiki kilifunuliwa kwa Ibrahimu kama ahadi katika Mwanzo 15:16 na dhambi zao zinaelezewa katika Lawi. 18:24-28.

18:13 “isiyo na mawaa” Hili ni neno la kidhabihu (BDB 1071) kwa mnyama asiye najisi ambaye ni “mkamilifu,” bila mawaa, na hivyo dhabihu inayokubalika (kama vile Kut. 12:5; 29:1; Law. 1:3,10; 3:1,6,9; 4:3,23,28,32;5:15,18; 6:6; n.k.). Hii inakuwa stiari ya wale wanaokubalika mbele za Mungu kwa kujiingiza katika matakwa ya agano (kama vile Mwa. 6:9; 17:1; II Sam. 22:24,26; Ayubu 1:1,8; 2:3; 12:4; Zab. 15:2; 18:23,25; Ezek. 28:15). Tazama Mada Maalum hapa chini.

MADA MAALUM: PASIPO LAWAMA, HATIA, KOSA, WALA MAWAA

A. Maelezo ya ufunguzi

1. Hii dhana kithiolojia inaelezea asili ya mwanadamu (yaani., Mwanzo 1, bustani ya Edeni)
2. Dhambi na uasi umekwisha haribu mazingira haya ya ushirika kamili (yaani., Mwanzo 3)
3. Wanadamu (wa kiume na wa kike) wanatamani urejesho wa ushirika na Mungu kwa sababu wameumbwa kwa sura na mfano wake Mungu (yaani., Mwa. 1:26-27)

4. Mungu ameshughulika na dhambi ya mwanadamu kwa njia kadhaa kwa kutumia
 - a. Watu wa Mungu (yaani., Abraham, Musa, Isaya)
 - b. mtindo wa utoaji dhabihu (yaani., Walawi 1-7)
 - c. Mifano ya ki-Mungu (yaani., Nuhu, Ayubu)
 5. Hatimaye Mungu anamtoa Masihi
 - a. Kama ufunuo kamili wake mwenyewe (kama vile Yn 1:1-14; Kol. 1:13-17; Ebr. 1:2-3)
 - b. Kama dhabihu kamili kwa ajili ya dhambi (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)
 6. Wakristo waliumbwa pasipo lawama
 - a. Wa kipekee kupitia haki ya Kristo iliyowekwa ndani yetu (kama vile Rum. 4:3,6,8,11,22,23,24; Yakobo 2:23)
 - b. Kwa mwendelezo wa kazi ya Roho (Yn 16:8-1)
 - c. Lengo la Ukristo ni kufanana kama Kristo (kama vile Rum. 8:28-30; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3; 5:23; 2 The. 2:13; Tit. 2:14; 1 Pet. 1:15), ambao katika ukweli, ni urejesho wa taswira ya Mungu iliyopotea katika anguko la Adamu na Hawa.
 7. Mbinguni ndio urejesho wa ushirika kamili wa Bustani ya Edeni. Mbinguni ndiko Yerusalemu Mpya inayotegemewa kuja nje ya uwepo wa Mungu (kama vile Ufu.21:2) kwenye ardhi iliyotakaswa (kama vile 2 Pet. 3:10). Biblia ilianza na kuishia kwenye maudhui yale yale ya:
 - a. Ushirika binafsi wa ndani na Mungu
 - b. Ndani ya muundo wa bustani (Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)
 - c. Kwa maelezo ya kinabii, uwepo na urafiki wa wanyama (kama vile Isa. 11:6-9)
- B. Agano la Kale
1. Kuna maneno mengi ya Kiebrania ya aina tofauti ambayo yanachukua dhana nzima ya utimilifu, pasipo lawama, pasipo hatia ambayo yanalikuwa vigumu kuyataja na kuonyesha namna yahusianavyo
 2. Maneno makuu yanayochukua dhana nzima ya utimilifu, kutokuwa na kosa, au kutokuwa na hatia (kutokana na Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kur. 94-99) ni:
 - a. *shalom* (BDB 1022)
 - b. *thamam* (BDB 1070)
 - c. *calah* (BDB 478)
 3. Tafasiri ya maandiko ya Kiyunani (yaani., Biblia ya kanisa la mwanzo) inazitafasiri dhana hizi za Kiebrania kwa maneno ya lugha ya kawaida ya Koine yaliyotumika katika Agano Jipya (angalia hapa chini)
 4. Dhana muhimu imejikita kwenye mtindo wa utoaji dhabihu
 - a. *amōmos* (kama vile Kut. 29:1; Law. 1:3,10; 3:1,6; Hes. 6:14)
 - b. maneno *amiantos* na *aspilus* pia yana vidokezo vya kimadhehebu
- C. Agano Jipya
1. Dhana ya kisheria
 - a. Kidokezo cha sheria cha kimadhehebu ya Kiebrania kimetafasiriwa kwa neno *amōmos* (kama vile Efe. 5:27; Fil. 2:15; 1 Pet. 1:19)
 - b. Vidokezo vya sheria za Kiyunani (kama vile. 1 Kor. 1:8; Kol. 1:22)
 2. Kristo yule asiye na dhambi, lawama, hatia (*amōmos*, kama vile. Ebr. 9:14; 1 Pet. 1:19)
 3. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kumfuata Yeye (*amōmos*, kama vile. Efe. 1:4; 5:27; Fil. 2:15; Kol. 1:22; 2 Pet. 3:14; Yuda 1:24; Ufu. 14:5)
 4. Dhana hii pia inatumiwa na viongozi wa kanisa
 - a. *aneglētos*, "pasipo mashtaka" (kama vile 1 Tim. 3:10; Tit. 1:6-7)
 - b. *anepileptos*, "zaidi ya shutuma" au "hapana nafsi ya lawama" (kama vile 1 Tim. 3:2; 5:7; 6:14; Tit 2:8)
 5. Dhana ya "kutokuwa najisi" (*amiantos*) imetumika kwa
 - a. Kwa Kristo mwenyewe (kama vile Ebr. 7:26)
 - b. Urithi wa Wakristo (kama vile 1 Pet. 1:4)

6. Dhana ya “ujumla” au “kusikika” (*holoklēria*) (kama vile Mdo. 3:16; 1 The. 5:23; Yakobo 1:4)
 7. Dhana ya kuwa “pasipo kosa,” “kutokuwa na hatia” linaelezwa kwa *amemptos* (kama vile Lk. 1:6; Fil. 2:15; 3:6; 1 The. 2:10; 3:13; 5:23)
 8. Dhana ya “kutokuwa kwenye lamama” linaelezwa kwa *amōmētos* (kama vile 2 Pet. 3:14)
 9. Dhana ya “kuwa safi,” “pasipo doa” mara nyingi zimetumika katika sura zenye moja ya maneno ya hapo juu (kama vile 1 Tim. 6:14; Yakobo 1:27; 1 Pet. 1:19; 2 Pet. 3:14)
- D. Idadi ya maneno katika Kiebrania na Kiyunani yanayoelezea dhana hii yanaonyesha umuhimu wake. Mungu ametupatia mahitaji yetu kupitia Kristo na sasa anatuita kuwa kama Yeye. Waamini kihali, kihukumu wametangazwa kuwa “sawa” “wenye haki” “wasio na lawama” kwa kazi ya Kristo. Sasa waamini wanatakiwa kumiliki nafasi yao. “Tembeeni katika nuru kama Yeye alivyo nuruni” (kama vile 1 Yn. 1:7). “tembeeni kwa thamani ya mwito wenu” (kama vile. Efe. 4:1,17; 5:2,15). Yesu ameirejesha taswira ya Mungu. Ushirika wa ndani sasa ni dhahiri, lakini kumbukeni Mungu anahitaji watu wanaoaksi tabia yake, kama Mwana wake alivyofanya, kwa ulimwengu uliopotea (yaani, mataifa). Hatukuitiwa chochote bali utakatifu (kama vile Mt. 5:20,48; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:13-16). Utakatifu wa Mungu, sio tu kisheria, bali namna uishivyo!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 18:15-22

¹⁵ Bwana, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msakilizeni yeye. ¹⁶ Kama vile ulivyotaka kwa Bwana, Mungu wako, huko Horebu, siku ya kusanyiko, ukisema, Nisisikie tena sauti ya Bwana, Mungu wangu, wala nisiuone tena moto huu mkubwa, nisije nikafa. ¹⁷ Bwana akaniambia, Wametenda vema kusema walivyosema. ¹⁸ Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru. ¹⁹ Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake. ²⁰ Lakini nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulinena, au atakayenena katika jina la miungu mingine, nabii yule atakufa. ²¹ Nawe ukisema moyoni mwako, Tutajuaje neno asilolinena Bwana? ²² Atakaponena nabii kwa jina la Bwana, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo neno asilolinena Bwana; kwa kujikinai amelinena huyo nabii, usimwogope.

18:15-22 Kitabu cha Kumbukumbu la Torati 8:9-14 kinaonesha namna isiyo sawa ya kutafuta mapenzi ya Mungu katika maisha ya mtu. Mistari 15-22 inaelezea njia sawia ya kung’amua maarifa kuhusu Mungu na makusudi yake.

18:15 “nabii kama mimi” Hili linakuwa jina la Masihi (kama vile Yohana 1:21, 25, 45; 5:46; 6:14; 7:40; Mdo. 3:22; 7:37). Yesu kama Musa “mpya”:

1. alitoa sheria ya agano jipya (kama vile Mathayo 5-7)
2. aliwalisha watu kama walivyotegemea (kama vile Yohana 6)
3. alikutana na Mungu katika Mlima (kama vile Mathayo 17)
4. aliwaombea watu wa agano (kama vile Yohana 17)

Kwa mjadala bora wa kazi ya unabii katika Israeli tazama kitabu cha *How To Read the Bible For All Its Worth* cha Gordon Fee na Douglas Stuart, kur. 184-189. Mjadala huu wa msaada unaendelea kushughulikia ufasiri wa vifungu vya kinabii na vitabu, kur. 189-204.

18:16 Hii inafunua tendo la Israeli kukutana na YHWH katika Mlima Sinai (kama vile Kut. 19- 20). Ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu ni kitu cha kupendeza sana (kama vile Kut. 20:18-21)! Watu walitaka msuluhishi!

Muktadha huu u, katika maana, kutimilizwa kwa nabii nyingi. Kiuhalisia inarejerea kurudiwa kwa huduma ya nabii katika maisha ya utaifa wa Israeli kama taifa (kama vile TEV). Mfalme na kuhani walitakiwa kutoka familia moja lakini nabii alitwa yeye mwenyewe na Mungu kuwa msuluhishi wa kati wa agano Lake kwa kila kizazi. Hata hivyo, inaelekeza kwa msemaji maalumu wa YHWH (UMOJA kwa Kiebrania, mist. 15,18 na maoni katika 34:10, yaani, Mtumwa atesekaye, Masihi). Huyu ndiye Yule aliyenenwa katika Mwa. 3:15; 49:10; II Sam. 7:12-13,16; Isa. 7:14; 9:1-7; 11:1-5; Dan. 7:13;9:25; Mika 5:2-5a; Zek. 9:9. Pia tazama katika Yohana 1:45 na 5:46.

18:17 Nahau hii hii, “wamezungumza vyema,” pia inapatikana katika 5:28, lakini sio katika Kut. 19-20. Hivyo hii haijaandikwa katika Ufunuo. Lazima tukumbuke kwamba Biblia ni sehemu tu ya neno la Mungu. Kwa imani, waaminio wanaeleza kwamba yale yote yaliyo ya muhimu kwa ajili ya maisha na mafundisho yamejumuishwa lakini hayatoshelezi. Kwa namna hii kuna mfanano wa maneno ya Yesu (kama vile Yohana 20:30; 21:25).

18:18 “Nitamwinua nabii” KITENZI (BDB 877, KB 1080, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) inatumika mara kwa mara juu ya makusudi ya kiagano ya YHWH katika historia (mfano Mwa. 6:18; 9:9,11,17; 17:7,19,21; Kut. 6:4; Kumb. 18:15,18; 28:9; Waamuzi 2:16,18; 3:9,15; I Sam. 2:35; I Wafalme 9:5; 11:14,23; 14:14; II Nyakati 7:18, n.k.). YHWH anashughulika na historia, kama nabii zenye kutabiri wakati ujao mfano wa huu wenye kumrejelea Yesu (pia tazama katika Mika 5:2) unaonyesha. Biblia ni “kitabu kitakatifu” pekee chenye kujumuisha unabii!

☐ **“Nitaweka maneno Yangu katika kinywa Chake”** Hii inarejerea kwaku yeye kuzungumzia YHWH Atazungumza kile tu ambacho YHWH atamwambia (ndicho Yesu alichokisema, kama vile Yohana 3:34; 12:49; 14:10; 17:8).

18:19 Tunawajibika kutendea kazi mapenzi ya Mungu mara moja tu baada ya kuyafahamu. Swali halisi ni kwa namna gani tunamjua yule kweli anayezungumza kwa ajili ya Mungu (kama vile 21)? Mistari ya 20-22 ni sehemu ndogo ya majibu. Kuna vigezo vingine (kama vile Kumb. 13:1-2; 18:20-22; Mt. 7; I Yohana 4:1-6). Mstari huu unanukuliwa katika Mdo. 3:22-23!

18:20-22 Mzungumzaji wa Mungu anajulikana kwa (1) anazungumza kwa jina la YHWH, na sio majina ya miungu mingine (kama vile mstari wa 20); (2) usahihi wa kauli zake (kama vile mstari 22); na (3) Kumb. 13:1-2 lazima pia iangaliwe kwasababu ya Mungu kushughulika na Israeli akikikita katika mwitikio wao wa kiroho.

Mtu anaweza kushangaa kwa namna gani wasikiaji wa kisasa wanatakiwa kumfahamu nabii ikiwa utabiri wao ni zaidi ya muda wa maisha yao. Pia vipi kuhusu unabii wenye masharti ambao unatokana na mwitikio wa toba ya kiimani wa watu wa siku hiyo wanaolengwa (yaani, Yona)?

Tathmini ya wale wanaodai kuwa kuzungumza na Mungu sio rahisi. Hapa ni baadhi ya vigezo:

1. dhima ya ujumbe
2. mtindo wa maisha wa mjumbe
3. mrandano wa ujumbe pamoja na vifungu vingine vya Biblia

Manabii wa uongo, walimu wa uongo mara kwa mara hubadilika badilika, watu wenye elimu, wanaotumia mantiki na wenye ushawishi. Katika siku zetu alama za wazungumzaji wa uongo inaweza kuwa:

1. msisitizo katika fedha
2. kujihalalisha kufanya ngono watakavyo
3. madai ya wao kuwa na nafasi za kipekee kuzungumza na Mungu

(azama *A General Introduction to the Bible* cha Norman Geisler na William Nix, kur. 241-242)

VITABU VYA MSAADA JUU YA UHALISIA WA ULIMWENGU WA ROHO

1. *Christian Counseling and the Occult* cha Kurt Kouch
2. *Demons in the World Today* cha Merrill F. Unger
3. *Principalities and Powers* cha John Warwick Montgomery
4. *Demons, Demons, Demons* cha John Newport
5. *Biblical Demonology* cha Merrill F. Unger
6. *Three Crucial Questions About Spiritual Warfare* cha Clinton E. Arnold

KUMBUKUMBU LA TORATI 19

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Mji wa Mkimbizi	Usimamiaji wa haki	Mji wa Mkimbizi	Mauaji na Miji ya Wakimbizi
19:1-3	19:1-3	19:1-7	19:1-4a
19:4-10	19:4-7		19:4b-6 19:7-10
	19:8-10	19:8-10	
19:11-13	19:11-13	19:11-13	19:11-13
Mipaka ya Mali		Mpangilio wa Mali za Kale	Mipaka
19:14	19:14	19:14	19:14
Sheria Kuhusu Ushahidi		Kuhusu Ushahidi	Ushahidi
19:15-21	19:15-21	19:15-21	19:1 19:16-21

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 19:1-3

¹Bwana, Mungu wako, atakapoyakatilia mbali hayo mataifa yenye nchi akupayo Bwana, Mungu wako, nawe ukawafuata, na kukaa katika miji yao, na katika nyumba zao; ² itenge miji mitatu iwe kwako katikati ya nchi yako, akupayo Bwana, Mungu wako, kuimiliki. ³ Itengeze njia, igawanye na mipaka ya nchi yako,

akurithishayo Bwana, Mungu wako, iwe mafungu matatu, ili kwamba kila mwenye kuaa mtu apate kukimbilia huko.

19:1 “atakapoyakatilia mbali” KITENZI hiki (BDB 503, KB 500, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinatumika katika maana kadhaa:

1. kuweka (“katilia”) agano, 4:23; 5:2,3; 7:2; 9:9; 29:1,12,14,25; 31:16
2. kuondoa, kuharibu, 12:29; 19:1
3. kuangusha (halisi, yaani., mti), 19:5; 20:19,20

☐ **“yenye nchi akupayo Bwana”** Tazama maelezo katika 1:8.

☐ **“na kukaa katika miji yao”** Maelezo ya tendo hili la Mungu kuikamilisha kazi hii mashariki mwa Mto Yordani yanaonekana katika Kumb. 4:41-43.

19:2,7 “miji mitatu” Hii ilikuwa miji ya makimbilio ya Kilawi, iliyojadiliwa katika Hes. 35; Yosh. 20, ambapo mtu aliyeshutumiwa kwa ajili ya mauaji (yaani., “muuaji”) angeweza kukimbia kwa ajili ya kujificha dhidi ya mashambulizi ya jamaa za yule aliyeuawa kwa kumwaga damu (yaani, “kisasi cha damu”). Viongozi wa miji walitakiwa kuupeleka ujumbe kwa ajili ya kupima ukweli wa jambo hilo(mistri ya 11-13) . Orodha ya miji ya makimbilio inapatikana katika Yohua 20:7-8:

1. Ng’ambo ya pili ya Mto Yordani
 - a. Bezeri huko Reubeni
 - b. Ramothi-Gileadi huko Gadi
 - c. Golani huko Manase (Bashani)
2. Kanaani
 - a. Kadeshi huko Naftali (Galilaya)
 - b. Shekemu huko Efraimu
 - c. Hebroni huko Yuda

Dhana hii ya sehemu ya usalama au miji ya makimbilio haikuwa ya kipekee kwa Israeli. Tamaduni nyingi za miji ya Mashariki ya Karibu ya Kale na Mediteranea ziliiruhusu miji hii maalum. Mara nyingi miji hii ilikuwa karibu na maeneo ya kidini ya kuabudia. Pia Israeli ilikuwa na dhana hii ya kuzitwaa “pembe za madhabahu” (kama vile Kut. 27:2; 30:10) katikati ya eneo la kuabudia (kama vile Kut. 21:14; I Fal. 1:50-53; 2:28-34). Hata hivyo, hii miji maalum ilikuwa ya kipekee kwa Israeli. YHWH alihusika na kifo cha mauaji ya wauaji wasiona hatia.

19:3 “Itengeze njia” Hiki KITENZI (BDB 465, KB 464, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) hapa kinamaanisha “kuandaa njia.”

Kuna maana zipatazo tatu:

1. umbali ulio sawa eneo lililojitenga
2. kufikika kwa haraka
3. “kuweka alama za barabara zionyes hazo pitio” (Rashi anayanukuu maelezo ya Wamakabayo)

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESWA): 19:4-7

⁴ Na hii ndiyo hukumu ya mwenye kuaa mtu, atakayekimbilia huko awe hai; atakayemwua mwenziwe pasipo kukusudia, wala hakumchukia tangu hapo; ⁵ kama aingiapo mtu na mwenziwe mwituni kwenda kukata kuni, akapeleka mkono wake na shoka ili kukata mti, likatoka shoka katika mpini, likampiga yule mwenziwe hata akafa; basi na akimbilie katika miji hii mmojawapo awe hai; ⁶ asije akaandamiwa mwuaji na mwenye kulipiza kisasi cha damu, moyo wake ukali na hasira, akampata kwa njia kuwa ndefu, akamwua; wala hana haki ya kuuawa, kwa kuwa hakumchukia tangu hapo. ⁷ Kwa sababu hii ninakuamuru, na kukuambia, Ujitengee miji mitatu.

19:4 “hukumu ya mwenye kuaa mtu” Huu ni upanuzi wa Kut. 21:12-14, ambao unahusiana na hifadhi kuu. Jambo

hili lilipanua usalama wa hifadhi kuu kwa miji sita ya makimbilio ya Kilawi.

☐ **“atakayekimbilia huko awe hai”** Ikiwa mtu alimuua mwenzake na kukimbilia (BDB 630, KB 681, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) katika miji mbalada na ikiwa mashtaka yatathibitisha kuwa hapakuwa na kusudi la kuua basi itampasa kuishi (BDB 310, KB 309, *Qal* ya KAULI TIMILIFU) ndani ya huo mji wa usalama hadi pale kitakapotokea kifo cha Kuhani Mkuu wa wakati huo (kama vile Yosh. 20:6).

☐ **“pasipo kukusudia”** Tazama maelezo katika 4:42. Hiki ni kinyume cha “tendo la mauaji ya kukusudia.”

19:6 “mwenye kulipiza kisasi cha damu” Kifungu hiki ni muundo wa maneno (BDB 145 I, KB 169, *Qal* ya KAULI ENDELEU na BDB 196, kama vile Hes. 35:9-28). Mtu huyu pia anajulikana kama “mkombozi wa ndugu wa damu” (mtu atendaye kwa niaba ya familia). Huu ni mfano mst. 21 wa kisasi kilicho na mipaka (kama vile Kut. 21:23-25; Law. 24:19-22).

☐ **“kwa kuwa hakumchukia tangu hapo”** Huu ni mwendelezo wa kithiolojia wa Mwa. 9:5-6. Hapa nia iliyo nyuma ya tendo inatazamwa kwa undani. Mauaji ya ghafla na yasiyokusudiwa yanasamehewa kutoka kisasi cha “jicho kwa jicho”. Kulikuwa na faini (ilimpasa kuishi ndani ya mji wa makimbilio hadi kutokea kwa kifo cha Kuhani Mkuu wa wakati huu). Israeli, kama alivyo YHWH, ilimpasa kuhusika na hukumu na kisasi chenye mipaka!

19:7 Musa aliwapa neno la YHWH katika mist. 1-3; anatoa maelezo katika mist. 4-6 na, kisha anaeleza upya juu ya amri ya YHWH katika mst. 7.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 19:8-10

⁸Na kama Bwana, Mungu wako, akiueneza mpaka wako kama alivyowaapia baba zako, akakupa na nchi yote aliyoahidi kwamba atawapa baba zako; ⁹ nawe ukiyashika maagizo haya yote nikuagizayo leo, na kuyafanya, kumpenda Bwana, Mungu wako, na kwenda sikuzote katika njia zake, ndipo ujiongezee miji mitatu tena, pamoja na mitatu ile; ¹⁰ isije ikamwagika damu ya asiye makosa kati ya nchi yako akupayo Bwana, Mungu wako, iwe urithi, ikawa na damu juu yako.

19:8 “kama” Hii KAULI ENDELEU isiyo na uhakika (BDB 49) inaeleza asili amrishi ya agano la YHWH pamoja na Israeli (kama vile mst. 9). Hapa anawapa eneo la ng’ambo ya pili ya Mto Yordani na ikiwa watatii atawapa nchi ya Kanaani.

19:9 “ukiyashika” Kuna KITENZI kimoja “kuyashika” (BDB 1036, KB 1581, *Qal* ya KAULI ISIYO TIMILIFU, tazama maelezo katika at 6:12) yakifuatiwa na VITENZIJIKA vya MIUUNDO YA MANENO:

1. “kuyafanya” - BDB 793, KB 889
2. “kumpenda” - BDB 12, KB 17
3. “kwenda” - BDB 229, KB 246, kama vile 10:12; 11:1,13,22; 30:16

☐ **“maagizo haya yote”** Hili neno la UMOJA (BDB 846, tazama Mada Maalum katika 4:1) linatumika kueleza juu ya mambo yote yahasuyo agano la YHWH (kama vile 4:2; 6:1; 11:8; 15:5; 19:9).

☐ **“ujiongezee miji mitatu tena”** Hii miji mitatu kuongeza ile ya mst. 2 inaonyesha miji sita ya makimbilio iliyotajwa katika Yoshua 20. Hii inarejelea (1) miji mitatu ya baadaye iliyo magharibi mwa upande wa Yordani, ambayo haijamilikiwa au (2) upanuzi wa baadaye wa Israeli wa andiko baada ya ushindi wa Yoshua (maboresho ya kihariri).

19:10 YHWH anahusika na kifo cha watu ambao hawakustahili kufa (yaani, “damu isiyo na hatia,” kama vile II Fal. 21:16; 24:4; Yer. 22:17). Katika Agano la Kale kuna tofauti kati ya utakaso wa kimaadili na wa kidini. Uhai ni wa thamani! Kuupoteza kuna madhara yake (“hatia ya damu,” kama vile Hes. 35:33-34). Haya ndiyo madhara na

uchafu mwingine wa kidini ambao ulihusika na (1) ule wa kila mwaka kupitia Siku ya Upatanisho, ilivyoelezwa katika Mambo ya Walawi 16 na (2) kwa namna ya kawaida kutoa dhabihu ya mnyama ambaye hajazaa (kama vile 21:1-9). Kama mji wa makimbilio ulivyoshughulika na matatizo ya kila mmoja, Kumb. 21:1-9 inashughulika na taratibu za kuzishughulikia hatia zilizo ndani ya jumuiya za watu.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 19:11-13

¹¹ Lakini mtu awaye yote akimchukia mwenziwe na kumwotea na kumwinukia, akampiga hata akafa; naye akakimbilia miji hii mmojawapo; ¹² ndipo wazee wa mji wake wapeleke ujumbe kumtwa huko, na kumuua katika mkono wa mwenye kulipiza kisasi cha damu, apate kufa. ¹³ Jicho lako lisimhurumie, lakini uondoe damu ya asiye makosa katika Israeli, ili upate kufanikiwa

19:11 Utambue mfululizo wa VITENZI vyenye kukueleza mauaji ya kukusudia:

1. “akimchukia” - BDB 971, KB 1338, *Qal* ya KAULI ENDELEVU, kama vile 4:42
2. “na kumwotea” - BDB 70, KB 83, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. “na kumwinukia” - BDB 877, KB 1086, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
4. “akampiga” - BDB 645, KB 697, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

19:12 “wazee wa mji wake” Kifungu hiki kinaurejelea mji ulio karibu sana na mharifu huyo ama mji wa makazi ya mtu huyo.

19:13 “Jicho lako lisimhurumie” Hii (BDB 299, KB 298, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ni dhana ya mara kwa mara iliyo katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (kv. 7:16; 13:8; 19:13,21; 25:12). Huruma ya mwanadamu au hisia za kitaifa haziwezi kuzibadili sheria za YHWH. Lazima Israeli iwe takatifu! Mafaniko ya baadaye ya Israeli (na hata kubaki kwake katika Nchi ya Ahadi) yanawekewa masharti katika utii wake.



NASB “uondoe damu ya asiye makosa katika Israeli”
NKJV “uiondoe hatia ya danu isiyo na hatia katika Israeli”
NRSV “uisafishe hatia ya damu isiyo na hatia katika Israeli”
TEV “lazima Israeli ijitoe katika mauaji”
NJB “yakupasa kuuondoa umwagaji wa damu isiyo na hatia katika Israeli”

KITENZI (BDB 128, KB 145, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinachomaanisha “kuchoma,” hapa kinatumika kistiari kumaanisha uondoaji wa jumla (kv. 13:8; 17:7,12; 19:13,19; 21:21; 22:21,22,24; 24:7).

Mauaji huuathiri uhusiano wa mtu (kama vile Mwanzo 4) na jamii (kv. 21:1-9) pamoja na baraka za YHWH. Dhambi na ubinafsi viliharibu kila kitu walichokigusa!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 19:14

¹⁴ Usiiondoe alama ya mpaka wa jirani yako, waliouweka watu wa kale katika urithi wako, utakaorithi ndani ya nchi akupayo Bwana, Mungu wako, uimiliki.

19:14 “Usiiondoe alama ya mpaka wa jirani yako” Katika ulimwengu wa kale wanakijiji walikwa wakilima ardhi kwa pamoja (yaani, kupalilia, kupanda, kuvuna). Kutokana na mtazamaji hili lilionekana kama shamba moja kubwa.

Hata hivyo, kila familia ilikuwa na shamba lake, ambalo lilikuwa limewekewa alama kwa mawe meupe. Familia hiyo, ingawa ilikuwa ikifanya kazi pamoja na wanakijiji, ilikuwa ikipokea mazao ya shamba lake. Kama mtu angeyaondoa mawe hayo, kwa kujiongezea ukubwa wa shamba (yaani, mazao), hili lilikuwa kosa dhidi ya jamii mzima na kwa YHWH, kwa sababu yeye aliwapa nchi kama urithi kwa kila kabila na kila familia (kama vile 27:17; Mit. 22:28; 23:10; Hos.5:10).

☐ **“waliouweka watu wa kale”** Hii ni aina ya usemi ambao umesababisha wanazuoni wengi kuukataa utawala wa Musa wa Kumbukumbu la Torati. Huu unaonekana kurejeea mgawanyo wa ardhi, ambao ulitokea baada ya Yoshua kuiteka ardhi (kv. Yoshua 13-19). Waandishi wa Kimisri waliyaboresha maandiko, ambapo waandishi wa Kimesopotamia hawakufanya hivyo. Waandishi wa Israeli walichukua mafunzo Misri.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 19:15-21

¹⁵ Shahidi mmoja asimwinukie mtu awaye yote kumshuhudia kwa uovu wo wote, wala kwa dhambi yo yote, katika makosa akosayo yo yote; jambo na lithibitishwe kwa vinywa vya mashahidi wawili, au watatu. ¹⁶ Shahidi mdhalimu akimwinukia mtu ye yote na kushuhudia juu yake ya upotoe; ¹⁷ ndipo wale watu washindanao kwa mambo yale na wasimame wote wawili mbele za Bwana, mbele ya makuhani na waamuzi watakaokuwapo siku hizo; ¹⁸ nao waamuzi na watafute kwa bidii; na tazama, yule shahidi akiwa shahidi wa uongo, naye ametoa ushahidi wa uongo juu ya nduguye; ¹⁹ ndipo mtamfanyia kama alivyodhani kumfanyia nduguye; ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako. ²⁰ Na watakaosalia watasikia na kuogopa, wasifanye tena uovu mfano wa huo katikati yako. ²¹ Wala jicho lako lisiwe na huruma; uzima kwa uzima, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu.

19:15 Mstari huu unaonyesha namna walivyo kuwa makini katika mambo ya kisheria (kv. 17:6; Hes. 35:30). KITENZI “kumwinukia” (BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kimetumika mara tatu katika andiko la Kiebrania katika mist. 15 na 16.

19:16 “Shahidi mdhalimu” NOMINO “mdhalimu” (BDB 329) kimsingi linamaanisha “vurugu,” lakini hapa linadokeza juu ya shahidi wa kukusudia ouvu, shahidi wa sheria za uongo (kama vile Kut. 23:1; Zab. 27:12; 5:11), hawa wananena kwa jina la YHWH (kiapo cha kisheria), huku akijua kuwa anapotosha ukweli. Mstari 19 unaonyesha madhara ya shahidi wa uongo (kama vile Kumb. 5:20 na sura 11).

NASB, NKJV,

NRSV “tenda visivyo”

TEV “mashtaka ya uongo”

NJB “tuhuma za ukanaji imani”

Neno la Kiebrania (BDB 694 II) mara nyingi linamaanisha “mtazamo wa kiuasi ambao baadaye huwa katika utendaji,” kv. 13:5; Yer. 28:16; 29:32. Hapa muktadha unamaanisha “uongo” uliokusudiwa, uliopangwa.”

19:17 “makuhani na waamuzi” Kifungu hiki kinarejelea:

1. waamuzi wenyeji, 16:18-20; 17:8-13
2. makuhani wa Kilawi wa mahali pa kujitakasia, 18:1-8

Tambua kwamba kujitokeza mbele ya waamuzi hawa walioteuliwa ni swa na kujitokeza mbele za YHWH (kv. 17:9,12).

19:18 “nao waamuzi na watafute kwa bidii” Tazama maelezo katika 13:15. Hili neno lenye kufanana (BDB 405, KB 408, *Hiphil* KITENZIJINA HALISI) pia linatumika katika 17:4.

19:19 “mtamfanyia kama alivyodhani kumfanyia nduguye” Huu ni mfano wa haki ya “tunavuna kile tulichopanda” au “jicho kwa jicho” (kv. Law. 24:19).

9:20 “Na watakaosalia watasikia na kuogopa” Kuna pingamizi la kisheria katika adhabu ya mtu binafsi toka katika jamii (kv. 13:11; 17:13).

19:21 Tazama maelezo katika mst. 13. Kifungu “jicho kwa jicho” kilichohusu haki ya Israeli, kinachoonekana kuwa cha kikatili sana (yaani, *Lex talionis*, ambacho pia ni sifa bainifu ya Mfumo wa Sheria za Hammurabi, tazama *Old*

Testament Times, na R. K. Harrison, kr. 57- 59) kilikuwa katika ukweli wa kumaanisha kustisha “vita vya kisasi” kati ya familia na makabila pamoja na kudumisha taratibu za utakaso wa watu wa Mungu wa agano.

Mtu anashangaa kuhusu namna sheria hii ilivyo tekelezwa kwa uhalisia wake. Inaonekana kwamba uharibifu wa kimwili uliondolewa kwa fidia. Hili linajikita katika muktadha wa karibu unaogusiwa na ufanano ulio katika Kut.21:23-25. Tendo la kuikumbuka upesi sheria ya awali na kuufuatisha muktadha linashughulika na fidia. Waalimu wa sheria za Kiyahudi waliofuatia walitoa mwongozo wa fidia ipasayo juu ya tendo linaloleta matokeo ya uharibifu kwa mtu. Hata hivyo, tendo la mauaji lilileta matokeo ya kuendelea kwa miiko ya kidini. Hili liliteta matokeo hasi ya agano la baraka toka kwa YHWH na lilipaswa kushughulika na usahihi wa jambo!

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mungu anauhimarisha mji wa mkimbizi?
2. Eleza dhana ya “mlipa kisasi cha damu.”
3. Ni kwa namna gani Waebrania walikabiliana na tendo la mtu kusema uongo?
4. Nini makusudi ya haki ya “jicho kwa jicho”?

KUMBUKUMBU LA TORATI 20

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Kanuni zinazoongoza vita	Sheria za kupigana vita takatifu	Kuhusiana na vita	Vita na wapiganaji
20:1-9	20:1-9	20:1-4 20:5-7 20:8-9	20:1-4 20:5 20:6 20:7 20:8 20:9 Miji iliyotekwa
20:10-18	20:10-18	20:10-15 20:16-18	20:10-14 20:15-18
20:19-20	20:19-20	20:19-20	20:19-20

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk.wa vii katika kipengele cha utangulizi) **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeee katika mwanga tuliona. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (soma mzunguko #3.uk. viii). linganisha mgawanyo wako na tafsiri nne hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu
8. Nk.

USOMAJI WA MAELEZO YALIYOPITA

- A. Sura ya 20 ni maelezo ya namna Israeli ilipaswa kuviongoza vita vitakatifu, vita iliyofanyika kwa jina la Mungu, vikiamriwa na Mungu, kwa sheria zilizoongozwa na Mungu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu (k.v. 20:1-20; 21:10- 14; 23:9-14; 24:5; 25:17-19).

- B. Matatizo ya leo yana kawaida ya aina hii ya andiko ambalo mara nyingi linahusiana na kanuni mbovu. Hata hivyo, sio haki kutumia mawazo ya leo kama kanuni na mazoezi ya vita kwa majeshi ya kale.

Jambo lingine ni tatizo la wakristo wa leo kujaribu kutumia kila andiko la Agano la kale katika siku zao. Hayakuwa mapenzi ya Mungu kwamba kila kizazi katika kila mahali kuiga tamadani za mashariki ya karibu ya kale, lakini tunatafuta mshikamano wa ukweli wa ndani juu ya matendo katika tamaduni, kisha tumia ukweli huu wa ulimwengu kwa utamaduni wetu. Kitabu kizuri katika lengo hili ni *How To Read the Bible For All Its Worth* cha Fee na Stuart.

Kwa sababu limekwishatokia na kuandikwa katika Biblia haimaanishi moja moja ni mapenzi ya Mungu kwa kila kizazi na kila tamaduni (mf, sheria za chakula, vita takatifu, ndoa ya wake wengi, utumwa, udhaifu wa mwanamke, nk.).

- C. Sura hii ni muunganiko wa rehema na ukali!

- D. Kwa ajili ya mjadala mfupi mzuri tazama Roland de Vaux, *Ancient Israel*, juzuu. 1, ukr. 258-267.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):20:1-9

¹ Utokapo kwenda vitani kupigana na adui zako, na kuona farasi, na magari, na watu wengi kuliko wewe, usiwaogope; kwa kuwa Bwana Mungu wako, yu pamoja nawe, aliyekukweza kutoka nchi ya Misri. ² Na iwe, msongepo mapiganoni, kuhani na akaribie na kusema na watu, ³ awaambie, Sikizeni, enyi Israeli, hivi leo mwasongea mapiganoni juu ya adui zenu mioyo yenu na isizime; msiche, wala msiteteme, wala msiingiwe na hofu kwa ajili ya wao; ⁴ kwa maana Bwana, Mungu wenu, ndiye awaandamaye kwenda kuwapigania juu ya adui zenu, ili kuwaokoa ninyi. ⁵ Na maakida na waseme na watu, na kuwaambia, Ni mtu gani aliye hapa aliyejenga nyumba mpya, wala hajaiweka wakfu? Aende akarudi nyumbani kwake, asije akafa mapiganoni, ikawekwa wakfu na mtu mwingine. ⁶ Ni mtu gani aliye hapa aliyepanda shamba la mizabibu, wala hajatumia matunda yake? Aende akarudi nyumbani kwake asije akafa mapiganoni, yakatumiwa na mtu mwingine matunda yake. ⁷ Ni mtu gani aliye hapa aliyemposa mke wala hajaoa? Aende akarudi nyumbani kwake asije akafa mapiganoni, huyo mwanamke akaolewa na mume mwingine. ⁸ Tena maakida na waseme zaidi na watu, wawaambie, Ni mtu gani aliye hapa tena mwenye hofu na moyo mnyonge? Aende akarudi nyumbani kwake, isije mioyo ya nduguze ikayeyuka mfano wa moyo wake. ⁹ Itakuwa hapo watakapokwisha wale maakida kusema na watu, na waweke majemadari wa majeshi juu ya watu.

20:1 “farasi na magari” Wakanaani walikuwa na farasi wengi na magari (yaani, silaha za kijeshi kwa wakati huo na mahali); Waisraeli hawakuwa nazo (k.v. Yosh. 11:4; 17:16; Isa. 31:1-3; Hos. 14:3). Waisraeli walipaswa kumtumaini YHWH ili kuwapatia ushindi, sio silaha bora (k.v. Isa. 30:15-17; 31:1-9).

☐ **“usiwaogope”** KITENZI hiki (BDB 431, KB 4387, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ni dhana iliyojirudia rudia katika muktadha wa vita takatifu (k.v. 1:21,29; 3:2,22; 7:18; 20:1,3; 31:6,8). Walitakiwa wasiogope nguvu au idadi kubwa ya maadui Wakanaani, lakini wamhofu YHWH (k.v. 4:10; 5:29; 6:2,13,24; 10:12,20; 13:4; 14:23; 17:19; 28:58; 31:12,13), kwa sababu ni Mungu wa kutisha (neno lile lile la kiebrania, k.v. 7:21; 10:17; 28:58).

☐ **“kwa kuwa Bwana Mungu wako, yu pamoja nawe, aliyekukweza kutoka nchi ya Misri”** Tazama Kut. 14:26-28 ni kwa ajili ya rejea ya ukombozi wa Mungu kwa watu wake kutoka kwa Farao. Msingi wa uaminifu kwa Israeli ulikuwa juu ya:

1. Ufunuo uliopita kwa mababa wa imani
2. Muujiza wa ukombozi toka kwa Wamisri
3. Miujiza ya kupewa chakula wakati wa kutangatanga jangwani
4. Ushindi wa ng'ambo mashariki mwa Yordan

20:2 “kuhani na akaribie na kusema na watu ” Walimu wa Kiyahudi wanamwita mtu huyu “kuhani wa vita aliyetiwa mafuta.” kabla ya vita, kuhani aliwaonya aliwataka wawe majasiri kwa sababu Mungu alikuwa pamoja nao. Na hata ikiwa mtu amekufa katika vita, bado Mungu aliendelea kuwajali na familia zao.

20:3-4 Tambua mfuatano wa maonyo kadhaa (“sikilizeni” BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI) ya kuhani katika mstari wa 3:

1. “mioyo yenu na isizime” - BDB 939, KB 1236, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini kwa maana ya KUAMURISHA, k.v. Isa. 7:4; Yer. 51:46
2. “msiche” - BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini kwa maana ya KUAMRISHA, tazama muhtasari katika mst. 1
3. “msiteteme” - BDB 342, KB 339, *Qal* KAULI YA WAKATI ISIO TIMILIFU, lakini kwa maana ya KUAMRISHA, k.v. Ayub 40:23 (mfano: I Sam. 23:26; II Fal. 7:15; Zab. 48:5)
4. “msiingiwe na hofukwa ajili ya wao” - BDB 791, KB 888, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini kwa maana ya KUAMRISHA, k.v. 1:29; 7:21; 31:6; Josh. 1:9

Sababu kwa ajili ya kujiamini inaanzia mst. 4:

1. “kwa maana Bwana, Mungu wenu, ndiye awaandamaye ” - BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEU
2. “kwenda kuwapigania ” - BDB 535, KB 526, *Niphal* KITENZI JINA CHA MUUNDO WA MANENO
3. “ili kuwaokoa” - BDB 446, KB 448, *Hiphil* KITENZI JINA CHA MUUNDO WA MANENO

20:5-8 “maakida” Hili ni neneo maalumu la kiebrania (BDB 1009) mara nyingi limetumika katika kuwaleta pamoja waamuzi wa mahali au viongozi wa kijeshi. Inamaanisha “wawakilishi toka kila kabila” (k.v. 1:15; 29:10; 31:28). Maakida walisamehe hukumu zozote zile.

Hapa kuna orodha ya hukumu zilizosamehewa ambazo mwanamme wa Israeli hakurusiwa kwenda vitani:

1. Aliyepanga nyumba mpya wala hajaiweka wakfu, mst. 5 (dhahili kwa tukio lijalo; hakuna kumbukumbu ya asili au kusudi la utaratibu huu kuandikwa katika Agano la kale, lakini neno ni lile lile kama lilivyotumika kwa ajili ya kuwekwa wakfu hekalu, BDB 335 II).
2. Aliyepanda shamba la mizabibu na wala hajatumia matunda yake, mst. 6 (dhahili kwa tukio lijalo, shamba la mizabibu huchukua miaka mitatu kuanza kutoa matunda, k.v. Law. 19:23-25).
3. Aliyemposa mke, lakini hajaoa, mst. 7, k.v. 24:5.
4. Aliye na hofu au moyo mnyonge, mst. 8, kwa sababu atasababisha wengine kuogopa, k.v. Amu. 7:3; I Mak. 3:56.

Namba 1, 2, na 3 inasimulia mambo ya urithi. Lakini yumkini pia wakaona katika nuru ya Kumb. 28:30. Mambo haya yaliyotajwa yamekuwa kama matokeo ya kutokutii agano.

☐ **“Aende akarudi nyumbani kwake ”** Tungo hii inaundwa kwa VITENZI:

1. “aende” - BDB 229, KB 246, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kama KITENZI AMRISHI
2. “akarudi” - BDB 996, KB 1427, *Qal* KITENZI AMRISHI

Vimerudiwa na kutajwa kwa kila orodha iliyosamehewa (k.v. mist. 5,6,7,8). Haukuwa ukubwa wa jeshi la Israeli, lakini ni nguvu za Mungu wao zilizofanya utofauti! Jeshi dogo na maandalizi duni, zaidi yalitukuza ushindi wa Mungu (k.v. Waamuzi 7).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 20:10-18

¹⁰ Utakaposongea karibu ya mji kwenda kupigana juu yake, ndipo utakapowapigia ukelele wa amani. ¹¹ Itakuwa utakapokujibu kwa amani, na kukufungulia, ndipo watu wote watakaonekana humo watakufanyia kazi ya shokoa, na kukutumikia. ¹² Na kwamba hautaki kufanya amani nawe, lakini utafanya vita juu yako, ndipo uuhusuru; ¹³ na Bwana, Mungu wako, autiapo mkononi mwako, mpige kila mume aliyemo kwa makali ya upanga; ¹⁴ lakini wanawake na watoto, na wanyama wa miji, na vilivyo mjini vyote, navyo ni nyara zake zote, uvitwae viwe mateka kwako; nawe utakula nyara za adui zako alizokupa Bwana, Mungu wako. ¹⁵ Utaifanyia vivyo miji yote iliyo mbali sana nawe, isiyokuwa miji ya mataifa haya. ¹⁶ Lakini katika miji ya mataifa haya akupayo Bwana, Mungu wako, kuwa urithi, usihifadhi kuwa hai kitu cho chote kipumzikacho; ¹⁷

lakini uwaangamize kabisa, Mhiti, na Mwamori, na Mkanaani, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi, kama alivyokuamuru Bwana, Mungu wako; ¹⁸ wasije wakawafunza kufanya mfano wa machukizo yao yote, waliyoifanyia miungu yao; hivyo itakuwa ni makosa juu ya Bwana, Mungu wenu.

20:10-15 Haya ni maagizo ya kukubali kushindwa kwa miji iliyokuwa mbali, miji ya pembezoni au nje ya mipaka ya nchi ya ahadi aliyowapa Mungu (yaani, nje ya mipaka ya urithi wa Israeli, k.v. mst. 15).

20:11 “watakufanyia kazi ya shokoa, na kukutumikia” Hii inafunua sehemu iliyozeleka ya vita vya mashariki ya karibu ya kale.

20:13 “makali ya upanga” ni dhahili kwa kiebrania “kwa kinywa cha upanga.” Inadokeza kwamba wanaumme wote wa umri Fulani waliuawa.

20:14 Katika ulimwengu wa kale maaskari hawakulipwa mshahara, lakini malipo yao yalikuwa mali walizoteka katika vita. Katika Israeli, hasa hasa “vita takatifu,” mateka walikuwa ni wa YHWH ili kuonyesha kwamba ushindi ulikuwa wake na kuwa nchi ni yake. Mistari hii inapingana kwa sababu miji hii ilikuwa nje ya nchi ya ahadi.

☐ **“wanawake”** hata mateka waliokamatwa walikuwa na haki (k.v. 21:10-14).

20:16-18 Mistari hii inarejelea miji iliyo ndani mwa nchi ya ahadi. Miji hii iliagamizwa kabisa (k.v. mist. 16-17).

20:16 “usihifadhi kuwa hai kitu cho chote kipumzikacho ” Hii ilimaanisha watoto wadogo, wanawake wenye mimba, wazee, wanyama...chochote kile chenye uhai (k.v. Yosh. 10:40; 11:11,14).

20:17 “uwaangamize kabisa ” Neno hili hapa ni *herem* (BDB 355, KB 353, *Hiphil* KITENZI JINA HALISI na *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, ambayo ni njia ya kisarufi ili kuonyesha mkazo), ambalo ni mpango wa kuwaangamiza kabisa kwa sababu ya kuwekwa wakfu kwa Mungu (k.v. 2:34; 7:1-5).

☐ **“Mhiti, na Mwamori, na Mkanaani, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi ”** Tazama Mada Maalumu: wakazi wa Israeli walioishi Palestina kabla katika 1:4.

20:18 Je hili liliweza kufanywa kwa namna gani na Mungu wenye upendo? Jibu moja linapatikana katika mst. 18 – sababu ya kitheolojia. Ikiwa hautawaondolea mbali kitheolojia watakunajisi wewe. Jibu lingine linapatikana katika Kumb. 9:4 na jibu la tatu katika Mwa. 15:12-21. Dhambi za wanadamu zina matokeo yake!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA):20:19-20

¹⁹ Wewe utakapohusuru mji siku nyingi kwa kufanya vita juu yake, upate kuutwaa, usiangamize miti yake kwa kupeleka shoka juu yake, kwani utaweza kula matunda yake; wala usiiteme, kwa maana huo mti wa kondeni, je! Ni mtu, hata ukauzuie? ²⁰ Ila miti ujuayo si miti ya kuliwa iangamize, na kuitema; ukajenge maburuji juu ya mji ufanyao vita juu yako, hata uanguke.

20:19-20 Miji yenye ngome katika mashariki ya karibu ya kale ilishambuliwa kwa maburuji. Mbao hizi zilitokana na miti isiyozaa matunda, kwa sababu inawezekana zilihajika baadae na wakazi wa Israeli kwa ajili ya kuushambulia mji.

20:19

NASB, NJB “huo ni mti wa kondeni”

NKJV “mti wa kondeni ni *chakula* cha mtu”

NRSV “mti wa kondeni ni mahitaji ya mtu”

TEV “miti siyo adui yako”

Maandiko ya kiebrania hapa ni magumu sana. Yanaonekana kwa kumaanisha kwamba miti sio adui! Ilikuwa ni njia kwa ajili ya YHWH kuwapatia chakula watu wake kwa wakati ujao.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani Israeli walihofu idadi kubwa na maarifa waliyokuwa nayo maadui?
2. Orodhesha aina nne za msamaha uliotolewa na jeshi:
3. Je, Mungu aliruhusu utumwa (mst. 11)?
4. Ni kwa namna gani mmoja anaweza kupatana mist. 16-17 nasi kwa mtazamo wa Mungu?
5. Orodhesha vipengele vyote vya fadhila katika sura hii.

KUMBUKUMBU LA TORATI 21

MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Sheria kuhusiana na mauaji yasiyotatuliwa	Sheria anwai (21:1-23:14)	Kuhusiana na mauaji yasiyotatuliwa	Mauaji yasiyotatuliwa
21:1-9	21:1-9	21:1-9	21:1-9
Mateka wa kiume		Kuhusiana na mateka wa kike	Wanawakw walichukuliwa vitani
21:10-14	21:10-14	21:10-14	21:10-14
Haki ya mzaliwa wa kwanza		Kuhusiana na urithi wa Mzaliwa wa kwanza	Haki za uzaliwa
21:15-17	21:15-17	21:15-17	21:15-17
Mwana mkaidi		Kuhusiana na mwana mkaidi	Mwana mkaidi
21:18-21	21:18-21	21:18-21	21:18-21
Sheria anwai (21:22-22:12)		Sheria mbalimbali (21:22-22:12)	Amri mbalimbali (21:22-22:12)
21:22-23	21:22-23	21:22-22:3	21:22-22:2

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu
8. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Tazama mfano uliopo wa neno “kama. . . hivyo.” hii ni mojawapo ya aina ya sheria huko Mashariki ya Karibu ya Kale (yaani., sheria za daawa au sheria ya ulaghai), zenye kutofautiana na sheria za awali (mf., amri kumi).

- B. Mfumo wa sheria za Kumbukumbu la Torati una miundo mbalimbali za kipekee:
1. Misisitizo ya mara kwa mara juu ya agano la upendo wa
 - a. YHWH kwa Israeli
 - b. Mwisraeli kwa Mwisraeli
 - c. Mwisraeli kwa asiye Mwisraeli
 - d. Mwisraeli kwa mnyama
 2. Uangalizi maalum kwa ajili ya maskini, uwekwaji huru, na wasio na msaada
- C. YHWH anawaagiza watu wake kwa namna iliyo ya wazi. Anawataka waelewe na kutenda ipasavyo. Matendo yao yaonyeshe tabia Zake kama namna ya kuwafikia wale wote wasiomjua (uhusiano wa imani binafsi na kitaifa). Sheria ni zawadi ya Mungu kwa taifa lililoanguka, na sio zoezi lenye udhibiti wa kubadilika! zinaonyeshwa kwa namna nyingi za kiutendaji na namna maalum ya jinsi “watu wasio watakatifu” waweza kubaki katika ushirika na Mungu!

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 21:1-9

¹Aonekanapo mtu ameuawa katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako, kuimiliki, amelala kondeni, wala haijulikani ni nani aliyempiga; ² na watoke nje wazee wako na waamuzi wako, nao wapime hapo mpaka miji iliyomzunguka huyo aliyeuawa; ³ na iwe, mji ulio karibu na yule aliyeuawa, wale wazee wake mji huo watwae mtamba katika kundi la ng'ombe, ambaye hajafanya kazi, wala hajakokota jembe la nira; ⁴ wazee wa mji huo na wamshushe yule mtamba mpaka bonde lenye maji ya mtoni, lisilolimwa wala kupandwa, wakamvunje yule mtamba shingo yake humo bondeni; ⁵ nao makuhani wana wa Lawi wasongee karibu, kwa kuwa ndio aliowachagua Bwana, Mungu wako, wamtumikie, na kubariki katika jina la Bwana na kila neno lishindaniwalo, na kila pigo, litakuwa kwa kufuata maneno yao; ⁶ na wazee wote wa mji ule, ulio karibu sana na yule aliyeuawa, na waoshe mikono yao juu ya huyo mtamba aliyevunjwa shingo yake humo bondeni; ⁷ na wajibizane kwamba, Mikono yetu haikumwaga damu hii, wala macho yetu hayakuiona. ⁸ Ee Bwana, samehe watu wako Israeli, uliowakomboa, wala usiache damu ya asiye makosa ikakaa katikati ya watu wako Israeli. Na ile damu utasamehewa kwao. ⁹ Ndivyo utakavyoondoa damu ya asiye makosa katikati yako, utakapofanya yaliyo sawa machoni pa Bwana.

21:1-9 Huu ni muktadha kuhusu namna ya kuitakasa nchi pale mtu anapopatikana ameuawa kwenye eneo la wazi, mbali na mji. Mauaji yalikuwa yanainajisi nchi ya YHWH (mf., 7:13; 11:9,21; 28:11; 30:20) na ni lazima lishughulikiwe kwa namna iliyo nzuri (yaani., kutoa dhabihu).

21:2 “wazee na waamuzi” Kuna wazee wakaao katika malango ya mji na kuziamua kesi za kwenye jamii. Ikiwa kutatokea tatizo watalipeleka kwenye mamlaka iliyo kuu (yaani., makuhani wa Kilawi, k.v. uk. 5). Walipima umbali toka pale mwili ulipopatikana na mji ulioko karibu. Mji uliopatikanana na mwili ulitakiwa kufanya utakaso fulani (k.v. kur. 3-8). Hili linaonyesha maamuzi yao mazuri ya kuyahukumu makosa kwa ukaribu. Mji uliokuwa karibu uliwajibika kwa ajili ya kosa la umwagaji damu, ambalo lingethiri baraka za YHWH kwenye eneo lote la mji (k.v. 19:13).

21:3 “mtamba..... ambaye hajafanya kazi, wala hajakokota jembe la nira” Hii inamaanisha ni mtamba ambaye hajatumika kwenye kazi yoyote ya kilimo.

21:4 “bonde lenye maji ya mtoni, lisilolimwa wala kupandwa” Neno hili ni bonde safi ambalo halijaathiriwa na shughuli zozote za kibinadamu au hali ya kiasili. Maji yanamaanisha namna ya kuusafisha uovu (linafanana na Yule mbuzi wa Mambo ya Walawi 16).

☐ **“wakamvunje yule mtamba shingo yake ”** Walimu wa sheria za Kiyahudi wa baadaye walisema “kukiondoa kichwa kwa shoka” kwa sababu kuivunja shingo ilikuwa ni kazi ngumu (k.v. Kut. 13:13; 34:20). Hata hivyo, damu

haikupaswa kuhusika kwenye taratibu za ibada, bali ni kwa dhana mbadala. Mtamba asiye na hatia alitolewa kama dhabihu kuwa mbadala wa muuaji asiyejulikana. Kusudi lilikuwa ni kuitakasa nchi kwa ajili ya damu isiyo na hatia iliyomwagika (k.v. Hes. 35:33-34).

21:5 “makuhani” Hawa wanaweza kuwalejelea Walawi wa nyumbani.

☐ **“kubariki katika jina la Bwana”** Kubariki ilikuwa ni moja ya kazi ya Makuhani/Walawi (k.v. 10:8; I Nya. 23:13). Moja ya mfano wa baraka za kikuhani umeandikwa katika kitabu cha Hes. 6:22-26. Baraka hizi zinahusiana na Israeli kulitunza agano (k.v. Hes. 6:27; Kumb. 28:3-6). Uwepo binafsi wa YHWH (yaani., jina) ulikubaliwa au kukataliwa na kila Mwisraeli mtiifu au mkaidi wa ufunuo wa YHWH (yaani., agano). Baraka ya Israeli, kwa mtu mmoja (k.v. Kut. 19:5-6) na shirika, ilibainishwa sio kwa uchaguzi wa holela holela, bali kwa imani binafsi katika YHWH, ikionyeshwa wazi na utii wa agano (stadi ya maisha). YHWH ilihitaji kubariki (k.v. Kut. 20:24; II Nya. 30:27).

☐ **“kila neno lishindaniwalo, na kila pigo, litakuwa kwa kufuata maneno yao”** KITENZI ni kile kilichozoeleka, “kuwa” (BDB 224, KB 243, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). Tafasiri ya neno “lishindaniwalo” linatokana na na kifungu kilichopita cha NOMINO, “kwa maneno yao” (BDB 804). Kuna aina mbili za matatizo ya kisheria yaliyotajwa:

1. “mabishano” (yaani., kesi za mahakamani) - BDB 936, k.v. 1:12; 19:17; 21:5; 25:1; Kut. 23:2,3,6
2. “shambulio” - BDB 619, k.v. 17:8.

Hapa linarejelea shambulio la mwili, lakini neno laweza kumaanisha ugonjwa, .v. 24:8 (mara nyingi katika Mambo ya Walawi).

21:6 “waoshe mikono yao juu ya huyo mtamba ” Hili linamaanisha kujitakasa (k.v. Mith. 26:6; 73:13) toka kwenye uovu kwa kuukaribia mwili wa mtu aliyekufa. Wazee wanawakilisha jamii nzima kwa pamoja wanapoyatakasa makosa yao toka kwenye kijiji au eneo husika.

21:7 “Mikono yetu haikumwaga damu hii, wala macho yetu hayakuiona ” Walimu wa sheria za Kiyahudi wanahusiana na hili kwa ajili ya wageni, maskini, yatima, au wajane. Pale wazee wote wa mji waliposhindwa kulikabili hitaji la mgeni lilipoletwa mbele yao kwa ajili ya kulisaidiwa walisamehewa kwa kutolishughulikia tatizo. Hii ingekuwa ni namna ya kuzuia familia iliyoathirika (yaani., mwenye kulipa kisasi) kwa kutomuua mtu asiye na kosa wa eneo jilani kwa kulipiza kisasi.

21:8

NASB, TEV,

NJB “Samehe”

NKJV “Toa msamaha”

NRSV “Msamaha”

REB “kubali kusamehe”

Hiki ni KITENZI cha Kiebrania cha neno “funika” (BDB 497, KB 493, *Piel* KAULI YA SHURUTISHI). Kimetumika mara mbili katika mstari huu (matumizi ya pili ni *Nithpael* KAULI ILIYO TIMILIFU). Neno hili, ni la kawaida katika kitabu cha Mambo ya Walawi na kitabu cha Hesabu, limetumika mara tatu tu katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (21:8[mara mbili]; 32:43). Maana yake ya msingi ni “kufunika kiibada kwa maana ya kutoa dhabihu.”

☐ **“uliowakomboa”** KITENZI hiki (BDB 804, KB 911, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini chenye maana ya KUAMURU) kinafanana na neno “kusamehe” (yaani., funika). Tazama Mada Maalum: Fidia/Komboa katika 7:8.

☐

NASB “wala usiache damu ya asiye makosa ikakaa katikati ya watu wako”

NKJV “wala usiweke damu ya asiye na makosa ikawahukumu watu wako”

NRSV “wala usiache damu ya asiye na makosa kubaki katikati ya watu wako”

TEV “usitung’ang’anize kuwajibika na mauaji ya mtu asiye na makosa”

NJB “usiache damu isiyo na makosa imwagike katikati ya watu wako”

KITENZI (BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini kikiwa na maana ya KUAMURU) ni ombi kwa ajili ya ibada ya msamaha kutokana na madhara ya mauaji yasiyojulikana. Tazama namna toleo la NJB lilivyokitafsiri kifungu katika hali ya KUAMURU.

21:9 Ibada au tambiko (k.v. mistari. 1-8) lilionekana kama “uondoaji ” (BDB 128, KB 145, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) wa madhara ya dhambi ya wote (yaani., mauaji yasiyojulikana) toka kwenye jamii nzima (yenye kufanana na ibada za “siku ya upatanisho” katika Mambo ya Walawi 16). Dhambi, hata ile ya kutokokusudia , iliathiri baraka za YHWH na hata kuleta ghadhabu kwa wote (yaani., laana, k.v. Kumbukumbu la Torati 27-29).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 21:10-14

¹⁰Utakapokwenda vitani kupigana juu ya adui zako, na Bwana, Mungu wako, awatiapo mikononi mwako, naye uwachukuapo mateka, ¹¹ukaona kati ya mateka mwanamke mzuri, ukafanya tamaa kwake, ukawaza kumtwa kuwa mkeo; ¹²ndipo umchukue kwenu nyumbani kwako, naye atanyoa kichwa, akate na kucha; ¹³avue na mavazi ya uteka wake akae nyumbani mwako, awakalie matanga babaye na mamaye mwezi mzima, kisha uingie kwake uwe mumewe, naye awe mkeo. ¹⁴Tena utakapokuwa huna furaha naye, mpe ruhusa aende atakako; lakini usimwuze kabisa kwa fedha, usimfanye kama mtumwa, kwa kuwa ulimtweza.

21:10-14 Mistari hizi zinaelezea namna ya kuwashughulikia wanawake ipasavyo (yaani., wasio Wakanaani, bali hao wengine, k.v. 20:10-15) waliokamatwa vitani, hata kama walikuwa na haki katika nchi ya YHWH. Uwajibikaji kwa ajili ya masikini na wasio na nguvu ulikuwa ni wa kipekee katika ulimwengu wa miundo ya sheria za kale.

21:11 “mwanamke” Huyu hakuwa mwanamke wa Kikanaani, huenda alikuwa mgeni, lakini sio Mkanaani.

☐ Tazama uendeleaji wa neno lenye kutumika kama kitenzi:

1. “tazama” - BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU
2. “upendo” - BDB 365 I, KB 362, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU, likitumika juu ya upendo wa YHWH kwa ajili ya Israeli katika 7:7; 10:15
3. “chukua” - BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU. Hapa halidokezi mambo ya kujamiiana, bali ni kumpeleka nyumbani kwako (k.v. mst. 12). Mtiririko ule ule unapatikana katika Mwa. 3:6!

21:12 “naye atanyoa kichwa, akate na kucha” Hili lilikuwa ni (1) hitimisho (k.v. Hes. 6:9,18-19); (2) kujitakasa (k.v. Law. 13:33; 14:8-9); au (3) kuomboleza (k.v. 14:1; Law. 21:5; Yer. 41:5; Ezek. 44:20) ibada. Hapa linamaanisha siku mpya, maisha mapya, familia mpya. Inafurahisha kuwa kuongoka kwake kwa ajili ya YHWH ni kwa kudhaniwa, na sio kutamka. Imani ya mwanaume ndiyo ilitakiwa kufuatwa na familia!

21:13 “awakalie matanga babaye na mamaye” Hata kama andiko halielezei kikamilifu kuwa huyu mwanamke hapaswi kuolewa tena, lakini linamaanisha hivyo. Halikutaja kukaa matanga pale unapopoteza mwanaume au mtoto.

☐ “kisha uingie kwake uwe mumewe, naye awe mkeo” Hii ni nahau ya Kiebrania kwa ajili ya kujamiiana (yaani., ili kukamilisha ndoa). Tazama kuwa shauku kwa ajili ya mahusiano ya kingono, hata na asiye Mwisraeli, halilaumiwi, lakini kuna muda maalum. Huu mwezi wa matanga unampa muda mwanaume wa Kiebrania kumjua mke sahihi. Kama mambo hayataenda vizuri, pana namna nyingine isio ya kutoa taraka. Pia tambua kutokuwepo kwa sherehe yenyewe ya ndoa (k.v. Mwa. 24:67).

21:14 “mpe ruhusa aende” Hili ni neno la kiufundi kwa ajili ya taraka (BDB 1018, KB 1511, *Piel* KAULI ILIYO TIMILIFU). Hatauzwa (*Qal* KITENZI JINA HALISI na *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU of BDB 569, KB 5181, ambalo lilikuwa ni namna ya kisarufi kuelezea msisitizo) kama mtumwa, lakini angeweza kutalikishwa. Tazama maelezo katika 24:1-4.



NASB “usimtende visivyo”

NKJV “usimtende vibaya”

NRSV, TEV “usimfanye kama mtumwa”

NJB -----

KITENZI (BDB 771 II, KB 849, *Hithpael* KAULI ISIO TIMILIFU) kinamaanisha “kumtenda pasipo haki” au “kumlazimisha kwenda kwa mtu mwenye nguvu” (k.v. 24:7). YHWH anashughulika na na utendaji haki hata kwa wanawake waliokamatwa mateka!



NASB, NKJV “kwa sababu ulimtweza”

NRSV “kwa vile umemnajisi”

TEV “kwa vile umelazimisha kulala nae”

NJB “kwa vile umemdhaliisha”

REB “kwa vile umelazimisha akubaliane nawe”

KITENZI (BDB 776, KB 853, *Piel* KAULI ILIYO TIMILIFU), katika muktadha huu, ni vizuri kitafasiriwe kama toleo la TEV (mf., Mwa. 34:2; Kumb. 22:24,29; Amu. 19:24; 20:5; II Sam. 13:12,14,22,32). Hawa wanawake wangelipitia masumbufu ya:

1. Kukamatwa vitani
2. Kupoteza familia
3. Matengano ya ndoa, pia kudhaniwa kubadili dini
4. Walilazimishwa kuiacha miji yao (pamoja na dhambi iliyodokezwa, k.v. Kumb. 24:1-4) wakiwa hawana mahali pa kwenda

Tambua kwamba hii aya, na ile inayofuata, zinamwekea ukomo wa mamlaka aliyonayo mwanaume wa Kiisraeli!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA):21:15-17

¹⁵ Akiwa mtu yuna wake wawili, mmoja ampenda, mmoja hampendi, nao wamemzalia watoto, ampendaye na asiyempenda wote wawili; na yule mzaliwa wa kwanza akiwa ni wa mke asiyependwa;¹⁶ ndipo itakapokuwa ya kwamba siku atakayowarithisha wanawe alivyo navyo, asimweke mwana wa ampendaye kuwa mzaliwa wa kwanza mbele ya mwana wa asiyempenda, naye ndiye mzaliwa wa kwanza huyu;¹⁷ lakini amkubali mzaliwa wa kwanza mwana wa yule asiyempenda, kwa kumpa mafungu mawili katika vyote alivyo navyo; kwa maana ndiye mwanzo wa nguvu zake; haki ya mzaliwa wa kwanza ni yake yeye.

21:15 Aya hii inatambua utamaduni wa ndoa za mitala. Mfano wa kwanza katika Kumbukumbu la Torati ni Lameki (Mwa. 4:23). Mtu wa kwanza anayefahamika zaidi kuwa na ndoa za wake wengi alikuwa Yakobo katika kitabu cha Mwanzo 29. Ndoa za mitala zilikuwa zikifanyika kwa watu matajiri au watu wenye mamlaka makubwa kwenye jamii, na sio kwa watu wa kawaida (ingawa mistari ya 10-14 yaweza kurejelea kwenye kosa la kuwa na wake wengi). Sababu hasa ya kutenda tendo hili haijulikani vizuri, huenda ni kwa ajili ya:

1. Kujamiiana tu
2. kuzaliana (kupata warithi)
3. hali ya kiuchumi
 - a. kuisadia familia maskini
 - b. namna ya kupata utajiri na umaarufu
 - c. namna ya kuwashikilia mateka wa vita
4. kuungana kisiasa ili kuyasaidia mataifa jirani kuendeleza amani (yaani., Daudi, Suleimani)

☐ **“asiyempenda”** Kiuhalisia hili neno ni “Yule achukiwaye” (BDB 971, k.v. mistari ya 15 [mara mbili],16,17). Lakini linatenda hapa kama nahau ya Kiebrania ya ulinganifu—apendwaye dhidi ya asiyependwa (k.v. Mwa. 29:30-31; Mal. 1:2-3; Rum. 9:13 [inanukuu Mal. 1:2-3]; Luka 14:26).

☐ **“mzaliwa wa kwanza”** Haki ya mzaliwa wa kwanza ilitambuliwa hata kama alikuwa mwana wa asiyependeka

(k.v. mstari. 17; Kut. 13:14-15; Law. 3:12-13).

21:17 “mafungu mawili” Nahau ya Kiebrania (BDB 804, “kinywa” na BDB 1040, “mawili”) pia imetumika kwenye shauku ya Elisha kutaka upako mara mbili wa Eliya katika kitabu cha II Fal. 2:9. Hii ndio sehemu pekee katika Agano la Kale ambapo mafungu mawili yametamkwa. Kama palikuwepo na vijana wawili, mkubwa alipokea theluthi mbili na mdogo alipokea theluthi moja; na kama walikuwa vijana watatu, hivyo ilikuwa ni 50%, 25%, 25%, n.k. kijana mkubwa alipaswa kuwatunza wazazi wao wenye umri mkubwa. Inafurahisha kuona kuwa wana historia wa hizi sheria wanathibitishiwa na mabaki ya elimukale yaliyopatikana:

1. Yakobo katika Mwanzo 49 anawapa wanawe kumi na wawili urithi sawa. Hili linathibitishwa kwenye mfumo wa Hammurabi
2. Hapa kutajwa kwa mafungu mawili kwa mzaliwa wa kwanza kunafanana na mabamba ya Nuzi na Mari.
3. Tofauti zilizoandikwa katika maandiko zinathibitisha tofauti iliyopo kwenye tamaduni zao za kisasa (tazama *The Old Testament Documents* by Walter C. Kaiser, Jr., uk. 86)

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 21:18-21

¹⁸ Mtu akiwa na mwana mkaidi, mshupavu, asiyetii sauti ya baba yake, wala sauti ya mama yake, nao wajapomwadhibu hawasikizi, ¹⁹ ndipo babaye na mamaye na wamkamate, na kumpeleka kwa wazee wa mji wake, katika lango la mahali pake; ²⁰ wawaambie wazee wa mji wake, Huyu mwana wetu ni mkaidi, mshupavu, hasikizi sauti yetu; ni mwasherati, tena ni mlevi. ²¹ Waume wote wa mji wake na wamtupie mawe, afe; ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako; na Israeli wote watasikia na kuogopa.

21:18-21 Kipengele hiki kinashughulika na wana wakaidi na namna wazazi walivyopaswa kuwatenda (k.v. Kut. 21:15,17; Law. 20:9). Wazazi hawakuwa na haki ya uzima au kifo juu ya mtoto, lakini mahakama ilikuwa nayo hiyo haki. Hili lilihusiana na (1) uvunjaji sheria ya 5:16; (2) urithi ndani ya familia; na (3) mshikamano ndani ya jamii.

21:18 Aina hii ya vijana kupingana na jamii ilielezwa kama:

1. “ukaidi” - BDB 710, KB 770, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU
2. “uasi” - BDB 598, KB 632, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU
3. Mambo hayo yote yanatumika pamoja katika Zab. 78:8 na Yer. 5:23

KAULI ENDELEVU tano katika mstari huu zinaonyesha mwendelezo wa kitendo. Mstari unaobaki unaelezea matendo yao:

1. Wale wasiotii sauti za baba zao, mistari ya 18,20
2. Hata hawasikizi, mtr. 18
3. mlafi, mstari 20 - BDB 272 II
4. mlevi, mstari. 20 - BDB 684 See *Hard Sayings of the Bible*, kur. 174-175.

21:19 “ndipo babaye na mamaye na wamkamate” Hili linamaanisha huenda (1) wote kujizuia kwa pamoja (BDB 1074, KB 1779, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU) au (2) hitaji la mashuhuda wawili (k.v. 17:6; 19:15; Hes. 35:10).

☐ **“katika lango”** Mahali pa kutolea haki palikuwa ni katika lango la mji, mahali ambapo wazee waliketi (mf., 19:12; 22:15; 25:7).

21:21 “Waume wote wa mji wake na wamtupie mawe, afe” Tazama dhana ya usamaria kwamba wazazi hawakupaswa kumtupia mawe mtoto wao. jamii (k.v. Law. 20:2,27; 24:14-23; Hes. 15:35) walitenda kujisafisha na uovu, na wanajumuiya wote wasio wema.

MADA MAALUM: HUKUMU YA KIFO KATIKA ISRAELI

Israeli ya kale ilipaswa kuzifunua tabia za YHWH kwa ulimwengu (k.v. Mwa. 12:3; 22:18; Kut. 19:5-6). Pale uasi wa agano wa kimakusudi ulipobadili kusudi la wamisheni, madhara makubwa yalijidhihirisha (yaani., adhabu ya kifo).

Vitabu vitano vya Musa vinaorodhesha namna mbalimbali:

1. kumtenda dhambi YHWH
 - a. Taratibu za ibada za Wakanaani – Kut. 22:18; Law. 20:2-3,27; Kumb. 18:10-11
 - b. Ibada ya sanamu (viumbe vya kimbingu) – Kut. 22:20; Kumb. 17:2-7
 - c. Makufuru – Kut. 22:28; Law. 24:15-16
 - d. Unabii wa uongo – Kumb. 13:1-11; 18:20-22
 - e. Kuivunja Sabato – Kut. 31:14-15; 35:2
2. dhambi za zinaa
 - a. Kujamiiana kwa maharimu – Law. 20:11-21
 - b. Uasherati – Law. 19:29; 21:9; Kumb. 22:13-21; 23:17-18
 - c. Uzinzi – Kut. 20:14; Law. 20:10; Kumb. 22:23-24
 - d. Ufilaji – Law. 18:22; 20:13
 - e. Kumwingilia mnyama – Kut. 22:19; Law. 20:15-16
3. kuvunja taratibu za agano dhidi ya Mwisraeli mwenzako
 - a. Kuuu – Kut. 20:13; 21:12-14; Law. 24:17; Hes. 35:16-21; Kumb. 5:17
 - b. Kuwauza mateka – Kut. 21:16; Kumb. 24:7 na yumkini Kut. 20:15; Kumb. 5:19
 - c. Kuwakaidi wazazi – Kumb. 21:18-21
 - d. kushuhudia uongo
 - e. kuwachukua mateka wa vita takatifu – Joshua 7

njia za utekelezaji hukumu pia zilitofautiana.

1. kuwatupia mawe – iliyokuwa ya kawaida
2. Kuwachoma na moto – Mwa. 38:24; Law. 20:14; 21:9
3. Kuwatundika – Kumb. 21:22-23
4. Kuwaua kwa upanga – Kumb. 13:15

kesi maalum zisizo za kawaida

1. miji ya makimbilio kufuatia jaribu – Joshua 20
2. Upelelezi mkali wa mashitaka – Kumb. 13:15; 17:4; 19:18
3. Kuhitajika mashuhuda wawili – Hes. 35:36; Kumb. 17:6; 19:15

Adhabu ya kifo ilitolewa kwa

1. Namna ya kuitakasa nchi – Kumb. 13:5; 17:12; 19:13,19; 21:9,21; 22:21,22,24; 24:7
2. Zuo kwa wengine – Kumb. 17:13; 19:20; 21:21
3. ni namna ya kuzuia fujo kwenye ukoo (yaani., hapakuruhusiwa mtu kulipiza kisasi, isipokuwa taratibu ziwekwe kwa ajili ya mlipa kisasi)

Tazama *Ancient Israel*, juzuu 1, kr. 147-163.



NASB “utakavyoondoa”

NKJV “utakavyouweka mbali”

NRSV “utakavyoondoa”

TEV “utakavyousafisha”

NJB “utakavyoufukuzia mbali”

KITENZI cha Kiebrania (BDB 128, KB 145, *Piel* KAULI ILIYO TIMILIFU) kinamaanisha kuteketeza kwa moto kwa maana ya kuondoa moja kwa moja (k.v 13:5; 17:7,12; 19:13,19; 21:9,21; 22:21,22,24; 24:7).

☐ “na Israeli wote watasikia na kuogopa” Adhabu ya kijamii ilitenda kazi kama ukomeshaji wa kitu Fulani ili kisitokee tena. Tazama maelezo katika 13:11.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 21:22-23

²²Akiwa mtu ametenda dhambi ipasayo kufa, akauawa, nawe ukamtundika juu ya mti; ²³mzoga wake usikae usiku kucha juu ya mti; lazima utamzika siku iyo hiyo; kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu; usije ukatia

21:22 “ukamtundika juu ya mti” Tazama Mada Maalum ifuatayo.

MADA MAALUM: KUJITUNDIKA

KITENZI cha neno "kujitundika" (BDB 1067, KB 1738) kina maana mbili.

1. kiuhalisia ni kujitundika kwa kamba mpaka mauti
 - a. kwa Kiarabu, "kufungua kamba"
 - b. utekelezaji wa Wafilisti, 2 Sam. 21:12
 - c. utekelezaji wa Waebrania, 2 Sam. 17:23 na Agano Jipya, Mt. 27:5
 - d. utekelezaji wa Wababeli, muundo wa Hammurabi (tazama ISBE, juzuu 2, kur. 1327-1332)
 - e. utekelezaji wa Kiajemi, k.v. Esta 2:23; 5:14; 6:4; 7:9-10; 9:13,25
2. kitendo cha kumfuma mtu kwenye hatari kali
 - a. taratibu za Kimisri, k.v. Mwa. 40:19; 41:13
 - b. taratibu za Kibabeli, k.v. muundo wa Hammurabi
 - c. taratibu za Kiajemi (k.v. Ezra 6:11)

mara nyingi kilifanyika baada ya mtu kuuwawa kwa namna nyingine kama njia ya kujiabisha wazi. Maziko halisi yalikuwa ya muhimu kwa watu wa kale na yaliathiri mtizamo wao wa kuridhika na maisha baada ya kifo (mf., Kumb. 21:23). Katika Biblia yenyewe ni vigumu kufahamu vilivyo kama #1 au #2 hapo juu uko sawa. Dhahiri shairi katika Kumb. 21:22-23; Yosh. 10:26-27; 1 Sam. 31:10,12; 2 Sam. 4:12; 21:12, watu walioonyeshwa wazi kuwa tayari walikuwa wamekwisha kufa, lakini vipi kuhusu Yos. 8:29 na 2 Sam. 21:9?

Walimu wa sheria za Kiyahudi wa zama za Yesu waliliona hili andiko likihusiana na kusulubisha kwa Warumi. Viongozi wa dini walimtaka Yesu asulubiwe ili kwamba apate kulaaniwa na YHWH kwa kujifanya Yeye kuwa Masihi (k.v. Kumb. 21:23). Kifo cha kawaida kwa ajili ya kukufuru kilikuwa ni kupigwa mawe. Mara nyingi nimesikia ikisemwa kuwa viongozi wa Kiyahudi kwenye zama za Yesu hawakuwa na haki ya kisheria ya kutoa hukumu ya kifo chini ya utawala wa Kirumi, hivyo wakampeleka Yesu kwa Pilato ili apate kuhukumiwa. Hata hivyo, walimpiga Stefano kwa mawe, nje tu ya lango la hekalu (k.v. Matendo ya Mitume 7) pasipo ruhusa ya Kirumi, kwa nini haikufanyika kwa Yesu? Walitaka Yeye asulubiwe ili kufunua sio tu kifo na aibu ya wazi, bali laana ya Mungu!

21:23 “lazima utamzika” Hili linakuza muundo wa pamoja wa KITENZIJINA HALISI na *Qal KAULI ISIO TIMILIFU* ya neno “kuzika” (BDB 868, KB 1064). Ghadhabu ya YHWH inadai aliyekosa afe iwe kama adhabu kwa ajili ya ukaidi wake. Hata hivyo, ghadhabu ya YHWH ingaliendea jamii kama mwili ya mkosaji aliyeuwawa usingeshughulikiwa vyema na kwa muda maalum.

☐ “(kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu)” Tazama Gal. 3:13 kwa ajili ya matumizi ya Paulo kwenye hiki kifungu. Paulo aliona kifo mbadala cha Yesu ni kama Yeye mwenyewe kuchukua laana ya sheria ya Musa. Mwanzoni hii laana ilihusianishwa na taratibu zifaazo za maziko kwenye nchi takatifu.

MADA MAALUM: LAANA

I. AGANO LA KALE

Kuna maneno mbalimbali kwa ajili ya neno "laana." *Herem* (BDB 356, KB 353) yaliyotumika kwa kitu Fulani kilichotolewa kwa Mungu (kama vile toleo la LXX linakitafasiri kama *anathema*, BAGD 54, Law. 27:28). Mara nyingi lilitumika kuangamiza vitu kwa sababu ni vitakatifu mno kwa mwanadamu kuvitumia (kama vile Kumb. 7:26; Yos. 6:17-18; 17:12). Lilikuwa ni neno lililotumika kwenye dhana ya "vita vitakatifu." Mungu alimwambia Yoshua kuwa angamiza Wakanani wote. Yeriko ilikuwa fursa ya kwanza, "matunda ya kwanza" ya maangamizo matakatifu.

II. AGANO JIPYA

Katika Agano Jipya neno *anathema* na miundo yake yenye kuhusiana ilitumika katika maana tofauti mbalimbali:

- A. Kama zawadi au matoleo kwa Mungu (kama vile Luka 21:5)
- B. Kama kiapo cha kifo (kama vile Mdo. 23:14)
- C. Kulaani na kuapa (kama vile Marko 14:71)
- D. Kanuni ya laana inayohusiana na Yesu (kama vile 1 Kor. 12:3)
- E. Kumtoa mtu Fulani au kitu Fulani kwenye hukumu au maangamizo kwa Mungu (kama vile Rum. 9:3; 1 Kor. 16:22; Gal. 1:8-9)

Namba D hapo juu ni yenye mkanganyiko. Nimejumuisha hoja zangu toka 1 Kor. 12:3:

"Yesu kushitakiwa" ni maelezo yenye kushtua. Kwa nini mtu yeyote angaliweza (isipokuwa mila za Kiyahudi) mwenye kudai kuzungumza kwa ajili ya Mungu aliseme hili? Neno (yaani., *anathema*) lenyewe lina mazingira ya Agano la Kale (yaani., Kiebrania, *herem*). Linahusiana na dhana ya vita takatifu, ambapo mji ulitolewa kwa Mungu na, kwahiyo, ukawa mtakatifu. Hii inamaanisha kuwa kila kitu ndani yake chenye kupumua, mwanadamu au mnyama, kinapaswa kufa (kama vile Yosh. 6:17; 7:12). Nadharia ya jinsi neno hili lilivyotumika huko Korintho ni:

1. Kuwa lina mazingira ya Kiyahudi yanayohusiana na kiapo cha kwenye Sinagogi (kama vile Mdo. 26:11, yaani., baadaye, kanuni za laana za dini ya Kiyahudi zilitumika kuuondoa Ukristo toka kwenye Sinagogi). Ili kubaki mshirika ilibidi mtu amukatae Yesu au kumulaani Yesu wa Nazareti.
2. Kuwa lina mazingira ya Kirumi yenye kuhusiana na kumwabudu mfalme mkuu ambapo Kaisari angeitwa "Bwana"
3. Kuwa lina mazingira ya ibada za kipagani ambapo laana ziliitishwa juu ya watu kwa kutumia jina la mungu. Hili baadaye lingeweza kutafasiriwa, "Yesu na akulaani _____" (kama vile 1 Kor. 16:22).
4. Kuwa mtu Fulani ahusianaye na kifungu kwenye dhana na kithiolojia ya Yesu kutoa laana ya Agano la Kale kwa ajili yetu (kama vile Kumb. 21:23; Gal. 3:13).
5. Uchunguzi wa hivi karibuni toka huko Korintho (kama vile tanbihi #1 uk. 164 katika nyaraka za Bruce Winter's *After Paul Left Corinth*) bamba za laana zimepatikana juu ya mji wa kale ulijengwa juu ya kilima huko Korintho. Wanazuoni wa Kibiblia wamedhani kuwa KITENZI chenye kuhusiana na neno "ni" yapaswa kuwekwa kwenye kifungu, "Yesu anashitakiwa," lakini huu ushahidi wa elimukale kwa uwazi unaonyesha kuwa hizi laana za kipindi cha Warumi cha karne ya kwanza toka Korintho zinapungukiwa KITENZI (kama zifanyavyo baadhi ya laana katika toleo la LXX la Kumb. 22:15-20), kama ilivyo 1 Kor. 12:3. Kuna ushahidi zaidi wa elimukale kuwa Wakristo wa karne ya kwanza ya Warumi huko Korintho walitumia kanuni ya laana kwenye utaratibu wa maziko (yaani., kipindi cha Byzantine, zilizopatikana kwenye makaburi ya Wakristo (J. H. Kent, *The Inscriptions*, 1926-50. Princeton: American School of Classical Studies, 1966, vol. 8:3, no. 644).

Baadhi ya vipengere vya kanisa huko Korintho walikuwa wakirudia kwenye laana za kipagani kwa jina la Yesu dhidi ya washirika wengine wa kanisa. Sio tu kwenye tatizo la utumiaji, bali pia kwenye muonekano wa chuki. Huu ni mfano mwingine wa mvutano ndani ya kanisa. Paulo aliwahitaji walijenga kanisa, kuliimarisha kanisa, walitaka kulaani sehemu ya kanisa!

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini palikuwepo na miji ya makimbilio kwa watu waliofanya mauaji pasipo kukusudia?
2. Ni kipi kilichokuwa si cha kawaida kuhusu mtamba na kifo chake?
3. Kwa nini wanawake waliokamatwa kama mateka walinyoa vichwa vyao?
4. Orodhesha faida za upendeleo alioupata mzaliwa wa kwanza.
 - a.
 - b.
 - c.
 - d.
5. Ni kwa vipi mstari wa 23 unatofautiana na kifo cha Yesu? Ni kwa vipi vinahusiana?

KUMBUKUMBU LA TORATI 22

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Sheria ndogo ndogo (21:22-22:12)	Sheria ndogo ndogo (21:1-23:14)	Sheria mbali mbali (21:22-23:12) 21:22-22:3	Sheria mbali mbali (21:22-23:12)
22:1-3	22:1-3		22:1-2 22:3
22:4	22:4	22:4	22:4
22:5	22:5	22:5	22:5
22:6-7	22:6-7	22:6-7	22:6-7
22:8	22:8	22:8	22:8
22:9	22:9	22:9	22:9
22:10	22:10	22:10	22:10
22:11	22:11	22:11	22:11
22:12	22:12	22:12	22:12
Sheria ya Maadili ya Kujamiiana		Sheria zihusianazo na Usafi wa kujamiiana	Sifa za mke kijana
22:13-21	22:13-19	22:13-14 22:15-19	22:13-19
	22:20-21	22:20-21	22:20-21 Uzinzi na Uasherati
22:22	22:22	22:22	22:22
22:23-24	22:23-24	22:23-24	22:23-27
22:25-27	22:25-27	22:25-27	
22:28-29	22:28-29	22:28-29	22:28-23:1
22:30	22:30	22:30	

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuwiwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu
8. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:1-4

¹Umwonapo ng'ombe wa nduguyo au kondoo wake akipotea, usijifiche kama usiyemwona; sharti utamrudisha kwa nduguyo. ² Na kwamba yule nduguyo hayupo karibu nawe, au ukiwa humjui, umchukue

kwenu nyumbani kwako, uwe naye hata aje nduguyo kumtafuta, nawe mrudishie. ³ Tena fanya vivyo kwa punda wake; tena fanya vivyo kwa mavazi yake; tena fanya vivyo kwa kila kitu kilichopotea cha nduguyo, kilichompotea ukakiona wewe; usijifiche kama usiyekiona. ⁴ Umwonapo punda wa nduguyo, au ng'ombe wake, ameanguka kando ya njia, usijifiche kama usiyemwona; sharti umsaidie kumwinua tena.

22:1 “Umwonapo. . . usijifiche kama usiyemwona” kuacha kwa kukusudia au kwa kujisahau (“kujificha,” BDB 761, KB 834, kama vile 22:1,3,4; Law. 20:4; Mith 28:27; Ezek. 22:26) juu ya ndugu muhitaji na mali yake kulikatazwa (kama vile mst. 3; Kut. 23:4-5).

☐ **“utamrudisha”** KITENZI hiki kilichozoeleka (BDB 996, KB 1427, *Hithapel*) kinatumika mara tatu katika mistari ya 1-2. Maana yake ya msingi ni “kurudi” au “kugeuka nyuma.” Israeli ilitakiwa kufanya kazi kama kitengo cha familia yenye kujali. Aya kama hii zinasema kile ambacho Law. 19:18 inamaanisha kimatendo kwa namna iliyo wazi. Ndugu kujaliana!

Matumizi haya ya kwanza yanakuzwa kwa matumizi ya KITENZI HALISI na KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU cha asili ile ile “hakika utawarudisha! Aina hii hii ya ukuzaji inatumika katika mst. 4, “umsaidie kumwinua tena” (yaani, KITENZI HALISI NA kitenzi cha WAKATI USIO TIMILIFU BDB 877, KB 1086).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 22:5

⁵ **Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako.**

22:5 Mstari huu umehakikiwa kimaandiko kuamua mavazi sahihi ya wanawake wa leo (yaani, wanawake wasivae mavazi mabaya kanisani). Lazima ikumbukwe kwamba wote mwanamke na mwanaume walivaa kanzu katika Mashariki ya Karibu ya Kale. Tofauti pekee ikiwa kwamba kanzu za wanawake katika Israeli zilikuwa na mapambo ya bluu katika mabega. Msukumo wa msingi wa andiko hili sio mababa wa imani bali kukataliwa kwa matendo ya kiibada ya Wakanaani (yaani, “chukizo,” kama vile Law. 18:26,27,29,30). Lazima kuwe na tofauti wa halisi kati ya tofauti aliyoitoa Mungu kati ya mwanamke na mwanaume (yaani, utaratibu ulioubwa). Hii haikusudiwi kuwa tofauti ya katazo hasi bali ukiri wa nguvu tofauti tofauti na kazi za kidesturi za jinsi! Inawezekana kabisa kwamba andiko hili linaunganishwa na hukumu ya kimaagano ya Musa ya mapenzi kati ya jinsi moja (kama vile Law. 18:22; 20:13) iliyokuwa inafanywa na Wakanaani katika mazingira ya kiibada.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 22:6-7

⁶ **Kiota cha ndege kikitukia kuwa mbele yako njiani, katika mti wo wote, au chini, chenye makinda au mayai, naye koo ameatamia juu ya makinda, au juu ya mayai, usimtwae yule koo pamoja na makinda;** ⁷ **sharti umwache yule koo aende zake, lakini makinda waweza kuyatwaa uwe nayo; ili upate kufanikiwa, ufanye siku zako kuwa nyingi.**

22:6-7 Mistari hii inaweza kuonekana kufanana na utunzaji wa vyanzo vya chakula kwa vizazi vingi vya Waisraeli. Baada ya Mwanzo 3 wanadamu wangekula nyama, lakini lazima walinde dhidi ya uharibifu wa chanzo cha nyama kwa faida ya vizazi vijavyo vya ndugu wa kimaagano (yaani, “ili siku zako zipate kuwa nyingi,” kama vile 4:40). Wanyama wa mwituni walikuwa zawadi ya Mungu ya Protini kwa watu Wake. Mengi kati ya masharti haya yenye uhalisia wa ndani yalikusudiwa kuwasababisha Waisraeli kufikiria juu ya majukumu ya kimaagano ya kupenda, kulinda na kutoa kwa ajili ya afya na ukuaji wa watu wa agano.

22:7 “sharti umwache yule koo aende zake” Aina ile ile ya msisitizo inapatikana katika mist. 1 na 4 (yaani, KITENZI HALISI na KITENZI CHA WAKATI USIO TIMILIFU cha asili ile ile, BDB 1018, KB 1511) chenye kurudiwa.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 22:8

⁸ **Utakapojenga nyumba mpya, fanya ukuta kando-kando ya dari lako, usije ukaleta damu juu ya nyumba**

yako, mtu akianguka huko.

22:8 “ukuta kando-kando ya dari lako” Neno ukuta (BDB 785, ambalo kwa Kiarabu linamaanisha “kukinga”) huu ulikuwa ukuta wa ulinzi kuzunguka nyumba ambazo paa ya juu zilikuwa zinalingana pande zote ili kuwafanya watu wasianguke. Tena Israeli walitakiwa kufikira kuhusu namna ya kuulinda ndugu wa kike na wa kume na wanafamilia!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:9

⁹**Usipande shamba lako la mizabibu aina mbili za mbegu; yasije yakaondolewa matunda yote, mbegu ulizopanda na maongo ya mizabibu yako.**

22:9 “Usipande shamba lako la mizabibu aina mbili za mbegu” Kifungu hiki kiuhalisia kinarejelea aina ya mizabibu katika shamba lakini kinafunua kuwa kanuni ingeamuru aina moja ya mizabibu. Hii inayarejelea mazao yanayovunwa kwa msimu kati ya mizabibu.

Hii inaweza kufunua (1) tabia ya Wakanaani kuwafurahisha miungu au (2) hali ya fikra kwamba kuchanganya vitu kunasababisha kupotea kwa usafi wake (kama vile Law 19:19).

▣ **“yasije yakaondolewa”** Neno *Kadosh* (BDB 872, KB 1073, *Qal* kauli ya wakati usio timilifu) linamaanisha kutenga kwa ajili ya Mungu (kama vile 15:19). Hii inaweza kumaanisha (1) ilitakiwa kuharibiwa au (2) kupewa kwa makuhani. Je, kanuni hii inafanya kazi leo? Ningeleeza kwamba sheria ya Agano la Kale lazima ijiirudie katika Agano Jipya ili iwe na nguvu ya kufunga kwa waaminio wa Agano Jipya (kama vile Mdo. 15; I Wakorintho 8-10; Wagalatia 3). Yesu mwenyewe alikanusha mifumo yote miwili ya kidhabihu na sheria za chakula (kama vile Marko 7:17-23). Tazama muundo mzima wa kitabu cha Agano Jipya cha Waebrania (yaani, Ukuu wa Agano Jipya juu ya Agano la Kale). Vitabu viwili ambavyo vinanisaidia mimi kufikiri juu ya jambo hili ni:

1. *How To Read the Bible For All Its Worth* cha Gordon Fee na Doug Stuart
2. *Gospel and Spirit* cha Gordon Fee

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:10

¹⁰**Usilime kwa ng'ombe na punda wakikokota jembe pamoja.**

22:10 “Usilime kwa ng'ombe na punda wakikokota jembe pamoja” Ngo'mbe walimao walikuwa safi, punda walikuwa si safi lakini katazo hili kama inavyosemekana na walimu wa sheria za kiyahudi lilifanyika kwa sababu ya kibinadamu ya kutowaweka pamoja wanyama wenye uwezo na tabia aina mbili tofauti. Hata hivyo, katika muktadha huu ni moja ya mfano wa “kutokuchanganya vitu!”

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:11

¹¹**Usivae nguo iliyochanganyikana sufu na kitani pamoja.**

22:11 “Usivae nguo iliyochanganyikana sufu na kitani pamoja” Hii ni moja wapo ya kutenga vitu ili visichanganywe (kama vile Lawi. 19:19). Hii inaweza kuwa ilikuwa stiari ya kuchanganya matendo ya kiibada ya YHWH na Wakanaani. Baadhi wanaiona hii kama (1) kuunganishwa na nguo za kimiujiza (yaani, taratibu za kuchanganya vitu) au (2) Magombo ya Bahari ya Chumvi (yaani, 4QMMT) inataja kwamba aina fulani tu za nguo ndizo zingeweza kuchanganywa (yaani, mavazi ya kikuhani yaliyotengenezwa kwa kitani na lineni, ambavyo vingetengeneza namna ya kuwa takatifu. Labda ndio maana vitu visivyokatazwa vilichukuliwa kuwa “najisi.”

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:12

¹²**Ujifanyizie vishada katika pembe nne za mavazi yako ya kujifunika.**

22:12 Katika muktadha huu yawezekana hii inaendeleza kukataliwa kwa kitu cho chote cha Wakanaani. Israeli ilikuwa na ibada tofauti, Mungu wa tofauti, mavazi tofauti! Katika Hesabu 15:37-42 mapambo haya yameongeza

maana ya kuwakumbusha Waisraeli kutunza na kuifurahia sheria. Uwakilishi huu unafunuliwa katika kitabu cha maombi (mwongozo wa maombi) wa siku za Yesu. Vazi linalorejelewa lilitakiwa kuwa vazi la pembe nne linalotumika kufunika sehemu ya juu ya mtu, hasa wakati wa ibada, maombi na usomaji wa Maandiko. Hapana uhakika kama kitabu cha maombi pia kililikuwa kinahitajika (au kuruhusiwa) katika mavazi ya wanawake. Hili linaweza kuwa jambo lingine linalohusiana na kuchanganya nguo (kama vile mstari wa 5).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:13-19

¹³ Mtu akitwaa mke, akamwingilia na kumchukia, ¹⁴ kisha akamshitaki mambo ya aibu kumzushia jina baya, akasema, Nimemtwa mwanamke huyu, nami nilipomkaribia sikuona kwake alama za ubikira; ¹⁵ ndipo babaye yule kijana na mamaye watakapotwaa alama za yule kijana za ubikira, wawatolee wazee wa mji langoni; ¹⁶ na baba yake yule kijana awaambie wazee, Mwanamume huyu nilimpa binti yangu awe mkewe, naye amchukia; ¹⁷ angalieni, amemwekea mambo ya aibu, asema, Sikuona kwa binti yako alama za ubikira, nazo hizi ndizo alama za binti yangu za ubikira. Na wayakunjue yale mavazi mbele ya wazee wa mji. ¹⁸ Basi wazee wa mji ule na wamtwae yule mtu mume na kumrudi, ¹⁹ wamtoze shekeli mia za fedha, wampe babaye yule kijana, kwa kuwa amemzulia jina baya mwanamwali wa Israeli; naye awe mkewe; hana ruhusa ya kumwacha siku zake zote.

22:13 “akamwingilia” Hii ni moja ya tafsida kati ya hizi tatu zenye kumaanisha kujamiiana ambapo imetumika katika muktadha huu:

1. “kumuingilia,” mst. 13 (BDB 97)
2. “wakati nilipomkaribia,” mst. 14 (BDB 897)
3. “kulala naye,” mist. 22,23,25,28,29 (BDB 1011)

☐ **“kumchukia”** Hili ni neno la Kiebrania “chukia” (BDB 971, KB 1338). Ni neno hilo hilo lililotumika katika 21:15, ambalo linatafsiriwa “isio pendwa” ni ulinganifu wa nahau ya Kiebrania ambayo ni dhana ya “inayopendwa zaidi,” “pendelewa zaidi.” Hata hivyo, hapa inachukua maana ya “iliyokataliwa” au “kutokuwa na furaha juu ya.”

22:14

NASB, NJB “kumzushia jina baya”
NKJV, REB “kumzushia jina baya”
NRSV “kumzushia”
TEV “kumshitaki kwa mashitaka ya uongo”

Kiuhalisia hii ni “kumtengenezea jina lenye uovu” (KITENZI - BDB 422, KB 425, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU na NOMINO -BDB 1027, na KIVUMISHI - BDB 948). Hii inafanana na Kumb. 24:1-4, ambapo talaka inatolewa kwa “utovu wa nidhamu,” ambayo kwa asili ni kujamiiana. Mwanamke anayeshitakiwa yeye anakuwa amepoteza kidogo au hajapoteza (yeye na familia yake) heshima. Maisha yake ya baadaye ya fursa za ndoa na urithi wa mtoto (ikiwa alipata ujauzito mapema) vinakuwa mashakani. Hili lilikuwa jambo nyeti kwa watu wa Mashariki ya Karibu ya Kale!

☐ **“sikuona kwake alama za ubikira”** Jamii ya Kiebrania iliweka kigezo cha kipaumbele katika ubikira (kama vile mst. 19). Urithi ulikuwa jambo muhimu sana na ukosefu wa uaminifu katika mahusiano vilipingwa sana!

KITENZI “kujua” (BDB 592, KB 619) kinatumika mara kadhaa katika muktadha huu:

1. kujua, kugundua
 - a. rasmi, mist. 14,17,20
 - b. kimwili, mist. 23,27,28
2. kukutiliza katika kitendo, mist. 22,23

22:15 “ndipo babaye yule kijana na mamaye watakapotwaa alama za yule kijana za ubikira” Hii aidha ni (1) dhana ya Kumbukumbu la Torati ya ushirikiano wa kuwainua wanawake katika kujumuishwa kwenye sheria au (2) kuhitajika kwa mashahidi wawili.

☐ **“alama za ubikira”** Hii inaweza kurejelea :

1. wazazi walitoa ubikira kabla hawajamkabidhi binti kuolewa na wakaweka damu yake katika vazi
2. kitanda ambacho kwa mara ya kwanza wanandoa hukutania kilitolewa na wazazi na kutunzwa na wazazi
3. ushahidi kwamba msichana alikuwa anaingia katika siku zake mara kwa mara kabla ya siku ya kufunga ndoa kulithibitisha kwamba hakuwa mjamzito

Namba 2 inaonekana kuwa dhaifu kwa sababu mwanaume asingejua hasa lini hili lilifanyika.

☐ **“wazee wa mji langoni”** Hii ingerejelea waamuzi walioteuliwa walioendesha mashitaka katika lango la mji au katika eneo lililoteuliwa (yaani, mti mkubwa, sehemu maalum iliyotengwa, au njia kuu.)

22:18 “wamtwae yule mtu mume na kumrudi” Hii inaweza kumaanisha kumpiga mwanaume fimbo arobaini (kama vile 25:2-3), lakini ikiwa hivyo ni matumizi pekee ya neno hili (BDB 415, KB418) katika Agano la Kale ambapo siku zote inarejelea maelekezo (kama vile 21:18, NIDOTTE, juzuu 2, kur. 479-481).

22:19 “kumtoza fidia” Mtu huyo alitakiwa kupewa adhabu na kutoa fidia kwa sababu alikuwa amedhalilisha (kiuhalisia, “amesababisha jina baya”) Israeli iliyo bikra. Dhahiri fidia ililipwa mara mbili ya kile alicholipa mwanzo (mahari) kama mchumba (kama vile 22:29). Maana yake inaweza kuwa mwanaume alitaka tu kurudishiwa fedha yake kutoka kwa baba wa msichana.

☐ **“bikra Israeli”** Hiki kilikuwa cheo cha heshima (japo ilitarajiwa) chenye kuelezea jina la mwana-mwali ategemewaye kuwa katika mahusiano ya milele na Mungu

22:19, 29 “atakuwa mkewe; hawezi kumwacha siku zake zote” Hiki kilikuwa ni kibano na uwekwaji wa ukomo juu ya haki za mwanaume. Wanawake katika Israeli walikuwa hawana haki ya kuacha. Sheria hii ilikuwa inalinda haki za watoto wa mwanamke juu ya urithi (kama vile 21:15-17).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 22:20-21

²⁰ Lakini likiwa ni kweli neno hili, la kutoonekana kwake yule kijana alama za ubikira; ²¹ na wamtoe nje yule kijana mlangoni pa nyumba ya baba yake, na waume wa mji wake wampige kwa mawe hata afe; kwa vile alivyofanya upumbavu katika Israeli, kwa kufanya ukahaba katika nyumba ya baba yake; ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako.

22:20, 21 Siku zote, kupigwa mawe kulifanyika nje ya lango la mji. Tazama Mada Maalum: Adhabu ya Kifo katika 21:21. Kwa sababu ya dhana ya Kiebrania ya ujumuishwaji, baba alikuwa na jukumu kwa matendo ya bintiye na hivyo adhabu ilipangwa katika mlango wake!

Adhabu kwa ushahidi wa uongo siku zote ilikuwa ni kifo. Adhabu isiyo haki inayonekana kutokea hapa ambapo ikiwa mashitaka ya mume juu ya binti ni ya kweli, basi msichana alipigwa mawe lakini ikiwa ni ya uongo (hata ya udanganyifu) anaonywa na kuambiwa atoe fidia lakini hapigwi mawe (kama vile 19:19). Wanawake hawakuwa na haki za kisheria na ulinzi kama wanaume katika Agano la Kale. Huruma inaoneshwa, lakini sio haki!

22:21 “tendo la kipumbavu” Neno hili (BDB 615) linatumika juu ya kujamiiana kusiko ruhusiya:

1. Mwa. 34:7 (Wasio Waisraeli kujilazimisha wenyewe kwa binti wa Yakobo)
2. Kumb. 22:21 (kupoteza ubikira)
3. Waamuzi 19:23; 20:6,10 (mpagani kushambulia suria wa Mlawi)
4. II Sam. 13:12-13 (Amnoni, mzaliwa wa kwanza wa Daudi anambaka dada yake asiye wa tumbo moja)

☐ **“kufanya ukahaba”** Neno hili ni *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO cha neno (BDB 275, KB 275), ambacho kinaashiria matendo ya kujamiiana yanayohusisha uasherati (tendo la ndoa kabla ya ndoa), uzinzi (kujamiiana baada ya ndoa na mtu mwingine tofauti na mkeo), na ukahaba (kujamiiana kwa kujiuza kwa malipo ya fedha).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:22

²² Akifumaniwa mtu mume amelala na mwanamke aliyeolewa na mume, na wafe wote wawili, mtu mume aliyelala na mwanamke, na yule mwanamke naye; ndivyo utakavyoondoa uovu katika Israeli.

22:22 “Akifumaniwa mtu mume amelala na mwanamke aliyeolewa na mume” Hata kama kuna mashaka, kuna njia ya kutokea (kama vile Hesabu 5:11-31). Tungo “mwanamke aliyeolewa na mwanaume” kwa uhalisia ni “mke wa mwanaume mwingine,” ambalo ni matumizi mara mbili ya neno b’l (BDB 127, KB 142, *Qal* KAULI TENDEWA YA WAKATI ENDELEVU na NOMINO YA UMOJA YENYE KIIMA chenye muundo wa JINSI YA KIUME YENYE KIIMA). Neno hili, siku zote linatafsirika “bwana” au “mume,” lina asili ile kama ya neno Ba’al, mungu wa kiume wa ustawi wa Wakanaani. Mume alikuwa “bwana” juu ya nyumba yake. Mkewe na watoto walikuwa kwa namna ya kisheria, mali. Kusema ukweli uvunjifu wa utaratibu wa kujamiiana ulionekana kama dhambi dhidi ya Mungu (kama vile Mwa. 39:9; II Sam. 12:13). Inavunja utaratibu uliotolewa na Mungu na uthabiti wa jamii na kuathiri urithi uliotolewa na Mungu wa familia na koo.

☐ **“na wafe wote wawili”** Walimu wa sheria wa kiyahudi walifasiri hili kumaanisha mtoto, ikiwa mwanamke alikuwa mjamzito kwasababu ya hali ya dhambi ya ujumuishi kwa wote. Tazama usawa wa adhabu ambayo hailingani na kosa katika Agano Jipya.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:23-24

²³ Pakiwa na kijana aliye mwanamwali ameposwa na mume, na mwanamume akimkuta mjini, akalala naye; ²⁴ watoeni nje katika lango la mji ule, mkawapige kwa mawe hata wafe; yule kijana, kwa kuwa hakupiga ukelele, naye yu ndani ya mji; na yule mume, kwa kuwa amemtweza mke wa mwenzake; ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako.

22:23 “ameposwa” Katika Israeli, kuposwa (BDB 76, KB 91) ilikuwa ni kifungo cha kuhesabika kama kuwa tayari umeshaolewa (yaani, Yosefu na Mariamu, kama vile Mt. 1:18-19).

22:24 “mkawapige kwa mawe. . . kwa kuwa hakupiga ukelele” wote wangepigwa kwa mawe mpaka kifo (kama vile Law. 20:10); mwanaume kwa sababu alimkosesha mwanamke wa jirani yake, mwanamke kwa sababu hakupiga kelele (BDB 858, KB 1042, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kwa ajili ya msaada.

☐ **“ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako”** Tazama dokezo katika 13:5.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:25-27

²⁵ Lakini yule mtu mume kama akimkuta kondeni kijana aliyeposwa, naye mume akamtenza nguvu, akalala naye; yule mtu mume aliyelala naye na afe pekee; ²⁶ lakini yule kijana usimfanye neno; hana dhambi yule kijana ipasayo kuuawa, kwa kuwa ni mfano wa mtu kumwondokea mwenzake akamwua, ni vivyo lilivyo jambo hili; ²⁷ kwani alimkuta kondeni; yule kijana aliyeposwa akalia, pasiwe na mtu wa kumwoko.

22:25-27 Utungwaji wa sheria ulikusudiwa kuwa wa haki na sio utawala wa sheria ili sheria iwepo tu. Kulikuwa na pande zisizo na hatia katika matendo ya dhambi!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:28-29

²⁸ Mtu mume akimwona kijana aliye mwanamwali ambaye hajaposwa, akamshika na kulala naye, wakaonekana; ²⁹ yule mtu mume aliyelala naye na ampe baba yake yule kijana shekeli hamsini za fedha, kisha na awe mkewe, kwa kuwa amemtweza; hana ruhusa ya kumwacha siku zake zote.

22:28 “Mtu mume akimwona kijana aliye mwanamwali ambaye hajaposwa, akamshika na kulala naye” kwa kuzingatia umri wa mapema ambao wasichana wa Kiyahudi waliposwa, inaonekana kwangu kwamba hii

inarejerea kwa (1) uvunjifu wa haki za mtoto au (2) unyanyasaji kwa familia masikini. Agano la Musa linalinda watu wanyonge na wadhaifu kijamii!

22:29 “yule mtu mume... naye na ampe baba yake yule kijana shekeli hamsini za fedha. . . hana ruhusa ya kumwacha” Ikiwa baba ni masikini sana kumposa bintiye au binti ni mwenye mtindio wa ubongo na mwanaume amemnajisi, alitakiwa mwanaume aliyefanya hivyo amlipie na kmuoa kwa ajili ya maisha yake (kama vile Kut. 22:16).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 22:30

³⁰ **Mtu mume asimtwae mke wa baba yake, wala asifunue ncha ya mavazi ya baba yake.**

22:30 “Mtu mume asimtwae mke wa baba yake” Hii inawezekana kumaanisha kuwa mwanaume hatakiwi kuoza mama yake wa kambo (yawezekana kati ya wake kadhaa wa baba yake), hata kama babaye amefariki au mwanamke amepewa talaka ya kuachwa.

☐ **“mavazi ya baba yake”** Hii ni njia ya kinahau ya kurejerea kwa matendo ya kindoa ya baba (kama vile Ruthu 3:9; Ezek. 16:8). Kuanza mahusiano ya kimapenzi na mwanamke ambaye hapo kabla alikuwa na baba yake ilikuwa kwa namna yake kumkosea baba (kama vile 27:20; Law. 18:8; 20:11).

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa kiasi gani surah ii unaweza kuisema kuwa inaendana na desturi zetu? Ni kwa namna gani unaamua maamuzi yako?
2. Nini kilichojificha/kilicho nyuma ya sheria hizi?

KUMBUKUMBU LA TORATI 23

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Wale waliotegwa katika Mkutano mwa	Sheria Mchanganyiko (21:1-23:14)	Kutengwa kutoka miongoni watu wa Mungu	Uasherati na Ukahaba (22:22-23:1)
23:	23:1	23:1	22:28-23:1 Ushiriki katika Ibada ya Kusanyiko
23:2	23:2	23:2	23:2-7
23:3-8	23: 3-6 23:7-8	23:3-6 23:7-8	
Kulitakasa eneo La Kambi		23:8-9 Kuitunza Kambi ya Kijeshi katika hali ya usafi	Elimu ya usafi katika Kambi
23:9-14	23:9 23:10-11 23:12-14	23:9-11 23:12-14	23:13-15 Mchanganyiko
Sheria Mchanganyiko	Sheria zinazoshughulika na Ubinadamu na Utii wa Kidini (23:15-25:19)	Sheraia mbalimbali	
23: 15-16	23:15-16	23:15-16	23:16-17
23:17-18	23:17-18	23:17-18	23:18-19
23:19-20	23:19-20	23:19-20	23:20-21
23:21-23	23:21-23	23:21-23	23:22-24
23:24-25	23:23-24	23:24-25	

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)**KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

Aya ya kwanza

Aya ya pili

Aya ya tatu

N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 23:1-6**

¹Aliyejeruhika konde, au aliyekatika tupu yake, asiingie mtu huyo katika mkutano wa Bwana. ²Mwana wa haramu asiingie katika mkutano wa Bwana; hata kizazi cha kumi asiingie aliye wake katika mkutano wa Bwana. ³Mwamoni wala Mmoabi wasiingie katika mkutano wa Bwana; wala hata kizazi cha kumi mtu wao asiingie katika mkutano wa Bwana milele; ⁴kwa sababu hapo mlipotoka Misri hawakuwalaki na chakula wala maji njiani; na kwa kuwa walimwajiri juu yako Balaamu mwana wa Beori kutoka Pethori iliyo Mesopotamia, aje akuapize. ⁵Lakini Bwana, Mungu wako, hakukubali kumsikiza huyo Balaamu; Bwana, Mungu wako, aliyageuza yale maapizo kuwa ni baraka, kwa vile alivyokupenda Bwana, Mungu wako. ⁶Usitafute amani yao wala heri yao siku zako zote, milele.

23:1 “Aliyejeruhika” Hili neno la Kiingereza limeyatafsiri maneno mawili ya Kiebrania:

1. “kwa kupondwapondwa” - BDB 194
2. “kwa kukata” - BDB 822, KB 954, *Qal* ya KAULI ENDELEVU

Hii inarejelea (1) kende za wanauume zilizoondolewa au (2) kwa kukata mirija iliyotoa manii (huenda kwa kuivunjavunja).

☐ **“au aliyekatika tupu yake”** Kifungu hiki kinarejelea kiungo cha kiume cha uzazi kilichokatwa (BDB 1050, “eneo linalotumia kupitisha manii”).

Hii ingeweza kuwa njia nyingine ya kuuzungumzia utowashi (kama vile Mt. 19:12). Hawa wanaume wawili walioathiriwa tupu zao wako katika mtiririko wa kwanza wa wale waliotengwa kutohudhuria katika mkutano wa Israeli (yaani, matukio yaliyofanyika ndani ya mahema). Kutengwa kwao ni ishara ya utakaso na utakatifu wa watu wa Mungu wanaoonekana kama ufalme wa makuhani (kama vile Kut. 19:6 na Law. 21:17-23; 22:17-25). Baadaye katika kitabu cha Agano la Kale wengi wao waliotengwa wamejumuishwa (m.f., Ruthu Mmoabu na yule towashi wa Isa. 56:3-5 na Matendo ya Mitume 8:26-40).

Pia inawezekana kwamba tendo hili la kuviharibu viungo muhimu vya uzazi vya wanaume ilikuwa sehemu ya matendo ya Kanaani. Makatazo memngi yanayoone kana kutokuwa ya kawaida katika sheria ya Musa yalitoa mwongozo wa moja kwa moja kwa jamii ya Kikanaani na taratibu za ibada.

▣ **“asiingie”** Hiki KITENZI (BDB 97, KB 112) kinatumika mara kadhaa ndani ya sura hii:

1. “asiingie,” mist. 1, 2(mara mbili), 3 (mara mbili), 8, 11(mara mbili), 20, 24, 25
2. “usilete,” mst. 18

Matumizi mengi yalikusiana na:

1. watu ambao wasingeweza kuingia (au kuudhuria katika matukio yaliyohusisha sikukuu za mahema) katika kusanyiko la Israeli:
 - a. wanaume walioharibiwa viongo vyao vya uzazi
 - b. watu haramu au vizazi vyao
 - c. Waamori, Wamoabu, au vizazi vyao
2. watu ambao wasingeweza kuingia:
 - a. Waedomu
 - b. Wamisri
3. watu ambao hawakupaswa kuingia ndani ya kambi ya Israeli kwa kipindi cha wakati:
 - a. wanaume wa waliofanya matukio wakati wa usiku
 - b. Waisraeli wote kujiamini wao wenyewe

▣ **“mkutano wa Bwana”** Kifungu “mkutano wa Bwana” kinatumika kumaanisha watu wa agano la YHWH waliokusanyika kwa ajili ya kufanya ibada iliyoanzia Ml. Horebu/Sinai:

1. Kut. 12:6, “kusanyiko lote la mkutano wa Israeli ”
2. Law. 16:17, “mkutano wote wa Israeli”
3. Hes. 16:3, “mkutano wote,” “mkutano wa Bwana”
Hes. 20:4, “kusanyiko la Bwana”
4. Kumb. 5:22, “mkutano wenu wote”
Kumb. 9:10; 10:4; 18:16, “siku ya mkutano”
Kumb. 23:1,2,3,8, “mkutano wa Bwana”
Kumb. 31:30, “kusanyiko la wana wa Israeli”
5. Yosh. 8:33, “watu wa Israeli”
kifungu hiki kinawakilisha:
 1. Kuabudu kwa Israeli
 - a. Ml. Sinai/Horebu
 - b. hema
 2. Kitabu cha *The Jewish Study Bible*, uk. 418, kinachojikita katika Amu. 20:2, kinaeleza kwamba kifungu hiki kinalirejelea baraza la uongozi au chombo kitawalacho (kama vile Hes. 16:3; 20:4) Hawa waliotengwa bado waliendelea kuwa na haki za kisheria za “makazi ya wageni” zinazotamkwa
 3. katika Kut. 22:21; Law. 19:9-10,33-34; 23:22; Kumb. 1:16; 5:14; 27:19. Tafasiri ya Maandiko ya Agano la kale la Kiebrania linalitafsiri neno la kiebrania *qahal* (BDB 874) kama *eklesia*, ambapo tunalipata neno la Kiingereza, “kanisa.” Yesu na waandishi wa Agano Jipya walilichagua neno hili ili kujaza kwamba watu wa Mungu wa Agano Jipya lazima watambuliwe kama upanuzi wa watu wa Mugu wa Agano la Kale (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38; Gal. 6:16; I Pet. 2:9; Ufu. 1:6).

23:2 “Mwana wa haramu” Kifungu hiki (BDB 561) kinaelezwa kama mojawapo ya (1) mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa; (2) jamaa wa karibu (kama vile Law. 18:6-18); au (3) mtoto wa ndoa mchanganyiko (Myahudi na mpagani, kama vile Ezra 9:2; Neh. 13:23-25; Zek. 9:6). Neno la Kiebrania linaendana vema na uchaguzi #2.

23:2,3 “kizazi cha kumi” Utambue ufanano wa kimuundo ulio katika kifungu, “kamwe (asi) ingie katika mst. 2 na 3. Namba kumi ni ya nahau ya utimilifu au milele (tazama Mada Maalum katika 4:40).

MADA MAALUM: UWAKILISHI WA NAMBA KATIKA MAANDIKO

- A. Namba fulani zilitenda kazi maeneo yote kama tarakimu na ishara.
1. Moja – Mungu (yaani, Kumb. 6:4; Efe. 4:4-6)
 2. Nne – dunia nzima (yaani, pande nne, pepo nne, yaani, Isa. 11:12; Yer. 49:36; Dan. 7:2; 11:4; Zek. 2:6; Mt. 24:31; Marko 13:27; Ufu. 7:1)
 3. Sita – kutokamilika kwa mwanadamu (moja chini ya 7, mf. Ufu. 13:18)
 4. Saba – itimilifu wa Kiungu (siku saba za uumbaji). Tambua matumizi ya kiishara katika Ufunuo:
 - a. vinara vya taa saba, Ufu. 1:12,20; 2:1
 - b. nyota saba, Ufu. 1:16,20; 2:1
 - c. makanisa saba, Ufu. 1:20
 - d. Roho saba za Mungu, Ufu. 3:1; 4:5; 5:6
 - e. taa saba, Ufu. 4:5
 - f. Mihuri saba, Ufu. 5:1,5
 - g. pembe saba na macho saba, Ufu. 5:6
 - h. malaika saba, Ufu. 8:2,6; 15:1,6,7,8; 16:1; 17:1
 - i. baragumu saba, Ufu. 8:2,6
 - j. ngurumo saba, Ufu. 10:3,4
 - k. elfu saba, Ufu. 11:13
 - l. vichwa saba, Ufu. 13:1; 17:3,7,9
 - m. mapigo saba, Ufu. 15:1,6,8; 21:9
 - n. vitasa saba, Ufu. 15:7; 21:9
 - o. wafalme saba, Ufu. 17:10
 5. Kumi– ukamilifu
 - a. matumizi katika Injili
 - 1) Mt. 20:24; 25:1,28
 - 2) Marko 10:41
 - 3) Luka 14:31; 15:8; 17:12,17; 19:13,16,17,24,25
 - b. matumizi katika Ufunuo
 - 1) Ufu. 2:10, siku kumi dhiki
 - 2) Ufu. 12:3; 17:3,7,12,16, pembe kumi
 - 3) Ufu. 13:1, vilemba kumi
 - c. Vigawe vya kumi katika Ufunuo
 - 1) 144,000 = 12x12x1000, kama vile Ufu. 7:4; 14:1,3
 - 2) 1,000 = 10x10x10, kama vile Ufu. 20:2,3,6
 6. Kumi na Mbili – ushirika wa mwanadamu
 - a. Wana kumi na wawili wa Yakobo (yaani, makabila kumi na mbili ya Israeli, Mwa. 35:22; 49:28)
 - b. nguzo kumi na mbili, Kut. 24:4
 - c. mawe kumi mawili juu ya kifua cha Kuhani Mkuu, Kut. 28:21; 39:14
 - d. mikate kumi na miwili, juu ya meza Mahali Patakatifu (ishara ya utoaji wa Mungu wa kwa makabila kumi na mawili), Law. 24:5; Kut. 25:30
 - e. Watu kumi na wawili, Kumb. 1:23;
 - f. mawe kumi na mawili, Jos. 4:2,3,4,8,9,20

- g. miktume kumi na wawili, Mt. 10:1
- h. matumizi katika Ufunuo wa Yohana
 - 1) makakabila kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri, Ufu. 7:5-8
 - 2) nyota kumi na mbili, Ufu. 12:1
 - 3) milango kumi na mikwili, malaika kumi na wawili, makabila kumi na mawili, Ufu. 21:12
 - 4) misingi ya mawe kumi na mawili, majina ya Mitume kumi na mawili, Ufu. 21:14
 - 5) Yerusalemu mpya ilikuwa vipimo vya mraba elfu kumi na mbili, Ufu. 21:16
 - 6) milango kumi na miwili ilitotengenezwa kwa lulu kumi na mbili Ufu. 21:21
 - 7) mti wa uzima uzao matunda, aina kumi na mbili, Ufu. 22:2
- 7. Arobaini –namba za nyakati
 - a. wakati mwingine ni halisi (kuhamishwa na kutangatanga nyikani, m.f. Kut. 16:35); Kumb. 2:7; 8:2
 - b. inaweza kuwa halisi au ya kiishara
 - 1) mafuriko, Mwa. 7:4,17; 8:6
 - 2) Musa juu ya Ml. Sinai, Kut. 24:18; 34:28; Kumb. 9:9,11,18,25
 - 3) mgawanyo wa maisha ya Musa:
 - a) miaka arobaini ndani ya Misri
 - b) miaka arobaini jangwani
 - c) miaka arobaini ya kuiongoza Israeli
 - 4) Yesu alifunga siku arobaini, Mt. 4:2; Marko 1:13; Luka 4:2
 - c. Tambua (kwa maana ya Upatanisho) tarakimu za wakati hii tarakimu inajitokeza katika wakati wa uteuzi ndani ya Biblia!
- 8. Sabini – namba ya jumla ya watu
 - a. Israeli, Kut. 1:5
 - b. wazee sabini, Kut. 24:1,9
 - c. matukio ya siku za mwisho, Dan. 9:2,24
 - d. kundi la huduma, Luka 10:1,17
 - e. msamaha (70x7), Mt. 18:22
- B. Marejeo mazuri
 - 1. John J. Davis, *Biblical Numerology*
 - 2. D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*

23:3 “Mwamoni wala Mmoabi” Mataifa haya yalikuwa matokeo ya wana haramu waliotajwa katika mst. 2. Baadhi ya waalimu wa Kiyahudi wanasema kwamba Mwa. 19:30-38 (mataifa yaliyotokana na uhusiano haramu wa Lutu pamoja na mabinti zake) inaonyesha kwamba hili limatumika kwa wanaume tu, ambapo iligundulika kuwa Ruthu alikuwa Mmoabi na uzao wa Mfalme Daudi. Hata hivyo, nyuma ya uzao haramu, sababu nyingine maalum za kukataliwa kwao zinatajwa katika mist. 4-6.

23:4 “Balaamu” Nabii huyu hakuwa wa uzao wa Ibrahimu, bali alimjua YHWH, kama alivyofanywa Melksedeki na Ayubu, ambao pia hawakuwa uzao wa Ibrahimu. Simulizi ya Balaamu inaelezwa tena katika Hesabu 22-24.

23:5 “kwa vile alivyokupenda Bwana, Mungu wako” Hii ni dhamira ya mara kwa mara iliyo katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati:

1. 4:37, “aliwapenda baba zenu”
2. 7:7-8, “Bwana anawapenda, na kwa sababu alitaka kuutimiza uapo wake aliowaapia baba zenu:
3. 7:12-13, “naye atakupenda na kukubarikia na kukuongeza tena” (kama ukitii)
4. 10:15, “Tena, Bwana aliwafurahia baba zako, na kuwapenda, akawachagua wazao wao baada yao”
5. 33:3, “awapenda hayo makabila ya watu”

Matendo ya YHWH yanaegemea uchaguzi wake, si wema wa Israeli (kama vile 7:7-8). Yeye alimchagua Ibrahimu ili auchague ulimwengu (tazama Mada Maalum: Upendeleo wa Kiinjilisti wa Bob 4:6).

23:6 “amani yao wala heri yao” Hii inaweza kuwa rejea ya (1) makubaliano au muungano (mf. Ezra 9:12) au (2) maombi badala yao (mf. Yer. 14:11).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 23:7-8

⁷Usimchukie Mwedomi; kwa kuwa ni ndugu yako; usimchukie Mmisri, kwa kuwa ulikuwa mgeni katika nchi yake. ⁸Wana wao watakozaliwa kizazi cha tatu na waingie katika mkutano wa Bwana.

23:7 “Usimchukie” Hiki KITENZI (BDB 1073, KB 1765, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kilichotumika mara mbili) kinamaanisha “chukizwa,” kutokana na NOMINO “chukizo” (mf. 7:26). Tazama Mada Maalum: Chukizo katika 14:3.

☐ **“Mwedomi; kwa kuwa ni ndugu yako”** Rashi anasema kuwa ofauti kati ya mist. 3 na 7 ni kwamba nchi zile zilezoorodheshwa katika mst. 3 ndizo zilizomsababisha Israeli kutenda dhambi (kama vile Mwa. 36). Taifa la Edomu linatokana na uzao wa Esau ndugu wa Yakobo (kama vile Mwa. 25:24-26; 36:1).

23:8 “Wana wao watakozaliwa kizazi cha tatu” Huenda tendo hili la kungoja lilitokana na wakati maalum wa kuungana kwa ukamilifu pamoja na jamii ya Israeli na taratibu za ibada.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 23:9

⁹Utakapotoka kwenda juu ya adui zako nawe u katika marago, jilinde na kila neno baya.

23:9 Israeli ilihusishwa katika “vita takatifu” (kama vile sura 20). YHWH alipigana kwa ajili yao, lakini iliwapasa kwendelea kushikilia “taratibu” halisi kwa ajili ya uwepo wa YHWH ili azidi kuwa nao (kama vile mst. 14; Yosh. 5:13-15).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 23:10-11

¹⁰Akiwa kwenu mtu awaye yote asiyekuwa ni tohara kwa ajili ya yaliyomtukia usiku, na atoke nje ya kituo, wala asiingie ndani ya kituo; ¹¹lakini na iwe ikaribiapo jioni, yeye ataoga maji; na jua likiisha kuchwa ataingia ndani ya kituo.

23:10 “yaliyomtukia usiku” Kwa Kiebrania ni “lililojiri au tukio lililotukia usiku” (BDB 899 MUUNDO WA MANENO 538).

Hili linaweza kuhusisha aina nyingine za majimaji yotokayo mwililini kama mkojo na kuharisha, n.k. Tendo lote la kutokwa na majimaji mwilini lilimfanya mtu kuwa najisi kwa mujibu wa taratibu zao (kama vile Mamba wa Walawi 15). Kumbuka, hili lilipaswa kufanywa kwa mujibu wa taratibu za kuuondoa unajisi, si dhambi.

23:11 “jioni” Israeli ilianza siku mpya wakati wa jioni, kwa kufuata mtiririko wa Mwanzo 1.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 23:12-14

¹²Tena uwe na mahali nje ya kituo, kwa kutokea nje; ¹³nawe uwe na jembe dogo katika silaha zako; napo uotamapo nje uchimbe kwa lile jembe, na kugeuka na kukifunika kikutokacho; ¹⁴kwa kuwa Bwana. Mungu wako, yuatembea katika kituo akuokoe, na kukutolea adui zako mbele yako; kwa hiyo na kiwe kitakatifu kituo chako; asije akaona kitu kwako kisichokuwa safi, akageuka na kukuacha.

23:12 “mahali” Lugha ya Kiebrania ina neno “uelekeo (BDB 388), ambalo huenda lilirejelea ishara ya kuthibitisha eneo la jumla lililolengwa kwa makusudi ya kutunzia kinyesi (BDB 844).

23:13

NASB “jembe”
NKJV “chombo”

NRSV, NJB “koleo”
TEV “ufito”

Hili Neno la Kiebrania (BDB 450) linarejelea aina fulani ya uchimbaji. Iwe ni kifaa cha kijeshi kilichotumika kwa makusudi mawili ama kifaa kilichotengwa kama mambo ya hema iliyobebwa kwa makusudi ya mtu fulani haijulikani.

☐
NASB “silaha”
NKJV, TEV,
NJB “kifaa”
NRSV “vyombo”

Maana ya neno hili (BDB 24) haijulikani. Maana ya Kiarabu inamaanisha “umiliki,” ambapo maana ya Kiaramu inamaanisha “siraha.” Katika muktadha huu hii inaonekana kuwa siraha ya kivita ambayo pia ilitumika kama kifaa cha kichimbia kilichohusishwa katika taratibu za utakaso na elimuafya kuhusiana na huifadhi wa kinyesi. Neno hili linatumika hapa tu katika Agano la Kale.

23:14 “Bwana. Mungu wako, yuatembea katika kituo” Kuna uwezekano wa kifungu hiki kuwa rejea kwa Walawi waliokuwa wakilibeba Sanduku la Agano (kama vile Kut. 25:10-22), ambalo lilichukuwa nafasi ya wingu *shekinah* (mf. Kut. 13:21-22; 14:19-20; 16:10; 19:9,16; Law. 16:2,13) kama ishara ya uwepo wa ki-Uungu baada ya Israeli kuvuka ng’ambo ya mto Yordani. Baadaye walimu wa Sheria za Kiyaudi waliuchukuwa mstari huu na kutoa tamko kwamba hakuna mbolea ambayo ingetumika kustawisha bustani ndani ya mji wa Yerusalemu.

☐ **“kitu kwako kisichokuwa safi”** Huu ni MUUNDO WA MANENO wa “neni” (BDB 182 IV, #6) pamoja na “utupu” (BDB 788, #2, kama vile 24:1). Katika muktadha huu unarejelea taratibu za utakaso zilizohusiana na majimaji yaliyokuwa yakitoka mwilini (kama vile Mambo ya Walawi 15). Hii inaonekana kuwa njia ya kuifundisha Israeli kwamba uwepo na nguvu ya YHWH pamoja nao lazima ioanishwe kwa “utakatifu” wao na mkesho wa kudumu.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESWA): 23:15-16

¹⁵ Usimrudishe kwa bwana wake mtumwa aliyejiponya kutoka kwa bwana wake kuja kwako; ¹⁶na akae nawe, katikati yako, ndani ya malango yako mojawapo, mahali atakapochagua palipo pema machoni pake; usimwonee.

23:15 “Usimrudishe kwa bwana wake mtumwa” Swali kuu lenye kufasirika ni utaiifa wa mtumwa na bwana wake. Je! hili linamrejelea nani? Hili lazima limrejeele mtumwa mgeni au bwana wa mtumwa aliye mgeni (au wote). Kwa uwazi kabisa hili linaurejelea ufahamu wa Israeli kwamba mtu ni zaidi ya siraha kifaa kilichonolewa. YHWH anauruhusu utumwa chini ya vikwazo na viziwi, bali pia kwajali wale wasio na uwezo, wasio na tumaini, na wanyonge!

23:16 Utambue uhuru uliorudiwarudiwa ambao YHWH anauhitaji kwa ajili ya watumwa wa kigeni waliopokonywa:

1. “na akae nawe, katikati yako” - BDB 442, KB 444
2. “mahali atakapochagua” - BDB 103, KB 119, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. “palipo pema” - BDB 373 II
4. “usimwonee” - BDB 413, KB 416, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

Ni uhuru na ulinzi ulioje! Mfumo wa sheria zote za Mashriki ya Karibu ya Kale ulidai juu ya (na ikiwezekana kifo) kurudishwa kwa watumwa waliotoroka. Agano la Musa linatazamia haki na ulinzi wa wanyonge, wasio na nguvu, walionyanyapaliwa kijamii, na maskini. Kifungu chenye uzito ni “wajane, yatima, na wale waliotengwa” (kama vile 10:18; 14:29; 16:11; 24:17,19; 26:12,13; 27:19).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESWA): 23:17-18

¹⁷ Pasiwe na kahaba katika binti za Israeli, wala pasiwe na hanithi katika wana wa Israeli wanaume. ¹⁸ Usilete ujira wa kahaba, wala mshahara wa mbwa, katika nyumba ya Bwana, Mungu wako, kwa ajili ya nadhiri yo yote; kwani haya ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako, yote mawili.

23:17 “kahaba katika binti za Israeli” Hili ni neno la jinsi ya kike la neno “aliye mtakatifu” (BDB 873 I). Hili linaonyesha kuwepo kwa ukahaba katika Kanaani (kama vile Kut. 34:15-16; II Fal. 23:7). Hata hivyo, kuna ushahidi mchache sana na mgumu wa tafiti za mambo ya kale katika Kanaani (kama vile NIDOTTE, juzuu 1, uk. 1124, #6). Ikiwa kulikuwa na ukahaba katika binti za Israeli na machukizo yalioendelea ndani ya jamii ya Israeli, basi wote wangekuwa waovu zaidi (kama vile Hosea 4:11-14; Luka 12:48).

☐ **“kahaba katika binti za Israeli”** Hili ni neno la jinsi ya kiume “aliye mtakatifu” (BDB 873 I). Katika kipindi hiki kahaba wa kiume anaitwa “mbwa” (kama vile mst. 18).

23:18 “ujira wa kahaba” Hili ni neno tofauti na mst. 17 (kama vile Hosea 9:1). Hili ni neno la kawaida lenye kumaanisha mwenza wa ibada ya ustawi (BDB 1072). Kuna baadhi ya mijadala kama maneno yanayozungumzia kahaba katika binti za Israeli katika mst. 17 yanafanana na neno hili la mst. 18 au ikiwa mst. 18 unarejelea kahaba asiye katika binti za Israeli (BDB 1072). Katika maandiko mengi kuna tofauti, lakini kuna ufananano unaonekana kwa makusudi. Ujira uliokuwa ukikusanywa iliwapasa kutoutoa kwa Mungu (kama vile Mika 1:7). YHWH anayakata makusanyo yote yaliyotokana na tozo za kizinzi!

☐ **“mshahara wa mbwa”** Hizi ni tozo zilizotolewa na kahaba wa kiume. YHWH anaikataa ibada ya ustawi na vipato vyake!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 23:19-20

¹⁹ Usimkopeshe ndugu yako kwa riba; riba ya fedha, riba ya vyakula, riba ya kitu cho chote kikopeshwacho kwa riba; ²⁰ mgeni waweza kumkopesha kwa riba, ila usimkopeshe ndugu yako kwa riba; ili Bwana, Mungu wako, apate kukubarikia katika yote utiayo mkono wako, katika nchi uingiayo kuimiliki.

23:19 “Usimkopeshe ndugu yako kwa riba” Maana halisi ya Kiebrania ni “jambo linalomuumiza” (BDB 675). Hili pia linajadiliwa katika Kut. 22:25 na Law. 25:35-37.

23:20 Kulikuwa na tofauti ya kuweka miongozo kati ya wenza wa agano na Mataifa (BDB 648, kama vile 14:21;15:3).

☐ **“ili Bwana, Mungu wako, apate kukubarikia katika yote utiayo mkono wako”** Zitambue baraka za YHWH, ambazo ziliimaanisha kuwa kielelezo ambacho kitauvutia ulimwengu kuja kwake, zilikuwa n amasharti ya Israeli kulitii agano. Agano la kale, kama lilivyo agano jipya, lilijikita katika neema, bali kazi ya kulitii agano ilikuwa kai ya Mungu na watu wake kwa sababu Mungu anaifunua tabia yake kwa wale waliopotea kiroho na wenye kuupenda ulimwengu. Wokovu wa Agano Jipya ni wa uhuru kabisa katika kazi ya Kristo iliyokwisha kumalizika, lakini nayo ni ya kimasharti na matarajio (yaani, toba, imani, utii, ustahimilivu). Shabaha ya kumjua Mungu ni kuishi katika mapenzi na tabia yake iliyofunuliwa. Tazama Mada Maalum: Upendeleo wa Kiinjilisti katika 4:6.

Inafurahisha kwamba mengi ya haya “maandiko yazungumziayo baraka” yanajitokeza katika muktadha wa Israeli kuwasaidia maskini na wahitaji (mf. 14:29; 24:19).

ANDIKO LA NASB (LILILOBNORESHWA): 23:21-23

²¹ Utakapoweka nadhiri kwa Bwana, Mungu wako, usiwe mlegevu katika kuiondoa; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, hataacha kuitaka kwako; nayo hivi itakuwa dhambi kwako. ²² Lakini ukijizuia usiweke nadhiri, haitakuwa dhambi kwako. ²³ Yaliyotoka midomoni mwako yashike kuyafanya; kwa mfano wa ulivyomwekea nadhiri Bwana, Mungu wako, ni sadaka ya hiari uliyohidi kwa kinywa chako

23:21 “nadhiri” Sheria kuhusu viapo (BDB 623, KB 674, *Qal* KAULI YA WAKATIUSIO TIMILIFU, kama vile 12:11,17) zinajadiliwa katika Mambo ya Walawi 27 na Hesabu 30 (Nadhiri za ki-Nazariti zilizoelzwa katika Hesabu 6). Hizi zilikuwa ahadi zilizofanywa na YHWH zilizojikita katika matukio fulani na mambo fulani.

Kifungu hiki kina:

1. Iliyokanushwa *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ya BDB 29, KB 24
2. *Piel* KITENZI CHA MUUNDO WA MANENO cha BDB 1023, KB 1532

Ukiweka nadhiri, iondoe kwa wakati upasao!

☑ **“usiwe mlegevu katika kuiondoa”** Baadaye waalimu wa Kiyahudi waliufasiri wakati huu kama “si sikukuu tatu zilizopita” (yaani, mwaka moja).

☑ **“hataacha kuitaka kwako”** Kifungu hiki ni cha msistizo (KITENZI CHA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU cha asili ile ile, BDB 205, KB 233). YHWH anaweka nadhiri kwa jina lake kwa mkazo (kaa vile Muh. 5:1-7).

23:22-23 Hii inaonyesha hekima ya kutoweka nadhiri kwa haraka (mf. Waamuzi 11). Hili linaonyesha mtazamo wa Kiebrania wa uweza na umuhimu wa neno lililonenwa (mf. Mwanzo 1; Isa. 55:11; Yohana 1:1). YHWH anayachukua yale tunayoyazungumza kwa msistizo kwa jina lake (kama vile Kut. 20:7, yaani, nadhiri za ndoa na ahadi nyingine zilizowekwa jina lake; [yaani, “kutoka kinywani mwako”]).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 23:24

²⁴ Uingiapo katika shamba la mizabibu la jirani yako, utaweza kula zabibu za kukushibisha, kama upendavyo; ila usitie katika chombo chako.

23:24-25 “utaweza” Hii inaurejelea uhitaji wa ardhi, yatima, mjane, aliyetengwa, na maskini. Hii ilikuwa sehemu ya sheria ya kusanyiko. Hii inatajwa katika maandiko kadhaa (kama vile Law. 19:9-10; 23:22; Kumb. 24:21; Amu. 8:2; 20:45; Ruth 2; Isa. 17:6; 24:13; Yer. 6:9; 49:9; Mik. 7:1). Hii inaonyesha uangalizi wa Mungu kwa maskini na umiliki wa mazao.

23:24 “za kukushibisha” Huu ni muungano wa kifungu “kama upendavyo” (BDB 659) na “hitaji lako” (BDB 959, kama vile Kut. 16:3; Law. 25:19; Ruthu 2:18; Zab. 78:25; Mit. 13:25). Huu unazungumzia, si vile vinavyopatikana, bali kula vyote unavyovitaka. Huu ni utoaji wa kushangaza kwa maskini, wahitaji, na waliotengwa. Pia hakuna mipaka ya ni mara ngapi mtu anaweza kurudi.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 23:25

²⁵ Uingiapo katika mmea wa jirani yako waweza kuyapurura masuke kwa mkono wako; ila usisongeze mundu katika mmea wa jirani yako.

23:25 Mistari ya 24 na 25 yote inaonyesha kwamba wahitaji wanaweza kula cho chote wanachokitaka, lakini hawawezi kuchukua mazao yote kwa matumizi ya baadaye au kwa ajili ya kuuza (mf. Mt. 12:1-8; Marko. 2:23-28; Luka 6:1-5). YHWH huwajali wote maskini na haki za wakulima.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipambebele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mungu mtu ye yote awe sehemu ya watu wake kutokana na hao?
2. Kwa nini Mungu aliweka tofauti kati ya mataifa fulani?
3. Ni kwa namna gani taratibu za kujitakasa zilihusiana na dhambi iliyo katika Agano la Kale
4. Ni kwa namna gani mist 24-25 inaweka ulinganifu wa mtu kumiliki mali pamoja na maskini na wahitaji?

KUMBUKUMBU LA TORATI 24

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Sheria zinazohusu Kuachana	Sheria zinazohusika na huruma na wajibu wa dini (23:15-25:19)	Kuachana na kuolewa tena	Kuachana
24:1-4	24:1-4	24:1-4	24:1-4
Sheria mbalimbali 24:5	24:5	Sheria mbalimbali 24:5	Ulinzi wa kila mmoja 24:5
24:6-7	24:6	24:6	24:6
	24:7	24:7	24:7
24:8-9	24:8-9	24:8-9	24:8-9
24:10-13	24:10-13	24:10-13	24:10-13
24:14-16	24:14-15	24:14-15	24:14-15
	24:16	24:16	24:16
24:17-18	24:17-18	24:17-18	24:17-18
(24:19-25:4) 24:19-25:3	24:19-20	24:19-22	24:19
			24:20
	24:21-22		24:21
			24:22

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. wa vii katika kipengele cha utangulizi) **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (soma mzunguko #3.uk. viii). linganisha mgawanyo wako na tafsiri nne hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. Nk.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 24:1-4

¹ Mtu akiisha kutwaa mke kwa kumwoa, asipopata kibali machoni mwake, kwa kuwa ameona neno oву kwake, na amwandikie hati ya kumwacha, akamtilie mkononi mwake, na kumtoa katika nyumba yake. ² Naye akiisha kuondoka katika nyumba yake, ana ruhusa kwenda akawa mke wa mtu mwingine. ³ Na huyo mumewe wa sasa akimchukia, na kumwandikia hati ya kumwacha, na kumpa mkononi mwake, na kumtoa katika nyumba yake; au akifa yeye mumewe wa sasa, aliyemtwa kuwa mkewe; ⁴ yule wa kwanza aliyemwacha asimtwae kuwa mkewe tena, akiisha kutiwa unajisi; kwa kuwa haya ni machukizo mbele za Bwana; kwa hiyo usitie dhambini nchi, akupayo Bwana, Mungu wako, iwe urithi.

24:1-4 “akiisha. . .kwa hiyo” Muundo huu ni wa *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (BDB 224, KB 243) “hata ikawa” na KAULI ENDELEU isiyu na uhakika (BDB 49). Hali hii ya nadharia tete ni endelevu kwa ajili ya mistari mitatu ya kwanza. Mistari ya 1-4 ni sentensi moja yenye hitimisho inayoelezewa katika mst. 4. Tambua kwamba huu sio mjadala wa jumla juu ya talaka, lakini ni jambo maalumu la talaka, kuoana tena, na talaka/kifo na kuolewa na mme wa awali. Ni vigumu pia kuelezea kweli nyingi za ulimwengu kutoka katika muktadha huu. Hata Yesu alijadili juu ya kifungu hiki na jambo la talaka lilifunika na viongozi wa dini wakijaribu kumnasa yeye katika mabishano kwa makusudi ya kupunguza utetezi wake kati ya watu na kutafuta uhalali/msingi wa kitheolojia ili kumtia hatiani. Talaka haijawai kuwa chaguo bora kamwe!

☐ **“ asipopata kibali machoni mwake ”** KITENZI hiki kilichozoeleka (BDB 592, KB 619) kimetumika mara tatu katika mstari huu (kwanza, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU na pili *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU). Kimetumika katika maana ya “kutambua sharti lililopo” (k.v. 22:14,17).

Neno “upendeleo” (BDB 336) kote limetumika kama upendeleo wa Mungu (mf, Mwa. 6:8; Kut. 33:17) na mwanadamu (mf, Mwa. 30:27; 33:8,10,15; Ruthu 2:2,10,13). Linamaanisha ukubalifu ufao au mtazamo wa uwajibikaji. Hapa linakanushwa. Linatambua hali ya anguko la upendo wa mwanadamu, ambao wakati mwingine ni mwepesi na kubadilika badilika.

Andiko hili limekua chanzo kikuu cha mabishano kati ya walimu wa kiyahudi. Shammai (kundi la walimu wa kiyahudi wapenda mabadiliko) wanasema linarejelea kwenye uzinzi pekee, ambapo Hillel (kundi la walimu wa kiyahudi wasiopenda mabadiliko) wanasema linaweza kurejelea kwa kila kitu, hata mambo yasiyo na maana (yaani, chakula kibaya, mahusiano mabaya katika sheria, kumpata mwanamke mzuri). Katika Israeli mwanamme pekee ndiye mwenye haki ya kutoa talaka.

☐

NASB “ uovu kwake”
NKJV “uchafu kwake”
NRSV “kitu kama kipingamizi”
TEV “ kitu asichopenda juu yake”
NJB “ uchafu kadhaa”
JPSOA “ machukizo kadhaa”

Ni dhahili hili linamaanisha “utupu wa kitu” (BDB 788). Katika 23:14 neno lile lile limetumika katika maana ya isiyu ya kimaadili. Hii haiwezi kurejelea asili ya uzinzi kwa sababu adhabu yake kwa kawaida ilikuwa ni kifo (k.v. 22:22). Yesu, aliponukuu andiko hili, inaonekana alilitafsiri neno “uzinzi” katika Mt. 19:9, ambalo ni neno la kiyunani (*porneia*) linalohusisha utovu wa nidhamu wa mapenzi au kutokuwa mwaminifu katika ndoa. Neno linaleta utata, na hivyo linafunika sehemu kubwa ya tukio.

Musa aliandika andiko hili ili kumlinda mwanamke aliyekataliwa. Inanishangaza mimi kwamba Yesu anadai kuwa utetezi wa kisheria wa kutoa talaka na kurudiana tena kwa wanandoa kamwe halikuwa kusudi la Mungu (k.v. Mt. 5:27-32; 19:7-12; Marko 10:2-12; Luka 16:14-18), lakini nia ya Musa ni kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya wana wa Israeli. Ni kwa namna gani mambo mengine kadhaa yaliyoandikwa katika vitabu vitano vya kwanza vya Biblia hayakusudii mapenzi ya Mungu? Yesu, kama Bwana wa maandiko, anaonyesha mamlaka yake kwa kukusanya maandiko yote ya Agano la kale na tafsiri zao (k.v. Mt. 5:17-48; Marko 7:1-23). Hili linatuhuzunisha sisi

kwa wainjilisti wa leo ambao hutilia mkazo wa Biblia kama “neni la Mungu” (na hakika ni kweli!), lakini ni lazima tukumbuke kwamba Yesu ni neno lililo hai na na tuna sehemu kidogo pekee ya mambo yote aliyotenda na kuyasemea (k.v. Yohana 20:30). Biblia ni msingi wa awali uliopangwa ili kutupatia wokovu (k.v. Yohana 20:31; II Tim. 3:15) na kisha kutuongoza katika maisha ya Ukristo (k.v. II Tim.3:16-17). Tuna taarifa zote ya kwamba tunahitajika kuokolewa na kuishi maisha ya kumpendeza Mungu. Hatuhitaji sheria na amri nyingine. Maandiko tuliyonayo na uongozi wa Roho akaaye ndani yetu hutuongoza katika sehemu yenye mashaka. Ninakumbuka kwamba Yesu alisema maandiko yote ya mafundisho juu ya namna gani tuishi kwa ajili ya Mungu yamejumuishwa katika maelezo mawili pekee ya awali (k.v. Mt. 22:34-40; Marko 12:28-34; Luka 10:25-28):

1. Kumb. 6:4-5 – mpende Mungu kikamilifu
2. Law. 19:18 – mpende jirani yako kama nafsi yako

☐ **“hati ya kumwacha”** Hii ni hati halali ya matengano. Yumkini ilihusisha kurudisha mahari. Hii baadae ilihitajika kuhusisha utaratibu halali ambao kwa matumaini ulitoa muda kwa wanandoa kupatana, lakini hapa inaonekana kuandikwa na mme au mwakilishi wake (yaani, Mlawi).

Kuachana na kurudiana tena pia kumejadiliwa katika uhusiano wa makuhani katika Law. 21:7,14 na 22:13. Ni lazima kufanane (k.v. Hes. 30:9).

24:2 “akawa mke wa mtu mwingine” haki ya kuolewa tena ilikuwa inaelezwa na kuthibitishwa. Hili lilikuwa ni kusudi la utaratibu.

24:3 “Na huyo mumewe wa sasa akimchukia” Neno “na huyo” halipo katika toleo la kiebrania MSS . Ni hali ya uthibitisho mwingine usio na uhakika (kama mst. 1).

KITENZI hiki “kugeuka” kiuhalisia ni “kuchukia” (BDB 971, KB 1338, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) na kimetumika katika Kiaramu kwa ajili ya “kumwacha.”

☐ **“akifa yeye mumewe wa sasa”** Huu unawezekana ni mpangilio wa tukio lingine la baadaye.

24:4 “yule wa kwanza asimtwae kuwa mkewe tena” Mumewe wa awali anatiwa moyo ili wapatane (utaratibu halali wa hati ya kuachana), lakini wakiachana na mwanamke akaolewa tena, mapatano hayaruhusiwi! Hili ndilo kusudi la masharti yaliyoko katika mist. 1-3. Yumkini hii ikawa ni njia ya kulinda ndoa ya pili.

☐ **“akiisha kutiwa unajisi”** Unajisi unaonekana kuhusishwa na tendo la kujamiana na wanaume wawili tofauti, ambapo itakua ni aina ya uzinzi ikiwa mwanaume wa awali atamchukua tena kuwa mkewe!

Utata wa maneno ya kifungu hiki ni vigumu kuelezea kanuni za kiroho kwa ulimwengu. Huu sio muktadha wa kuachana kwa uovu na kuolewa tena, bali kwa mume wa awali kumchukua tena mkewe waliyechana baada ya ndoa ya pili. Kuachana na kuolewa tena ilikuwa ni jambo lililozoeleka katika mashariki ya karibu ya kale.

Fasiri ya awali ya Biblia toleo la IVP lina maoni yenye shauku:

“Muundo usio wa kawaida wa kitenzi cha kiebrania kilichotumika katika mstari wa 4 unaweka wazi kuwa mwanamke katika jambo hili ni mwathirika, sio sehemu ya hatia. Analazimishwa kutoa tamko la uchafu wake bila huruma matendo ya mume wake wa awali, na ndoa yake ya pili kuthibitisha kwamba mume mwingine ana uwezo wa kumsaidia kivyovyote vile kwa ‘unajisi’ aliotenda nae. Lengo la amri hii ni kuzuia mume wa awali kumuoa mwanamke huyu tena (kwa jambo ambalo anageweza kuongeza baadhi ya mali), ambapo ikiwa mwanamke alikuwa najisi amri ingekuwa juu yake na anaweza kuzuia mahusiano ya ndoa na mtu yeyote” (uk. 198).

☐ **“kwa hiyo usiitie dhambini nchi”** Mungu anatamani ndoa za wacha-Mungu na familia imara. Wakitoa uwezo, uthabiti, na elimu kwa ajili ya kizazi kinachofuata cha watu wa maagano. Ndoa imefanywa kuwa mfano zaidi kuliko kufundisha! Kuachana sio dhambi, bali mume wa awali kumchukua tena mwanamke wake baada ya kuolewa na mume mwingine!

Manabii wawili wanatumia kifungu hiki cha stiari kuelezea uhusika wa Mungu na uaminifu wa Israeli (Isa.

50:1; Yer. 3:1,8). Kuifuata miungu mingine ilifikiriwa ni “uzinzi wa kiroho.”

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 24:5

⁵Mtu atwaapo mke mpya, asiende vitani pamoja na jeshi, wala asipewe shughuli juu yake yo yote; akae faragha mwaka mmoja nyumbani mwake, apate mfurahisha mkewe aliyemtwa.

24:5 “Mtu atwaapo mke mpya ” Mtu atwaapo mke mpya hakutakiwa kwenda kuhudumu katika jeshi au shughuli zingine za kiraia kwa mwaka mmoja. Hii ilikuwa kwa kusudi la kuthibitisha urithi (k.v. 20:7).

☐ **“apate mfurahisha mkewe aliyemtwa ”** KITENZI hiki (BDB 970, KB 1333, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinamaanisha “kufurahia” au “kufurahi.” Hili lilikuwa kusudi la YHWH kwa ajili ya watu wake wa agano. Sheria za Kumbukumbu la Torati zilikuwa ni kumsaidia mwanadamu aliyeanguka ili kupata na kudumisha furaha, katika jamii yenye furaha.

Toleo la NIDOTTE, juzuu. 3, uk. 1252, lina nukuu njema kwa jambo hili:

“furaha pia itakuwa ya manufaa katika mahusiano ya kifamilia. Musa alimsihi mtu aliyeoa kujitenga binafsi ili kumfanya mkewe awe na furaha (Kumb. 24:5) na kumshauri kwa hekima mume ili kumfurahia mke wa ujana wake (Mit. 5:18). Ingawa baba wa mpumbavu hana furaha (Mit.17:21), mwana mwenye hekima humfurahisha babaye (Mit.10:1; 15:20; 23:24-25; 27:11; 29:3).”

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 24:6

⁶Mtu awaye yote asitwae jiwe la kusagia, la juu wala la chini, kuwa rehani; kwani hivi ni kutwaa maisha ya mtu kuwa rehani.

24:6 “jiwe la kusagia, la juu wala la chini ” Hii inarejelea jiwe la juu kati ya mawe mawili ya kusagia unga (BDB 932, 939, k.v. Kut. 11:5; Amu. 9:53; II Sam. 11:21), ambalo lilitumika kutengeneza unga wa kuandalia mkate wa kila siku. Jiwe la juu halikutumika bila ya kuliunganisha na jiwe la chini.

☐ **“kuwa rehani”** Neno hili, “kuwa rehani,” (BDB 286, KB 285) kimsingi linamaanisha “tia sharti.” Mtu anapokopa anatakiwa kulipa. Ili kulinda malipo haya (bila riba kwa ndugu mwisraeli) mkopeshaji anaweza kuchukua kitu chenye thamani na kukizuia:

1. Jiwe la kusagia, 24:6
2. nguo, 24:17; Kut. 22:25-27; Ayub 24:7,10
3. Nchi na nyumba ya familia, Neh. 5:3 (inawezekana Ayub 24:2)
4. Mnyama muhimu, Ayub 24:3
5. Msaada muhimu, kwa wana, Kut. 21:7; Law. 25:39-43; II Fal. 4:1; Ayub 24:9

Vitu hivi kila kimoja kilikuwa ni sehemu muhimu kwa uwepo wa kilimo kila siku. Kwa kuondoa mojawapo ya hivi kulihatarisha familia, hata uzima wake. Huruma za YHWH na kuwajali Israeli ilikuwa ni kuwafuatisha waisraeli waliokuwa na mali. Mungu atawabariki kwa ajili ya huruma zao. Watapewa zaidi ili kwamba waweze kugawa zaidi (k.v. mst. 13; II Kor. 9:6-10).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 24:7

⁷Mtu akionekana anamwiba nduguze mmojawapo katika wana wa Israeli, akamfanya kama mtumwa, au kumwaza; na afe mwivi huyo; ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako.

24:7 “anamwiba” KITENZI cha kiebrania hapa ni “kuiba” (BDB 170, KB 198, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILU). “anamwiba” kinaonekana kama kuiba uzima (dhahili, “kuiba *nephesh*, BDB 659). Wengi wanaamini hiki ndicho kile amri kumi zinakirejelea kwa mamlaka “usiibe.” Hukumu yake ilikuwa ni kifo, ambayo imeonekana mara kadhaa kwa wizi wa kawaida (k.v. Kut. 21:16; Kumb. 5:19).



NASB “akamfanya... mtumwa”
NKJV “kumtesa”
NRSV “utumwani”
TEV “kuwafanya watumwa wako”
NJB “akamfanya kuwa mtumwa wake”

Asili hii (BDB 771) ina maana kadhaa:

1. mganda, Kumb. 24:19 au miganda iliyofungwa, Zab. 129:7
2. pishi - BDB I, Kut. 16:18,22,32,33
3. Makubaliano dhalimu - BDB II, Kumb. 21:14; 24:7
4. Maisha marefu (Asili ya kiarabu) - BDB III

Maoni na muktadha uliochaguliwa ambao unamaanishwa ulikuwa umepangwa kwa asili ya pande tatu hizi. Chaguo #3 linapatikana mara tatu pekee katika Agano la Kale, yote katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati.

☐ **“ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako ”** Hii ni Nahau inayojirudia rudia. Tazama muhtasari katika 13:5 (k.v. 17:7,12; 19:13,19; 21:9,21; 22:21,22,24; Amu. 20:13).

ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA): 24:8-9

⁸ Angalia katika pigo la ukoma, utunze kwa bidii, kwa kufanya mfano wa yote watakayowafundisha makuhani Walawi; tunzeni kwa kuyafanya vile vile kama nilivyowaamuru wao. ⁹ Kumbukeni na Bwana, Mungu wako alivyomtenda Miriamu katika njia mlipotoka Misri.

24:8 “angalia” KITENZI hiki (BDB 1036, KB 1581) kimetumika mara tatu katika mstari huu:

1. *Niphal* KAULI SHURUTISHI, “angalia”
2. *Qal* KITENZI JINA CHA MUUNDO WA MANENO, ongeza KIELEZI “sana” (BDB 547) na KITENZI “kwa kufanya” (BDB 793, KB 889, *Qal* KITENZI JINA CHA MUUNDO WA MANENO)
3. *Qal* ukosefu, “angalia ukafanye” ongeza KITENZI “kwa kufanya” (BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)

Maana ya kimsingi ya neno ni “kutunza,” “kuangalia,” au “kulinda.” Angalia uwe mtiifu kwa maongozi ya YHWH yamesisitizwa kwa kurudiwa rudiwa mara tatu.

☐ **“ukoma”** Huu (BDB 863) sio ugonjwa wa leo kama tunavyoufahamu. Neno hili limefunika mambo mengi tofauti (yaani, ngozi, mavazi, ngozi laini, nyumba). Mwongozo na utaratibu umejadiliwa katika Mambo ya Walawi 13-14. Hii inadokeza kwamba Walawi tayari walikuwepo kwa muda huu. Vitabu vitano vya kwanza vya Biblia vimeyaunganisha yote.

24:9 Tukio hili limerejelewa kama lilivyoandikwa katika kitabu cha Hesabu 12, ambapo wote Haruni na Miriamu walinung’unuka juu ya uongozi wa Musa kwa ajili ya kumuoa mwanamke Mkushi (mwanamke mweusi). Kwa kujibu YHWH anauthibitisha uongozi wa Musa na kumpiga Miriamu kwa ukoma (Miriamu alipoteza rangi ya ngozi yake),lakini kwa maombi ya Musa, alirejeshewa rangi yake.

ANDIKO LA NASB (LILLOBORESHWA): 24:10-13

¹⁰ Umkopeshapo jirani yako cho chote kikopeshwacho usiingie katika nyumba yake kwenda kutwaa rehani kwake. ¹¹ Simama nje, yule umkopeshaye akuletee nje ile rehani. ¹² Naye akiwa ni mtu maskini, usilale na rehani yake. ¹³ Sharti umrudishie rehani lichwapo jua, apate kulala na mavazi yake, na kukubarikia; nayo itakuwa ni haki kwako mbele za Bwana, Mungu wako.

24:10 “usiingie katika nyumba yake kwenda kutwaa rehani kwake ” Heshima na faragha ya mwenye nyumba ilikuwa inatunzwa. Mtu huyu pia aliweza kuchagua ni nguo ipi aitumie kama rehani.

KITENZI hiki (BDB 716, KB 778, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO) kimetiliwa mkazo kwa kutumia NOMINO ile ile (BDB 716) ya neno “rehani.” Rehani ilikuwa ni kitu cha kushikika, katika muktadha huu, nguo ya nje ya mtu ilitumika kama ulinzi kwa ajili ya mkopo (k.v. mist. 11-13).

Nguo hizi hazikuwa za thamani sana, lakini zilikuwa za muhimu kwa mahitaji ya kila siku ya maskini. Kuchukua nguo ya mtu ilikuwa ni zaidi ya ulinzi kwa ajili ya mkopo. Ilikuwa ni kudhihirisha dharau kwa ajili ya mtu maskini. Katika macho ya Mungu wanadamu wote wana thamani kwa sababu wameumbwa kwa mfano wake na sura yake (k.v. Mwa. 1:26-27). Watu wa agano la Mungu ni lazima watambue thamani na maana aliyoiweka kwa wanadamu yenye kufaa kuipokea!

24:12 “Naye akiwa ni mtu maskini, usilale na rehani yake” Hii inarejelea joho ambalo maskini hulitumia kujifunika wakati wa kulala (k.v. Kut. 22:26-27).

24:13 “Sharti umrudishie ” Hiki ni KITENZIJINA HALISI kilichounganishwa na KITENZI KISICHO TIMILIFU cha asili ile ile (BDB 996, KB 1427), kinachodokeza mkazo.

☐ **“na kukubarikia ”** YHWH anawalinda maskini, mjane, mgeni, na yatima mwenye haki na mtu. Kuwatesa watu hao kuna sababisha hasira kutoka kwa YHWH mwenyewe (mf, Kut. 22:23; Kumb. 15:9; 24:15)!

☐ **“nayo itakuwa ni haki kwako ”** Tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania yanalitambua neno hili kama lilivyotumika hapa ili kurejelea kwa Wayahudi juu ya “utoaji sadaka” (kv. 6:25; 15:7-11; Mt. 6:1-4).

MADA MAALUMU: KUWAS Aidia WAHITAJI

- I. Neno lenyewe
 - A. Neno hili lilikuwa ndani ya Uyahudi.
 - B. Hili linarejelea kuwapa wahitaji na/ama maskini.
 - C. Neno la Kiyunani, kuwasaidia wahitaji, linatokana na ufupisho wa neno la Kiyunani *eleēmosunē*.
- II. Dhana ya Agano la Kale
 - A. Dhana ya kuwasaidia wahitaji iliidhinishwa katika torati ya kale
 1. Muktadha unaofanana, Kumb. 15:7-11
 2. kusaza," kubakiza sehemu ya mavuno kwa wahitaji, Law. 19:9; 23:22; Kumb. 24:20
 3. "mwaka wa sabato," uliwaruhusu maskini kula mazao ya mwaka ambao hawakulima,
 - B. Dhana hii iliendelezwa katika Hekima ya Fasihi (mifano iliyoteuliwa)
 1. Ayubu 5:8-16; 29:12-17 (Yule dhalimu anaelezewa katika 24:1-12)
 2. Zaburi, 11:7
 3. Mithali 11:4; 14:21,31; 16:6; 21:3,13
- III. Uendelezwaji katika Uyahudi
 - A. Mgawanyo wa kwanza huko Mishna unashughulika na kuwatunza wahitaji, maskini, na Walawi wa mahali pale pale.
 - B. Nukuu zilizoteuliwa
 1. Kitabu cha Mhubiri (pia kinajulikana kama Hekima ya Bin Sira) 3:30, "kama maji yazimishavyo ndimi za moto, ndivyo kuwasaidia wahitaji kulipiavyo dhambi" (NRSV)
 2. Tobiti 4:6-11, ⁶"Maana ukitenda vitu kwa uaminifu utafanikiwa katika mambo yako yote. ⁷Toa sehemu ya mali yako kuwapa maskini. Kamwe usimpe kisogo mtu maskini naye Mungu hatakupa kisogo. ⁸Toa ulicho nacho. Ukiwa na zaidi, toa zaidi. Hata kama unacho kidogo tu, toa sehemu yake ⁹Kwa kufanya hivyo utajiwekea hazina bora kwa wakati wa shida. ¹⁰Kwa maana kusaidia maskini huokoa mtu kifoni na kumkinga asiingie katika makao ya giza. ¹¹ Naam! Kusaidia maskini, kwa wale wanaofanya hivyo, ni sadaka bora mbele ya Mungu Mkuu." (NRSV)

3. Tobiti 12:8-9, "⁸Afadhali sala pamoja na ukweli na kusaidia maskini pamoja na kutenda haki kuliko kuwa tajiri na kukosa uaminifu. ⁹Sadaka kwa maskini humwoko mtu na kifo na kumtakasa dhambi zake. Wale wanaowasaidia maskini watajaliwa uhai." (NRSV)
- A. Nukuu ya mwisho kutoka Tobiti 12:8-9 inaonyesha uendelevu wa tatizo. Matendo ya mwanadamu/ faida za mwanadamu zilionekana kama utaratibu kwa misamaha yote na utele.
- B. Dhana hii iliendelea baadaye katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani ambapo neno la Kiyunani la "kuwasaidia wahitaji" (*eleēmosunē*) lilikujakuwa kisawe cha neno "mwenyehaki" (*dikaiosunē*). Haya yangeweza kubadili kila kitu katika kutafsiri Kiebrania "mwenye haki" (BDB 842, agano la upendo wa Mungu na uaminifu, kama vile Kumb. 6:25; 24:13; Isa. 1:27; 28:17; 59:16; Dan. 4:27).
- C. Matendo ya mwanadamu ya huruma huwa na kusudi ndani yake ili kufanikisha utele wa mtu binafsi, hapana wokovu wakati wa kifo. Tendo lenyewe, badala ya nia iliyo nyuma ya tendo, huwa sifa ya kitheolojia. Mungu huangalia mioyo, kasha hupima kazi ya mikono. Hili lilikuwa fundisho la Walimu wa sheria za Kiyahudi, lakini kwa kiasi Fulani hii imepotezwa katika haki binafsi (kama vile Mika 6:8).

IV. Wajibu wa Agano Jipya

A. Neno hili linapatikana katika

1. Mt. 6:1-4
2. Luka 11:41; 12:33
3. Matendo ya Mitume 3:2-3,10; 10:2,4,31; 24:17

B. Yesu anaelezea uelewa wa kitamaduni kuhusu haki (kama vile II Clement 16:4)

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 24:14-15

¹⁴Usimwonee mtumishi mwenye ujira aliye maskini na uhitaji, kama ni wa nduguzo, au kama ni wageni wako mmojawapo walio katika nchi yako, ndani ya malango yako; ¹⁵ mpe ujira wake kwa siku yake, wala jua lisichwe juu yake; kwa maana ni maskini, moyo wake umeutumainia huo; asije akamlilia Bwana juu yako, ikawa ni dhambi kwako.

24:14 "au kama ni wageni wako " Uangalizi wa Mungu kwa ajili ya mjane, yatima, na mgeni unaonekana dhahili katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (k.v. 10:18; 14:29; 16:11,14; 24:17,19,20,21; 26:12,13; 27:19).

24:15 "mpe ujira wake kwa siku yake " Maskini alihitaji (yaani, "moyo wake uliutumainisha hapo") ujira wa siku ili kununua chakula kwa ajili yake na familia yake. Mwajiri alitaka kuutunza ujira ili kuhakikisha kwamba mfanyakazi anaweza kurudi kazini siku inayofuata (k.v. Law. 19:13; Mal. 3:5; Yakobo 5:4).

☐ **"asije akamlilia Bwana juu yako "** Uangalizi wa Mungu na kusikiliza kilio cha maskini, unafarikisha na kutenganisha! Tazama muhtasari katika 24:13.

☐ **"ikawa ni dhambi kwako"** Katika muktadha huu hiki ni kinyume cha neno "haki" katika mst. 13.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 24:16

¹⁶ Mababa wasiuawe kwa ajili ya watoto wao, wala watoto wasiuawe kwa ajili ya baba zao; kila mtu na auawe kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe.

24:16 Hii inafanana sana na Ezek. 18:1-33; 17:12-20; Yer. 31:29-30; na II Fal. 14:6. Inalenga katika dhana nzuri mno ya kuwajibika kila mmoja katika Agano la kale. Huu ni uwiano kwa Kut. 20:5; 34:7; Hes. 14:18. Kwa kawaida Agano la Kale lililenga katika mwili (k.v. Kumb. 5:9).

Tambua mabano-matatu yametumia katika KITENZI “wasuuawe” (BDB 559, KB 562, zote *Hophal* KAULI ZA WAKATI USIO TIMILIFU). Uasi ni jambo la hatari sana! Kutokutii kuna matokeo!

Sheria hii hairejelei kwa uasi dhidi ya Mungu (mf, ibada ya sanamu), lakini kwa matendo yaliyochaguliwa na jamii (mf, matendo dhidi ya kuimarisha mamlaka ya kiraia au matendo dhidi ya ndugu wa agano).

Wanadamu wanawajibika kushikiliwa kwa ajili ya dhambi ya mtu, lakini mara nyingi dhambi hizi zinahusishwa kwa familia au desturi za utamaduni. Sisi sote ni wa kihistoria, hali ya kiutamaduni. Tunafanya maamuzi, lakini maamuzi haya yana mipaka kwa kuongozwa. Jamii, familia, na kila mmoja wameunganishwa pamoja bila kutenganishwa! Wote wanaathiriwa na wazazi, utamaduni, na maamuzi ya mtu! Mungu anaihukumu jamii, familia, na kila mmoja. Uhuru wa wanadamu ni zawadi ya ajabu/kushangaza!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 24:17-18

¹⁷Usipotoshe hukumu ya mgeni, wala ya yatima; wala usitwae mavazi ya mjane, yawe rehani; ¹⁸ bali kumbuka ya kuwa ulikuwa mtumwa katika Misri, Bwana, Mungu wako, akakukomboha huko; kwa hiyo nakuamuru kutenda neno hili.

24:17 “Usipotoshe hukumu ” KITENZI hiki (BDB 639, KB 692) kimsingi kinamaanisha “pindisha,” “tawanya” au “geuka.” Mara nyingi hiki kimetumia stiari ya “kugeuka kulia au kushoto na kuiacha sheria ya Mungu iliyofunuliwa dhahili” (k.v. Kumb. 5:32; 17:11,20; 28:14; Yosh. 1:7; 23:6).

Kuna sehemu kadhaa ambapo kusudi hili la kugeuka/kupotosha ni “haki” (BDB 1048, k.v. Kut. 23:6; Kumb. 16:19; 24:17; 27:19; I Sam. 8:3; Mit. 17:23; Omb. 3:35; na Amos 2:7). Haki ni mapenzi ya YHWH kwa ajili ya kila mmoja katika jamii ya Israeli kwa sababu inafunua tabia yake na kuwajali wao (k.v. 32:4).

☐ **“mgeni, wala ya yatima; wala usitwae mavazi ya mjane, yawe rehani ”** Tazama 10:18 na Kut. 22:22-24. Muundo wa sheria ya Musa ni tofauti na muundo wa sheria nyingine za Mesopotamia ya kale katika kuwajali maskini, mhitaji, na jamii iliyo dhaifu!

24:18 “bali kumbuka” Tambua kwamba mkazo huu unahusiana na Kumbukumbu (BDB 269, KB 269, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) umetajwa mara tatu katika sura hii (24:9,18,22). Wakati wa sasa unaweza kuathiri wakati ujao. Israeli walitakiwa kukumbuka na kisha kutenda kwa usahihi leo!

☐ **“akukomboha”** Tazama Mada Maalumu katika 7:8.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 24:19-20

¹⁹Uvunapo mavuno yako katika shamba lako, ukasahau mganda shambani, usirudi kuuchukua; na uwe wa mgeni, au yatima, au mjane; ili Bwana, Mungu wako, akubariki katika kazi yote ya mikono yako. ²⁰ Utakapochuma matunda ya mizeituni yako, usirudi kuchuma mara ya pili; yaliyobaki apewe mgeni, na yatima, na mjane.

24:19-21 Kanuni hizi za kilimo zilimaanisha kutoa chakula kwa ajili ya maskini na mhitaji (tazama Law. 19:9-10; 23:22; Ruthu 2). Hii iliitwa “masazo ya mavuno.”

Kuna sheria kadhaa katika Kumbukumbu la Torati juu ya utoaji wa chakula kwa ajili ya mhitaji:

1. Mwaka wa tatu toa fungu la kumi kwa ajili ya maskini, 14:28-29; 26:12-15
2. Chakula kilitolewa wakati wa kusherehekea sikukuu ya majuma/sikukuu ya vibanda, 16:9-17
3. Masazo ya mavuno ya mwaka kutoka katika mavuno ya mwaka, 24:19-21

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 24:21-22

²¹Uchumapo zabibu katika shamba lako la mizabibu, usichume mara ya pili; zilizobaki apewe mgeni, na yatima, na mjane. ²² Nawe kumbuka ya kuwa ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri; kwa hiyo nakuamuru kutenda neno hili.

24:22 Wana wa Israeli walitakiwa kuwa na huruma kwa watumishi na wageni kwa sababu na wao warishiriki hali hii huko Misri. Mungu aliwaonea huruma wao, hivyo, pia nao inawapasa kuwaonea huruma wengine!

Mara nyingi katika Kumbukumbu la Torati wito wa kukumbuka kipindi cha utumwa wa Israeli umetumika kuchochea matendo ya leo:

1. Jamii yote kuitunza sabato, 5:12-15
2. Kuachilia watumwa wa Waisraeli katika mwaka wa saba, 15:12-18
3. Jamii yote kushiriki katika sikukuu ya majuma, 16:9-17
4. Usipotoshe hukumu ya mgeni au yatima, wala usitwae mavazi ya mjane yawe rehani, 24:17-18
5. Usivune shamba lote na usirudi kuvuna mara ya pili, 24:19-22
6. Kutumia maneno mengine, lakini na mkazo ule ule, utiifu, 6:10-15; 8:2,18

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani Kumbukumbu la Torati 24:1-4 linahusisha kuachana na kuolewa tena?
2. Ni kwa namna gani hili linahusisha maneno ya Yesu katika kuachana?
3. Orodhesha misingi ya kibinadamu katika sura hii.
4. Kwa nini mst. 16 ni muhimu sana? Unahusishwa na Kumbukumbu la Torati 5:9.

KUMBUKUMBU LA TORATI 25

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Sheria anwai (24:5-25:4)	Sheria zinazoshughulika na Wajibu wa kidini na huruma (23:15-25:19)	Sheria mbalimbali (24:5-25:4)	Ulinzi wa mtu binafsi (24:5-25:4)
24:19-25:3			
	25:1-3	25:1-3	25:1-3
25:4	25:4	25:4	25:4
Kazi ya mwenye kumrithi Mke wa nduguye		Kazi ya mwenye kumrithi nduguye	Sheria za Kilawi
25:5-10	25:5-10	25:5-10	25:5-10
Sheria anwai		Sheria nyinginezo	Staha katika mapigano
25:11-12	25:11-12	25:11-12	25:11-12
			Viambatisho
25:13-16	25:13-16	25:13-16	25:13-16
Uwaangamize Wamaleki		Amri ya kuwaua Wamaleki	
25:17-19	25:17-19	25:17-19	25:17-19

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Maeneo tofauti yaliyolindwa na sheria za Musa
 1. Sheria ya jinai
 2. Sheria zenye kuhusu raia

3. Sheria ya familia
 4. Sheria ya ibada
 5. Sheria ya hisani
- B. Kwa ajili ya mjadala mzuri juu ya uwasilishaji wa sheria na naman ya kuzitumia siku za leo tazama:
1. *Introduction to Biblical Interpretation* by Klein, Blomberg, and Hubbard, kur. 278-283
 2. *How To Read the Bible for All Its Worth* by Fee and Stuart, kur. 163-180
 3. *Cracking Old Testament Code*, chapter 6, "Law" by Richard E. Everbeck, kur. 113-138

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 25:1-3

¹ Pakiwa na mashindano kati ya watu, wakaenda maamuzini, na hao waamuzi wakawaamua; na wampe haki mwenye haki, na wamhukumie makosa yule mwovu; ² na iwe, ikimpasa kupigwa yule mwovu, alazwe chini na mwamuzi, na kupigwa mbele ya uso wake, kwa kadiri ya uovu wake, kwa kuhesabu. ³ Aweza kumpiga fimbo arobaini asizidisha asije akaonekana nduguyo kuwa amedharauliwa kwako, azidishapo kwa kumpiga fimbo nyingi juu ya hizi.

25:1 "Pakiwa na mashindano" Hili linarejelea kwenye kesi ya kisheria kati ya ndugu wa agano (BDB 936, k.v. 17:8-13; 19:17; 21:5). Kesi za kisheria zinamaanisha kuzuia kulipiza kisasi wewe mwenyewe.

☐ **"mwenye haki"** Mahakama hufanya maamuzi ya haki na sahihi (k.v. 1:16-17). KITENZI (BDB 842, KB 1003, *Hiphil* KAULI ILIYO TIMILIFU) na KIVUMISHI (BDB 843) vinatoka kwenye asili moja ya neno. Tazama Mada Maalum: Haki katika 1:16.

☐ **"wamhukumie makosa yule mwovu"** Kama mfanano uliopita hapo juu, hili linahusiana na KITENZI (BDB 957, KB 1294, *Hiphil* KAULI ILIYO TIMILIFU na KIVUMISHI (BDB 957) vyenye kutoka katika asili moja .

25:2 "mwamuzi" Huenda hili ni (1) kumtii Mlawi au (2) kumkamata Mlawi. Baadaye dini ya Kiyahudi ilihitaji mashuhuda watatu kwa ajili ya kutoa adhabu ya kupiga, Mpigaji, na msoma maandiko.

☐ **"mbele ya uso wake"** Hili kiuhalisia ni "mbele ya uso wake," lenye kumaanisha mwamuzi lazima aangalie kuhakikisha adhabu inatekelezwa. Kifungu hiki kilitafasiwa baadaye na dini ya Kiyahudi kurejelea sehemu ya kumpiga yule anayetaka kuadhibiwa, "kupigwa kifuani moja ya tatu ya idadi ya fimbo anazotakiwa kupigwa na mgongoni theruthi mbili ya idadi ya fimbo anazostahili kupigwa."

☐ **"idadi ya fimbo kulingana na kosa lake"** Adhabu ilitolewa kulingana na kosa. Idadi ya ya mapigo ilitofautiana (k.v. Neh. 13:25).

25:3 "mara arobaini" Hii ndiyo ilikuwa hesabu ya juu ya mapigo ya fimbo aliyostahili (k.v. Kut. 21:20; sheria za Ashuru ya Kati, A18) au mjeredi uliotengenezwa kwa ngozi. Kipindi cha Agano Jipya ilikuwa viboko therathini na nane kiwango cha juu (k.v. Mishnah Makkoth, III, 13-14; II Kor. 11:24).

☐ **"fimbo"** Neno hili (BDB 912 I) linamaanisha alama za kufungwa. Lina elimu maana pana na laweza kurejelea (1) kovu (k.v. Isa. 1:6) au (2) ugonjwa (k.v. 28:61).

☐ **"nduguyo kuwa amedharauliwa kwako"** Hata kwenye adhabu roho ya usamaria ilitawala. Urejeshaji na tabia zilizobadilika ndiyo lilikuwa lengo.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 25:4

⁴Ng'ombe apurapo nafaka usimfunge kinywa.

25:4 “**Ng'ombe apurapo nafaka usimfungue kinywa**” Hili lilionesha kuwahurumia wanyama (k.v. 22:6-7; Mith. 12:10). Hili lilitumiwa na Paulo katika Agano Jipya ili kuwezesha ujira kwa viongozi wa Kikristo (k.v. I Kor. 9:9; I Tim. 5:18). Paulo anatumia (1)maneno ya Yesu katika Luka 10:7 (k.v. I Tim. 5:18) na (2) namna ya sheria za Kiyahudi ya utafasiri na matumizi yake iliyoitwa “dogo zaidi kwenda kubwa.” Kama maelezo haya ni kweli kwa ajili ya ng'ombe, hakika yatakuwa ya kweli kwa ajili ya binadamu wenye kufanya kazi. See *Expository Hermeneutics* by Elliott E. Johnson, kur. 235-236.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 25:5-10

⁵Watakapoketi pamoja mtu na nduguye, mmojawapo akafa, wala hana mwana wa kiume, mke wa yule aliyekufa asiolewe nje na mgeni; nduguye yule mumewe amwingilie amweke kwake awe mkewe, kumfanyia yampasayo nduguye mumewe. ⁶Na iwe, yule mzaliwa wa kwanza atakayemzaa, amfuate nduguye aliyekufa kwa jina lake, lisije likafutwa jina lake katika Israeli. ⁷Na yule mtu kwamba hapendi kumtwaa mke wa nduguye, aende huyo mke wa nduguye langoni kwa wazee, akawaambie, Nduguye mume wangu yuakataa kumsimamishia nduguye jina katika Israeli, hataki kunitimizia yampasayo nduguye mume wangu. ⁸Ndipo wamwite wazee wa mji wake waseme naye; naye akisimama na kusema, Sitaki mimi kumtwaa mwanamke huyu, ⁹ndipo mke wa nduguye amkaribie mbele ya hao wazee, amvue kiatu chake mguuni mwake, na kumtemea mate ya uso; kisha atajibu yule mwanamke, aseme, Mume akataaye kumjengea nduguye nyumba yake na afanywe hivi. ¹⁰Na jina lake katika Israeli liitwe, Nyumba ya mvuliwa kiatu.

25:5 “**Watakapoketi pamoja mtu na nduguye**” Huu ni mwanzo wa mazungumzo ya “ndoa za Kilawi” (k.v. Mwanzo 38). Neno “taratibu za kale za Kilawi” ni kutoka kwenye neno la Kilatini shemeji wa kiume. Kusudi zima ya hii sheria ni kutunza urithi ndani ya familia. Kama hapana mtu ndani ya hiyo familia atakaye kumwoa huyo mjane hivyo kaka mtu amwinulia mrithi kwa ajili yake (k.v. Mt. 22:24; Marko 12:19; Luka 20:28). Tambua kuwa mandiko hasa yanaelezea kuwa ni ndugu wawili “waishi pamoja.” Taratibu za utunzaji wa urithi wa mababu toka kwa YHWH, uliotolewa toka kwa Yoshua, ndiyo suala hasa la sheria hii. Kumbukumbu la Torati linatabiri uanzishaji wa vijiji na miji. Sheria zake zinafanyika kwenye jamii hizi za mashambani.

25:6 “**mzaliwa wa kwanza**” Mwana wa mzaliwa wa kwanza angerithi mali ya kakaye marehemu (k.v. Hes. 27:6-11).

25:7 “**hapendi kumtwaa**” Kusudi lenyewe halielezewi, lakini yaweza kuwa ni uchoyo juu ya sehemu ya maisha ya kakaye au yumkini wivu wa kaka aliyekufa. Madhara ya kutopenda kwa nduguye yameelezewa.

☐ “**lango**” Hili lilikuwa ni eneo la mahakama ya nyumbani ya wazee (mf., 16:18-20; 19:12; 21:1-9,19; 22:15).

25:9-10 “**amvue kiatu chake mguuni mwake**” Katika muktadha hili lilikuwa ni tendo la udhalilishaji (k.v. Isa. 20:2). Toleo la Biblia la NET, uk. 381, SN #16, inataja kuwa tendo la kuvua viatu lilimaanisha kuwa ndugu aliyepo hukabidhi haki zote za kisheria kwa ndugu aliyerithishwa. Katika kitabu cha Zaburi 60:8 na 108:9 uvuaji wa viatu wa YHWH kuivuka Edomu kiishara kulimaanisha umiliki wake. Hili laweza kuelezea Ruth 4. Uvuaji wa viatu pia ulioandikwa katika bamba za Nuzi (Lacheman 53-56) zina namna za kisheria.

25:9 “**kumtemea mate ya uso**” Hili lilikuwa ni tendo la ishara ya unyanyasaji (k.v. Hes. 12:14). Ilimfanya mtu kuwa najisi (k.v. Law. 15:8).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 25:11-12

¹¹Washindanapo waume wao kwa wao, akakaribia mke wa mmojawapo, ili kumwokoza mumewe katika mkono wa ampigaye, yule mke akatoa mkono wake, na kumkamata tupu yake; ¹²umkate ule mkono wake, lisiwe na huruma jicho lako.

25:11 “tupu yake” Tena, hili linaonyesha umuhimu wa haki ya urithi katika Israeli ya kale!

25:12 “Umukate ule mkono wake” Huu ni uondoaji maalum uliotajwa katika sheria za Musa. Hukumu yenyewe ya “jicho kwa jicho” (*Lex talionis*) katika kesi hii haikuwa rahisi. Baadaye sheria za Kiyahudi ziliitafasiri hii kama “kutoa fidia kwa ajili ya,” ambazo zilitumika kwenye maandiko mengi ya Musa.

☐ **“usimuhulumiwe”** Hiki kifungu kimerudiwa katika muktadha mbalimbali (k.v. 7:16; 13:8; 19:13,21; 25:12; na kifungu kama kile kile katika 7:2). Sheria za Mungu, na sio mihemuko ya kibinadamu, lazima zifuatwe.

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 25:13-16

¹³Usiwe na mawe ya kupimia mbalimbali, kubwa na dogo, katika mfuko wako. ¹⁴Usiwe na vipimo mbalimbali, kikubwa na kidogo, katika nyumba yako. ¹⁵Uwe na jiwe timilifu la haki, uwe na kipimo kitimilifu cha haki; zipate kuwa nyingi siku zako, katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako. ¹⁶Kwa kuwa wote wayatendao mambo kama haya, wote watendao yasiyo haki, ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako.

25:13 “kipimia mbalimbali” Kiuhalisia fungu la maneno “kikubwa na kidogo,” ni kipimio kimoja cha kununulia, kipimio kimoja cha kuuzia (k.v. Zab. 11:1; 16:11). Haki na uaminifu kati ya ndugu wa agano ni wa muhimu.

MADA MAALUM: UZANI NA VIPIMO VYA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE (USOMAJI WA VIPIMO)

Uzani na vipimo vilivyotumika katika masuala ya biashara vilikuwa ni vya muhimu katika uchumi wa kilimo hapo kale. Biblia inawasihi Waisraeli kuwa wasiwe na upendeleo kwenye mambo yao wanayoyafanya na wengine (kama vile Law. 19:35-36; Kumb. 25:13-16; Mith. 11:1; 16:11; 20:10). Tatizo kubwa lilikuwa sio tu uaminifu, bali kutokuwepo na istilahi zilizo sawa na muundo uliotumika huko Palestina.

Inaonekanakuwapalikuwepojozimbilizauzani; moja “nyepesi” nanyingine “nzito” kwakilaidadi (angalia *The Interpreter's Dictionary of the Bible*, juzuu 4, uk. 831). Pia muundo wa desimali (ulioegamia kwenye sehemu ya 10) wa Misri umekuwa ukijumuishwa na sehemu ya 6 huko Mesopotamia.

Wingi wa “vipimo” na “idadi” vilivyotumika vilitokana na sehemu ya mwili wa mwanadamu, wanyama, mizigo, vibebeo vya wakulima, hakuna hata kimoja kilichokuwa sawia. Kwa hiyo, chati hapa chini ni makadilio tu na ya majaribio. Njia rahisi ya kuonyesha uzani na vipimo iko katika uwiano.

I. Istilahi za uzito zilizotumika mara nyingi

A. Vipimo vya vitu vikavu

1. Homeri (BDB 330, yumkini "mzigo wa punda," BDB 331), mf. Law. 27:16; Hosea 3:2
2. Lateki (AU lethech, BDB 547, yumkini inadokeza katika Hosea 3:2)
3. Efa (BDB 35), mf. Kut. 16:36; Law. 19:36; Ezek. 45:10-11,13,24
4. Se'ah (BDB 684), mf. Mwa. 18:6; 1 Sam. 25:18; 1 Fal. 18:32; 2 Fal. 7:1,16,18
5. Homeri (BDB 771 II, yumkini "mganda" [safu ya mbegu zilizoanguka], BDB 771 I), mf. Kut. 16:16,22,36; Law. 23:10-15
6. Hini (BDB 798, "sehemu ya kumi" yaefa), mf. Kut. 29:40; Law. 14:21; Hes. 15:4; 28:5,13
7. Kibaba (BDB 866), kama vile 2 Fal. 6:25

B. Vipimo vya vimiminika

1. Kori (BDB 499), mf., Ezek. 45:14 (inawezakuwa kipimo cha vitu vikavu, kama vile II Nya. 2:10; 27:5)
2. Bathi (BDB 144 II), mf. I Fal. 7:26,38; II Nya. 2:10; 4:5; Isa. 5:10; Ezek. 45:10-11,14
3. Hini (BDB 228), mf. Kut. 29:40; Law. 19:36; Ezek. 45:24
4. Logi (BDB 528), kama vile Law. 14:10,12,15,21,24

C. Chati (iliyochukuliwa toka kwa Roland deVaux, *Ancient Israel*, juzuu. 1, uk. 201 na *Encyclopedia Judaica*, juzuu. 16, uk. 379)

Homeri (kikavu) =Kori kimiminika au kikavu	1						
Efa (kavu) =bathi (kimiminika)	10	1					
Se'ah (kikavu)	30	3	1				
Hini (kimiminika)	60	6	2	1			
Homeri (kikavu)	100	10	-	-	1		
Kibaba (kikavu)	180	18	6	3	-	1	
Logi (kimiminika)	720	72	24	12	-	4	1

II. Istilahi za uzani zinazotumika mara nyingi

A. Uzani unaotumika mara nyingi, taranta, shekeli, nagera.

- Kipimo kikubwa katika Agano la Kale ni talanta. Toka Kutoka 38:25-26 tunajifunza kuwa talanta moja ni sawa na shekeli 3,000 (yaani, "uzani wa jumla," BDB 503)
- Neno shekeli (BDB 1053, "uzani") hutumika mara nyingi kama inavyodhaniwa, lakini hakijaelezewa katika andiko. Kuna thamani mbalimbali za shekel zilizotajwa katika Agano la Kale.
 - "kipimo cha kibiashara" (toleo la NASB la Mwa. 23:16)
 - "shekel ya madhabahuni" (toleo la NASB la Kut. 30:13)
 - "kwa uzani wa Mfalme" (toleo la NASB la II Sam. 14:26), pia uliitwa "uzani wa Kifalme" kwenye mafunjo ya Elephantine.
- Gera (BDB 176 II) ilithaminiwa na shekeli 20 (kama vile Kut. 30:13; Law. 27:25; Hes. 3:47; 18:16; Ezek. 45:12). Uwiano ulitofautiana toka Mesopotamia hadi Misri. Israeli ilifuatisha uthaminishaji uliokuwa ukitumika huko Kaanani (Ugariti)
- Mina (BDB 584) inathaminishwa na shekeli 50 au 60. Neno hili linapatikana hasa katika vile vitabu vya Agano la Kale (yaani Ezek. 45:12; Ezra 2:69; Neh. 7:71-72). Ezekielilitumiauwianowa 1 ya 60, wakati Wakanaani walitumia uwiano wa 1 ya 50.
- Beka (BDB 132, "nusu ya shekeli," kama vile Mwa. 24:22) imetumika mara mbili katika Agano la Kale (kama vile Mwa. 24:22; Kut. 38:26) na inathaminishwa na nusu shekeli. Jina lake linamaanisha "kugawanya."

B. Chati

1. Imesimamia juu ya Torati

Taranta	1				
Mina	60	1			
Shekel	3,000	50	1		
Beka	6,000	100	2	1	
Gera	60,000	1,000	20	10	1

2. Ikisimamia juu ya Ezekieli

Taranta	1				
Mina	60	1			
Shekeli	3,600	60	1		
Beka	7,200	120	2	1	
Gera	72,000	1,200	20	10	1

25:15 "zipate kuwa nyingi siku zako katika nchi" Hii ni ahadi ya muda mrefu ya kijamii (k.v. 4:40; 5:16,33; 6:2; 11:9; 22:7; 25:15; 30:18; 32:47).

25:16 “wote watendao yasiyo haki, ni machukizo kwa Bwana ” Baraka na laana zinahusiana na utii wa agano (k.v. sura za 27-29).

📌 **“chukizo”** Tazama Mada Maalum katika 14:3.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 25:17-19

¹⁷ Kumbuka aliyokufanya Amaleki katika njia mlipokuwa mkitoka Misri; ¹⁸ jinsi alivyokukuta katika njia, akapiga katika watu wako walioachwa nyuma, wote waliokuwa wanyonge nyuma yako, ulipokuwa umechoka na kuzimia; wala asimche Mungu. ¹⁹ Basi itakuwa, hapo atakapokwisha kukupumzisha Bwana, Mungu wako, katika adui zako wote walio kando-kando, katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako, iwe urithi uimiliki, ndipo uufute ukumbuko wa Amaleki chini ya mbingu; usisahau.

25:17-19 Kitabu cha Kumbukumbu la Torati kina vifungu mbalimbali vyenye kuhusiana na namna Israeli inavyopaswa kuendesha “vita takatifu” (k.v. 7:1-26; 20:1-10; 21:10-14; 25:17-19). Vita takatifu ilikuwa ni vita ya YHWH. Ilikuwa na sheria na taratibu maalum!

25:17 “Amaleki” Hili kundi lawezakuwa ni kizazi cha Esau (k.v. Mwa. 36:15-16), likajakuwa ni alama ya uovu kwa Israel kwa sababu ya mbinu zao za uvamizi (k.v. mstari. 18-19; 17:8-16). Walikuwa ni kundi la wafugaji wenye kuhamahama ambao waliishi kusini mwa Bahari ya Chumvi. Wote Sauli na Daudi walipigana dhidi nao (k.v. I Sam. 15:2; 27:8).

25:18 “nyuma yako” Neno hili (BDB 275) linamaanisha “hitimisho.” Pindi linapotumika kama KITENZI (BDB 275, KB 274, *Piel* KAULI ISIO TIMILIFU) linamaanisha kushambulia (1) kutokea nyuma au (2) kulinda kwa nyuma. linapatikana hapa tu katika Yosh. 10:19.

25:19 “uufute ukumbuko” Katika mistari ya 5-10 kumpoteza nduguyo pasipo na uzao kunajadiliwa. Hapa kuupoteza uzao kunatawala! Hawakumhofu Mungu (mstari 18); waliivamia Israeli iliyokuwa dhifu; lazima wafe (k.v. Kut. 17:14; I Sam. 15:2-4; 30:16-20; I Nya. 4:43)!

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini mstari wa 1 ni wa muhimu kwenye thiolojia?
2. Ni lipi lilikuwa kusudi la ndoa za Kilawi ?
3. Kwa nini mistari ya 11-12 imejumuishwa katika vitabu vitano vya Musa?
4. Nani alikuwa Amaleki na kwa nini walilaaniwa?

KUMBUKUMBU LA TORATI 26

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Utoaji wa malimbuko ya Kwanza na Zaka 26:1-11	Liturujia za kuhitimisha na Maonyo 26:1-11	Sadaka za mavuno 26:1-3 26:4-10a 26:10b-11	Malimbuko ya kwanza 26:1-3 26:4-10a 26:10b-11 Zaka ya mwaka wa tatu
26:12-15 Watu maalumu wa Mungu	26:12-15	26:12-15 Watu wa Bwana Mwenyewe	26:12-15 Mwisho wa pitio la pili (26:16-28:68)
26:16-19	26:16-19	26:16-19	26:16 26:17-19

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi) *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 26:1-11

¹ Na itakuwa, ukiisha kuingia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako, iwe urithi, na kuimiliki, na kukaa ndani yake; ² twaa malimbuko ya ardhi, utakayoyavuna katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako; ukayatie katika kikapu, ukaende hata mahali pale atakapopachagua Bwana, Mungu wako, ili alikalishe jina lake huko. ³ Ukamwende kuhani atakayekuwapo siku zile, ukamwambie, Ninakiri leo kwa Bwana, Mungu wako, ya kuwa nimeingia katika nchi Bwana aliyowaapia baba zetu ya kwamba atatupa. ⁴ Naye kuhani atakipokea kikapu mkononi mwako, akiweke chini mbele ya madhabahu ya Bwana, Mungu wako. ⁵ Nawe ujibu, ukaseme mbele za Bwana, Mungu wako, Baba yangu alikuwa Mwarami karibu na kupotea, akashuka Misri, akakaa huko ugenini, nao ni wachache hesabu yao; akawa taifa kubwa huko, yenye nguvu na watu wengi. ⁶ Wamisri wakatuonea, wakatutesa, wakatutumikisha utumwa mzito. ⁷ Tukamilia Bwana, Mungu wa baba zetu; Bwana akasikia sauti yetu, akaona na taabu yetu, na kazi yetu, na kuonewa kwetu. ⁸ Bwana akatutoa kutoka Misri kwa mkono wa nguvu, na kwa mkono ulionyoshwa, na kwa utisho mwingi, na kwa ishara, na kwa maajabu; naye ametuingiza mahali hapa, na kutupa nchi hii, nchi ijaayo maziwa na asali. ¹⁰ Na sasa, tazama, nimeleta malimbuko ya mazao ya ardhi uliyonipa, Ee Bwana. Kisha ukiweke chini mbele za Bwana, Mungu wako, ukasujudu mbele za Bwana, Mungu wako; ¹¹ ukayafurahie mema yote ambayo Bwana, Mungu wako,

26:1 “ukiisha kuingia katika nchi” Hii inaweka kumbukumbu ya ukweli kwamba bado Israeli katika safu za milima ya Moabu upande wa mashariki mwa Yordani wakati maneno haya ya Musa yalipotolewa.

☐ **“Bwana, Mungu wako”** Tazama Mada Maalum katika 1:3.

☐ **“iwe urithi”** Hii ni nahau ya uchaguzi wa Israeli (kama vile Kutoka 6:4,8; 15:17; 23:30; 32:13; Kumb. 1:6-8; 4:38,40; 5:31; 7:13; 8:1-10; 9:4-6; 11:8-12,17; 26:1,9; 32:49,52; 34:4). Ardhi (ardhi yote) ni mali ya YHWH (kama vile Kut. 19:5; Law. 25:23). Ikiwa wana wa Israeli wasingetii agano la YHWH angewanyang’anya (kama vile Law. 26:14-33; Kumb. 4:25-28; Yosh. 23:14-16), lakini YHWH bado angekuwa mwenye rehema (kama vile Kumb. 4:29-31; 30:1-3,10).

26:2 “twa malimbuko ya ardhi” Kiwango halisi cha sadaka ya malimbuko ya kwanza hakiwekwi bayana (lakini ingekuwa kikapu kimoja, kama vile mistari ya 3,4). Hii hadithi inaonekana kuwa tukio la wakati mmoja katika fu za nilima ya Moabu lakini inaaksi taratibu za kiibada za baadaye (kama vile Kut. 22:29; 23:16,19). Tendo hili lilikuwa njia ya kisitiari ya kuonesha umiliki wa Mungu wa jumla wa mazao. Umiliki huo huo wa njia ya uwakilishi unakuzwa katika (1) mzaliwa wa kwanza; (2) fungu la kumi; (3) Sabato; (4) mwaka wa Sabato; na (5) Mwaka wa Yubile.

☐ **“mahali pale atakapopachagua Bwana, Mungu wako, ili alikalische jina lake”** Hii inaurejelea uchaguzi wa Mungu wa mahali pa madhabahu kuu ambayo ni ya tofauti katika namna ya msisitizo wa Kumbukumbu la Torati (kama vile 12:5,11,14,18,21,26; 14:23,24,25; 15:20; 16:2,6,7,11,15,16; 17:8,10; 18:6; 26:2; 31:11). Kiasili ilikuwa Gilgali, alafu Shekemu, alafu Shilo, alafu Mizpa, na baadaye baada ya mapigano ya Daudi ya Yebusi, Yerusalemu (kama vile II Sam. 5:6-7; I Nyakati 11:5,7). Kusudi la madhabahu kuu lilikuwa la kikabila na umoja wa kidini. Ilikuwa pia ni kutunza na kuwaweka Waisraeli mbali na madhabahhu za Baali.

26:3 “Ukamwende kuhani atakayekuwapo siku zile” Mwanzoni hii inaonekana kurejelea kwa Uzao wa Ukuhani mkuu wa Haruni (kama vile *The Tyndale OT Commentary, “Deuteronomy,”* uk. 254), lakini muktadha unadai kwamba inarejerea kwa familia tofauti tofauti za makuhani wa Haruni waliokuwa wanapeana zamu kuhudumu katika madhabahu kuu.

☐ **“na kumwambia”** Hayo yote yanayofuatia ni liturujia ya kurudiwa na wale ambao kwa utii wanaleta malimbuko yao ya kwanza kwenye Hema au baadaye madhabahu kuu.

☐ **“BWANA Mungu wangu”** Toleo la MT lina neno Mungu “wako.” Kutofautiana huku katika KIWAKILISHI hakuna maana ya kithiolojia. Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania tu ya kuzungumza na mtu juu ya mamlaka ya kidini.

26:4 “Naye kuhani atakipokea kikapu mkononi mwako, akiweke chini mbele ya madhabahu” Wengi wanalinganisha mst. 10 na kudai kuwa kuna mkanganyiko. Tatizo ni, hatuna masimulizi ya kina kuhusiana na taratibu hizi.

26:5 “Baba yangu” Hii inarejelea kwa baba wa imani Yakobo, baadaye anaitwa Israeli (kama vile Mwa.32:28 na Mada Maalum: Israeli katika 1:1). Hii ilikuwa kauli ya kithiolojia kuhusu wao kuwa watu waliochaguliwa na Mungu. Hili lilikuwa tamko la imani la ukubalifu wao.

☐

NASB, NRSV,

TEV, NJB

NKJV

REB

“watangaji”

“walio karibu na kupotea”

“wasio na makazi”

Hii inamaana ya “kupotea” (BDB 1, KB 2, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU). Wakati mwingine neno hili linatumika kwa kumaanisha kupotea au kutanga tanga (I Sam. 9:3; Yer. 50:6; Ezek. 34:4,16)

☐ **“Mwarami”** Hii inarejerea kwa Padani-Aram au Shamu (BDB 74, kama vile Mwa. 25:20; 28:5; 31:20,24). Labani alikuwa anatokea eneo hili ambalo lilijumuisha mji wa Harami (kama vile Mwa. 31:40-42). Yakobo aliishi huko kwa miaka kadhaa na baadaye kukimbia mbali na Labani.

☐ **“ugenini”** KITENZI hiki (BDB 157, KB 184, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) inamaanisha kukaa kama mtu wa kuja au mkazi aliye mgeni (kama vile Mwa. 47:4).

☐ **“nao ni wachache hesabu yao”** Katika Mwa. 46:27 na Kut. 1:5 inasema kwamba kiasili walikuwa watu 70 tu. Wakati walipokimbia Misri hesabu yao ilikuwa juu kama kiasi (kama vile 1:10; 20:22; Kut. 1:9) cha watu 1,500,000 mpaka watu 2,500,000. Hesabu inategemea utafsiri sahihi wa neno la Kiebrania “elfu.” Hili linaweza kumaanisha (1) kiasi cha 1,000 kama inavyotajwa; (2) ukoo; au (3) kipengele cha kijeshi (kama vile Kut. 12:37). Tazama Mada Maalum katika 1:15.

26:7 “Tukamilia Bwana. . akasikia sauti yetu, akaona na taabu yetu” Mungu alikuwa ameahidi na kumwambia Ibrahimu hapo kabla juu ya hili (kama vile Mwa. 15:12-21; Kut. 3:7, 9).

☐ **“Bwana, Mungu wa baba zetu”** Hii ilitambua Mungu wa baba wa imani, El Shaddai (kama vile Kut. 6:2-9), pamoja na YHWH, aliyemkabili Musa (kama vile Kut. 3:14). Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.

26:8 “kwa mkono wa nguvu, na kwa mkono ulionyoshwa”Hii ilielezwa katika lugha ya Mungu kwa kutumia lugha ya wanadamu juu ya nguvu na ushindi. Tazama dokezo katika 4:34. Pia inawezekana kwamba nahau hii ilichaguliwa kwasababu ilitumika mara kwa mara katika fasihi ya Kimisri na sanaa kwa ajili ya nguvu ya Farao.

☐ **kwa utisho mwingi, na kwa ishara, na kwa maajabu”** Hii inafanana na mapigo kumi katika Misri (mfano, 4:34; 6:22; 7:19; 11:3; 26:8; 29:2; 34:11).

26:9 “nchi ijaayo maziwa na asali”Hii ilikuwa vyote maelezo ya nje na maelezo ya kisheria kwa Palestina katika nyaraka za Kiashuru.Mungu aliwapa ulithi mzuri wa kupendeza (yaani, Kanaani au Palestina, kama vile 6:3; 11:9; 26:9; 27:3; 31:20).

26:10 “uliyonipa, Ee Bwana”Hii inaonesha mtazamo wa kweli wa kidini juu ya maisha (kama vile mstari wa 2; 8:11-20). Mstari huu unamaanisha kwamba majira mojawapo ya kuvuna yamekwishakupita au kwamba Waisraeli waliweka wakfu mazao waliyokuta yanamea.

☐ **“ukasujudu”**Hii kiuhalisia ni “kujilaza na kuwa sawa na ardhi” (BDB 1005, KB 295, *Hishtapael* KAULI YA WAKATI TIMILIFU).

26:11 “ukayafurahie mema yote ambayo Bwana, Mungu wako, amekupa, na nyumba yako” Tazama kipengele cha karamu katika Mungu kuhusiana na watu wake aliofanya nao Agano (na wengine alioishi pamoja nao, yaani wageni). Kuabudu kunatakiwa kuwe ni tendo la furaha! Kuabudu kwa heshima hakuwezi kuwa na maana ya kukaa kimya na kuwa mpole! Walimu wa sheria za Kiyahudi baadaye walitumia mstari huu kurejerea kufurahia juu ya utoaji mwa sheria (kama vile mstari wa 14).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 26:12-15

¹² Utakapokwisha kutoa zaka, katika zaka zote za maongeo yako mwaka wa tatu, ambao ndio mwaka wa kutolea zaka, umpe zile zaka Mlawi, na mgeni, na yatima, na mjane, wapate kula ndani ya malango yako na

kushiba; ¹³ nawe sema mbele ya Bwana, Mungu wako, Vitu vilivyo vitakatifu nimeviondoa katika nyumba yangu, nami mimewapa Mlawi, na mgeni, na yatima, na mjane, kwa mfano wa maagizo yako uliyoniusia yote; sikukosa maagizo yako yo yote, wala sikuyasahau; ¹⁴ katika vitu hivyo sikula wakati wa kukaa matanga mimi, wala sikuviondoa nikiwa na unajisi, wala sikutoa kwa ajili ya wafu katika vitu hivyo; sauti ya Bwana, Mungu wangu, nimeisikiza, nimefanya yote, kama ulivyoni amuru. ¹⁵ Uangalie kutoka makazi yako matakatifu mbinguni, uwabarikie watu wako Israeli, na nchi uliyotupa kama ulivyowaapia baba zetu, nchi imiminikayo maziwa na asali.

26:12 “zaka” Tazama Mada maalum hapa chini.

MADA MAALUM: ZAKA KATIKA UTUNGAJI WA SHERIA YA MUSA

A. Maandiko ya rejea

1. Kwa makuhani na Madhabahu kuu
 - a. Law. 27:30-32
 - b. Kumb. 12:6-7, 11, 17, 14:22-26
 - c. Hes. 18:21-24
 - d. Neh. 12:44
 - e. Mal. 3:8, 10
2. Kwa makuhani wa maeneo yao
 - a. Kumb. 12:12; 14:27; 26:12-15
 - b. Hes. 18:25-29 (Walawi lazima watoe zaka kwa madhabahu kuu)
 - c. Neh. 10:37,38
3. Kwa ajili ya maskini wa maeneo yao
 - a. Kumb. 14:28-29
 - b. Neh. 12:44

B. Mifano ya utoaji zaka unaotangulia utungwaji wa sheria ya Musa

1. Mwanzo 14:20, Ibrahimu mpaka Melkizedeki (Ebr. 7:2-9)
2. Mwanzo 28:22, Yakobo mpaka YHWH

C. Zaka za Israeli zilitumika kusaidia madhabahu kuu lakini kila mwaka wa tatu zaka ya kitaifa ilielekezwa kwa maskiniwa maeneo husika.

☐ **“mwaka wa tatu”** Hii inazirejelea “zaka dhaifu,” zilizokuwa zikitolewa katika maeneo ya kukutanikia (kama vile 14:28-29) zilizotolewa na mtoaji wa zaka lakini ikithibitishwa na madhabahu kuu (kama vile mstari wa 13).

26:13 “Vitu vilivyo vitakatifu” Zaka ilikuwa mali ya Bwana na hivyo ilikuwa takatifu (kama vile Law. 27:30)

26:14 “wakati wa kukaa matanga” Baadhi ya maombolezo na taratibu za ibada zilikuwa za kipagani kwa asili. Hili neno la Kiebrania lilihusianishwa na kuabudu miungu mingine (BDB 19, kama vile Hos. 9:4 na Yer. 16:5-7), ambayo inajumuisha baadhi ya desturi hizi za kuabudu za kipagani. Wanazuoni wengi wanaamini kwamba taratibu zote zinazotajwa katika mstari wa. 14 zinahusiana na matendo ya kuabudu ya Wakanaani.

☐ **“nikiwa na unajisi”** Toleo la Jerusalem Bible linakitafsiri kifungu hiki kama, “sijawahi kutumia chochote ambacho si safi”; toleo la Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani linasema “kwa makusudi yasiyosafi” (kama vile Hag. 2:13), lakini toleo la MT linarejelea kwa ushuhuda wa mtu mmoja mmoja anayetoa.

☐ **“wala sikutoa kwa ajili ya wafu”** *Lamsa*, katika tanbihi ya Peshitta, ilitafsiri katika Kingeleza, kuwa “kutotumia kulisha ndugu baada ya maziko,” lakini katika muktadha. Inawekana inamaanisha kurejelea kwa matendo ya kipagani ya kiibada

☐ **“nimeisikiza, . . nimefanya yote, kama ulivyoni amuru”** Mtoaji mmoja mmoja anakiri utii wake na kutendea kazi (VITENZI vyote viwili ni *Qal* YA WAKATI TIMILIFU) kwa sheria ya YHWH kufunuliwa kupitia Musa (“kuamuru” BDB 845, KB 1010, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU).

26:15 Hii inamueleza YHWH kwa maneno ya ukuu sana (kama vile 4:36; I Wafalme 8:27-30; Isa. 66:1). Alibakia mbinguni. Alituma malaika kwa watu Wake (kama vile Kut. 23:20,23; 32:34; 33:2). Mtu lazima aweke uwiano wa Utakatifu wa Mungu (ukuu) na upendo wake wa karibu wa sasa (umilele).

VITENZI, “kutazama chini” (BDB 1054, KB 1645, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI) na “kubariki” (BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI SHURUTISHI), ni kauli shurutishi au maombi.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 26:16-19

¹⁶ Leo hivi akuamuru Bwana, Mungu wako, kuzifanya amri hizi na hukumu; basi uzishike na kuzifanya kwa moyo wako wote na roho yako yote. ¹⁷ Umemwungama Bwana leo, kuwa ndiye Mungu wako, na kuwa yakupasa kutembea katika njia zake, na kushika amri zake na maagizo yake, na hukumu zake, na kusikiza sauti yake; ¹⁸ naye Bwana amekuungama hivi leo kuwa taifa iliyotengwa iwe yake yeye, kama alivyokuahidi, na kuwa yakupasa kushika maagizo yake yote; ¹⁹ na kuwa atakutukuza juu ya mataifa yote aliyoyafanya, kwa sifa, na jina, na heshima, nawe upate kuwa taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako, kama alivyosema.

26:16 Huu ni muhutasari wa hitimisho na kujizatiti (yaani, uthibitisho) kwenye sheria halisi za sura ya 12-26. Ukiri huu wa agano ulitakiwa kurudiwa na kila kizazi kipya, mmoja mmoja.

☐ **“amri hizi na hukumu”** Tazama Mada maalum: Istilahi kwa Ufunuo wa YHWH katika 4:1.

☐ **“uzishike na kuzifanya”** Utii ni muhimu!

☐ **“kwa moyo wako wote na roho yako yote.”** Utii pekee haukuwa unatosheleza. Lazima uendane na shauku ya kumuheshimu na kumtumikia YHWH (kama vile 4:29;6:5; 10:12).

26:17

NASB	“Umemwungama”
NKJV	“umetangaza”
NRSV, NJB	“umepata”
TEV	“umetambua”

Hili ni neno nadra la Kiebrania (BDB 55, KB 65) katika shina la neno *Hiphil*, linatumika hapa tu katika mstari wa 17 na mstari wa 18. Mtu anayeabudu alitangaza utii wake na uaminifu kwa YHWH na YHWH alitangaza kwa mtu anayeabudu uchaguzi wake na wito kuwa watu wa kipekee (yaani, agano).

26:18

NASB	“kuwa taifa iliyotengwa iwe yake”
NKJV	“Watu Wake wateule”
NRSV	“Watu Wake awaoendao”
TEV, NJB	“watu wa milki Yake”

Hili pia ni neno nadra la Kiebrania (BDB 688, kama vile Kut. 19:5; Kumb. 7:6; 14:2; Zab. 135:4). Kwa sababu liturujia ya sura ii haitaji kibayana tukio la Mlima Sinai/Horebu, hivyo baadhi ya wanazuoni wa leo wanakataa historia ya tukio. Hata hivyo matumizi nadra ya neno hili, yote katika Kut. 19:5 na Kumbukumbu la Torati (kama vile 7:6; 14:2; na hapa) yanapendekeza kwamba matumizi yake ni maelezo ya tukio!

Tamko hili pia halitaji uumbaji. Je, ni sawa pia kukataliwa kama tukio la kihistoria?

26:19 “atakutukuza juu ya mataifa yote” Hii inarudiwa katika 28:1,13, lakini tazama janga la Yer. 13:11 na 7:23-26! Toleo la NIDOTTE, juzuu 1, uk. 1035, pia linaona mstari huu kama jukumu la Israeli kuaksi uaminifu na kustahili kwa YHWH kwa ulimwengu! Hivyo, huu ni mstari wa “Agizo Kuu”! Israeli ilikuwa na jukumu la “umisheni” (mfano, Yer. 3:17; 4:2; 12:14-17; 16:19; 33:9)! Tazama Mada Maalum katika 4:6!

▣ **“taifa takatifu”** Hii kiuuhalisia ni neno “takatifu” (BDB 872), ambalo linamaanisha “kutenga kwa ajili ya matumizi ya Mungu.”

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani malimbuko ya kwanza yanafanana na zaka? Aina ngapi za zaka zilikuwepo huko?
2. Kwanini mstari wa 5 ni muhimu sana?
3. Elezea historia ya nyuma ya mstari wa 14 na kuendelea.
4. Kwanini na kwa namna gani Wayahudi wanachaguliwa?

KUMBUKUMBU LA TORATI 27

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Sheria Inaandikwa juu ya jiwe	Taratibu za Shekemu	Sheria za Mungu zinaandikwa juu ya jiwe	Maandiko ya Sheria na ya taratibu za Kidini
27:1-8	27:1-8	27:1-8	27:1-3 27:4-8
27:9-10	27:9-10	27:9-10	27:9-10
Laana inatangwazwa toka Mlima Ebeli		Laana ya kutotii	
27:11-13	27:11-14	2:11-14	27:11-14
27:14-26			
	27:15	27:15	27:15
	27:16	27:16	27:16
	27:17	27:17	27:17
	27:18	27:18	27:18
	27:19	27:19	27:19
	27:20	27:20	27:20
	27:21	27:21	27:21
	27:22	27:22	27:22
	27:23	27:23	27:23
	27:24	27:24	27:24
	27:25	27:25	27:25
	27:26	27:26	27:26

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Musa anatajwa katika nafsi ya tatu (mst. 1). Je! hii inamaanisha utofauti wa kifasihi au uandishi (wa sasa au wa baadaye)? Huu wa sasa lazima ukubali kwamba muundo na hatua za uumbaji wa vitabu vya Agano la Kale unajulikana kwetu.
- B. Hapa kunaonekana kuwepo ushahidi wa kimaandiko kwa mhariri (wa sasa au wa badaye). Baadhi ya mifano iliyo katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati cha mhariri huyu au kauli ya tatu (msimuliaji) ni 1:1-5; 2:10-12,20-23; 3:9,11,13b-14; 4:41- 5:1a; 10:6-7,9; 27:1a,9a,11; 28:69; 29:1; 31:3,7a,9-10a,14a,14c-16a,22-23a,24-25,30; 32:44-45,48; 33:1; 34:1-4a,5-12 (tazama *An Introduction to the Old Testament* na Raymond B. Dillard na Fremper Longman III, uk. 100).
- C. Taratibu za agano la awali huko Shekemu haziendani na tarehe iliyofuatia kwa ajili ya kuiunga mkono dhana ya maeneo maalum yaliyotengwa katika Yerusalemu. Vitabu vingi vya Musa vinaendana na maisha ya siku zile za Musa.
- D. Ni dhahiri kuwa wahariri walikuwa na sehemu katika uumbaji wake (mfano mmoja dhahiri ni Hes. 12:3).
- E. Kuna ufananao dhahiri wa kifasihi kati ya Kumb. 11:26-32 na Kumbukumbu la Torati 27. Utaratibu huu wa kulirudisha upya agano unaumba muundo wa kifasihi ambao unakigawa kitabu cha Kumbukumbu la Torati katika muundo wa sheria na masimulizi na kutambua hotuba tofauti tofauti za Musa.
- F. Sura hii inaeleza makubaliano ya mgawo wa ardhi kwa kufuatisha utaratibu wa makubaliano ya Hittite (yaani, kitabu cha Kumbukumbu la Torati kama kilivyo na Yohana 24). Ebali, kuhani mkuu anapachagua katikati ya nchi ya Kanaani kiishara inaonyesha hatua za mabadilishano ya nchi kwa Waisraeli. Hata hivyo, kudumisha haki na vipaumbele vya umiliki, utii wa agano na uaminifu kwa YHWH unatakiwa.
- G. Historia ya dhoruba ya Israeli inaweza kuonekana kupitia kioo cha Kumbukumbu la Torati 27-29. Utii wa agano unaorudiwarudiwa kutotii kulikokomaza hukumu ya YHWH. Ilimpasa huyu kuwa nguzo ya furaha na jamii yenye mafanikio (udugu wa haki), lakini alikomaza tufani ya laana za YHWH! Ahadi za YHWH zinatenda kazi kwa aliyetubu pekee, aaminiye, mtiifu, mtu wa agano. Uchaguzi hauondoi utiini (kama vile Wagalatia 3).

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 27:1-8

¹ Musa na wazee wa Israeli wakawaagiza wale watu wakawaambia, Shikeni maagizo yote niwaagizayo leo. ² Na iwe, siku mtakayovuka Yordani kwenda nchi akupayo Bwana, Mungu wako, ujisimamishie mawe makubwa, ukayatalize matalizo, ³ uyaandike maneno yote ya torati hii juu yake, utakapokwisha kuvuka; ili upate kuingia nchi akupayo Bwana, Mungu wako, nchi imiminikayo maziwa na asali, kama alivyokuahidi Bwana, Mungu wa baba zako. ⁴ Na iwe, mtakapokwisha vuka Yordani myasimamishie mawe haya, niwaagizayo hivi leo, katika mlima Ebali, nawe yatalize matalizo. ⁵ Na huko umjengee madhabahu Bwana, Mungu wako, madhabahu ya mawe, usitumie chombo cha chuma juu yake. ⁶ Jenga hiyo madhabahu ya Bwana, Mungu wako, kwa mawe yasiyochongwa; ukamtolee Bwana, Mungu wako, sadaka za kuteketezwa juu yake; ⁷ ufanye na sadaka za amani, ukale huko; nawe furahi mbele za Bwana, Mungu wako. ⁸ Kisha, andika juu ya mawe hayo maneno ya torati hii yote, waziwazi sana.

27:1 “na wazee wa Israeli Israeli” Musa alifahamu kwamba kitambo kidogo watu wangeingia katika Nchi ya Ahadi na kwamba asingeweza kwenda (kama vile Hes. 20:12; 27:12-14; Kumb. 3:26-27). Yeye alikuwa akijaribu kulitia

moyo kundi la uongozi wa kikabila.

☐ **“Shikeni maagizo yote”** Hii ni dhamira ya mara kwa mara (kama vile mst. 10) na sharti kwa Israeli kuishi ndani ya nchi hiyo.

27:2 “siku mtakayovuka Yordani . . . ujisimamishie mawe makubwa” Kuna aina tatu za mawe:

1. huko Gilgali (mist. 1-3, kv. Yoshua 4)
2. huko Shekemu (mist. 4-8)
3. baada ya kuteka na ugawaji wa nchi sheria ya Mungu iliandikwa juu ya jiwe kubwa na juu ya kitabu/torati (BDB 706, kama vile Yosh. 24:26-27)

Inawezekana kwamba kifungu “hadi leo” kinaweza kueleweka kama “lini,” kwa maana ya vyote kuirejelea Shekemu.

Kwa uhalisia kile kilichoandikwa juu ya mawe hayo kinajadaliwa. Haya yalikuwa mawe makubwa hivyo yangehimiri idadi kubwa ya maandiko. Wengi wanadhani kwamba ni Kumbukumbu la Torati 12-26 au 27-28 au 5:8-21 au hata Kut. 20:22-23:33.

☐ **“ukayatalize matalizo”** Hiki KITEMZI (BDB 966, KB 1319, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) kinapatika katika Agano la Kale katika mist. 2 na 4 pekee. Hii ilikuwa njia ya Kimisri ya uandaaji wa maandiko. Hii ilikuwa njia ya mwisho ya maandiko kuwa katika mwonekano. Sababu ya kuiandika Sheria ilikuwa kwamba kila mtu aweze kuisoma kwa ajili yao (kama vile mst. 8).

27:3 “uyaandike maneno yote ya torati hii juu yake” Kuna marejeleo kadhaa ndani ya Vitabu Vitano ya Musa ambayo yanatajwa katika maandiko ya Musa:

1. Kutoka - 17:14; 24:4; 34:27,28
2. Hesbu - 33:2
3. Kumbukumbu la Torati 27:3,8; 28:58; 29:21; 30:10; 31:9,22,24-26

☐ **“kama alivyokuahidi Bwana, Mungu wa baba zako”** (kv. mst. 12) Shekemu [MI. Gerizimu] ni mahali ambapo Ibrahimu (kv. Mwa. 12:6-9) na Yakobo (kv. Mwa. 33:18-20) alijenga madhabahu. Hili lilionyesha utimilifu wa ahadi za Mungu za awali kwao.

27:4 “mlima Ebal” Kuna milima miwili (yaani, hatua 3,080 juu) pengine upande wa mji wa Shekemu (yaani, ukingo mrefu). Huu ulikuwa moja ya hiyo. Shekemu lilikuwa eneo la kwanza ambalo Ibrahimu alijenga madhabahu (kv. Mwa. 12:6-7).

27:5 “usitumie chombo cha chuma juu yake” Huenda hii ilihusiana na muundo wa madhabahu za Kanaani (kv. Kutoka 20:24-25). Mungu alihitaji madhabahu zake kuwa tofauti na zile madhabahu za Kanaani zilizotengenezwa kwa mkono wa mwanadanu (yaani, mawe yaliyochongwa, mst. 6). Maelezo haya yanaifunua Yosh. 8:30-35.

27:6 “sadaka za kuteketezwa juu yake” Sadaka za kuteketezwa ni kile kinachoharibiwa kwa ujumla (yaani, kilichotolewa kwa YHWH kwa ujumla, Law. 1:1-7).

27:7 “sadaka za amani” Huu ni uchomaji wa kawaida unaofanywa madhabahuni, sehemu nyingine wanapewa makuhani, sehemu nyingine inatolewa kwa ajili ya mlo wa jumuiya (kv. Law. 3:1,7).

☐ **“nawe... furahi”** Hii ni dhamira iliyo katika Kumbukumbu la Torati (BDB 970, KB 1333, *Qal* kauli ya wakati timilifu, kv. 12:7,12,18; 14:26; 16:11,14; 26:11; 27:7). YHWH alihitaji kuibariki Israeli ili kuuvuta umakini wa mataifa yaliyoizunguka.

27:8

NASB “waziwazi sana”

NKJV “dhahiri sana”
NRSV “kwa ushahidi sana”
TEV “aliandika kwa wazi kabisa”
NJB “kwa umakini”

Hii tafsiri ya Kiingereza inaundwa na VITENZIJINA HALISI viwili:

1. BDB 91, KB 106, *Piel*
2. BDB 405, KB 408, *Hiphil*

Huku ni kuyasema maneno haya, kila neno, ni muhimu.

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 27:9-10

⁹ Musa na makuhani Walawi wakawaambia Israeli wote wakasema, Nyamaza, usikize, Ee Israeli; leo umekuwa watu wa Bwana, Mungu wako. ¹⁰ Basi isikize sauti ya Bwana, Mungu wako, ufanye maagizo yake na amri zake nikuagizavyo leo.

27:9-10 Katika mistari hii Musa na makuhani walinea na Wana wote wa Israeli. Watu hawa waliamriwa kukaa kimya (BDB 698, KB 756, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI) na kusikia (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI) pamoja na mtazamo juu ya utii (kv. mst. 10).

27:9 “leo umekuwa watu” Kuna baadhi ya mjadala kuhusu kipindi halisi cha kuanza kwa agano:

1. wakati wa Israeli kuondoka Misri, Kut. 6:6-7
2. huko Ml. Sinai/Horebu, Kumb. 4:20; Kut. 19:5-6
3. juu ya safu za Moabu, mst. 9; 28:1
4. ng’ambo yam TO Yordani, Yosh. 4:19-24
5. huko Gilgali (eneo la kambi ya kwanza)
6. huko Shekemu (kufanya upya agano), Yosh. 8:30-35

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 27:11-14

¹¹ Musa akawaagiza wale watu siku iyo hiyo, akasema, ¹² Hawa na wasimame juu ya mlima wa Gerizimu kwa kuwabarikia watu, mkiisha vuka Yordani; Simeoni, na Lawi, na Yuda, na Isakari, na Yusufu, na Benyamini; ¹³ na hawa na wasimame juu ya mlima wa Ebali kwa laana; Reubeni, na Gadi, na Asheri, na Zabuloni, na Dani, na Naftali. ¹⁴ Kisha Walawi na wajibu, wawaambie watu wote wa Israeli kwa sauti kuu,

27:11 Mstri huu unaanza na kipengele cha laana na baraka. Baraka hazikuorodheshwa. Katika sura hii, bali katika sura ya 28.

27:12-13 Nusu ya makabila ya Israeli ingeweza kuwa Ml. Gerizimu (izungumziwayo Baraka, kv. 28:1-14) nusu nyingine ingeweza kuwa Ml. Ebali (izungumziwayo laana, kama vile 28:15-68), Gerizimu ikiwa kusini mwa mlima, Ebali kaskazini. Makuhani walisimama katikati ya milima huku wakiwa na Sanduku la Agano (kv. Yosh. 8:30,35).

☑ **“Yusufu”** Utambue mgawanyo wa Yusufu katika Erahimu na Manase haukuwai kuandikwa (kv. Mwa. 49:22-26; Kut. 1:5; Kumb. 33:13-17).

27:14 “Walawi” Hii lazima iwarejeele watunzaji wa Sanduku la Agano. Makuhani wote walikuwa Walawi, lakini si Walawi wote waliokuwa Makuhani. Kwa uwazi, baadhi ya Walawi (yaani, kutoka kabila la Walawi, mst.12) walikuwa juu ya mliama (kv. mst.12).

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 27:15

¹⁵ Na alaaniwe mtu afanyaye sanamu ya kuchonga, au ya kusubu, machukizo kwa Bwana, kazi ya mikono ya fundi, akaisimamisha kwa siri. Na watu wote wajibu, waseme, Amina.

27:15-26 “alaaniwe” Neno “alaaniwe” ni neno lenye kumaanisha kwamba, “Alaaniwe na HWH” (BDB 76). Kuna laana kumi na mbili (neno hili linatumika mara 39 katika Kumbukumbu la Torati 27-29). Zote hizi ziko katika mfumo wa *Qal* kauli tendwa endelevu (mist. 15,16,17,18,19,20,21,22,23,24,25,26; pia tazama 28:16-19). Ya kwanza ni laana dhidi ya ibada ya sanamu (kama vile Kumb. 4:15- 18; 5:8-9; Kut. 20:3-4,23; 34:17). Zilizo nyingi, kama si zote, za sheria za Musa zinaeza kuonekana katika utofauti wake na jamii ya ki-Kanaani.

27:15 “akaisimamisha kwa siri” KITENZI (BDB 962, KB 1321 ni *Qal* KAULI TIMILIFU, kv. mst. 24). Mara nyingi kinatumika kumaanisha kazi dhaifu.

■ **“Amina”** Hii kanuni ya kiruturjia iliyordiwarudiwa inaonyesha ukubalifu wa watu kuhusu sheria (kv. mist. 15-26). Itambue dhana ya Kiyahudi ya ushirika.

MADA MAALUM: AMINA

I. AGANO LA KALE

- A. Neno “Amina” linatokana kwenye na neno la Kiebrania lenye maana ya
 1. “ukweli” (*emeth* BDB 49)
 2. “Uaminifu” (*emun, emunah*, BDB 53)
 3. “imani” au “uaminifu”
 4. “amini” (*dmn*, BDB 52)
- B. Asili yake inadokeza mkao wa mwili wa mtu ulivyo imara. Kinyume cha hili kinaonyesha mwili wa mtu usio imara, unaoteleza (kv. Zab. 35:6; 40:2; 73:18; Yeremia 23:12) au kizuizi (kv. Zab. 73:2). Kutokana na utumiaji huu wa fasihi unatengeneza upanuzi wa kiisitiari wa imani, uaminifu, utiifu na wa kutegemewa (kv. Hab. 2:4)
- C. Utumiaji maalumu (tazama [Mada Maalumu: Kuamini, Sadiki, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale](#))
 1. nguzo, 2 Fal. 18:16 (1 Tim. 3:15)
 2. kuthibitika, Kut. 17:12
 3. uimalifu, Kut. 17:12
 4. uthabiti, Isa. 33:6
 5. ukweli, 1 Fal. 10:6; 17:24; 22:16; Mit. 12:22
 6. thabiti, 2 Nya. 20:20; Isa. 7:9
 7. stahili (sheria alizopewa Musa), Zab. 119:43,142,151,160
- D. Katika Agano la Kale maneno mawili ya Kiebrania yanatumika kwa ajili ya imani thabiti
 1. *bathach* (BDB 105), sadiki
 2. *yra* (BDB 431), hofu, heshima, abudu (kama vile. Mwa. 22:12)
- E. Kwa maana ya kusadiki au uaminifu ulioanzishwa kwa matumizi ya liturujia ambayo ilitumika kuthibitisha maelezo ya kweli ya mtu mwingine (kama vile Hes. 5:22; Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Neh. 5:13; 8:6; Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48; Yer. 11:5; 28:6).
- F. Kiongozi cha kithiolojia kwenye neno hili sio uaminifu wa mwanadamu, bali ni wa Mungu mwenyewe (kama vile Kut. 34:6; Kumb. 32:4; Zab.108:4; 115:1; 117:2; 138:2). Tumaini la mwanadamu aliyeanguka ni neema, uaminifu, kutii Agano la Mungu na ahadi zake. Wale wanaomfahamu Mungu wanahitajika kufanana naye (kama vile Hab. 2:4). Biblia ni historian na kumbu kumbu ya Mungu kurejesha taswira yake (kama vile Mwa. 1:26-27) kwa mwanadamu. Wokovu unarejesha uwezo wa mwanadamu kuwa na ushirika wa ndani na Mungu. Hii ndio sababu ya kuumbwa kwetu.

II. AGANO JIPYA

- A. Utumiaji wa neno “amina” kama hitimisho la kiliturujia kwa minajili ya kuthibitisha ukweli wa maelezo/taarifa ni la kawaida katika Agano Jipya (kama vile 1 Kor. 14:16; Ufu. 1:7; 5:14; 7:12).
- B. Utumiaji wa neno kama kifungio cha maombi ni wa kawaida katika Agano Jipya (kama vile Rum. 1:25;

9:5; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 6:18; Efe. 3:21; Flp. 4:20; 2 The. 3:18; 1 Tim. 1:17; 6:16; 2 Tim. 4:18).

- C. Yesu ndiye yeye aliyelitumia hili neno (limezidishwa mara 25 katika Yohana, yaani., Yohana 1:51; 3:3,5,11; n.k.) kuyatambulisha maelezo muhimu (kama vile. Luka 4:24; 12:37; 18:17,29; 21:32; 23:43).
- D. Linatumika kama cheo kwa Yesu katika Ufu. 3:14 (pia angalia 2 Kor. 1:20, yamkini jina la heshima la YHWH linaokana na kutoka Isa. 65:16)
- E. Dhana ya kusadiki au sadiki, au kuamini au amini inaelezewa katika neno la Kiyunani *pistos* au *pistis*, ambalo linatafasiliwa katika Kiingereza kama “sadiki”, “imani”, “kuamini” (tazama [Mada Maalumu: Imani, Kuamini au Kusadiki](#)).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 27:16

¹⁶ Na alaaniwe amdharauye baba yake au mama yake. Na watu wote waseme, Amina.

27:16 “amdharauye” Ili kufanya uzito mdogo au mchache (BDB 885 II, KB 1101, *Hiphil* KAULI ENDELEVU). Hiki ni kinyume cha neno la Kiebrania “heshima” (BDB 457, kv. 5:16; Kut. 20:12). Kwa upekee hili linaweza kumrejelea mtoto “aliyelaaniwa” na wazazi wake (kama vile Kut. 21:17; Law. 20:9), lakini neno lenyewe linamaanisha ukosefu wa heshima na adabu, ambako kunaweza kudokeza kutokutii. Maelekezo ya kidini yanatokana na wazazi (kama vile 4:9,10,20-25; 6:7; 11:19; 32:46). Kuwakataa wazazi kulileta matokeo ya kupungua kwa imani!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 27:17

¹⁷ Na alaaniwe aondoaye mpaka wa jirani yake. Na watu wote waseme, Amina.

27:17 “aondoaye mpaka wa jirani yake” Hili lilikuwa na mkazo kwa sababu lilifanywa pamoja na wizi wa ardhi waliorithishwa na Mungu, waliyopewa na Yoshua (kv. Yoshua 12-19; Kumb. 19:14; Job 24:2; Mit. 22:28; 23:10; Hosea 5:10)

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 27:18

¹⁸ Na alaaniwe ampotezaye kipofu akakosa njia. Na watu wote waseme, Amina.

27:18 “ampotezaye kipofu akakosa njia” Hii inaweza kuwa nahau ya Kiebrania yenye kumaanisha mtu atoaye ushauri kwa mtu mwingine katika eneo ambalo si rasmi na hivyo kumpa ushauri mbaya. Kwa sababu ya tabia ya huruma inayoelezwa katika Kumbukumbu la Torati, Nafikiri hili linaweza kusemekana kama kutojipatia manufaa kwa mtu aliyekatwa mikono (kv. Law. 19:14).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 19

¹⁹ Na alaaniwe apotoaye hukumu ya mgeni, na yatima, na mjane aliyefiliwa na mumewe. Na watu wote waseme, Amina.

27:19 Hii inafananishwa katika 24:17 na kuonyesha kujali au kuchukua rushwa katika 1:17; 10:17; 16:19. KITENZI “kubadili” (BDB 639, KB 692, *Hiphil* KAULI ENDELEVU) kinamaanisha “kurudi,” lakini hapa na 16:19; 24:17; na Kut. 23:6, kinadokeza kugeuza au kupotosha kile kilicho sahihi/haki.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 27:20

²⁰ Na alaaniwe alalaye na mke wa baba yake, kwa kuwa amefunua mavazi ya babaye. Na watu wote waseme, Amina.

27:20 “alalaye na” Hii (BDB 1011, KB 1486, *Qal* KAULI ENDELEVU) ni tafsida ya kifungu “uhusiano wa kimapenzi,” mara nyingi hili ni katazo la asili (yaani, kujamiiana kwa ndugu wa damu moja, ngono za kikatili, ngono za jinsia moja, kv. Law. 20:11,12,13,18,20; Kumb. 27:20,21,22,23). Ujinsia wa mwanadamu ni wa vyote zawadi ya

ki-Uungu na hamu yenye nguvu. Lazima tendo hili lielezwe na kuelekezwa kwa amani, jamii iendeleayo. Kwa mjadala ulio mzuri kuhusu mashariti ya tendo la ndoa katika Israeli tazama NIDOTTE, juzuu. 4, kr. 1198-1211.

Tendo la kujamiiana kwa ndugu wa damu moja liliathiri amani ya nyumba na familia pamoja na jamii kwa ujumla. Watu halisi walitokana na wale waliozuiwa kuoza kwa kubadilisha tamaduni hadi tamaduni, lakini tamaduni zote za Mashariki ya Kale ya Karibu (isipokuwa familia ufalme wa Kimisri) zina maagizo kuhusu zinaa hii ya ndugu wa damu moja!

☐ **“mavazi ya babaye”** Hii ni ishara ya tendo la ndoa (kv. 22:30; Law. 18:8). Haya ni machafuko mengine ya ukosefu wa heshima. Hii inaashiria dhambi kama ilivyo kwangu kwa gharama yo yote ile!

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 27:21

²¹ Na alaaniwe alalaye na mnyama wa aina yo yote. Na watu wote waseme, Amina

27:21 “alaaniwe alalaye na mnyama wa aina yo yote” Hili linakatazwa katika Law. 18:23; 20:15. Kutoka 22:19 na Luka 15:23 inaonyesha kuwa kimktadha hili lazima lifanyike pamoja na ibada ya sanamu (yaani, taratibu za ushirikina toka Ugariti). Maandiko ya Hittite yanaonyesha kuwa kushiriki pamoja na wanyama waliotenggwa kuliashiria umoja na uungu.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 27:22

²² Na alaaniwe alalaye na umbu lake, binti ya babaye, au binti ya mamaye. Na watu wote waseme, Amina.

7:22 Hizi ni sehemu za sheria za kutokujamiiana kwa ndugu wa damu moja (kv. Mambo ya Walawi 18)

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 27:23

²³ Na alaaniwe alalaye na mkwewe, mamaye mkewe. Na watu wote waseme, Amina.

27:23 Katazo hili limenukuliwa katika Law. 18:8; 20:14.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 27:24

²⁴ Na alaaniwe ampigaye mwenzake kwa siri. Na watu wote waseme Amina.

27:24-25 Mistari hii inashughulika na mauaji (kv. 5:17; Kut. 20:13; 21:12; Lev. 24:17,21). Mauaji yaliichafua nchi yote (kama vile 21:1-9)

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) KUMBUKUMBU LA TORATI 27:25

²⁵ Na alaaniwe atwaaye ujira wa kumwua asiye makosa. Na watu wote waseme, Amina.

27:25 Hili limenukuliwa katika Kut. 23:6-8. Hili linaweza kurejelea (1) muuaji au (2) hakimu aliyepewa rushwa na mtu astahiliye kifo.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 27:26

²⁶ Na alaaniwe asiyeyaweka imara maneno ya torati hii kwa kuyafanya. Na watu wote waseme, Amina.

27:26 “alaaniwe. . . asiyeyaweka imara maneno ya torati hii kwa kuyafanya” Huu ni muhtasari wa mstari wenye kufanana na Amri za Mungu zenye kuhitimisha. Hii inanukuliwa na Paulo katika Gal. 3:10.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Musa anatajwa katika nafsi ya tatu?
2. Kwa nini umuhimu mkuu namna hii anapewa Shekemu (Mt. Gerizimu)?
3. Kwa nini baraka hazitajwi pamoja na laana?

KUMBUKUMBU LA TORATI 28

MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Baraka juu ya utii	Hitimisho la hotuba ya pili ya Musa	Baraka juu ya utii	Ahadi za baraka
28:1-14	28:1-2 28:3 28:4 28:5 28:6 28:7-14	28:1-2 28:3 28:4 28:5 28:6 28:7 28:8 28:9-14	28:1-2 28:3-8 28:9-14
Laana za kutokutii		Madhara ya kutokutii	Laana
28:15-19	28:15 28:16 28:17 28:18 28:19	28:15 28:16 28:17 28:18 28:19	28:15 28:16-19
28:20-46	28:20-24 28:25-44	28:20-24 28:25-29 28:30-35 28:36-37 28:38-42 28:43-44 28:45-46	28:20-26 28:27-29a 28:29b-35 28:36-37 28:38-42 28:43-44 28:45-46
28:47-57	28:47-57	28:53-57	Kuhusu vita na kwenda uhamishoni 28:47-48 28:49-57
28:58-63	28:58-63	28:58-63	28:58-62a 28:62b-68
28:64-68	28:64-68		

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya ya tatu
4. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

Hii ni sehemu ya fasihi, sura ya 27-28, ambayo mara nyingi inarejelea kama kipengere cha “laana na baraka” ya agano.

- A. Nafikiri Agano la Kale lote laweza kuonekana kama ni matokeo ya kushindwa kulitenda agano ipasavyo, na kwa hiyo, wakatembelewa na laana iliyoko sura ya 27:15-26; 28:15-68.
- B. YHWH alihitaji Israeli kuwa mwongozo wa kimafunuo kwa ajili ya ulimwengu wote upate kumjua. Alihitaji kuibariki Israeli ili kupata uelewa wa mataifa yote na hivyo basi kuyavuta mataifa yote kuja kwake. Tazama Mada Maalum: Upendeleo wa Kiinjilisti wa Bob katika 4:6.
- C. Laana ya ukaidi ni kubwa zaidi kuliko baraka iliyoahidiwa. Muundo ule ule unafananihwa na mikataba ya Mashariki ya Karibu ya Kale (tazama Meredith G. Kline, *Treaty of the Great Kings: The Covenant Structure of Deuteronomy* and D. Brent Sandy and Ronald L. Giese, Jr., *Cracking Old Testament Codes*, kur. 125-128.
- D. Kipengere cha kulaani na kubariki kinafanana na kile kilichopo katika kitabu cha Mambo ya Walawi 26.
- E. Hii ni hotuba ya pili ya Musa (yaani., sura ya 5-28). Hotuba ya kwanza inarejelea nyuma kwenye neema ya YHWH, iliyoiondoa kwa nguvu Israeli toka Misri na uwepo Wake na uangalizi wake kipindi chote cha kutangatanga jangwani. Hotuba ya pili inaangazia juu ya mapenzi ya YHWH kwa ajili ya taifa la Israeli huko kwenye nchi ya ahadi. Aliifanya Israeli kuwa ya kipekee ili kumfunua Yeye katika ulimwengu. Hotuba ya tatu (sura ya 29-32) inashughulika na kulifanya upya agano na uthibitishaji juu ya uaminifu wa Israeli na utii kwa YHWH pekee.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGIU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 28: 1-2

¹Itakuwa utakapoisikia sauti ya Bwana, Mungu wako, kwa bidii, kutunza kuyafanya maagizo yake yote nikuagizayo leo, ndipo Bwana, Mungu wako, atakapokutukuza juu ya mataifa yote ya duniani; ²na baraka hizi zote zitakujilia na kukupata usikiapo sauti ya Bwana, Mungu wako.

28:1,2,9,13 “Itakuwa utakapoisikia” Hili kwa wazi linaonyesha asili ya kimasharti ya sheria za Musa na kwa hali hiyo, kumaanisha maagano yote ya Agano la Kale (tazama Mada Maalum: Agano katika 4:13) isipokuwa lile la Nuhu (k.v. Mwa. 9:8-17). Dhana ya kimasharti pia inaonekana katika Agano Jipya (k.v. Marko 1:15; Mdo. 20:21 na Efe. 2:8-9 na 10). Asili ya neno “ikiwa utakapoisikia . . .ndipo” la agano linaonyesha hitaji la uajibikaji lililotarajiwa upande wa mwamini. Shida ni kuwa mwanadamu aliyeanguka hawezi na hataweza kulitenda, kwa hiyo, Agano la Kale linataka hitaji kwa ajili ya Agano Jipya (k.v. Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-32; Gal. 3:15-29).

28:1,2,13 “kwa bidii.....kutunza kuyafanya ” Neno la kwanza “kwa bidii uyatunze” ni KITENZIJINA HALISI na *Qal* KAULI ISITIMILIFU ya asili ile ile ya neno (BDB 1033, KB 1570), ambayo ilikuwa ni namna ya kisarufi ya kuonyesha msisitizo. Hili linafuatiwa na *Qal* VITENZIJINA VYA MUUNDO WA MANENO viwili:

1. “kuwa mwangalifu” - BDB 1036, KB 1581
2. “kulifanya” - BDB 793, KB 889 lazima ielezwe kuwa uhusiano wa agano la mwamini linaloendelea na Mungu linaathiriwa kwa utii wao katika nuru na ukweli walionao.

☐ “maagizo ”tazama Mada Maalum katika 4:1.

☐ “nikuagizayo leo” KITENZI hiki (BDB 845, KB 1010, *Piel* ENDELEVU) kinarudiwa kote katika sura hii (k.v. mistari ya 1,8,13,15,45). YHWH ni Mkuu. Mara zote huweka mipaka na utosherevu wa agano na kuanzisha ukabiliano na wanadamu.

28:1 “ndipo Bwana, Mungu wako, atakapokutukuza juu ya mataifa yote ya duniani” Kusudi la kutukuza ni ufunuo (k.v. 26:19; 28:13)! Mungu anahitaji kuuvuta ulimwengu wote kuja kwake kupitia Israeli (k.v. Mwa. 12:3; 22:18;Kut. 19:5- 6). Tazama Mada Maalum: Mapendeleo ya Kiinjilisti ya Bob katika 4:6.

28:2 “na baraka hizi zote” Neno (BDB 139) linahusiana kwenye asili ya maneno “kupiga magoti” (BDB 138). YHWH aliwapa Israeli kuchagua (k.v. 11:26-31; 30:1,19). Haya makubaliano na agano la YHWH yanahitaji kuamua hatma!

☐ **“zitakujilia”** Kifungu cha kinahau (BDB 97, KB 112, *Qal* KAULI TIMILIFU) kimetumika hapa kwa ajili ya kubariki, lakini katika mstari wa 15 kwa ajili ya laana.

☐ **“kukupata”** KITENZI (BDB 673, KB 727, *Hiphil*) kimetumika:

1. kubariki, kutenda, na kuichukua Israeli kwa sababu ya utii wake, mstari. 2
2. Kulaani, kutenda na kuichukua Israeli kwa sababu ya ukaidi wake, mistari. 15,45

☐ **“usikiapo”** Katika mstari wa 1 neno (BDB 1033, KB 1570) lilikuwa ni namna ya *Qal* KITENZI JINA HALISI na *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU. Hapa kuna *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU (k.v. mistari ya . 15,49; 30:10,12,13,17; 31:12) na katika mstari wa 45, 62 ni *Qal* KAULI TIMILIFU (k.v. 30:8).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 28:3

³Utabarikiwa mjini, utabarikiwa na mashambani.

28:3 Utabarikiwa mjini..... mashambani” Hii ni namna ya kiistiari ya kuelezea baraka za wote (k.v. mstari. 4-6, 8)

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 28:4

⁴Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, maongeo ya ng’ombe wako, na wadogo wa kondoo zako.

28:4 “Utabarikiwa. .uzao wa tumbo lako. .wanyama. .mifugo. .maongeo ya ng’ombe wako” Wingi wa wanyama wenye afya pamoja na watoto ilikuwa ni ishara ya mafanikio na utajiri. Mtu mwenye familia kubwa, kundi kubwa la mifugo, ni yule aliyekuwa amebarikiwa na Mungu (k.v. 7:13; 28:4,11; 30:9). Hizi zilikuwa ni ishara za wazi za kubarikiwa na Mungu (k.v. Mwa. 1:22,28)

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 28:5

⁵Litabarikiwa kapu lako, na chombo chako cha kukandia unga.

28:5 “Litabarikiwa. ..kapu lako” Hili kapu lilitumika kuchukulia matunda au nafaka (k.v. 26:2). Hili linaongelea mafanikio ya kilimo.

☐ **“Litabarikiwa. .chombo cha kukandia”** Hiki kilikuwa ni chombo cha kuandalia chakula (yaani., mkate wa kila siku). Hii ilikuwa ni namna ya kusema, “siku zote patakuwepo na chakula cha kutosha mezani.” Kinyume chake kimeelezewa katika mstari wa 17.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 28:6

⁶Utabarikiwa uingiapo, utabarikiwa na utokapo.

28:6 “Utabarikiwa. .uingiapo. .na utokapo” Huu ni msemo wa Kiebrania (k.v. 31:2; Zab. 121:8; Isa. 37:28) kwa ajili ya maisha yaliyobarikiwa kwa namna zote (k.v. kinyume na mstari wa 19).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 28:7-14

⁷Bwana atawafanya adui zako wainukao juu yako kupigwa mbele yako; watakutokea kwa njia moja, lakini watakimbia mbele yako kwa njia saba. ⁸Bwana ataiamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na mambo yote utakayotia mkono wako; naye atakubarikia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako. ⁹Bwana atakuweka uwe taifa takatifu kwake, kama alivyokuapia; utakaposhika maagizo ya Bwana, Mungu wako, na kutembea katika njia zake. ¹⁰Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa jina la Bwana, nao watakuwa na hofu kwako. ¹¹Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri, katika uzao wa tumbo lako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako, katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako kwamba atakupa. ¹²Atakufunulia Bwana hazina yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati wake, na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako; nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe. ¹³Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini; utakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kufanya; ¹⁴msipokengeuka katika maneno niwaamuruyo leo kwa lo lote, kwenda mkono wa kuume wala wa kushoto, kwa kuifuata miungu mingine na kuitumikia.

28:7 “adui zako” Hii KAULI ENDELEVU (BDB 33, KB 38 *Qal* KAULI ENDELEVU) imetumika mara nane katika sura hii (k.v. mistari ya. 7,25,31,48,53,55,57,68). Inarejelea kwenye uadui uliopo wa mtu na mtu au kikundi na kikundi. YHWH anaahidi juu ya adui wale waichukiao Israeli (k.v.Kut. 23:22), lakini kutokana na wao kulikaidi agano sasa Yeye ni adui kwa Israeli! Kama Israeli watamtii YHWH naye atapigana na maadui zao (k.v. 30:7; 33:27-29).

☐ **“watakimbia mbele yako kwa njia saba”** Huu ni msemu unaorejelea maadui wa Israeli wasiounkana pamoja, wenye kujaa hofu waliokimbia kurudi nyuma (k.v. mistari ya 20, 25). Tazama Mada Maalum: Uwakilishi wa Namba katika Maandiko katika 23:3.

28:8 “baraka ije juu . . . ghala zako ” Hili linarejelea kwenye maghala yenye kutunza chakula (k.v. Mith. 3:10). Wayahudi wa leo wanasema hili linarejelea kwenye baraka za siri za YHWH.

☐ **“katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako”** Hili linarudi nyuma kwenye ahadi za Ibrahimu katika Mwa. 12:1-3. Nchi ilikuwa ni ahadi maalum ya Mungu iliyotimizwa wakati wa ushindi wa Israeli.

28:9 “Bwana atakuweka” KITENZI (BDB 877, KB 1086, *Hiphil* CHA KAULI ISIO TIMILIFU) kimsingi kinamaanisha “kuinuliwa.” Kimetumika katika maana tofauti mbali mbali katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati kwenye neno *Hiphil* (yaani., [1] kulithibitisha agano, k.v. 8:18; [2] kuwa juu ya matazamio, k.v. 18:15,18; [3] kuyaongeza makundi ya wanyama, k.v. 22:4; na [4] kuweka kumbukumbu, k.v. 27:3). Hapa limetumika kwa maana ya kiistiari ya neno “atakuweka,” kama ilivyo katika 25:7 na 29:13.

☐ **“kuwa taifa takatifu”** Neno “takatifu” linamaanisha “kujitenga kwa ajili ya huduma ya Mungu” (BDB 871 na 872, tazama Mada Maalum katika 5:12, k.v. Kut. 19:5-6). Israeli ilimaanishwa kuwa ufalme wa kikuhani kuyaleya mataifa yote kwa YHWH.

☐ **“utakaposhika”** Hii ni stiari ya kibiblia kwa ajili ya imani katika mfumo wa maisha na utii (k.v. 5:33; 8:6; 10:12; 11:22; 19:9; 26:17; 30:16).

28:10 “Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa jina la Bwana” Kifungu “umeitwa kwa jina la Bwana” (BDB 894, KB 1128, *Niphal* KAULI ILIYO TIMILIFU) kinaonyesha umiliki wa YHWH kwa Israeli (k.v. II Sam. 6:2; Isa. 43:7; Yer. 7:10-12; 14:9; 15:16; 32:34; Dan. 9:18,19; Amos 9:12). YHWH anahitaji Israeli kuwa njia ya kimafunuo kwa ajili ya ulimwengu wote ili wamujue Yeye. Anataka kuibariki Israeli ili kuyasikilizisha mataifa na hivyo kuyavuta mataifa yamwendee Yeye (k.v. v. 25, 37). Tazama Mada Maalum katika 4:6.

☐ **“nao watakuwa na hofu kwako”** Baraka za YHWH, kwa maeneo yote ya majumbani na sehemu za vita, kuleta hofu/heshima (BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI TIMILIFU, k.v. 7:19; 17:13) upande wa wapagani wenye kuamini mambo ya ushirikina kwa mataifa jirani yaliyoizunguka. Israeli haikutakiwa kuwa na hofu (BDB 431, KB 432) kwa

sababu YHWH alikuwa pamoja nao, kwa ajili yao, na kuwapigania (mf., 1:21,29; 3:2,22; 7:18; 20:1,3; 31:6,8).

28:11 Haya ni maelezo mafupi ya baraka za YHWH kwa watu watiifu wa agano (yaani., 11:14).

28:12 “hazina yake nzuri” Hii (BDB 373 II and 69) ilikuwa ni alama ya mbingu na mvua (k.v. mistari ya. 23-24; Zab. 85:12; Mal. 3:10). Yumkini ni kejeli kwa ajili ya ibada ya *Ba'al*. *Ba'al* alikuwa ni mungu wa wakanaani wa mafanikio (yaani., mvua, k.v. I Fal. 17-18). Na bado, alikuwa ni YHWH aliyetoa baraka zote kwa watu wake (k.v. mstari wa 47; 11:14; Lev. 26:4).

☐ **“kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati wake”** Kitenzi hiki (BDB 678, KB 733) kinatumika mara nyingi katika sura hii kwa ajili ya zawadi za baraka za agano la YHWH (k.v.mistari ya 1,7,8,11,12,13). Sio tu YHWH atayafungua madirisha ya mbingu na kuleta mvua, bali atatenda kwa wakati muafaka (yaani., mvua za mwanzoni na mwisho,wakati wa kupanda na mazao kukomaa).

☐ **“nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe ”** Hii ilikuwa ni ishara nyingine ya baraka za Mungu walizotakiwa kuwa nazo ili kuwakopesha wengine (k.v. 23:20)! Matokeo ya kutokutii kwa kiasi kikubwa yanakinzana katika mstari 44!

28:13 Mstari huu una nahau mbili za mafanikio na uweza:

1. Kichwa wala sio mkia
2. Mtakuwa juu, wala sio chini

Lakini kumbuka kipengere cha kimasharti. Nahau ile ile ilitumika katika mstari wa 1, “uwe mwangalifu kuyashika” (VITENZIJINA VYA MUUNDO WA MANENO viwili). Matokeo yaliyo sababishwa na ukaidi yanaonekana katika mstari wa 44

28:14 “msipokengeuka..... kwenda mkono wa kuume wala wa kushoto” Kiuhalisia kinatumika katika Hes. 20:17; 22:26; Kumb. 2:27, lakini mara nyingi ni nahau ya Kiebrania kwa ajili ya “kukengeuka kwa namna yeyote toka njia kuu ni dhambi” (k.v. 5:32; 17:11,20; Yosh. 1:7; 23:6; II Fal. 22:2). Tazama hapa, ibada ya sanamu imerejelewa (k.v. 5:7-9; 27:15; Kut. 20:23; 34:17).

☐
NASB, NRSV “Niwaamuruyo leo”
NKJV “Nitakayowaamuru hii leo”
TEV
NJB “maneno niwaamuruyo ninyi leo”
Hiki kifungu kinaonekana kudokeza siku maalum ya kuzitoa sheria (k.v. mistari ya 1,13,14,15). Hata hivyo neno, *'olam* laweza kurejelea kipindi cha wakati. Tazama Mada Maalum katika 4:40. Sababu kwa ajili ya swali hasa ni nini “kitabu” kinarejelea kwenye mistari ya 58 na 61?:

1. Kumbukumbu la Torati lote
2. Moja ya hotuba za Musa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati
3. Sehemu kubwa ya sheria ikijumuisha sehemu za vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi na Hesabu

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 28:15

¹⁵Lakini itakuwa usipotaka kuisikiza sauti ya Bwana, Mungu wako, usiyaangalie kufanya maagizo yake yote na amri zake, nikuagizazo hivi leo, ndipo zitakapokujia laana hizi zote na kukupata.

28:15-37 Kipengele hiki cha laana hakihitaji tafasiri ya wazi. Hivyo, kilikuwa kinajenga wazo la kuwepo na janga. Aina hii ya majanga yatakuandama kama kutakuwepo na ukaidi. Ilikuwa ni namna ya kuyajenga mawazo juu ya kile kinatakachotokea ikiwa Israeli watakaidi sheria ya YHWH.

28:15 “usiyaangalie kufanya ” Huu ni msamiati wenyewe na muundo wa kisarufi unaoapatikana katika mistari ya 1,13; 32:46. Miundo kama ile ile ya maneno yale yale unapatikana katika 28:58 and 29:8. Utii ni wa muhimu. Utii sio msingi wa agano, bali ni anguko la asili! Agano limewekwa katika hali ya upendo na ukuu wa YHWH, lakini mwendelezo wake na uaminifu unatunzwa katika utii. Kama utanipenda, na kuyatunza maagizo yangu!

☐ **“maagizo yake yote na amri zake”** Tazama Mada Maalum katika 4:1.

☐ **“laana”** Huu ni muundo wa NOMINO toka kwenye asili ya neno “kuwa chini ya kiwango” (BDB 886-887, k.v. 27:15-26, 28:15-68). Laana hizi zilimaanisha kuisababisha Israeli kumrudia YHWH.

☐ **“kukupata”** Tazama maelezo katika mstari wa 2

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 28:16

¹⁶Utalaaniwa mjini, utalaaniwa na mashambani.

28:16-19 Mistari hii inafanana kabisa. Mistari ya 3-6 inahusiana na baraka; mistari ya 16-19 inahusiana na laana.

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): KUMBUKUMBU LA TORATI 28:17

¹⁷Litalaaniwa kapu lako na chombo chako cha kukandia.

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 28:18

¹⁸Utalaaniwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, maongeo ya ng'ombe wako, na wadogo wa kondoo zako

2:18

NASB, NJB “uzao wa tumbo lako”

NKJV “uzao wa tumbo lako”

NRSV “uzao wa umbu lako”

TEV “watoto”

Kifungu halisi ni, “uzao wa umbu lako.” Kuwa na watoto wengi, walio na afya ilikuwa ni moja ya baraka (k.v. mistari ya 4,11), lakini ukaidi ulileta matokeo yaliyo kinyume ya ahadi ya agano!

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 28:19

¹⁹Utalaaniwa uingiapo, utalaaniwa na utokapo,

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 28:20-24

²⁰Bwana atakuletea laana na mashaka, na kukemewa, katika yote utakayotia mkono wako kuyafanya, hata uangamie na kupotea kwa upesi; kwa ule uovu wa matendo yako, uliyoniacha kwayo. ²¹Bwana atakuambatanisha na tauni, hata atakapokwisha kukuondoa katika nchi uingiayo kwa kuimiliki. ²²Bwana atakupiga kwa kifua kikuu, na kwa homa, na kwa kuwashwa, na kwa hari ya moto, na kwa upanga, na kwa ukaufu, na kwa koga; navyo vitakufukuza hata uangamie. ²³Na mbingu zako zilizo juu ya kichwa chako zitakuwa shaba, na nchi iliyo chini yako itakuwa chuma. ²⁴Bwana atafanya mvua ya nchi yako iwe vumbi na mchanga; itakujilia juu yako kutoka mbinguni hata uangamie.

28:20 “mashaka” Hili neno (BDB 223) linatumika kwenye kuvishinda vita (k.v. 7:23). Ni kinyume cha mistari ya 7 na 25. Mashaka yatakuwa juu ya Israeli kama watalikaidi neno la Mungu.

☐ **“kukemewa”** Neno (BDB 172) linapatikana hapa tu katika Agano la Kale.

☐ **“uangamie na kupotea kwa upesi”** Angalia ufanano uliopo:

1. “ataangamiza” - BDB 1029, KB 1552, *Niphal* KITENZI CHA MUUNDO WA MANENO, k.v. 4:26; 6:15
2. “kupotea” - BDB 1, KB 2, *Qal* KITENZI CHA MUUNDO WA MANENO, k.v. Law. 26:38; Kumb. 4:26; 8:19-20; 11:17; 30:18-20; Yosh. 23:13,16 pamoja na KIWAJILISHI “haraka” (BDB 555 II)

☐ **“kwa ule uovu wa matendo yako, uliyoniacha kwayo”** Tambua kuwa kukengeuka kwenye maagizo kunaonekana kama kumusahau YHWH!

28:21 “tauni” Hili (BDB 184) linarejelea kwenye mapigo (k.v. Law. 26:25; Hes. 14:12) kama YHWH alivyoyatuma kule Misri (k.v. Kut. 5:3; 9:15).

☐ **“kuambatinishia”** KITENZI (BDB 179, KB 209, *Hiphil*) ni chenye KUAMURU katika muundo. Hukumu ya YHWH itakuwa karibu nao mpaka pale itakapotimiliza kazi yake (yaani., “kukuangamiza wewe” BDB 477, KB 476, *Piel* KITENZI CHA MUUNDO WA MANENO). Neno linatumika kwa ajili ya kile Israeli ilipaswa kukifanya kwa YHWH (yaani., kuambatana naye, k.v. 10:20; 11:22; 30:20).

28:22 “upanga” Tazama orodha ya vitu YHWH atakavyovituma kwa Israeli iliyokaidi:

1. utakupiga (BDB 1006, kv. Law. 26:16), ugongwa wa mapafu
2. homa (BDB 869, kv. Law. 26:16)
3. kuwashwa (BDB 196)
4. hari ya moto (BDB 359, #2,3, na 4 yote inahusiana na moto; hili linaonekana kudokeza hali ya ukame, k.v. NRSV)
5. upanga (BDB 352)
6. ukaufu (BDB 995, kuyakausha mazao, k.v. I Fal. 8:37; II Nya. 6:28; Amos 4:9)
7. koga (BDB 439, k.v. I Fal. 8:37; II Nya. 6:28; Amos 4:9; Hag. 2:17; neno linamaanisha “kijani kibichi,” kwa hiyo, “koga la kijani kibichi”)

Wanadamu na masuala ya kilimo watateseka na kufa! Tambua idadi ya kiishara ya mateso (yaani., saba; pia pana baraka saba zilizoorodheshwa katika sura hii). Tazama Mada Maalum katika 23:3.

28:23 “chuma” Chuma mara nyingi ni stiari kwa ajili ya ugumu wa kitu:

1. Nchi kutozalisha kitu, kwa sababu ya kukosekana kwa mvua kunasababisha kuwe kugumu kama chuma, mstari wa 23, k.v. Law. 26:19
2. Kongwa la chuma litawekwa katika shingo ya Israeli, mstari wa 48
3. Misri kama chuma cha moto wa mateso, k.v. 4:20

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 28:25-26

²⁵Bwana atakufanya upigwe mbele ya adui zako; utawatokea juu yao kwa njia moja, lakini utakimbia mbele yao kwa njia saba; nawe utatupwa huko na huko katika falme zote za duniani. ²⁶Na mzoga wako utakuwa chakula cha ndege wote wa angani, na wanyama wote wa duniani, pasiwe na mtu wa kuwafukuza.

28:25 “; utawatokea juu yao kwa njia moja, lakini utakimbia mbele yao kwa njia saba” Hii ni stiari yenye kuelezea mpango wa kijeshi wa Israeli kuwa usiofaa. Saba ni alama ya kihesabu kwa ajili ya “ulinzi.” Israeli itakuwa katika hali tete ya kukimbia. Ahadi za “vita takatifu” zimekwisha badilishwa!

☐ **“nawe utatupwa huko na huko katika falme zote za duniani”** Israeli itatumiwa na YHWH kumfunua Yeye mwenyewe kwa ulimwengu; upande mmoja katika hali ya wema (yaani., baraka) au upande wa pili katika hali isiyo njema (yaani., laana, k.v. mstari wa 37; II Nya. 29:8; Yer. 15:4). YHWH anahitaji kuitumia Israeli kwa ajili ya kumfikia mwanadamu (tazama Mada Maalum: Mapendeleo ya Kiinjilisti ya Bob katika 4:6). Hii inalithibitisha kusudi lake!

28:26 “mzoga wako utakuwa chakula” Kwa ajili ya Israeli hili lilikuwa ni janga kubwa kwa mtu kutozikwa na hivyo kuliwa na mnyama (k.v. I Sam. 17:44-46). Kwa sababu ya kuwataja “ndege,” wengi wao wanaliona hili kama nukuu ya matukio ya siku za mwisho (k.v. Isa. 18:14; Yer. 7:33; 16:4; 19:7; 34:20; Ezek. 29:5; 32:4; 39:4).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 28:27-37

²⁷ Bwana atakupiga kwa majipu ya Misri, na kwa bawasiri, na kwa pele, na kwa kujikuna, ambayo hupati kupoa. ²⁸ Bwana atakupiga kwa wazimu, na kwa upofu, na kwa bumbuzi la moyoni; ²⁹ utakwenda kwa kupapasa-papasa mchana, kama apapasavyo kipofu gizani, wala hufanikiwi katika njia zako; nawe sikuzote utaonewa na kutekwa nyara, wala hapatakuwa na mtu wa kukuokoa. ³⁰ Utaposa mke na mume mwingine atalala naye; utajenga nyumba usiikae; utapanda mizabibu usitumie matunda yake. ³¹ Ng'ombe wako atachinjwa mbele ya macho yako, usile nyama yake; utanyang'anywa punda wako mbele ya uso wako kwa jeuri, usirudishiwe; kondoo zako watapewa adui zako, usipate mtu wa kukuokoa. ³² Wanao na binti zako litapewa taifa lingine, na macho yako yataangalia, na kuzimia kwa kuwatamani mchana kutwa; wala hapatakuwa na kitu katika uwezo wa mkono wako. ³³ Matunda ya nchi yako, na taabu yako yote, vitaliwa na taifa usilolijua; utaonewa tu, na kupondwa chini daima; ³⁴ hata uwe mwenye wazimu kwa yaonwayo na macho yako, utakayoyaona. ³⁵ Bwana atakupiga magoti na miguu kwa jipu lililo zito, usilopata kupozwa, tokea wayo wa mguu mpaka utosi wa kichwa. ³⁶ Bwana atakupeleka wewe, na mfalme wako utakayemweka juu yako, kwa taifa usilolijua wewe wala baba zako; nawe huko utatumikia miungu mingine ya miti na mawe. ³⁷ Nawe utakuwa ushangao, na mithali, na dharau, kati ya mataifa yote huko atakakokuongoza Bwana.

28:27 “kwa majipu ya Misri” Angalia orodha ya mapigo na majanga (mapigo ya Misri na kinyume cha baraka za agano) ambayo YHWH atayaweka juu ya Israeli iwapo hawatalitii agano lake. Kwake Yeye vingi hupatikana, na kuhitajiwa (mf., Luka 12:48).

1. NASB, NKJV, NRSV, TEV “majipu,” k.v. mistari. 27,35
 NJB “upele”
 JPSOA “kujikuna”
 BDB 1006, k.v. Kut. 9:9-11. Inarejelea kwenye aina ya majipu yenye kufura/kutumbuka.
2. NASB, JPSOA “uvimbe,” mstari. 27
 NKJV “bawasiri”
 NRSV “upele”
 TEV “uchungu”
 NJB “kujikuna kusiko poa”
 BDB 779 II, k.v. I Sam. 5:6,9,12. Wasomi wengi wamelitafasiri hili kama dalili za tauni (yaani., mtoki, uvimbe mkubwa wenye kuvilia, k.v. I Sam. 5:9-6:17, ambavyo, kwa namna fulani, laweza kuhusianishwa na panya)
3. NASB, NKJV “upele,” mstari. 27
 NRSV, NJB “kujikuna”
 JPSOA “makovu yenye kuwasha”
 BDB 173, k.v. Law. 21:20; 22:22
4. NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB “upele,” mstari. 27
 BDB 360 III. Neno hili linapatikana mahali hapa tu katika Agano la Kale na linarejelea kwenye mwasho wa ngozi usababishwao na nyenyere (k.v. NIDOTTE, juzuu. 2, uk. 278).
5. NASB, NKJV, NRSV, NJB “wazimu,” mistari. 28,35
 TEV “kupotelewa na ufahamu”
 BDB 993, k.v. Zak. 12:4
6. NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB “upofu, mistari ya 28,29
 BDB 734, k.v. Lam. 4:14; Zef. 1:17
7. NASB “bumbuzi la moyoni,” mstari 28
 NKJV “mashaka ya moyo”

- NRSV "kuvurugikiwa na akili"
 TEV "mashaka"
 NJB "kuharibikiwa na akili"
 BDB 1069, k.v. Zak. 12:4
8. NASB, NKJV "utaonewa ... siku zote," mstari wa 29
 NRSV "kudharauliwa siku zote"
 TEV "kuonewa siku zote"
 NJB "kuvunjwa moyo"
 BDB 798, *Qal* KAULI TENDWA YA HALI YA KUENDELEA, . Law. 6:2
9. NASB, TEV "utatekwa nyara," mstari 29
 NKJV "kutekwa nyara siku zote"
 NRSV "siku zote utatekwa nyara"
 NJB "kuteka nyara"
 BDB 159, *Qal* KAULI TENDWA YA HALI YA KUENDELEA, k.v. Law. 6:2
10. NASB "mke ... kutoheshimika," mstari wa 30
 NKJV, NRSV "atalala nae"
 BDB 993, KB 1415, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU
11. Utajenga nyumba na usiikae, mstari wa 30
 12. Utapanda mizeituni usiitumie, mstari wa 30
 13. Utachinja ng'ombe wako watakula wengine, mstari wa 31
 14. Binti zako watachukuliwa, mstari wa 32
 15. Matunda yako yataliwa na wengine, mstari wa 33
 16. Taabu yako yote watafaidi wengine, mstari wa 33
 17. 17. NASB, NKJV "utaonewa tu," mstari wa 33
 NRSV "utadharauliwa"
 TEV "utaonewa"
 NJB "utakatishwa tamaa"
 BDB 798, KB 897, *Qal* KAULI TENDWA YA HALI YA KUENDELEA, k.v. v. 29; I Sam. 12:4; Amos 4:1
18. NASB, NKJV, NRSV, NJB "utapondwa chini," mstari wa 33
 TEV "utaonewa"
 BDB 954, KB 1285, *Qal* KAULI TENDWA YA HALI YA KUENDELEA, k.v. I Sam. 12:3-4; Amos 4:1
19. NASB, NKJV, NRSV, NJB "utapata wazimu," mstari wa 34
 TEV "utachanganikiwa" BDB 993, KB 1415, *Pual* HALI YA KUENDELEA, k.v. mstari wa 30
20. NASB "atakupiga. . .kwa jipu lililo chungu," mstari wa 35
 NKJV "atakupiga. . .kwa jipu lililo zito"
 NRSV "atakupiga. . .na jipu lililo baya"
 TEV "ataku funika. . .na majipu yenye kutaabisha"
 NJB "atakupiga chini na vimbe zenye kutoa usaha"
 BDB 645, KB 697, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU na VISHAMIRISHO viwili, BDB 1006 na 948
21. Mfalme ataondolewa na kuwekwa watawala wengine, mstari wa 36
 22. Utaitumikia miungu ya kigeni, mstari wa 36
 23. utakuwa:
- a.
 NASB "na hofu," v. 37
 NKJV "na mshangao"
 NRSV "kitu chenye kujaa hofu"
 NJB "kupata mshangao"
 BDB 1031 I, k.v. II Fal. 22:19; Yer. 5:30; 25:9,11,18,38; 29:18; 42:18; 44:12,22; 49:13,17; 50:23; 51:37,41

b.

NASB, NKJV, NRSV
NJB
BDB 605, k.v. I Fal. 9:7; Yer. 24:9

“mithali,” mstari wa 37
“kudharauliwa”

c.
NASB
NKJV, NRSV
NJB
BDB 1042, k.v. I Fal. 9:7; Yer. 24:9

“dharau,” mstari wa 37
“kudharauliwa”
“kukejeliwa”

24. NASB
NKJV, NRSV
NJB
“Bwana atakuongoza”
“Bwana atakuongoza”
“Yahweh atakuchukua mbele”

KITENZI hiki (BDB 624 I, KB 675, *Piel* KISICHO TIMILIFU) kimetumika kuwaongoza wanyama (mf., Kut. 3:1). Kikajakuwa ni stiari ya (1) kuwaongoza watu katika hukumu (mf., 4:27; I Sam. 30:2,22; Isa. 20:4) au (2) YHWH kuongoza kama mchungaji mwema (k.v. Zab. 48:14; 78:26,52; 80:1). Wanadamu wataongozwa (mchungaji) au kuongozwa (mwamuzi) kwa kuitii imani yao. Hili linawakumbusha wale waliopigwa na majipu huko Misri (k.v. Kut. 9:8 na kuendelea). Na haya mapigo yakaipata Israeli yenye ukaidi (k.v. 7:15; 28:60,61).

28:32 Tambua masumbufu haya ya Waisraeli:

1. Watoto wao watapewa taifa lingine (BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI TENDA ENDELEVU)
2. macho yataangali (BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU)
3. macho yao yatatamani mchana kutwa (neni, BDB 479, linapatikana hapa tu katika Agano la Kale)
4. hawana uweza wa kuyazuia (BDB 34 II, MUUNDO WA MANENO, BDB 43)

28:33 “wataonewa” Hili neno lilitumika mara kadhaa kwa kujinufaisha kutokana na masikini na wenye kuchukiwa, lakini hapa linatumiwa na YHWH kuwasulubu watu wakaidi.

28:35 “tokea wayo wa mguu mpaka utosi wa kichwa” Hii ni stiari kwa ajili ugonjwa uliotapakaa ambao mtu hawezi pona (k.v. Ayubu 2:7; Isa. 1:5-6).

28:36 “mfalme wako” Musa alitambua kuwa kutakuwepo na mfalme muda fulani (k.v. 17:14-20). Waisraeli walikuwa ni jamii ya kikabila. Hapakuwepo na mfalme mpaka pale walipompata Sauli (k.v. I Samuel 8).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 28:38-44

³⁸Mbegu nyingi utazichukua nje shambani, lakini utavuna haba, kwa kuwa nzige watazila. ³⁹Utapanda mizabibu na kuitengeza, wala hutakunywa katika divai yake, wala kuichuma kwani italiwa na mabuu. ⁴⁰Utakuwa na mizeituni katika mipaka yako yote usijipake mafuta yake; kwa kuwa mzeituni wako utapukutika. ⁴¹Utazaa wana na binti, lakini hawatakuwa wako wewe; kwa sababu watakwenda utumwani. ⁴²Miti yako yote, na mazao ya nchi yako, nzige watakuwa nayo. ⁴³Mgeni aliye kati yako atazidi kupaa juu yako; nawe utazidi kushuka chini. ⁴⁴Yeye atakukopesha, wala wewe usimkopeshe; yeye atakuwa ni kichwa, wewe utakuwa mkia.

28:38-42 Angalia tena orodha za majaribio ya Israeli ya kutaka kufanikiwa, ambayo yalikatiliwa mbali na YHWH:

vitendo

1. mbegu nyingi, mstari wa 38
2. watapanda mizabibu, mstari wa 39
3. utapanda miti ya mizeituni, mstari 40
4. utazaa watoto, mstari wa 41
5. miti itazaa, mstari wa 42

matokeo yake

1. nzige watazila
2. italiwa na mabuu
3. itapukutika
4. watakwenda utumwani
5. nzige wataila

Ahadi ya mafanikio ya YHWH yanakanushwa kwa Israeli ya agano iliyokaidi!

28:40 “usijipake mafuta” Watu wa Mashariki ya Karibu ya Mbali walijipaka mafuta ya mizeituni kwenye nyuso zao kama alama ya mafanikio na furaha (mf., Ruth 3:3; II Sam. 12:20; 14:2).

28:43-44 Hii mistari miwili inaelezea majukumu yaliyo kinyume ya Israeli na wakaazi walio wageni (wapiti njia, BDB 158):

1. wageni watainuka juu yenu
 - a. watakuwa juu na juu zaidi (BDB 751)
 - b. mtakuwa chini tena chini zaidi (BDB 641) [kinyume cha mistari wa 13]
2. wageni watawakopesheni [kinyume cha mistari wa 12]
3. mgeni atakuwa kichwa kwenu [kinyume cha mistari wa 13]

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 28:45-46

⁴⁵Na laana hizi zote zitakujilia juu yako, zitakuandama na kukupata, hata uangamizwe, kwa kuwa hukuisikiza sauti ya Bwana, Mungu wako, kushika maagizo yake na amri zake alizokuagiza; ⁴⁶nazo zitakuwa juu yako kwa ishara na ajabu, na juu ya uzao wako milele.

28:45-48 Angalia sababu na madhara ya hukumu ya agano la YHWH:

1. Kisababishi
 - a. Israeli hawatasikia (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI TIMILIFU) na kuitunza (BDB 1036, KB 1581, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO) sheria na maagizo ya YHWH, mistari wa 45
 - b. Israeli hawakumtumikia (BDB 712, KB 773, *Qal* KAULI TIMILIFU [mara mbili]) YHWH, mistari wa 47:
 - 1) Kwa furaha
 - 2) Kwa moyo wa furaha
 - 3) Watashukuru kwa ajili ya utele wa vitu
2. madhara
 - a. laana
 - 1) itawajilia juu yenu, mistari wa 45, BDB 97, KB 112, *Qal* KAULI TIMILIFU
 - 2) zitawaandama, mistari wa 45, BDB 922, KB 1191, *Qal* KAULI TIMILIFU
 - 3) zitawapata, mistari wa 45, BDB 673, KB 727, *Hiphil* KAULI TIMILIFU
 - 4) hata ziwaangamize, mistari wa 45, BDB 1029, KB 1552, *Niphal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO, k.v. 4:25-26
 - b. maadui
 - 1) utawatumikia adui zako, mistari wa 48
 - 2) katika njaa (BDB 944)
 - 3) katika kiu (BDB 854)
 - 4) kwa uchi (BDB 735)
 - 5) kwa uhitaji wa vitu
 - 6) atakuvika kongwa la chuma
 - 7) mpaka uangamie (BDB 1029, KB 1552, *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO, kv. 4:25-26)

28:46 “milele” Tazama Mada Maalum katika 4:40.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 28:47-48

⁴⁷kwa kuwa hukumtumikia Bwana, Mungu wako, kwa furaha na moyo wa kushukuru, kwa ajili ya ule wingi wa vitu vyote; ⁴⁸kwa hiyo utawatumikia adui zako atakaowaleta Bwana juu yako, kwa njaa, na kwa kiu, na kwa uchi, na kwa uhitaji wa vitu vyote; naye atakuvika kongwa la chuma shingoni mwako, hata atakapokwisha kukuangamiza.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 28:49-57

⁴⁹Bwana atakuletea taifa juu yako kutoka mbali, kutoka ncha ya dunia, kama arukavyo tai; taifa usiloufahamu ulimi wake; ⁵⁰ taifa lenye uso mkali, ambalo haliangalii uso wa mzee, wala halipendelei kijana; ⁵¹ naye atakula uzao wa ng'ombe wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako mpaka utakapokwisha kuangamizwa; wala hatakuachia nafaka, wala divai, wala mafuta, wala maongeo ya ng'ombe wako, wala wana-kondoo wako, hata atakapokwisha kukuangamiza. ⁵² Naye atakuhusu katika malango yako yote, hata kuta zako ndefu, zenye maboma, ulizokuwa ukiziamini, zishuke, katika nchi yako yote kila upande; naye atakuhusu katika malango yako yote kila upande, katika nchi yako yote aliyokupa Bwana, Mungu wako. ⁵³ Nawe utakula uzao wa tumbo lako mwenyewe, nyama ya wana wako na binti zako aliokupa Bwana, Mungu wako; katika mazingirwa na katika mkazo utakaokazwa na adui zako. ⁵⁴ Mtu mume kati yenu aliye mwororo na laini sana, jicho lake litakuwa ovu juu ya nduguye, na juu ya mke wa kifuani mwake, na juu ya masalio ya wanawe waliosalia naye; ⁵⁵ hata asitake wao mmojawapo apewe katika nyama ya wanawe atakaowala, kwa kuwa hana kitu kilichomsalia kwake; katika mazingirwa na mkazo utakaokazwa na adui yako katika malango yako yote. ⁵⁶ Mwanamke kati yenu aliye mwororo na laini, ambaye hangehatirisha kuweka wayo wa mguu wake nchi kwa umalidadi na ulaini, jicho lake huyu litakuwa ovu juu ya mume wa kifuani mwake, na juu ya mwanawe, na juu ya binti yake, ⁵⁷ na juu ya mchanga wake atokaye katikati ya miguu yake, na juu ya wanawe atakaowazaa; kwa kuwa atawala kwa siri, kwa uhitaji wa vitu vyote; katika mazingirwa na mkazo utakaokazwa na adui yako katika malango yako.

28:49-57 Madhara ya ukaidi yanaendelea. Aya hii inaorodhesha matatizo yanayohusiana na kuzingirwa vitani huko Mashariki ya Karibu ya Kale:

1. Uvamizi ulioelezwa:
 - a. Uvamizi ulioletwa na YHWH, mstari wa 49
 - b. Taifa toka mbali, mstari wa 49
 - c. Taifa lenye nguvu ya kijeshi, mstari wa 49
 - d. Taifa usiolijua, mstari wa 49
 - e. Taifa lisilokuwa na heshima kwa wale lililowavamia, mstari wa 50
 - f. Taifa litakalochukua mazao yote pamoja na mifugo ya Israeli kwa ajili ya chakula, mstari wa 51
 - g. Taifa litakalozingira kila mji wa Israeli wenye maboma, mstari wa 52
2. Madhara kwa ajili ya Israeli:
 - a. Wataangamia kwa kukosa chakula, mstari wa 51
 - b. Israeli itakula uzao wa tumbo lake, mstari wa 53 (k.v. Law. 26:29) na kuwala kama chakula (k.v. mstari wa 57)
 - c. Wanaume na wanawake (BDB 940) laini watawaka tamaa za asili na kindugu na kugeuka kuwa waovu, mistari ya 54,56
 - d. Atawala wanae kwa siri kama chakula, mstari wa 57

28:49 “Bwana atakuletea taifa juu yako kutoka mbali” Hili linarejelea kwa Ashuru (k.v. Hos. 8:1) na/au Babeli (k.v. Yer. 5:15).

28:50 “ambalo haliangalii uso wa mzee, wala halipendelei kijana” Hasa wale Waashuru, lakini pia Wababeli, wangeliwauwa watu wenye umri mkubwa (kinyume na Law. 19:32) na wanawe kama namna ya kuwavunja moyo watu kabla ya kuondoka kwenda maeneo ya mbali na kukaa kwenye nyumba za watu wengine.

28:51 Katika mstari huu mataifa yenye kuvamia yanaelezwa kwa namna ya uharibifu wao wa mali wenye kufananishwa na nzige wale wa kwenye vitabu vya Yoeli, Amosi, na Mika.

28:52 “hata kuta zako ndefu, zenye maboma, ulizokuwa ukiziamini” Israeli wangeliondelea kuamini (BDB 105, KB 120, *Qal* KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA) katika maandalizi ya jeshi lao (k.v. II Nya. 32:7-8)!

28:53-57 “juu ya wanawe atakaowazaa; kwa kuwa atawala kwa siri” Hii inaonyesha hali ya hofu ya kuzingirwa (yaani., hali ya kuliwa nyama, k.v. Law. 26:29; II Fal. 6:24-30; Yer. 19:9; Omb. 2:20; 4:10; Ezek. 5:10).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 28:58-68

⁵⁸Kama hutaki kutunza kufanya maneno yote ya torati hii yaliyoandikwa katika kitabu hiki, upate kulicha jina hili la fahari na utisho, Bwana, MUNGU WAKO; ⁵⁹ndipo atakapofanya Bwana mapigo yako yawe ya ajabu, na mapigo ya uzao wako, mapigo makubwa kwa kweli, ya kudumu sana, na magonjwa mazito ya kudumu sana. ⁶⁰Naye atakurejezea maradhi yote ya Misri juu yako uliyokuwa ukiyaogopa, nayo yataambatana nawe. ⁶¹Tena kila ugonjwa, na kila pigo yasiyoandikwa katika kitabu cha torati hii, atakutia nayo Bwana juu yako, hata utakapokwisha kuangamizwa. ⁶²Nanyi mtasalia wachache kwa hesabu, ninyi mliokuwa mfano wa nyota za mbinguni kwa wingi; kwa kuwa hukuisikiza sauti ya Bwana, Mungu wako. ⁶³Tena itakuwa, kama vile alivyokuwa akifurahi Bwana juu yenu kwa kuwatendea mema na kuwafanya kuwa wengi, ndivyo atakavyofurahi Bwana juu yenu kwa kuwapoteza na kuwaangamiza; nanyi mtanyakuliwa katika hiyo nchi mwingiayo kuimiliki. ⁶⁴Bwana atakutawanya katika mataifa yote, tokea ncha hii ya dunia hata ncha hii ya dunia; nawe huko utatumikia miungu mingine usiyojua wewe wala baba zako, nayo ni miti na mawe. ⁶⁵Wala katika mataifa hayo hutapata raha iwayo yote, wala hutakuwa na kituo cha wayo wa mguu wako; lakini Bwana atakupa huko moyo wa kutetema, na macho ya kuzimia, na roho ya kudhoofika; ⁶⁶na uzima wako utakuwa na wasiwasi mbele yako; nawe utakuwa na woga usiku na mchana, wala hutaamini kamwe maisha yako; ⁶⁷asubuhi utasema, Laiti ingekuwa jioni! Na jioni utasema, Laiti ingekuwa asubuhi! Kwa kicho cha moyo wako utakavyokucha, na kuona kwa macho yako utakavyoona. ⁶⁸Bwana atakurudisha tena Misri kwa merikebu, kwa njia ambayo nilikuambia, Hutaiona tena po pote; nanyi huko mtajiiza nafsi zenu kwa adui zenu kuwa watumwa na wajakazi, wala hapana atakayewanunua.

28:58-68 “ikiwa. . .teana” Tazama masharti ya agano na madhara kwa sababu ya kutokutii:

1. “ikiwa”
 - a. “hutakuwa mwangalifu wa kuyatunza maneno ya sheria hii” (BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU na BDB 793, KB 889, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO)
 - b. “utaliheshimu jina la Bwana Mungu wako” (BDB 431, KB 432, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO, k.v. 4:10; 5:29; 6:2,13,24; 10:12,20; 13:4; 14:23; 17:19; 28:58; 31:12,13)
 - c. Tazama mistari ya 1,13,15,58; 29:9; 31:12; 32:46. Utii ni wa lazima!
2. “hivyo”
 - a. YHWH ataleta juu yenu tauni, mstari wa 59
 - 1) Isiyo na mfano (BDB 810, KB 927, *Hiphil* KAULI TIMILIFU)
 - 2) kubwa (BDB 152)
 - 3) ya kudumu (BDB 52, KB 63, *Niphal* KAULI TIMILIFU)
 - 4) mateso, (BDB 948)
 - 5) ya kudumu (BDB 52, KB 63, *Niphal* KAULI TIMILIFU)
 - b. YHWH atayarudisha mapigo (BDB 188, k.v. 7:15), ambayo Israeli ilikuwa ikiyaogopa (BDB 388, KB 386, *Qal* KAULI TIMILIFU), ya Misri (BDB 179, KB 209, *Qal* KAULI TIMILIFU) kuwajilia juu yao, mstari wa 60
 - c. YHWH atawaletea kila magonjwa (BDB 315) na kila pigo (BDB 646, k.v. Law. 26:21) ambayo hayakutajwa katika kitabu cha sheria, mstari wa 61
 - d. YHWH atageuza ahadi Zake za mafanikio na wingi wa mali, mistari ya 62-63
 - e. YHWH atageuza safari ya kutoka Misri kwenda nchi ya ahadi na kuwatawanyisha (BDB 806, KB 918, *Hiphil* KAULI TIMILIFU) watu Wake wa Agano, mstari wa 64
 - 1) Kuitumikia miungu wengine, mstari wa 64
 - 2) Hutapata raha, mstari wa 65
 - 3) Moyo wa kutetemeka, mstari wa 65
 - 4) Macho ya kuzimia, mstari wa 65
 - 5) Roho ya kudhoofika, mstari wa 65

- 6) nawe utakuwa na woga usiku na mchana, mistari ya 66,67
- 7) wala hutaamini kamwe maisha yako, mistari wa 66 (tazama Mada Maalum katika 1:32)
- 8) watumwa, mistari wa 68

28:58

NASB “ jina hili la fahari na utisho”

NKJV, NRSV “jina la utukufu na utiisho”

TEV “jina la ajabu na utiisho”

NJB “jina la utukufu na utiisho wenye kuvuviwa”

“jina” linasimama kwa ajili ya mtu na tabia za YHWH (mf. Ayubu 1:21; Isa. 48:9-11; Ezek. 20:44; Amosi 2:7).
Linaelezewa na *Niphal* KAULI ENDELEVI mbili:

1. BDB 457, KB 455, kutoka kwenye KITENZI, “kuwa na uzito,” kikitumika kiistiari kwa ajili heshima au utukufu (k.v. Isa. 26:15; 66:5; Ezek. 28:22; 39:13)
2. BDB 431, KB 432, toka KITENZI, “kuhofu,” kikitumika katika maana ya utiisho wa YHWH na matendo Yake ya ukombozi (mf., 7:21; 10:17,21; Neh. 1:5; 4:14; 9:32; Zab. 145:6)

28:61 “na kila pigo yasiyoandikwa katika kitabu cha torati hii” Haijulikani ikiwa hili linarejelea:

1. Torati yote
2. Sheria za kuondoka - Hesabu
3. Kumbukumbu la Torati lote (k.v. 31:24)
4. sehemu ya Kumbukumbu la Torati
 - a. mifumo ya sheria
 - b. laana na baraka ya kwenye “kitabu” ikimaanisha gombo, lakini hili halidai kuwa Musa alikiandika kitabu au kumbukumbu la sheria ya YHWH kumzungumzia Yeye (k.v. 27:3,8; 28:58; 29:21,29; 30:10).

28:62 “wachache kwa hesabu” Hii ni kinyume cha ahadi ya Ibrahimu. Mungu aliahidi kuwa watakuwa (1) kama “nyota za mbinguni (k.v. Mwa. 15:5; 22:17; 26:4); (2) kama “mchanga” (k.v. Mwa. 22:17; 32:12); na (3) kama “mavumbi ya nchi” (k.v. Mwa. 13:16; 28:14; Hes. 23:10).

28:63 “akifurahi Bwana juu yenu” KITENZI hiki (BDB 965, KB 1314) kimetumika kwa namna mbili:

1. kubariki (*Qal* KAULI TIMILIFU, k.v. 30:9)
 - a. kuwatendea mema (BDB 405, KB 408, *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO)
 - b. kuwafanya kuwa wengi (BDB 915 I, KB 1176, *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO)
2. kulaani (*Qal* KAULI ISIO TIMILIFU)
 - a. atawapoteza (BDB 1, KB 2, *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO)
 - b. atawaangamiza (BDB 1029, KB 1552, *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO)
 - c. mtanyakuliwa katika hiyo nchi (BDB 650, KB 702, *Niphal* KITENZI TIMILIFU)

YHWH hufanya kuwapa na kuwaadabisha wana wake. Tendo la kuwaadabisha ni kwa makusudi ya urejesho na ujumuisho.

☐ **“nanyi mtanyakuliwa katika hiyo nchi”** KITENZI (BDB 650, KB 702, *Niphal* KITENZI TIMILIFU) mara nyingi kinatumika kuhusu hukumu ya YHWH (k.v. Zab. 52:5; Mith. 15:25). Huu ulikuwa ni urejesho kamili wa ahadi za Ibrahimu (k.v. Mwa. 12:1-3).

28:64 “Bwana atakutawanya katika mataifa yote” Hili linarejelea na suala la kwenda uhamishoni (k.v. mistari wa 68.)

☐ **“nayo ni miti na mawe”** Hii (BDB 629 I) ilikuwa ikitumika mara mbili kwa ajili ya habari ya Mwanzo 8 kipindi cha gharika ya Nuhu:

1. Safina ilituama juu ya Mlima Ararati, mistari wa 4
2. Hua aliyetumwa kuangalia sehemu ya ardhi kavu lakini hakupata sehemu ya kutua, mistari wa 9

YHWH anawahitaji watu wake kuwa na sehemu ya kupumzika (yaani., nchi ya ahadi, k.v. 3:20; 12:9-10; 25:19; Yoh. 1:13,15; 21:44), lakini mapenzi yao ya kulikaidi agano liliwarejesha utumwani (yaani., kwenda uhamishoni, k.v. Zab. 95:11).

28:65 “na macho ya kuzimia” Sura hii inataja kupoteza uwezo wa kuona mara kadhaa:

1. Upofu kama hukumu ya YHWH kwa kulikaidi agano, mistari ya 28-29
2. Hukumu kuonekana mbele ya macho yao, mistari ya 30-33
3. Kile ukionacho kitakutia wazimu, mistari wa 34
4. Stiari kwa ajili ya vurugu za kupangwa dhidi ya mmojawapo wa nduguye (yaani., “jicho litakuwa ovu juu ya”), mistari ya 54-56
5. Mapigo ya Misri, mojawapo litakuwa ni giza totoro, mistari ya 60-61
6. “macho ya kuzimia,” stiari kwa ajili ya hofu na kukata tamaa, kutokuwa na tumaini kabisa, mistari ya 65-66
7. Macho yenye kusababisha uwoga zaidi, mistari wa 67

28:66-67

NASB, NRSV “uwoga”

NKJV “hofu”

TEV “hofu kuu. . .wasiwasi”

NJB “uwoga. . .hofu kuu”

JPSOA “hofu kuu. . .uwoga”

Neno hili (BDB 808 l) linamaanisha “kujawa hofu,” au “kutetemeka,” kunakosababishwa na hofu na furaha! Hapa inaonekana kuwa ni hofu (mf., Isa. 33:14). YHWH alihitaji kusababisha “uwoga” kwa maadui wa Israeli (k.v. 2:25; 11:25), lakini kwa sababu ya ukaidi wao, waligeuka kuwa wenye hofu!

28:68 “Bwana atakurudisha tena Misri” Urejesho wa kuondoka Misri. Kutekwa tena kwa Israeli!

☐ **“kwa njia ambayo nilikuambia ”** Hii nukuu ya maelezo ya YHWH haijulikani.

☐ **“wala hapana atakayewanunua”** KITENZI cha neno “kununua” (BDB 888, KB 1111, *Qal* KAULI TENDAJI YA HALI YA KUENDELEA) mara nyingi kilitumiwa na YHWH kwa ajili ya kuinunua Israeli toka utumwani mwa Misri (k.v. Kut. 15:16; Zab. 74:2), lakini hapa kinatumika juu ya mateso ya Israeli ambapo hata Misri yenyewe isingaliwanunua tena kuwarudisha utumwani. Hakika walikataliwa na Mungu.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini kipengere cha laana ni kirefu kuliko kile cha baraka?
2. Nini kusudi la sura hii?
3. Ni kwa vipi kazi za haki zenye kuhusiana na baraka zimeunganishwa hapa?
4. Ni kwa nini hukumu ya Mungu ni kali mno?

KUMBUKUMBU LA TORATI 29

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFASIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Agano linafanywa upya Huko Moabu	Hotuba ya tatu ya Musa	Agano la Bwana na Israeli huko Moabu	Hotuba ya mara ya tatu
29:1	29:1	29:1	29:1-3
29:2-9	29:2-9	29:2-9	29:4-5 29:6-7 29:8 Agano la huko Moabu 29:9-14
29:10-13 29:14-29	29:10-29	29:10-15	29:15-16
		29:16-21	29:17-20 Tishio la kwenda Uhamishoni 29:21-23
		29:22-28	29:24-28
		29:29	[usomaji aya wa toleo la MT]

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 29:1

¹Haya ndiyo maneno ya agano Bwana alilomwamuru Musa alifanye na wana wa Israeli katika nchi ya Moabu, pamoja na agano alilofanya nao Horebu.

29:1 “Haya ndiyo maneno ya agano Bwana alilomwamuru Musa” Hii ni hotuba ya tatu ya Musa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (sura za 29-30). Anatumkumbusha sisi kuwa sheria hizi ni kutoka kwa YHWH, na sio yeye mwenyewe.

☐ **“pamoja na agano”** Hili linarejelea kwenye agano katika Mlima Sinai/Horebu (tazama Mada Maalum katika 1:2, k.v. 5:2 na kuendelea; Kutoka 19-24) na juu ya nyanda za Moabu (k.v. 1:5; 5:1,3,5-26). Hili limeelezwa kinagaubaga katika kitabu cha Kutoka 20-31. Lilifanywa upya katika kitabu cha Kutoka 34; Kumbukumbu la Torati 29-30; na Yohana 24. Kwa ajili ya neno “Agano” tazama Mada Maalum katika 4:13.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):29:2-9

²Musa akawaita Israeli wote akawaambia, Mmeyaona yote Bwana aliyomfanya Farao katika nchi ya Misri mbele ya macho yenu, yeye na watumwa wake wote, na nchi yake yote; ³yale majaribu makuu yaliyoyaona macho yako; hizo ishara, na ile miujiza makuu; ⁴lakini Bwana hakuwapa moyo wa kujua, wala macho ya kuona, wala masikio ya kusikia, hata leo hivi. ⁵Nami miaka arobaini nimewaongoza jangwani; nguo zenu hazikuchakaa juu yenu, wala kiatu chako hakikuchakaa katika mguu wako. ⁶Hamkula mkate, wala hamkunywa divai, wala kileo; ili mpate kujua kwamba Mimi ndimi Bwana, Mungu wenu. ⁷Nanyi mlipokuja mahali hapa, walitutokea kupigana juu yetu Sihoni mfalme wa Heshboni, na Ogu mfalme wa Bashani, tukawapiga; ⁸tukaitwaa nchi yao, nayo tukawapa Wareubeni, na Wagadi, na nusu ya kabila ya Manase, iwe urithi. ⁹Shikeni basi maneno ya agano hili myafanye, ili mfanikiwe katika yote mfanyayo.

29:2 “Israeli wote ” Hili mara nyingi linarejelea kwa wazee tu, lakini kwa sababu ya mistari ya 1-13, linaonekana kurejelea taifa lote. Kwa ajili ya neno “Israeli” tazama Mada Maalum katika 1:1.

29:2-3 “Mmeyaona . . . yaliyoyaona macho yako” Haya ni maelezo ya hotuba (k.v. 4:34; 7:19) kwa sababu hawa watu walikuwa ni wana wa wale waliokwisha kuyaona (k.v. Hes. 14:29). Mistari ya 2-8 inaunda tafakuri za kihistoria kama zilivyo sura za 1-4, ambacho kilikuwa ni kipengere cha kawaida kwenye mikataba ya huko Mashariki ya Karibu.

☐ **“ishara, na ile miujiza ”** Maneno haya “ishara” (BDB 16) na “miujiza” (BDB 68) yametajwa mara kwa mara katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (k.v. 4:34; 6:22; 7:19; 11:3; 26:8; 29:2; 34:11) kusaidia kizazi kilichopo cha Israeli kuyakumbuka matendo ya nguvu na neema ya YHWH ya ukombozi na utoaji (k.v. mistari 5-7) wakati wa safari ya kutoka Misri na kipindi cha kutangatanga jangwani.

29:4 “hata leo hivi ” Upofu wa Israeli kuelekea mahali pao maalum katika mpango wa ukombozi wa milele wa YHWH halikuwa tu tatizo la zamani (yaani., mstari 4), bali pia ni tatizo lililopo sasa (k.v. Mt. 13:14-17; Marko 4:10-12; Luka 8:9-10; Yohana 12:36b-43; Mdo. 28:26-27; na hasa Rum. 11:25-32). Injili imeelezwa kama mpango wa Mungu ulioamriwa kabla na kujulikana kabla (k.v. Mdo. 2:23; pia angalia 3:18; 4:28; 13:29). Tazama Mada Maalum: Mapendeleo ya Bob ya Kiinjilisti katika 4:6.

☐ **“Bwana hakuwapa moyo wa kujua, wala macho ya kuona, wala masikio ya kusikia”** Waisraeli wa kipindi cha kutoka Misri na kipindi cha kutangatanga jangwani waliuona mwili, lakini hawakuweza kutambua ukubwa wa kiroho wa matendo ya YHWH (yaani., walikuwa ni watu maalum wa agano ambao walikuwa ni sehemu ya mpango wa ukombozi wa milele). kifungu hiki kikajakuwa ni stiaji kwa ajili ya upofu na ugumu wa kiroho (k.v. Isa. 6:9-10; Mdo. 28:26-27; Rum. 11:8). Kuna mchezo wa maneno hapa kati ya mstari wa 2, “mmeyaona” na mstari wa 4, ambapo unasema pasipo kuwa na macho ya kuona! Hili laweza kurejelea kwenye ukaidi wa Israeli ulitajwa katika 9:7-24. Pasipo imani Mungu hawezi onekana katika historia, bali ukiwa na imani historia inakuwa ni kumbukumbu ya njia ya Mungu. Inagharimu kuwa na karama (yaani., “uliopewa,” BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU) ya neema ya YHWH kwa ajili ya mwanadamu aliyanguka kuhisi na kuelewa uwepo wake!

29:5 “nguo zenu hazikuchakaa. . . wala kiatu chako hakikuchakaa” Rashi anasema nguo na viatu viliendelea kukua kwa kadri watoto walivyokua (k.v. 8:4; Neh. 9:21).

29:6 Mistari ya 5 na 6 inaonyesha uangalizi wa Mungu wenye tija wakati wa kipindi kizima cha hukumu kijulikancho kama kipindi cha kutangatanga jangwani (k.v. 8:2-3). Waisareli walitakiwa kuendeleza mahusiano yao kwa kujitazamisha kwa YHWH (si chakula wala kinywaji kilichozalishwa kwa mikono ya mwanadamu, bali kwa utoaji Wake). Lakini mistari hii pia zinaonyesha upofu endelevu wa kiroho wa watu wa Mungu (k.v. Isa. 6:9-10).

29:7 Hili linaonyesha uwepo wa kijeshi wa YHWH kwa niaba ta Israeli (k.v. Hes. 21:21-24, 33-35; na Kumb. 2:26-3:17).

29:8 Haya ni makabila yaliyokaa upande wa mashariki mwa Yordani (k.v. 3:12-13; Hes. 32:28-32).

29:9 “Shikeni basi maneno. . . myafanye” Hali ya kiasili ya agano (yaani., “shikeni,” BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI TIMILIFU na “myafanye,” BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI TIMILIFU) ni lenyekujirudia katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati (k.v. 4:2,6,9,15,23,40; 5:1,10,12,29,32; 6:2,3,12,17,25; 7:9,11,12; 8:1,2,6,11; 10:13; 11:1,8,16,22,32; 12:1,28,32; 15:5; 16:12; 17:19; 19:9; 24:8; 26:16,17,18; 27:1; 28:1,9,13,15,45,58; 29:9; 30:10,16; 31:12; 32:46). Utii ni hatua ya kiroho yenye kuonekana ya Israeli iliyo aminifu. Kumpenda YHWH ni kumtii YHWH! Huu mstari baadaye ulisomwa na walimu wa Kiyahudi wakati baadhi ya watu walipopigwa fimbo wazi (k.v. 25:3). Unajumuisha maneno 13 yanayoendana na kupigwa fimbo mara 13. Zaburi 78:38 pia nao ulisomwa.

■ **“ili mfanikiwe katika yote mfanyayo”** KITENZI (BDB 968, KB 1328, *Hiphil* KISICHO TIMILIFU) mara nyingi kinamaanisha “wenye busara” au “waangalifu,” lakini katika shina la kitenzi *Hiphil* chaweza kumaanisha “kufanikiwa,” “kuwa na mafanikio” (k.v. Yosh. 1:7-8; I Sam. 18:5,14,15; I Fal. 2:3; II Fal. 18:7; I Nya. 22:13). Tambua kuwa mafanikio na ustawi ni sehemu ya utii!

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 29:10-13

¹⁰ Leo mmesimama nyote mbele za Bwana, Mungu wenu; wakuu wenu, na kabila zenu, na wazee wenu, na maakida wenu, waume wote wa Israeli, 11 vijana vyenu, na wake wenu, na mgeni wako aliye kati ya kituo chako, tokea mchanjaji wa kuni zako hata mtekaji wa maji yako; 12 ili uingie katika agano la Bwana, Mungu wako, na kiapo chake, afanyacho nawe Bwana, Mungu wako, hivi leo; 13 apate kukuweka leo uwe taifa kwake naye apate kuwa Mungu kwako, kama alivyokuambia, na kama alivyowaapia baba zako, Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo.

29:10 “Mmesimama” Tazama makundi tofauti ya jamii ya Israeli yaliyotajwa katika mistari ya 10-11:

1. Wakuu wenu, BDB
2. Kabila zenu, BDB 986
3. Wazee wenu, BDB 278
4. Maakida wenu, BDB 1009, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU
5. Wanaume wote wa Israeli, BDB 481, 35, 975 (ni kama #2)
6. Vijana, BDB 381
7. wake, BDB 61
8. wageni, BDB 158
9. watumwa, walioelezewa kwa kazi zao

Makundi yote haya tofauti yalitakiwa kuonyesha utii wao kwenye agano (k.v. mistari 14-15). Hii ni sherehe ya ufanywaji upya rasmi wa agano! Idadi ya makundi yaliyotajwa yanatofautiana toka tafasiri moja hadi nyingine. Baadhi ya tafasiri (REB) zinadhani kuwa #1 na 2 inapaswa kuwekwa pamoja (yaani., KJV, “wakuu wa kabila zenu,” JPSOA, “wazee wenu”). Matoleo ya ASV, NASB, NIB yote yana #1-4.

29:12-13 Hili ni andiko jipya la agano. Tazama namna neno “agano” (BDB 136) na “kiapo” (BDB 46) vinavyofanana. Taratibu za YHWH zimehusishwa kwenye ahadi Zake! YHWH anataka kuzitimizwa ahadi zote zilizofanyika kwa

mababa wa imani katika kitabu cha Mwanzo kwa kuwaimarisha watu (k.v. 28:9), mtu Yule anayefunua tabia Zake!

29:12

NASB, NKJV,

NRSV, TEV “ili uingie katika agano”

NJB “na ukaribie kuliingia agano”

KITENZI CHA MANENO (BDB 716, KB 778, *Qal* KITENZIJIINA CHA MUUNDO WA MANENO) kiuhalisia kinamaanisha “kutozingatia.” Lakini hapa limetumika kwa maana ya kuingia kwenye agano. Yumkini kinahusiana na wazo la “kupita kati ya” agano kwa kupita katikati ya vipande viwili vya mnyama aliyetolewa kama dhabihu kama ilivyo katika kitabu cha . 15:17-18. Wazo ni kuwa mabaya yote ya mnyama yaende juu ya Yule aliyefanya agano ikiwa atakiuka masharti yaliyowekwa.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 29:14-21

¹⁴Wala sifanyi na ninyi peke yenu agano hili na kiapo hiki; ¹⁵ila na yeye aliyesimama hapa nasi hivi leo mbele ya Bwana, Mungu wetu, na yeye naye asiye kuwapo pamoja nasi leo; ¹⁶(kwani mwajua mlivyoketi nchi ya Misri, na tulivyo kuja katikati ya mataifa hayo mliyopita katikati yao; ¹⁷nanyi mliona machukizo yao, na sanamu zao, miti na mawe, fedha na dhahabu, zilizokuwako kwao;) ¹⁸asiwe mtu katikati yenu, mume wala mke, wala jamaa, wala kabila, ageukaye moyo wake leo amwache Bwana, Mungu wetu, kwenda kuitumikia miungu ya mataifa hayo; lisiwe katikati yenu shina lizaalo uchungu na pakanga; ¹⁹ikawa asikiapo maneno ya laana hii, ajibarikie mtu huyo moyoni mwake, na kusema, Nitakuwa katika amani, nijapotembea katika upotoe wa moyo wangu kwa kuangamiza mbichi na kavu; ²⁰Bwana hatamsamehe mtu huyo, lakini wakati huo hasira ya Bwana na wivu wake vitafuka moshi juu ya mtu yule, na laana yote iliyoandikwa katika kitabu hiki itamkalia juu yake, na Bwana atalifuta jina lake chini ya mbingu. ²¹Bwana atamtenga kwa uovu, kutoka kabila zote za Israeli, kwa laana zote za agano lililoandikwa katika chuo hiki cha torati.

29:15 “na yeye naye asiye kuwapo pamoja nasi leo” Hili linarejelea kwa kizazi kijacho (k.v. mistari. 22,29; 5:3-5; 12:25,28).

29:16-17 Mistari hii inaunda muhtasari wa nyongeza kuhusu mataifa ya kipagani yaliyokabiliana na Israeli wakati wakikimbilia nchi ya ahadi.

☐ **“machukizo yao”** Tazama Mada Maalum: Machukizo katika 14:3.

29:18 Maonyo dhidi ya kutolitii agano (hasa ibada ya sanamu) ni wazi limeondolewa kwa kila mwanajamii na kundi a kijamii katika Israeli yote (yaani., watu binafsi, familia, makabila).

☐ **“lisiwe katikati yenu shina lizaalo uchungu na pakanga”** Kifungu hiki kinafanana na kile “ambao mioyo yao ilipogeukia mbali” (BDB 815, KB 937, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU). Uchungu ni ukaidi na madhara yake ni makali!

1. YHWH kamwe hatawasamehe (mstari 20, kanushi *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 2, KB 3) na *Qal* KITENZIJIINA CHA MUUNDO WA MANENO (BDB 699, KB 757).
2. Hasira na wivu wa YHWH utakuwa juu yao (mstari 20, BDB 798, KB 896, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU).
3. Kila laana itakuwa juu yao (mstari 20, BDB 918, KB 1181, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU). KITENZI kile kile kinaieleza dhambi kama mnyama aliyejikunyata kwenye kitabu cha Mwa. 4:7.
4. YHWH ataliondoa jina lake chini ya mbingu (mstari 20, BDB 562, KB 567, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU).
5. YHWH atamtenga katika uovu (mstari 21, BDB 95, KB 110, *Hiphil* KAULI ILIYO TIMILIFU).

29:19 “ajibarikie mtu huyo moyoni mwake, na kusema, Nitakuwa katika amani, nijapotembea katika upotoe wa moyo ” Hii ni tabia inayojirudia ya wenye dhambi wenye kuchukulia utulivu wa Mungu kama msamaha wa kuendelea kuasi. Hukumu ya Mungu, ingawa mara nyingi inaonekana kuchelewa, itamwita kila mkaidi mwenye kulivunja agano kutoa hesabu yake (yaani., tunavuna kile tulicho panda, k.v. Ayu. 34:11; Zab. 28:4; 62:12; Mith.

29:12; Mhu. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 14:12; I Kor. 3:8; II Kor. 5:10; Gal. 6:7-10; II Tim. 4:14; I Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12).



NASB “kuangamiza eneo bichi na kavu”
NKJV “kama mlevi atakavyojumuishwa na asiye kunywa”
NRSV “(kwa kuleta madhara kwenye mbichi na kavu)”
TEV “kwa kuwaangamizeni ninyi nyote, wema na wabaya”
NJB “kwa maji mengi kukiondoa kiu”
JPSOA “kwa kuangamiza mbichi na kavu”
NET Bible “Hili litaangamiza eneo bichi na kavu”

Hii ni mithali ambayo maana yake haijulikani, lakini muktadha unahitaji nahau ya maangamizo. Kwa sababu kaidi mmoja mwenye kulivunja agano la YHWH Israeli nzima iliumia. Leo hii tungesema, “chachu kidogo huchachua kapu lote” au “samaki mmoja akioza wote wameoza.”

29:20 “Bwana hatamsamehe mtu huyo” Kutia kwingi chumvi lazima kuendane dhidi ya matakwa ya nyuma ya YHWH ya kusamehe na kumkubali mwamini mmoja mwenye kutubu. Baadhi ya walimu wa Biblia wanaanisha huu mstari na ule wa Zab. 103:9 na kudai kuwa kuna ukomo au upenyu kwenye neema ya YHWH. Sikubaliani na hili la Zab. 103:9 katika muktadha (yaani., mistari ya 8-14) inayoonyesha atasamehe! Tatizo sio msamaha wa Mungu, bali ni dhambi endelevu ya mwanadamu mkaidi, aliyeanguka! Mahusiano yamevunjika toka upande wa mwanadamu na yamebaki kuvunjika toka upande wa mwanadamu. Masuala ya kutokuamini na kuasi katika uharibifu, yote ni ya muda na milele!

☐ **“wivu”** Neno hili (BDB 888) linatokana na kitu fulani kilichonakshiwa sana kwa rangi nyekundu (yaani., pale hasira inaposababisha damu kumwagika usoni). Hisia za mwanadamu zinatumiwa kuzielezea hisia za YHWH (nadharia ya lugha ya binadamu kumwelezea Mungu). Ana moyo kwa ajili ya watu wake (kv. Isa. 26:11). Moyo huu waweza kugeuka na kuwa wivu (k.v. Ezek. 5:13; 16:38,42; 23:25; 36:5,6; 38:19; Zef. 1:18; 3:8).

☐ **“atalifuta jina lake chini ya mbingu”** Nahau hii inamaanisha (1) hapana mtoto au (2) kifo (k.v. Mwa. 7:4; Kut. 17:14; 32:32; Kumb. 9:14; II Fal. 14:27; Zab. 9:5-6).

29:21 “laana zote za agano” Tazama mistari ya 27-28; 27:15-26; 28:15-19,20-26,27-37,38-48,49-57

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 29:22-28

²² Na kizazi cha baadaye, wanenu watakaoinuka baada yenu, na mgeni atakayekuja kutoka nchi ya mbali, watasema, watakapoyaona mapigo ya nchi ile, na magonjwa aliyoitia Bwana; ²³ ya kuwa nchi yake nzima ni kibiriti, na chumvi, na kuteketea, haipandwi, wala haizai, wala nyasi hazimei humo, kama mapinduko ya Sodom na Gomora, Adma na Seboimu, aliyoipindua Bwana kwa ghadhabu yake na hasira zake; ²⁴ mataifa yote watasema, Mbona Bwana ameifanyia hivi nchi hii? Ni nini maana yake hari ya hasira hizi kubwa? ²⁵ Ndipo watakaposema watu, Ni kwa kuwa waliacha agano la Bwana, Mungu wa baba zao, alilofanya nao hapo alipowatoa katika nchi ya Misri; ²⁶ wakaenda wakatumiwa miungu mingine, wakaiabudu miungu wasiyojua, asiyowapa yeye; ²⁷ ndipo ikawashwa hasira ya Bwana juu ya nchi hii, kwa kuleta juu yake laana yote iliyoandikwa katika kitabu hiki; ²⁸ Bwana akawang'oa katika nchi yao kwa hasira, na ghadhabu, na makamio makuu, akawatupa waende nchi nyingine, kama hivi leo.

29:22-23 Baraka za YHWH, zilizomaanisha kuwavuta wale wote wasio mjua, zitageuka na kuwa maswali ya dhihaka kwa wageni:

1. Mapigo ya nchi, mstari wa 22
2. magonjwa, mstari wa 22
3. nchi nzima kibiriti, mstari wa 23
4. nchi nzima kuwa chumvi, mstari wa 23

5. nchi nzima kuteketea, mstari wa 23
6. nchi haipandwi, wala haime, mstari wa 23
7. nchi haime, mstari wa 23
8. nchi haime nyasi, mstari wa 23
9. nchi kama mapinduko ya miji (k.v. Mwa. 19:24)

Haya yote ni YHWH aliyatuma (k.v. mstari ya 22-28).

29:22 “Na kizazi cha baadaye . . . kitasema” Huu muundo wa kifasihi (yaani., watoto kuuliza maswali) ulionekana mapema katika 6:20, ambao unafunua kitabu cha Kut. 13:8,14; 10:2; 12:26,27. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati kinazungumza juu ya kuwafundisha watoto (mf., 4:10; 6:7).

29:23 “nchi yake nzima ni kibiriti, na chumvi” Nchi itakuwa kama eneo la Bahari ya Chumvi, ambalo lilikuwa ni eneo la miji ya Sodom na Gomora (k.v. Mwa. 19:24-26).

29:24 “mataifa yote watasema” Israeli ilikuwa ni alama ya mataifa yote kuhusiana na YHWH. Iliamaanisha kuwa ni alama ya baraka lakini hata kama kuna hukumu juu yake, bado itabaki kuwa alama!

29:25 “Ni kwa kuwa waliacha agano la Bwana” Hii ilikuwa na imebaki kuwa sababu ya msingi kwa ajili ya laana za Kimungu (k.v. II Fal. 17:9-23; II Nya. 36:13-21).

29:26 “miungu. . . miungu” Kiuhalisia hili ni *Elohim*. Neno liko katika hali ya uwingi. Mara nyingi linatafasiriwa “Mungu.” Pia laweza kurejelea kwenye viumbe vya kimalaika na waamuzi. Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.



NASB, NRSV,

JPSOA “Asiyoichagua Yeye”

NKJV “Asiyowapa Yeye”

NJB “isiyo sehemu ya urithi wao toka Kwake”

katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania ya 32:8 ya neno “*Elohim*” (yaani., “kuhusiana na idadi ya malaika wa Mungu”) linaonekana kurejelea kwenye malaika wa kitaifa, kama ilivyo hapa (k.v. Isa. 24:21; Dan. 10:13,20).

29:27 “ndipo ikawashwa hasira ya Bwana juu ya nchi” Nchi inaathiriwa na dhambi za Israeli (k.v. Mwa. 3:17) na dhambi za wanadamu kwa pamoja (k.v. Rum. 8:18-22). Mungu anatumia tabia za kiasili kuyaeleza tena mawazo ya mwanadamu na vipaumbele.

29:28 “Bwana akawang'oa” KITENZI hiki (BDB 684, KB 737, *Qal* KISICHO TIMILIFU, k.v. I Fal. 14:15; II Nya. 7:20; Yer. 12:14) ni kinyume cha neno “yaliyopandwa”! Agano limekwisha kubadilishwa! Tazama namna matendo ya YHWH yalivyoelezewa:

1. katika hasira - BDB 60 I
2. katika ghadhabu - BDB 404
3. katika makamio makuu - BDB 893 and 152
4. akawatupa waende nchi nyingine (yaani., kukimbilia uhamishoni, BDB 1020, KB 1527, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU)

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 29:29

²⁹Mambo ya siri ni ya Bwana, Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele, ili tuyafanye maneno yote ya sheria hii.

29:29 “Mambo ya siri ni ya Bwana” Hili linarejelea (1) makao ya mwanadamu (k.v. mstari wa 19- 20; (2) maarifa kamili ya Mungu; au (3) mipango Yake ya baadaye.

☐ **“lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi”** Wanadamu wanawajibika kwa ajili ya nuru walio nayo. Kama hawana mawasiliano na Biblia au injili, wanawajibika kwa ajili ya ufunuo kiasili (k.v. Zab. 19:1-6; Warumi 1) na asili adilifu ya ndani (k.v. Warumi 2). Kama watajiweka wazi kwenye maandiko, wanawajibika kwa ajili ya yaliyomo! Waamini wanaweza kuufahamu ukweli na wakawajibika kwa ajili ya ukweli huo!

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mungu mara nyingi aliruhusu ufanyaji upya wa agano (mstari wa 1)?
2. Kwa nini Mungu aliyapofusha macho ya Wayahudi kwenye kusudi lake (mistari ya 4-6)?
3. Je Mungu kamwe hapendi kumsamehe mtu (mstari wa 20)?
4. Ni kwa nini nchi iteseke kwa ajili ya dhambi za mwanadamu (mstari wa 27)?
5. Ni kipi mstari wa 29 unakirejelea?

KUMBUKUMBU LA TORATI 30

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Baraka za kumrudia Mungu	Mahubiri ya tatu ya Musa (29:1-30:20)	Masharti kwa ajili ya Urejesho na Baraka	Kurudi kutoka Uhamishoni na Kuongoka
30:1-10	30:1-5	30:1-10	30:1-5
Uchaguzi wa uzima na Mauti	30:6-10		30:6-10
30:11-14	30:11-14	30:11-14	30:11-14
30:15-20	30:15-20	30:15-20	Njia mbili 30:15-20

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi) *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (mzunguko wa tatu wa usomaji #3, ukur. viii). Linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya ya tatu
12. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 30:1-5

¹Tena itakuwa, mambo haya yote yatakapokujilia, baraka na laana nilizoweka mbele yako, nawe utakapozikumbuka kati ya mataifa yote, huko atakakoupeleka Bwana, Mungu wako, ²nawe utakapomrudia Bwana, Mungu wako, na kuitii sauti yake, mfano wa yote nikuagizayo leo, wewe na wanao, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote; ³ndipo Bwana, Mungu wako, atakapougeuza utumwa wako, naye atakuhurumia, tena atarejea na kukukusanya kutoka mataifa yote, huko alikokutawanyia Bwana, Mungu wako. ⁴Watu wako waliotawanyika wakiwako katika ncha za mbingu za mwisho, kutoka huko atakukusanya Bwana, Mungu wako; kutoka huko atakutwaa; ⁵atakuleta Bwana, Mungu wako, uingie nchi waliyomiliki baba zako, nawe utaimiliki; naye atakutendea mema, na kukufanya uwe watu wengi kuliko baba zako.

30:1 “Tena itakuwa, mambo haya yote yatakapokujilia” Ubaadaye wa Israeli utakuwa moja ya uhalisia uliojikita katika utii wao wa agano. YHWH anatamani “baraka,” lakini uchaguzi wao utaamua uhalisia wa namna gani (yaani, baraka au laana) utakaoachiliwa. Hakuna namna nyingine!

☐ **“Baraka na laana”**Hii inajulikana katika fasihi za hekima kama “njia mbili.” Hizi zinatajwa na kuelezwa katika sura za 27 na 28.

☐ **“Nimekuwekea”** KITENZI hiki (BDB 678, KB 723, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile mistari ya 15,19 na tazama 11:26) ni stiari ya hitaji la Israeli kuchagua moja ya matokeo mawili yanayohusiana na Agano Lake.

☐ **“nawe utakapozikumbuka”** Hii ni nahau “kuwasababisha kurudisha mioyo” (BDB 996, KB 1427, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile 4:39; I Wafalme 8:47; Isa. 44:19; 46:8).

☐ **“kati ya mataifa yote, huko atakakokupeleka Bwana”** Huu ni unabii uliotabiriwa wa uchaguzi wa Israeli ambao ungesababisha kwenda uhamishoni. Tambua kuwa YHWH alifanya hivi kwa sababu ya Israeli kwendeleakulivunja agano na kuiga matendo ya Wakanaani.

30:2 “utakapomrudia” KITENZI hiki hiki (BDB 996, KB 1427, *Qal* kauli ya wakati timilifu) kilitumika katika mstari wa1 (*Hiphil* kauli ya wakati timilifu) kurejelea kuonywa kwa Israeli juu ya agano la YHWH. Hapa kinatumika kwa namna ya toba.

MADA MAALUM: TOBA (AGANO LA KALE)

Dhana hii ni ya muhimu sana lakini ni vigumu kuitolea ufafanuzi. Wengi wetu tunao ufafanuzi ambao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu “mwelekeo” wa ufafanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) amabayo kwa upekee wake hayamaanishi “elekea” ufafanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba waandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania waliotumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenyewe ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.

1. *nacham* (BDB 636, KB 688)
2. *shub* (BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha “kueleza pumzi ya ndani” linatumika katika maana kadhaa.

- a. “kupumzika” au “kufaraji” (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)
- b. “kuhuzunika” (mf. Mwa. 6:6,7)
- c. “kughairi” (mf. Kut. 13:17; 32:12,14; Hes. 23:19; Ayubu 42:5-6)
- d. “huruma” (mf. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahusisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa watu wengine, lakini pia kuelekea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana “kutubu” (kama vile Mwa. 6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha “kurudi” (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha “kugeuka” au “kurejea tena” Kitenzi hiki kinaweza kutumika kwa

1. kumuelekea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
2. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isingeweza kutubu (kama vile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojama Mungu kupitia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipya inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [AJ]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu inaweza kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Maro 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nacham* linarejea juu ya hisia zenye nguvu za kutambaua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi's sin with Bathsheba (kama vile 2 Samuel 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13).

Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahijika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejesha ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

30:2-3 Mukdadha huu unaleta uhalali unaohitajika kithiolojia kwenye hukumu iliyowazi ya sura 29:19. Tatizo sio uasi bali hali ya kuasi inayoendelea kujirudia. Toba siku zote inapatikana upande wa Mungu bali wanadamu huifanya migumu mioyo yao wenyewe kwa uasi wa makusudi na kutotii!

☐ **"BWANA"** YHWH ni jina la kimaagano la Mungu ambalo Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema linazifunua Rehema zake (kama vile Kut. 3:13-14). Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.

☐ **"Mungu"** *Elohim* ni jina la Mungu la ujumla ambalo linaashiria nguvu, uweza na uwezo. Walimu wa sheria za Kiyahudi wanasema kuwa linatumika kumaanisha hukumu na haki ya Mungu. Toofauti kati ya majina haya mawili inaweza kuonekana katika Zab.103, YHWH, na Zab 104, *Elohim*. Tazama Mada Maalum katika 1:3.

☐ **"tii"** Tambua kuwa kifungu cha maneno "kurudi kwa BWANA" kinafanana na kifungu "kumtii Yeye" (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU).

Utii unaelezewa kwa maneno ya ubinafsi:

1. kutii sauti yake - BDB 876
2. kwa moyo wako wote - BDB 523
3. kwa nafsi yako yote - BDB 659

Hii inafanana na 4:29-30; 6:5; 10:12

Tazama idadi na maana tofauti tofauti za neno *shub* (BDB 996, KB 1427):

1. "wakumbushe" kiuhalisia ni "kuwasababisha wakurudi, katika moyo wako, mst. 1
2. "ninyi mtamrudi kwa BWANA," mst. wa 2
3. "tena Mungu atakurejesha wewe utumwani," mst. 3
4. "tena," mist. 3,8,9
5. "ukimwelekea BWANA," mstari wa 10

☐ **"kwa moyo na nafsi yako yote"** Hii ni nahau juu ya sehemu zote za mtu zinazomfanya awe kamili kabisa (kama vile mist. 2,6,10; 4:29; 6:5; 10:12;11:13; 13:3; 26:16).

☐ **“wewe na wanao”** Agano la kale linafanywa upya kwa kizazi cha sasa (kama vile 29:1). Israeli ilitakiwa kutoa elimu kwa watoto juu ya historia ya msingi wa imani yao (kama vile 4:9,10; 6:7,20-25; 11:19; 32:46).

30:3-4 “Mungu atarejesha. . Mungu ametawanya” Tambua kuwa Mungu anashughulikia historia. Anatomia mataifa na mtu mmoja mmoja lakini yeye ndiye Matawala mkuu (kama vile Isa. 10:5; 44:28-45:1).

30:3-9 Tazama kile ambacho YHWH amekiahidi kukifanya kwa Israeli (ikiwa watatii, mist. 8,10):

1. Atarejesha (mst. 3, BDB 996, KB 1427, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
2. Atahurumia (mst. 3, BDB 933, KB 1216, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
3. Atawakusanya (BDB 867, KB 1062, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, mara mbili, mst. 3 and 4)
4. Atawarudisha (mst. 4, BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
5. Atawaleta katika nchi (mst. 5, BDB 97, KB 112, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
6. Atawatajirisha (mst. 5, BDB 405, KB 408, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
7. Atawazidisha (mst. 5, BDB 915 I, KB 1176, *Hiphi* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
8. Atawatahiri mioyo yenu (mst. 6, BDB 557 II, KB 555, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
9. Atawaachia laana juu ya adui zenu (mst. 7, BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
10. Atawatajirisha kwa utele (mst. 9, BDB 451, KB 451, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
 - a. kazi ya mikono yenu
 - b. uzao wa miili yenu
 - c. uzao wa mifugo yenu
 - d. mazao ya nchi yenu (kinyume chake kiko katika 28:38-42)
11. Atawafurahia tena kwa ajili ya wema (mst. 9, BDB 965, KB 1314 [mara mbili], *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO na *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)

30:4

NASB “ncha za mbingu za mwisho”

NKJV “sehemu za mbali mwisho kabisa chini ya mbingu”

TEV “mwishoni mwa ncha ya dunia”

NJB “mwishoni mwa mbingu”

Hii kiuhalisia ni “mwisho wa mbingu,” ambayo ni kutia chumvi (kama vile 4:32; 28:64; Yer. 31:8). Inarejerea kwa ustaarabu wa mbali wowote wanaoujua (yaani, desturi za Mashariki ya Karibu ya Kale na Mediterania).

30:5 “ambayo baba zenu walimiliki” Hii ingeweza kurejelea:

1. Mababa wa imani (siku za Musa)
2. kurudi kutoka uhamishoni (wahariri wa baada ya uhamisho)

Kutokana na kujifunza kwangu #1 unaonekana kuwa bora zaidi. Mstari wa 9 unazungumzia kundi lile lile.

☐ **“atawatajirisha na kuwazidisha”** Hii ni sehemu ya ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu (kama vile Mwa. 12, 15, 17, n.k)

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 30:6-10

⁶Bwana, Mungu wako, atautahiri moyo wako, na moyo wa uzao wako, ili umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, upate kuwa hai. ⁷Na laana hizi zote Bwana, Mungu wako, atawatia adui zako na hao wakuchukiao, waliokuwa wakikutesa. ⁸Nawe utarudi, uitii sauti ya Bwana, na kuyafanya maagizo yake yote nikuagizayo leo. ⁹Na Bwana, Mungu wako, atakufanya uwe na wingi wa uheri katika kazi yote ya mkono wako, katika uzao wa tumbo lako, na katika uzao wa ng'ombe wako, na katika uzao wa nchi yako; kwa kuwa Bwana atafurahi tena juu yako kwa wema, kama alivyofurahi juu ya baba zako; ¹⁰ukiwa utaiuata sauti ya Bwana, Mungu wako, kwa kuyashika maagizo yake, na amri zake zilizoandikwa katika chuo hiki cha torati; ukimwelekea Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote.

30:6 “Mungu atawatahiri mioyo yenu” Hii ni sitiari ya kuwepo kwa uhuru wa kusikia neno la Mungu. Kinyume chake kinatajwa katika mst. 17. Katika 10:16 na Yer. 4:4; 9:25-26, Waisraeli wanaitwa kutenda tendo hili la kiibada (kama vile Rom. 2:28-29), na bado hapa Mungu lazima afanye. Mvutano huu huu ulio kati ya utawala na ukuu wa Mungu na tendo la mwanadamu unaonekana katika Ezek. 18:31 dhidi 36:26. Hapa tohara ni stiari ya mtazamo sahihi wa kiroho. Tazama dokezo kamili katika 10:16.

☐ **“moyo”** Kwa Waebrania hiki kilikuwa ni kitovu cha matendo ya kiali. Tazama Mada Maalum katika 2:30.

☐ **“wazao”** Hili kiuhalisia ni neno “uzao” (BDB 282). Neno hili linatumika katika namna ya kisitiari mara kadhaa katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 1:8; 4:37; 10:15; 11:9; 28:46,59; 30:6,19; 31:21; 34:4).

☐ **“nafsi”** Hili ni neno la Kiebrania *nephesh* (BDB659). Tazama dokezo katika 11:13.

30:8-9 Hii inaaksi kile ambacho Mungu alitaka kufanya kwa Israeli na kwa ulimwengu wote! Tazama Mada Maalum: Upendeleo wa Kiinjilisti wa Bob katika 4:6.

30:10 “ikiwa. . .ikiwa” Hii inaonesha asili ya kimasharti ya agano. Tazama kwamba utii (kusikia na kutunza) vinarandana na uaminifu na kujizatiti (kwa moyo wako wote na nafsi).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 30:11-14

¹¹Kwa maana maagizo haya nikuagizayo leo, si mazito mno kwako, wala si mbali. ¹²Si mbinguni, hata useme, Ni nani atakayetupandia mbinguni akatuletee, aje atuambie tusikie, tupate kuyafanya? ¹³Wala si ng'ambo ya pili ya bahari, hata useme, Ni nani atakayetuvukia bahari, akatuletee, aje atuambie, tusikie, tupate kuyafanya? ¹⁴Lakini neno li karibu nawe sana, li katika kinywa chako na moyo wako, upate kulifanya.

30:11-14 Mapenzi ya YHWH kwa Israeli hayakushindikana (kama vile 28:29). Mstari huu unaonekana kushusha makali ya mafundisho ya wanamaguzi wa “uovu kamili.” Kuna maeneo kadhaa katika Agano la Kale ambapo uhindaji wa kibinadamu wa dhambi unawezekana (mfano, Mwa. 4:7).

Kanisa linachukua Mwanzo 3 kama chanzo cha dhambi kwa mwanadamu wakati walimu wengi wa kiyahudi wanachukua Mwanzo 6 kama chanzo cha mgogoro. Kama Ukristo unavyoelezea anguko la uumbaji wote, akijumuishwa mwanadamu, Dini ya Kiyahudi wema wa mwandamu. Kwao uovu ni uchaguzi na sio msingi wa asili.

Hata hivyo, inaonekana kwangu kuwa uwajibikaji wa kimaadili umejikita katika uwezekano halisi wa kuyafahamu mapenzi ya Mungu na uwezo wa kuyafanyia kazi. Bila kuwepo uwezekano wa kitendo sahihi, uwajibikaji wa kiungu hauwezi kuwepo! Naweza kuhukumiwa kwa kile ambacho siwezi kufanya?

30:12 “Nani atapanda mbinguni” Paulo anatumia hili katika Rom. 10:6-9. Linaaksi neno la zamani la kisumeri la Etana, lakini yawezekana inafanana na mtazamo wa Kiebrania wa ukuu wa Mungu.

Kuna VITENZI kadhaa vinavyotumika kwa namna ya kaulli shurutishi katika mstari huu (kulingana na Mwongozo wa Maelezo ya Agano la Kale):

1. “kulipata” - BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini KAULI YA KUSIHI katika maana
2. “kutufanya kusikia” - BDB 1033, KB 1570, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini ikiwa na KAULI YA KUSIHI katika maana
3. “tuweze kulifuata” - BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini ikiwa na KAULI YA KUSIHI katika maana

30:13 “ng'ambo ya pili ya bahari” Baadhi wanaliona hili kama lenye kufanana na habari ya mafuriko ya Babeli iitwayo Gilgamesh Epic, lakini inawezekana inafananana hofu za Wayahudi wasafirio au stiari ya mwisho wa nchi.

30:14 “Lakini neno li karibu nawe sana, li katika kinywa chako na moyo wako” Hii inalirejelea agano la YHWH lililofunuliwa. Watu wa kale walisoma maandiko kwa sauti ya juu! Walitakiwa kuitikia vyema kwa ndani juu ya kile ambacho walikuwa wamekisisia (yaani, kusoma wao wenyewe au kusoma kwa sauti).

☐ **“upate kulifanya”** Mwanadamu lazima afanye maamuzi. Hili liko katika uwezo wake kulifanya. Mungu anaanzisha lakini mwanadamu sharti aitikie na kuendelea kuitikia katika toba, imani na utii!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 30:15-20

¹⁵Angalia, nimekuwekea leo mbele yako uzima na mema, na mauti na mabaya; ¹⁶kwa hivi nikuagizavyo leo kumpenda Bwana, Mungu wako, kuenenda katika njia zake, na kushika maagizo yake, na amri zake, na hukumu zake, upate kuwa hai na kuongezeka; Bwana, Mungu wako, apate kukubarikia katika nchi uingiayo kuimiliki. ¹⁷Lakini moyo wako ukikengeuka, usipotaka kusikiza, lakini ukavutwa kando kwenda kuabudu miungu mingine, na kuitumikia; ¹⁸nawahubiri hivi leo hakika mtaangamia; hamtazifanya siku zenu kuwa nyingi juu ya nchi, uivukiayo Yordani, uingie kuimiliki. ¹⁹Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako; ²⁰kumpenda Bwana, Mungu wako, kuitii sauti yake, na kushikamana naye; kwani hiyo ndiyo uzima wako, na wingi wa siku zako; upate kukaa katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako, Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, kuwa atawapa.

30:15 “Angalia” Hiki (BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI SHURUTISHI) KITENZI kinatumika kumaanisha “kuwa mwangalifu” (kama vile Mwa. 27:27; 31:50). Hiki kinatumika mara kadhaa katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 1:8,21,35; 2:24,31; 4:5; 11:26; 30:15; 32:39).

☐ **“nimekuwekea leo mbele yako uzima na mema, na mauti na mabaya”** Hata Israeli ya kiagano ilitakiwa kuchagua! Hii inarejerea kwa baraka na laana (kama vile Law. 26 na Kumb. 27-28). Kumbuka uchaguzi unawekwa katika agano la neema. Hii ni sawa na nahau ya Fasihi ya Hekima ya “njia mbili” (kama vile Mithali4:10-19; Yer. 21:8; Mt. 7:13-14). Uchaguzi wetu unaonesha jinsi tulivyo! Namna tunavyoitikia mambo ya maisha “ya nje na ndani” huu unaufunua mwenendo wetu wa kiroho!

30:16-18 Mistari hii ni muhtasari wa masharti ya kimaagano:

1. majukumu (kama vile 8:6; 19:9; 26:17; 28:9)
 - a. “kumpenda Bwana,” mst. 16 (BDB 12, KB 17, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO)
 - b. “kutembea katika njia zake,” mstari wa16 (BDB 229, KB 246, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO)
 - c. “kutunza hukumu zake,” mstari wa16 (BDB 1036, KB 1581, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO)
2. matokeo ya utii
 - a. “mpate kuwa hai,” mst.16 (BDB 310, KB 309, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
 - b. “ili muweze kuzidi,” mst.16 (BDB 915, KB 1156, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
 - c. “Mungu wenu aweze kuwabariki,” mstari wa16 (BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
3. masharti na matokeo ya kutotii
 - a. ikiwa mioyo yenu itageuka mbali,” mstari wa17 (BDB 815, KB 937, *Qal*KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
 - b. “ikiwa hamtatii,” mstari wa17; (BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
 - c. ibada ya sanamu
 - (1) Kuchukuliwa mbali (BDB 623, KB 673, *Niphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
 - (2) kuabudu (BDB 1005, KB 295, *Hishtaphel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
 - (3) kutumikia (BDB 712, KB 773, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU)
 - d. “hakika mtapotea,” mst.18 (BDB 1, KB 2, *Qal* KITENZIJINA HALISI na*Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, ambacho kinaonesha undani)
 - e. “hamtaishi siku nyingi,” mst.18 (BDB 73, KB 88, *Hiphil*KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)

Tazama namna mstari wa 20 unavyohamasisha majukumu haya ya kiagano ili kwamba baraka za Mababa wa imani ziweze kutimilizwa! Misamiati hii ni tabia ya kitabu cha Kumbukumbu la Torati.

30:19 “Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo” Mashahidi hawa hawakuwa wa kipekee kwa agano la Israeli bali wanapatikana katika maandiko kadhaa ya Mashariki ya Karibu ya Kale. Viashiria hivi viwili vya kudumu vya uumbaji wa Mungu (kama vile Mwa. 1:1) vinafanya kazi kama Mungu anavyotaka (kama vile 17:6; 19:15; Hes. 35:30). Msisitizo huu wa kisheria unatokea mara kadhaa katika Kumbukumbu la Torati (kama vile 4:26;30:19; 31:28; 32:1). Kwa “Dunia” tazama Mada Maalum katika 5:8.

☑ **“basi chagua uzima, ili uwe hai”** Mungu amewapa wanadamu haki na wajibu wa kufanya maamuzi ya kimaadili. Ni sehemu ya Sura Yake na mfano wake katika mwanadamu! KITENZI cha Kiebrania, “kuchagua” au “kuteua,” kinatumika asilimia 70% ya muda wa maamuzi ya mwanadamu (kama vile NIDOTTE, juzuu 1, uk. 639). Lazima tuchague (kama vile Ezek. 18:30-32).

☑ **“wewe na uzao wako”** Kitabia kitabu cha Kumbukumbu la Torati kinasisitiza hitaji la kurithisha historia ya kimaagano na majukumu kwa kizazi kinachokuja (kama vile 4:9,10; 6:7,20-25; 11:19; 32:46). Watoto wetu wanaathiriwa na maamuzi ya mtindo wetu wa maisha na maelekezo (kama vile Kut. 20:5-6; Kumb. 5:9-10; 7:9).

30:20 Kuna mfululizo wa *Qa/* VITENZI VYA MUUNDO WA MANENO ambavyo vinaweka muhtasari wa agano:

1. majukumu
 - a. kupenda
 - b. kutii
 - c. kushikilia
2. madhara
 - a. ili muweze kuishi katika nchi

Tazama dokezo katika 30:16-18. Agano la YHWH lilihitaji imani, upendo na ustahimilivu wa mwanzo na kuendelea kwa vitu hivi.

YHWH aliahaidi nchi kwa mababa wa imani wa Israeli (kama vile Mwa. 12:7; 13:14-17; Kumb. 9:4-6), lakini Israeli sharti iyatii mahitaji ya kimaagano au nchi ingechukuliwa katika mikono yao (kama vile 11:31-32; 28:36,63-68; 30:19-20). Neema ya bure sharti iitikiwe vema na kuhifadhiwa!

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini kweli kuu ya sura hii?
2. Je, sura hii inazungumzia mtu kufanyika mwamini au mwamini kuwa mwaminifu?
3. Je, sura hii inakinzana na thiolojia ya Paulo juu ya mwanadamu kutokuwa na uwezo wa kushika sheria (yaani, Wagalatia 3; Warumi 3)?

KUMBUKUMBU LA TORATI 31

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Yoshua Kiongozi Mpya wa Israeli 31:1-8	Hitimisho la Matukio ya maisha ya Musa 31:1-6 31:7-8	Yoshua Anakuwa Mrithi wa Musa 31:1-6 31:7-8	Wajibu wa Yoshua 31:1-6 31:7-8
Sheria Kusomwa kila Baada ya Miaka Saba 31:9-13	31:9-13	Sheria Kusomwa kila Baada ya Miaka Saba 31:9-13	Utaratibu wa Kusoma Sheria 31:9-13
Utabiri juu ya uasi wa Israeli 31:14-15 31:16-23	31:14-15 31:16-22	Maagizo ya Mwisho ya Bwana kwa Musa 31:14-15 31:16-18	Maagizo ya Yahweh 31:14-15 31:16-18
			Wimbo wa Mashahidi 31:19-21 31:19-22 31:22
	31:23	31:23	31:23
			Sheria inawekwa kando Ya sanduku
31:24-29	31:24-29	31:24-29	31:24-27
			Israeli Inakusanyika ili Kusikiliza Wimbo (31:28-32:44)
Wimbo wa Musa (31:30-32:47) 31:30		Wimbo wa Musa (31:30-32:44) 31:30	31:28-29 31:30

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)
KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo (soma mzunguko #3.uk. viii). linganisha mgawanyo wako na tafsiri nne hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya ya tatu
12. Nk.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 31:1-6

¹ Musa akaenda akawaambia Waisraeli maneno haya yote. ² Akawaambia, Mimi leo ni mwenye miaka mia na ishirini; siwezi tena kutoka na kuingia, na Bwana ameniambia, Hutavuka mto huu Yordani. ³ Bwana Mungu wako, ndiye atakayevuka mbele yako, atawaangamiza mataifa haya mbele yako, nawe utawamiliki; na Yohua atavuka mbele yako, kama Bwana alivyonena. ⁴ Na Bwana atawatenda hao kama vile alivyowatenda Sihoni na Ogu, wafalme wa Waamori, na nchi yao, ambao aliwahaibu. ⁵ Naye Bwana atawatia mikononi mwenu, nanyi mtawatenda kadiri ya amri ile niliyowaamuru. ⁶ Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana Bwana, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha.

31:1 “akawaambia maneno haya” inawezekana haya yakawa “maneno ya mwisho,” kufuatana na tafsiri ya maandiko ya Kale ya Maandiko ya Kiebrania na baadhi ya machapisho ya magombo ya Bahari ya Chumvi, ambayo yamebadili konsonanti mbili za Kiebrania (k.v. toleo la NRSV, REB). Huu ni mwisho wa mahubiri matatu ya Musa.

31:2 “Mimi leo ni mwenye miaka mia na ishirini” Miaka 120 ya maisha ya Musa (k.v. 34:7) inaweza kugawanywa katika sehemu tatu katika miaka 40. Musa alikuwa na miaka 40 alipoandaliwa katika elimu za kifalme za Misri, miaka 40 ya kufundishwa wito jangwani, na miaka 40 kutoka muda alipokutana na kichaka kiwakacho moto hadi sasa (k.v. Kut. 7:7 na Mdo. 7:23 na kuendelea). Kwa nini ametaja umri wake? Hizi sababu inawezekana: (1) katika fasihi ya Wamisri miaka 110 ulikuwa umri wa watu wenye hekima, lakini katika Shamu ilikuwa ni miaka 120; (2) ukomo wa umri katika Mwa. 6:3; au (3) sababu nyingine ya Musa ni vile ambavyo hatawaongoza kwenda Nchi ya Ahadi.

☐ **“siwezi tena kutoka na kuingia”** Hii ni Nahau ya Kiebrania yenye kumaanisha nguvu (Yosh. 14:11; Toleo la NRSV, TEV, NJB, JPSOA)! Hata hivyo, umri wa uzee haukuzichukua nguvu za Musa, k.v. Kumb. 34. Inawezekana hii ikawa sababu (k.v. 1:37) inayomhusisha Musa kutokutii mbele ya jamii ya wana wa Israeli iliyoandikwa katika Hes. 20:11-12. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati 3:23-29 kimeandika utetezi wa Musa kwa Mungu ili amruhusu kuingia katika Nchi ya Ahadi (k.v. 32:48-52).

31:3 “Bwana Mungu wako, ndiye atakayevuka mbele yako” Mungu anapigana kwa ajili yao, ingawa wao ni lazima wajiandae kwa ajili ya kushiriki vita (k.v. mist. 3-6, yaani, maneno ya vita takatifu). Musa alikuwa chombo kilichotumiwa na Mungu. Mungu, mwenyewe, ndiye yeye aliyewakomboza watu. Kwa uwazi ni YHWH, sio Yohua, aliyewatangulia watu wake mbele katika vita!

☐ **“Yohua atavuka mbele yako”** Kiongozi mpya alihitajika kwa sababu ya kutokutii kwa Musa. Mungu angekuwa na Yohua, lakini analazimika pia ilimpasa kuyatii masharti ya agano (k.v. 1:38; 3:28).

31:6 “Iweni hodari na moyo wa ushujaa” Mstari huu una miundo kadhaa ya shurutishi:

1. “kuwa hodari” - BDB 304, KB 302, *Qal* KAULI SHURUTISHI, k.v. mist. 7,23
2. “jipe moyo” - BDB 54, KB 65, *Qal* KAULI SHURUTISHI, k.v. mist. 7,23
3. “usiogope” - BDB 431, KB 432, inakanushwa *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, imetumika katika maana ya KITENZI AMRISHI

4. “usitetemeke” - BDB 791, KB 888, inakanushwa *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, imetumika katika maana ya KITENZI AMRISHI, k.v. 1:29; 7:21; 20:3; Yosh. 1:9

Namba 1 na 2 imerudiwa na Musa kwa Yoshua katika mst. 7 na namba 3 na 4 imerudiwa katika mst. 8 (#4 ni wenye kufanana, lakini KITENZI ni tofauti, “kuwa na hofu,” BDB 369, KB 365, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). Mtazamo sahihi na imani ni msingi! Kulikuwa na majitu katika nchi, lakini YHWH alikuwa na watu wake (k.v. mist. 3,4,5,6).

☐ **“hatakupungukia wala kukuacha”**

1. YHWH ataenda nao (yaani, “kutembea,” BDB 229, KB 246, *Qal* TUNGO TENDAJI ENDELEVU)
2. YHWH hatawaacha (yaani, “kukuacha,” BDB 951, KB 1276, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
3. YHWH hatawapungukia (“kuwaacha,” BDB 736 I, KB 806, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, k.v. Mwa. 28:15)

Ahadi hizi zimerudiwa kwa Yoshua katika Yosh. 1:5 na kurudiwa kama ahadi kwa waaminio wa Agano la Kale katika Ebr.13:5! Tumaini letu ni katika neema isiyobadilika ya tabia ya YHWH (mf, Kut. 34:6; Neh. 9:17; Zab. 103:8; 145:8; Yoeli 2:13)!

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 31:7-8

⁷ Musa akamwita Yoshua, akamwambia machoni pa Israeli wote, Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana utakwenda pamoja na watu hawa hata nchi Bwana aliyowaapia baba zao, ya kwamba atawapa; nawe utawarithisha. ⁸ Naye Bwana, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaika.

31:7 Huu ni uhamisho wa mamlaka mbele ya makutano! Huu ni utimilifu wa 1:38 na 3:28!

31:8 “atakuwa pamoja nawe” Hii imeelezwa upya, “nitakuwa pamoja nawe,” katika mst. 23! Ahadi binafsi ya uwepo wa YHWH ni baraka kubwa iliyoweza kutolewa (k.v. Kut. 3:12; 4:12,15; 33:14-16; Kumb. 4:37; Yosh. 1:5). Ndiyo sababu iliyowafanya viongozi wake na watu wake kutokumwabudu mtu au kitu chochote!

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 31:9-13

⁹ Musa akaiandika torati hii, akawapa makuhani, wana wa Lawi, waliolichukua sanduku la agano la Bwana, na wazee wote wa Israeli. ¹⁰ Musa, akawaamuru, akasema, Mwisho wa kila mwaka wa saba, wakati wa maachilio, wakati ulioamriwa wa sikukuu ya vibanda, ¹¹ Israeli wote wafikapo ili kuonekana mbele za Bwana, Mungu wako, mahali pale atakapopachagua, uisome torati hii mbele ya Israeli wote masikioni mwao. ¹² Wakusanye watu, wanaume na wanawake na watoto, na mgeni wako aliyemo malangoni mwako wapate kusikia na kujifunza, na kumcha Bwana, Mungu wenu, na kuangalia kutenda maneno yote ya torati hii; ¹³ na watoto wao wasiojua, wapate kusikia na kujifunza kumcha Bwana, Mungu wenu, siku zote mtakazokaa katika nchi mnayoivukia Yordani ili kuimiliki.

31:9 “Musa akaiandika torati hii” Mara nyingi katika Vitabu Vitano vya Kwanza vya Biblia vinasema, “Musa akaiandika” (k.v. Kut. 17:14; 24:4,22; 34:1,27,28; Hes. 17:2,3; 33:2; Kumb. 4:13; 5:22; 31:9,22). Musa aliwapa wana wa Israeli sheria ili kuyafanya mapenzi ya Mungu kuwa ya aina moja kwa ajili ya vizazi vijavyo.

☐ **“makuhani, wana wa Lawi”** Inatia shauku kwamba kuna baadhi ya tofauti hasa “makuhani:”

1. kabila la Lawi (daima)
2. wana wa Haruni (mara nyingi)

Makuhani wote ni Walawi, lakini Walawi wote hawakuwa makuhani.

☐ **“na wazee”** Hii inarejelea kwa wazee wa makabila. Katika mstari huu Musa anakabidhi sheria kwa viongozi wa dini wa Israeli na viongozi wa kidunia (yaani, kikabila). Hata hivyo, kiuhalisia, viongozi wote wa Israeli na wale wa sheria walionekana kama wa kidini (yaani, mapenzi ya YHWH). Hakukuwa na viongozi wa kidunia dhidi ya

watakatifu katika Israeli. Wote walikuwa ni watakatifu kwa sababu wote walikuwa wa YHWH! Kulikuwa na sehemu maalumu na siku maalumu, lakini maisha yote yalitunzwa kwa agizo la Uungu!

31:10 Kuna tarehe mbili zinarejelewa katika mstari huu:

1. moja ilikuwa kila mwaka, sikukuu ya vibanda
 - a. Kut. 23:16-17; 34:22

Law. 23:33-43

- b. Kumbt. 16:13-15
2. moja ilikuwa kila baada ya miaka saba (yaani, mwaka wa sabato)
 - a. Kut. 23:10,11
 - b. Law. 25:1-7
 - c. Kumb. 15:1-6

Hapa Musa anaongezea utaratibu wa kawaida wa kusoma agano.

Sikukuu ya vibanda lilikuwa tukio la kila mwaka lililomaanisha ukombozi ili kuwakumbusha Waisraeli neema na matendo yenye nguvu za YHWH wakati wa kutoka Misri na utoaji wake wa chakula na uwepo wake kipindi cha kutangatanga jangwani. Sikukuu hii ya shukrani kwa ajili ya ukombozi/uhuru, kama vile kutoka katika utumwa wa madeni, ilitokea kila mwaka wa saba (yaani, mwaka wa sabato, k.v. Mambo ya Walawi 25). Muunganiko wa matukio haya mawili ya uhuru ulikuwa ni muda sahihi wa kuipitia upya sheria ya Musa ya agano na neema hii, Mungu mfanya agano!

MADA MAALUM : SIKUKUU ZA ISRAELI

- I. Sikukuu za kila Mwaka za Musa (k.v. Kutoka 23:14-17; Mambo ya Walawi 23; Hesabu 28; Kumbukumbu la Torati 16)
 - A. Wanaume wote wa kiyahudi walipaswa kuhudhuria sikukuu za kila mwaka (k.v. Kut. 23:14,17; 34:23) ikiwa inawezekana.
 - B. Sikukuu hizi zilikuwa za kilimo, pamoja na umuhimu wake kitaifa.
 - C. Kila moja ilikuwa siku ya mapumziko, kuabudu, na ushirika wa jamii.
 - D. Sikukuu tatu zilihataji kila mwaka
 1. Pasaka (k.v. Kut. 12:1-14,21-28; Law. 23:4-14; Hes. 28:16-25; Kumbt. 16:1-8; tazama [Mada Maalumu: Pasaka](#)
 - a. shukrani na mavuno shayiri takatifu
 - b. kuadhimisha safari ya kutoka uhamishoni
 - c. ilikuwa inafuatiwa na siku saba za sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu (k.v. Kut. 12:15-20;34:18-20)
 2. Pentekoste (sikukuu ya majuma, k.v. Kut. 23:16; 34:22)
 - a. shukrani na mavuno ya ngano takatifu
 - b. kuadhimisha siku ya kutolewa Torati kwa Musa katika Mlima Sinai na kisio la walimu wa kiyahudi
 - c. Tazama Law. 23:15-21; Hes. 28:26-31
 3. Hema la kukutania/Vibanda/Vibanda (*Succoth*)
 - a. shukrani kwa ajili ya mavuno jumla
 - b. kuadhimisha mwanzo wa kipindi cha kutangatanga jangwani
 - c. tazama Kut. 23:16; 34:22; Law. 23:34-44; Kumb. 16:13-17
 - d. ilikuwa inafuatiwa na siku nane za sikukuu (k.v. Law. 23:36; Hes. 29:35-38)
 - E. Sikukuu zingine za kila mwaka
 1. Kusheherekea mwaka mpya (*Rosh Hashanah*)
 - a. tazama Law. 23:23-25; Hes. 29:1-6
 - b. siku hii ya mapumziko na sadaka ilifanyika katika siku ya kwanza ya *Tishri*
 - c. sehemu ya sikukuu katika siku hii, ilikuwa ya kawaida katika kipindi cha Agano Jipya, haikutajwa katika Torati

2. Siku ya Upatanisho – "siku ya kufunikwa" au *Yom Kippur* (siku pekee ya kufunga)
 - a. siku ya mapumziko, kufunga, na kutubu
 - b. utaratibu kwa ajili ya kuondoa ushirika wa unajisi (hema la kukutania, makuhani, na watu)
 - c. tazama Kut. 30:10; Law. 16; 23:26-32; 25:9; Hes. 29:7-11
 - d. ni vigumu kuunganisha kwa pamoja ni wakati gani sikukuu hii ilianzishwa tena baada ya uhamisho
- II. Siku nyingine ya sikukuu ya Musa
- A. Sabato (tazama [Mada Maalumu: Sabato](#))
 1. Siku ya juma ya mapumziko na kuabudu
 2. tazama Mwa. 2:1-3; Kut. 16:22-30; 20:8-11; 23:12; 31:12-16; Law. 23:1-3; Hes. 28:9-10
 - B. Mwaka wa Sabato
 1. kila baada ya miaka saba nchi itapumzishwa kulimwa (hakuna kupanda)
 2. tazama Kut. 23:10-11; Law. 25:1-7; Kumb. 15:1
 3. ni ishara kwamba YHWH alimiriki nchi na kuwapatia Israeli
 4. watumwa wote waliachiliwa huru (k.v. Kut. 21:2-6) na madeni yote kusamehewa (k.v. Kumb. 15:1-6)
 - C. Mwaka wa Yubilee
 1. kila mwaka wa Sabato (yaani, miaka 50)
 2. tazama Law. 25:8-18; 27:17-24
 3. kuachilia deni na kurudisha nchi, kuachilia watumwa (k.v. Lev. 25:10,13, inafanana sana na Mwaka wa Sabato)
 4. sikukuu yake haikuandikwa kamwe
 - D. Mwezi Mpya
 1. sadaka za kuteketezwa maalumu na siku ya mapumziko
 2. tazama Hes. 10:10; 28:11-15
 3. inawezekana mpangilio wake wa kuadhimisha ni juu ya hema la kukutania (k.v. Kut. 40:2,17)
 4. Kalenda ya Kiyahudi iko katika mzunguko wa mwezi
- III. Taratibu hizi na desturi zinaonyesha maendeleo kwa wakati. Sikukuu hizi na siku moja ya kufunga yumkini zilianza katika kalenda za kipagani (tazama [Mada Maalumu: Kuabudu Mwezi](#)), lakini ziliboreshwa kuwa sifa na ibada za kiyahudi pekee kwa ajili ya YHWH. Asili (majira), kilimo (kupanda, mvua na mavuno), na matukio ya kitaifa (Kutoka, kupewa sheria, nk.) yameunganishwa ili kuonyesha nyakati halisi za mwaka kwa ajili ya kuabudu.

31:11 “mahali pale atakapopachagua” Mstari huu katika siku za Musa ulirejelea kusanyiko la wanaume wote mara tatu kwa mwaka (k.v. Mambo ya Walawi 23) katika Hema la kukutania (k.v. Kut. 20:24; Kumb. 12:5,11,13; 14:25; 15:20; 16:7,16; 17:8,10; 18:6; 26:2).

Baadaye Ukarejelea eneo maalumu la kuabudia huko Yerusalemu.

☐ **“uisome torati hii mbele ya Israeli wote”** Hili lilikuwa ni tukio la kulifanya upya agano. Sheria ilikuwa inafunuliwa kwa uwazi (yaani, kusoma) na Israeli kuahidi kuitunza! Kila jamii ya Israeli ilitakiwa iwepo siku hiyo (k.v. mist. 12-13), hata kizazi kipya (yaani, cha umri *Bar Mitzvah*, mf, Isa. 7:16).

Sheria haikuwa kwa ajili ya mfalme wa baadae wala kwa viongozi wa wakati huu pekee, lakini kwa ajili ya watu kupitia kwa kizazi chao na hata kwa wageni wakazi!

31:12 “wapate kusikia ... kujifunza... kumcha” Tambua mfuatano wa VITENZI:

1. “kusikia” - BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, iliyozoeleka katika Kumbukumbu la Torati, ikimaanisha “kusikia na kutenda”
2. “kujifunza” - BDB 540, KB 531, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. “kumcha” - BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (tazama kifungu cha mwisho hapa chini)

4. “kuangalia kutenda”
 - a. BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
 - b. BDB 793, KB 889, *Qal* KITENZI JINA CHA MUUNDO WA MANENO

Tambua kwamba #1,2,3 vimerudiwa katika mst. 13 ili kuhusisha kizazi kipya, ambacho bado hatukifahamu (BDB 393, KB 390, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU). Sheria hii ilimaanisha ifahamike na kutunzwa kupitia wingi wa vizazi vya wana wa Israeli.

Kwa njia zingine mfuatano huu unanikumbusha mimi juu ya Ezra (k.v. Ezra 7:10). Israeli ni lazima wamche au kumheshimu (BDB 431) YHWH (k.v. 4:10; 14:23; 17:19), lakini sio kumcha mwingine au kingine zaidi!

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 31:14-18

¹⁴ Bwana akamwambia Musa, Tazama, siku zako za kufa zinakaribia, umwite Yoshua, nanyi mkajihudhurishe katika hema ya kukutania, ili nipate kumwagiza kazi. Musa na Yoshua wakaenda, wakajihudhurisha ndani ya hema ya kukutania. ¹⁵ Bwana akaonekana katika Hema katika nguzo ya wingu; na ile nguzo ya wingu ikasimama juu ya mlango wa Hema. ¹⁶ Bwana akamwambia Musa, Angalia, wewe utalala na baba zako; na watu hawa wataondoka, wataifuata kwa ukahaba miungu ya kigeni ya nchi waiendeayo kuwa kati yao, nao wataniacha mimi na kulivunja agano langu, nililofanya nao. ¹⁷ Ndipo hasira yangu itakapowaka juu yao siku hiyo, nami nitawaacha, nitawaficha uso wangu, nao wataliwa, tena watajiliwa na mambo maovu mengi na mashaka; hata waseme siku hiyo, Je! Kujiliwa kwetu na maovu haya si kwa sababu Mungu wetu hayumo kati yetu? ¹⁸ Nami nitawaficha uso wangu kwa kweli siku hiyo, kwa maovu yote waliyoyafanya, kwa kuigeukia hiyo miungu mingine.

31:14 “umwite. . .mkajihudhulishe” Hizi ni KAULI SHURUTISHI mbili.

1. “umwite” - BDB 894, KB 1128, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. “mkajihudhulishe” - BDB 426, KB 427, *Hithpael* KAULI SHURUTISHI (hii inarejelea agizo la amri litolewalo na YHWH, k.v. I Sam. 10:19, au kupitia upya agano, k.v. Yosh. 24:1)

☐ **“hema ya kukutania”** inaonekana kuna mahema mawili maalumu yanayomhusisha YHWH:

1. Hema linaloelezewa katika kitabu cha Kutoka 25-27, lililokuwa nyumba ya sanduku la agano na liliwekwa katikati ya kambi za wana wa Israeli
2. Hema la kukutania linaloelezewa katika kitabu cha Kut. 33:7-11, lililosimamishwa nje ya kambi za wana wa Israeli, ambapo Musa alikutana na YHWH
3. Kwa kawaida wingu (yaani, ambalo walimu wa kiyahudi wanaliita wingu la utukufu (*Shekinah*)), ambalo ni kielelezo cha uwepo binafsi wa YHWH, aliyejidhihirisha mwenyewe katika #1, lakini hapa katika #2 (k.v. mst. 15; Kut. 33:9)
4. Inawezekana kwamba rejea kadhaa zinahusika kwa #2—Kut. 18:7-16; Hes. 11:16,24,26; 12:4

☐ **“, ili nipate kumwagiza kazi”** Katika mst. 7 Musa anamwita Yoshua mbele za watu. Hapa YHWH anawaita Musa na Yoshua mbele zake mwenyewe.

31:15 “nguzo ya wingu” Hii ni nguzo ya wingu ile ile iliyokuwa inawatenganisha wana wa Israeli na jeshi la Misri (k.v. Kut. 13:21-22; 14:19-20). Nguzo hii ndiyo iliyolifunika hekalu wakati Isaya alipomwona Mungu “Mkuu na aliyeinuliwa juu” katika Isaya 6. Hiki kilikuwa ni kielelezo cha kimwili cha uwepo wa Mungu. Nguzo hii ilikaa na Waisraeli muda wote wa kutangatanga kwao jangwani. Ilifanya kazi kwa njia kadhaa:

1. Ilionyesha uwepo wa YHWH
2. Iliwaongoza Waisraeli kutoka sehemu moja kwenda nyingine
3. Iliwapatia kivuli wakati wa mchana
4. Ilitia nuru kambi zao wakati wa usiku

Walipovuka mto Yordani, uwepo wa YHWH ulikuwa ukijidhihirisha juu ya sanduku la agano, lakini wingu lilitoweka.

31:16 “watu hawa wataondoka, wataifuata kwa ukahaba” Hili linafunua ufahamu wa YHWH wa kujua jambo litakalotokea kwa Israeli kuendeleza dhambi ya kuabudu sanamu (k.v. 4:15-28; 31:29). Tambua mfuatano wa kuabudu ya sanamu katika VITENZI:

1. “wataondoka” - BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, mf, Kut. 32:6
2. “wataifuata kwa ukahaba” - BDB 275, KB 275, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
 - a. Kutenda kama kahaba
 - 1) Law. 21:7,9,14
 - 2) Kumb. 22:21; 23:18
 - b. Stiari ya nchi ya ahadi, Law. 19:29
 - c. Stiari ya muungano wa kigeni
 - 1) Isa. 23:17
 - 2) Yer. 3:1
 - 3) Ezek. 16:26,28
 - d. Stiari ya kuabudu ibada ya ustawi
 - 1) Kut. 34:15,16
 - 2) Law. 17:7; 20:5
 - 3) Kumb. 31:16
3. “wataniacha mimi” - BDB 736, KB 806, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. 28:20; Amu. 10:6,10; Yer. 1:16
4. “kulivunja agano langu” - BDB 830, KB 974, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. 31:20; Law. 26:15; Yer. 11:10

31:17 “Ndipo hasira yangu itakapowaka”KITENZI hiki (BDB 354, KB 351, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) mara nyingi kimetumika kama hasira za YHWH:

1. Dhidi ya Musa, Kut. 4:14
2. Dhidi ya Israeli, Kut. 22:24; 32:10; Hes. 11:1,10; 32:10; Kumb. 6:15; 7:4; 11:17; 31:17
3. Dhidi ya wapelelezi, Hes. 12:9
4. Dhidi ya Balaamu, Hes. 22:22
5. Dhidi ya nchi, Kumb. 29:27

☐ **“nami nitawaacha, nitawaficha uso wangu”** VITENZI hivi viwili vinaelezea lugha za kibinadamu kwa batilisho la YHWH juu ya agano. YHWH anawatendea kama vile na wao walivyomtendea (k.v. mst. 16).

1. “nitawaacha” - BDB 736, KB 806, *Qal* KAULI WAKATI TIMILIFU
2. “nitawaficha uso wangu” - BDB 711, KB 771, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. mst. 18; 32:20; Isa. 59:2; 64:7). Hii ni Nahau kwa ajili ya kuondoa ushirika wa agano na baraka.

Matokeo yake ni:

1. wataliwa
 - a. KITENZI, “kuwa” - BDB 224, KB 243, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
 - b. Wataliwa/kuteketezwa - BDB 37, KB 46, *Qal* KITENZI JINA CHA MUUNDO WA MANENO
2. Wataijiliwa na mambo mengi maovu na mashaka
 - a. “wataijiliwa” - BDB 592, KB 619, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
 - b. maovu - BDB 949
 - c. mashaka - BDB 865 I
3. Uwepo wa YHWH (k.v. mist. 6,8) hautakuwa pamoja nao (yaani, “Mungu wetu hayupo kati yetu”)

31:18 Tishio kutoka mst. 17 (yaani, “nitawaficha uso wangu”) limerudiwa kwa mkazo (*Hiphil* KITENZI JINA HALISI na *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU).

☐ **“miungu mingine”** Toleo la *Jewish Study Bible* linadai kwamba “Mungu wetu” mst. 17 unaweza kutafsiriwa kuwa “miungu wetu” na unahusisha kwa “miungu mingine” katika mst. 18 (k.v. uk. 439).

Neno la kwanza (BDB 43) linaonekana kuwa muundo wa umoja ulilotolewa toka neno *Elohim* (BDB 43) katika mst. 18. Neno la kwanza linaweza kuwa limetumika kwa miungu ya wapagani (k.v. II Nya. 32:15; Dan. 11:37), lakini pia kwa ajili ya YHWH (k.v. Kumb. 32:15,17; Zab.50:22; 114:7; 139:19; Mit. 30:5; Isa. 44:8).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 31:19-22

¹⁹ Basi sasa jilandikieni wimbo huu, uwafundishe wana wa Israeli; kawatie vinywani mwao, ili uwe shahidi kwangu wimbo huu, juu ya wana wa Israeli. ²⁰ Kwa kuwa nitakapokwisha kuwatia katika nchi niliyowaapia baba zao, imiminikayo maziwa na asali; nao watakapokwisha kula na kushiba, na kuwanda; ndipo watakapoigeukia hiyo miungu mingine, na kuitumikia, na kunidharau mimi, na kulivunja agano langu. ²¹ Tena itakuwa, wakiisha kujiliwa na mambo maovu mengi na mashaka, utashuhudia wimbo huu mbele yao kama shahidi, kwa maana hautasahauliwa katika vinywa vya uzao wao; kwani nayajua mawazo yao wayawazayo, hata sasa kabla sijawatia katika nchi niliyoapa. ²² Basi Musa akauandika wimbo huu siku iyo hiyo, akawafundisha wana wa Israeli.

31:19 “Basi sasa jilandikieni wimbo huu” Huu utakuwa ni ushahidi wa Mungu dhidi ya matendo yajayo ya Israeli. Huu, hasa, ni stiari halali (k.v. 4:26; 30:19; 31:28; Yosh. 24:22)! Israeli ilitakiwa kuwajibika ili kuwafundisha sheria za YHWH kwa kila kizazi kipya!

31:20 “nao watakapokwisha kula na kushiba, na kuwanda; ndipo watakapoigeukia hiyo miungu mingine” Wakati ambao ni mgumu sana kwa watu wa Mungu ni kipindi cha mafanikio makubwa! Tunaelekea kusahau kwa wepesi sana (k.v. 6:10-15; 8:11-20; 32:15-18).

☐ Tambua mfululizo wa uasi hapa chini:

1. Watakapoigeukia miungu mingine - BDB 815, KB 937, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. mst. 18; 29:18; 30:17
2. kuitumikia - BDB 712, KB 773, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. 4:19; 7:4; 8:19; 11:16; 13:6,13; 17:3; 28:14,36,64; 29:18,26; 30:17
3. Kunidharau mimi - BDB 610, KB 658, *Piel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. Hes. 14:11,23; Isa. 1:4
4. Kulivunja agano langu - BDB 830, KB 974, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, k.v. mst. 16; Law. 26:15; Yer. 11:10; 31:32

31:21 “wakiisha kujiliwa na mambo maovu mengi na mashaka” Maovu na mashaka haya yalikuwa yametajwa katika mst. 17 na kutabiriwa katika 4:30.

☐ **“(kwa maana hautasahauliwa katika vinywa vya uzao wao)”** Hii ni ahadi ya mabaki waaminifu na kuendeleza maarifa ya sheria ya YHWH.

☐ **“mawazo”** Neno la Kiebrania *yetzer* wakati mwingine hutafsiriwa kama “mawazo ya moyo” (BDB 428 I, linaweza kuwa katika maana dhahili, Isa. 26:3). Hii ni njia ya Agano la Kale inayosema kwamba YHWH anajua mwelekeo wa uasi ambao uko ndani ya mwanadamu (yaani, Mwa. 6:5; 8:21; Zab. 103:14; Yer. 18:23).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 31:23

²³ Akamwagiza Yoshua, mwana wa Nuni, akamwambia, Uwe hodari na moyo mkuu, kwa kuwa utawapeleka wana wa Israeli katika nchi niliyowaapia; nami nitakuwa pamoja nawe.

31:23 Musa alinena maneno haya kwa wana wa Israeli katika 31:6. Musa alinena maneno haya kwa Yoshua katika 31:7 (k.v. 1:38; 3:28). Sasa (mst. 23) YHWH anasema maneno haya moja kwa moja kwa Yoshua (k.v. Yosh. 1:6,7,9), aliyesimama na Musa katika mlango wa hema la kukutania.

1. “uwe hodari” - BDB 304, KB 302, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. “moyo mkuu” - BDB 54, KB 65, *Qal* KAULI SHURUTISHI

☐ **“nami nitakuwa pamoja nawe”** maelezo haya yanatambulisha KIWAKILISHI NOMINO cha neno “nawe” cha mst. 23a. Hii ni zawadi kubwa sana ya YHWH (k.v. Kut. 3:12; 4:12,15; 33:14-16; Kumb. 4:37; 31:6,8; Yosh. 1:5)!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 31:24-29

²⁴ Basi ikawa hapo Musa alipomaliza kuandika maneno ya torati hii katika chuo, hata yakaisha, ²⁵ ndipo Musa akawaamuru Walawi waliokuwa wakilichukua sanduku la agano la Bwana akawaambia, ²⁶ Twaeni chuo hiki cha torati, mkiweke kando ya sanduku la agano la Bwana, Mungu wenu, ili kiwepo kama shahidi juu yako. ²⁷ Kwa kuwa uasi wako naujua, na shingo yako ngumu; angalieni, mimi nikali hai pamoja nanyi leo, mmekuwa waasi juu ya Bwana; siuze nitakapokwisha kufa! ²⁸ Nikutanishieni wazee wote wa kabila zenu, na maakida yenu, ili niseme maneno haya masikioni mwao, na kuwashuhudizia mbingu na nchi juu yao. ²⁹ Kwa sababu najua baada ya kufa kwangu mtajiharibu kabisa, na kukengeuka katika njia niliyowaamuru; nayo mabaya yatawapata siku za mwisho, kwa vile mtakavyofanya maovu machoni pa Bwana kumtia kasirani kwa kazi ya mikono yenu.

31:26 “kando ya sanduku la agano” Toleo la KJV lina neno “ndani,” lakini tafsiri bora zaidi ni “kando” (toleo la NKJV, NRSV, TEV, NJB, k.v. Kut. 25:16; I Fal. 8:9); na kwa ajili ya “sanduku” tazama Kut. 25:10-22.

Katika Agano la Kale inaonekana dhahili bamba mbili za mawe pekee ambazo kwazo amri kumi zilizoandikwa na Mungu (Kut. 31:18) ziliwekwa pamoja katika sanduku (pamoja na vipande vya bamba la awali alilovunja Musa, mf, Kut.32:19; 34:1). Kuna vitu vitatu ambavyo viliwekwa kando ya Sanduku:

1. kopo la mana, Kut. 16:33-34
2. Fimbo ya Haruni iliyochipua, Hes. 17:10
3. Sheria hii iliyoandikwa Musa

Hata hivyo, lazima kuwepo baadhi ya utata juu ya hili ndani ya jamii ya walimu wa sheria za Kiyahudi wanaofanana, kwa sababu mwandishi wa kitabu cha Waebrania anadai kwamba sanduku lilikuwa na bamba za mawe na #1 na #2 (k.v. Ebr. 9:4).

☐ **“agano”** Tazama Mada Maalumu katika 4:13.

31:27 “Kwa kuwa uasi wako naujua, na shingo yako ngumu” Musa aliutambua mwelekeo wa uasi wa Israeli (k.v. mst. 21) kipindi cha uhai wake (k.v. 9:7-29).

☐

NASB “shingo yako ngumu”

NKJV “shingo ngumu”

NRSV, TEV “mkaidi”

NJB “wenye kiburi”

Neno lenyewe ni muunganiko wa “shingo” (BDB 791) na “ngumu” au “nzito” (BDB 904). Israeli mara nyingi inaelezwa kwa muungano huu usiopendeza (k.v. Kut. 32:8; 33:3,5; 34:9; Kumb. 9:6,13; 31:27). KITENZI hiki kimetumika katika Kumb. 10:16; I Fal. 17:14; Neh. 9:16,17,29; Yer. 7:26; 17:23; 19:15. Mawazo yale yale yameelezwa katika Isa. 48:4 na Ezek. 2:4; 3:7.

Katika maana ya mist. 27-29 ni unabii, unaosisitiza matendo ya Israeli yaliyopita. Aina hii ya unabii pia unapatikana katika Yosh. 24:19-20. Jitihada bora zaidi za Israeli hazikutosha. Agano la kwanza halikufaulu kurejesha ukaribu wa ndani uliopangwa kati ya YHWH na uumbaji wake mkuu (yaani, mwanadamu) katika bustani ya Edeni. Akafanya agano jipya (k.v. Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38) lenye msingi wa matendo ya YHWH. Mwanadamu daima alikuwa muasi (k.v. Mwa. 6:5; 8:21; Yer. 17:9).

31:28 Mstari huu una VITENZI vitatu amrishi:

1. “nikutanishieni” - BDB 874, KB 1078, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
2. “niseme” - BDB 180, KB 210, *Piel* HALI YA KUSIHI
3. “kuziita” - BDB 729, KB 795, *Hiphil* HALI YA KUSIHI

Musa anawaelezea viongozi (yaani, wazee na viongozi), ambao ni kielelezo kwa Israeli wote, wanao ongoza. Hii inarejelea kwa wawakilishi wa baraza la taifa (mf, Amu. 21:16).

☐ **“na kuwashuhudizia mbingu na nchi juu yao”** Uthibitisho wa mashahidi mara nyingi umetajwa katika muktadha wa agano (k.v. 4:26; 30:19; 31:28; 32:1).

Katika sura hii pia kuna mashahidi wengine wawili:

1. Wimbo wa Musa, mist. 19,21
2. Hati ya Sheria, mst. 26

31:29 Tambua mfululizo wa unabii hapa chini baada ya kifo cha Musa (k.v. Yosh. 24:19-28):

1. mtajiharibu - BDB 1007, KB 1469, zote *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU na KITENZI JINA HALISI, k.v. 4:16,25; 9:12
2. kukengeuka katika njia - BDB 693, KB 747, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
3. mtafanya yaliyo mabaya (BDB 948 II) machoni pa Bwana - BDB 793 I, KB 889, *Qal*

KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

4. Kumtia hasira kwa kazi za mikono yenu (BDB 795 na 388, yaani, kuabudu sanamu) - BDB 494, KB 491, *Hiphil* KITENZI JINA CHA MUUNDO WA MANENO, k.v. 4:25; 9:18; 32:16; I Fal. 16:7; II Fal. 17:7; 21:6; Yer. 25:6,7; 32:30; 44:8

31:30 Mstari huu unaweza kuendana na sura ya 32.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini anawabadilisha viongozi?
2. Ni kwa namna gani utambuzi wa jambo kabla halijatokea na uchambuzi wa mtu unahusika katika sura hii?
3. Kwa nini wana wa Israeli walimuacha Mungu?

KUMBUKUMBU LA TORATI 31:30-32:52

MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Wimbo wa Musa	Wimbo wa Musa	Wimbo wa Musa	Wana wa Israeli Wanakusanyika ili Kuusikiliza wimbo wa Musa
(31:30-32:47)	(31:30-32:47)	(31:30-32:44)	(31:28-32:44)
32:1-14	32:1-43	32:1-43	32:1-44
(mst. 1-6)	(mst. 1-3)	(mst. 1-3)	(mst. 1-3)
	(mst. 4-9)	(mst. 4-6)	(mst. 4-9)
(mist. 7-9)		(mist. 7-9)	
(mist. 10-12)	(mist. 10-27)	(mist. 10-12)	(mist. 10-11)
			(mist. 12-14)
(mist. 10-12)	(mist. 10-27)	(mist. 10-12)	(mist. 10-11)
			(mist. 12-14)
(mist. 13-14)			(mist. 13-14)
32:15-18		(mist. 15-18)	(mist. 15-39)
32:19-22		(mist. 19-22)	
32:23-27		(mist. 23-27)	
32:28-33	(mist. 28-33)	(mist. 28-33)	
32:34-43			
(mist. 34-35)	(mist. 34-38)	(mist. 34-38)	
(mist. 36-38)			
(mist. 39-42)	(mist. 39-43)	(mist. 39-42)	
		(mst. 43)	(mst. 43)
32:44-47	32:44-47	32:44	(mst. 44)
		Maagizo ya Mwisho ya Musa	Sheria, chimbuko la Uzima

		32:45-47	32:45-47
Musa kufa juu ya Mlima Nebo			Kifo cha Musa Kinatabiria
32:48-52	32:48-52	32:48-52	31:48-52

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)
KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkaao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu
8. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Hii inaweza kuwa aina ya uwasilishaji wa kifasihi wa Mashariki ya Kale ya Karibu ambapo kiongozi aliachilia baraka zake, maonyo, na unabii kabla ya kifo chake:
 1. Yakobo – Mwanzo 49 (pia muundo wa kiushairi)
 2. Musa - Kumbu. 29:2-34:12
 3. Yoshua - Yosh. 23:1-24:33
 4. Samueli - I Samueli 12
 5. Daudi - I Fal. 2:1-9
- B. Baadhi ya wanazuoni wanauona ushairi huu: (1) katika mwangaza wa mwongozo wa makubaliano ya Hittite, lakini (2) wengine wanauona huu kama mandhari ya ua. Katika muktadha wa kitabu cha Kumbukumbu la Torati, uchaguzi 2 unaonekana bora zaidi, japo kitabu kizima cha Kumbukumbu la Torati kinaendana na mwongozo wa makubaliano ya milenia ya pili K.K. (wenye kutoa ushahidi wa uandishi wa Musa).
- C. Shairi hili ni la kale (miundo ya zamani). Takribani wanazuoni wengi wanadhani kwamba hili linarejelea nyakati za kale katika historia ya Israeli.
- D. Kuna madokezo mengi ya nyimbo zilizo katika Agano la Kale, hasa Zaburi na Isaya. Hizi zinaimbwa nyakati za ushindi:
 1. ngome za ulinzi za Kimisri ziliharibiwa katika Bahari ya Shamu, Kutoka 15
 2. kabla ya kuingia ng'ambo ya pili ya Mto Yordani, Hes. 21:17
 3. jeshi la kikanaani la Hazori liliangamizwa, Waamuzi 5
 4. Babeli iliagamizwa (Isaya 13) na Masihi wa YHWH (Isaya 11), Isa. 12:5
- E. Ushairi wa Kiebrania

MADA MAALUM: USHAIRI WA KIEBRANIA

- I. UTANGULIZI
 - A. Aina hii ya fasihi (yaani, inategemea namna inavyofafanua) inatengeneza 1/3 ya Kitabu cha Agano la

Kale. Sana sana hii ni kawaida katika vipengele vya sheria za Kiebrania vya "Manabii" (vyote lakini kitabu cha Hagai na Malaki vina ushairi) na "Maandiko".

- B. Ni tofauti sana na ushairi wa Kiingereza. Ushairi wa Kiingereza unakuzwa kutokana na ushairi wa Kiyunani na Kilatini. Ushairi wa Kiebrania unahusiana sana na ushairi wa Ki-kanaani. Kuna mistari yenye kuwekewa mkazo, mizani au vina katika ushairi wa Mashariki ya Karibu ya Kale.
- C. Ugunduzi wa utafiti wa mambo ya kale kaskazini mwa Israeli huko Ugariti (RasShamra) umewasaidia wanazuoni kuuelewa ushairiwa Agano la Kale. Ushairi huu wa karne ya 15 K.K. una uhusiano wa mara kwa mara pamoja na ushairi wa kibiblia.

II. SIFA PAMBANUZI ZA USHAIRI KWA UJUMLA

- A. Ni mfupi sana.
- B. Hujaribu kuzungumza ukweli, hisia au uzoefu katika hali ya kutumia taswira.
- C. Hapo awali haukuandikwa katika masimulizi. Umeundwa katika namna ya juu sana. Muundo huu unaelezwa katika:
 - 1. Mistari yenye ulinganifu (ufanano)
 - 2. Katika mbinu za maneno
 - 3. Katika mbinu za sauti

III. MUUNDO (R. K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, kr.965-975)

- A. Askofu Robert Lowth katika kitabu chake, *Lectures on the Sacred Poetry of the Hebrews* (1753) alikuwa wa kwanza kutoa sifa pambanuzi za ushairi wa kibiblia kama mistari yenye ulinganifu wa mawazo. Tafsiri nyingi za Kiingereza zinapangwa ili kuonyesha mistari ya ushairi.
 - 1. Maneno yenye kufanana—mistari inaeleza wazo lile lile katika maneno tofauti tofauti:
 - a. Zaburi 3:1; 49:1; 83:14; 103:3
 - b. Mithali 20:1
 - c. Isaya 1:3
 - d. Amosi 5:24
 - 2. kinyume—mistari hii inaeleza ukinzani wa mawazo kwa maana ya kutofautisha au kwa kuanza na uyaakinifu na ukanushi:
 - a. Zaburi 1:6; 90:6
 - b. Mithali 1:6,29; 10:1,12; 15:1; 19:4
 - 3. uambatani—mistari miwili au mitatu inakuza wazo- Zab. 1:1-2; 19:7-9; 29:1-2 pattern
 - 4. wema – mtindo wa ushairi unaolezea ujumbe katika utaratibu wa kupanda na kushuka. Lengo kuu linapatikana katikati ya mstari (tazama III. D; yaani, Amosi 5:4b-6a)
- B. Charles A. Briggs katika kitabu chake cha, *General Introduction to the Study of Holy Scripture* (1899) anaendeleza hatua inayofuatia ya uchambuzi wa ushairi wa Kiebrania:
 - 1. ishara—kifungu kimoja kilicho sahihi na cha pili kilicho cha kistiari, Zab. 42:1; 103:3.
 - 2. mwinuko au kilicho kaa kama daraja—kifungu hiki kina fungua ukweli katika mtindo wa kufuata mwinuko, Zab. 19:7-14; 29:1-2; 103:20-22.
 - 3. Uliyokingana ama kupishana—mfuatano wa vishazi, mara nyingi huwa ni vine vinavyohusiana na muundo wa ndani wa mstari wa 1 hadi 4 na 2 hadi 3 - Zab. 30:8-10a (zaidi kama chiasm)
- C. G.B. Gray katika kitabu chake, *The Forms of Hebrew Poetry* (1915), anaikuza dhana ya vishazi vyenye ulinganifu kwa:
 - 1. Ulinganifu kamili—ambapo kila neno lililo katika mstari wa kwanza linarudiwa au kuwekewa ulinganifu kwa neno lililo katika mstari wa pili - Zaburi 83:14 na Isaya 1:3

2. Ulinganifu ambapo vishazi havina urefu unaofanana - Zab. 59:16; 75:6

- D. Leo kuna utambuzi unaokua wa mtindo wa muundo wa fasihi ya kiebrania unaoitwa chiasm, ambao kwa kawaida unadokeza idadi ya mistari inayofanana (a.b,b,a; a,b,c,b,a) yenye kuunda muundo wa kioo, mara nyingi mistri ya katikati (s) inatiliwa mkazo.
- E. Utaratibu wa aina za sauti zinazopatikana kwenye ushairi kwa ujumla, lakini mara nyingi sio katika ushairi wa mashariki
1. uchezaji katika alfabeti (chemsha bongo, k.v. Zab. 9,34,37,119; Mit. 31:10nakuendelea; Maombolezo 1-4)
 2. uchezaji katika konsonanti (takriri, k.v. Zab. 6:8; 27:7; 122:6; Isa. 1:18-26)
 3. uchezaji katika irabu (mshabaha wa irabu, k.v. Mwa. 49:17; Kut. 14:14; Ezek. 27:27)
 4. uchezaji katika kurudia rudia maneno yenye maana tofauti (mchezo wa maneno)
 5. uchezaji katika sauti za maneno yenye kufanana, sauti kama jina la kitu (tanakali-sauti)
 6. ufunguzi na uhitimishaji mahususi (ujumuishwaji)
- F. Kuna ainakadhaazaushairikatikaAgano la Kale. Nyingine ni mada zenye kuhusiana na nyingine zinazounda uhusiano:
1. Wimbo wa kutunukia - Hes. 21:17-18
 2. Nyimbo zenye kutenda kazi - (zilizodokezwa lakini hazikuchukuliwa kumbukumbu katika Amu. 9:27); Is. 16:10; Yer. 25:30; 48:3
 3. tumbuizo - Hes. 21:27-30; Is. 23:16
 4. nyimbo za mvinyo - kanushi, Isa. 5:11-13; Amosi 6:4-7 na yakini, Is. 22:13
 5. mashairi ya mapenzi–Wimbo Ulio Bora, arusi yenye kutatanisha - Amu. 14:10-18, nyimbo za arusi - Zab. 45
 6. maombolezo/wimbo wa maziko - (uliodokezwa lakini haukunukuliwa katika II Sam. 1:17 na II Nya. 35:25) II Sam. 3:33; Zab. 27, 28; Yer. 9:17-22; Omb.; Eze. 19:1-14; 26:17-18; Nah. 3:15-19
 7. nyimbo za vita -Mwa. 4:23-24; Kut. 15:1-18; Hes. 16:35-36; Yosh. 10:13; Amu. 5:1-31; 11:34; I Sam. 18:6; II Sam. 1:18; Isa. 47:1-15; 37:21
 8. Baraka maalumu au za kiongozi - Mwa. 49; Hes. 6:24-26; Kumb. 32; II Sam. 23:1-7
 9. Maandiko yenye kuzungumzia ushirikina - Balaamu, Hes. 24:3-9
 10. Ushairi mtakatifu–Zaburi
 11. Mashairi ya chemsha bongo - Zab. 9,34,37,119; Mit. 31:10nakuendelea na Maombolezo 1-4
 12. laana - Hes. 21:22-30
 13. mashairi ya dhihaka - Is. 14:1-22; 47:1-15; Eze. 28:1-23

IV. MWONGOZO WA KUFASIRI USHAIRI WA KIEBRANIA

- A. Angalia kitovu cha ukweli wa ubeti au sehemu ya wimbo (hii ni kama aya iliyo katika nathari au lugha ya mjazo.) Toleo la RSV ilikuwa tafsiri ya kwanza ya sasa ili kuutambua ushairi kupitia beti. Zilinganishe tafsiri za sasa kwa ajili ya msaada wa utambuzi.
- B. Itambue lugha ya kiishara na kueleza katika nathari. Kumbuka aina hii ya fasihi ni ya kimaafikiano sana, mengi yanabakizwa kwa ajili ya msomaji kuyajaza (tazama Mada Maalumu: Fasihi ya Hekima).
- C. Hakikisha unayahusianisha mashairi yaliyojikita katika jambo la muda mrefu katika muktadha wake wa kifasihi (mara nyingi kitabu chote) na mpangilio wa kihistoria.
- D. Waamuzi 4 na 5 zinasaidia sana katika kuona namna ushairi unavyoieleza historia. Waamuzi 4 ni nathari ama lugha ya mjazo na Waamuzi 5 ni ushairi wa tukio lile lile.
- E. Jaribu kuitambua aina ya ufanano uliomo, kwa vyovyote visawe, ukinyume, au uambatani. Hili ni la muhimu sana.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 31:30

³⁰ Musa akasema maneno ya wimbo huu masikioni mwa kusanyiko la wana wa Israeli hata yakaisha.

31:30 “Musa akasema. . . maneno ya wimbo huu” Mstari huu lazima uendane na sura 32 ya kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Tambua kwamba toleo la NASB linaangalia mwanzo wa aya pamoja na nukta pacha za mwishoni, si kipindi (kama vile JPSOA).

☐ **“masikioni mwa kusanyiko la wana wa Israeli”** Mtu anastaajabu juu ya watu waliokuwa katika muktano huu. Huu ungehusisha wanaume, wanawake, na watoto au mtindo wa 31:12. Bali hii inarejelea jiji au mji. Ni kwa namna gani watu wangukuwa wameweza kumsikiliza mtu mmoja akizungumza? Mara nyingi kiongozi alizungumza na:

1. viongozi wa na hawa walipitisha maazimio (kama vile 31:28)
2. Walawi na walipitisha maazimio

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 32:1-14

¹ Sikilizeni, enyi mbingu, nami nitanena;

Na nchi isikie maneno ya kinywa changu.

² Mafundisho yangu yatadondoka kama mvua,

Maneno yangu yatatona-tona kama umande;

Kama manyunyu juu ya majani mabichi;

Kama matone ya mvua juu ya mimea.

³ Maana nitalitangaza Jina la Bwana;

Mpeni ukuu Mungu wetu.

⁴ Yeye Mwamba, kazi yake ni kamilifu;

Maana, njia zake zote ni haki. Mungu wa uaminifu, asiye na uovu,

Yeye ndiye mwenye haki na adili.

⁵ Wametenda mambo ya uharibifu,

Hawawi watoto wake, hii ndiyo ila yao;

Wao ni kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka.

⁶ Je! Mnamlipa Bwana hivi,

Enyi watu wapumbavu na ujinga?

Je! Yeye siye baba yako aliyekununua?

Amekufanya, na kukuweka imara.

⁷ Kumbuka siku za kale,

Tafakari miaka ya vizazi vingi;

Mwulize baba yako, naye atakuonyesha;

Wazee wako, nao watakuambia.

⁸ Yeye Aliye Juu alipowapa mataifa urithi wao,

Alipowabagua wanadamu,

Aliweka mipaka ya watu Kwa kadiri ya hesabu ya wana wa Israeli.

⁹ Maana, sehemu ya Bwana ni watu wake,

Yakobo ni kura ya urithi wake.

¹⁰ Alimkuta katika nchi ya ukame,

Na katika jangwa tupu litishalo;

Alimzunguka, akamtunza;

Akamhifadhi kama mboni ya jicho;

¹¹ Mfano wa tai ataharikishaye kioto chake;

Na kupapatika juu ya makinda yake, Alikunjua mbawa zake, akawatwaa,

Akawachukua juu ya mbawa zake;

¹² Bwana peke yake alimwongoza,

Wala hapakuwa na mungu mgeni pamoja naye.

¹³ Alimpandisha mahali pa nchi palipoinuka,

Naye akala mazao ya mashamba;

Akamnyonyesha asali iliyotoka jabalini, Na mafuta yaliyotoka katika mwamba wa gumegume;

¹⁴ Siagi ya ng'ombe, na maziwa ya kondoo,

Pamoja na mafuta ya wana-kondoo, Kondoo waume wa Kibashani,

na mbuzi, Na unono wa ngano iliyo nzuri;

Ukanywa divai, damu ya mizabibu.

32:1-3 Kuna mfululizo wa lugha ya kiushurutishi:

1. Katika mst. 1 hizi tatu zinahusiana na kusikia:
 - a. "Sikilizeni" - BDB 24, KB 27, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
 - b. "nitanena" - BDB 180, KB 210, *Piel* HALI YA KUSIHI
 - c. "isikie" - BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya HALI YA KUSIHI
2. Katika mst. 2 hizi mbili zinahusiana na umande:
 - a. "yatadondoka" - BDB 791, KB 887, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya HALI YA KUSIHI
 - b. "yatatona-tona" - BDB 633, KB 683, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya HALI YA KUSIHI
3. Katika mst. 3 "Mpeni" - BDB 396, KB 393, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (penda "hubiri" kama *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU pia inatumika katika maana ya HALI YA KUSIHI, ambayo inaleta muundo linganifu kama mist. 1 na 2)

32:1 "enyi mbingu. . . nchi" Haya mambo mawili ya kudumu (kama vile Mika 6:1-2). Kulikuwa na uhitaji wa mashahidi ili kuthibitisha ukweli (kama vile 4:26; sura 4 na 31-32 [kama vile 30:19; 31:28; 32:1] yanaunda mabano ya kifasihi). Neno "mbingu" linawakilisha mbingu (kama vile Mwa. 1:1). Kifungu hiki kinafanana namna Isaya analitambulisha shauri la YHWH (kv. Isa.1:2).

32:2 Mvua ilitumika kama mfanano wa viwango vya kuyatoa maisha kwa ajili ya neno la Mungu. Kwa maneno tofautitofauti mvua inatumika (BDB 564, 378, 973, 914). Hili pia ni dokezo la YHWH kama mstawishaji, si *Ba'al* (kv. 11:14,17; 28:12,24; 33:28).

32:3 "Jina la Bwana" Maana ya Kiebrania ilikuwa muhimu sana kama sifa wakilishi. Waalimu wa sheria za Kiyahudi walisema kwamba neno "Bwana" lilimfunua Mungu katika pendu lake, wema, na huruma. Tazama Mada Maalum katika 1:3.

☐ Tambua katika mist. 3-4 sifa nyingi zinatumiwa kutoa wasifu wa Mungu wa Israeli:

1. "ukuu" - BDB 152, kama vile 3:24; 5:24; 9:26; 11:2; 32:3; Hes. 14:19
2. kifungu "kazi yake ni kamilifu" - BDB 1071, chenye maana "kuwa na afya," "kuwa na heshima"
 - a. kilichomaanisha kazi ya Mungu, Kumb. 32:4
 - b. kilichomaanisha njia za Munngu, Zab. 18:30
 - c. kilichomaanisha sheria ya Mungu, Zab. 19:7-8
3. "njia zake zote ni haki" - BDB 1048, kama vile Mwa. 18:25; Ps. 33:5; 37:28; 99:4; 111:7; Isa. 5:16; 28:17;30:18; 61:8
4. "Mungu wa uaminifu" - BDB 53, kama vile Zab. 36:5; 88:11; 89:1,2,5,8,24,33,49; 92:2, 119:90; Isa. 25:1; Hosea 2:22
5. "Mungu ... asiye na uovu" - BDB 732, kama vile Ayubu 34:10, hili linashutumiwa nadai ya watu wake, Law.19:15,35; Kumb. 25:16

6. “Yeye ndiye mwenye haki” - BDB 843, kama vile Ayubu 34:17; Zab. 116:5; 119:137; 129:4; 145:17
7. “na adili” - BDB 449, kama vile Zab. 25:8; 92:15

☐ **“Mungu”** Neno hili linatokana na neno la Kiebrania *Elohim*. Tazama Mada Maalum katika 1:3.

32:4 “Mwamba” Jina hili (BDB 849) lilitumika kumaanisha Mungu katika mist. 15,18,30, na Zab. 18:1-2; 19:14; II Sam. 22:2 na kuendelea; Zab. 78:35; Isa. 44:8). Hili linazungumzia (1) nguvu, uimara, asili ya Mungu wa kweli asiyebadilika au (2) Mungu kama mkuu, ngome isiyonekana.

☐ **“kamilifu”** Neno la Kiebrania (BDB 1071) linamaanisha “kujitoshereza,” “timilifu,” “tosherevu” (kama vile II Sam. 22:31; Zab. 18:30).

Zitambue mbinu mbalimbali ambazo zimetumika kumwelezea YHWH (yaani, “ukuu wa Mungu,” mist. 3):

1. kazi yake ni kamilifu - BDB 1071
2. njia zake ni za haki - BDB 1048
3. Mungu wa uaminifu - BDB 53
4. Mungu asiye na uovu - BDB 732
5. Yeye ndiye mwenye haki - BDB 843
6. Yeye ni adili- BDB 449

Ni maelezo ya nguvu ya Mungu iliyoje ya uumbaji na wokovu. Mungu ambaye katika yeye wanadamu wote wanaweza kusadiki na kuwa na tumaini (mf. kwa sifa nyinginezo tazama Kut. 34:6; Hes. 14:18; Kumb. 4:31; Neh. 9:17; Zab. 103:8; 145:8).

☐ **“Mungu wa uaminifu”** Hili ni neno lile lile (BDB 53) linalotumika katika mst. 20 lenye kurejelea matendo ya mwanadamu. Hili linatafsiriwa kama “imani” katika Hab. 2:4, “mwenye haki ataishi kwa imani yake.” Kifungu hiki kinaonyesha kipaumbele ambacho Mungu amekiweka kwa waaminifu wake na mst. 20 unaonyesha kipaumbele alichokiweka katika imani ya watoto wake. Imani na neema zote ni dhana za kibiblia kuliko dhana za Agano Jipya. Njia pekee ya kuwa na mwitikio wa neema ya Mungu ni kupitia imani. Tazama Mada Maalum katika 1:32.

32:5 Kama YHWH anavyoelezwa katika mist. 3-4, sasa agano ni la watoto wake, ambao iliwapasa kuifunua tabia yake (kama vile mist. 3-4), lakini haikuwa hivyo, inavyoelezwa:

1. “Wametenda mambo ya uharibifu” - BDB 1007, KB 1469, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 4:16,25; 9:12; 31:29; Mwa. 6:12; Kut. 32:7; inaelezwa katika Zab. 14:1-3, mara nyingi inadokeza ibada ya sanamu
2. “Hawawi watoto wake” - BDB 119 kanushi
3. “hii ndiyo ila yao” - BDB 548
 - a. uharibifua ambao ulimtenga mtu katika huduma ya kikuhani, kama vile Law. 21:17,18,21,23, na wanyama kutotolewa kama sadaka, kama vile Law. 22:20-21; Kumb. 15:21; 17:1
 - b. mawaa ya kiroho, kama vile Law. 22:25; Ayubu 11:15; Mit. 9:
4. “ukaidi” - BDB 786 I, kama vile mist. 20, maana ya msingi inapotoshwa, yenye kudokeza hali yamawaa (sheria) sifa ya YHWH (haki)
5. “kilichopotoka” - BDB 836, linapatikana hapa, maana yake inafananishwa na #4

32:6 “Je! Yeye siye baba yako” Toleo la NIDOTTE, juzuu. 1, uk. 222, lina mapendekezo ya kufurahisha kuhusiana na stiari yenye kumzungumzia Mungu. Hii inatumika shingo upande katika Agano la Kale kwa sababu ya uhusiano yakini pamoja na ibada ya ustawi (mf. Yer. 2:27). Wimbo huu wa Musa ni moja ya matumizi ya kale sana ya kumwelezea Mungu (kama vile Kut. 4:22; Kumb. 1:31; 8:5 na baadaye katika manabii, kama vile Isa. 1:2; 63:16; Yer. 3:19; Hos. 11:1-3; Mal. 1:6). “ubaba” wa Mungu unatajwa katika mist. 6,18 na 19-20.

Ubaba huu wa wana wa Israeli walioungana unatambuliwa katika uhusiano na Mungu na ufalme wa Daudi (kama vile II Sam. 7:14; Zab. 2:7; na 89:26).

Stiari za kifamilya (baba-mwana; mume-mke) ni njia zenye nguvu zaidi za kueleza uhusiano ambao Mungu aliukusudia pamoja na uumbaji wa mwandamu wake (aliyeumbwa kwa sura na mfano wake). Wanadamu wanaweza kuuelewa undani wa hisia za Mungu na kujitoa kwake kupita ufanano wa uzoefu huu wa misingi ya mwanadamu (yaani, familia, ndoa, watoto).

32:6-14 Sehemu hii inaendeleza sifa bainifu za Israeli na kuanza kwa mashtaka ya kisheria dhidi yao kwa kutaja yale yote ambayo YHWH ameyafanya kwao:

1. Matendo yao kwa YHWH
 - a. “wapumbavu” - BDB 614 I, kama vile Mst. 21
 - b. “wajinga” - BDB 314, kinyume katika mst. 29; 4:6; Zab. 107:43
2. Matendo ya YHWH kwao:
 - a. Alikuwa Baba yao, mst. 6 - BDB 888 I, KB 1111, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
 - b. Aliwaumba, mst. 6 - BDB 793 I, KB 889, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Mwa. 14:19,22 (hii inaweza kurejelea uumbaji asilia, bali katika muktadha huu, Anawatambulisha kama taifa katika Kutoka)
 - c. Amewaweka imara, mst. 6 - BDB 465, KB 464, *Polel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, Ayubu 31:15; Isa. 62:7
 - d. Aliwakuta, mst. 10 - BDB 592, KB 679, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - 1) katika nchi ya ukame
 - 2) katika jangwa tupu litishalo
 - e. Aliwazunguka, mst. 10 - BDB 685, KB 738, *Polel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, yani, kwa ajili ya ulinzi
 - f. Aiwatunza, mst. 10 - BDB 106, KB 122, yaani, kwa ajili ya ulinzi, yaani., kwa kuwaangalia kwa umakini (hapa pekee)
 - g. Aliwahifadhi, mst. 10 - BDB 665, KB 718, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Zab. 25:21; 31:23; 41:11-12; 61:7; Isa. 26:3; 42:6; 49:8
 - h. Aliwatunza Mfano wa tai ataharikishaye kitoto chake, mst. 11, kama vile Kut. 19:4
 - 1) “Na kupapatika juu ya makinda yake” - BDB 734, KB 802, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, yaani, kwa matendo yake
 - 2) “kupapatika” - BDB 934, KB 1219, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Mwa. 1:2
 - 3) aliwafundisha watoto kuruka
 - a) alikunjua mabawa zake - BDB 831, KB 975, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
 - b) aliwatwaa - BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - c) aliwachukua - BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - i. Aliwaongoza, mst. 12 - BDB 634, KB 685, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - j. Alimpandisha mahali pa nchi palipoinuka, mst. 13 - BDB 938, KB 1230, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Isa. 58:14
 - k. Aliwanyonyesha, mist. 13-14
 - 1) “akala” - BDB 37, KB 46, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - 2) “akamnyonyesha” - BDB 413, KB 416, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
 - 3) “akanywa” - BDB 1059, KB 1667, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

32:7 Kuna amri nyingi katika mstari huu zinazohuisiana na wana wa Israeli kuukumbuka uangalizi na utoaji wa YHWH:

1. “Kumbuka” - BDB 269, KB 269, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. “Tafakari” - BDB 106, KB 122, *Qal* KAULI YA WAKATI ISIO TIMILIFU
3. “Mwulize” - BDB 981, KB 1371, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
4. “Wazee wako, nao watakuambia” - BDB 616, KB 665, *Hiphil* KITENZI AMRISHI

Hii ilikuwa habari ya kihistoria iliyoshuhudiwa katika (1) tamaduni ya kihenga iliyopo kizazi hata kizazi (kama vile 4:9-10; 6:7,20-25; 11:19; 32:46) na (2)Wimbo huu wa Musa ndiyo uliotoa ushuhuda dhidi ya wana wa Israeli!

32:8 Mstari huu unadai kwamba Mungu wa wana wa Israeli pia ndiye Mungu pkee (kama vile 4:35,39; Isa. 54:5; Yer. 32:27). Yeye na ndiye pekee awekaye mipaka ya mataifa yote (kama vile 2:5,9,19; Mwanzo 10). Hii si imani ya kumpa heshima mungu mmoja, bali Imani katika Mungu!

▣ **“Yeye Aliye Juu”** Hili jina linalomaanisha Mungu (BDB 751) linatumika katika Hes. 24:16 (*Elyon*). Hili linaonekana kuwa kifupi cha neno *El Elyon* (kama vile Mwa. 14:18,19,20,21; Zab. 78:35). Jina hili la Uungu linatumika katika mahusiano na “mataifa” (kama vile Zab 47:1-3). Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.



NASB “Kwa kadiri ya hesabu ya wana wa Israeli”
NKJV, NJB “Kwa kadri ya idadi ya wana wa Israeli”
NRSV “Kwa kadri ya idadi ya miungu”
TEV “alichagua kulifundisha taifa mambo ya kimbingu”
REB “kwa kadri ya idadi ya wana wa Israeli”

Tafsiri ya Maandiko ya Kiebrania ina kifungu “hesabu ya tai wa Mungu” (*El*). Tafsiri hii inaonekana kuendana vema (kv. *The Jewish Study Bible*, uk. 441) kwa sababu: (1) kv. 29:26; (2) inaufuatisha usomaji wa gombo lililopatikana ndani ya pango miongoni mwa magombo manne ya Qumran; (3) malaika wa kila taifa mataifa wanaotajwa katika Danieli 10 na 12. Malaika alitumwa kila taifa (kv. Dan. 10:13), lakini wana wa Israeli wlikuwa na YHWH (japo Mikaeli pia anasemekena kuwa malaika wa wana wa Israeli, kv. Dan. 12:1).

32:9 “sehemu ya Bwana ni watu wake” Kwa upande mwingine sehemu ya watu wake ni Mungu Mwenyewe (kv. Kut. 19:5; Zab. 16:5; 73:26; Omb. 3:24). Waisraeli walikuwa katika maana ya kipekee ya watu wa kipekee wa YHWH (kv. 4:20;7:6; 14:2; 26:18). Tazama Mada Maalum: Upendeleo wa Kiinjilisti wa Bob katika 4:6.

32:10 “Alimkuta katika nchi ya ukame,

Na katika jangwa tupu litishalo” Hili ni dokezo la uchaguzi wa YHWH wa Israeli katika maneno ya msistizo (kv. Yer. 2:23-; Hos. 2:14-15). Taswira hii inaongeza wazo la uhamisho (kv.1:19). Hii inaeleza juu ya pendo la awali la YHWH kwa Israeli kupitia matumizi stiari yenye nguvu (kama vile 10:14-15; Amosi 3:2).

Kuna njia mbili zenye mkanganyiko katika fasihi ya Musa ya kutathmini kipindi cha kutangatanga jangwani:

1. kipindi cha imani na uaminifu
 - a. Kumb. 32:10-14
 - b. Yer. 2:1-3
 - c. Hosea 2:14-23
2. kipindi cha kukosa uaminifu
 - a. Hes. 14:1-17:11
 - b. Kumb. 1:26-33
 - c. Zab. 95:8-11
 - d. Hosea 9:10-14
 - e. Yer. 2:4-13
 - f. Ezekieli 23

▣ **“mboni ya jicho”** Katika lugha ya Kiingereza hili lingekuwa “kipenzi chake.” Hii ni stiari nyingine yenye kudokeza Israeli kama mwana wa pekee (kama vile Zab. 17:8). Kiuhalisia kwa Kiebrania ni “mtu mdogo wa jicho lake.”

32:11

NASB, NKJV “Mfano wa tai. . . ataharikishaye kioto chake”
NRSV “mfano wa tai avizingiravyo kiota chake”
TEV “mfano wa tai akilindavyo kiota chake”
NJB “kama tai akilindavyo kitoto chake”

Hili linamuonyesha Mungu kama mzazi alindaye na mwenye nguvu sana (kama vile mst. 19). Dhana hii ya Mungu kama tai ni ile ya Mungu kama kuku avifunikavyo vifaranga vyake (kama vile mst. 18; Mwa. 1:2; Kuto. 19:4; Mt. 23:37; Luka 13:34). Uungu unaelezwa katika jinsi zote ya kiume (kv. 6) na ya kike (kv. 11). Tafsiri za toleo la NJB na REV zinaifuatisha tafsiri ya Maandiko ya Kale ya Kiebrania.

MADA MAALUM: KIVULI [(kwa kutumia vifungu kadhaa vyenye uhusiano)]

Hii ni Nahau ya Kiebrania yenye kumaanisha

1. "kivuli" kama ulinzi
 - a. wa YHWH – Isa. 16:3-4
 - b. wa Misri – Isa. 30:2-3
 - c. wa Masihi wa YHWH – Omb. 4:20
1. "kivuli cha makono," pia ulinzi wa YHWH – Zab. 121:5; Isa. 49:2; 51:16; pia muhtasari wa Kut. 33:22)
2. "kivuli cha paa langu," Nahau nyingine kwa ajili ya ulinzi – Mwa. 19:8
3. "kivuli cha wingu maalumu la YHWH kipindi cha wakati wa kutangatanga jangwani" (yaani, kivuli wakati wa mchana, nuru wakati wa usiku lililowaongoza wao) – Kut. 13:21-22; 14:19,20,24; Isa. 4:6; 25:4-5; 32:1-2
4. "kivuli cha mbawa" – Nahau ya Kiebrania ya Mungu kama ndege mwenye kuwalinda vifaranga vyake – Zab. 17:8; 36:7; 57:1; 61:4; 91:1,4; Isa. 31:5 (stiari ile ile katika Kumb. 32:10-11; Ruthu 2:12; Mt. 23:37; Luka 13:34)
5. "kivuli cha mti"
 - a. mfano katika mahusiano na Abimeleki – Amu. 9:15
 - b. mfano wa tai na mzabibu – Ezek. 17:23
 - c. mfano wa Misri – Ezek. 31:6,17
 - d. ndoto ya Nebukadreza – Dan. 4:12
 - e. tawsira ya mateka wa Israeli – Hosea 14:7

Kivuli kilikua na nguvu, stiari ya kuokoa maisha kwa watu wa jangwani.

32:12 “Bwana peke yake alimwongoza” Neno hili (BDB 94) linatumika kudhihirisha uhusiano wa YHWH uliotengekwa kwa Israeli. Yeye na ndiye aliwaongoza kwa upekee!

32:13 “Alimpandisha mahali pa nchi palipoinuka” Stiari hii yenye kumaanisha utele wa YHWH (kama yale yote ya mst. 14) wanapewa wana wa Israeli (kv. Isa. 58:14; Hab. 3:19).

☑ **“asali iliyotoka jabalini”** Hili linairejelea asali ya nyuki wa mwituni, ambao mara nyingi waliishi ndani yanyufa za majabali (kv. Zab. 81:16).

☑ **“mafuta yaliyotoka katika mwamba wa gumegume”** Kifungu hiki kinairejelea miti ya mizeituni ya jangwani ambayo iliota mahali ambapo hata majani yasingeota. Mistari 13 na 14 inazungumzia utele wa mazao ya Nchi ya Ahadi.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 32:15-18

¹⁵ Lakini Yeshuruni alinenepa, akapiga teke;

Umenenepa, umekuwa mnene, umewanda;

Ndipo akamwacha Mungu aliyemfanya, Akamdharau Mwamba wa wokovu wake.

¹⁶ Wakamtia wivu kwa miungu migeni,

Wakamkasirisha kwa machukizo.

¹⁷ Walitoa sadaka kwa pepo, si Mungu,

Kwa miungu wasiyojua, Kwa miungu mipya iliyotokea siku zilizo karibu,

Ambayo baba zenu hawakuigopa.

32:15 “Yeshuruni” Neno hili limamaanisha “mnyoofu” (BDB 449), na jina la kiushairi la Israeli (kv. 33:5,26; Isa. 44:2, tazama Mada Maalum: Jina Israeli katika 1:1). Huu ni mtindo wa kejeli (yaani, mist. 15-16).

▣ **“akapiga teke”** KITENZI hiki (BDB 127, KB 142, *Qal* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU) kinatumika mara mbili tu katika Agano la Kale na kuonekana kuwa stiari ya kukataa (kama vile I Sam. 2:29). Kama teke la ng’ombe kwa wamiliki wake ndivyo alivyo Israeli kwa Mungu wake!

32:15-18 “alinenepa” Israeli alipobarikiwa (kv. 31:20) alimkataa YHWH:

1. “walimwacha Mungu aliyewaumba” (kv. 6) - BDB 643, KB 695, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 31:16,17; Amu.10:6
2. “aliudharau Mwamba wa wokovu wake” (kv. Mst. 4) - BDB 614, KB 663, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, huu ni muundo wa KITENZI wa KIVUMISHI “wapumbavu,” kinachopatikana katika mst. 6 (kv. Zab. 74:18)

Ni kwa namna gani Israeli “alimwacha” na “kumdharau” YHWH?

1. kwa kumtia wivu kwa miungu migeni, mst. 16
2. kwa kumkasirisha kwa machukizo, mst. 16
3. kwa kutoa sadaka kwa pepo, si Mungu, mst. 17
 - a. ambao hawakujulikana
 - b. miungu mipya
 - c. wasiojulikana kwa baba zao
4. waliukataa Mwamba, mst. 18 - BDB 1009, KB 1477, *Qal* HALI YA KUSIHI lakini iliyo katika maana ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (hapa tu)
5. wakamsahau Mungu wao, mst. 18 - BDB 1013, KB 1489, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kv. 4:23, kulisahau agano ni kumsahau YHWH

32:17 “Walitoa sadaka kwa pepo, si Mungu” Dhana hii pia inatumika katika Zab. 106:37. Kitabu cha Agano la Kale kinazungumza kwa uchache sana kuhusu malaika na pepo. Paulo anadokeza juu ya mstari huu katika I Kor. 10:20.

MADA MAALUM: MALAIKA NA PEPO KATIKA AGANO LA KALE

- A. Watu wa kale waliamini kwamba viumbe vyote vina uhai. Walifikiri kwamba sifa za mwanadamu ni sawa na nguvu ya asili, wanyama, na viumbe vya asili. Maisha yalielezeka kupitia mwingiliano wa uwepo wa vitu/viumbe hivi na wanadamu.
- B. Mifano hii wakati mwingine ilileta matokeo ya kuabudu miungu mingi (miungu wengi). Kwa kawaida mapepo (*genii*) ilikuwa miungu midogo au nusu miungu (mizuri au miovu) ambao ilileta matokeo kadha wa kadha katika maisha ya watu binafsi.
 1. Machufuko na migogoro huko Mesopotamia,
 2. Mpangilio na kazi huko Misri,
 3. Kanaani, tazama W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel*, Toleo la Tano, kur. 67-9
- C. Agano la Kale halielezi sana au kukuza jambo la miungu wadogo, malaika, au pepo, huenda ni kwa sababu ya msistizo wake mkali unaozungumzia Imani ya Mungu mmoja (tazama Mada Maalumu : Mungu mmoja_ Imani ya Mungu mmoja kama vile Kut. 8:10; 9:14; 15:11; Kumb. 4:35,39; 6:4; 33:26;

Zab. 35:10; 71:19; 86:8; Isa. 46:9; Yer. 10:6-7; Mik. 7:18). Haliizungumzii miungu ya uongo ya mataifa ya wapagani (*Shedim*, BDB 993, kama vile Kumb. 32:17; Zab. 106:37) na halitaji majina au kufananisha baadhi yao.

1. *Se'im* (mazimwi au majitu yenye manyoya, BDB 972 III, KB 1341 III, kama vile Law. 17:7; 2 Nya. 11:15; Isa. 13:21; 34:14)
2. *Lilith* (jike, pepo apotoshaye kizunifu nyakati za usiku, BDB 539, KB 528, kama vile Isa. 34:14)
3. *Mavet* (neni la Kiebrania liliotumika kumtaja mungu mwovu wa Wakanani, Mot, BDB 560, KB560, kama vile Isa. 28:15,18; Yer. 9:21; na kwa kadri iwezekavyo Kumb. 28:22)
4. *Resheph* (mahali, moto, au mawe yenye kutiririsha mvua ya mawe, BDB 958, KB 958, kama vile Kumb. 32:24; Zab. 78:48; Hab. 3:5)
5. *Dever* (uharibifu, BDB 184, kama vile Zab. 91:5-6; Hab. 3:5)
6. *Az'azel* (jina halina uhakika, lakini huenda akawa pepo wa jangwani au jina la mahali, BDB 736, KB 736, kama vile Law. 16:8,10,26)

(Mifano hii inachukuliwa kutoka *Encyclopedia Judaica*, juzuu I. 5, uk. 1523.).Hata hivyo, hakuna imani ya Mungu wawili au uhuru wa malaika kutoka kwa YHWH katika Agano la Kale. Ibilisi chini ya YHWH (kama vile Ayubu 1-2; Zekaria 3), hayuko huru, ni adui anayejiongoza (kama vile A. B. Davidson, *A Theology of the Old Testament*, kr. 300-306).

- D. Dini ya Kiyahudi iliendelezwa kipindi cha uhamisho wa Babeli (586-538 b.k). Kitheolojia iliathiriwa aina mbili za Kiajemi zilizochukua nafasi kwa wafuasi wa Zoroaster, mungu mkuu na mzuri alitwa Mazda au Ormazd na mpinga uovu aitwaye Ahriman. Huyu aliruhusiwa ndani ya dini ya Kiyahudi baada ya uamisho na kuwa mfano wa aina mbili kati ya YHWH na malaika Zake na Ibilisi malaika zake au pepo.

Theolojia ya dini ya Kiyahudi yenye kutoa mfano wa uovu inaelezwa na kunakiliwa vema katika Edersheim ya Alfred *The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII (kur. 749-863) na XVI (kur. 770-776). Dini ya Kiyahudi ilitoa mifano ya uovu katika njia tatu.

1. Ibilisi au Malaika wa maangamizi
2. kusudi la uovu (yetzer hara) ndani ya mwandamu
3. Malaika wa Mauti

Edersheim anayabainisha haya kama

1. Mshitaki
2. Mjaribu
3. Mwadhibishaji (juzuu. 2, uk. 756)

Kuna tofauti zinazodhihirika kitheolojia kati ya dini ya Kiyahudi iliyokuwepo baada ya uhamisho na nanma uwasilishaji na maelezo ya uovu inavyofanyika ndani ya Agano Jipya.

- E. Agano Jipya, haswa Injili, linadai uwepo na upinzani wa uovu wa viumbe vya kiroho kwa mwanadamu na kwa YHWH (katika dini ya Kiyahudi, Ibilisi alikuwa adui wa mwanadamu, lakini si kwa Mungu). Hawa wanayapinga mapenzi ya Mungu, amri, na ufalme.

Yesu alikabiliana na kuvifukuza hivi viumbe vya kimapepo, pia viliitwa (1) roho chafu (kama vile. Luka 4:36; 6:18) au (2) roho za uovu kama vile. Luka 7:21; 8:2), kutoka kwa wanadamu. Yesu kwa udhuhinisho alitengeneza tofauti kati ya maradhi (kimwonekano na kiakili) na hali ya kimapepo. Aliithibitisha nguvu Yake na mtazamo wa ndani wa kiroho kwa kuwatambua na kuwafahamu hawa pepo wabaya. Mara nyingi walimtambua na kumwita, lakini Yesu aliukataa ushuhuda wao, alihitaji wawe kimya, na kuyafukuzia mbali. Utambuzi wa pepo hawa ni ishara ya kuvunja ufalme wa Ibilisi.

Kuna upungufu wa ajabu wa habari ndani ya barua za Kitume za Agano Jipya kuhusiana na somo hili. Utambuzi huu kamwe haukuorodhesha karama za kiroho, wala methodolojia au hatua yake iliyotolewa kwa ajili ya vizazi vijavyo vya huduma au waamini.

- F. Mwovu yu dhahiri; mwovu ni mtu binafsi; mwovu yupo. Si asili yake wala kusudi lake linalofunuliwa. Biblia inatetea ukweli wake na kwa ukali inapinga ushawishi wake yule mwovu. Ndani ya ukweli hakuna hatima yenye mitazamo yenye uwili ndani yake. Mungu yu ndani ya utawala wake mwenyewe; mwovu anaangamizwa na kuhukumiwa na ataondolewa kutoka katika uumbaji.

- G. Watu wa Mungu yawapasa kumpinga mwovu (kama vile Yakobo 4:7). Hawawezi kutawaliwa na naye

(kama vile 1 Yohana 5:18), bali wanaweza kujaribiwa na ushuhuda na ushawishi wake kuangamizwa (kama vile Efe. 6:10-18). Mwovu ni sehemu ya mtazamo wa ulimwengu kwa wakristo uliofunuliwa. Wakristo wa sasa hawana haki ya kueleza wazi kwa mara nyingine (kutafasiri upya maandishi ya Rudolf Baltmann); kuyaua maovu (miundo ya kijamii ya Paul Tillich), wala kujaribu kuelezea kwa ukamilifu katika namna ya kisaikolojia (Sigmund Freud). Ushawishi wake umeenea kote, lakini umeangamizwa. Waamini wanahitaji kuenenda ndani ya ushindi wa Kristo!

MADA MAALUMU: UOVU BINAFSI

I. SOMO KUHUSU SHETANI NI NGUMU SANA

- A. Agano la Kale halibainishi adui mkubwa wa (Mungu), bali mtumishi wa YHWH ambaye anawapa wanadamu mbadala na kutuhumu huyu mwanadamu kwa kutokuwa na haki (A. B. Davidson, *A Theology of the OT*, kur. 300-306).
- B. Dhana ya adui mkubwa wa Mungu ulianza wakati wa fasili kati ya Biblia (zisizo na taratibu za kikanisa) katika kipindi cha dini ya kiislamu iliyoanzishwa na Zoroaster huko Uajemi. Hii kwa namna nyingine, kwa kiwango kikubwa ilisababisha sheria ya dini ya Kiyahudi (yaani, waliokuwa wametengwa na kuishi nje ya Israel yaani Babiloni, na Uajemi).
- C. Agano Jipya linaunda dharura ya Agano la Kale katika ugumu wa ajabu lakini makundi yaliyochaguliwa kama mtu anaanza kusoma habari za uovu katika mtizamo wa thiolojia ya biblia (kila kitabu au mwandishi au michoro alisoma na kuandika kwa kifupi kwa kutenganisha) basi mawazo mbalimbali kuhusu uovu yangeibuliwa. Hata hivyo, mtu ataanza kusoma kuhusu uovu lakini kwa njia isiyo ya kibiblia au nje zaidi ya biblia mfano dini za kiulimwengu au dini za mashariki, basi sehemu kubwa ya mambo mengi ya maendeleo ya Agano Jipya yalionyeshwa katika pande mbili za uajemi na tabia za uyunani na kiroma.

Kama mtu alidhaniwa kujitoa kwa uwezo wa kiungu neno la Mungu (kama nilivyo!), kwa hiyo mambo ya Agano Jipya lazima yaonekane kama ufunuo endelevu. Wakristo yawapasa wajilinde dhidi ya kuruhusu simulizi za Kiyahudi au fasihi za Kiingereza (yaani, Dante, Milton) kufafanua zaidi dhana hiyo bila shaka miujiza na maana tofauti tofauti katika eneo hili la wokovu. Mungu amechagua kutobainisha mambo yote ya uovu, asili yake (tazama Mada Maalumu: Lusifa), kusudi lake, lakini amebainisha kushindwa kwake!

II. SHETANI KATIKA AGANO LA KALE

Katika Agano la kale neno "Shetani" (BDB 966, KB 1317) au "mshitaki" linaonekana kuhusiana na makundi matatu tofauti.

- A. Washtaki wa wanadamu (1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 5:4, 11:14,23,25; Zab. 109:6,20,29)
- B. Washtaki wa malaika (Hes. 22:22-23; Zak. 3:1)
 1. Malaika wa Bwana – Hes. 22:22-23
 2. Shetani – 1 Nya. 21:1; Ayubu 1-2; Zak. 3:1
- C. Washtaki wa kimapepo (bila shaka shetani) (1 Fal. 22:21; Zak. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha kuingia agano jipya ibilisi wa Mwanzo 3 alijulikana ni shetani (kama vile Kitabu cha Hekima 2:23-24; II Enoch 31:3), na hata baadaye ambapo anakuja kuwa chaguo la viongozi wa kidini wa Uyahudi (kama vile Sot 9b na Sanh. 29a). "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 wanakuwa malaika wa uovu katika I Enoch 54:6. Wanakuwa waanzilishi wa uovu katika thiolojia ya viongozi wa kidini wa Kiyahudi. Nalitaja hili sio kwa kuonyesha usahihi wake wa kithiolojia, bali kuonyesha maendeleo yake katika Agano Jipya, shuguli hizi za Agano la Kale zinachangia katika uovu wa malaika wa nuru (yaani shetani,)katika 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9.

Asili ya uovu wa yule aliyejigeuza kuwa malaika wa nuru ni mgumu au haiwezekani (kutegemea maoni yako) kuupima toka katika Agano la Kale. Sababu moja wapo ni ile imani ya nguvu juu ya uwepo wa Mungu mmoja tu. (kama vile Kumb. 6:4-6; 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amosi 3:6). Majeruhi wote walipelekea YHWH kuonyesha kwa vitendo alivyo wa pekee na mkuu (kama vile. Isa. 43:11;

44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Uwezekano wa vyanzo vya habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo shetani ni mojawapo wa wana wa Mungu "mwana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14; Ezekieli 28, ambapo ujivuni karibu na wafalme wa mashariki (Babiloni na Uturuki) wamekuwa wakielezea sifa au ujivuni wa shetani (kama vile. 1 Tim. 3:6). Nimechanganya mihemko kuhusu kuliendea suala hili. Ezekieli anatumia bustani ya Edeni kama neno mbadala sio tu kwa mfalme wa Uturuki kama shetani (kama vile Ezek. 28:12-16), lakini pia kwa ufalme wa Misri kama mti wa maarifa wa mema na mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa kurasa 12-14, anaonekana kuelezea uasi wa malaika kupitia majivuno kama Mungu alivyotaka kubainisha kwetu jinsi alivyo hasa na asili ya shetani hii ni njia isiyo elezea moja kwa moja na mahali pa kuifanya (tazama Mada Mada Maalumu: Lusifa). Lazima tujilinde dhidi ya mwenendo wa Theolojia wa kuchukua sehemu ndogo ndogo, tata toka kwenye maeneo yenye maana mbalimbali ya waandishi, vitabu, na kuviunganisha kama vipande vipande vya fumbo la Kiungu.

III. SHETANI KATIKA AGANO JIPYA

Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII [kur.. 748-763] na XVI [kur. 770-776]) anasema mafundisho ya sheria za Kiyahudi yameathiriwa wazi kabisa na umiliki wa pande mbili za Uajemi na mtizamo wa kimapepo. Viongozi hawa wa kidini sio vyanzo vizuri vya ukweli katika eneo. Yesu kimsingi anakwepa kutoka kwenye mafundisho ya sinagogi. Nafikiri kuwa dhana ya viongozi wa dini ya kiyahudi ya upatanisho wa kimalaika (kama vile Matendo 7:53) na upinzani katika kutoa sheria za Musa kwenye mlima Sinai ilifungua mlango kwa dhana ya adui mkuu wa YHWH kadhalika na mwanadamu. Palikuwa na Mungu wawili wa pande mbili za Iran (ufuasi wa Zoroaster).

1. *Ahura Mazda*, baadaye akaitwa *Ohrmazd*, aliyekuwa mungu muumbaji, mungu mwema
2. *Angra Mainyu*, baadaye alitwa *Ahriman*, roho aangamizaye, mungu mwovu,

Vita juu ya ukuu na dunia ikawa kama uwanja wa vita. Umiliki wa pande mbili ukajengeka ndani ya pande mbili za Kiyahudi zenye ukomo kati ya YHWH na shetani.

Hakika kuna mafunuo endelevu katika agano Jipya kama ilivyo kwenye uovu, lakini sio kama ilivyo elezewa kama walimu wa dini ya Kiyahudi wanavyodai. Mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita vya mbinguni." Kuanguka kwa shetani (Mwovu) ni mantiki yenye umuhimu, lakini sehemu husika haikutolewa (Tazama Mada Maalumu: Kuanguka kwa shetani na malaika wake). Hata hivyo kile kilichotolewa kimefichika kwenye mafunuo tanzu (k.v. Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa shetani ameshindwa na kutupwa duniani, bado anatenda kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20).

Lazima tuthibiti kiu yetu katika eneo hili. Kuna nguvu binafsi ya majaribu na uovu lakini bado kuna Mungu mmoja tu na mwanadamu bado anawajibika kwa uchaguzi wake. kuna vita ya kiroho kabla na baada ya wokovu. Ushindi wawezakuja tu na kubakia ndani na kupitia Mungu wa Utatu. Uovu umekwisha shindwa na utaondolewa (kama vile Ufu. 20:10)!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 32:19-22

¹⁹ Bwana akaona, akawachukia,

Kwa sababu ya kukasirishwa na wanawe na binti zake.

²⁰ Akasema, Nitawaficha uso wangu,

Nitaona mwisho wao utakuwaje;

Maana, ni kizazi cha ukaidi mwingi,

Watoto wasio imani ndani yao.

²¹ Wamenitia wivu kwa kisicho Mungu;

Wamenikasirisha kwa ubatili wao;

Nami nitawatia wivu kwa wasio watu, Nami nitawakasirisha kwa taifa lipumbaalo.

²² Maana, moto umewashwa kwa hasira yangu,

Unateketea hata chini ya kuzimu,

Unakula dunia pamoja na mazao yake,

32:19-22 Aya hii ni marudio ya dhima zilizopita. Ushairi huu umerudiwa sana. Watu wa Agano la Mungu walimkataa na yeye aliwakataa (kama vile Hosea 1:9; 2:23; Rum. 9:25). Kuwakataa kwake (yaani, hasira) ni kwa sababu mapatano. Yeye atatumia “watu” kumchokoza Israeli mwenye wivu (na tumaini la imani, kama vile Rum. 11:11,14).

Kwangu mimi hili linaonekana kuwa vema kama ulivyo mjadala wa Paulo ulio katika Warumi 9-11. Hata Paulo anaunukuu mst. 21 katika Rum. 10:19! Kejeli iliyoongezwa ni ile kwamba Israeli alimwacha YHWH kwa sababu ya miungu isiyo na uhai (yaani, yenye majisifu, kv. Yer. 2:13). Jamani, huu ni upumbavu wa mwanadamu kuiabudu miungu (kv. Isa. 40:19-20; 44:9-20; Yer. 10:3-5,14)!

32:20 “Nitawaficha uso wangu” Hii ni stiari ya uhasama wa uangalizi binafsi na uzingativu wa YHWH (kv. 31:17-18).

☐ **“Maana, ni kizazi cha ukaidi mwingi, Watoto wasio imani ndani yao”** Mistari hii miwili inaeleza huzuni ya Israeli ambaye alikuwa na uangalizi na uwepo maalum wa YHWH (kv. Rum. 9:4-5). Haya yanabainishwa kama:

1. ukaidi (BDB 246) – mara nyingi hili neno linatumika katika Mithali (kv. 2:12,14; 6:14; 8:13; 10:31,31; 16:30; 23:33). Hili lilihusiana na neno la Kiebrania “uzushi” (BDB 246), ambao humweka mtu katika mapotoe au hali ya mageuzi.
2. kukosa uaminifu (BDB 53 kanushi) – neno hili pia ni la kawaida katika kitabu cha Mithali (kama vile 13:17; 20:6; pia tambua Zab. 31:23; Isa. 26:3; tazama Mada Maalum katika 1:32).
3. ubainishaji huu una ufanano na 32:5:
 - a. ukaidi (BDB 786 I)
 - b. kupotoshwa (BDB 836)

YHWH ndiye mwimili au mtawala sahihi (tazama Mada Maalum katika 1:16). Watu wa Agano lake wamekengeuka kwa kuuacha mwimili huu.

☐ **“Nitaona mwisho wao utakuwaje”** YHWH alikuwa amemwonyesha Musa mapema hali itakayojiri kuwahusu wana wa Israeli katika 31:29, kama alivyfanya baadaye katika Yohana katika 24:19.

32:21 “kisicho Mungu” Kiuhalisia hii ni “kitu chenye kudhaaniwa” au “majivuno” (BDB 210) na kinawakilisha kile kisicho na thamani au kisichoishi. Hapa, kama Yer. 2:5; 8:19; 10:14-15; 16:19-20, kifungu hiki kinamaanisha miungu. Tazama ubunifu wa neno lililo katika Isa. 57:13.

32:22 Mstari huu ni stiari ya maangamizi ya jumla na hukumu ambayo Mungu ataiteta juu ya Israeli iliyo asi (kv. Yer. 15:14; 17:4). Uumbaji wote wa Mungu (yaani, nchi, *sheol*) unaharibiwa! Hii si rejea ya mahali pa adhabu ya milele.

MADA MAALUMU: WALIOKUFA, WAKO WAPI? (SHEOL/HADES, GEHENNA, TARTARUS)

- I. Agano la Kale
 - A. Watu wote wanakwenda shimoni (*sheol*) (hakuna mizizi yenye chanzo kimoja cha neno na asili ya neno lenyewe haijulikani, BDB 982, KB 1368), ambayo ndiyo ilikuwa njia ya kurejerea mahali pale wafu wanaishi au kaburi, hasa hasa katika kitabu cha Ayubu na Isaya. Katika Agano la Kale ilikuwa ni kivuri, utambuzi, lakini maisha yasiyo na furaha (kama vile Ayubu 10:21-22; 38:17)
 - B. Tabia za shimoni (*sheol*)
 1. Inahusiana na hukumu ya Mungu (moto), Kumb.32:22

2. Gereza lenye vizuizi, Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18
3. eneo ambalo huwezi rudi tena, Ayu. 7:9 (sifa ya mkazi wa Akkad kwa ajili ya umauti)
4. Eneo/ulimwengu wa giza, Ayu. 10:21-22; 17:13; 18:18
5. Mahali penye utulivu, Zab.. 28:1; 31:17; 94:17; 115:17; Isa. 47:5
6. panahusiana na mateso hata kabla ya siku ya hukumu, Zab. 18:4-5
7. panahusiana na *utelekezaji* (maangamizo; angalia Mada Maalumu: *Kutelekezwa. . Apollyon*), ambapo pia Mungu yupo, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Amo. 9:2
8. panahusiana na “shimo lefu” (kaburi), Zab.16:10; 88:3-4; Isa. 14:15; Ezek. 31:15-17
9. waovu hushuka ndani ya shimo la *sheol*, Hes. 16:30,33; Ayu. 7:9; Zab.. 55:15
10. mara nyingi hujibadilisha kama mnyama mwenye mdomo mkubwa, Hes. 16:30; Mith. 1:12; Isa. 5:14; Hab. 2:5
11. kule watu huitwa *Repha'im* (yaani., "roho za mauti"), Ayu. 26:5; Mith. 2:18; 21:16; 26:14 Isa. 14:9-11)
12. Hata hivyo, YHWH yupo hata hapa, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Mithali. 15:11

II. Agano Jipya

- A. Kwa Kiebrania *Sheol* limetafasiliwa kwa Kiyunani kama Kuzimu (ulimwengu usio onekana)
- B. Tabia za kuzimu (nyingi zinafanana kama za *Sheol*)
 1. Anarejerea mauti, Mt. 16:18
 2. imehusianishwa na mauti, Ufu. 1:18; 6:8; 20:13-14
 3. mara nyingi panafanana na mahali pa mateso ya milele (Gehenna), Mt. 11:23 (nukuu toka agano la kale); Lk. 10:15; 16:23-24
 4. mara nyingi inafanana na kuwekwa kaburini, Lk. 16:23
- C. Yumkini imegawanywa na (walimu wa dini ya Kiyahudi)
 1. Sehemu ya watakatifu iitwayo Paradiso (ki-ukweli ni jina lingine la Mbinguni, kama vile. 2 Kor. 12:4; Ufu. 2:7), Lk. 23:43
 2. Sehemu ya waovu iitwayo “kwenye vifungo vya giza”, iliyoko chini kabisa ya kuzimu, 2 Petr 2:4, mahali palipowekwa kwa ajili ya malaika waovu (k.v Mwanzo 6; I Enoch). Inahusiana na kutupwa “shimoni” Luk. 8:31; Rum. 10:7; Ufu. 9:1-2,11; 11:7; 17:18; 20:1,3
- D. *Gehenna*
 1. inaangazia kwenye kifungu cha agano la kale, “bonde la wana wa Hinnom (kusini mwa Yerusalem). Palikuwa ni mahali Wafoenike walipoichoma miungu ya , Molech (BDB 574, KB 591), ilikuwa inaabudiwa wakati wa kuwadhabihu watoto (kama vile 2 Fal. 16:3; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6), ambavyo ilikuwa imekataliwa katika Law. 18:21; 20:2-5.
 2. Yeremia alibadili toka sehemu ya ibada ya wapagani kuwa mahali pa hukumu ya YHWH (Kama vile Yer. 7:32; 19:6-7). Ikajakuwa mahali pa hukumu kali, ya milele katika I Enoch 90:26-27 na Sib. 1:103.
 3. Wayahudi wa enzi ya Yesu waliogopeshwa na ushiriki wa wazee wao katika ibada ya kipagani kwa kuwadhabihu watoto, kwamba waliigeuza sehemu hii kuwa sehemu ya kutupa takataka kwa ajili ya Jerusalemu. Mingi ya misemo ya Yesu kwa ajili ya hukumu ya milele ilitokana na sehemu hii iliyojaza (moto, moshi, minyoo, funza, kama vile Mk 9:44,46). Neno Gehenna limetumiwa na Yesu tu (hasa katika Yakobo 3:6).
 4. Matumizi ya Yesu juu ya neno Gehenna
 - a. Moto, Mt. 5:22; 18:9; Mk. 9:43
 - b. Mahali pa milele, Mk. 9:48 (Mt. 25:46)
 - c. mahali pa maangamizo (kwa mwili na roho), Mt. 10:28
 - d. panafanana na *Sheol*, Mt. 5:29-30; 18:9
 - e. Panaainisha waovu kama “wana wa Jehanamu” Mt. 23:15
 - f. Ni matokeo ya hukumu ya kimahakama, Mt. 23:33; Luk 12:5
 - g. Dhana ya Gehenna inafanana na mauti ya pili (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14) au ziwa la moto (k.v. Mt. 13:42,50; Ufu. 19:20; 20:10,14-15; 21:8).Yawezekana ziwa la moto pakawa ndo

mahali pa watu kuishi milele (wanaotoka kuzimu) na malaika waovu (waliotoka shimoni, 2 Petr. 2:4; Yuda 1:6 au shimoni, kama vile Luk 8:31; Ufu. 9:1-11; 20:1,3).

h. ilikuwa haikusaniwa kwa ajili ya binadamu, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya shetani na malaika wake, Mt. 25:41

E. yawezekana, kwa sababu ya kupishana kwa maneno shimoni (*sheol*), kuzimu (*hades*) na Jehanamu(*Gehenna*) kuwa

1. kiasili watu wote walikwenda shimoni/kuzimu
2. uzoefu wao wa (mema/mabaya) utazidishwa kwenye siku ya hukumu ya mwisho, lakini sehemu ya watenda maovu itabaki kuwa ile ile (hi indo kwa sababu toleo la KJV linaitafasili kama kuzimu (kaburi) kama Jehanamu .
3. Andiko katika agano jipya linalotaja kuhusu mateso kabla ya hukumu ni pale penye mfano katika Luka 16:19-31(Lazaro na mtu tajiri). Sheol pia pameelezwa kama mahali pa mateso (kama vile Kumb. 32:22; Zab. 18:1-5). Hata hivyo, mtu hawezi kutengeneza andiko juu ya mfano.

III. Hali ya mwingiliano kati ya mauti na ufufuo

A. Agano jipya halifundishi juu ya “zinaa ya nafsi,” ambacho ni moja ya kitu kati ya mitazamo mingi ya kale juu ya maisha baada ya kufa , ambapo panadaiwa kuwa

1. nafsi ya mwanadamu huwepo hata kabla ya maisha haya ya kimwili
2. nafsi ya mwanadamu ni ya milele kabla na baada ya kifo cha kimwili
3. mara nyingi mwili unaonekana kuwa gereza na mauti inaurudisha kwenye hali uliokuwanayo kabla

B. Agano Jipya linadokeza juu ya hali ya kutoungana kati ya mauti na ufufuo

1. Yesu anaongelea juu ya utengano wa mwili na roho, Mt. 10:28
2. Ibrahimu angeweza tayari kuwa na mwili, Mk. 12:26-27; Lk. 16:23
3. Musa na Eliya walikuwa na mwili wa nyama kipindi Yesu anageuka sura, Mathayo 17
4. Paulo anadai kuwa kipindi cha Yesu kurudi mara ya pili, waamini watakuwa na mwili mpya, 1 The. 4:13-18
5. Paulo anadai kuwa waamini watapata mili mipya ya kiroho siku ya kufufuka, 1 Kor. 15:23,52
6. Paulo anadai kuwa waamini hawaendi kuzimu, lakini huwa wamekufa huwa na Yesu, 2 Kor. 5:6,8; Fil. 1:23. Yesu aliyashinda mauti na kuwachukuwa watakatifu akaenda nao mbinguni, 1 Pet. 3:18-22.

IV. Mbinguni

A. Neno hili limetumika kwa maana tatu katika Biblia.

1. kwa maana ya anga juu ya dunia, Mwa. 1:1,8; Isa. 42:5; 45:18
2. Mbingu yenye nyota, Mwa. 1:14; Kumb. 10:14; Zab. 148:4; Ebr. 4:14; 7:26
3. Mahali pa kiti cha Enzi cha Mungu, Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Zab. 148:4; Efe. 4:10; Ebr. 9:24 (Mbingu ya tatu, 2 Kor. 12:2)

B. Biblia haifunui mengi kuhusu maisha baada ya kifo, yumkini kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka hana njia au uwezo wa kuelewa (kama vile 1 Kor. 2:9).

C. Mbinguni kumesimama kwa yote ni mahali (kama vile Yn. 14:2-3) na mtu kamili (kama vile 2 Kor. 5:6,8). Mbinguni paweza kuwa ni bustani ya Edeni iliyorejeshwa (Mwanzo 1-2; Ufunuo 21-22). Dunia itatakaswa na kurejeshwa (k.v. Mdo.3:21; Rum. 8:21; 2 Pet. 3:10). Taswira ya Mungu (Mwa. 1:26-27) imerejeshwa katika Kristo. Sasa ushirika ule wa ndani kwenye bustani ya Edeni yawezekana ukarejea tena. Hata hivyo, huu wawezakuwa ni msemu (mbinguni kama mji mkubwa Ufu. 21:9-27) na sio halisi. 1 Korintho 15 inaelezea tofauti kati ya mwili halisi na mwili wa kiroho kama mbegu ya mti uliokomaa. Tena, 1 Kor. 2:9 (nukuu toka Isaya 64:4 na 65:17) ni ahadi kubwa na tumaini! Nafhamu kuwa tutakapomwona Yeye tutafanana naye (kama vile 1 Yoh.3:2).

V. Vyanzo vya kusaidia

A. William Hendriksen, *The Bible On the Life Hereafter*

B. Maurice Rawlings, *Beyond Death's Door*

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 32:23-27

- ²³ Nitaweka madhara juu yao chunguchungu; Nitawapiga kwa mishale yangu hata ikaishe;
²⁴ Watakonda kwa njaa, wataliwa na makaa ya moto, Na uharibifu mkali;
Nitawapelekea meno ya wanyama wakali,
Pamoja na sumu ya wadudu watambao mavumbini.
²⁵ Nje upanga utawafiliza Na ndani ya vyumba, utisho;
Utaangamiza mvulana na msichana, Anyonyaye pamoja na mwenye mvi,
²⁶ Nalisema, Ningewatawanyia mbali,
Ningekomesha kumbukumbu lao kati ya wanadamu;
²⁷ sipokuwa naliogopa makamio ya adui, Adui zao wasije wakafikiri uongo,
Wasije wakasema, Mkono wetu umetukuka,
Wala Bwana hakuyafanya haya yote.

32:23-25 Aya hii inaeleza kistiari juu ya hukumu ya YHWH kwa wana wa Israeli:

1. "Nitaweka madhara juu yao chunguchungu" - BDB 705, KB 763, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, inayopatikana hapa tu. Hii *Qal* inamaanisha "kupeperusha" au "kukwapua."
2. "Nitawapiga kwa mishale yangu" - BDB 477, KB 476, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU. Maana yamsingi ya KITENZI hiki "ni kuweka kitu fulanikatika hitimisho," yaani kuaharibu moja kwa moja (kv. Mist. 2).
 - a. Watakonda kwa njaa, mst. 24, kv. 28:22
 - b. wataliwa na makaa ya moto, mst. 24 (au njaa, BDB 536 II, "moyo wenye maumivu")
 - c. Na uharibifu mkali, mst. 24 (au moto wenye sumu, kv. #e)
 - d. meno ya wanyama wakali, mst. 24, kv. Law. 26:22
 - e. sumu ya wadudu watambao mavumbini, mst. 24, kv. Amosi 5:18-19
 - f. upanga (nje), mst. 25
 - g. utisho (ndani), mst. 25
 - 1) mvulana (mwenye umri wa kuoa)
 - 2) msichana (bikra mwenye umri wa kuolewa)
 - 3) watoto (wanyonyao)
 - 4) mzee (mtu mwenye mvi)

32:26-27 YHWH angewaangamiza:

1. kwa kuwakata vipandevipande, mst. 26 - BDB 802, KB 907, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, lakini yenye maana ya HALI YA KUSIHI katika maana ya kuoanisha KITENZI kinachofuatia (hapa pekee, Toleo la LXX lina kifungu "kuwatawanyia")
2. kwa kukomesha kumbukumbu zao, mst. 26 - BDB 991, KB 1407, *Hiphil* HALI YA KUSIHI (yaani., kuangamiza moja kwa moja)
3. Hili ni moja ya maandiko pekee ambalo linaeleza juu ya kuangamiwa kwa Israeli ikiwa haitalitii agano (kv. 4:26; 28:20-22; 30:19).

Lakini ili kufanya hivyo Yeye angeghairi makusudi yake kwa Israeli. Maadui wa Israeli wangetamani ushindi na kumpa sifa YHWH (kv. mst. 27).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 32:28-33

- ²⁸ Maana hawa ni taifa wasio shauri,
Wala fahamu hamna ndani yao.

²⁹ Laiti wangukuwa na akili, hata wakafahamu haya,
Ili watafakari mwisho wao.

³⁰ Mmoja angefukuzaje watu elfu, Wawili wangekimbizaje elfu kumi,
Kama Mwamba wao asingaliwauza, Kama Bwana asingaliwatoa?

³¹ Maana, Mwamba wao si kama Mwamba wetu,
Hata adui zetu wenyewe ndivyo wahukumavyo.

³² Maana, mzabibu wao ni mzabibu wa Sodoma,
Nao ni wa mashamba ya Gomora;
Zabibu zao ni zabibu za uchungu, Vichala vyao ni vichungu.

³³ Mvinyo yao ni sumu ya majoka, Uchungu mkali wa nyoka.

32:28-33 Swali ni kwamba ni nani ambaye aya hii inamzungumzia—Israeli au maadui zao (kv. mist. 26-27)?

1. dhidi ya Israeli?
 1. mist. 28-29
 2. mst. 30 kama wenye kupingana na dhana ya vita takatifu
 3. mst. 32 uasi wa sasa wa Israeli
2. dhidi ya maadui zake?
 - a. mst. 30 kama kushindwa kwa sasa kwa jeshi la sehemu ya Israeli (kv. Yosh. 23:10)
 - b. mst. 30-31, Mwamba wao amewauza na Bwana amewarejesha
 - c. mst. 32-33, machukizo ya Kikanaani
 - d. mist. 34-43 inahusu kukataliwa kwa YHWH na hukumu ya sanamu za Kikanaani

32:28-29 Yatambue maneno yaliyo katika mist. 28-29 yenye kumaanisha “kufikiri”:

1. “kukosa washauri” - BDB 1, KB 2, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU
2. “kahana ufahamu ndani yao” - BDB 108 iliyokanushwa
3. “Laiti wangukuwa na akili” - BDB 53, *Qal* KAULI TENDAJI YA WAKATI TIMILIFU
4. “hata wakafahamu haya” - BDB 968, KB 1328, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
5. “Ili watafakari mwisho wao” - BDB 106, KB 122, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU

Israeli haina uwezo wa kufikiri vyema!

32:30 utambue ufananao wa mstari 30 c na d:

1. “Mwamba wao asingaliwauza” - BDB 569, KB 581, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kv. Amu. 2:14; 3:8; 4:2; 10:7; Zab. 44:10; Isa. 50:1
2. “Bwana asingaliwatoa” - BDB 688, KB 742, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
3. Ushindi wa Israeli unawezekana kwa sababu Shujaa wa ki-Ungu (vita takatifu) amewaacha kwa sababu ya kutolitii agano. Mistari 32-33 ni stiari uliyowekewa upanuzi wa mzabibu wenye kuashiria ibada za Kikanaani. Hii ni ya wafu (yani, sumu, chungu, yenye kuchukiza)!

ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): 23:34-43

³⁴ Je! Haya hayakuwekwa akiba kwangu?

Na kutiwa muhuri kati ya hazina yangu?

³⁵ Kisasi ni changu mimi, na kulipa, Wakati itakapoteleza miguu yao;

Maana siku ya msiba wao imekaribia,

Na mambo yatakayowapata yatafanya haraka.

³⁶ Kwa kuwa Bwana atawaamua watu wake,
 Atawahurumia watumwa wake,
 Aonapo ya kuwa nguvu zao zimeondoka,
 Na ya kuwa habaki mtu, aliyefungwa wala asiyefungwa,

³⁷ Naye atasema, Iko wapi miungu yao,
 Mwamba ule walioutumaini;

³⁸ Uliokula shahamu za sadaka zao,
 Na kunywa divai ya sadaka zao za kinywaji?
 Na waondoke na kuwasaidia ninyi;
 Na wawe hao himaya yenu.

³⁹ Fahamu sasa ya kuwa Mimi, naam, Mimi ndiye,
 Wala hapana Mungu mwingine ila Mimi;
 Naua Mimi, nahuisha Mimi, Nimejeruhi, tena naponya;
 Wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu,

⁴⁰ Maana, nainua mkono wangu mbinguni, Na kusema,
 Kama Mimi niishivyo milele,

⁴¹ Nikiunoa upanga wangu wa umeme,
 Mkono wangu ukishika hukumu,
 Nitawatoza kisasi adui zangu,
 Nitawalipa wanaonichukia.

⁴² Nitailevya mishale yangu kwa damu,
 Na upanga wangu utakula nyama;
 Pamoja na damu ya waliouawa na waliotekwa nyara,
 Katika vichwa vya wakuu wa adui.

⁴³ Furahini, enyi mataifa, pamoja na watu wake;
 Kwa maana atatwaa kisasi kwa damu ya watumwa wake,
 Atawatoza kisasi adui zake,
 Tena atafanya kafara kwa nchi yake, na watu wake.

32:34 Inaonekana katika muktadha fulani kwamba mst. 34 unaweza kuhusiana na mist. 32-33. Pia inawezekana kwamba huu unarejelea mst. 35 (nukuu kutoka kwa YHWH [yaani, mist. 34-35] kama ilivyo mist. 39-42). Muktadha mpana sana unaendelea kuitunza hukumu ya YHWH kwa Israeli ili mataifa yasipate habari au ujumbe usio sahihi. YHWH atawahukumu na kuwathibitisha watu wake.

Muktadha huu haueleza kama Israeli inatubu au makusudi ya YHWH ya ukombozi wa milele lazima yaruhusiwe kudhihirishwa katika historia. Watu wa agano la uasi wako chini ya uovu wa aina mbili (yaani, mataifa yenye kuabudu sanamu). Masihi atakuja na Israeli wataendelea kuwa wavunja agano!

Mstari huu una *Qa*/ KAULI TENDWAJI ENDELEVU mbili:

1. akiba kwangu - BDB 485, KB 481 (inapatikana hapa pekee)
2. kutiwa muhuri - BDB 367, KB 364, kv. Ayubu 14:17

32:35 Mstari wa kwanza wa kifungu hiki unanukuliwa katika Agano Jipya katika Rum. 12:19 na Ebr. 10:30. Neno “Kisasi” (BDB 668) pia linatajwa katika mist. 41 na 43. Hili mara nyingi linatumiwa na Isaya na Yeremia:

1. dhidi ya Israeli - Isa. 59:17
2. dhidi ya maadui wa Israeli - Isa. 34:8; 35:4; 61:2; 63:4; Jer. 46:10; 50:15,18; 51:6,1

Neno “kulipa” (BDB 1024) pia linapatikana katika Isa. 59:18 (mara mbili) katika muktadha huu ambapo YHWH atairejesha Israeli yenye dhambi (yaani, Sayuni).

☐ **“siku ya msiba wao imekaribia”** KITENZI hiki (BDB 556, KB 555, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kinaweza kurejelea:

1. mtu anayeingia matatizoni – Daudi katika Zab. 38:17
2. hukumu ya kiungu - Isa. 24:19
3. Ahadi ya kiungu ihusuyo urejesho - Zab. 94:18; Isa. 54:10

Wanadanu hujakwaa na asili ndiyo iwetengayo (kv. Isa. 24:19), bali Mungu atavirejesh vyote (kv. Rum. 8:18-25).

☐ Mistari miwili ya mwisho ya ushairi iliyo katika mst. 35 inadokeza juu ya ujio wa haraka wa haki ya Mungu:

1. siku ya majanga (BDB 15) iko karibu (BDB 898)
2. mambo yajayo juu yao yako karibu (BDB 301 I, KB 300, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU)

32:36 Katika wimbo huu wa maonyo na utabiri wa kutotii kwa Israeli yanaleta matokeo ya hukumu ya ki-Uungu, pia kuna ahadi ya msamaha na urejesho wa YHWH.

1. Bwana atawathibitisha watu wake - BDB 192, KB 220, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kv. Zab. 135:14
2. Bwana atawahurumia watumishi wake - BDB 636, KB 688, *Hithpael* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU Mungu atawahukumu watu wake (Zab. 7:8; 96:10), bali katika kufanya hivyo, atawahimarisha!

32:37-38 YHWH anaidhiki miungu ya Kikanaani (kv. Yer. 2:27-28; 11:12-13). Yeye anaiacha miungu yao kutenda badala yao (mst. 38):

1. Na waondoke - BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika kama HALI YA KUSIHI
2. Na kuwasaidia - BDB 740, KB 810, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika kama HALI YA KUSIHI
3. Na wawe hao himaya yenu - BDB 224, KB 243, *Qal* HALI YA KUSIHI (neni hili [BDB 340, KB 337, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFUT] mara nyingi inatumika kumaanisha ulinzi katika YHWH. Yeye na ndiye sehemu salama pekee)

32:39-40 YHWH anauhimarisha upekee (Imani ya Mungu Mmoja). Yatambue matumizi ya pinzani yanayofanana:

1. Tazama - BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. Mimi niishivyo- kv. Kut. 3:13-14 (YHWH)
3. Wala hapana Mungu mwingine ila Mimi - kv. 4:35,39; 33:26; Kut. 8:10; 9:14; Isa. 44:6,8; 45:7
4. Naua Mimi, nahuisha Mimi - kv. I Sam. 2:6; II Fal. 5:7 (pia itambue Warumi 9)
5. Nimejeruhi, tena naponya- kv. Ayubu 5:18; Isa. 45:7; Hos. 6:1; Amosi 3:6 (mara nyingi katika Agano la Kale viumbe vyote ni vya Mungu kama njia kueleza kweli ya Imani ya Mungu Mmoja)
6. Wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu - kv. Zab. 50:22; Isa. 43:13; Dan. 4:35

Katika mst. 40 YHWH (Mungu anayeishi milele, Mungu aishiye pekee) anaapa kwa sifa yake mwenyewe! Kuinua mkono (BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kunaweza kuwa tofauti katika makabila (yaani, kuinua mikono kama ishara ya ushindi kwa Israeli) katika mst. 27. YHWH anainua mkono wake kuapa kiapo (kv. Eze. 20:5-6).

32:41-43 YHWH anaeleza matendo yake ya hukumu dhidi ya waabudu sanamu (mst. 41-42). Katika mst. 43 Yeye anajitoa kwa ajili ya ahadi yake kwa Israeli.

Paulo anautumia mstarai wa kwanza wa aya. 43 katika Rum. 15:10 na kudai kuwa huu unaonyesha kwamba YHWH anayapenda na kuyajumuisha Mataifa. Paulo, katika Warumi 15, pia anainukuu Zab. 18:49 au II Sam. 22:5;

Zab. 117:1 na Isa. 11:10; 42:4 (kv. Mt. 12:21) ili kueleza kweli ile ile.

YHWH anahiari ya kuisamehe Israeli msamaha unaojikita katika sifa yake na ahadi, si matendo yao. Hili katika asili yake, ni agano jipya la Yer. 31:31-34 na Eze. 36:22-38. Tumaini la mwanadamu mwishowe linakuwa katika sifa isiyo badilika ya neema ya Mungu ndani ya wale ambao sura na mfanano wake uko ndani yao!

32:43 “Furahini” KITENZI hiki (BDB 943, KB 1247) ni *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU. Hizi ni kelele za furaha, kv. Ayubu 38:7; Isa. 12:6; 24:14; 44:23; 49:13; 54:1; Yer. 31:7.

☐ Kuna kifungu kilichoongezwa hapa toka Tafsiri ya Maandiko ya Kale ya Kiebrania ambacho kinanukuliwa na mwandishi wa kitabu cha Agano Jipya cha Waebrania (aliyetumia tafsiri ya Maandiko ya Kale ya Kiebrania) katika 1:6.

☐ Tambua namna VIWAKILISHI vilivyo katika mist. 34-43 vinavyobadilika toka nafsi ya kwanza hadi nafsi tatu. Hii ni tofauti za kifasihi, si waandishi tofautitofauti. YHWH anazungumza.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 32:44-47

⁴⁴ Musa akaja akasema maneno haya yote ya wimbo huu masikioni mwa watu, yeye na Yoshua, mwana wa Nuni. ⁴⁵ Musa akamaliza kuwaambia Israeli wote maneno haya yote; ⁴⁶ akawaambia, Yawekeni mioyoni mwenu maneno yote ambayo nashuhudia kwenu hivi leo; nayo waamuruni watoto wenu, wayatunze na kuyafanya maneno yote ya torati hii. ⁴⁷ Kwa maana si jambo lisilofaa kwenu; maana, ni maisha yenu, na kwa jambo hili mtazifanya siku zenu kuwa nyingi juu ya nchi mwivukiayo Yordani kuimiliki.

32:44 “Yoshua” Majina Yoshua na Yesu yanajikita katika maneno mawili yale yale ya Kiebrania, “YHWH” na “wokovu” (lazima KITENZI kiwe kamili).

Yoshua anapewa nafasi na Musa kabla ya watu kuthibitisha na kuimarisha kazi ya utawala wake.

32:46 “Yawekeni mioyoni mwenu” KITENZI hiki (BDB 962, KB 1321) ni *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU. Nahau ile ile inaweza inaweza kuonekana katika Eze. 44:5. Israeli inao uchaguzi, uchaguzi uliarifiwa unajikita katika matendo ya YHWH ya mwisho na ahadi za sasa (kv. 4:26; 30:19; 31:28), bali lazima achague sasa! Kwa neno “Moyo” tazama Madam Maalum katika 2:30.

☐ **“nayo waamuruni watoto wenu”** Kifungu hiki kinasistiza juu ya wajibu wa wazazi kuhusu elimu (kv. 32:7).

32:47 “Kwa maana si jambo lisilofaa kwenu; maana, ni maisha yenu” Hii ni dhana ya neno la Mungu kama lenye uweza wa kujitegemea pale lizungumzwapo (kv. Kumb. 8:3; Zab. 33:6,9; Isa. 55:11). Neno hili (Maandiko ya Musa) linaweza kuua na kuuisha (kv. 30:20) au kifo na uharibifu (kv. 30:19). Utii ndiyo nsingi endelevu wa kufanikiwa kwake!

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 32:48-52

⁴⁸ Bwana akasema na Musa siku iyo hiyo, akamwambia, ⁴⁹ Kwea katika mlima huu wa Abarimu, mpaka kilima cha Nebo, kilicho katika nchi ya Moabu, kuelekea Yeriko; ukaangalie nchi ya Kanaani niwapayo wana wa Israeli kuimiliki; ⁵⁰ ukafe katika kilima, huko ukweako, ukusanywe uwe pamoja na jamaa zako; kama alivyokufa nduguyo Haruni katika mlima wa Hori, akakusanywa awe pamoja na watu wake; ⁵¹ kwa sababu mlinikosa ninyi juu yangu katikati ya wana wa Israeli katika maji ya Meriba huko Kadeshi, katika bara ya Sini; kwa kuwa hamkunitakasa katikati ya wana wa Israeli. ⁵² Kwani utaiona hiyo nchi mbele yako, lakini

32:49-50 Mistari hii miwili ina USURUTISHI kadhaa:

1. “Kwea,” mst. 49 - BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. “ukaangalie,” mst. 40 - BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI SHURUTISHI
3. “ukafe,” mst. 50 - BDB 559, KB 562, *Qal* KAULI SHURUTISHI
4. “ukusanywe,” mst. 50 - BDB 62, KB 74, *Niphal* KAULI SHURUTISHI

Matendo ya mwisho ya mwisho Musa yaliandikwa na Mungu aliyempenda, alimtumia, na kumshikilia kwa ajili ya matendo yake!

32:49 “Abarimu” Hii ni aina ya mlima (kv. Hes. 27:12-14).

☐ **“kilima cha Nebo”** Hii ni sehemu ya juu sana katika mlima ule. Huenda eneo hili li karibu sana na sehemu ya kaskazini mwa Bahari ya Magombo ya Chumvi ng’ambo ya Yeriko mkabala na upande wa Bonde la Mto Yordani.

32:50 “ukafe katika kilima” Dokezo la mistari ni kwamba huu utakuwa mwisho wa maisha ya Musa hapa duniani (kv. mst. 34), bali ataishi na familia yake na watu wan chi yake waliokufa kabla yake.

☐ **“mlima wa Hori”** Kifo cha na maziko ya vimeandikwa kwa mara yha kwanza katika Hes. 20:22-29; 33:38-39. Hata hivyo, Kumb. 10:6 inasema kuwa huyu alikufa na kuzikwa huko Moserothi (kv. Hes. 33:30-31). Kitabu cha *Hard Sayings of the Bible*, uk. 166, kinasema Mosera ni jina la eneno ulipo Mlima Hori jina la mlima wa kipekee.

32:51 “kwa sababu mlinikosa ninyi juu yangu” (kv. Hesabu 20; 27:14; Kumb. 1:37; 3:23-27). Hiki ni kifungu kinachofanana na kifungu “kwa sababu hamkunitenda kama Mtakatifu.” Uwazi na kutotii mara kwa mara kwa Musa mbele za watu katika Hesabu 20 na tena katika Hesabu 27, ulimsababisha kuhukumiwa na Mungu hadharani na kutokuingia katika Nchi ya Ahadi.

32:52 Hili linapanuliwa baadaye katika sura ya 34.

KUMBUKUMBU LA TORATI 33

MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Baraka za mwisho za Musa Kwa Israeli	Baraka za Musa	Musa anayabariki makabila ya Israeli	Makabila
33:1-5	33:1-29 (mist. 1-5)	33:1-5 (mist. 2-5)	33:1-29 (mst. 1) (mst. 2) (mst. 3) (mst. 4-6)
33:6-7	(mist. 6-7)	33:6 33:7	(mist. 7)
33:8-11	(mist. 8-11)	33:8-11	(mist. 8-11)
33:12	(mist. 12)	33:12	(mist. 12)
33:13-17	(mist. 13-17)	33:13-17	(mist. 13-17)
33:18-19	(mist. 18-19)	33:18-19	(mist. 18-19)
33:20-21	(mist. 20-21)	33:20-21	(mist. 20-21)
33:22	(mist. 22)	33:22	(mist. 22)
33:23	(mist. 23)	33:23	(mist. 23)
33:24-29	(mist. 24-25) (mist. 26-29)	33:24-29 (mist. 24-25) (mist. 26-29)	(mist. 24-25) (mist. 26-29)

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k.

TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Sura hii ni yenye kufanana na ile ya kitabu cha Mwanzo 49. Sura zote zinafunua taratibu za kale za Kiyahudi za mababa wa imani za namna ya kuwabariki watoto wao (yaani., Yakobo kwa wanae katika kitabu cha Mwanzo 49). Hapa Musa anakuwa baba mbadala kwenye makabila ya Israeli na kuzitamkia baraka na maonyo kwa kila familia.
- B. Wimbo ule wa sura ya 32, ukiwa na maonyo makali, lazima uambatane na baraka za ile sura ya 33 ili kuyaona maongozi kamili ya YHWH!
- C. Ushairi huu unaonekana kuuzuia mwendelezo kati ya 32:48-52 na suara ya 34. Ni kwa nini uliingizwa hapa, lini na kwa nani, haliwezi jibiwa. Unadhaniwa kuwa ni ushairi wa baraka uliovuviwa wenye kuhusianishw

na Musa.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 33:1-5

¹ Hii ndiyo baraka ya Musa, huyo mtu wa Mungu, aliyowabarikia wana wa Israeli kabla ya kufa kwake.

² Akasema, Bwana alitoka Sinai,

Akawaondokea kutoka Seiri;

Aliangaza katika kilima cha Parani,

Akaja Meribath-Kadeshi.

Upande wake wa kuume Palikuwa na sheria ya moto-moto kwao.

³ Hakika awapenda hayo makabila ya watu;

Watakatifu wake wote wamo mkononi mwako;

Nao waliketi miguuni pako;

Watapokea kila mmoja katika maneno yako.

⁴ Musa alituagiza torati,

Ni urithi kwa mkutano wa Yakobo.

⁵ Akawa mfalme katika Yeshuruni,

Walipokutanika wakuu wa watu,

Makabila yote ya Israeli pamoja.

33:1 "baraka. . . aliyowabarikia" KITENZI (BDB 138, KB 159, *Piel* TIMILIFU) na NOMINO kinajitokeza hapa katika mstari wa 1.

MADA MAALUM: BARAKA

Kuna aina mbali mbali za baraka (BDB 139) katika Agano la Kale. Aina mbili zilizozoeleka ni

1. baraka za Mungu
 - a. kwa mataifa yote kupitia Ibrahimu (na mababa wa imani), Mwa. 12:3; 22:18; 27:29; Mdo. 3:25; Gal. 3:8
 - b. Toba yenye masharti, Kut. 32:29; Yoeli 2:14
 - c. Masharti ya kulitii agano, Law. 25:21
 - d. Uhusiano mzuri na Mungu huleta mafanikio (yaani., laana dhidi ya baraka), Kumb. 11:26,27,29; 23:5; 28:2,8; 30:1,19; Yosh. 8:34; Zab. 133:3
 - e. Juu ya utii wa Israeli, Kut. 12:15; 16:17; 32:13; Isa. 44:3; Ezek. 34:25-31; Mal. 3:10-12
 - f. Juu ya makuhani wa Kilawi, Ezek. 44:30; Mal. 3:3-4,10-12
 - g. Juu ya uzao wa Daudi wa Kimasihi, 2 Sam. 7:29; Zab. 3:8; 21:3; 118:26 (k.v. Mt. 21:9; 23:39; Marko 11:9; Luka 13:35; 19:38; Yohana 12:13)
 - h. Juu ya Yule aliyetumwa na Mungu, Zab. 118:26; 129:8
2. Baraka za wazazi
 - a. Isaka alimbariki Yakobo (kwa ujanja), Mwa. 27:12,18-29,35
 - b. Yakobo, Mwa. 49:3-27,28-29
 - c. Musa (mzazi wa kambo), Kumb. 33:1-25

Neno la Mungu, na kwa hiyo basi, baraka zilzotamkwa kwa mababa wa imani, ikajakuwa ni nguvu ya bure, yenye kuelekezwa kulitimiliza kusudi, Isa. 55:11; 45:23; Mt. 24:35 (5:17-19); Marko 13:31; Luka 21:33. Mamlaka ya kulinena neno inaweza kuonekana katika:

1. Uumbaji (yaani., "akaseam. . .")
2. "Neno" liliitwa Mungu," Yohana 1:1,14; 1 Yohana 1:1; Ufu. 19:13

Baraka kubwa ya Mungu ni Yeye Mwenyewe! Uwepo wake binafsi u pamoja nasi na kwa ajili yetu!

☐ **“huyo mtu wa Mungu”** Kifungu hiki (BDB 35 CHENYE MUUNDO WA MANENO 43) kilikuwa kikitumika kuwaelezea manabii (k.v. Yosh. 14:6; I Sam. 2:27; 9:6-7; I Fal. 9:6; 12:22; 13:1,30; II Fal. 1:9-13; 5:8; 23:17; Yer. 35:4).

33:2 Huu unaelezea uwepo wa kimafunuo wa YHWH kwa Israeli (yaani, Mungu kujidhihirisha kwa mwanadamu). Udhahirisho wa ajabu kati ya Mungu na mwanadamu ulikuwa unaogopesha (k.v. Kutoka 19; Zab. 50:2-3). Uwepo wa YHWH uliendelezwa katika muundo wa wingu maalum (yaani, *Shekinah* wingu la utukufu). YHWH alikuja na kukaa na watu Wake toka Ml. Sinai/Horebu mpaka pale walipovuka Mto Yordani. Hata baadaye, uwepo Wake maalum ulikuwa pamoja na sanduku la Agano, juu ya mbawa za makerubu. Ni dhahiri shahiri kutoka kwenye mstari huu kuwa YHWH anaonekana kama mwenye kuhusiana na milima (k.v. I Fal. 20:23,28).

1. Moria (Mwa. 22:2; II Nya. 3:1, mahali palipokuwa na hekalu)
2. Ml. Sinai/Horebu (Kutoka 19-20)
3. Ml. Seiri (hapa, Amu. 5:4)
4. Ml. Parani (hapa, Hab. 3:3)
5. Ebal/Gerizimu (27:4; Yosh. 8:30-33)
6. Tabori (Amu. 4:6)
7. Carmeli (I Fal. 18:20-39; II Fal. 4:25-27)
8. Perazimu (II Sam. 5:20; Isa. 28:21)
9. Ml. Sayuni (Isa. 2:1-4; Mic. 4:1-4; Zab. 68:16, jina kwa ajili ya Yerusalem)
10. Ml. Nebo (Kumbukumbu la Torati 34, kwa Musa tu)

☐ **“Sinai”** Hapa ni mahali palipotolewa zile sheria. Panaitwa Sinai (BDB 696) hapa tu katika Kumbukumbu la Torati. mara nyingi huitwa Horebu (BDB 352). Tazama Mada Maalum: Mahali Ulipo Mlima Sinai katika 1:2.

☐ **“Seiri”** Jina hili (BDB 973) linawakilisha vitu tofauti mbali mbali katika Agano la Kale:

1. Laweza kurejelea nchi ya Edomu - Mwa. 32:3; 36:30; Hes. 24:18; Kumb. 1:44; 2:8,12,22,29; 33:1; Yosh. 11:17; Amu. 5:4.
2. Laweza kurejelea mlima /kilima cha Edomu - Mwa. 36:8-9; Kumb. 1:2; 2:14; Yosh. 24:4.
3. Laweza kurejelea kwa watu - Mwa. 36:20-30; II Nya. 25:11,14; Ezek. 25:8 (wa Edomu)
4. Laweza kurejelea mlima/kilima huko Yuda - Yosh. 15:10(?).

☐ **“Mlima Parani”** Hii ni safu ya milima (BDB 803) karibu na nyanda za moabu (k.v. 1:1) upande wa magharibi mwa Araba, upande wa chini wa magharibi mwa Ghuba ya Agaba. Huenda orodha hii ni ya safari ya wana wa Israeli pindi wanatoka Sinai kwenda nchi ya ahadi (pia yawezakuwa nyika, k.v. Hes. 10:12; 12:16; 13:3,26). Mungu alikuwa akisema kuwa amekuwa nao muda wote wa kipindi cha kutangatanga jangwani na bado alikuwa nao.

☐

NASB “katikati ya makumi elfu ya walio watakatifu”

NKJV “akiwa na watakatifu makumi elfu”

NRSV “idadi kubwa ya walio watakatifu”

TEV “makumi elfu ya malaika wakiwa pamoja nae”

NJB -----

MAANDIKO YA KIMASORETI hapa yana neno “Ribebboth-Kodesh.” kumbukumbu la Torati 32:51 linatafasiri konsonanti kama zile zile “Meribah Kadesh. Hili laweza kurejelea (1) jina la mahala au (2) “malaika” (k.v. Dan. 7:10; Ufu. 5:11) au “watakatifu” (k.v. mstari wa 3; 7:6; 14:2; 26:19; 28:9). Walimu wa sheria wanalitumia andiko hili ili kutetea majukumu ya mwamuzi wa kimalaika (k.v. Mdo. 7:53; Gal. 3:19; Ebr. 2:2).

☐

NASB “miali ya moto”

NKJV “sheria kali”

NRSV “kusanyiko lililo lake”

TEV “moto-moto”
NJB “zikiwa za moto”

Kiuhalisia neno hili ni “sheria kali” (BDB 77 na 206). Hata hivyo, katika muktadha huu linarejelea utukufu angavu ujao wa YHWH (k.v. Isa. 60:1-3).

33:3 “Hakika awapenda hayo makabila ya watu” KITENZI (BDB 285, KB 284, *Qal* KAULI YA WAKATI ENDELEU) kinaonekana kufunua sura za 4:37; 7:7-8; 10:15. KISHAMIRISHO cha neno “watu” kiko kwenye HALI YA UWINGI na kinarejelea kwenye uzao wa mababa wa imani.

NASB “Watakatifu wake wote wamo mkononi mwako ”
NKJV “Watakatifu wake wote wamo mkononi mwako ”
NRSV “Watakatifu wake wote wako chini ya uangalizi wako”
TEV “anawalinda wale wote walio wake”
NJB “Watakatifu wako wote wako chini yako”

Neno “aliye mtakatifu” (BDB 481 MUUNDO WA MANENO 872) linarejelea kwenye watu wa agano. Hili lingalitafasiriwa kama “watakatifu” (mf., 7:6; 14:2,21; “watakatifu wako”).

☐
NASB “walifuata”
NKJV “waliketi”
NRSV “walipita”
TEV “waliinama”
NJB “walianguka”

Hili kiuhalisia ni neno “waketio ” (BDB 1067, KB 1730, *Pual* KAULI ILIYO TIMILIFU, KITENZI kisichokuwa cha kawaida kinaonekana hapa tu). Pia laweza kurejelea kwenye nafasi ya Yule ajifunzae (yaani., kuinamia, k.v. TEV, akaae miguu pake , k.v. NET Bible). Linarejelea watu wa Israeli.

☐ “Watapokea kila mmoja katika maneno yako” Hili linarejelea kwenye upokeaji wa sheria pale Mlima Sinai/Horebu katika kitabu cha Kutoka 20. Watu wa Mungu waliyafahamu mapenzi ya Mungu na sheria. Watu wa agano wana wajibu maalum wa kuzifunua tabia za Mungu. Wote wanathibitisha ukubalifu wao wa kuifuata torati ya Mungu.

33:4 “Musa alituagiza torati” Hili linaonekana kulithibitisha wazo kwenye mistari inayoendelea kuwa rejeo katika mstari wa 3 na ni jina la mahala na kuwa mistari inazungumzia kuhusu watu wa Mungu, na wala sio malaika.

☐ “Ni urithi kwa mkutano wa Yakobo” Neno “umiliki” (BDB 440) linarejelea kwenye urithi (BDB 439). Lilitumika mwanzoni kwa ajili ya kabila la Israeli (Yakobo, BDB 784) katika kitabu cha Kut. 6:8 na limetajwa mara kadhaa katika kitabu cha Ezekieli (k.v. 11:15; 33:24; 36:2,3,5). Neno “mkutano” (BDB 875) linamaanisha “kusanyiko la watu” (k.v. asili ile ile ya neno katika 23:2,3,4,8; 31:30). Kwa sababu ya ufanano katika mstari wa 4, huu utumiaji mahsusi wa neno “urithi” laweza kuwa ni stiaji kwa ajili ya agano (yaani., sheria). Watu wa Mungu wanarithi mafunuo vile vile na nchi!

33:5 “akawa mfalme” Hili laweza kuwa rejeo kwa YHWH kama mfalme (BDB 572 I, k.v. Kut. 15:18; Hes. 23:21; 24:7; I Sam. 8:4-9).

☐ Mistari miwili ya mwisho inafanana na kifungu cha maneno “wakuu wa watu” na “makabila ya Israeli.” Linarejelea kwenye uanzishaji wa agano pamoja na watu wapya wa Mungu katika Mlima Sinai/Horebu (k.v. Kut. 19-20).

☐ “Yeshuruni” Hili kiuhalisia linamaanisha “mtu mnyoofu” (BDB 449) na linarejelea kwa Israeli (k.v. mstari wa 26; 32:15; Isa. 44:2). Tazama Mada Maalum katika 1:1.

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 33:6

Reubeni na aishi, asife; Lakini watu wake na wawe wachache.

33:6 “Reubeni na aishi, asife” Mstari wa 6 una miundo mitatu ya *Qal* KITENZI AMRISHI:

1. aishi - BDB 310, KB 309
2. asife - BDB 559, KB 562 (kanushi)
3. aishi - BDB 224, KB 243 (kanushi)

Reubeni alikuwa ni mzaliwa wa kwanza wa Yakobo, lakini alimtenda Mungu dhambi (k.v. Mwa. 35:22) na kupoteza sifa yake (k.v. Mwa. 49:3-4).



NASB “Lakini watu wake na wawe wachache”

NKJV “Lakini watu wake na wawe huru”

NRSV “Hata hivyo hesabu yake ni chache”

TEV “Ingawa watu wake ni wachache”

NJB “hata hivyo watu wake na wawe wachache”

Kama ndivyo, hii ni sehemu ya sifa aliyopoteza (k.v. TEV, NJB). Kifungu hiki mara nyingi kinamaanisha “watu wachache” (k.v. Mwa. 34:30; Kumb. 4:27; Zab. 105:12; Yer. 44:28).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 33:7

⁷Na baraka ya Yuda ni hii; akasema, Isikize, Ee Bwana, sauti ya Yuda, Umlete ndani kwa watu wake; Alijitetea kwa mikono yake; Nawe utakuwa msaada juu ya adui zake.

33:7 “Isikize” KITENZI (BDB 1033, KB 1570,*Qal* SHURUTISHI) kinatumika mara nyingi katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati, lakini mara nyingi ni YHWH (au Musa) akiongea na Israeli.

☐ **“Ee Bwana”** Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 1:3.

☐ **“sauti ya Yuda”** Katika muktadha Musa anamwomba YHWH kuyasikiliza maombi ya Yuda (yaani., maombi ya kabila la Yuda). Hakuna chochote katika baraka za Musa chenye kudokeza mahali maalum pa Yuda kama kabila la kifalme, kwa hiyo ni dhahiri shairi katika baraka za Yakobo za kitabu cha Mwanzo 49:8-12. Ukweli kwamba kabila la simioni kutotajwa limesababisha baadhi kuhusianisha huu unabii kwenye kipindi cha baadaye pale Simioni alipojiungamanisha na Yuda (k.v. Yosh. 19:1-9; Amu. 1:3-4). Sehemu ya Simeoni ilikuwa ipo kusini magharibi mwa Yuda, ambayo ilikuwa mkabara na miji mitano ya Wafilisti.



NASB “Alijitetea kwa mikono yake”

NKJV “Na mikono yake na iwatetee”

NRSV “Akawaimarisha kwa mikono yake”

TEV “Akawapigania, Bwana”

NJB “na mikono yake ilinde haki zake”

Kifungu hiki cha Kiebrania hakijulikani. Chaweza kurejelea kwa Yuda kujilinda dhidi ya maadui, ambacho chaweza kuonyesha mgawanyiko wa tawala iliyoungana mwaka wa 922 k.k. kwa Yuda na Israeli (ni mtizamo tu).

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 33:8-11

⁸Akamnena Lawi, Thumimu yako na Urimu yako vina mtakatifu wako, Uliyemjaribu huko Masa; Ukateta naye kwenye maji ya Meriba. ⁹Aliyemtaja baba yake na mama yake, Mimi sikumwona; Wala nduguze hakuwakubali; Wala hakuwajua watoto wake mwenyewe; Maana wameliangalia neno lako, Wamelishika agano lako. ¹⁰Watamfundisha Yakobo hukumu zako, Na Israeli torati yako, Wataweka uvumba mbele zako,

Na sadaka nzima za kuteketezwa madhabahuni mwako.¹¹ Ee Bwana, ubariki mali zake, Utakabali kazi ya mikono yake; Uwapige viuno vyao waondokao juu yake, Na wenye kumchukia, wasiinuke tena.

33:8-11 Katika fasihi ya elimukale ya huko Qumran, magombo yaliyopatikana katika mapango kaskazini magharibi mwa Bahari ya Chumvi, Kumbu. 18:18 na Hes. 24:15-17, yenye kuelezea nabii za Kimasihi, zinazohusianishwa na hiki kifungu. Walifikiri kuwa Masihi alihusiana na Walawi (k.v. Zab. 110:4-7; Zakaria 3-4). Hii baraka ilijumuisha sio tu tendo la kiuaminifu la Haruni lililopita (k.v. Zab. 106:16), bali pia la Musa (k.v. mistari miwili ya mwisho ya mstari wa 8 na Kut. 17:1-7).

33:8 “Thumimu yako na Urimu yako” Vitu hivi viwili (BDB 1070 na 22) vilikuwa (1) ni namna ya kiufundi (yaani., utele) au (2) nuru ionekanayo yenye kumaanisha unabii wa kujua mapenzi ya YHWH. Inavyoonekana vilikuwa vikitunzwa na kuhani mkuu kwenye kifuko cha kifuani (k.v. Kut. 28:30; Law. 8:8; I Sam. 14:37-42; 23:9-12). Hasa kujua ni nini kilikuwa na namna gani vilifanya kazi vimekwisha potea (k.v. NIDOTTE, juzuu. 1, kur. 329-331).

☐ **“mtakatifu wako”** Hili laweza kurejelea kwa Haruni au Musa au kizazi cha kuhani Mkuu, lakini rejea ya kihistoria iliyotajwa inarejelea kwa Musa.

☐ **“Masa. . Meriba”** Soma Kut. 17:7. Hata hivyo, uasi katika eneo hili haumtaji Lawi au makuhani kwa namna yeyete ile. Uhusiano kamili haujulikani.

☐ Inavyoonekana YHWH anawajaribu wote Israeli na uongozi wake wakati wa kipindi cha kutanga tanga jangwani kuangalia kama kweli waliendelea kumwamini pamoja kwamba aliwatunza na kuwakinga na uvamizi wowote (k.v. Kut. 17:7).

1. kuthibitika/kujaribu - BDB 650, KB 702, *Piel* KAULI ILIYO TIMILIFU
2. kujaribu/kushindana - BDB 936, KB 1224, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU

Tazama vile YHWH mara nyingi alivyowajaribu (BDB 650) kwa makusudi na ahadi kwa wale waliodai kumjua na kuamini katika Yeye:

1. Ibrahim - Mwanzo 22
2. Israeli - Kut. 15:25; 16:4; 20:20; Kumb. 8:2,16; 13:3 Amu. 2:22; 3:1,4
3. Musa - Kumb. 33:8
4. Hezekia - II Nya. 32:31
5. Yesu pia nae alijaribiwa - Mathayo 4; Luka 4

Neno lile lile linatumika mara nyingi kwa ajili ya wanadamu “kumjaribu” Mungu, ambalo mara nyingi linaonekana kuwa kinyume!

33:9 Hili linarejelea kwenye kifungu kile cha kitabu cha Kutoka 32, ambapo Israeli ilipojihusisha na ibada ya sanamu katika kuitengeneza na kuiabudu (yaani., karamu za ulafi) ndama wa dhahabu. Kwa hali hiyo Musa akaamuru Walawi wote waaminifu (kabila lake) kuwaua ndugu zao wengi wa Kiisraeli kwa kuwahukumu kwa kitendo walichofanya (k.v. 32:25-29). Kwa kitendo hiki, hata dhidi ya familia zao wenyewe, waliheshimika kwa ajili ya:

1. Kulishika neno - BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU, k.v. 29:9
2. Kulitunza agano - BDB 665, KB 718, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, k.v. Zab. 25:10; 78:7; 119:2,22, 33,34,56,69,100,115,129,145

33:10 “watamfundisha. . wateweka uvumba. . na sadaka zote za kuteketeza” Hizi ni shughuli zilizokuwa za makuhani wa Kilawi:

1. kufundisha - BDB 434, KB 436, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU, k.v. 31:9-13, ikijumuisha pamoja na kutoa hukumu, k.v. 17:9-10
2. shughuli zote za hekaluni

33:11 Huu mstari mfupi una VITENZI vinne na KAULI ENDELEVU mbili:

1. “ubariki” - BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI SHURUTISHI, k.v. mistari. 1,13,20,24; 28:3(mara mbili),4,5,6(mara mbili),8,12,19; 30:16. Hiki ndicho YHWH anakihitaji!
2. “utakabali” - BDB 953, KB 1280, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU. Hili ni neno la kidhabihu, k.v. Law. 1:4; 7:18; 19:7; 22:23,25,27, ambalo pia laweza kumaanisha “furahia,” Law. 26:34 (mara mbili)
3. “uwapige” - BDB 563, KB 571, *Qal* KAULI SHURUTISHI, likitumika kumhusu YHWH katika 32:39, hapa linatumika kuwahusu maadui za (k.v. #4, #5, and #6)
4. “wenye kumwinukia” - BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU, likitumika kwa wale wamchukiao
 - a. Mungu, Kut. 15:7
 - b. Israeli, Kut. 32:25; Zab. 109:28
 - c. Jirani yako, Kumb. 19:11
5. “wale wamchukiao ” - BDB 971, KB 1338, *Piel* KAULI ENDELEVU, mara nyingi katika kitabu cha Zaburi kwa ajili ya maadui, k.v. 18:40; 44:7,10; 55:12; 68:1; 89:23
6. “wainukao tena” (kanushi) –asili ile ile kama #4, lakini hapa ni *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU.

Hili laweza kurejelea kwa Waisraeli wengine waliokuwa wakiushambulia uongozi wa Musa na Haruni kipindi kile cha kutanga tanga jangwani.



NASB, NKJV

NRSV “uwabarikie vitu vyao”

TEV “uwasaidie makabila yao kuwa yenye nguvu”

NJB “uwabarikie mali zao”

Neno hili (BDB 298) laweza kuwa na madokozo mbalimbali:

1. Maana yake ya kimsingi ni “uwezo” au “mamlaka”
2. “nguvu”
3. “uwezo,” “maarifa”
4. “mali”
5. “mafanikio”
6. “urithi”

☐ **“uwapige viuno”** hili kiuhalisia ni “kuvunja mguu” (yaani, sehemu kubwa ya mwili itumikayo kwa ajili kuushikilia mwili wote). Hii ni stiari ya Kiebrania kwa ajili ya kumdhoofisha mtu. Yumkini yaweza kuwa na dokezo la kuzuia kuzaa, hivyo basi, kutokuwepo na kizazi kingine.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 33:12

¹² Akamnena Benyamini, Mpenzi wa Bwana atakaa salama kwake; Yuamfunika mchana kutwa, Naye hukaa kati ya mabega yake.

33:12 “ Benyamini. . .mpenzi wa Bwana”Aweza (BDB 122) kuitwa mpenzi wa Bwana kwa sababu alikuwa kipenzi cha baba yake, Yakobo (k.v. Mwa. 44:20).

☐ **“atakaa salama kwake”** KITENZI (BDB 1014, KB 1496, ni *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, lakini kikiwa na maana ya KUAMURU, k.v. mstari wa 12 [mara mbili], 16,20,28; Kut. 25:8; 29:45,46). YHWH ni rafiki wake wa karibu katika mstari wa 12.



NASB “amkingae mchana kutwa”

NKJV “Yuamfunika mchana kutwa”

NRSV “amuzungukae mchana kutwa”

TEV “awalindae mchana kutwa”

NJB “amlindae mchana kutwa”

KITENZI (BDB 342, KB 339, *Qa/* KAULI TENDAJI ENDELEVU) kinatumika mahali hapa tu na kinaweza kumaanisha “kumzunguka” au “kumzingira” au “kumfunika.”



NASB, NKJV “hukaa kati ya mabega yake”
NRSV “hukaa kati ya mabega yake”
TEV “naye hukaa katikati yao”
NJB “hukaa kati ya vilima vyake”

Hii ni stiari kwa ajili ya (1) mahali penye ulinzi na amani (mistari ya 20,28) au (2) sehemu ya kuishi iliyozingirwa (yaani., Shilo, Betheli, au Yerusalem [ushauri wa S. R. Driver])

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 33:13-17

¹³ Na Yusufu akamnena, Nchi yake na ibarikiwe na Bwana; Kwa vitu vya thamani vya mbinguni, kwa huo umande, Na kwa kilindi kilalacho chini, ¹⁴ Na kwa vitu vilivyo bora vya matunda ya jua, Na kwa vitu vilivyo bora vya maongeo ya miezi, ¹⁵ Na kwa vitu viteule vya milima ya kale, Na kwa vitu vilivyo bora vya vilima vya milele, ¹⁶ Na kwa vitu vilivyo bora vya nchi, na kujaa kwake, Na uradhi wake aliyekaa ndani ya kile kijiti; Na ije baraka juu ya kichwa chake Yusufu, Juu ya utosi wa kichwa chake aliyetengwa na nduguze. ¹⁷ Mzaliwa wa kwanza wa ng'ombe wake mume, enzi ni yake; Na pembe zake ni pembe za nyati; Kwa hizo atayasukuma mataifa yote, hata ncha za nchi; Nao ni makumi ya maelfu ya Efraimu, Nao ni maelfu ya Manase.

33:13-17 Baraka iliyodumu sana, mbali na kabila la Lawi, iliwaendea wana wa Yusufu, Ebrahim na Manase (k.v. mstari wa 17, wanae wawili waliokuwa Misri). Haya yalikuwa ni makabila yenye nguvu yaliyokuwa eneo la kaskazini. Katika mistari wa 13-16b Musa anaelezea baraka za mavuno kwenye makabila haya mawili. Katika mstari wa 16 c na nafasi ya Yusufu huko Misri inatambulika. katika mstari wa 17 uwezo wa haya makabila mawili unaelezewa katika stiari za wanyama.

33:13 Hii mistari inarejelea kwenye uwingi wa unyevunyevu kutokana na umande na vyanzo vya ardhini (k.v. Mwa. 49:25). Maji yalimaanisha wingi wa shughuli za kilimo!

33:15 “Na kwa vitu viteule vya milima ya kale . . .na... vilima vya milele ” Hili laweza kurejelea kwenye miti mingi, kwa hali zote chakula na mambo ya ujenzi.

33:16 “Na uradhi wake aliyekaa ndani ya kile kijiti ” Hili laweza kurejelea kwenye kichaka cha moto (k.v. Kut. 3:2-4). Hili neno la kichaka (BDB 702) limetumika mara tano katika Agano la Kale, kati ya hizo mara nne katika kitabu cha Kut. 3:2-4.



NASB “Juu ya utosi wa kichwa chake aliyetengwa na nduguze ”
NKJV “Juu ya utosi wa kichwa chake aliyetengwa tokwa kwa nduguze”
NRSV “juu ya utosi wa kichwa katikati ya nduguze”
TEV “kwa vile alikuwa ni kiongozi wa nduguze”
NJB “juu ya utosi wa aliyewekwa wakfu kati ya nduguze”

Hili linafunua baraka za Yakobo katika kitabu cha Mwa. 49:26. Uongozi na sifa za Yusufu ziliendelea hadi kwa kizazi cha wanae.

33:17 “Na pembe zake ni pembe za nyati” Katika Kiebrania neno “pembe”(BDB 901) ni alama ya mamlaka.

■ “hata ncha za nchi” Huu ni MUUNDO WA MANENO wa BDB 67 na 75. Una umuhimu wa nguvu kithiolojia.

1. Upekee wa YHWH (na hivyo kufanya uwepo wa Mungu Mmoja)
 - a. Isa. 45:6,14; 46:9; 47:8,10
 - b. Zef. 2:15

2. Uweza na utukufu wa YHWH
 - a. Mith. 30:4
 - b. Zilizoko chini ya #3
3. Mwendelezo wa ibada ya YHWH na utawala wake dunia nzima
 - a. Kut. 33:17
 - b. I Sam. 2:10
 - c. Zab. 22:25-31; 59:13; 67:1-7; 98:2-9
 - d. Isa. 45:22; 52:10
 - e. Yer. 16:19
4. Kimasihi
 - a. I Sam. 2:10
 - b. Zab. 2:8
 - c. Mika 5:4-5

☐ **“makumi ya maelfu ya Efraimu.....Nao ni maelfu ya Manase”** Kifungu hiki kinaonyesha kipaumbele cha Efraimu katika wingi wake na uwezo. Tazama Mada Maalum: Efu katika 1:15.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA):33:18-19

¹⁸ Na Zabuloni akamnena, Furahi Zabuloni, katika kutoka kwako; ¹⁹ Watayaita mataifa waje mlimani; Wakasongeze huko sadaka za haki; Kwa kuwa watanyonya wingi wa bahari, Na akiba zilizofichamana za mchangani.

33:18 “Na Zabuloni. . .na , Isaka” Haya makabila mawili pia yameorodheshwa pamoja kama ilivyo katika kitabu cha Mwa. 49:13-15.

☐ **“Furahi”** KITENZI hiki (BDB 970, KB 1333, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) kinatumika kwa maana ya “kufurahia maisha mazuri, salama na yenye utele.”

☐ **“wakasongeze”** Hiki (BDB 422, KB 425, *Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO) kinaonekana kutumika katika maana ya uzima wa bure (k.v. 28:6,19; 31:2).

☐ **“mahemani mwenu”** Hili (BDB 13) linarejelea majumbani mwao wakati wakiwa jangwani kipindi cha kutangatanga, lakini lilikujakuwa ni stiari kwa ajili ya familia ya mtu. Hizi mistari miwili inayofanana inadokeza maisha tulivu yenye fuaraha.

33:19 Ufanano kati ya “mlima” (BDB 249) na “dhabihu za haki” (k.v. Zab. 4:5; 51:19) unadokeza muundo wa ibada (k.v. Kut. 15:17). Swali lifuataro lililotafsiriwa ni, mistari miwili inayofuatia ya ushairi inaendeleza fikra hizi au imebadilika kwenye mada nyingine? Uhusika wa Zabuloni katika bahari umetajwa katika kitabu cha Mwa. 49:13.

☐ **“watanyonya wingi wa bahari, Na akiba zilizofichamana za mchangani”** Hii mistari miwili inafanana. Yote ni VISHAMIRISHO vya KITENZI kimoja, “kunyonya” au “fichamana” (BDB 413, KB 416, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU). Hii ni stiari kwa ajili ya utele (k.v. 32:13).

1. Ya kwanza inarejelea :
 - a. chakula (yaani., utoaji dhabihu au maisha mazuri)
 - b. bidhaa (yaani., matumbawe, makombe, sifongo au nakshi)
2. ya pili inaundwa na *Qal* KAULI TENDWA ENDELEU mbili:
 - a. “kufunika,” lakini hapa inamaanisha “akiba” au “kuweka akiba” (BDB 706)
 - b. “kufichama” (BDB 380)

Zinaonekana kurejelea biashara ya kusafirisha bidhaa (k.v. Mwa. 49:13-14).

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 20-21

²⁰ Na Gadi akamnena, Na abarikiwe amwongezaye Gadi; Yeye hukaa kama simba mke, Hurarua mkono, naam, na utosi wa kichwa. ²¹ Akajichagulia sehemu ya kwanza, Kwani ndiko lilikowekwa fungu la mtoa-sheria; Akaja pamoja na wakuu wa watu, Akaitekeleza haki ya Bwana, Na hukumu zake kwa Israeli.

33:20 “abarikiwe amwongezaye Gadi” Hii inaonekana kurejelea kwa YHWH.

☐ “Yeye hukaa kama simba mke” Neno lenyewe ni “simba jike” (BDB 522, k.v. Mwa. 49:9; Hes. 24:9; Ayu. 4:11). Simba jike ndiye aliyewinda na kuleta chakula kwa simba dume na watoto. Gadi anarejelewa kama simba jike. Kabila la Gadi lilibarikiwa kwa sababu ya uaminifu wao katika vita (k.v. Mwa. 49:19).

33:21 Mstari huu ni kejeli juu ya Gadi au shujaa wa vita (katika stiari ya simba). Alichagua sehemu ya nchi upande wa mashariki mwa Yordani kumiliki, lakini yeye na ukoo wa Rubeni na ndugu wa kabila la Manase walikuwa ni kundi la kwanza la kijeshi kwenda vitani kwenye nchi ya ahadi (k.v. Yosh. 4:12-13; 22:1-3).

☐ “Kwani ndiko lilikowekwa fungu la mtoa-sheria” Maana ya Kiebrania haijulikani!

☐ “Akaja pamoja na wakuu wa watu” Hii yaweza kuyarejelea makabila yale matatu yaliyomuomba Musa na wazee ruhusa ya kwenda kuishi upande wa mashariki mwa Mto Yordani.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 33:22

²² Na Dani akamnena, Dani ni mwana-simba, Arukaye kutoka Bashani.

33:22 “Dani ni mwana-simba, Arukaye kutoka Bashani” Kumtaja Dani kwa namna kunavyohusiana na Bashani (k.v. 1:4; 3:1,3,4,10,11,13,14) kunashangaza. Mwanzoni mahali lilipokuwa kundi la kabila la Dani ni kusini magharibi (yaani., eneo la Wafilisti) na baadaye walielekea pande za kaskazini (k.v. Waamuzi 18). Huu yaweza kuwa ni unabii wenye kuhusianishwa kwenye makazi yasiyo ruhusuwa.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 33:23

²³ Na Naftali akamnena, Ee Naftali, uliyeshiba fadhili, Uliyejawa na baraka ya Bwana; Umiliki magharibi na kusini.

33:23 “Umiliki magharibi na kusini” KITENZI (BDB 439, KB 441, *Qal* KAULI SHURUTISHI) kinatumika mara nyingi katika kitabu cha Kukmbukumbu la Torati kwa ajili ya Israeli kumiliki nchi (k.v. 1:8,21,39; 2:24,31; 9:23; 11:31; 17:14; 26:1). Kinadokeza kuchukua kwa nguvu na kumiliki kama makazi ya kudumu.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 33:24-25

²⁴ Na Asheri akamnena, Na abarikiwe Asheri kwa watoto; Na akubaliwe katika nduguze, Na achovye mguu wake katika mafuta. ²⁵ Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako.

33:24 “Na Asheri akamnena

‘Na abarikiwe Asheri kwa watoto;

Na akubaliwe katika nduguze” KITENZI (BDB 224, KB 243, “be”) ni *Qal* CHENYE KUAMURU. Hii inaonyesha kuyatendea kazi mawazo ya Kiebrania. Kwa Myahudi, mtoto wa kiume alikuwa ni baraka kubwa iliyotarajiwa. Walimu wa Kiyahudi wanautafasiri mstari huu kumaanisha kuwa ni kwa sababu ya uzuri uliopitiliza wa mabinti wa Asheri walichaguliwa na hawa vijana. Maana yake haijulikani.

☐ **“Na achovye mguu wake katika mafuta”** Mahali alipokuwa Asheri, upande wa Pwani ya kaskazini, palikuwa ni sehemu nzuri kwa ajili ya mizeituni. Kifungu hiki yumkini kinarejelea kwenye tendo la biashara ya uuzaji mafuta ya mizeituni.

33:25 “Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba” Asili ya Kiebrania kwa ajili ya neno “makomeo” (BDB 653) au “nguzo” (BDB 653) laweza pia kutafasiriwa kama “viatu” (BDB 653). Muundo uliotumika hapa unapatikana hapa tu. Kwa sababu ya eneo la kijiografia alipoishi Asheri, upande wa barabara kuu itokayo eneo hilali lenye rutuba kuelekea Misri, kama Asheri aliangamia, nchi yote nayo iliangamia (uvamizi pande za kusini). Alifikiriwa kuwa lango na komeo kwenye nchi ya ahadi.

☐

NASB “Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako”

NKJV, NJB “mji wa makimbilio”

NRSV “huitiisha miungu ya kale”

TEV “huwawekea ulinzi”

Swali lililotafasiriwa ni kile ambacho NOMINO ya mwisho inakimaanisha (BDB 179)?

1. nguvu (yaani., maisha yenye kustahili)
2. ulinzi (yaani., hakuna mavamizi)

ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 33:26-29

²⁶ Hapana aliyefanana na Mungu, Ee Yeshuruni, Ajaye amepanda juu ya mbingu ili akusaidie. Na juu ya mawingu katika utukufu wake. ²⁷ Mungu wa milele ndiye makazi yako, Na mikono ya milele i chini yako. Na mbele yako amemsukumia mbali adui; Akasema, Angamiza. ²⁸ Na Israeli anakaa salama, Chemchemi ya Yakobo peke yake, Katika nchi ya ngano na divai; Naam, mbingu zake zadondoza umande. ²⁹ U heri, Israeli. Ni nani aliye kama wewe, taifa lililookolewa na Bwana! Ndiye ngao ya msaada wako, Na upanga wa utukufu wako; Na adui zako watajitiisha chini yako, Nawe utapakanyaga mahali pao pa juu.

33:26-29 Hii mistari ni sehemu ya tafasiri yenye kusifia uweza na upekee wa YHWH! Yeshuruni linatumika kama jina kwa ajili ya Israeli (k.v. 32:15). Mistari hizi (yaani., mistari wa 26 b & c; mistari wa 28 c & d; mistari wa 29: f) inatumia vifung ambavyo vimezoeleka vyenye kurejelea kwa mungu wa ustawi, *Ba'al*, ikidokeza kuwa vitu vyote vilivyokwisha kusemwa kuhusu *Ba'al* havikuwa vya kweli kumhusu yeye, lakini vilikuwa kweli kumhusu YHWH. YHWH ndiye Mungu pekee.

33:26 “Hapana aliyefanana na Mungu” Tazama maelezo katika 4:35.

33:27 “Mungu wa milele ” Jina *Elohim* limejumuishwa na sifa hizi:

1. *Elohim* wa milele, hapa
2. *Elohim* aishiye milele, Isaya 26
3. *Elohim* wa kweli, II Nya. 15:3; Isa. 65:16
4. *Elohim* wa wenye miili wote, Yer. 32:27 (unafanana na Hes. 16:22; 27:16)
5. *Elohim* wa mbinguni, Mwa. 24:3,7; II Nya. 36:23; Ezra 1:2; Neh. 1:4,5; 2:4,20
6. *Elohim* wa karibu, Yer. 23:23
7. *Elohim* wa wokovu wetu, Zab. 18:46; 24:5; 25:5; 27:9; 65:5; 79:9; 85:4; Isa. 17:10
8. *Elohim* wa haki, Zab. 4:1
9. *Elohim* mwamba wangu, II Sam. 22:3; Zab. 18:2
10. *Elohim* ngome yangu, Zab. 43:2
11. *Elohim* sifa yangu, Zab. 109:1 (orodha ni kutoka toleo la BDB uk. 44, #4, b.)

☐

NASB “ndiye makazi yako ”

NKJV “mji wa makimbilio”

NRSV “makazi yako”

TEV -----

NJB “visima vya Yakobo vimechaguliwa”

Neno hili (BDB 733) laweza kurejelea pango la wanyama (k.v. Ayu 37:8; 38:40; Amos 1 3:4) au stiari kwa ajili ya mji wa makimbilio uliotolewa na Mungu kwa ajili ya watu wake (hapa tu). Dhana ile ile inapatikana katika Zab. 71:3; 91:9.

☐ “Na mikono ya milele i chini yako” Hii ni stiari kwa ajili ya:

1. YHWH kuwapigania (k.v. kipengele c, mstari 29)
2. Kwa uangalizi wa YHWH usio na mwisho, YHWH ni Mungu anayetenda!

Yawezekana kuwa hili ni dokezo kwenye kitabu cha Mwa. 49:24 (mistari ya b & c).

☐ “kuangamiza” KITENZI (BDB 1029, KB 1552, *Hiphil* SHURUTISHI) kinamaanisha “kuangamiza.” Ni sehemu ya msamiati unaohusu “vita takatifu,” k.v. 1:27; 2:22; 6:15; 9:20; Yosh. 7:12; 9:24. Kama Israeli italitii agano Yeye atawapigania kwa ajili yao, lakini kama sivyo, Yeye atapigana dhidi yao! Waisraeli walitegemea kujiandaa kwa ajili ya vita na kuyachukua maeneo kwa ajili ya adui zao, lakini alikuwa ni YHWH aliyeshinda vita!

33:28

NASB “chemichemi ya Yakobo peke yake”

NKJV “chemichemi ya Yakobo pekee”

NRSV “makazi ya Yakobo pekee yasiyo na usumbufu”

TEV -----

NJB “chemichemi ya Yakobo pekee inachaguliwa”

Neno “chemichemi” (BDB 745 II) linamaanisha “chanzo cha maji” na linarejelea kwenye uzao. Neno “peke yake” (BDB 94, “pekee”) ni stiari kwa ajili ya ulinzi.

33:29 Huu mstari unatumia neno “vita takatifu” kuelezea ukombozi wa YHWH toka Misri, tokea jangwani, na tokea mikononi mwa Wakanaani!

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya majadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki.

Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana

1. Kwa nini Musa hakuvingia katika nchi ya ahadi?
2. Kwa nini kuna tafasiri nyingi kuhusiana na sura ya 33:2-3?
3. Kwa nini Simoni hakuorodheshwa kwenye baraka?
4. Kuna nukuu ya Kimasihi katika hizi baraka?

KUMBUKUMBU LA TORATI 34

MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA			
NKJV	NRSV	TEV	NJB
Musa anakufa mlima Nebo	Kifo cha Musa	Kifo cha Musa	Kifo cha Musa
34:1-8	34:1-8	34:1-8	34:1-4 34:5-9
34:9-12	34:9 34:10-12	34:9 34:10-12	34:10-12

MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Tazama uk. vii katika kipengele cha utangulizi)

KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasisi, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasisi.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya ya tatu
12. N.k.

USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : 34:1-8

¹ Musa akapanda kutoka uwanda wa Moabu mpaka mlima Nebo, hata kilele cha Pisga kukabili Yeriko. Bwana akamwonyesha nchi yote ya Gileadi hata Dani; ² na Naftali yote, na nchi ya Efraimi na Manase, na nchi yote ya Yuda, mpaka bahari ya magharibi; ³ na Negebu, na uwanja wa bonde la Yeriko, mji wa mitende, hata mpaka Soari. ⁴ Bwana akamwambia, Hii ndiyo nchi niliyowaapia Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, nikisema, Nitawapa wazao wako. Basi nimekuonyesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko. ⁵ Basi Musa, mtumishi wa Bwana, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la Bwana. ⁶ Akamzika bondeni, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth-peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo. ⁷ Musa alikuwa mtu wa miaka mia na ishirini alipokufa; jicho lake halikupofuka, wala nguvu za mwili wake hazikupunguka. ⁸ Wana wa Israeli wakamwombolezea Musa katika uwanda wa Moabu siku thelathini; basi siku za maombolezo ya matanga ya Musa zikaisha.

34:1 “uwanda wa Moabu” Hata ni mazingira ya kijiografia ya hitimisho la kitabu cha Hesabu (k.v. 36:13), na kitabu chote cha Kumbukumbu la Torati (k.v. 4:44-49). Haya yako upande wa mashariki mwa ng'ambo mto Yordani, kutoka Yeriko (k.v. mst. 1).

☐ **“mpaka mlima Nebo, hata kilele cha Pisga”** Milima hii hii imetajwa katika Kumb. (k.v. 3:17). Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya “mwinuko” au “kilele” (BDB 612 I). Hili linaonekana kwamba mlima Nebo na Pisga (BDB 820 “nafasi”) inakirejelea kilele kile kile cha mlima. Kwa upekee Mungu alilichagua eneo hili ili aweze kutimiliza neno lake kwa Musa kwamba atamwonyesha Nchi ya Ahadi ingawa hata Musa hataweza kuingia. Mwishoni,

katika mst. 5, Mlima Nebo utakuwa sehemu ya kifo cha Musa. Pia, tamaduni za Kiyahudi zinasema kwamba Yeremia alilificha Sanduku la Agano katika mlima huu.

☐ **“Bwana akamwonyesha nchi yote”** Kuna vifungu kadhaa ambavyo vimeandika dhambi ya Musa ambayo iliyomzuia kuingia katika Nchi ya Ahadi (k.v. Kumb. 3:23-28; 32:48-52 na Hes. 27:12-14). Musa aliomba maombi kadhaa na kumsihi Mungu juu ya hili jambo, lakini bado hakuruhusiwa kuingia katika Nchi ya Ahadi. Ingawa mara zote dhambi huongoza njia yake na ina matokeo yake, neema ya Mungu inaonekana kwa kumruhusu Musa kuitazama Nchi ya Ahadi ingawa hasingeweza kuingia ndani yake.

34:2 “bahari ya magharibi” Hii inairejelea bahari ya Mediterania (k.v. 11:24). Neno “magharibi” kiuhalisia ni “sehemu ya nyuma” (BDB 30).

34:3 “Negebu” Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya “nchi ya kusini” (BDB 616) na linairejelea kwa nchi ya jangwa isiyokaliwa na watu ambayo iko kusini mwa Beersheba.

☐ **“uwanda”** Huu unalirejelea kwa bonde linalofahamika kama Bonde la Ufa ambalo lina bahari ya chumvi. Yeriko iko kaskazini-magharibi na Soari iko kusini-magharibi.

☐ **“Yeriko, mji wa mitende”** Yeriko unafahamika kama mji wa mitende (k.v. Amu. 1:16) na ni mmojawapo ya miji ya kale zaidi katika ulimwengu huu. Ulikuwa ng’ambo ya mto Yordani kutoka sehemu ambayo Israeli walipiga kambi.

☐ **“Soari”** Neno hili (BDB 858) linamaanisha usio na thamani (k.v. Mwa. 19:20-22).

34:4 “Hii ndiyo nchi niliyowaapia Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo” Huu ni utimilifu wa ahadi ya Mungu iliyoandikwa katika Mwa. 12:7; 26:3; 28:13. Ahadi zote kwa Ibrahimu zilihusisha nchi na uzao. Agano la Kale linatilia mkazo juu ya nchi na watoto wakati Agano Jipya linatilia mkazo juu ya mwana wa pekee (k.v. Isa. 7-12). Ahadi hii ya kale imerudiwa rudiwa mara nyingi. Hapa kuna baadhi ya mifano: Kut. 33:1; Hes. 14:23; 32:11; Kumb. 1:8; 6:10; 9:5; 30:20.

☐ **“Basi nimekuonyesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko”** Ni dhahili dhambi ya kupiga mwamba kwa fimbo mbele za wana wa Israeli badala ya kuuambia mwamba (k.v. Hes. 20:7-12) ni hatia kwa Musa iliyomsababishia kuhukumiwa. Watu walishuhudia dhahili tendo la kutokutii kwa Musa.

34:5 “Basi Musa, mtumishi wa Bwana” Neno hili “mtumishi wa Bwana” ni jina la heshima alilopewa Musa. Alipewa Yoshua pekee baada ya kifo cha Musa. Alitunukiwa mfalme Daudi. Mwishoni linamrejelea Masihi ajaye (k.v. mtumishi wa nyimbo za Isaya 40-56). Yumkini ikawa ni chanzo cha tungo ya Pauline katika Agano Jipya, “mtumwa wa Mungu.” Dhana ya mtumishi katika Agano la Kale ni ya maana sana. Katika Agano Jipya kuchaguliwa au utumishi ulikuwa ni kutimiliza kusudi la Mungu, sio muhimu kwa ajili ya wokovu. Koreshi alitwa “Masihi wa Mungu” (k.v. Isa. 45:1) na Ashuru alitwa “fimbo ya hasira yake” (k.v. Isa. 10:5). Taifa hili katili na mfalme mpagani walifaa katika mpango wa Mungu lakini walikuwa hawahusiani naye kiroho. Maneno haya “uchaguzi” na “chaguo” yana vidokezo pekee katika Agano Jipya.

☐ **“akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la Bwana”** Hapa kwa Kiebrania dhahili ni “kwa kinywa cha Bwana,” (BDB 804), ambayo kinaonekana kuwa stiari ya neno la Mungu (k.v. Mwa. 41:40; 45:21; Kut. 17:1; 38:21; Hes. 3:16,39). Hata hivyo, walimu wa sheria za Kiyahudi wanasema kwamba hili ni “busu la Mungu.” Wanasema kwamba Mungu alimbusu Musa kwenye mdomo na kuitwaa pumzi yake. Hii inafanana sana katika nahau ya utamaduni wetu “busu la kifo.” Ikiwa ndiyo hivyo, ni maelezo mazuri ya uwiano kati ya haki na rehema ya Mungu katika maisha ya Musa.

34:6 “Akamzika bondeni, katika nchi ya Moabu” Neno “yeye” linamdokeza Mungu mwenyewe. Hili linafanana sana na Mwa. 7:16, ambapo Mungu aliufunga mlango wa safina. Sababu moja ya Mungu mwenyewe kumzika Musa ni kwa sababu Mungu aliyafutilia mbali maeneo ya kale na waliyoyabuni ili kwamba wayaabudu badala yake. Tambua kwamba Musa hakuzikwa katika mlima Nebo bali chini ya bonde. Kifungu cha ajabu katika Agano Jipya katika Yuda 9 kinasimulia maelezo haya, lakini ni kwa namna gani isiwe dhahili. Yuda 9 inaonekana kunukuu kitabu kilichowakfishwa zaidi kijulikanacho kama neno la Musa lisilohakikishwa. Kusudi halisi la shetani kuutaka mwili wa Musa halijulikani.

☐ **“lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo”** Hii ilikuwa kazi ya mhariri wa mwisho. Wengi wanadai kwamba Musa hakuweza kuandika sura hii ya mwisho ambayo inasimulia kifo chake. Rashi anasema kwamba Yoshua ndiye aliyeandika juu ya kifo cha Musa, wakati IV Esdras anadai kwamba Musa aliandika juu ya kifo chake mwenyewe. Ninaamini katika uandishi wa Musa wa Torati, lakini hautoi mamlaka kwa baadhi ya mawazo ya mhariri kama hili lililojitokeza kutoka nyakati hadi nyakati. Mfanano wa Kiebrania kati ya Vitabu Vitano vya Kwanza vya Biblia na kitabu cha Yoshua unaonekana kudokeza kwamba Yoshua alikuwa na sehemu katika Kumbukumbu ya maandiko ya Musa. Hata hivyo, sehemu muhimu ya Ezra katika Ualimu wa Kiyahudi kama mhariri wa Agano la Kale lote inawezekana pia.

34:7 “Ingawa Musa alikuwa mtu wa miaka mia na ishirini alipokufa” Hiki kipindi cha miaka mia moja na ishirini kinazungumzwa kwa urefu katika mahubiri ya Stephano katika Matendo ya Mitume 7:23 katika mgawanyiko wa vifungu vitatu vya miaka arobaini kila kimoja: (1) miaka arobaini katika mfumo wa elimu ya Misri; (2) miaka arobaini katika jangwa lile lile ambalo wangekuja kuongoza wana wa Israeli; na (3) miaka arobaini katika jangwa katika kipindi cha kutanga tanga jangwani. D. L. Moody anasema, “Kwa miaka arobaini Musa alidhani alikuwa mtu Fulani muhimu. Kwa miaka arobaini alijifikiria kuwa yeye si kitu wala cho chote. Kwa miaka arobaini aligundua nini Mungu angeweza kufanya kupitia mtu ambaye si lo lote wala cho chote.”

☐ **“jicho lake halikupofuka, wala nguvu za mwili wake hazikupunguka”** Hii inaonekana kurejelea afya ya Musa, wakati Kumb. 31:2 inaonekana kuwa ni udhuru uliotolewa na Musa juu ya sababu ya kutoingia Nchi ya Ahadi (kwamba alikuwa mzee sana na aliyechoka). Huu sio mkanganyiko, bali ni moja ya jaribio la Musa kujaribu kuondoa dhambi yake aidha kwa kulaumu watu au umri wake au sababu zingine.

34:8 “Hivyo wana wa Israeli wakamwombolezea Musa. . . siku thelathini” Hiki kilikuwa kipindi cha mzunguko mmoja wa mwezi. Kipindi hiki hiki cha muda kilitolewa kwa ajili ya kumuombolezea Haruni (kama vile Hes. 20:29). Kila kizazi kilichoasi katika jangwa kilikufa huko isipokuwa cha Yoshua na Kalebu.

ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): 34:9-12

⁹ Na Yoshua, mwana wa Nuni, alikuwa amejaa roho ya hekima; maana Musa alikuwa amemwekea mikono yake juu yake; wana wa Israeli wakamsikiliza, wakafanya kama Bwana alivyomwamuru Musa. ¹⁰ Wala hajainuka tena katika Israeli nabii kama Musa, ambaye Bwana alimjua uso kwa uso; ¹¹ katika ishara zote na maajabu yote, ambayo Bwana alimtuma kuyatenda katika nchi ya Misri, kwa Farao, na kwa watumishi wake wote, na kwa nchi yake yote; ¹² na katika ule mkono wa nguvu wote, tena katika ule utisho mkuu wote, alioutenda Musa machoni pa Israeli wote.

34:9 “Na Yoshua, mwana wa Nuni” Jina Yoshua linamaanisha “YHWH huokoa” (BDB 221). Ni jina hilo hilo kama la “Yesu” (kama vile Mt. 1:21). Hili linaundwa na neno la Kiebrania, “Hosea,” ambalo linamaanisha “wokovu” na kifupi cha jina la Agano kwa ajili ya Mungu linalounganisha mwanzoni.

☐ **“alikuwa amejaa roho ya hekima”** Dhana hii ya “kujazwa” (BDB 569, KB 583, *Qa/* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) inatakiwa kulinganishwa na Hes. 27:18 na dhana inayofanana na hiyo ya wajuzi katika Kut. 28:3. Kiuhalisia Roho wa Mungu alihusika katika maisha ya watu katika Agano la Kale pamoja na Agano Jipya.

☐ **“hekima”** Hii inaonekana (BDB 315) kuurejelea uwezo wa Yoshua kuongoza watu kuelekea vitani na katika haki ya utawala. Yoshua hakuwa anatokea kabila la Walawi na hivyo kwa namna yo yote asingeweza kuwa kuhani, japo alikuwa kiongozi mwenye karama.

☐ **“maana Musa alikuwa amemwekea mikono yake juu yake”** Dhana hii ya kuwekewa mikono ni ya muhimu sana na inaonekana katika Agano la Kale. Tunaona kitendo hiki kiuhalisia katika Hes. 27:22-23; pia tazama katika Kumb. 31:1-8. Ni kwa namna fulani inahusiana na kuwekewa mikono kwa mwathirika wa kidhabihu ambapo kwa namna fulani dhambi iliamishwa. Kwa namna fulani pia uongozi wa Musa uliamishwa kwa Yoshua.

MADA MAALUM: KUWEKEWA MIKONO KATIKA BIBLIA

Hii ishara ya kujumuishwa inatumiwa sana katika njia mbalimbali katika Biblia.

1. kula kiapo (yaani mkono katika uvungu wa paja [kama vile Mwanzo 24:2,9; 47:29])
2. kuchukua uongozi wa familia (kama vile Mwanzo 48:14,17,18)
3. kutambua kifo cha dhahihu ya mnyama kama mbadala
 - a. Makuhani (kama vile Kutoka 29:10,15,19; Law. 16:21; Hes. 8:12)
 - b. kuwalaza watu (kama vile Law. 1:4; 3:2,8; 4:4,15,24; 2 Nyakati. 29:23)
4. mtu wa kukaa pembeni kumtumikia Mungu kwa ajili ya jukumu maalumu au huduma (kama vile Hes. 8:10; 27:18,23; Kumb. 34:9; Mdo. 6:6; 13:3; 1 Tim. 4:14; 5:22; 2 Tim. 1:6)
5. kushiriki katika kurusha mawe kwa kimahakama kwa kumpiga mwenye dhambi (kama vile Law. 24:14)
6. mkono katika mdomo wa mtu huashiria ukimya au tafakari (kama vile Waamuzi. 18:19; Ayubu 21:5; 29:9; 40:4; Mika 7:16)
7. Mkono wa mtu ukiwa katika kichwa chake humaanisha huzuni/ombolezo (2 Sam. 13:19)
8. kupokea Baraka za afya, furaha na utauwa (kama vile Mt. 19:13,15; Marko 10:16)
9. ikihusiana na uonyaji wa mwili (kama vile Mt. 8:3; 9:18,20; Marko 5:23; 6:5; 7:32; 8:23; 16:18; Luka 4:40; 13:13; Mdo. 9:17; 28:8)
10. kupokea Roho Mtakatifu (kama vile Mdo. 8:17-19; 9:17; 19:6, angalia Kumb. 34:9)

Kwa kushangaza kuna ukosefu wa mfanano katika vifungu ambavyo kihistoria vimekuwa vinatetea kuwekwa wakfu kwa viongozi kwa ajili ya kazi ya injili (yaani kuwekwa wakfu, tazama Mada Maalum: Kuwekwa Wakfu).

1. Katika Mdo. 6:6 Ni mitume wanaoweka mikono yao kwa ajili ya huduma ya watu saba ya kanisa la mahali pamoja.
2. Katika Mdo. 13:3 Ni Mitume na Walimu wanaoweka mikono juu ya Barnaba na Paulo kwa ajili ya huduma ya kimishenari.
3. Katika Mdo. 1 Tim. 4:14 Ni viongozi wa kanisa la nyumbani (wazee) waliojumuishwa katika wito wa kwanza na kuwekwa rasmi.
4. In Katika 2 Tim. 1:6 Ni Paulo anayeweka mikono yake juu ya Timotheo.

Mtawanyiko na utata unaonyesha kukosekana kwa mpangilio katika kanisa la karne ya kwanza. Kanisa la kwanza lilikuwa zaidi katika kuendelea na kubadilika badilika na mara zote likitumia karama na vipawa vya roho vya waamini (kama vile Wakorintho 12; 14). Agano Jipya kwa ufupi tu limeandikwa kutetea au kushusha mfano wa serikali (Tazama mtawanyiko huu katika Mdo 15) au taratibu za kuwekwa wakfu. Mpangilio wa desturi za kikanisa ni muhimu lakini sio kibiblia. Uungu wa uongozi ni zaidi kiumuhimu kuliko mfumo ya uongozi (yaani dola).

34:10 “Wala hajainuka tena katika Israeli nabii kama Musa” Mistari 10-12 ni fasiri ya mwandishi wa Musa au yawezekana zaidi, mhariri wa baadaye. Kiuhalisia hii inaurejelea unabii wa kimasihwa wa Kumb. 18:15-22. Haya maudhui yanakuzwa katika Ebr. 3:1-6, ambapo Yesu na Musa wanatofautishwa.

☐ **“ambaye Bwana alimjua uso kwa uso”** Neno “kujua” (BDB 393, KB 390, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ni nahau ya Kiebrania yenye kumaanisha “ushirika wa karibu wa upendo” (kama vile Mwa. 4:1; Yer. 1:5). Hii

haiyarejelei maarifa ya ndani. Tungo “uso kwa uso” inaonyesha ukaribu wa kiupendo ambao Mungu alikuwa nao katika kuzungumza na Musa (kama vile Kut. 33:11; Hes. 12:6-8).

34:11-12 Mstari 11 inaonekana kumaanisha kwamba mapigo ya Misri ambayo yalichukua kipindi cha miezi kumi na nane yalimaanisha kuhukumu juu ya miungu ya Misri na kujaribu kuwaongoza Wamisri kwenda katika kumtumaini YHWH. Mstari wa 12 unatuonyesha kwamba miujiza ambayo Mungu aliifanya dhidi ya miungu ya Wamisri ilikuwa pia imekusudia kuongeza imani ya Wana wa Israeli kama miujiza ya Yesu ilivyokuwa imekusudiwa kuongeza imani ya wanafunzi. Pia inawezekana kwamba mst. 12 unahusiana na kipindi cha kutangatanga jangwani.

MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini uwekwaji wa maeneo ya kijiografia ya matukio katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati ni muhimu sana?
2. Kwa nini Mungu alilificha kaburi la Musa?
3. Ni kwa namna gani mstari wa 7 unaonekana kukinzana na 31:2?
4. Ni nini umuhimu wa Musa kumuwekea mikono Yoshua? Ni kwa namna gani hili linafanana na uwekwaji wakfu wa siku za leo?
5. Kwa nini Yoshua hakuchukuliwa kuwa nabii kama Musa (k v.mst. 10)?
6. Nini makusudi ya miujiza (kv. mst. 11-12)?

KIAMBATISHO CHA KWANZA

I. UTANGULIZI WA UNABII WA AGANO LA KALE

A. Maelezo ya Ufunguzi

1. Jamii ya waaminio haiamini namna ya ya kutafsiri unabii. Kweli zingine zimekwisha weka wekwa bayana kama ilivyo kwa nafasi ya Waorthodox katika karne nyingi, lakini si katika karne hii.
2. Zipo hatua kadhaa za unabii wa Agano la Kale
 - a. Premornarchial (Kabla ya utawala wa Kifalme)
 - (1) Watu binafsi walioitwa manabii
 - (a) Ibrahimu – Mwanzo 20:7
 - (b) Musa – Hesabu 12:6-8; Kumbukumbu la Torati 18:15; 34:10
 - (c) Haruni – Kutoka 7:1 (Msemaji wa Musa)
 - (d) Miriam – Kutoka 15:20
 - (e) Medad na Eldad – Hesabu 11:24-30
 - (f) Debora – Waamuzi 4:4
 - (g) Wasiokuwa na majina – Waamuzi 6:7-10
 - (h) Samweli - 1 Samweli 3:20
 - (2) Rejea ya manabii kama kundi – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
 - (3) Kundi la Kinabii au ushirika – 1 Samweli 10:5-13; 19:20; 1 Wafalme 20:35, 41; 22:6, 10-13; 2 Wafalme 2:3,7; 4:1, 38; 5:22; 6:1, nakadhalika.
 - (4) Masihi aitwaye nabii – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
 - b. Manabii wa utawala wa kifalme wasioandikwa (wakimlenga mfalme);
 - (1) Gadi – 1 Samweli 22:5; 2 Samweli 24:11; 1 Mambo ya Nyakati 29:29
 - (2) Nathan – 2 Samweli 7:2; 1 Wafalme 1:22
 - (3) Ahijah – 1 Wafalme 11:29
 - (4) Yehu – 1 Wafalme 16:1, 7, 12
 - (5) Wasiotajwa – 1 Wafalme 18:4, 13, 22
 - (6) Eliya – 1 Wafalme 18- 2 Wafalme 2
 - (7) Mikaya – 1 Wafalme 22
 - (8) Elisha 2 Wafalme 2:9, 12-13
 - c. Maandiko ya kale ya manabii (yanayo lenga taifa pamoja na mfalme); Isaya–Malaki (isipokuwa Danieli)

B. Istilahi za Kibiblia

1. *Ro'eh* = "muonaji" (BDB 906, KB 1157), 1 Samweli 9:9. Rejea hii yenyewe inatuonesha mpito kutoka katika neno nabi. *Ro'eh* inatokana na istilahi ya jumla "kuona." Mtu huyu alizielewa njia za Mungu na mipango yake na aliulizwa kutambua mapenzi ya Mungu katika jambo lolote.
2. *Hozeh* = "muonaji" (BDB 302, KB 3011), 2 Samweli 24:11. Ni jamii ya neno lenye maana sawa na *Ro'eh*. Inatokana na neno "kuona." Njeo ya wakati uliopita ya neno hili ni "tazama" ambalo limetumika mara nyingi ikimaanisha manabii.
3. *Nabi'* = "nabii" (BDB 611, KB 661), inayohusiana na lugha ya Akkadia ya kitenzi *Nabu* = "kuita" na kiarabu *Naba'a* = "kutangaza". Hili ni neon limetajwa mara nyingi katika Agano la kale kumaanisha nabii. Limetumika zaidi ya mara 300. Asili kabisa haijulikana kwa hakika japo "kuita" kwa wakati huu inaonekana kama mbadala mzuri zaidi. Yawezekana uelewa mzuri zaidi unatoka YHWH's yanayoeleza mahusiano ya Musa kwa Farao kupitia Haruni. (rejea kutoka 4:10-16; 7:1; Kumbukumbu la torati 5:5). Nabii ni mtu anayezungumza kwa niaba ya Mungu kwa watu wake. (Amosi 3:8; Yereimia 1:7,17; Ezekieli 3:4).
4. Istilahi zote tatu zinatumiwa katika huduma ya Nabii katika 1 Mambo ya Nyakati 29:29; Samueli – *Ro'eh*; Nathan – *Nabi'* and Gadi – *Hozeh*.

5. Kifungu cha maneno, 'ish ha – 'elohim, "Mtu wa Mungu" pia ni namna pana ya kumaanisha msemaji wa Mungu. Inatumika mara 76 katika Agano la Kale kwa kumaanisha "nabii"
6. Neno "Nabii" kwa asili ni la Kigiriki. Inatokana na neno (1) *pro* = "kabla" au "kwa niaba ya" na (2) *phemi* = "kuzungumza."

II. MAANA YA UNABII

- A. Neno unabii lilikuwa pana kimaana katika lugha ya kiebrania kuliko Kingereza. Vitabu vya historia vya YOSHUA, Wafalme (isipokuwa Ruth) vinatajwa na Wayahudi kama "Manabii waliopita". Wote Ibrahimu (Mwanzo 20:7; Zaburi. 105:15) and Moses (Kumbukumbu la Torati 18:18) wanatajwa kama Manabii (pia Miriam, Kutoka 15:20). Kwahiyo kuwa makini unapokuwa unatazama maana kutoka katika lugha ya Kingereza!
- B. "Unabii kisheria kabisa waweza kusema ni ule uelewa wa historia unaokubali maana zile tu zinazohusiana na uungu, kusudi la kiungu, ushirika wa kiungu," *Interpreter's Dictionary of the Bible*, toleo la. 3, ukurasa wa. 896.
- C. "Nabii si mwanafalsafa au mwana taaluma ya Theolojia, bali msaidizi wa agano aletaye neno la Mungu kwa watu wake ili kutengeneza hatima zao kwa kufanya mageuzi ya siku zao za sasa," *Prophets and Prophecy, Encyclopedia Judaica* toleo la. 13 ukurasa wa. 1152.

III. KUSUDI LA UNABII

- A. Unabii ni njia ya Mungu kuzungumza na watu wake, kuwapa miongozo katika mazingira yao ya sasa na tumaini katika kuyaendesha maisha yao na matukio ya duniani. Ujumbe wao ulikuwa wa jumla. Ilikusudiwa kuonya, kutia moyo, kuhamasisha imani na toba, na kuwafahamisha watu wa Mungu kuhusu Mungu mwenyewe na mipango yake. Iliwashikilia watu wa Mungu katika maagano na Mungu. Katika hili inatakiwa iongezwe kuwa mara nyingi imekuwa ikitumika kufunua uchaguzi wa Mungu wa wasemaji (Kumbukumbu la Torati 13:1-3; 18:20-22). Hii ukiipa umaanani kabisa utagundua ilimaanisha Mesiya
- B. Mara nyingi nabii aliichukua historia na migongano ya kithiolojia ya siku zake na kuangazia hayo katika mazingira ya matukio ya siku za mwisho. Namna ya muono huu wa siku za mwisho kihistoria katika Israel ni wa kipekee na katika hali yakeya uchaguzi wa kiungu na ahadi za kiagano.
- C. Ofisi ya nabii inaonekana kutengeneza usawa (Yeremia 18:18) na kuchukua ofisi ya Kuhani Mkuu kama njia ya kufahamu mapenzi ya Mungu. Urimm na Thummim inabadilika katika ujumbe wa mdomo kutoka kwa msemaji wa Mungu. Ofisi ya nabii inaonekana pia kupita mbali katika Israeli baada ya Malaki. Haitokei mpaka baada ya miaka 400 baadae kwa Yohana Mbatizaji. Haeleweki namna ambavyo kipawa cha "unabii" kwa Agano Jipya kinavyoshabihiana na Agano la Kale. Manabii wa Agano Jipya (Matendo ya Mitume 11:27-28; 13:1; 15:32; 1 Wakorintho. 12:10,28-29; 14:29,32,37; Waefeso. 4:11) sio vifunuo vya ufunuo mpya au maandiko, bali wasimulizi wa yajayo na wazungumzaji wa mambo ya mbele ya mapenzi ya Mungu katika hali za agano.
- D. Unabii hauna msingi sana au hausisitizi katika utabiri kwa asili. Utabiri ni njia mojawapo ya kutthibitisha ofisi yake na ujumbe wake, ila lazima izingatiwe "chini ya asilimia 2% ya unabii wa Agano la Kale ni kuhusu wa kimasiya". Chini ya asilimia 5% kiuhalisia inafunua nyakati za Agano Jipya. Chini ya asilimia 1% inahusu matukio yajayo. "fee na Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa wa 166).
- E. Manabii wanamwakilisha Mungu kwa watu, wakati Makuhani wanawawakilisha watu kwa Mungu. Haya ni maelezo ya jumla. Kuna utofauti kwa kama Habakkuki, ambaye anauliza maswali kwa Mungu.
- F. Sababu moja inayoleta ugumu kuwaelewa manabii ni kwasababu hatujui muundo wa vitabu vyao. Havina mfuatano unaoeleweka. Vinaonekana ni vyenye hoja na mada kweli lakini si kama vile mtu angetegemea. Mara nyingi hakuna mazingira ya wazi ya kihistoria wala muda maalumu, au mgawanyiko wa wazi wa mambo ya kiungu. Vitabu hivi ni vigumu (1) Kuvisoma kwa mara moja (2) Kufafanua kwa mada (3) Kug'amua kweli kuu au kusudio la mwandishi katika kila uungu.

IV. TABIA ZA UNABII

- A. Katika Agano la Kale inaonekana kukua kwa dhana ya “nabii” na “unabii”. Hapo mwanzo katika Israeli kulitokea ushirika wa manabii, ukiongozwa na viongozi shupavu wenye uvuvio wa Mungu kama Eliya na Elisha. Kuna wakati neno “wana wa manabii,” ilitumika kuzungumzia kundi hili (II Wafalme 2). Manabii walikuwa na tabia ya kujawa na furaha ya kupiliza (1 Samweli 10:10-13; 19:18-24)
- B. Hata hivyo kipindi hiki kilipita mara kwa mara kwa manabii mmoja mmoja. Kulikuwa manabii (wa kweli na waongo) waliojitambulisha pamoja na mfalme, na waliishi katika Kasri la Kifalme (Gad, Nathan). Pia, kulikuwa na wale waliojitegemea, wakati mwingine wasiokuwa na hadhi kabisa za jamii ya ki-Israeli (Amos) walijumuisha wote wanawake na wanaume (2 Wafalme 22:14)
- C. Nabii mara nyingi alikuwa mfunuaji ya hatima, anayefanya katika mazingira ya mwanadamu yanavyoenda. Mara nyingi jukumu la nabii ilikuwa ni kufunua mpango wa Mungu kwa uumbaji wake ambao hauathiriwi na mwikio wa kibinadamu. Huu mpango wa wa ulimwengu wa matukio ya mwisho wa nchi ni wa kipekee katika manabii wa Mashariki ya Karibu ya Kale. Utabiri na Agano ni mapacha waendao pamoja katika ujumbe wa kinabii (rejea Fee na Stuart, ukurasa wa 150). Hii inamaanisha manabii husisitiza ujumuishwaji katika lengo. Siku zote, japo si kila eneo, hujelekeza katika kuambia taifa.
- D. Mambo mengi ya kinabii yakitolewa kwa njia ya kinywa. Baadae iliunganishwa kwa njia ya mada, mfululizo, au namna nyingine ya uandishi wa Mashariki ya Karibu ambao imepotea huku kwetu. Kwakuwa ilikuwa kwa njia ya kinywa, haikuwa na muundo kama unaokuwa katika kazi iliyo andikwa. Hii inafanya vitabu kuwa vigumu kusoma na ngumu kuelewa bila kuwa na historia ya mazingira halisi.
- E. Manabii walitumia namna kadhaa kuwasilisha jumbe zao
 - 1. Matukio ya kimahakama – Mungu anawapeleka watu wake mahakamani, mara nyingi ni kesi ya kutalikiana ambapo YHWH anamkataa mke wake (Israeli) kwasababu ya kukosa uaminifu wake (Hosea 4; Micah 6).
 - 2. Mazingira ya msiba – mzani haswa kwa jaili ya ujumbe wa namna hii na tabia zake “ole” inajitenga kama aina yake kivyake vyake (Isaiah 5; Habbakkuk 2)
 - 3. Matamko ya Agano la Baraka - asili ya masharti ya Baraka imesisitizwa na madhara yake, yote ya wema na ubaya, yanatajwa kwa ajili ya baadae (Kumbukumbu la Torati 27-28).

V. SIFA ZA KIBIBLIA KWA AJILI YA KUMDhibitisha Nabii wa Kweli

- A. Kumbukumbu la Torati 13:1-5 (utabiri/ishara zinahusianishwa kwenye uwazi wa kuamini uwepo wa Mungu mmoja)
- B. Kumbukumbu la Torati 18:9-22 (manabii wa uongo/manabii wa kweli)
- C. Wote waume kwa wake huitwa na kuchaguliwa kama manabii wa kiume au manabii wa kike
 - 1. Miriam - Kutoka 15
 - 2. Debora - Waamuzi 4:4-6
 - 3. Hulda - II Wafalme 22:14-20; II Mambo ya Nyakati 34:22-28
- D. Katika tamaduni zilizokuwa zimewazunguka nabii alitambulika kwa namna ya kutoa unabii/kutabiri. Katika Israeli walithibitishwa kwa
 - 1. Jaribio la kithiolojia – matumizi ya jina la YHWH
 - 2. Jaribio la kihistoria – utabiri ulio sahihi

VI. MIONGOZO YA KUKUSAIDIA KATIKA KUTAFSIRI UNABII

- A. Tafuta kujua lengo la kwanza la nabii (mwandishi) kwa kuzingatia mazingira ya kihistoria na muktadha wa maandishi ya kiungu.
- B. Soma na tafsiri mambo yote, sio sehemu tu; fafania na yaliyomo. Angalia inavyoshabihiana na mazingira ya unabii. Jaribu kufafania kitabu kizima.
- C. Endelea na kufanya makisio ya utafsiri wa kawaida wa hadithi mpaka vitu katika habari vikuelekeze katika matumizi yaliyofichwa kimaana; hivyo badili lugha iliyofichwa katika maandishi.

- D. Fafanua matendo ya kiishara katika ufahamu wa mazingira ya kihistoria na usambamba wa hadithi. Kuwa na uhakika wa kukumbuka maanadishi ya kale ya Mashariki ya Karibu si kama yale ya kisasa ya kimagharibi.
- E. kuwa mwangalifu wa utabiri
 - 1. Je, unahusisha siku za mwandishi?
 - 2. Je, uliwahi kutimia katika historia ya Israeli?
 - 3. Je, ni kweli yamekwisha kuwa matukio yajayo?
 - 4. Je, yana kutimizwa kwa sasa nab ado yanasubiri kutimizwa siku zijazo?
 - 5. Waruhusu waandishi wa Biblia wakuongoze katika majibu na sio waandishi wa kisasa.
- F. Vitu vya kuzingatia
 - 1. Je, utabiri umekidhi kigezo cha sharti la mwitikio
 - 2. Kuna uhakika kwa Yule ambaye unabii umemlenga? (Na kwa nini)?
 - 3. Je, kuna uwezekano, wa kibiblia na/au kihistoria, wa kutimia mara mbili?
 - 4. Waandishi wa Agano Jipya, chini ya uvuvio waliweza kumuona mesiya katika sehemu nyingi katika Agano la Kale kiasi ambacho hakipo kwetu. Wanaonekana kutumia aina hii ya mchezo. Kwakuwa hatujavuviwa basi ni bora tukawaachia utaratibu huu wao.

VII. VITABU VYA KIMSAADA

- A. *A Guide to Biblical Prophecy* by Carl E. Amending and W. Ward Basque
- B. *How to Read the Bible for All Its Worth* by Gordon Fee and Douglas Stuart
- C. *My Servants the Prophets* by Edward J. Young
- D. *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic* by D. Brent Sandy
- E. *Cracking the Old Testament Code*, D. Brent Sandy and Ronald L. Giese, Jr.

KIAMBATISHO CHA PILI

MAPITIO YA HISTORIA FUPI YA MAMLAKA ZA MESOPOTAMIA

(tukitumia tarehe zenye kusimamia kimsingi juu ya John Bright's A History of Israel, uk. 462 na kundelea):

- I. Himaya ya Waashuru (Mwa. 10:11):
 - A. dini na tamaduni kwa kiasi kikubwa zilishawishiwa na himaya ya Wasumeri/Wababeli
 - B. Orodha ya mfano ya watawala na makisio ya tarehe:
 1. 1354-1318 Asshur-Uballit I:
 - (1) akaupiga mji wa Wahiti wa Karkemishi.
 - (2) wakaanza kuondoa ushawishi wa Wahiti na kuruhusu Ashuru kukua.
 2. 1297-1266 Adad Nirari I (mtawala mwenye nguvu).
 3. 1265-1235 Shalmaneser I (mtawala mwenye nguvu).
 4. 1234-1197 Tukulti-Ninurta I – ushindi wa kwanza wa himaya ya Babeli kuelekea Kusini.
 5. 1118-1078 Tiglath-Pileser I – Ashuru inakuwa tawala yenye nguvu huko Mesopotamia.
 6. 1012- 972 Ashur-Rabi II
 7. 972- 967 Ashur-Resh-Isui II.
 8. 966- 934 Tiglath-Pileser II.
 9. 934- 912 Ashur-Dan II.
 10. 912- 890 Adad-Nirari II.
 11. 890- 884 Tukulti-Ninurta II.
 12. 890- 859 Asshur-Nasir-Apal II.
 13. 859- 824 Shalmaneser III.
 - vita ya Qarqar katika mwaka wa 853
 14. 824- 811 Shamashi-Adad V.
 15. 811- 783 Adad-Nirari III.
 16. 781- 772 Shalmaneser IV.
 17. 772- 754 Ashur-Dan III.
 18. 754- 745 Ashur-Nirari V.
 19. 745- 727 Tiglath-Pileser III:
 - a. wakitwa kwa jina la kiti chao cha enzi cha Babeli, Pul, katika II Fal. 15:19
 - b. mtawala mwenye nguvu sana
 - c. wakaanzisha utaratibu wa kuwaondoa watu walioshindwa
 - d. katika mwaka wa 735 K.K. palikuwepo na uanzishaji wa ligi ya “Syro-Ephramatic,” ambayo ilikuwa ikijaribu kuunganisha rasilimali zote zilizopo za kijeshi za mataifa ya ng’ambo ya Yordani tokea kwenye vyanzo vya Mto Frati huko Misri kwa ajili ya kusudi la kubatilisha kuinuka kwa mamlaka ya jeshi la Ashuru. Mfalme Ahazi wa Yuda akakataa kuungana nao na kuvamiwa na Israeli na Shamu. Akamwandikia Tiglath-Pileser III kwa ajili ya msaada dhidi ya ushauri wa Isaya (kama vile Isa. 7-12).
 - e. katika mwaka wa 732 Tiglath-Pileser III akavamia na kuzishinda Shamu na Israeli na kuweka mfalme kibaraka juu ya kiti cha enzi cha Israeli, Hoshea (732-722 k.k.). maelfu ya Wayahudi wakakimbilia huko Umedi (kama vile II Fal. 15-16).
 20. 727- 722 Shalmaneser V
 - a. Hoshea akatengeneza ushirikiano na Misri na kuvamiwa na Ashuru (kama vile II Fal. 17)

- b. Akaizingira Samaria katika mwaka wa 724 K.K
- 21. 722- 705 Sargon II:
 - a. baada ya kuuzingira mji kwa muda wa miaka mitatu, kulikoanzishwa na Shalmanesa V, jemedari wake na mrithi Sargon II, akaupiga mji mkuu wa Israeli, Samaria. Zaidi ya watu 27,000 wakakimbilia Umedi.
 - b. Himaya ya Wahiti pia ikapigwa.
 - c. katika mwaka wa 714-711 ushirika mwingine wa mataifa yaliyoko ng'ambo ya Yordani na Misri yakaasi dhidi ya Ashuru. Ushirika huu ulijulikana kama "uasi wa Ashdodi." Hata Hezekia wa Yuda mwanzoni alishiriki. Ashuru ikavamia na kuiangamiza miji mbalimbali ya Wafilisti.
- 22. 705- 681 Senakeribu:
 - a. katika mwaka wa 705 ushirika mwingine wa mataifa yaliyoko ng'ambo ya Yordani na Misri yakaasi baada ya kifo cha babaye, Sargon II. Hezekia aliunga mkono kikamilifu huu uasi. Senakeribu akavamiwa katika mwaka wa 701. Uasi ulishindwa lakini Yerusalemu ikahurumiwa kwa tendo la Mungu (kama vile Isa. 36-39 na II Fal. 18-19.)
 - b. Senakeribu pia akauweka chini uasi huko Elam na Babeli.
- 23. 681- 669 Esarhaddon:
 - a. mtawala wa kwanza wa Ashuru kuivamia na kuipiga Misri.
 - b. alikuwa na huruma kubwa kwa ajili ya Babeli na kuujenga upya mji wake mkuu.
- 24. 669- 663 Asshurbanipal:
 - a. pia uliitwa Osnappar katika Ezra 4:10
 - b. kakaye Shamash-shum-ukin alitawazwa kuwa mfalme wa Babeli. Pakaja kuwepo na miaka mingi ya amani kati ya Ashuru na Babeli lakini palikuwepo na mipango ya chini kwa chini ya kudai uhuru iliyoripuka katika mwaka wa 652, ikiongozwa na kakaye.
 - c. kuanguka kwa Tebesi, 663
 - d. kushindwa kwa Elamu, 653, 645
- 25. 633- 629 Asshur-Etil-Ilani.
- 26. 629- 612 Sin-Shar-Ishkun.
- 27. 612- 609 Asshur-Uballit II:
 - a. mfalme aliyetawazwa akiwa uhamishoni huko Harani
 - b. kuanguka kwa Asshur katika mwaka wa 614 na Nineva katika mwaka wa 612.

II. Himaya ya Babeli mpya:

- A. 703- ? Merodach-Baladan:
 - akaanzisha uasi mbalimbali dhidi ya utawala wa Ashuru.
- B. 652 Shamash-Shum-Ukin:
 - 1. mwana wa Esarhadoni na nduguye Ashurbanipal.
 - 2. akaanzisha uasi mpya dhidi ya Ashuru lakini alishindwa.
- C. 626- 605 Nabopolasar:
 - 1. alikuwa ni mtawala wa kwanza wa himaya ya Babeli mpya.
 - 2. aliivamia Ashuru tokea kusini wakati Kaizari wa Umedi akavamia tokea Kaskazini.
 - 3. mji mkuu wa kale wa Ashuru, Ashurr uliangushwa mwaka wa 614 na mji mkuu maarufu wa Nineva ukaangushwa mwaka wa 612
 - 4. mabaki ya jeshi la Ashuru yakakimbilia Harani. Hata wakaamua kumsimamisha mfalme
 - 5. katika mwaka wa 608 Farao Necho II (kama vile II Fal. 23:29) akaelekea Kaskazini kusaidia mabaki ya jeshi la Ashuru kwa ajili ya kusudi la kuunda kinga ya ulinzi dhidi ya mamlaka inayoinukia ya

Babeli. Yosia, mfalme wa Yuda mwenye maadili ya Kiungu (kama vile II Fal. 23), akakipinga kikundi cha jeshi la Misri kilichopitia Palestina. Kulikuwepo na vita ndogo huko Megido. Yosia alijeruhiwa na kufariki (II Fal. 23:29-30). mwanae, Yehoahazi, akawa mfalme.

Farao Necho II akachelewa kuuzuia uharibifu wa majeshi ya Waashuru huko Harani.

Alishambuliwa na majeshi ya Babeli yaliyoamriwa na mwana wa mfalme

Nebukadneza II na alishindwa vibaya katika mwaka wa 605 huko Karkemishi juu ya mito ya Frati. akiwa njia kuelekea Misri akasimama Yerusalemu na kuuteka nyara mji. Alimbadilisha na kumwondoa Yehoahazi baada tu ya miezi mitatu. Akamweka mwanae mwingine wa Yosia kwenye kiti cha ufalme, Yehoiakimu (kama vile II Fal. 23:31-35).

6. Nebukadneza II akalifukuza jeshi la Wamisri kuelekea kusini kupitia Palestina lakini alipokea ujumbe wa kifo cha babaye na akaamua kurudi Babeli.

Baaadaye mwaka huo huo akarudi Palestina. Akamwacha Yehoiakini akiwa kwenye kiti cha ufalme wa Yuda lakini akawachukua mateka wakazi wengi na jamii ya familia ya kifalme. Danieli na rafikize walikuwa ni moja ya watu walifukuzwa.

D. 605-562 Nebukadneza II:

1. tokea mwaka wa 597-538 Babeli rasmi ikaitawala Palestina.
2. katika mwaka wa 597 safari nyingine toka Yerusalemu ikatokea kwa sababu ya Yehoiakimu kushirikiana na Misri (II Fal. 24). Akafa kabla ya kuja kwa Nebukadneza II. Mwanae Yehoiakini alitawala kwa muda wa miezi mitatu tu mpaka pale alipokimbilia Babeli. Watu elfu kumi, akiwemo Ezekieli, wakaweka makazi karibu na mji wa Babeli kwenye mfereji wa Kebari.
3. katika mwaka wa 586, baada ya kuendelea kucheza na Wamisri, mji wa Yerusalemu moja kwa moja ukaangamizwa (II Fal. 25) na kundi kubwa la watu kukimbia likatokea. Zedekia, aliyewekwa mbadala wa Yehoiakini, alikimbia na Gedalia akachaguliwa kuwa gavana.
4. Gedalia aliuwawa na majeshi yaliyoasi. Na majeshi haya yalikimbilia Misri na kumrazimisha Yeremia kwenda nao. Nebukadneza akavamia mara ya nne (605, 596, 586, 582) na kuwafukuza Wayahudi wote walioonekana kubaki.

E. 562-560 yule mwovu-Merodaki, pia alijulikana kama Amel-Marduk

- akamwachia Yehoiakimu toka gerezani lakini alitakiwa kubaki huko Babeli (kama vile II Fal.25:27-30; Yer. 52:31).

F. 560-556 Neriglissar.– alikuwa generali mkuu wa Nebukadneza aliyeuangamiza mji wa Yerusalemu

G. 556- Labaski-Marduk

- alikuwa mwana wa Neriglisa lakini aliuwawa baada ya miezi minane tu

H. 556-539 Nabonidasi:

1. Nabonidasi hakuwa akihusiana na nyumba ya kifalme kwa hiyo akamwoa binti wa Nebukadneza II
2. alitumia muda wake mwingi kulijenga hekalu la mungu wa mwezi Sin huko Tema. Alikuwa mwana wa kuhani wa kike wa mungu wa kike. Hii ilimsababishia uadui na makuhani wa Marduk, mungu mkuu wa Babeli.
3. alitumia muda wake mwingi akijaribu kuutuliza uasi na kuimalisha ufalme
4. alielekea Tema na kuachia mambo yote ya kiserikali kwa mwanae, Belshaza, ndani ya mji mkuu huko Babeli (kama vile Dan. 5)

I. ? -539 Belshaza (mtawala mwenza)

- mji wa Babeli ulianguka haraka mikononi mwa jeshi la Wamedi na Waajemi chini ya Gobryas wa huko Gutiumu kwa kuchepusha maji ya Mto Frati na kuingia ndani ya mji pasipo kuzuiliwa. Makuhani

na watu wa mji waliwaona Waajemi kama wakombozi na warejeshaji wa Marduku. Gobryasi alifanywa kuwa gavana wa Babeli na Koreshi II. Huenda Koreshi II au Gobryasi ni “Dario Mmedi” wa Dan. 5:31 na 6:1. Jina Dario linamaanisha “mtu wa familia ya kifalme.”

- III. Himaya ya Umedi na Uajemi: Utafiti juu ya kuinuka kwa Koreshi II (Isa. 41:2,25;44:28-45:7; 46:11; 48:15):
- A. 625-585 Kaizari alikuwa mfalme wa Umedi aliyeisaidia Babeli kuipiga Ashuru.
 - B. 585-550 Astyages alikuwa mfalme wa Umedi. Koreshi II alikuwa mwanae mkubwa kwa Cambyses I (600-559, Uajemi) na Mandane (binti wa Astyages, Mmedi).
 - C. 550-530 Koreshi II wa Anshamu alikuwa mfalme kibaraka aliyeeasi.
 1. Nabonida, mfalme wa Babeli, alimuunga mkono Koreshi.
 2. Kamanda mkuu wa Astyages, Harpagus, akaliongoza jeshi kuungana na Koreshi II kuasi
 3. Koreshi II akamwondoa kwenye kiti cha utawala Astyages.
 4. Nabonida, ili kurejesha usawa kwenye madaraka, alishirikiana na:
 - a. Misri.
 - b. Kroesa, mfalme wa Lidia (Asia Ndogo).
 5. 547- Koreshi II akaukabili mji wa Sardi (mji mkuu wa Lidia).
 6. November 2, 539, Gobryas wa Gutiumu, akiwa na jeshi la Koreshi, akaichukua Babeli pasipo upinzani. Gobryas akawa gavana wa Babeli.
 7. 539- kwenye mwezi wa kumi, Koreshi II “mkuu” binafsi akaingia kama mkombozi. Sera zake za wema kwenye makundi ya kitaifa yakaigeuza sera ya kitaifa ya miaka ya kuikimbia nchi.
 8. 538- Wayahudi na wengineo wakaruhusiawa kurudi nyumbani na kuyajenga makazi yao.
 9. 530- Mwana wa Koreshi, Kambiase II, akamurithi babaye.
 - D. 530-522 kutawala kwa Cambiase II
 1. aliongeza himaya ya Misri katika mwaka wa 525 kuwa moja ya himaya ya Umedi na Uajemi.
 2. Alitawala kwa muda mfupi
 - a. Wengine wanasema yawezekana alijiua.
 - b. Herodito anasema alijikata mwenyewe na upanga wake wakati akiwa amempanda farasi wake na hatimaye kufa.
 - E. 522-486 Dario I akaingia kwenye kutawala.
 1. alikuwa sio mmoja wa ukoo wa kifalme lakini alikuwa generali wa jeshi
 2. aliimiliki himaya ya Uajemi akitumia mipango ya Koreshi kwa ajili ya maliwali wa Kiajemi (kama vile Ezra 1-6; Haggai; Zekaria)
 3. Akaweka sarafu kama Lidia.
 4. Alijaribu kuivamia Ugiriki, lakini akaasi
 - F. 486-465 kutawala kwa Ahasuaero I:
 1. aliuangusha uasi wa Wamisri.
 2. akakusudia kuivamia Ugiriki na kutimiza ndoto ya Uajemi lakini akapigwa kwenye vita vya Thermoply katika mwaka wa 480 na Salamisi katika mwaka wa 479.
 3. Mume wa Esta aliyetwa Ahasuaero katika Biblia aliuawa katika mwaka wa 465.
 - G. 465-424 Artashasta I akatawala (kama vile Ezra 7-10; Nehemia; Malaki):
 1. Ugiriki ikaendelea kusonga mbele mpaka walipokabiliana na vita ya ndani ya Pelopanisia.
 2. Ugiriki ikagawanyika (Atheni - Pelopanisian).
 3. Vita ya ndani ya Uturuki ilidumu kwa muda wa mika 20.
 4. wakati wa kipindi hiki jamii ya Wayahudi iliendelea kuimalika.
 5. Utawala mfupi wa Ahasuaero II na Sekydianos - 423

- H. 423-404 Dario II akatawala.
- I. 404-358 Artashasta II akatawala.
- J. 358-338 Artashasta III akatawala.
- K. 338-336 Arsa akatawala.
- L. 336-331 Dario III akatawala.

IV. mapitio juu ya Misri:

- A. Hyksos (mfalme wa wachungaji – mtawala wa Kisemiti)-1720/10-1550 K.K.
- B. Utawala wa karne ya 18th (1570-1310 K.K.)
 - 1. 1570-1546 Amosi
 - a. Akaufanya Thebes kuwa mji mkuu
 - b. Akavamia upande wa kusini mwa Kanaani
 - 2. 1546-1525 Amenophi I (Amenhotep I).
 - 3. 1525-1494 Thutmosi I
 - 4. 1494-1490 Thutmosi II- akamwoa bintie Thutmosis I, Hatshepsut
 - 5. 1490-1435 Thutmosi III (mpwae Hatshepsut)
 - 6. 1435-1414 Amenophi II (Amenhotep II)
 - 7. 1414-1406 Thutmosi IV
 - 8. 1406-1370 Amenophi III (Amenhotep III)
 - 9. 1370-1353 Amenophi IV (Akhenaten)
 - a. Waliliabudu jua, Aten
 - b. Wakaanzisha ibada ya mungu mkuu (nadharia ya Mungu mmoja)
 - c. Nyaraka za Tel-El-Amarna ni za kipindi hiki
 - 10. ? Smenkhare
 - 11. ? Tutankhamun
 - 12. ? Ay (jicho kwa jicho)
 - 13. 1340-1310 Haremhab
- C. Utawala wa karne ya 19 (1310-1200 K.K.):
 - 1. ? Ramesesi I (Ramses)
 - 2. 1309-1290 Seti I (Sethos)
 - 3. 1290-1224 Ramesesi (Ramesesi II)
 - a. Toka ushahidi wa elimukale wengi wanapendelea Farao wa kipindi cha wana wa Israeli wakitoka Misri
 - b. Miji ya Avaris, Pithom na Ramses ikajengwa na watumwa wa Habaru (yumkini alikuwa ni Msemiti au Mwebrania)
 - 4. 1224-1216 Marniptah (Merenptah)
 - 5. ? Amenmesesi
 - 6. ? Seti II
 - 7. ? Siptah
 - 8. ? Tewosret
- D. Utawala wa karne ya 20 (1180-1065 K.K.):
 - 1. 1175-1144 Ramesesi III
 - 2. 1144-1065 Ramesesi IV – XI
- E. Utawala wa karne ya 21 (1065-935 K.K.):
 - 1. ? Smenda

2. ? Heriho
- F. Utawala wa karne ya 22 (935-725 K.K - Libya):
 1. 935-914 Shishaki (Shosenki I au Sheshong I)
 - a. Akamlinda Yeroboamu 1 mpaka Suleimani alipokufa
 - b. Wakaipiga Palestina mnamo mwaka wa 925 (k.v. I Fal. 14-25; II Nya. 12)
 2. 914-874 Osorkoni I
 3. ? Osorkoni II
 4. ? Shoshneki II
- G. Utawala wa karne ya 23 (759-715 K.K. - Libya)
- H. Utawala wa karne ya 24 (725-709 K.K.)
- I. Utawala wa karne ya 25 (716/15-663 K.K. - Kushi/Nubi):
 1. 710/09-696/95 Shabako (Shabaku)
 2. 696/95-685/84 Shebteko (Shebitku)
 3. 690/89, 685/84-664 Tirhakah (Taharqa)
 4. ? Tantamun
- J. Utawala wa karne ya 26 (663-525 K.K. - Saitic):
 1. 663-609 Psammetichus I (Psamtik)
 2. 609-593 Neco II (Necho)
 3. 593-588 Psammetichus II (Psamtik)
 4. 588-569 Apries (Hophra)
 5. 569-525 Amasis
 6. ? Psammetichus III (Psamtik)
- K. Utawala wa karne ya 27 (525-401 K.K. - Uajemi):
 1. 530-522 Cambyses II (mwana wa Korshi II)
 2. 522-486 Dario I
 3. 486-465 Ahusuaero I
 4. 465-424 Artashasta I
 5. 423-404 Dario II

*kwa ajili ya kuutofautisha mfuatano wa matukio angalia Zondervan's Pictorial Bible Encyclopedia, juzuu ya 2 uk. 231.

- V. Utafiti juu ya Ugiriki:
 - A. 359-336 Filipo II wa Makedonia:
 1. Akaijenga Ugiriki.
 2. Aliuawa mwaka wa 336.
 - B. 336-323 Iskanda II "mkuu" (mwana wa Filipo):
 1. Akamkimbia Dario II, mfalme wa Uajemi, kwenye vita ya Isus.
 2. Akafa mwaka wa 323 huko Babeli kwa homa akiwa na umri wa miaka 33/32.
 3. magenerali wa Iskanda wakaigawa himaya wakati wa kifo chake:
 - a. Cassander - Makedonia na Ugirik
 - b. Lysimicus – Thrace
 - c. Seleucus I - Shamu na Babeli
 - d. Ptolemy – Misri na Palestina
 - e. Antigonus - Asia Ndogo (hakudumu muda merfu)

- C. Wajumbe wa utawala wa Uyunani waliokuwa wakitawala Shamu (Seleucids) dhidi ya majina ya watawala wote wa Makedonia walioko Misri (Ptolemies) kwa ajili ya kuitawala Palestina
1. Shamu (wajumbe wa utawala wa Uyunani):
 - a. 312-280 Seleucus I
 - b. 280-261 Antiochus I Soter
 - c. 261-246 Antiochus II Theus
 - d. 246-226 Seleucus II Callinicus
 - e. 226-223 Seleucus III Ceraunus
 - f. 223-187 Antiochus III the Great
 - g. 187-175 Seleucus IV Philopator
 - h. 175-163 Antiochus IV Epiphanes
 - i. 163-162 Antiochus V
 - j. 162-150 Demetrius I
 2. Watawala wa Misri (Ptolemaic):
 - a. 327-285 Ptolemy I Soter
 - b. 285-246 Ptolemy II Philadelphus
 - c. 246-221 Ptolemy III Euegetes
 - d. 221-203 Ptolemy IV Philopator
 - e. 203-181 Ptolemy V Epiphanes
 - f. 181-146 Ptolemy VI Philometor
 3. mapitio kwa ufupi:
 - a. 301- Palestina chini ya mtawala Ptolemy kwa miaka mingi
 - b. 175-163 Antioko IV Epifane, mtawala Seleucidi wa karne ya 8, akataka kuwabadili Wayahudi kuwa Wayunani kwa nguvu:
 - (1) akajenga nyumba ya kufanyia mazoezi ya viungo.
 - (2) akajenga madhabahu ya wapagani ya Zeu Olympia ndani ya hekalu
 - c. 168 - Desemba 13 – Ogu akauwawa juu ya madhabahu huko Yerusalem na Antioko IV Epifane. Baadhi wanaridhani hili kuwa “chukizo la uharibifu” katika Danieli 9 & 11.
 - d. 167 - Mattathias, kuhani huko Modini, na mwana wa uasi. Mwanae aliyejulikana sana alikuwa ni Yuda Mmakabayo, “Judas the Hammer.”
 - e. 165 - Desemba 25 – hekalu likawekwa wakfu upya. Hii huitwa sikuu ya vibanda (Hanukkah) au “sikukuu ya kuwasha mishumaa.”

Kwa ajili ya mjadala mzuri wa tatizo la kupanga tarehe, utaraibu na makisio tazama *The Expositors Bible Commentary*, juuzu. 4, kur. 10-17.

KIAMBATISHO CHA TATU

JEDWALI LA AGANO LA KALE (kwenye ukurasa unaofuata)

MATAKI

ARTAXERXES I (P)
XERXES I - AHSUERUS (P)

EZRA
7-10
NEH.
Ezra

UKUTA WA YERUSALEMU - NEHEMIA
KURUDI MARAYA TATU - EZRA

BABELI UAJEHII

DARID I (P)
CAMBECC II (P)
KORESHI II (P)
BELSHAZAR (B)
NABONIDA (B)

OBADIA
YOELI
HAGAI
ZAKARIA
EZRA 1-6
RUKIMBIA
UHAMUSHONIA

KURUDI MARA YA PILI - ZERUBABELI
KURUDI MARA YA KWANZA - SHESHBARA

ASHURI

ASUR-BANI-PALI (A)
ESAR-HADONI (A)
SENAKERIBU (A)
SAGONI II (A)
YONA
SHALMANESAR V (A)
TIGRATH-PILESER III (A)

YEREMIA
EREKIEI
DANIELI
NATHUMU
HABAKUKI
SEFANIA
L M N R O

MISRI KANANI FILISTIA SHAMU

ELIYA ELISHA HOSEA
f
g
e

ISRAELI
ISAAYA
MIKA
b l j k l m n o

1 82 SAMWELI
1 82 WAFALME
1 MAMBO YA NYAKATI
2 MAMBO YA NYAKATI

- P - GEDALIA (P)
- O - ZEDEKIA (J)
- R - YETHAKINI (J)
- M - YETHAKIMU (J)
- L - YETHAHARI (J)
- K - YOSIA (P)
- J - MANASE (J)
- i - HEZEKIA (J)
- h - UZIA (J)
- g - YEROBOAMU II (I)

- f - AHABU (I)
- e - YEROBOAMU I (I)
- d - REHOBOAMU (J)
- c - SULEIMANI (UM)
- b - DAUDI (UM)
- a - SAULI (UM)

Ayubu

- Mwanzo - MNARA WA BABELI (A)
- 1 - GHARIKA YA NUTU (B)
- 1 - ANGUKO LA MWANADAMU (2)
- 1 - UUMBATI (I)

DR. BOB UTLEY
BIBLE LESSONS IN/L 96

Matukio yasiyoandikwa muda wake

1. Uumbaji (Mwa. 1-2)
2. Anguko la mwanadamu (Mwa. 3)
3. Gharika siku za Nuhu (Mwa. 6-9)
4. Mnara wa Babeli (Mwa. 10-11)

Matukio yaliyoandikwa muda wake

1. Kipindi cha mababa wa imani (Mwa. 12-50 na Ayubu) mwaka wa 2000 K.K
2. Safari ya wana wa Israeli kutoka Misri (Kutokas) mwaka wa 1445 au 1290 K.K.
3. Ushindi wa Kanaani (Yoshua) mwaka wa 1440 au 1250 K.K.
4. Utawala uliougana (Sauli, Daudi, Suleimani) 1000 K.K.
5. Utawala uliogawanyika (Rehoboamu-Yeroboamu I) mwaka wa 922 K.K.
6. Anguko la Samaria (Israeli) mikononi mwa Ashuru mwaka wa 722 K.K.
7. Anguko la Yerusalemu (Yuda) mikononi mwa Babeli mwaka wa 586 K.K.
8. Tamko la Koreshi (Uajemi) la kurudi mwaka wa 538 K.K.
9. Hekalu linajengwa tena mwaka wa 516 K.K.
10. Kufungwa kwa kipindi cha Agano la Kale (Malaki) mwaka wa 430 K.K.

Orodha ya Wafalme

A. Falme zilizoungana

1. Sauli (a)
2. Daudi (b)
3. Suleimani (c)

B. Israeli

1. Yeroboamu I (e)
2. Ahabu (f)
3. Yeroboamu II (g)

C. Yuda

1. Rehoboamu (d)
2. Uzzia (h)
3. Hezekia (i)
4. Manase (j)
5. Yosia (k)
6. Yehoahazi (l)
7. Yehoiakimu (m)
8. YehoiaKini (n)
9. Zedekia (o)
10. Gedalia (p)

D. Ashuru

1. Tiglath Pileser III (745-727)
2. Shalmanesa V (727-722)
3. Sargon II (722-705)
4. Sennacherib (705-681)
5. Esarhaddon (681-669)
6. Ashurbanipal (669-663)

E. Babeli

1. Nabopolasa (626-605)
2. Nebuchadnezza (605-562)
3. Nabonidus (556-539)
4. Belshazza

F. Uajemi

1. Koreshi II (550-530)
2. Cambees II (530-522)
3. Dario I (522-486)
4. Ahusuaero I (486-465)
5. Artashasta I (465-424)

KIAMBATISHO CHA NNE

KAULI YA KIMAFUNDISHO

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhilihisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhilihisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milele kwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwingine”. Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.

9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

“Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.”